MAHUSIANO YA MZAZI NA MTOTO

MWONGOZO WA MALEZI

Hisham Altalib. AbdulHamid AbuSulayman. Omar Altalib

MAHUSIANO YA MZAZI NA MTOTO

MWONGOZO WA MALEZI

Hisham Altalib
AbdulHamid AbuSulayman
Omar Altalib

International Institute of Islamic Thought
London • Washington

©International Institute of Islamic Thought, 1434AH/2013CE
Swahili Version 1438 H/2017CE
P.O.Box 669, Herndon, VA 20172, USA
www. iiit.org

London Office
P.O.Box 126, Richmond, Surrey, Tw9 2UD, UK
www.iiituk.com

Kitabu hiki kina hakimiliki. Hairuhusiwi kuzalisha au kusambazwa sehemu yoyote ya kitabu hiki bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa wachapishaji.

ISNN 978-1-56564-582-0 Jalada la nyuma

Maono na mawazo yaliyoelezwa katika kitabu hiki ni yale ya wachangiaji na si lazima yawe ya mchapishaji. Mchapishaji, waandishi na wahariri au yeyote alie changia katika ukamilifu wa kitabu hiki hana haki ya kisheria ya uhusika na matumizi, rejea ya mawazo, data na hitimisho, au mapendekezo yaliyomo katika kitabu hiki. Mchapishaji hatahusika na taarifa zitakazotolewa kutoka katika kitabu hiki na kudaiwa kuwa chanzo cha madhara yatakayotokea. Mchapishaji hatawajibika na matumizi ya michoro au picha zilizomo katika kitabu hiki ikiwa zimetoka katika vyanzo vingine vya kielektroniki au vilivyochapishwa. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa kuhakikisha taarifa hizi zinaandikwa katika kitabu hiki kwa ukamilifu wake na usahihi, mchapishaji hawajibiki kwa usahihi wa taarifa inayotokana au kupitia URL za mitandao zilizotumika katika kitabu hiki na hazimhakikishii kuwa kila kilichomo humo katika mtandao kiko sahihi au kitakuwa sahihi siku zote.

Kimefasiriwa kwa Kiswahili na:

Sadiki M. Feruzi, Iddi Jengo, Ahmad Msamaa, Hassan Mohammed, Tawaqal Juma
Kisra S. Mchoro, Hadija Mohamed, Abdallah Hamad na Jafar Salum.

Idara ya Lugha na Ukalimani
Muslim University of Morogoro,
East Africa Tanzania.

Picha za Jalada kwa hisani ya Familia ya: Hamisi Kandege, Mohammed Soloka, Mohammed Suleiman na Zuhura Hussein.

Local photos provided by: Iddi Suleiman Kikong'ona

Page layout by: Iddi Suleiman Kikong'ona
iddkiko@ymail.com

i

WAANDISHI WA KITABU HIKI

❒ Hisham Yahya Altalib

Dkt. Hisham Yahya Altalib alizaliwa katika kitongoji cha Mosul, Nivela,Iraq mwaka 1940. Alipata shahada yake ya kwanza ya uhandisi wa umeme kutoka Chuo Kikuu cha Liverpool mwaka 1962 na shahada ya uzamivu ya uhandisi wa umeme Chuo Kikuu cha Purde huko Layette, Indiana Marekani (1974).

Akiwa katika ajira yake kama mhandisi wa umeme, Dkt. Altalib alianza kujishughulisha na harakati za Uislamu huko Amerika Kaskazini ambazo anaendelea nazo hadi sasa. Ameshika nyadhifa mbalimbali ndani ya jumuiya za Kiislamu, ikiwa ni pamoja na kuwa Mkurugenzi wa kwanza wa kudumu katika Idara ya Mafunzo ya uongozi kwa Jumuiya ya Wanafunzi wa Kiislamu wa Marekani na CANADA (MSA) (1975-1977) na Katibu Mkuu wa Shirikisho la Kimataifa la Jumuiya ya Wanafunzi wa Kiislamu (IIFSO) 1976. Amesimamia kambi za mafunzo na Semina nyingi mbalimbali ndani na nje ya Marekani.

Alikuwa mwanachama mwanzilishi na Mkurugenzi wa Taasisi ya SSAR (1983-1995) pia mwanachama mwanzilishi wa Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) 1981, pia ni mwandishi wa *Mithāq al-Sharaf al-Da`awy* (kwa Kiarabu) na kitabu maarufu kiitwacho *Mwongozo wa Mafunzo kwa watumishi wa Uislamu*, ambacho mpaka sasa tayari kimeshafasiriwa katika lugha zaidi ya 20. Kwa sasa Dkt. Hisham ni Mkurugenzi wa IIIT katika idara ya uchumi.

Pia Dkt. Hisham ana watoto na wajukuu.

❒ AbdulHamid Ahmad Abusulayman

Dkt. AbdulHamid Ahmad Abusulayman alizaliwa katika mji wa Makka mwaka 1936, ambako pia alimaliza elimu yake ya juu ya sekondari. Alipata shahada yake ya kwanza ya Biashara katika Chuo Kikuu cha Cairo (1959), na shahada yake ya uzamili ya Sayansi ya Siasa Chuo Kikuu cha Cairo (1963) na baadaye shahada ya uzamivu ya Uhusiano wa Kimataifa Chuo Kikuu cha Pennyslyvania (1973).

Ameshika nyadhifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa katibu wa kamati ya mipango ya taifa ya Saudia Arabia (1963-1964); mwanachama mwanzilishi wa Jumuiya ya wanasayansi wa Kiislamu (AMSS) (1972); Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana wa Kiislamu Duniani (WAMY) (1973-1980); Mwenyekiti, idara ya Sayansi ya Siasa katika Chuo Kikuu cha Mfalme Saud kilichopo Riyadh, Saudi Arabia (1982-1984); na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kiislamu (IIU); Malaysia (1988-1998).

Amekuwa mshiriki mwandamizi katika mambo yote yanayohusu uendeshaji wa mikutano ya kitaaluma na Semina mbalimbali. Dkt. Abusulayman kwa sasa ni rais wa Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) na pia mwandishi wa makala na vitabu mbalimbali juu ya mabadiliko ya jamii za Kiislamu, pamoja na Nadharia ya Kiislamu juu ya Mahusiano ya Kimataifa: *Mbinu na fikra mpya juu ya muelekeo wa Uislamu; Muislamu na mgogoro wa kifikra; Migongano ya Ndoa: Kushikamana na Mafundisho ya Uislamu katika kujenga Utu wa Mtu; Kuhuisha Elimu ya juu katika Ulimwengu wa Kiislamu na Mtazamo wa Qur'an juu ya Ulimwengu: jukwaa la Mabadiliko ya utamaduni.*

Dkt. AbdulHamid ni baba na pia ni babu wa watoto na wajukuu.

❒ Omar Hisham Altalib

Dkt. Omar Hisham Altalib alizaliwa katika mji wa Kirkuk, Iraq mwaka 1967 na kwenda Marekani akiwa na wazazi wake mwaka 1967. Alihitimu shahada yake ya kwanza ya Uchumi na shahada nyingine ya Elimu Jamii (Sosholojia) kutoka Chuo Kikuu cha George Mason 1989. Mwaka 1993 alihitimu shahada ya umahiri ya Elimu Jamii (Sosholojia) na baadaye shahada ya uzamivu ya Elimu Jamii (Sosholojia) mwaka (2004) katika Chuo Kikuu cha Chicago.

Mwaka 1989-1992 alipata udhamini wa masomo ya elimu ya juu kutoka taasisi ya Taifa ya Sayansi na kuwa muhadhiri wa masomo ya Elimu Jamii (Sosholojia) katika vyuo vikuu; Chuo Kikuu kishiriki cha Daley, Chicago (1998) na Chuo Kikuu cha Indiana cha Kaskazini Magharibi, Gary, Indiana.

Mwaka (2000-2003) Dkt. Hisham alikuwa Profesa msaidizi wa masomo ya Elimu Jamii (Sosholojia) na Elimu Jinai katika Chuo Kikuu cha Ashland, Ohio na mwaka (2005-2006) alifanya kazi kama mhandisi msaidizi katika Jumuiya ya Kimataifa ya Sayansi huko Alexandria, Virginia. Pia akawa Profesa msaidizi wa masomo ya Elimu Jamii (Sosholojia) katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kiislamu, Malaysia mwaka (2009-2011). Dkt. Hisham ameandika makala nyingi kuhusu familia, elimu, wakfu, asasi za kihisani na mambo ya kijamii. Amehudhuria mikutano mingi ya kitaaluma na kusafiri sehemu kadhaa duniani.

SHUKRANI

Shukrani za dhati zinastahiki bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Kimataifa ya fikra za Uislamu (IIIT), Kwa uamuzi wake wa kutuamini kufanya kazi hii kubwa ya kuandika kitabu hiki .

Tunatoa shukrani zetu zisizokifani kwa Dkt. Ahmad Totonji, Dkt. Fathi Malkawi, Dkt. Jamal Barzinji, na Dkt. Yaqub Mirza kwa kuwa na nia njema ya kusimamia Taasisi hii ya (IIIT) kwa wakati wote wa uandishi wa kitabu hiki.

Kwa wahakiki wote ambao wametoa maoni yenye thamani kubwa sana katika maboresho ya kurasa , hususani Batool Al- Toma, Zainab Alawi, Michele Messaoudi, Wanda Krause, Maida Malik, Sara Mirza na Gasser Auda.

Shukrani za dhati zimwendee Dkt. Iqbal Unus, Lina Malkawi na Zeena Altalib kwa mchango wao wenye thamani kubwa.

Wengine ni: Akbar Ali Mir, Ashraf Sabrin, Saif Altalib, Zaid Altalib, Noha Altalib na Mahmoud Sherif waliochapa na kudurufu nakala kadhaa za mswada wa kitabu hiki.

Dkt. Tanveer Mirza na Salma Ashmawi ambao walitumika kama mifano halisi ya maisha katika kongamano juu ya Malezi lililofanyika ADAMS (maeneo yote ya Dulles yenye jamii ya Waislamu) huko Herndón, Virginia, Marekani.

Junaina Abdullah ambaye alisaidia kupitia seti za video juu ya malezi na Layla Sein kwa maoni yake yenye manufaa.

Hassan Altalib, kwa kuandaa marejeo ya kutosha na maoni madhubuti juu ya muonekano, yaliyomo na muundo wa kitabu hiki.

Tumebahatika pia kuwa na Salwa Medani ofisini kwetu ambaye alifanya kazi kwa uangalifu mkubwa katika hatua ya mswaada wa kitabu hiki na kukiboresha siku hadi siku. Shukrani maalumu

zimwendee kipenzi chetu Shiraz Khan aliyopo katika ofisi yetu ya London. Ni mhariri pekee na mbunifu wa aina yake aliyetupa hamasa isiyokifani.

Vile vile hatuwezi kumsahau Dkt. Imad-ad-Dean Ahmad, rais wa jumuiya ya Minaret of Freedom kwa kazi yake ya uhariri sambamba na ushauri wake .

Kwa heshima kubwa tunapenda kumshukuru Bi Silvia Hunt kwa kazi yake ya kunakili na kuhariri sehemu mbalimbali za kitabu hiki. Salma Mirza kwa kazi ya kukidurusu kitabu chote. Pia shukrani zimwendee Abdallateef Whiteman kwa ubunifu wake usio kifani wa mpangilio mzuri wa kitabu.

Shukurani za pekee pia zimfikie Hanna, binti yake Abdallateef kwa kutuwekea michoro mizuri aliyoichora kwa mikono yake mwenyewe.

Shukurani zetu za dhati ziwaendee wafanyakazi wa ofisi yetu ya IIIT iliyopo London kwa kuhakikisha kitabu hiki hatimaye kinakamilika.

Tunatoa shukrani kwa wote waliotoa michango na mawazo ya kitaaluma yasiyo kifani, kutoka kwa manguli wa fani ya Elimu na Saikolojia: Dkt. Ishaq Farhan, Dkt. Abdul Latif Arabiyyat, Dkt. Mahmoud Rashdan, Dkt. Fathi Malkawi na Dkt. AbdulRahman al Nageep ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa kukifanya kitabu hiki kuwa bora.

Tunazishukuru familia zetu kwa kutupa utulivu na kwa kutuandalia mazingira mazuri yaliyotuhamasisha kuifanya kazi hii kwa wepesi na kutuondoshea khofu wakati wote wakuandaa rasimu ya kitabu. Tunapenda kutambua mchango wa pekee kutoka kwa Dkt. Hishami, kwa kujitolea maisha yake kwa muda wa miaka 46, ambaye pasina ushawishi na kujitolea kwake kazi hii isingelikamilika. Mawazo na michango yake juu ya malezi ilikua ndiyo chachu ya msukumo katika mafanikio. Sehemu kubwa ya muda wa kazi hii ulitoka kwa wanafamilia zetu kwa pamoja hususani wajukuu zetu Yusuf na Ameen, wenye umri wa miaka saba na miezi mitano.

Sifa zote zimwendee yule aliyetujaalia maarifa na nguvu kwa kutujaalia uwezo wa kuikamilisha kazi hii.

TABARUKU

Kwa mama na baba zetu wapendwa, waliotulea kwa mapenzi ya dhati, waliojitoa muhanga juu yetu na huruma zao kwetu kwa muda wote wa maisha yetu, kuwa chachu ya malezi bora juu ya makuzi yetu kwa kadri ya uwezo wao. Japo walikosa mafunzo na elimu rasmi, walirithi matendo mema ya wazazi wao kwa hekima na busara pamoja na uzoefu wao kutokana na maisha na ustaarabu wa vizazi vilivyopita ili kutufundisha mambo mema, imani na kujitegemea. Mwenyezi Mungu awalipe yaliyo mema kwa ukarimu wao.

Kwa wazazi wote duniani, wanaopigana kadri ya uwezo wao juu ya malezi bora, walio na fikra nzuri japo wanahitaji maarifa ya msingi na ujuzi ili kuwawezesha kuwasiliana vyema na watoto wao na kujenga familia yenye upendo na mahusiano mazuri na mazingira ya nyumbani ambayo ndiyo matamanio ya kila mmoja wetu.

Kwa familia zote zinazokusudia kuwalea watoto wao kuwa wake na waume wenye kujitambua, wenye tabia njema, wenye thamani na ubora katika kuzingatia usawa, uaminifu, ujasiri, mapenzi, ubunifu na wenye imani pamoja na uwezo wa akili na uwajibikaji.

Kwa wake na watoto wetu kwa subira na kustahamili kwao kwa muda mrefu na kwa kutokata tamaa wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi ya utafiti na hatimaye kuandika kitabu hiki.

Kwa ujumla wao tunapenda kutambua michango yao ya dhati.

Eeh! Mwenyenzi Mungu, uliye mmoja na wapekee, pokea kwa huruma na kwa mapenzi yako jitihada zetu hizi katika kuleta umoja, amani, na maendeleo chanya kwa wanadamu.

YALIYOMO

Sehemu 1

{Sura 1—7}

▸▸ Malezi: —: Kuweka Misingi

SURA YA KWANZA 2

Malezi bora:Ni nini maana yake, na namna gani bora ya kuweza kuyaanza? 2

Utangulizi 4
Fikiri juu ya maswali yafuatayo 5
Hatua za Makuzi ya Mtoto 6
Tunavyowalea watoto: Aina mbalimbali za malezi 6
Ni vipi viashiria vya aina ya malezi? 11
Kuanza Malezi Bora: Maelezo kuhusu Kazi iliyo mbele yetu 12
Muda bora wa Kushiriki na Watoto 16
Kutumia ipasavyo Vyanzo vya Taarifa kuhusu Malezi 17
Ni lazima elimu ya malezi ifundishwe shuleni? 20
Hitimisho 24
Kazi za kufanya 25

SURA YA PILI **30**

Kitengo cha Familia: Kwa Nini Ni Muhimu? Kazi Zake Ni Zipi? **30**

Utangulizi 32
Kuelekea kuwa Mzazi 33
Athari za Watoto katika Kuimarika kwa Ndoa 34
Talaka na Takwimu za Watoto 36
Familia ya Mzazi Mmoja 38
Je Mzazi mmoja Anaweza kuwa mbadala wa Mwingine? 45
Umuhimu wa Familia katika Uislamu 49
Kipi kimeenda Kombo katika Familia za Waislamu? 54
Maendeleo ya Mtoto na Mifumo imara ya Elimu 56
Hadithi za Malezi Marekani 62
Mafunzo kutoka katika Mauaji ya Shule ya Columbine 66
Kufundisha Watoto Maadili: Malumbano ya Ukale na Usasa 67
Mlinganisho wa Familia katika nchi za Waislamu na Marekani 68
Hadithi za Waislamu Wanaoishi Uingereza 70
Athari za Umagharibi katika Malezi Ya Kiislamu 70
Malezi katika Nchi za Uingereza na Marekani 71
Wapi pakukuzia Watoto? 75
Matatizo ya Kiutamaduni: Mashariki na Magharibi 75
Dhana Mbili zinazokosekana katika fikra ya Kimagharibi 77
Thamani ya Aqida Dhidi Ya Umuhimu Wake 78
Familia ni mfano wa Kilimo 80
Kazi za kufanya 81

SURA YA TATU **86**

Malezi bora: Kuweka malengo sahihi **86**

Hatua ya Kwanza katika Kutekeleza Malezi Sahihi 88
Uchambuzi wa kina kuhusu Malengo 90
Kahawa na vipaumbele vya Familia 95
Hitimisho 96
Kazi za kufanya 97

SURA YA NNE **100**

Lengo lenye Maana zaidi: Kulea Watoto wanaompenda Mungu **100**

Utangulizi 102
Mbinu za Kisasa za Kuwafunda Imani Watoto Wetu 103
Kukosekana kwa Ushiriki katika Masuala ya Kijamii 104
Kukosekana uwajibikaji wa mtu binafsi 108
Kupitwa na wakati na Ushirikina 109
Mbinu yenye Busara 111
Wafundishe Watoto Upendo wa Qur'an 112
Ukumbusho Endelevu wa Mwenyezi Mungu 115
Wafundishe Watoto Kutubia (Kufanya Tawbah) 116
Wafundishe Kuhusu Muhammad (s.a.w) na Mitume Mingine 117
Wafundishe Watoto Maadili 118
Kitu gani umueleze Mtoto wako kwanza? 118
Matatizo ya Elimu ya Kiarabu 119
Kazi za kufanya 121

SURA YA TANO **126**

Kukabili Matatizo na Changamoto za Kila Siku **126**

Utangulizi 128
Changamoto kubwa zinazowakabili wazazi 129
Masomo ya malezi kutoka kwa Musa ndani ya Bibilia 135
Hitimisho 136
Kazi za kufanya 137

SURA YA SITA **138**

Kuepuka Imani za Kibubusa na Dhana Potofu **138**

Utangulizi 140
Kukanusha dhana potofu maarufu na changamoto 141
Baadhi ya Uongo wa Malezi uliofichuliwa 144
Kazi za kufanya 149

SURA YA SABA **150**

Mambo Yanapoenda Kombo **150**

Utangulizi 152
Hasira, Ukaidi, Hamaki na Kulia 153
Uonevu: Mtoto wako na Wewe 155
Ikiwa mtoto wako ameonewa, nini kifuate? 155
Vijana: Uchambuzi kuhusu Dhana ya Baleghe 156
Hasira kwa Vijana wetu na Sisi Wenyewe 158
Tufanye nini kwa kijana wetu na sisi wenyewe? 160
Kanuni chache za mawasiliano mazuri 160
Kazi za kufanya 163

Sehemu 2

{Sura 8—13}

⏩ **Malezi: —: Makuzi ya Mtoto**

SURA YA NANE **166**

Ujenzi wa tabia si wa kuakhirishwa **166**

Hatua za Makuzi 170
Ni kwa kiwango gani elimu Saikolojia inaweza kuaminiwa? 171
Hatua za ukuaji wa Mwanadamu ndani ya Qur'an 172
Maajabu ya mimba, ujauzito na kujifungua 175
Makuzi ya mwanadamu: Kuanzia kuzaliwa hadi utu uzima 176
Kipindi cha kupata hedhi kwa wasichana (Kuanzia miaka 11-13) 183
Miaka 13 – 15 : Pindi wavulana wanapopevuka 183
Kuwaelewa Vijana 184
Kutilia mkazo hatua za Makuzi 189
Kijana wa Kiajemi Hafidh mwenye umri wa Miaka 6 191
Hafidh wa miaka 4½ kutoka Syria 192

Kuhifadhi: Mashariki na Magharibi 192
Kazi za kufanya 193

SURA YA TISA 194

Njia za Afya Kwa Mtoto: Usafi, Lishe, Mazoezi na Kulala 194

Afya kwanza 196
Wakati wa ujauzito 197
Baada ya kujifungua: Mjadala kuhusu chanjo 198
Hoja dhidi ya Chanjo 199
Usafi na Elimusiha 200
Wanaume, wanawake na usafi 201
Afya: Baadhi ya mifano katika Uislamu 201
Usafi katika Vyoo 202
Nywele na Kucha 203
Lishe 205
Matatizo ya Unene Uliopitiliza 206
Maoni ya Imam Al-Ghazali juu ya tabia za kula 207
Ukweli kuhusu Watoto na Lishe 208
Mfano wa Chakula kwa Mtoto wa Miaka 2 Hadi 10 209
Maswali Yanayoulizwa Sana 209
Mwongozo wa Qur'an kuhusu chakula 216
Watoto na Mazoezi ya Viungo 218
Watoto na Viatu 219
Namna ya kukuza juhudi kwa Watoto 219
Ratiba za mazoezi zilizokokotezwa 221
Kulala 222
Vileo: Unywaji & uzuiaji wa dawa za kulevya 224
Watoto na Vishawishi 225
Alama za awali za kumgundua mtumiaji madawa 225
Vitu atakiwavyo mzazi kufanya ili kuzuia ulevi 226
Ushauri wa Mlevi kwa vijana 228
Kuvunja Sheria 230
Mwili ni amana: Ni neema isiyo na mbadala 232
Kazi za kufanya 233

SURA YA KUMI **236**

Unyonyeshaji: Maziwa Ya Mama **236**

Utangulizi 238
Unyonyeshaji katika Qur'an 239
Kiwango Cha Unyonyeshaji Nchini Marekani Na Uingereza 245
Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto Nchini Marekani 245
Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto Nchini Uingereza 246
Maziwa ya Kiwandani, ukuaji duni na Maradhi 246
Maoni ya Imamu Ali na Ibn Hazm Kuhusu Unyonyeshaji 248
Muda wa Unyonyeshaji 248
Dondoo Muhimu kwa Akina Mama Wanyonyeshao 249
Mlo unaopendekezwa kwa Mama anayenyonyesha 251
Taifa imara: kimwili 252
Kazi za kufanya 253

SURA YA KUMI NA MOJA **258**

Ubongo wa Mtoto:Kuutumia au Kutoutumia Ipasavyo **258**

Utangulizi 260
Wigo wa fursa mbalimbali 260
Uwezo wa ubongo kuhifadhi vitu 261
Ukuaji wa neva na mfumo mzima wa ubongo 262
Msongo wa Mawazo Unaweza Kuunda Hisia 267
Mfumo wa Utembeaji (Ujongeaji) 268
Msamiati na uwezo wa Kukumbuka Utotoni 269
Jinsi Ubongo Unavyobadilika 269
Wazazi wanatakiwa Wazungumze Vizuri na Watoto Wao 269
Kuanza kwa Masomo ya Awali Nchini Marekani 271
Wazazi Wanaweza Kufanya Kitu Gani? 272
Uislamu, Uimbaji na Muziki 273
Avicenna akizungumzia kunyonyesha,na muziki 275
Picha na Michoro katika Uislamu 276
Kukua kwa Ubongo wa Mtoto Mdogo 277
Je mafanikio ya mtu huamuliwa kabla ya umri wa miaka mitano? 280
Kazi za kufanya 281

SURA YA KUMI NA MBILI 282

Kuwalea Watoto wa Kiume na wa Kike kuna tofauti yoyote? 282

Utangulizi 284
Uhusiano wa kihisia 288
Hisia 289
Hadhi 289
Lugha ya alama 290
Kasumba ya kuwabagua wasichana na wavulana 290
Huzuni 291
Tofauti za kijinsi 291
Busara ya tofauti za kijinsia: Majukumu, si kwa upendeleo 292
Utengano wa kijinsia unaanzia wapi? 296
Jike-dume, dume-jike 298
Malezi kwa kutazama Jinsi 299
Kwanini Hakuna Usawa? 300
Dhana Potofu na Ukweli Kuhusu Akina Baba 301
Madhara wayapatayo watoto kwa kutokuwepo Baba zao 302
Mahitaji Tofauti ya Wavulana na Wasichana 302
Mahitaji ya Msichana Mdogo 302
Mahitaji ya Mvulana Mdogo 304
Usawa Katika Masuala ya Tofauti za Kijinsia 305
Kuchanganya Jinsia na Hulka 306
Wasichana na Wavulana Hujifunza Tofauti 307
Malezi na Jinsia: Mtazamo wa Kiislamu 313
Njia ya Mungu ni Njia Bora: Mfano wa China, Ujerumani na India 316
Kazi za kufanya 318

SURA YA KUMI NA TATU 320

Jinsia na Elimu ya Jinsia: Je tunawaeleza nini watoto wetu? 320

Elimu ya Jinsia ni Nini? 322
Ukimwi na Vifo nchini Thailand 327
Kwanini Profesa Mmoja Aliamua Kuhama Nchini Marekani? 327
Maadili na Jinsia: Jana na Leo 329
Kwanini Elimu ya Jinsia? Ni Lazima Kufundisha? 331

Kitu Gani Wafundishwe Watoto?	333
Muingiliano wa kimwili usiokubalika kisheria! Jinsi ulivyoenea!	334
Hekima ya hukumu ya kisheria kuhusu Uzinzi	337
Maradhi yanayoenea kwa njia ya Kujamiiana	338
Watoto Wenye Watoto	343
Utoaji Mimba	344
Uleaji wa Kunasibisha Mtoto	345
Mahusiano ya jinsia Moja na Wazazi	346
Elimu ya jinsia kwa Mujibu wa Uislamu	350
Jukumu la Wazazi kwa Watoto	352
Jinsia na Usafi wa Mwili	353
Vijana na Kujizuia	354
Mwongozo wa kufuata kuzuia Matatizo	356
Kuwa na haya kwa Jinsia Tofauti	359
Utaratibu wa Mavazi	364
Hakuna kuchanganyika na kukutana faragha	365
Vishawishi rika (makundi) na sababu nyingine	366
Ndoa za Mapema	367
Kuwalinda watoto dhidi ya ukatili wa kijinsia wa watu wazima	371
Umri unaofaa kwa watoto kuwatahadharisha kuhusu Ukahaba	373
Pindi Mtoto Anapokuwa Mhanga wa Kubakwa na nduguye	374
Mtaala wa elimu ya jinsia kwa mujibu wa Uislamu	376
Kazi za kufanya	378

Sehemu 3

{Sura 14—21}

⏩ Malezi: —: Ujenzi wa Tabia na Haiba

SURA YA KUMI NA NNE 382

Tabia Na Haiba 382

Utangulizi 384
Tabia Ni Nini? 385
Ujenzi wa Tabia 387
Tabia si muonekano wa nje, ina mizizi mirefu 388
Kuharibu Tabia Ya Mtoto 389
Haiba ni nini? 389
Ua la waridi, Mtoto, na Wazazi 389
Kazi za kufanya 390

SURA YA KUMI NA TANO 392

Kupandikiza Ujasiri 392

Utangulizi 394
Kanuni za Msingi za Ujasiri naWoga 396
Kufahamu Kujengeka kwa Woga kwa Watoto 398
Watoto Wanahitaji Kujifunza Hisia Pamoja na Ujasiri wa Kimwili 400
Baina ya Ujasiri na Utii 400
Msukumo wa Makundi Rika 401
Wazazi, Ushupavu, na Utamaduni 403
Kazi za Kufanya 405

SURA YA KUMI NA SITA **410**

Kupandikiza Mapenzi **410**

Utangulizi 412
Misingi ya Kuwezesha hisia 414
Upendo: Dhana ya Akili ya Kibunifu na Qur'an 415
Dondoo Muhimu kwa Wazazi 417
Itakuwaje Mwanao Akikwambia "Nakuchukia" 418
Mtoto Wa Kwanza 419
Kwanini Wazazi Huwapenda Watoto Wao? 420
Upendo na Kujiamini kwa Wazazi 422
Njia za Kivitendo za Kujenga Mapenzi 422
Je, Wazazi Wanapaswa Kuwafundishwa Watoto Chuki! 427
Kazi za Kufanya 428

SURA YA KUMI NA SABA **430**

Kufundisha Ukweli na Uaminifu **430**

Utangulizi 432
Wazazi wanapaswa kuwaamini watoto wao lakini wajue walipo! 434
Kanuni za Msingi 435
Kufanyia Kazi Tabia na Mtazamo wa Ulimwengu Mzima 437
Kwanini Watoto Hudanganya: Namna ya Kutibu Uwongo 438
Waeleze watoto visa vyenye malengo 440
Kazi za Kufanya 442

SURA YA KUMI NA NANE **444**

Kufundisha Uwajibikaji **444**

Utangulizi 446
Tabia na Mtazamo wa Kiulimwengu 448
Fursa katika Hatua Mbalimbali za Maendeleo ya makuzi 450
Kanuni za msingi za kuimarishwa 451
Jenga uwajibikaji taratibu 453
Kataza tabia ya mtu kusema 'lile si jukumu langu' 454
Ushauri wa kutekelezwa 454
Unganisha Hadhi na Uwajibikaji: Mifano 456
Kazi za Kufanya 459

SURA YA KUMI NA TISA **462**

Kufundisha kujitegemea **462**

Makuzi binafsi ndani ya Amerika 464
Kuna kejeli za kutisha kama utaifanyia kazi nyanja hii 464
Je tunamaanisha kujitegemea ama kutegemeana? 466
Umri –kipindi cha kukamilisha majukumu 468
Naweza fanya mwenyewe 468
Waache watoto watafute suluhu wao wenyewe 469
Hofu ya kutengana: kukabiliana na tabia ya ung'ang'anizi. 470
Ujana – Hali halisi 471
Athari za mitindo ya malezi 473
Ujuzi katika Kumuandaa Mtoto Kujitegemea 476
Vidokezo kwa wazazi 481
Ushauri na Uhuru: Binti na Mamayake 483
Je unalazimisha uvaaji hijabu kwa binti yako? 485
Kama wazazi hawawapendi marafiki wa watoto zao. 486
Kuwasaidia watoto kufanya maamuzi huwajengea kujitegemea 486
Hatua za kufuata katika kufanya maamuzi 487
Kazi za Kufanya 488

SURA YA ISHIRINI **490**

Kustawisha Ubunifu **490**

Utangulizi 492
Mbinu za kukuza ubunifu 494
Ugunduzi mbalimbali wa kihistoria 496
Kuimarisha Ubunifu wa watoto 497
Mambo yanayozuia ubunifu 497
Njia za kukuza ubunifu 500
Uandishi wa Watoto 501
Usanii kwa Watoto 502
Imani potofu: Mawazo ya ajabu au yasiyo na tija 504
Wazazi wafanye nini? 504
Ya kuzingatia katika midoli (wanasesere). 505
Kazi za Kufanya 508

SURA YA ISHIRINI NA MOJA 512

Watoto wa Kudekezwa na Kujitambua 512

Kujitambua 514
Vipi tutadhibiti malezi ya watoto wanaodeka? 516
Kazi za Kufanya 518

SURA YA ISHIRINI NA MBILI 520

Kumchagulia Mwanao Rafiki Mwema 520

Marafiki wa mtoto wako 522
Aina za marafiki 524
Matatizo yatokanayo na marafiki wabaya 525
Vishawishi vya kila siku vya makundi shuleni 525
Kuchagua rafiki Wema 525
Itakuwaje endapo mtoto wako atachagua marafiki wasiofaa? 526
Kwanini kuna vitu vyenye kuwavutia zaidi vijana? 527
Mahusiano mbali mbali ya kijamii 528
Familia zinapokuwa katika mazingira mabaya 529
Kazi za Kufanya 530

SURA YA ISHIRINI NA TATU 532

Runinga, Video Na Michezo Ya Kompyuta 532

Dodoso la wazazi 535
Madhara ya Runinga 537
Kabla ya Runinga 539
Mgeni 543
Weka mipaka katika kile ambacho watoto wako wanatazama. 544
Mambo mbadala wakati wa kutazama TV katika familia 546
Njia mbadala 547
Mambo bora zaidi ya kuchagua 548
Shughuli za Jamii 548
Shughuli Asilia 549
Michezo ya Kuchezesha 549
Sauti za Asili 550
Wape Fursa Waweze Kufahamu Mazingira Asilia 550
Kula chakula na watoto wako 551

Madhara ya kutumia Intaneti kupindukia 551
Michezo ya kompyuta 552
Michezo ya Video 552
Kuonekana kwa utofauti wa jinsi katika Runinga 553
Uharibifu wa Familia 554
Kwa Ufupisho 555
Kazi za Kufanya 556

HITIMISHO **560**

Hitimisho 562
Aya Teule za Qur'an na Hadithi za Mtume Kuhusu Malezi 565
Orodha ya Kazi za Kufanya 570
Orodha ya Marejeo ya Vitabu, Hazina ya tovuti, Faharisi na Indeksia 574

HISTORIA YA KITABU

Kitabu hiki kimeandikwa kwa ajili ya wazazi wote, wowote wawaye na popote walipo. Hata hivyo, mtazamo wa kitabu hiki ni sehemu ya mipango ya muda mrefu ya dira ya Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) katika kuuzindua ulimwengu wa Kiislamu kutokana na udumavu kitaaluma, hivyo kuifufua misingi hiyo ya taaluma ambayo ilikuwa nembo ya ustaarabu.

Pia kitabu hiki kinakusudia kuhimiza dira ya IIIT juu ya malezi, Kujikita katika kuzindua ari ya kitaaluma na maadili ya Uislamu kupitia elimu. Hata hivyo, uchunguzi wa juu ya mbinu zilizotumika huko nyuma nakushindwa kuwasaidia Waislamu katika kuleta mageuzi na mabadiliko ya Waislamu hautojadiliwa katika kitabu hiki. Urejeshwaji wa fikira za Uislamu ndiyo dhana inayo himizwa katika machapisho na makongamano ya IIIT ili kufufua masuala ya kitaaluma.

Kivitendo, haiyumkiniki kuwepo wazazi wasiojuwa namna nzuri ya kuwalea watoto, kwa kuwa misingi ya kisaikolojia na utu wake hujengwa na mazingira ya nyumbani wakati wa mwanzo kabisa wa makuzi yake. Hivyo tutazingatia kwa kiasi kikubwa juu ya jinsi gani utamaduni na maarifa ya jamii yanayotolewa nyumbani yanaweza yakawa ni msingi sahihi wa kumkuza kiakili na kifikra juu ya maendeleo yake. Ingawa nyumbani ndipo panapopatikana msingi wa masuala ya tabia na chachu ya ushawishi kwa mtoto katika kutofautisha haki na batili, haitoshi kulibaini jambo jema na kulifanya tu. Kwa kawaida binadamu huamini na kukubali kile kilicho katika utashi wa akili yake kuwa ni sahihi na kukifanyia kazi ipasavyo. Hapa ndipo wajibu wa wazazi unapokuwa muhimu.

Shule na taasisi nyingine za elimu kubakia kufundisha mambo ya kihistoria, kanuni, ujuzi, na kutoa taarifa juu ya mambo mengine ambayo kimsingi hutekelezwa nyumbani na familia ya mtoto kwa ujumla wake, na jambo hili ndilo linalosisimua tabia njema, ujuzi na kupanua fikra za mtoto.

Kazi hii inadhamiria kuchangia katika maendeleo na malezi bora ya mtoto. Taasisi ya kimataifa ya Kiislamu (IIIT) imefanikiwa kufanya makongamano mbalimbali na kutoa machapisho mengi ili kutimiza lengo hili; miongoni mwa

machapisho hayo ni;“Mwongozo wa mafunzo kwa watumishi wa Kiislamu” “(Kitabu kilichotafsiriwa katika lugha zaidi ya 20),” Dalīl Maktabat al-Usrah al-Muslamah” (Mwongozo katika maktaba za familia za Kiislamu), na “ Azmat al-Irādah wal-Wujdān al-Muslaim” (Waislamu na migogoro ya matashi dhidi ya vishawishi).

Wazo la kuandika kitabu juu ya mahusiano baina ya mzazi na mtoto lilitolewa katika mkutano wa bodi ya wadhamini ya Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) mnamo mwezi Agosti 1994 huko kisiwani Tioman Malaysia. Kilitizamiwa kuwa kitabu cha tatu kuchapishwa na taasisi katika orodha ya vitabu juu ya maendeleo na mawasiliano ya binadamu. Pia kama kuitikia ombi la Taasisi, Dkt. Ismail al-Fārūqī mwaka (1982) alichapisha kitabu “Tawhīd: Athari yake katika Fikra na Maisha” (Kitabu cha mwongozo wa Muislamu katika masuala ya Iman na Aqidah). Baadaye mwaka 1991, (IIIT) na Shirikisho la Kimataifa la umoja wa wanafunzi wa Kiislamu (IIFSO) kwa pamoja walichapisha kitabu kilichopata mafanikio makubwa:- “Mwongozo wa Mafunzo kwa Watumishi Waislamu”, kitabu cha pili katika mfululizo wa machapisho, ambacho kilikusudiwa kumuelimisha Muislamu mmoja mmoja au katika kikundi juu ya taaluma ya uongozi.

Kwa kutambua umuhimu wa kitengo cha familia. Dkt. AbdulHamid AbuSulayman, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kiislamu, Malaysia, (1988-1998) alitoa agizo la kuanzishwa kozi mpya ya lazima ya Familia na Malezi, (katika ngazi ya stashahada) kwa mtizamo wa kuhuisha dhana ya maadili na malezi bora kwa wanafunzi pamoja na kuzalisha walimu wa kutosha watakao fundisha kozi hiyo.

Aidha waanzilishi wa IIIT walianzisha mfululizo wa semina za mafunzo ya uongozi uliopangwa katika awamu tatu na wazo la kuzalisha kitabu juu ya malezi lilitamalaki katika awamu ya tatu.

Awamu ya 1 (1975-1990)

Ilihusisha ufafanuzi, maandalizi na uhamasishaji. Ilishughulikia katika kutoa ujuzi na mbinu za kiharakati zilizohitajika ili kuboresha ufanisi na utendaji wa kazi. Ni katika awamu hii kilichapishwa kitabu Mwongozo wa Mafunzo kwa watumishi wa Kiislamu, (1991) kitabu cha pili katika mfululizo wa machapisho uliobainishwa hapo juu.

Awamu ya 2 (1991-2000)

Taasisi kwa kutumia uwezo na juhudi za wakufunzi mahiri wakiwemo Dkt. Omar Kasule wa Kuala Lumpa, Dkt. Iqbal Unus wa Washington, Dkt. Mansoor Atam wa New Delhi na Dkt. Anas Al-Shaikh-Ali wa London, walitoa mafunzo mbalimbali duniani kote.

Awamu ya 3

Ilikuwa karne ya ishirini na moja ambapo ilijikita zaidi katika malezi. Wakati awamu ya 1 na 2 ililenga zaidi harakati za vijana, awamu hii ilibainisha waziwazi kuwa ujenzi wa tabia njema kwa sehemu kubwa ndio ulikuwa msingi muhimu wa malezi tangu mtoto anapozaliwa. Kwa hivyo Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) ilisisitiza nafasi ya wazazi kwa kutumia elimu ya malezi kuwafanya watoto kuwa raia wema na viongozi

wazuri wa baadaye waliojengwa kwa sifa njema. Ni kutokana na msukumo huo kitabu hiki kikaandikwa.

Malezi si kazi rahisi wala haipaswi ichukuliwe kwa wepesi. Athari yake juu ya watoto tuwaleao, aina ya jamii ambayo tunayoishi na pia aina ya ustaarabu wa vizazi vijavyo ni kubwa. Kwa mintarafu hiyo, suala la malezi ni la msingi na ni lazima lipewe kipaumbele. Tunaamini jambo hili la malezi ni la kuenziwa na kuhimizwa. Tunawashawishi waandishi wengine waandike zaidi juu ya kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki kwa kufanya tafiti zaidi. Taasisi ya Kimataifa ya Fikra za Uislamu (IIIT) imeimarisha timu kadhaa za kitaaluma ili kuandika zaidi juu ya mada hizi na kuzifasiri katika lugha kuu mbalimbali za dunia. Kitabu hiki ni hatua ya kwanza tu katika kujenga misingi ya malezi sahihi kwa vitendo.

Kwa mujibu wa wataalamu walio wengi, “biashara kubwa sana duniani, kazi iliyo bora zaidi na uwekezaji wenye manufaa zaidi ni kuenzi malezi bora kwa watoto.

MALENGO NA MAKUSUDIO

Ni rahisi kusoma kitabu hiki kinachowatambulisha mamilioni ya wazazi katika ulimwengu wa leo, Waislamu kwa ujumla na hata watu wa imani nyingine na hata wasio wazazi, wasiokuwa baba au bibi na hata ndugu ambao wanatamani kunufaika kutokana na ushauri uliotolewa katika kitabu hiki. Pia hakikuwalenga wasomi na wataalamu tu peke yao. Lengo lake mahsusi ni juu ya dhamiri ya malezi, kubainisha matatizo na kutoa suluhisho pamoja na kutoa mbinu za malezi bora, maadili na kutoa vijana watakaokuwa na sifa za uongozi.

Malengo makuu ya kazi hii ni:

Kusisitiza umuhimu wa malezi bora katika kuwakuza watoto na familia, kwa kuyafanya majukumu ya wazazi kuwa ni wajibu na kuwa kipaumbele. Pia lisichukuliwe kinadharia bali kimatendo zaidi.

Kuwaonesha wazazi namna ya kupata elimu na ujuzi muhimu juu kutekeleza suala la malezi sahihi ili kuwajenga watoto kuwa raia wema, wenye tabia nzuri na wenye maadili; wenye sifa kuntu watakao kuwa msingi imara wa jamii na kuwa chimbuko la ustaarabu wa binadamu katika wakati ujao.

Mwisho, kuwasaidia wazazi kujenga familia zenye furaha, amani, umoja, kuandaa mazingira ya ushirikiano na kuwa na mahusiano mazuri miongoni mwa wanafamilia ili kudumisha ustawi wa familia bora.

Katika sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, tumesisitiza juu ya suala zima la malezi bora, kwa kutoa fasili ya dhana ya malezi na utekelezaji wake ili kutoa suluhisho linalofaa juu ya matatizo ya kizazi cha Kiislamu ulimwenguni na jamii nzima kwa ujumla. Pia tumeeleza kwa mukhtasari hadhi ya malezi kwa namna yanavyofanywa hivi leo, ikiwa ni pamoja na kupitia vyanzo vya habari vinavyopatikana katika ulimwengnu wa Kiislamu na nchi zilizoendelea kiviwanda duniani juu ya suala hili la malezi.

Tulijikita pia katika uchunguzi wa namna nzuri ya kulea watoto wawe wenye tabia njema na maadili bora ili kuwa chachu ya mabadiliko ya jamii. Mbinu na njia zinazohitajika katika kuwakuza kimwili na kuimarisha fikra zao zimeelezwa katika sehemu ya pili ya kitabu hiki. Sehemu ya tatu imejikita katika ujenzi wa tabia na kujadili athari za matumizi yaliyopita kiasi ya runinga, kompyuta na michezo ya

video kwa watoto na familia kwa kueleza njia mbadala juu ya athari hiyo.

Mwishoni mwa kila sura, tumeweka mazoezi rafiki ya kufanywa na wazazi na watoto. Lengo kuu likiwa kuhimiza mjadala unaoendelea pia mawasiliano miongoni mwa wanafamilia ili waweze kujuana vizuri, kufurahia pamoja, kushiriki katika utoaji wa maamuzi na kubadilishana ujuzi. Hili litasaidia kuimarisha mahusiano na kuzifanya familia ziwe zenye furaha daima. Ni mambo machache tu yanayohitaji vitendeakazi toka nje kama vile matumizi ya maktaba, kutafuta ushauri anuwai toka kwa wazazi wengine au kutafuta ushauri wa kitaalamu. Tunapendekeza tena kwa kusisitiza kuwa mambo haya yote yafanyike nyumbani au wakati wa chakula cha pamoja wanapotoka kupata chakula nje ya nyumbani wakati wa jioni.

Ni matumaini yangu kuwa kazi na mijadala hii itaziba pengo la kimalezi ambalo wazazi kwa namna moja au nyingine hawakuweza kulifikia, pia kuwezesha mijadala juu ya masuala anuwai ndani ya familia ambayo ni nadra kuzungumzwa.

Mwisho, kitabu hiki na mambo yote yaliyojadiliwa humu yatafuatiwa na kazi za ziada ambazo zitagawanyika katika makundi makuu mawili:

1. (a) Kuelewa wajibu wa wazazi juu ya elimu, imani, na mafunzo ya ujuzi; (b) Familia zenye Furaha: Vidokezo muhimu katika makuzi na maendeleo ya viongozi wazuri wa baadaye.

Katika suala la 1(a), wazo kuu ni kuwasaidia wazazi kuelewa na kukubali wajibu wao katika kukuza dhana ya dini na ujuzi wa uongozi kwa watoto wao. Na katika kipengele 1(b), lengo ni kuweka mazingira ya nyumbani kuwa mazuri na ya furaha ili yawe chachu ya malezi bora kwa watoto ambao watakuwa na ghera ya uwajibikaji. Masuala ya mawasiliano, zawadi, udadisi, hasira na pengine wakati unaotumiwa na familia kukaa pamoja huwakilisha hatua za kiutendaji zinazohitajika katika kujenga na kuendeleza mazingira sahihi ya kimalezi. Aidha, wazo la kwamba "watoto ni watizamaji wazuri zaidi ya wachambuzi", litajadiliwa. Majaribio ya vitendo yatatolewa kwa wazazi ili kuona ni jinsi gani watoto wanavyoamiliana katika maisha halisi, aidha wao kwa wao, wao na babu na bibi zao,ndugu zao, wageni, jirani, masikini, jamii, wanyama, mimea, mazingira na dunia kwa ujumla wake.

2. Mifano mizuri ya Kuigwa ni lazima itokane na:- Wazazi - Mitume.

Wazazi watafahamishwa juu ya kujua umuhimu wa tabia zao dhidi ya makuzi ya mtoto. Kwa kuwa watoto ni waigaji wa mambo, ni lazima wazazi wajitahidi kuwa kiigizo chema, hivyo kwa kuwaiga wazazi wao nao wanaweza kuwa wazuri kama walivyo wao.

Maisha ya Mtume Muhammad ﷺ yanapashwa kuwa mfano bora wa kuigwa juu ya jinsi gani baba, babu, rafiki wa karibu wa mtoto na kiongozi mkubwa anapaswa kuwa. Ukweli ni kwamba, katika kusoma tabia ya Mtume Muhammad ﷺ na mwenendo wake, itakuwa kama dira na kigezo cha mjadala wetu katika kitabu hiki.

Mwisho, endapo wazazi watajitahidi kwa kadri wawezavyo katika kutekeleza mapendekezo yetu, basi tunatarajia kupatikana malezi chanya na endelevu. Makuzi mazuri ya watoto wenye afya na furaha ambao watakuwa watendaji katika jamii na ambao watakuwa mfano mzuri wa wazazi.

Ikiwa mama au baba wakati fulani wa maisha yao wataulizwa “Je mlifanya nini ili kuyafanya maisha yenu kuwa yenye thamani?” bila shaka watajibu kwa kujiamini: “Mimi nilikuwa mzazi bora na pengine ni babu au bibi mwenye furaha”.

? Je mlifanya nini ili kuyafanya maisha yenu kuwa yenye thamani ”

UTANGULIZI

Binadamu ameumbwa kwa namna iliyo bora kabisa na kujaaliwa kuwa kiumbe kinachoweza kustaarabika. Kwa namna hiyo, malezi ya mtoto yana-hitaji ujuzi wa nadharia na vitendo kuhu-su makuzi yake. Kwa kuwa wanaoanza kuchukuwa nafasi ya uzazi wanakuwa na uzoefu mdogo juu ya malezi, wanahitaji kujifunza namna ya kulea watoto pengine hata kabla ya kutunga mimba.

Bahati mbaya, pamoja na juhudi kubwa ya utafutaji wa mali ili kuwa na makazi bora, magari na samani, tumeshindwa kabisa kutumia juhudi hizo hizo katika malezi, tukidhani mambo yatatunyookea bila kuwa na maandalizi. Malezi si kitu cha kuachwa patapotea kwani nafasi ya kuharibika ni kubwa na madhara yake pia ni makubwa.

Mara nyingi wazazi hupata ujuzi kwa kujaribu na kwakufanya makosa na baadaye kuwa hodari kwa wanaye wa mwisho wala si watoto wa mwanzo, baada ya kujifunza kutokana na uzoefu. Hata hivyo, tatizo ni kwamba wakati ambao somo hili linaeleweka vizuri mzazi anakuwa tayari amechelewa. Watoto wa kwanza watalelewa katika hali hiyo hadi wanakuwa watu wazima na hivyo kutowezekana kuwapa malezi stahiki. Malezi bora ni muhimu nakamwe hayajitengenezi. Nikazi yenye changamoto inayo hitaji uangalizi wa karibu. Hii ndiyo kazi iliyombele yetu, hivyo ni lazima ienziwe kwa kukusudia kulifanya wenyewe, wake zetu na familia zetu kwa ujumla.

Jambo kubwa linalosisitizwa katika kitabu hiki kuhusu malezi ya watoto ni mawasiliano. Mawasiliano mazuri kwa watoto huwafanya watoto kuwa wenye furaha na kuwa vijana wawajibikaji. Nimuhimu kufahamu namna na wakati mzuri wa kuzungumza na watoto, na kubwa zaidi namna ya kuwasilkiliza kwa umakini na kuwaelewa.

Wakati wazazi wanaonesha kwa watoto wao mapenzi yasiyo na masharti, wanatakiwa kuboresha mawasiliano nao na wawe tayari kuwasikiliza. Mawasiliano ni mfumo wa njia mbili hivyo yasiachwe upande mmoja. Wazazi wanawajibu wa kuwasaidia watoto wao kukuza vipaji vyao bila kutumia nguvu kupita kiasi. Kuwaweka katika mazingira halisi ya malezi itawasaidia wazazi kutumia ujuzi na mbinu mpya katika kutatua matatizo.

Wazazi pia wanatakiwa wakati mwingine kutizama kwa makini baadhi ya mambo yao ya kale kwa kuwa si kila la kale ni dhahabu. Kadri muda unavyopita yapo mambo mapya huibuka, mambo hayo huhitaji ubunifu na njia mpya za kuyakabili. Ni suala la asili kwa kila mzazi kutumaini kuwa wanawe watakuwa watoto wema. Hapa tutajadili baadhi ya makosa yanayofanywa na wazazi japo si kwa kukusudia na athari zake.

Eneo lingine lililoelezwa katika kazi hii ni ukuzaji wa sifa ya "uongozi" kwa watoto. Hili linaweza kuonekana kuwa si suala la kutiliwa mkazo. Kwa mtizamo huu, tutadodosa suala la uongozi si kwa lengo la kuwandaa wawe watafuta madaraka bali kukuza ari ya ujasiri, imani na maadili madhubuti na sifa zingine za kumjenga kuwa mwana jamii hai na mwenye ari ya uwajibikaji.

Kwa vijana walio wengi hivi leo, nyumbani kumefanywa kuwa hoteli na migahawa, kwa maana ya kula tu na kuondoka. Ni muhimu kwa wazazi na watoto kutengeneza mazingira ya nyumbani kuwa sehemu ya furaha na amani. Nyumbani siyo mahali kama palivyo mahali pengine bali ni kama kiatamizi, ukumbi au jukwaaa ambapo wahusika wa familia ndio kama waigizaji na mawasiliano kama andiko la tamthiliya. Hivyo kila mtu ni lazima ajifunze kuyakabili majukumu yake. Inahuzunisha kuona kwamba wazazi wengi na watoto wa sasa hawawezi kuamiliana vyema, hivyo kupelekea makazi yasiyo na amani. Wakati mwingine wazazi na watoto huogopana au kutiliana mashaka na wengi wao hawajui namna ya kuboresha mahusiano yao. Wanaweza hata kuliwacha suala hili la kuleta mahusiano, kwa kujawa na hasira na msongo wa mawazo miongoni mwao, hatimaye kuharibu mahusiano yao kabisa.

Ingawa kazi ya malezi si jukumu kubwa kupindukia lakini haipaswi kufanywa kama kazi ya ziada. Kamwe hatuja chelewa kukabiliana na changamoto hizi na bado tunayo nafasi kubwa ya kuweza kuboresha mahusiano yetu kama tutaepuka kulaumiana kwa yale tuliyokosea. Haina maana kusema: "kama tungefanya hili au tusingefanya lile".Kuleta majuto na kuendelea kuweka mazingira ya "kama ingekuwa…"Hili halisaidii na halileti tija badala yake ni kuharibu na kutupa maumivu.

Ingawa tunaweza kuwa tulifanya chaguo lisilo sahihi na lenye athari kwa familia zetu ni lazima tuweke akilini yakuwa malengo yetu yalikuwa kutaka mafanikio. Tunapaswa kutumia muda kidogo au mchache kutafakari yaliyopita na kutumia muda mwingi kutafakari mambo yaliyo mbele yetu. Hatupaswi kujaza rundo la mawazo juu ya mambo ambayo tungekuwa tumeyafanya, tunahitaji kujikita katika mambo tunayoweza kuyafanya sasa ili kuijenga kesho.

Tunaweza pia kuweka ahadi za mafungamano mema na watoto wetu ili kuboresha uhusiano wetu wenyewe, hivyo kuwa wazazi wazuri kwa kuzingatia yaliyo pita kama somo la maisha na yajayo kama sehemu ya mabadiliko. Inaweza kusaidia ikiwa tutayaona yaliyo pita kama zege na yajayo kama udongo wa mfinyanzi unao hitaji kufinyangwa kuleta sura nyingine.

Wazazi wengi siku hizi (tukiwemo sisi wenyewe) wanatamani wangejuwa sanaa na sayansi ya malezi bora kabla

ya kupata watoto. Wangefanya hivyo wangeyaboresha makuzi ya watoto wao kwa haraka sana. Wazazi wengi wana dhani kwamba muda mwingi ungetumika katika kuboresha mawasiliano ya kimalezi. Tukitafakari juu ya maisha yetu, ni dhahiri inatia uchungu kwamba hatukuitumia vyema fursa iliyokuwepo kujijengea uzoefu wa kimalezi.

Tunatumaini kwamba watoto wetu watatusamehe kwa makosa yetu na kwamba wazazi wajao wataepuka makosa haya. Pia tunamuomba Mwenyenzi Mungu amlinde kila mzazi kutokana na ugumu wa kazi ya malezi.

Mtizamo wetu katika kazi hii ni kuweka mwongozo wenye mtazamo wa kutoa kinga badala ya kutibu. Sisi hatudai kwamba tunaweza kutibu matatizo kama matumizi ya dawa za kulevya, ulevi, mfadhaiko, uhalifu, na magonjwa yanayotokana na zinaa. Badala yake, tunaweza kutoa kinga na miongozo kwa familia ili kupunguza nafasi ya kutokea madhara hayo kwa kuchukua hadhari.

Malezi ya kawaida nayo yanahitaji ujuzi na maandalizi ili watoto wawe ni wenye kufanikiwa na kuwafanya wazazi kujifaharisha kwao. Kwa bahati nzuri taarifa nyingi na ujuzi kuhusu malezi zinapatikana kwa wingi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Hakuna njia ya mkato katika malezi, kama ambavyo hakuna njia ya mkato kupata kitu chochote cha thamani, haujachelewa sana kuanza kuwa mzazi bora kwa kuwa wewe ni mzazi sasa na utakuwa mzazi daima bila kujali wanao wana umri wa miaka 4 au 40.

Ni tumaini la kila mzazi kuwalea watoto wake wawe wenye furaha na baadaye kuwa vijana maridadi. Kwa hivyo kitabu hiki kitakuongezea nafasi ya kukamilisha hili na kuikamilisha ndoto yako ya mafanikio. Kuna usemi usemao “usielekee ndoto inapokupeleka bali ielekeze ndoto wapi unataka uelekee”. Japo muda muafaka katika kuwalea vijana ulikuwa miongo kadhaa iliyopita, nafasi nzuri ya pili ni kesho hivyo itumie vyema. Mwenyezi Mungu atabariki dhamira na juhudi zako.

Kitabu hiki kimehusisha takwimu kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kumpa msomaji mwelekeo na kujenga imani juu ya kazi hii. Takwimu hubadilika mara kwa mara, hivyo huchukuliwa kama mwongozo na si kama ukweli usiobadilika.

Wataalamu wengi wametoa maoni yao juu ya muundo na uchapaji wa mtiririko wa vitabu hivi. Baadhi yao walionelea kazi hizi zichapishwe katika vijarida na wengine wakaonelea kazi zigawanywe kwa misingi ya nadharia na vitendo, pia wapo waliotaka iwe mwongozo tu kwa msingi wa “fanya mwenyewe” pindi nadharia na vitendo vinapohitajika kwa pamoja. Mawazo yote yamezingatiwa ila kwa sasa tunatoa toleo hili la kwanza katika muundo huu. Ni tumaini yetu kuwa tutapokea mawazo adhimu kutoka kwa wasomaji wetu ili tuyafanyie kazi katika toleo lijalo litakalo chapwa katika muundo na ukubwa tofauti tofauti.

Siyo rahisi kuyaeleza mambo yote ya kitamaduni ya kila jamii katika kitabu hiki kimoja, hata hivyo tunatumaini kuwa tafsiri ya kitabu hiki katika lugha mbalimbali zitawasaidia hadhira yetu hususani walimu na wasomaji.

Tafsiri ya Kiswahili ya aya kadhaa kutoka katika Qur’an zimechukuliwa kutoka

katika tafsiri ya Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani na sheikh Abdallah Saleh Alfarsi na yapo maboresho kidogo ambayo yamefanywa na waandishi.

Kitabu hiki ni matokeo ya uzoefu walioupata waandishi hawa katika ulimwengu wa Kiislamu na Magharibi. Kinajaribu kueleza hekima ya mapokeo matakatifu, mwongozo wa Mtume na mafanikio ya binadamu katika pande zote urithi wa Waislamu na tamaduni za Kimagharibi. Ni juhudi za kuonesha namna ambavyo pande hizi mbili zinavyo ingiliana ikiwa zitachambuliwa na kutathminiwa vyema. Hivyo kutoa mchango adhimu katika uga wa mahusiano baina ya mzazi na mtoto.

Waandishi

Januari 2013, Washington D.C., USA

Mahusiano ya Mzazi na Mtoto: **Mwongozo wa Malezi**

Alinijia, mwaka wa 1969, akiwa Analia

Akitiririkwa machozi, mama alisema: "kaka Altalib tafadhali naomba nisaidie, suala la binti yangu. Nimemlea na kumpa kila kitu alichohitaji. Na sasa hivi binti yangu ana miaka 19 lakini ametoroka nyumbani jana usiku akiwa na rafiki yake wa kiume, na sijui yuko wapi."

Nilisema: "dada , unamaanisha nini unaposema umempa mwanao kila kitu?" Alijibu: "chakula, mavazi, vifaa vya kuchezea, fedha- kiufupi kila alichohitaji!" Nilimuuliza: "ulimfundisha masuala ya dini yake, Qur'an, maisha ya Mtume na historia ya Waislamu?" Alisema: "Hapana, lakini nilimpa kila kitu!"

Nilijisemea kimoyomoyo: Inatosha! Tunalea watoto wetu nje ya mafundisho ya Mwenyezi Mungu na tunawanyima mafundisho imara ya kimaadili, halafu tunataraji waje kuwa watu wachamungu, kama Abubakar, Omar na Ali! Machungwa na maembe hayawezi tokana na mti wa mnazi. Tumechelewa kwa miaka kumi na tisa! Hatuishi kwa mkate pekee.

Ilituchukua muda wa uvumilivu, upendo na hekima kumrudisha binti yetu na mume wake(ambaye alikuwa mpenzi wake) kwa rehma za Mwenyezi Mungu kuwafanya kuwa watu wema wanaofurahia ndoa yao wakiwa na watoto wao wanne.

Ukitaka kuwajibika vizuri kwa watoto wako , unatakiwa kuwa na mahusiano ya kindugu na watoto wako. Wanahitaji kujua ya kwamba wewe unawajibika kwao na wakati wowote watakao kuhitaji watakupata. Kuwekeza muda, fedha, na nguvu zako kwa watoto ndio "uwekezaji bora" unaoweza kuufanya!! Mtoto wako anakusihi wewe, anasema kwa sauti Mama,Baba, tafadhali.

"usitembee mbele yangu, kwa kuwa sitokufuata wewe,
Usitembee nyuma yangu , kwa kuwa sitakuongoza,
Tembea pembeni yangu na kuwa kama rafiki yangu." (Albert Camus)

Je umesikia kilio chao?

Sehemu 1

Malezi: Kuweka Msingi

- Sura 1 —: Malezi Bora 2
- Sura 2 —: Kitengo cha Familia 30
- Sura 3 —: Malezi Bora 86
- Sura 4 —: Lengo lenye Maana zaidi 100
- Sura 5 —: Kukabili Matatizo na Changamoto za kila siku 126
- Sura 6 —: Kuepuka Imani za Kibubusa na Fikra Potofu 138
- Sura 7 —: Mambo Yanapoenda Kombo 150

SURA YA KWANZA

- **MALEZI BORA**
  Ni nini maana yake, na namna gani bora ya kuweza kuyaanza?

SURA YA KWANZA 2

Malezi bora:Ni nini maana yake, na namna gani bora ya kuweza kuyaanza? 2

Utangulizi 4
Fikiri juu ya maswali yafuatayo 5
Hatua za Makuzi ya Mtoto 6
Tunavyowalea watoto: Aina mbalimbali za malezi 6
Ni vipi viashiria vya aina ya malezi? 11
Kuanza Malezi Bora: Maelezo kuhusu Kazi iliyo mbele yetu 12
Muda bora wa Kushiriki na Watoto 16
Kutumia ipasavyo Vyanzo vya Taarifa kuhusu Malezi 17
Ni lazima elimu ya malezi ifundishwe shuleni? 20
Hitimisho 24
Kazi za kufanya 25

Utangulizi

Uonapo familia zinaishi kwa furaha, amani, mapenzi na zenye mazingira salama na zaidi ya hapo watoto wakaishi katika misingi ya uchamungu, usidhani mambo hayo yametokea kwa bahati nasibu. Nimatokeo ya kazi kubwa na jitihada za kuimarisha uhusiano mzuri baina ya mzazi na mtoto. Malezi bora ni mradi endelevu na ndiyo ufunguo wa mafanikio katika makuzi ya mtoto kisaikolojia, kimwili na kifikra.

Hakuna shaka, malezi bora hujenga mazingira rafiki katika makuzi ya watoto. Mazingira hayo ni muhimu sana katika kuboresha mawasiliano na kuwaleta watoto na wazazi karibu. Mawasiliano mazuri baina ya mtoto na mzazi huhitaji mtizamo chanya na siyo uimla, makemeo au kuhukumu. Malezi haya humfanya mtoto muda wote kuwa mwenye wasiwasi.

Kuna matatizo mengi katika malezi ya Waislamu leo hii. Wazazi walio wengi hawasomei masuala ya ulezi hivyo wanakosa elimu hiyo, uzoefu na ujuzi katika malezi. Wanalazimika kuwalea watoto kimazoea, utaratibu uliopitwa na wakati na utaratibu uliorithiwa kutoka kwa mababu zetu ambao kwao suala la malezi lina maana tofauti ya kitamaduni. Hata hivyo, wapo wazazi wenye elimu ya kutosha ila ni wenye kuiga tamaduni za Kimagharibi kibubusa. Wazazi pia hufuata wazazi wenzao na majirani zao wasio na maarifa sahihi juu ya malezi. Wapo wazazi wanaojaribu kutimiza ndoto zao zisizotekelezeka kwa watoto wao. Pia wapo wazazi wasio jali au hukimbia wajibu wao wa kimalezi. Kwakutokujuwa au kwakukosa muda huwaachia jukumu hili wasaidizi (mayaya), walimu, ndugu, runinga na michezo ya kompyuta. Kwa nchi zinazo ingiza mayaya kutoka nje hususani nchi tajiri za Arabuni na Asia zimeonekana kukumbwa na athari hasi juu ya tabia za watoto wao.

Tunayo dhamira ya kuwasaidia wazazi kuondokana na athari hizo na kukomesha au kupunguza makosa ambayo hutokea bila kukusudia. Kwa maana hiyo, tunatoa sera nzuri dhidi ya makosa na changamoto nyingi ambazo wazazi wengi wanaonekana kukumbana nazo.

Bahati mbaya, leo hii malezi yanachukuliwa kama suala la kawaida sana kiasi cha kutotiliwa mkazo. Hivi ni wazazi wangapi ambao wanalichukua suala hili la malezi kama moja ya majukumu yao? Itatusaidia ikiwa tutafanya hivyo kwa kuwa tutagundua kuwa malezi ni suala linalohitaji mipango, mbinu na ujuzi wa aina yake.

Fikiri juu ya maswali yafuatayo

Swali la 1: Ni kazi gani inayohitaji ujuzi wa uongozi, saikolojia, sosholojia, anthilopolojia, unesi, usanii na mawasiliano?

Swali la 2: Ni kazi ipi isiyohitaji shahada, stashahada au leseni katika utekelezwaji wake?

Swali la 3: Ni kazi ipi miongoni mwa kazi ambazo hazijafahamika vyema na zilizotelekezwa?

Swali la 4: Ni kazi ipi ambayo imepelekea udhalilishaji na machafuko?

Swali la 5: Ni kazi ipi iliyo muhimu sana ambayo inaathiri maisha ya watu hata watu wazima?

Swali la 6: Ni kazi gani iliyo mwalimu kwa mtoto?

Jibu lake ni moja tu: **Malezi**

Hebu fikiri, kwanini hatuwatafuti fundi gari, fundi bomba au fundi umeme kwa kazi zetu ila wale wenye sifa? Sasa iweje wengi miongoni mwetu tunakuwa wazazi tusio na mafunzo juu ya malezi? Tunasoma kwa miaka ipatayo 16 kupata shahada vyuoni, lakini tunakuwa wazazi tena wakati tungali vijana bila maandalizi ya juu ya kuyakabili majukumu makubwa yaliyo mbele ya kila mzazi. Pia, japo tunajua kuwa ni lazima kuwa na leseni ili kuendesha gari, kuwinda au kurusha ndege lakini hatuoni umuhimu wa watu kupata mafunzo ya malezi.

Kwa hivyo, ni jambo gani ambalo watu wengi kati yetu hulifanya kwa uzuri katika malezi ya watoto? Japo zipo nadharia nyingi za malezi na ushauri wa kutosha kwa wazazi lakini hazitiliwi maanani kwa kuwa wazazi hulichukulia suala la malezi kama jambo la kimazoea na kutumaini kuwa kila kitu kitakuwa kizuri. Ni lazima waoneshe jitihada na wahudhurie mikutano ya umoja wa Wazazi na Walimu mashuleni, watilie manani maendeleo ya watoto wao, waguswe na matokeo ya watoto wao na washiriki ziara za kifamilia kwa maana ya uwepo wao katika ziara na kutia nguvu zao za ziada. Yapo mambo mengine zaidi ya hayo wazazi huyafanya japo madogo madogo.

Hata hivyo, hakuna mwongozo wa moja kwa moja unaoweza kuutumia, bali kuna taratibu ambazo zikitumika zinaweza kusaidia kufikia lengo. Sambamba na hayo, tuligundua kuwa hatujapata njia nzuri ya malezi japo tunaweza kufanya maboresho lakini hatuwezi kuharakisha mchakato wa malezi. Siku zote usitafute njia ya mkato ya malezi bora kwa sababu haipo.

NADHARIA SITA, BILA WATOTO, WATOTO SITA, HAKUNA NADHARIA

'Kabla sijaoa nilikuwa nina nadharia sita juu ya malezi ya watoto, sasa nina watoto sita na sina nadharia'

John Wilmont, Earl of Rochester (Brown 1994)

Hatua za Makuzi ya Mtoto

Tuanze kwa kutambua kuwa watoto hupitia hatua mbalimbali katika makuzi yao. Inakuwa faida kwa mzazi kuzifahamu vyema hatua hizi kwa kuwa katika kila hatua mahitaji ya msingi hubadilika. Hatua za makuzi ya mtoto zinaweza kugawanywa kama ifuatavyo:, Utoto (miaka 0-1); uchanga (miaka 1-3), Kabla ya kuanza shule ya msingi (miaka 3-5) umri wa kuanza shule ya msingi (miaka 5-12) ujana wa kati (miaka 12-18) na ujana kamili (miaka 18-21). Katika kila moja ya hatua hizo mtoto huhitaji mahitaji ya kimwili, kiakili, kijamii, kisaikolojia na kihisia kutoka kwa wazazi wake.

Hatimaye mtoto hukua kutoka katika hali ya utegemezi wa moja kwa moja hadi kujitegemea. Ni muhimu kwa walezi na watoto kuridhiana katika kipindi hiki cha mpito. Wananadharia wa migogoro wameeleza namna wazazi na watoto wanavyo pambana katika kuhodhi madaraka na mali. Kila mmoja akihitaji kuwa juu ya mwingine na mara zote huwa na mitizamo tofauti juu ya namna gani mali na rasilimali (pesa, mahala na muda) itumike. Kadri mtoto anavyo ingia katika kipindi cha baleghe na utu uzima wazazi huhitaji kuliwacha jukumu la kuwaongoza katika maisha yao. Hapa swali linabadilika pindi wazazi hao wanapokuwa wazee na kuwa wategemezi wa hao watoto. Dhana ya kujitegemea hubadilika na kuwa kutegemeana, hivyo kuwepo kwa mashauriano na kujaliana baina ya watoto na wazazi.

Tunavyowalea watoto: Aina mbalimbali za malezi

Kuna njia za aina nne za malezi ya watoto.Lakini katika uhalisia malezi hayajikiti katika namna moja rasmi, bali yanaweza changanya namna mbili au zaidi, lakini pia kutakuwa na mtindo ambao unatawala katika namna ya kulea.

1. Udikteta/kutumia mabavu: Wazazi hawa mara nyingi huhitajia utii na huadhibu kwa ukali/vibaya pale wasipo tiiwa. Mtoto hushiriki kwa kiasi kidogo au kutoshirikishwa nao kabisa na hutegemewa kufuata sheria na taratibu za wazazi bila kuuliza swali lolote [au kitu chochote]. Mawasiliano ya wazi kati ya mtoto na wazazi na maelewano yao kiujumla huwa hayapo katika hali ya kihisia. Umuhimu mkubwa huelekezwa juu ya utii na heshima kwa mwenye mamlaka. Kiufupi , wazazi hawa huhitajia utii wa watoto bila kuwepo kwa uwajibikaji wao.

2. Umamlaka: Wazazi ambao huwasiliana [na watoto] katika njia ya ukaribu na kujali, huimarisha kujikubali kwa mtoto na kumfanya kila anachofanya anakitambua katika mazingira ambayo si rafiki kuwa makini. Wazazi bado hawako tayari katika kuwasiliana na watoto wao. Wanaweka kanuni, lakini pia wanahamasisha maendeleo tegemezi kwa watoto. Hii hoja ya kushirikisha inamsaidia mtoto kuwa na hisia za kuzungumza na kuuliza maswali. Wazazi wanapendelea kusikiliza maswali. Baumrind amependekeza kuwa 'usimamizi na uangalizi' wa wazazi ni msingi sahihi wa tabia za watoto wao. Wao ni wenye kuthubutu, lakini si wasumbufu na hawana vikwazo. Mbinu zao za kinidhamu ni za kusaidia, badala ya kutoa adhabu. Wanataka watoto wao wawe na msimamo pamoja na kushiriki masuala ya kijamii, kwa kujitolea na kushiriki moja kwa moja."(Baumrind 1991 na kunukuliwa na Cherry 2015)

3.Mzazi ruhsa: Wazazi wa aina hii huruhusu [huwaruhusu] mtoto [watoto] kufanya kama ambavyo anataka/anavyopendelea, huku wakimwekea au kutomwekea matakwa yao. Wazazi hawa huwa na

imani kuwa, mtoto ana uwezo wake binafsi wa kufanya maamuzi bila kuhitajia msaada/usimamizi wao kama wazazi. Kuna mgogoro mdogo, kwa sababu wazazi ruhsa hutofautiana na matarajio ya watoto na hukwepa mikwaruzano/majadiliano. Wazazi hawa hutumia makubaliano ili kuleta heshima na matokeo tarajiwa mfano kama ufaulu wa kielimu. Na matokeo ya uwajibikaji wao mkubwa ukifuatiwa na matakwa madogo, sio tu hupelekea wazazi kuwa na utawala mdogo kwa mtoto wao, lakini pia huwa ni rahisi kwao kutawaliwa na mtoto wao. Hali hii hupelekea kutokuwepo hata mzazi mmoja kati ya wazazi kuwa juu ya mtoto kimaamuzi. Mtindo huu wa malezi ni mtindo wa mashirikiano sana, ambapo wazazi kiujumla hulea kwa kubembeleza na kwa upendo.

4. Kutoshirikishwa: Pia hujulikana kama malezi tengevu/yanayotenga/ yenye kumtenga mtoto. Aina hii ya malezi huwahusisha wazazi ambao wamejiondoa kabisa katika maisha ya mtoto, huku wakitoa kiasi kidogo cha mahitaji ya chakula na malazi, na huenda pia wakimuacha mtoto ajikuze mwenyewe. Wazazi hawa huwa hawahitajii na wala hawawajibiki kwa mtoto na hawahisi uhusika wao hawajihusishi kifikra katika maisha ya mtoto na juu ya ulazimu wao katika kuonyesha upendo na ukaribu. Hii hutokana na kujikita sana na kazi, kujiweka mbali sana katika kumjali mtoto, au hata kujitafutia sababu zitakazompelekea yeye kutokuwa na majukumu ya kumlea/kumkuza mtoto. Watoto wa aina hii mara nyingi huwa na hisia za woga na huenda hisia hizi zikawapelekea katika tabia mbaya katika maisha yao Walton 2012).

Athari ya njia za malezi

Njia za malezi zina mchango. Chunguzi za watafiti zimepelekea kupatikanika kwa makubaliano mengi juu ya athari ya njia za malezi kwa watoto, kama ilivyojumuishwa na Cherry (2014)

Njia ya kidikteta: kwa ujumla hupelekea watoto ambao hutii na huwa mahiri, lakini hukosa furaha, utambuzi kwa jamii na heshima binafsi.

Njia ya umamlaka: hupelekea kupatikana watoto wenye furaha , wenye kujiamini na wenye mafanikio[Maccoby, 1992]

Wazazi ruhsa: mara nyingi hupelekea upatikanaji wa watoto walio na furaha kiasi kidogo na wasio na uwezo wa kujipangia utaratibu binafsi. Aina hii ya watoto mara nyingi hupitia matatizo na huwa na uwezo mdogo shuleni.

Njia ya wazazi kutokushirikisha watoto: huwa na nafasi ndogo katika mazingira yote ya kimaisha. Watoto hawa hushindwa kujiongoza, hukosa heshima, na uelewa mdogo kuliko vijana wenzao.

TANBIHI

Malezi ya kiimla: Utamaduni wa ubabe na vitisho

Kuna imani potofu iliyoenea miongoni mwa wazazi wa Kiislamu na baadhi ya watu wengine kuwa malezi ya kiimla ndiyo yenye manufaa zaidi yanayoweza kurekebisha tabia mbovu za watoto wetu. La kushangaza ni kwamba dhana hii inaonesha kuegemea katika kuzuia matendo maovu badala ya kushajiisha fikra nzuri na tabia njema. Dhana ya woga na kushindwa kujiongoza hujengeka kwa mtoto ambapo mahusiano kati yake na familia yanakuwa siyo ya kawaida, matokeo yake tabia hiyo hasi ya mtoto hukua na kisha kuleta athari katika jamii kwa ujumla. Kwa sababu hii, na kwa umaarufu wa aina hii ya malezi, tumeamua kujikita katika suala hili. Tabia hii iliyopo ya wazazi wa Kiislamu ya kutumia nguvu, kukosa majadiliano, mijadala na mashauriano katika malezi. Mbegu hii ya malezi ya kiimla hupandikizwa katika familia kuanzia utotoni kisha huenea hadi nje ya nyumbani kama vile shuleni, jumuiya za kijamii hatimaye serikalini na katika mifumo ya siasa.

Katika familia, baba amejivisha mamlaka ya lazima juu ya watoto, kaka wakubwa katika familia nao pia kujipa mamlaka ya lazima juu ya wadogo na vijana wa kiume dhidi ya vijana wa kike. Kwa ujumla wanaume hujifanya mabosi hatimaye kukosekana dhana ya umoja na utekelezaji wa majukumu. Aidha, Mtume ﷺ alihimiza dhana ya uchunga;

> " Ninyi nyote ni wachunga na kila mmoja wenu ataulizwa juu ya kile alichochunga" (Bukhari)

Imezoeleka kwa wazazi kutoa amri na maagizo kwa watoto bila kujali mambo gani anatakiwa afanye na yepi hatakiwi kufanya. Ikitokea mtoto kuhitaji ufafanuzi zaidi atajibiwa "fanya kama ulivyoagizwa," "hivyo ndivyo ilivyo" au atajibiwa "mtoto usipende kuhoji hoji." Wakati mwingine watoto wadadisi wanakuwa wahanga wa kudhaniwa kuwa watovu wasio na nidhamu. Kuwanyamazisha watoto wa namna hii, baadhi ya wazazi wanaweza kuwapa majibu ya maswali wanayoulizwa yasiyo sahihi badala ya kuwaambia kuwa hawajui.

Hii haimaniishi kuwa wazazi hao hawawajali watoto wao bali wanawajali na wanawapenda sana. Hata hivyo katika harakati za kuwa makini na katika kudhibiti watoto hatimaye huwafanya kuwa jeuri. Tabia hii ya ujeuri haisaidii kimalezi kwa watoto ambao kihisia, kisaikolojia na kiakili wako vizuri. Ili kuwafanya watoto kuwa imara, wazazi hawana budi kuwashirikisha katika mambo yanayoihusu familia kwa ujumla. Qur'an inasema

> "…mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao, na kutokana na tulicho waruzuku wakawa wanatoa."
>
> (Qur'an 42:38)

> Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea.
>
> (Qur'an 3:159)

Japo malezi ya kiimla yanaweza kumfanya mtoto kuwa na nidhamu, lakini nidhamu hiyo itakuwa imejengeka juu ya woga kuliko heshima na mapenzi. Dhana hii ya woga imejadiliwa katika sura ya 15. Malezi haya ya kiimla yameenea hadi katika mfumo wa elimu ambapo nidhamu ya wanafunzi kwa mwalimu haijajengeka juu ya mapenzi ya kutaka kujifunza bali woga dhidi ya ukali wa mwalimu na adhabu. Hatimaye, wanafunzi wanaweza wasifanye vyema kitaaluma. Mbinu ya ushurutishaji imekuwa ikitumika katika mfumo wa elimu katika baadhi ya nchi ambazo mfumo wa usomaji kwa kiwango kikubwa unawafanya wanafunzi kukariri badala ya ufahamu na usomaji shirikishi. Kwa mfumo huo shule na wazazi hawastahiki kujipongeza. Watakachokuwa wamefanya ni kusaidia katika "kuzalisha" vijana ambao tabia zao zimejengeka juu ya mfumo wa kiimla na kimamlaka.

Huu ndio mtizamo wa kitumwa ambao unao dhihiri katika mamlaka za Kiserikali, vyama vya kisiasa, miamala ya kijamii, idara za polisi, jeshini, taasisi na viwandani. Vijana wachache waliofanikiwa kuukwepa mfumo huo wa elimu na wasiofanya dhulma katika jamii, si wenye kumiliki mali. Wanalazimika kuwa wasaliti na kufuata kundi lililo kubwa au kutofaa na kuwa mwiba kwenye mfumo huo ulio na uozo.

Kuna mkanganyiko au mgogoro wa kifikra vichwani mwa Waislamu kuhusu namna ya kuwalea vyema watoto wa Kiislamu kihisia na kisaikolojia. Kukosekana kwa mbinu madhubuti yenye manufaa mazuri, mmomonyoko na wingi wa mapote katika elimu vinahusika katika upotoshaji wa utamaduni na fikra thabiti za Kiislamu. Ukosefu wa utayari katika taaluma ya malezi ni sawa na kuwadhulumu watoto kifikra na kisaikolojia. Mtizamo wa sasa wa Waislamu walio wengi juu ya malezi hauendi sambamba na dira ya Qur'an ya 'imran (kutengeneza na kuendeleza ustaarabu), itqan (ukamilifu) na tafakkur (tafakuri); badala yake wamekuwa na mtizamo finyu, wa kitumwa na wakuiga. Badala ya kuwa na fikra za kisayansi, zenye malengo na mbinu, Waislamu wamekuwa wenye imani potofu. Wamegubikwa na dhana kuhusu mashetani na ushirikina, hivyo suala nyeti la sayansi limetupiliwa mbali.

Inafahamika kuwa namna ya kutatua matatizo ya wasomi na migogoro ya fikra inayouathiri Umma wa Kiislamu ni mzigo wa wakufunzi. Hata hivyo, ingawa wanayonafasi kubwa katika kutatua matatizo hayo bado suluhisho lipo kwa wazazi. Ikiwa wazazi watashajiishwa vya kutosha bila shaka watachukua nafasi zao za malezi bora, hivyo kutengeneza vijana wenye mtizamo mwema wenye manufaa na ambao wataubadilisha kabisa Umma.

Huzuni ya zama hizi katika malezi inaweza kuelezwa kwa sifa-bainifu zifuatazo:

- ❒ Tatizo la ujinga miongoni mwa wazazi juu ya malezi, hili ndilo jambo linalokwamisha utafutaji wa mafunzo ya malezi;
- ❒ Tabia ya woga inayopelekea dhana ya "akili ya utumwa" bila kujikita katika ubunifu;
- ❒ Kufanya mambo kibubusa na unyenyekevu kwa watu wengine "kufuata mkumbo" bila ya kufanya upembuzi wa kina; na
- ❒ Utawala kandamizi na wa kimabavu nyumbani na hata katika taasisi za Umma.

Malezi yanaweza kuwa chanzo cha uvunjifu wa familia, jamii na ama ustaarabu kwa ujumla. Ujenzi wa ustaarabu kamwe hauishi na si kazi ya wakati mmoja, hili ni suala la kuendelea kwa maana ya maisha kwa ujumla. Kazi hii ina mwanzo lakini haina mwisho. Ustaarabu huendelea kukuwa na kutengemaa. Ni jambo linalohitaji utafiti endelevu, ugunduzi na uboreshaji (ihsani). Tunawashajiisha wazazi kuwa na picha kubwa katika fikra zao na kufikiria madhara yanayoweza kutokea juu ya malezi dhidi ya jamii kwa ujumla.

Watoto wanapokulia katika mazingira ya woga na manyanyaso, wanakuwa wenye woga kuthubutu katika jambo au kutoa maamuzi juu ya jambo fulani. Hatimaye, wanakosa hamasa ya uwajibikaji na kushindwa kutoa maamuzi. Watoto watiifu nao pia huwa na mtizamo wa kudeka ambao huwapelekea kukosa ushiriki katika masuala ya kijamii na hili hupelekea kutokuwa na ujasiri wa kuhoji uwajibikaji wa viongozi. Watoto

waliokulia katika malezi ya namna hii hawawezi kukemea rushwa na ubadhirifu na wanakuwa wenye aibu katika kutekeleza majukumu yao ya kijamii. Ari ya kufanya kazi kama timu imepotea na hii imezuia hamasa muhimu zinazoijenga jamii. Kuwa nyuma kwa kiwango hiki na utamaduni usiobadilika wa imani potofu iliyo pandikizwa katika akili za vijana hao unaonesha bila shaka kupotea kwa dhana ya sayansi na tekinolojia.

Zilifika zama za dhahabu za ustaarabu wa Kiislamu kwa kuwa sababu zote hizo zilikita katika akili za watoto wakati wa malezi. Kwa mfano, suala la unyonyeshaji lilionekana kama sehemu muhimu ya malezi kwa mtoto, ambapo mkazo uliwekwa katika mambo muhimu ya makuzi ya kihisia na kisaikolojia. Hata hivyo swali la kujibu "kwanini zama hizo adhimu za ustaarabu zilipotea na kuwa staarabu za tabaka la chini kabisa?" swali hilo limeegemea upande mmoja muhimu: namna tunavyowalea watoto kuanzia kuzaliwa kwao. Ukosefu wa malengo juu ya malezi bora ndio msingi mkubwa unaokosekana katika kuijenga historia ya Waislamu.

Japo malezi ya kiimla yanaweza kumfanya mtoto kuwa na nidhamu, lakini nidhamu hiyo itakuwa imejengeka juu ya woga kuliko heshima na mapenzi. Malezi haya ya Kiimla yameenea hadi katika mfumo wa elimu ambapo nidhamu ya wanafunzi kwa mwalimu haijajengeka juu ya mapenzi ya kutaka kujifunza bali woga dhidi ya ukali wa mwalimu na adhabu.

Ni vipi viashiria vya aina ya malezi?

Hivi kuna uhusiano baina ya miamala yetu na wazazi wetu na namna tunavyo amiliana na watoto wetu? Mara nyingi wazazi walio wengi wanao wanyanyasa watoto wao husema hata wao walinyanyaswa na wazazi wao wakiwa wadogo. Hivi historia ya malezi inaweza kuashiria aina fulani ya malezi katika kizazi kijacho? Hivi kuna nadharia inayoeleza urithi wa aina ya malezi kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto?

Historia ya malezi ya mzazi mwenyewe juu ya mwanawe ni jumla ya mambo kadhaa ambayo kwa pamoja huweza kujulikana kama aina fulani ya malezi. Kwa ujumla wazazi ambao wamepata malezi mazuri wakati walipokuwa watoto, na wao pia wanakuwa wapole na kuwa wazazi makini kwa watoto zao. Baumrind (2008) anasema, Malezi bora huhusiana na kuimarika na ukuwaji wa akili katika umri wa miaka mitatu.

Kuna utofauti mkubwa wa kuamiliana kati ya wazazi wa kiume na wazazi wa kike kwa watoto wao. Utakuta wazazi walio wengi wa kiume na wazazi wa kike wana mwitikio, vishawishi, mapenzi na mafunzo sawa kwa watoto wao, hata hivyo utakuta wazazi wa kiume wakijihusisha sana na mambo ya kimwili kuliko wazazi wa kike. Hata hivyo, wazazi wote hujishughulisha sana katika michezo ya kimwili na watoto wao wa kiume kuliko wa kike. Kiwango cha elimu cha wazazi pia kina mnasaba na maendeleo mazuri ya mtoto shuleni na mahala pengine. Cha kuvutia zaidi ni kwamba kadri kiwango cha elimu cha baba kinapokuwa juu, mama ndiye anakuwa na nafasi kubwa ya kuwa karibu na watoto (Ricks 1985).

Bila kutizama mtindo wa malezi unaotumiwa na wazazi wetu, wakati mwingine tunapinga kabisa mtindo wao huo wa malezi. Huenda kukawa na utofauti wa mitindo mbalimbali ya malezi toka kizazi kimoja hadi kingine. Takribani nusu ya babu zetu wanaona kuwa wajukuu

wao wanalelewa tofauti na namna wao walivyowalea watoto wao. Nusu yao wanaona kuwa kizazi chao kimekuwa na upole mno juu ya wajukuu zao tofauti na walivyokuwa wao. Huku wachache kati yao wakisema hawa wajukuu zao wanapewa kazi kidogo sana za nyumbani kuliko walivyofanya wao, hivyo watoto wa leo wanao muda mwingi kuliko waliopata watoto wao (Zogby international 2006).

Wazazi bila kujali ujana wao wenyewe, asili ya familia zao, elimu au kipato chao, wazazi makini wanajuwa kwamba kujaaliwa kupata watoto wao wenyewe ni fursa pekee ya kuboresha namna wao walivyo lelewa. Wanaweza wakatumia mbinu hiyo ya malezi kama ilivyotumika na wazazi wao au wakaiboresha katika kuwalea watoto wao.



Kimsingi, vyovyote wazazi watakavyofanya, ukweli unabaki kuwa, watoto wao ni watu huru wanaojitegemea na kwamba wenyewe watahesabika na kuwajibika kwa vitendo wanavyofanya. Kwa ujumla wazazi wanaweza kuwaunga mkono na kuwaongoza. Na ipo siku watafurahi na kujigamba kuwa, "sisi tulikuwa wazazi bora".

Kuanza Malezi Bora: Maelezo kuhusu Kazi iliyo mbele yetu

Malezi bora huanza kabla hata ya kutunga mimba. Kabla ya ndoa unahitaji kuchagua mwenza sahihi. Baada ya ndoa, mama mjamzito anatakiwa kuwa makini na afya yake, chakula anachokula na kujiepusha na kila kinachoweza kumletea madhara ya afya yake. Baba anawajibika kutekeleza majukumu yake kwa kadri awezavyo katika kumpunguzia majukumu na kumpa muda wa kutosha kupumzika. Hapa tutatowa mtizamo wa jumla kwa wazazi juu ya elimu na ujuzi muhimu katika malezi bora.

Ni vizuri kujua mawanda halisi ya changamoto zinazowakabili wazazi ili iwasaidie kutathmini kiwango cha ugumu wanachopambana nacho. Ikiwa wanadhani suala la malezi ni jambo rahisi basi hawatoona haja ya maandalizi ya kukabiliana na hali hiyo na ikiwa watahisi jukumu la malezi ni jambo kubwa sana basi huenda wakakata tamaa na kuliacha kabisa.

Japo suala la malezi linaweza kuwa lenye malipo, kichocheo na hatimaye kujenga uzoefu pindi likitekelezwa vizuri ni suala la msingi katika mambo yaliyo ya msingi zaidi. Maisha yetu yote kwa ujumla yamejengewa na mlolongo wa majaribu, hivyo malezi ya watoto ni changamoto kubwa. Hivyo, dhana ya mapenzi ni lazima iwekwe pembeni na kushikilia uhalisia wa mambo. Malezi bora si rahisi na hayakamiliki bila makosa. Watoto watajaribu kufanya yasiyo wapendeza

wazazi ilimradi kutizama kiasi cha uvumilivu walionao, hata hivyo pindi watoto wawapo mbali bado mioyo na mawazo ya wazazi yanakuwa juu yao, maisha yao hubadilika ghafla pindi wanaporudi. Watoto wote huwa na vipaji kama walivyo wazazi, hivyo malezi si suala linaloweza tekelezwa na mzazi mmoja mmoja. Wazazi walio wengi wana mtandao unaowasaidia katika malezi ya watoto wao ambao unawahusisha walimu, mayaya, ndugu, viongozi wa dini na marafiki.

Pindi tu mimba inapotungwa tunaweza kuanza kutumia miongozo ifuatayo. Inasaidia kujenga mtizamo mpana na kusaidia kuepuka mkanganyiko juu ya lipi lifanywe na lipi lisifanywe. Jaribu kuanza kujaribu kufahamu miongozo nane ifuatayo ili kukusaidia kutathmini maisha ya familia na nyumbani kwako katika mizani sawa.

Shikilia misingi bora ya malezi. Hebu sema hata kama twaweza kufanya makosa kwa "ujinga" na bila hatia, ujinga haufanyiki bila ya MIMI na WEWE.

1. FAHAMU KUWA MAKUZI YA MTOTO NI MCHAKATO MREFU NA TETE

Kumpata mtoto mwema, raia muwajibikaji na kiongozi makini ni kazi inayotakiwa kufanywa kila siku na huchukua miaka kadhaa na si miezi. Japo mapenzi miongoni mwetu yanaweza kuwa hafifu na urafiki ukakoma, uhusiano wa mzazi na mtoto huwa tofauti kwani ni imara na usiovunjika kwa urahisi, ni miongoni mwa mahusiano imara na thabiti katika ulimwengu huu.

2. WEKA MALENGO NA MIKAKATI IMARA NA JITIHADA ENDELEVU ILI KUONGEZA UFANISI

Madhumuni hutusaidia kuepuka mikanganyiko ya kiutendaji pia hufasiri matendo. Huainisha kwa kuweka bayana kule tuendako na namna ya kufika. (katika sura zifuatazo tumeweka chati maalumu kusaidia kutoa mwongozo wa malengo katika malezi) Bila ya malengo au dira wazazi wanaweza kufanya makosa hata bila kuji-

tambua kwa kuwa hawana malengo yaliyo wazi ambayo yangetumika kupima matendo yao. Hii haina maana kuwa makosa hayawezi kutokea ; yanaweza kutokea. Suala la msingi hapa ni kuyafahamu makosa tunayoyafanya na kujifunza kutokana nayo hasa kwa kuwa wawajibikaji. Njia hii pia itumike kwa watoto; je tumewapa watoto wetu miongozo iliyo wazi? Tunawaelekeza namna nzuri ya kuishi nasi kwa amani? Tumewapa stadi muhimu za kuwasaidia kuishi kwa namna tulivyotegemea?

3.INGIZA KATIKA UTENDAJI KANUNI ULIZO ZISOMA NA MBADILISHANE UZOEFU HUO NA WAZAZI WENGINE

Ikiwa tutapitia maandiko juu ya malezi au juu ya ushauri nasaha utakuta miongozo kadhaa ya kutusaidia. Japo wazazi wanaweza kukubaliana na miongozo katika ujumla wake, Mara nyingi wazazi hawaiweki katika matendo (kwa kukosa ujuzi, uzoefu au kwa kuwa na shughuli nyingi). Hata hivyo, pindi wanapo badilishana uzoefu na wazazi wengine husaidia pande zote kupata stadi nzuri za malezi. Iwe hujaoa au kuolewa, umeoa au kuolewa, uwe nyumbani au umeajiriwa mbali na nyumbani, suala la malezi ni muhimu sana kutengewa muda.

4.KUWA MFANO WA KUIGWA NA WAFUNZE WATOTO JUU YA KUJITEGEMEA

Moja ya vitu muhimu sana ambavyo mzazi anaweza kuwafundisha wanawe ni namna wanavyoweza kutekeleza mambo kadhaa bila ya kuwategemea wazazi. Ni mazingira ya nyumbani ambapo watoto hujifunza heshima, nidhamu, ujasiri, mapenzi, huruma na kutekeleza majukumu. Haitoshi kuwafunza watoto kwa njia ya mahubiri pekee, bali kuwapa watoto nyenzo muhimu za kuwafanya kuwa akina baba au akina mama wenye tabia za kuigwa. Tabia njema za mzazi huwa darasa tosha kuliko mahubiri.

5. WAFUNZE WATOTO KUBAINI JAMBO JEMA NA BAYA

Wazazi wanaposikia taarifa juu ya tabia mbaya za watoto wengine, mara kadhaa husema: “mwanangu hawezi kufanya hivyo. Mwanangu anautofauti wa kipekee.” Ni jambo baya kudhani kuwa mtoto wetu hawezi kufanya mambo mabaya na kwamba kwa namna alivyo atakuwa mwenye mafanikio. Kwa uhalisia, mtoto anaweza kuwa na tabia tusiyo itarajia. Hili lisitushangaze kwa kuwa watoto wetu hawana tofauti na maelfu ya watoto ambao wanawazunguka na kuamiliana nao. Kwa kuwa sote ni kizazi cha Adamu na Hawa, tunao uwezo wa kubainisha mambo mema na mabaya na hivyo kuyafanyia kazi maarifa haya. Kwa kukabiliana na changamoto za namna hii na mazingira haya, kila mmoja ana uwezekano wa kutenda makosa, japo utofauti utakuwa kiwango cha makosa kwani wapo watakao fanya makosa mengi kuliko wengine, na wapo miongoni mwetu watakao tubu makosa yao na wengine kutofanya hivyo. Japo kila mmoja ana utofauti dhidi ya mwingine bado tunakabiliwa na mambo mengi yanayo fanana. Ni vigumu sana kwa mtu kukabiliwa na jambo katika maisha yake ambalo hajawahi mtu mwingine na mahala popote kukabiliwa nalo.

6.FANYA KAZI KWA BIDII ILI KUKUZA NA KUHAMASISHA TABIA NJEMA

Kwa kuweka matarajio makubwa akilini mwetu, kuna kuibuka upya kwa ustaarabu sahihi wa kiuungwana ambao unaweza kufanikishwa kwa kuanzishwa kwa taasisi imara. Taasisi hizi lazima ziwe na watendaji wenye tabia njema, wasio wabinafsi, wasio kata tamaa na wasio wabadhirifu. Watendaji hawa pamoja na mambo mengine wawe na sifa ya uaminifu na unyenyekevu na mapenzi kwa watu wengine. Tabia njema si suala la bahati nasibu, ni zao la nyumba yenye furaha, mazingira rafiki na wazazi wenye msimamo thabiti.

7. JENGA TABIA YA MAJADILIANO

Ongea! Fanya mazungumzo na wanao juu ya kitu chochote na kilakitu juu ya uliyoyafanya kwa siku, namna uyaonavyo mambo na namna wanao wanavyofikiri juu ya jambo X, Y na Z. Ni muhimu watoto kujifunza namna unavyoyafikiria mambo. Weka kipaumbele katika mawasiliano na jitahidi kuwajuwa na kuwafahamu vyema wanao. Mbali na kujenga tabia ya majadiliano, kuongea nao ni jambo la msingi sana katika kukuza lugha na kumfanya mtoto kujenga uwezo wa kuongea. Usimfanye mtoto ajifunze kupitia runinga, intaneti au michezo ya kompyuta na hivyo kuwa mbali nawe. Uzuri wa maongezi huibua kipaji kisicho hai kuwa hai. Kwa msingi huo tumeweka sura katika kitabu hiki juu ya madhara yatokanayo na utizamaji wa runinga uliopita kiasi. Mawasiliano yanahusisha mijadala lakini pia wazazi wanatakiwa kufanya mizaha na kucheza na watoto wao kwani ucheshi huimarisha mapenzi na kuondosha chuki. Wazazi wengi hujishughulisha na kuzaa tu bila kufaidi uwepo wao, hii ni hasara kubwa sana. Watoto huishi katika ulimwengu wa aina yao na hufurahia sana maisha hayo. Inasikitisha kuona wazazi kupoteza muda mwingi kutizama runinga badala ya kutoka na watoto wao kwenda kucheza na kufurahi nao. Kwa kuwa ulimwengu umejaa furaha na hofu, watoto wanaweza kuwa suluhisho la msongo wa mawazo kwa kuingia katika ulimwengu wa watoto japo kwa muda mfupi. Wapo wazazi wanaodhani kuwa kucheza na watoto ni kuonesha udhaifu au sawa na kupoteza muda. Ukweli ni kwamba unapocheza na watoto, unawafanya nao wajisikie furaha, wajiamini, kujenga ukaribu na ukaribu pia huwafanya kuwa huru kujieleza. Kuwafanyia mizaha na kucheka nao ni sehemu muhimu sana ya mawasiliano.

8. FURAHIA MALEZI MAZURI!

Huu ni muendelezo kutoka katika nukta zilizopita kanuni zilizoelezwa nyuma zinamaanisha kuingizwa katika utekelezaji zikiambatana na huruma pamoja na furaha. Baadhi ya wakati ili mzazi upate mafanikio imara katika malezi unatakiwa ujikite kwenye malengo ambayo ni sehemu ya furaha ya familia. Kuwa makini na hili. Kiujumla malezi mazuri ni dhana pana na ni jukumu linalohitaji huruma ya hali ya juu, kwa hiyo uzoefu katika malezi ni jambo muhimu katika kufikia malengo.



Muda bora wa Kushiriki na Watoto

Utasikia wazazi walio wengi wakidai kuwa hutumia muda mwingi wakiwa na watoto wao. Ukweli ni kwamba wanachoamini sicho kinacho kusudiwa. Japo wanaweza kuwa na watoto wao chumbani lakini wakiwa wameshughulishwa na runinga, wakiwa wanajisomea, wakiwa wanaongea katika simu, wakiwa wanasoma barua pepe au wakiwa wanaongea na wageni wao. Kinacho kusudiwa hapa ni kuwa mshiriki hai wakati wote uwapo na watoto. Hii inamaanisha kuwa kama unasoma usome pamoja na mtoto, kucheza michezo pamoja, kupika na kula pamoja, kujadili mambo mbalimbali pamoja, kufanya matembezi pamoja, kuosha vyombo pamoja na kutaniana. Kwa maneno mengine ni kwamba unapodhamiria kucheza na watoto basi kuwa mshiriki hai muda wote na shiriki matendo yao yote.

Hii ndiyo namna bora na nzuri ya kutumia muda pamoja na watoto. Yaya (msaidizi wa kazi) au mtu mwingine hawezi kuwa mbadala wa muda huo adhimu mtoto anaotumia kuwa na wazazi.

HASAN ALTALIB

Kutumia ipasavyo Vyanzo vya Taarifa kuhusu Malezi

Moja ya njia ambayo tunaweza kutumia kuanzisha malezi bora ni kuwaomba ushauri wataalamu na kusoma dondoo mbalimbali.

Vyanzo vya Kiislamu dhidi ya Vyanzo vya Kimagharibi

Yapo makala mengi kuhusu malezi Amerika ya Kaskazini (jedwali 1.1). Yapo maelekezo mengi kuhusu malezi bora kwa wazazi wa Kimagharibi na vipo vitabu vya kutosha, maktaba na kwa kutumia mtandao wanaweza kupata msaada mkubwa sana kufanya jambo la malezi kwa ufanisi.

Jedwali 1.1

UPATIKANAJI WA MAELEZO KUHUSU MALEZI

MAKTABA	IDADI
Maktaba ya Bunge la Amerika	2,464
Jumuiya ya vyuo vikuu 6 vya Marekani	3,215
Maktaba ya Fairfax ya Virginia	432
Maktaba ya Taifa ya Kanada	362

Kutoka kwa Bowker katika mfumo wa vitabu vya kuhifadhi kumbukumbu imeonekana kwamba, idadi ya vitabu vya malezi vilivyochapishwa au kusambazwa viliongezeka kutoka 2,774 mpaka 3,520 ndani ya mwaka 2011 (Peterson 2012)

Vyanzo:

United states library of Congress (www.loc.gov). Fairfax county Public library (www.fairfaxcounty.gov/library). library and archives Canada (www.collectionscanada.gc.ca)

Kinyume chake ni kwamba, lini wazazi wa Kiislamu watatafuta ushauri juu ya malezi bora kutoka katika vyanzo vya Kiislamu, ni kipi walichokuwanacho? Al-Tall na al Qaysi (katika lugha ya Kiarabu 1990) walieleza juu ya uhaba wa vitabu vizuri vya Kiislamu vya malezi. Ni vitabu vichache ambavyo vinatowa taarifa za kina juu ya kushajiisha tabia zinazokubalika kwa watoto. Wazazi hupata shida sana kutumia vitabu vya kitaaluma vya malezi. Vitabu vya kale vinahusu zaidi nyakati na changamoto tofauti lakini vinakosa ufafanuzi na maelezo. Taarifa za malezi kwa Waislamu zipo kila kona ikiwemo: Maandiko ya sharia, maelezo ya Qur'an, kazi za kihistoria, mashairi ya Kisufi na vitabu vya maonyo.

Katika kitabu cha Dkt. al-Za'balawi kilicho andikwa kwa Kiarabu juu ya malezi ya vijana anaeleza kuwa kuna maandiko ya Kiislamu machache sana juu ya malezi ya watoto na maandiko machache maalumu juu ya vijana. Jumuiya ya Wanafunzi wa Kiislamu Amerika na Kanada waliweza kuchapisha kitabu cha kwanza cha watoto mwaka 1973. Vitabu vya namna hiyo havikuwepo awali na wazazi waliokuwa wakiishi nchi za Magharibi walikuwa na uhaba wa maandiko juu ya watoto.

Dkt. Manazir Ahsan, mkurugenzi wa taasisi ya Kiislamu ya Leicester Uingereza anasema, japo jamii ya Kiislamu katika nchi za Magharibi wamefanikiwa kuanzisha taasisi nyingi, misikiti na shule, hata hivyo wameshindwa "kuchapisha maandiko ya kutosha katika lugha ya Kiingereza yanayoweza kutumika kufundishia kizazi hiki nyumbani na mashuleni" (D'Oyen 1996).

Maandiko yaliyokwisha chapishwa ni kiasi kidogo sana. Vitabu vingi zaidi vinahitajika. Maktaba nyingi za Kiislamu zinauhaba wa vitabu vya malezi na makuzi ya watoto. Vitabu vilivyo vingi vimejikita katika elimu ya watu wazima na vichache vinatoa elimu juu ya makuzi ya watoto na saikolojia ya vijana. Maandiko mengi yameandikwa na wasomi wakubwa juu ya mikabala rasmi ya ndoa; haki na wajibu wa mume, wake na watoto: changamoto na talaka pamoja na mahesabu ya mirathi. Kuna hitajio kubwa la vitabu vya Kiislamu vinavyo jikita zaidi katika mambo ya kifamilia na uhusiano wao hususan juu ya mambo ya kijamii, saikolojia na makuzi. Wazazi wanapohitaji ushauri na maelekezo juu ya masuala ya kifamilia ambapo hupata vitabu vilivyo jikita katika mambo ya Kifiqih.

Zaidi ya hayo, vitabu vya historia ya Uislamu vinavyofundishwa katika shule za sekondari katika ulimwengu wa Kiarabu hupuuza miamala ya kibinadamu na makuzi ya mtu binafsi bali hujikita katika siasa na masuala ya amani. Ni kurasa chache sana zinazoeleza masuala ya mapenzi, ukamilifu na heshima aliyokuwa nayo Mtume Muhammad (SAW) juu ya wanawe na namna alivyo kabili mambo yote yaliyoihusu familia yake kama utashi wake wa dhati katika kushiriki michezo na wanawe. Mtume hakupata fursa ya kuwalea watoto wake wa kiume kwa kuwa walifariki utotoni mwao, hata hivyo aliwalea binti zake (Fatma, Zaynab, Ruqayyah na Umm Kulthum) na pia alitoa mchango mkubwa katika malezi ya wajukuu zake na watoto wa ndugu zake na jamii yake kwa ujumla. Pia alimlea binamu yake Ali ibn Abi Talib na mwanawe wa kufikia Zayd ibn Harithah. Inashangaza sana namna Mtume alivyo fanya watoto kuwa kipaumbele kwa kuwajali, kuwaheshimu na kuwahurumia wakati huo huo akiwa ametingwa na harakati za kuanzisha jamii mpya iliyokuwa inakabiliwa na vitisho kutoka kwa maadui.

Wanaume wengi suala la malezi hawalipi kipaumbele kwa sababu kwa kiasi kikubwa linafanywa na akina mama. Kigezo alichotuonesha mama wa waumini hakijazingatiwa ipasavyo, kwa hakika sifa na matendo hayo yamesahaulika au kutupiliwa mbali. Tunatakiwa kuwashawishi wasomi kufanya tafiti mbalimbali na kuandika vitabu juu ya namna wake wa Mtume na maswahaba wanawake walivyo tekeleza jukumu la malezi. Hili litasaidia kuonesha umuhimu na nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya jamii pia kuongeza wigo wa maandiko katika maktaba. Zaidi ya hayo, maandiko hayo yaeleze mafanikio ya wanawake waliofanikiwa kuwalea viongozi maarufu wa nyakati za hivi karibuni na sasa.

Msisitizo mkubwa katika malezi hivi leo umejikita sana katika malengo badala ya matendo ambayo ni sehemu na chachu ya makuzi sahihi ya mtoto. Uharibifu mkubwa umefanywa miaka mingi sana wakati nchi za Kiislamu zimetawaliwa ambapo kipaumbele kiliwekwa katika ukombozi wa ardhi na malezi yakiwekwa kando. Mabadiliko ya kijamii, utawala bora na maendeleo hayakuwa sehemu za agenda. Kuandika kuhusu malezi haikuwa kipaumbele na haikuwa sehemu ya utafiti na kupewa msukumo wa dhati kwa muda mrefu.

Wanaharakati wa Kiislamu kama ibn Sahnun, ibn al-Jazzar na Ali al-Qabsy,

wote katika Qayrawan, Tunis na bila kuwasahau Al-Ghazzali, Al-Mawardi na Al-Shbeehi walihimiza sana unyonyeshaji, kulea, kuwafunza heshima na kuwaadhibu watoto darasani. Hawakutilia mkazo saikolojia, makuzi, elimu na malezi ya mtoto. Ili kuijenga jamii makini tunatakiwa kuwa na elimu ya kutosha juu ya malezi bora pia tunatakiwa kuwa na ujuzi, imani thabiti na maelezo sahihi. Inakinaisha namna Qur'an inavyo wataja Mitume kama kiigizo kwetu. Watoto wanaweza kujengewa sifa za uongozi mapema kabisa katika makuzi yao ikiwa tungekuwa na elimu ya malezi.

Mwaka 2002, mwanazuoni mkubwa profesa Mumtaz Anwar wa Chuo Kikuu cha Kuwait aliombwa na IIIT kufanya utafiti wa maandiko yaliyopo juu ya malezi kwa Waislamu. Hakupata vitabu vizuri kwa Waislamu na pia kuna kiwango kidogo sana cha wasomi katika ulimwengu wa Kiislamu, hususani miongoni mwa wanaume. Wazazi Waislamu walio wengi hutegemea sana uzoefu wao na namna waonavyo mambo katika malezi ya watoto jambo ambalo halitoshelezi kufanikisha kazi ngumu hiyo ya malezi. Kuna uhaba wa vitabu vizuri na mafunzo maalumu juu ya malezi bora lakini pia inakuwa vigumu kutoa takwimu ya idadi ya maandiko yaliyopo katika lugha yoyote itumikayo katika ulimwengu wa Kiislamu. Haja ya kuandika vitabu vizuri na kwa wingi bado ipo ambavyo vitasaidia kutatua matatizo ya jamii kuanzia ngazi ya chini.

SIFA ZA BAADHI YA MITUME KATIKA QUR'AN

ISTILAHI YA QUR'AN	تعابير قرآنية
Mkweli	صديقا
Mpole na mwenye huruma sana	رؤوف رحيم
Aliye zidishiwa ukunjufu katika elimu na afya	زاد بسطة في العلم و الجسم
Mwenye nguvu na mwaminifu	القوي الأمين
Mwenye elimu na busara	حكما و علما
Mjuzi na mwaminifu(mwenye kuhifadhi amana)	حفيظ علي

Ni lazima elimu ya malezi ifundishwe shuleni?

Ikiwa malezi ni kazi ya wajibu, kwanini elimu hiyo haifundishwi katika mfumo rasmi? Watu saba kati ya kumi wanadhani malezi ni suala wanalotakiwa kujifunza au kufundishwa

Longfield na Fitzpatrick 1999

Dunia imebadilika toka mwisho wa vita kuu ya pili ya dunia. Kizazi kilichotangulia katika familia moja kiliishi katika kijiji au mji huo huo. Mabibi na mababu, wajomba na mashangazi na ndugu walikuwa na nafasi ya kutoa ushauri nasaha na kusaidia malezi. Kwa sasa maisha ya kifamilia yana changamoto nyingi. Familia za mzazi mmoja ni nyingi na kuna wingi wa ndoa zinazovunjika, na pia wakina mama wengi kuwa wafanya kazi kuliko ilivyo kuwa huko nyuma. Kama sanaa ya kueneza malezi bora imeharibika kiasi ya kwamba tunataka kutekeleza wajibu wa mwalimu na kuwacha wajibu wetu wa kuimarisha mtandao wa kifamilia. Je tunataka shule ifanye kazi hii?

Japo kutoa elimu ya malezi inaonekana ni jambo lenye kuleta mantiki na lenye tija, lakini bado kiuhalisia ni jambo gumu kwa kuzingatia mazoea. Tunahitaji kujua juu ya mambo ambayo yafundishwe katika kozi. Malezi yatolewayo na walimu bado pia yana matatizo. Maisha yetu ya kifamilia hayako kisayansi; yako kihisia zaidi, mahusiano na ujamaa. Wale wanaokataa kozi ya malezi kufundishwa shuleni wanasema suala la malezi si la kufundishwa kama somo lililo katika mitaala ya taasisi za serikali. Taasisi za elimu zinazopenda kuingilia maisha ya familia na kuweka siasa zisiruhusiwe kupenyeza fikra zao katika mahusiano ya familia. Msaada wa wataalam juu ya malezi unaweza tumika, lakini jukumu la malezi lisiachwe kwa walimu na wataalam wengine. Kwa kuwa kila familia ina upekee, wazazi wanashauriwa kutumia busara, hekima na maamuzi binafsi. Kujifunza kutokana na kosa la mtu mwingine ni katika msaada na ustawi na uhuru wa familia uhifadhiwe. Walimu hodari wa kusomesha nadharia ya malezi siyo lazima pia wawe mabingwa wa kulea kwa vitendo.

Kwa mujibu wa daktari wa tiba saikolojia Donald Winnicott,

"Katika maisha yangu yote ya kitaaluma nimejiepusha kutoa ushauri. Japo ni kwa dhamira njema, madaktari mara nyingi hutoa ushauri ambao huyaharibu mahusiano ya akina mama na watoto wao, au ya wazazi na watoto wao."

WINNICOTT 1992

Kubwa zaidi, katika kutowa miongozo ya malezi, tunatakiwa kuwa makini ili kuepusha mkanganyiko wa ustawi wa familia na kuweka utawala wa kiimla. Hili linaweza kudhoofisha dhana ya kujiamini na uwajibikaji wa wazazi. Walimu ambao hawakupata mafunzo wasijipe jukumu la usuluhishi wa migogoro ya familia.

Baada ya kusema hayo, bado tunaona faida ya kuwa na mfumo maalumu wa kozi za mafunzo ya malezi. Badala ya kuwabwaga watoto katika mabwawa ya kuogelea na kwenye michezo kadhaa ni lazima tuwafundishe dhana ya uwajibikaji inayotokana na familia yenyewe, muda na gharama. Mfano wa kozi ya malezi inayojadiliwa hapo chini imechukuliwa kutoka Uingereza hata hivyo ulimwengu wa Kiislamu nao umeanza kufundisha elimu ya malezi. Kwa mfano inahimizwa kujuwa kuwa mwaka 1998, Chuo kikuu cha Kiislamu cha Malaysia kilianzisha shahada ya ndoa na malezi na stashahada ya elimu ya malezi kwa walimu.

Miongozo ya kozi katika shule za sekondari za Uingereza

Kama ilivyojadiliwa, lazima kuwepo majukumu kati ya wazazi na shule ambayo si lazima yaainishwe na uanzishwaji kwa madarasa ya lazima. Japo taasisi zinazojihusisha na afya hutowa misaada ya uzazi na malezi kwa wanawake wenye ujauzito wa kwanza, elimu ya mambo ya kijamii ina mikanganyiko mingi kwa kuwa kila jamii ina uzoefu wake. Uingereza ilianza kufundisha elimu ya malezi katika mfumo rasmi katika shule za watoto mwaka 2000. Kuvunjika kwa familia na familia za mzazi mmoja ni mambo yanayoonesha utete wa tatizo miongoni mwa Waingereza na limefikia hatua mbaya katika nchi za Ulaya (Woolf 1999). Kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na wanataaluma, wafanyakazi na wanasaikolojia, serikali ya Uingereza ilitoa miongozo ya kufundisha wanafunzi wa shule ya msingi kwa kuzingatia mada zifuatazo (Burgess 2009);

- ❒ Migogoro katika ndoa
- ❒ Namna ya kutoa adhabu kwa watoto
- ❒ Dondoo juu ya namna ya kumdhibiti mtoto mlizi mkiwa dukani
- ❒ Majukumu tarajiwa kwa baba na mama
- ❒ Gharama na uwajibikaji katika jukumu la malezi
- ❒ Kukuza dhana ya kujiamini kwa watoto na wazazi
- ❒ Thamani ya mapenzi, utu na usalama dhidi ya rasilimali vitu
- ❒ Haki ikienda sambamba na uwajibikaji bila kusahau uhuru
- ❒ Thamani ya ndoa
- ❒ Matumizi sahihi ya muda
- ❒ Namna ya kukabiliana na msongo wa mawazo katika maisha ya kifamilia.

Kwa mtalaa huu serikali ya Uingereza ilihisi itakuwa imesaidia kupunguza mimba za utotoni na tabia mbaya za watoto. Kwa kujifunza kuishi kwa kuzingatia sheria za familia ni hatua ya kwanza kujifunza kuishi kwa kufuata sheria za kijamii na kuepukana na vifungo vya jela.

Japo kuna changamoto nyingi katika malezi, bado ni kiburudisho kwa mlezi, ni jambo lenye malipo kwa Mungu na lenye kujenga uzoefu ambao wengi katika sisi wangependa kuupata.

(Batool Al-Toma, mwandishi na mama, barua binafsi)

Sayansi inahitaji methodolojia, miundo, stratejia na dhana.
Sanaa hii inahitaji busara, mbinu, mapenzi na hekima.
Malezi ni sayansi, sanaa na jitihada katika imani.

Je Watoto Wetu Wanaulemavu?

Kwa kuzingatia ugumu wa malezi, baadhi ya wazazi wamefikia hatua ya kuamini kuwa kizazi hiki si cha kawaida. Mama mmoja alisema:

"miaka ya nyuma kabla hatujapata watoto mimi na mume wangu tuliwashangaza jirani zetu kwa kuwafanyia usafi nyumba yao walipokuwa safari. Walikuwa na watoto wadogo watatu, walijaza wanasesere wengi kila mahala humo ndani. Masaa sita baada ya kuanza usafi ule wote tulikuwa tumechoka na kujipumzisha kwenye sofa huku tukishika vichwa pasipokuamini hali ile, hii haiwezi kuwa hali ya kawaida. Kama hivi ndivyo hatuhitaji watoto. Baada ya miaka miwili na kufanikiwa kupata watoto wawili, niliona kawaida tu kama ilivyo nyumba ya jirani zangu. Nyumba yetu wenyewe ina watoto kama walewale jionee mwenyewe."

FABER NA MAZLISH 1982

Watoto ndiyo Taifa la kesho: Kupitia Watoto Tunaweza Kuubadilisha Ulimwengu

- ❒ Kuna uwezekano mkubwa wa watoto kuishi kama unavyotaraji wawe: Kama utawaambia wanao "mnaweza jambo fulani" watafanya na kuliweza na kama utawakatisha tamaa kwa kuwaambia " hili hamliwezi" kweli watashindwa.
- ❒ Taifa ni jumla ya muunganiko wa familia mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanaume, wanawake na watoto.
- ❒ Ikiwa tunahitaji kulibadilisha taifa, lazima tuzibadilishe nyumba zetu.
- ❒ Ikiwa kuna mtoto alie katika hatari basi kuna familia pia iliyo katika hatari.
- ❒ Unadhifu si kitu cha kujiangalia namna ulivyo, bali namna unavyoweza kuwa.
- ❒ Ili Kuibadilisha familia ni lazima tuanze kufanya mabadiliko sisi wenyewe kwanza.
- ❒ Kadri watoto wakuavyo, basi ni wajibu wako kama mzazi kufanya mabadiliko kutoka kuwa mkurugenzi na msimamizi na kuwa mshauri.

……Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyo katika nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anapowatakia watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake.

(Qur'an 13:11)

HITIMISHO

IWE masomo haya yanafundishwa katika mfumo rasmi au la, lipo jambo moja la kuzingatia: Malezi bora na yenye athari katika jamii kwa ujumla hukua kwa haraka na kufahamika. Kukabiliana na hakika juu ya ndoa, malezi na makuzi ya watoto kabla hata mambo haya hayajatokea inaweza kuwa ni suluhisho lenye kufaa katika kudhibiti baadhi ya mitaanziko kwa hali ya baadaye inayoweza kuwasibu wazazi.

Hata hivyo, inaweza kuwa hatua ya kimantiki dhidi ya elimu ya jinsia, athari ya mahusiano ya kijinsia, malezi ya watoto; hata hivyo isionekane kuwa elimu hii inaweza kuchukua nafasi ya wajibu wa wazazi wenyewe. Ikiwa wazazi watatambua hadhi ya nafasi zao na mafanikio yanayotokana na juhudi hizo kwao na jamii, wangependa kujifunza sanaa na sayansi ya malezi bora na kwa kujitoa muhanga wa kweli kwa kadri ya uwezo wao kwa maslahi ya kizazi chao.

Kuitarajia serikali, shule au vyombo vya habari kutuambia ni kipi kigezo cha raia mwajibikaji, kigezo katika mambo mema, ni kucheza pata potea, na kwa hakika n uvivu wa wazazi na kukwepa majukumu. Ni nani basi atakaye beba mzigo wa ustawi wa watoto zaidi ya wazazi? Jukumu hili haliwezi kuchukuliwa na mtu mwingine!

KAZI ZA KUFANYA

KAZI YA 1: ULIWAHI KUJIULIZA KWANINI?

Jadili na wanao mambo yafuatayo na taja uzoefu wako kutoka kwa jamaa zako na rafiki. Zingatia swali "kwanini":

Mtu anaweza kuwa msomi mkubwa lakini kijamii akawa si mwenye mafanikio?

Mzazi anaweza kuwa mwenye mapenzi na furaha, lakini akashindwa kutenga muda wa kukaa na familia?

Mtu anaweza kuwa mwenye ujasiri lakini akakosa kuwaamini wengine?

Mtu anaweza kuwa mwenye dini lakini akakosa mantiki?

Mtu anaweza kuwa mwenye utambuzi wa juu lakini akakosa mpangilio wa mambo?

Mtu anaweza kujifanyia ukarimu mwenyewe lakini akawa mgumu kuwafanyia ukarimu wengine?

Mtu anaweza kuwa tajiri lakini akawa bakhili?

Malezi bora yangeweza kuchukuwa nafasi katika kushughulikia mambo haya!

KAZI YA 2: MTINDO WAKO WA MALEZI!

Ni mbinu gani ya malezi iliyo bora kwako? Ainisha udhaifu wako katika mbinu yako hiyo ya malezi na onesha hatua zinazofaa ili kuboresha. Jadili jambo hilo na wanao.

KAZI YA 3: ORODHA YA TABIA KWA WATOTO

Je mwanangu yuko tofauti na watoto wengine?

Wapo wazazi wanaodhani kuwa watoto wao ni aidha wazuri zaidi ya wengine au wabaya zaidi, kana kwamba wao ni kizazi maalumu. Kimsingi, watoto wana tabia zinazofana kulingana na wakati na mazingira. Hivyo, kubadilisha uzoefu miongoni mwa wazazi ni jambo bora zaidi. Andaa orodha ya tabia mbaya ambazo wanazo wanao na jadili namna ya kuboresha. Ili kuwapa motisha watoto anza na vitu ambavyo ni rahisi kurekebishika.

4. ANDAA ORODHA NA UJIULIZE: "MWANANGU ANA MATATIZO GANI?"

Orodha ifuatayo ni baadhi ya tabia mbaya zilizooneshwa na baadhi ya watoto:

☒ Kufeli masomo shuleni
☒ Kuwa mjinga
☒ Kula sana au kula kidogo

☒ Unyoaji wa nywele usiopendezwa nao
☒ Kutoa majibu yasiyo faa
☒ Kuwa na marafiki usiowapenda

☒ Kutofanya ibada
☒ Kutosaidia kazi za nyumbani
☒ Kununa kwa muda mrefu

☒ Kujiapiza na kulaani
☒ Kutizama runinga kwa muda mrefu na kushughulika na simu
☒ Uchokozi

☒ Tabia ya malumbano
☒ Kutizama filamu za kutisha
☒ Kupenda kula vikorokoro

☒ Kutokuwa nadhifu
☒ Kutokuwa makini na jambo la hatari
☒ Kutowaheshimu wakubwa

☒ Kurudi nyumbani usiku sana
☒ Kutopenda kukaa nyumbani
☒ Kutopenda kufanya matembezi

☒ Wizi
☒ Uongo
☒ Uvutaji

☒ Kuwakaripia majirani/watu wakubwa
☒ Kuvaa nguo usizopendezwa nazo
☒ kuweka sauti kubwa ya redio/runinga

☒ Kutokoga
☒ Kukaa muda mwingi bafuni
☒ Kuweka vitu ndani ovyo ovyo

Jambo la kuzingatia wazazi:

Unaweza kubadilisha mazingira ya kazi hii na kuwaacha wanao kuorodhesha " mambo mabaya kwa wazazi wangu?!" Je una busara na ujasiri wa kushiriki nao katika zoezi hili?!

KAZI YA5: TATHMINI KUPITIA SHAIRI

Kaa na wanafamilia yako na kisha muombe mwanao mmoja akuimbie shairi lifuatalo kwa sauti. Waombe wanafamilia kutathmini tabia ya kila mmoja wao kwa kuzingatia ujumbe katika shairi na kutoa mapendekezo thabiti ili kujirekebisha.

Nilimkimbilia mgeni mmoja
alipokuwa akipita

"Ooh, tafadhali ndugu" nilimwambia

Nae akasema, " usijali ndugu"

Sikujua kama wanifuata

Wote tukawa kimya mimi na mgeni,

Tukashika njia na kuagana.

Lakini nyumbani tunasimuliwa
habari tofauti

Namna tunavyo wajali wapendwa
wetu, vijana na wazee

Jioni ya siku ile, kikiwa chapikwa
chakula cha jioni

Kijana wangu wa kiume akasimama
pembeni yangu

Wakati nikigeuka nyuma, ilikuwa
nimpamie na kuanguka chini

"Hebu toka njiani," Nilimwambia
kwa hasira

Alisimama na kuondoka, akiwa kakata tamaa

Sikuwa nimetambua ukali wa maneno yangu

Nikiwa nimepumzika kitandani,

Sauti nyororo ilinijia ikisema

“Uamilianapo na mgeni,

Unakuwa mwenye huruma,

Japo familia uipendayo, waonekana

Kuinyanyasa

Nenda jikoni na katizame sakafuni

Utakuta maua pale mlangoni

Hayo nimaua kijana wako kakununulia

Kayachuma mwenyewe: samawati, njano na bluu,

Alisimama kimyakimya ili asiharibu murua wa zawadi

Bila kuonesha machozi yaliyojaa macho yake madogo,

Muda huu, nilijihisi mdogo,

sasa machozi yakaanza kunitoa

Taratibu nilikwenda na kupiga magoti,

kitandani pake;

”hebu amka, amka.” Nilimwambia

Haya ni maua uliyonichumia?

Akatabasamu,”niliyaona mtini.

Niliyachuma kwa sababa ni mazuri

kama wewe

Nilihisi utayapenda, hususani ya bluu

Nikamwambia,”mwanangu, nisamehe

Kwa namna nilivyokutendea leo;

Sikupaswa kukufanyia vile

Akasema,”Oh! Mama, usijali.

Bado nakupenda.”

Nikamwambia,”mwanangu,

ninakupenda pia,

Na nimeyapenda maua,

hususan ya bluu.”

KAZI YA 6: WAZAZI WA LEO WAKILINGANISHWA NA WAZAZI WA JANA

Tafakari na jadiliana na familia yako juu ya maswali haya :

Je uko karibu na wanao zaidi ya ulivyokuwa kwa wazazi wako katika umri huo? (70% ya Wazazi wa Kimarekani walisema ndiyo)

Kuna tofauti ipi ya mahusiano kati yako na watoto wako ukilinganisha na mahusiano yako na wazazi wako? Ni vipi yanafanana/ ni ipi mifanano yake na tofauti zake.

Unazungumza/unawasiliana kwa ukaribu zaidi kuliko ambavyo wazazi wako walikuwa wakizungumza au kuwasiliana na wewe?

Waombe wanafamilia kufikiria njia zinazoweza kuongeza hali ya mawasiliano na muamala mzuri, kusimulia hadithi za babu na wajukuu kwa kadri uwezavyo. Hadithi hizi zinaweza kukuza chimbuko la familia na kuwa kitambulisho cha familia katika makuzi ya watoto. Pia zinaweza kuwa sehemu ya historia ya taifa isiyo na mtizamo hasi wa kikoloni ambao umeenea katika vitabu vingi katika nchi zilizoendelea kiviwanda.

Jadili na familiya yako juu ya mambo yafuatayo.

Rafiki yangu aliniambia: “Wala si muhimu namlea vipi mwanangu. Mimi ni mtu mmoja nitaleta athari gani!”

Ikiwa kila mmoja miongoni mwetu ulimwenguni kote ataacha jitihada za kuleta mabadiliko mazuri eti kwa kuwa “yeye ni mtu mmoja,” ni nani basi anaweza kuleta mabadiliko hayo? Huu ni upuuzi kabisa. Sote tunajuwa kuwa Mitume ya Mungu ilikuja kwa namna ya kila mmoja na zama zake, kama ilivyo kwa maswahaba, wanazuoni na pia watu wenye busara katika historia. Walileta mabadiliko katika ulimwengu. Hebu wafikirie watu kama Steve Jobs na Bill Gates. Kisha jiulize: nani aliyekuletea mabadiliko katika maisha yako? Je ni ndugu yako? Rafiki? Mwalimu? Kocha? Au kiongozi wako wa dini? Simulia hadithi yako kwa wanao kisha waombe waeleze aliyeshajiisha mabadiliko katika maisha yao.



KAZI YA 7: WATOTO: KIPI MNACHOTARAJIA KUTOKA KWA WAZAZI WENU?

Muombe mmoja kati ya wanao aisome kwa sauti hadithi ya " Mti mkarimu" iliyotungwa na Silverstein. Kisha waulize watoto wakueleze wanachotarajia kutoka kwako. Kipi, lini na kwa namna gani? Baadaye ueleze unachotarajia kutoka kwa wanao!

"Mti mkarimu" hadithi iliyotungwa na Shel Silvertein inaeleza kuhusu uhusiano kati ya kijana mmoja na mti uliokuwa nyikani. Mti huo ulikuwa mara zote ukimpa kijana yule kila alichohitaji. Katika umri wa ujana wa kijana huyo mti huo ulimwezesha kijana kubembea katika matawi yake. Kisha mti huo kumwekea kivuli, kumpa matunda na matawi akajengea nyumba. Kadri kijana yule alivyokuwa mtu mzima aliuhitaji mti umpatie mahitaji mengi lakini kwa sasa mti ule haukuweza kumtekelezea mahitaji yake. Hatima ya mti ule ilikuwa ni kujitoa muhanga kwa kijana yule ambaye sasa ni mtu mzima ili aukate na atengeneze boti litakalomwezesha kusafiri. Kijana anaachana na ule mti na kuuona si kitu bali kisiki tu. Baada ya miaka mingi kijana yule akiwa mzee sasa anarudi mahala pale palipokuwa mti ule akitafuta mahala tulivu ili ajipumzishe. Mti ule ambao sasa ni kisiki unafurahi kujumuika na kijana yule kwa mara nyingine.

SURA YA PILI

2

KITENGO CHA FAMILIA

Kwa Nini Ni Muhimu?

Kazi Zake Ni Zipi?

SURA YA PILI **30**

Kitengo cha Familia: Kwa Nini Ni Muhimu? Kazi Zake Ni Zipi? **30**

Utangulizi 32
Kuelekea kuwa Mzazi 33
Athari za Watoto katika Kuimarika kwa Ndoa 34
Talaka na Takwimu za Watoto 36
Familia ya Mzazi Mmoja 38
Je Mzazi mmoja Anaweza kuwa mbadala wa Mwingine? 45
Umuhimu wa Familia katika Uislamu 49
Kipi kimeenda Kombo katika Familia za Waislamu? 54
Maendeleo ya Mtoto na Mifumo imara ya Elimu 56
Hadithi za Malezi Marekani 62
Mafunzo kutoka katika Mauaji ya Shule ya Columbine 66
Kufundisha Watoto Maadili: Malumbano ya Ukale na Usasa 67
Mlinganisho wa Familia katika nchi za Waislamu na Marekani 68
Hadithi za Waislamu Wanaoishi Uingereza 70
Athari za Umagharibi katika Malezi Ya Kiislamu 70
Malezi katika Nchi za Uingereza na Marekani 71
Wapi pa kukuzia Watoto? 75
Matatizo ya Kiutamaduni: Mashariki na Magharibi 75
Dhana Mbili zinazokosekana katika fikra ya Kimagharibi 77
Thamani ya Aqida Dhidi Ya Umuhimu Wake 78
Familia ni mfano wa Kilimo 80
Kazi za kufanya



Utangulizi

Familia ni nini na kusudio la uwepo wake ni lipi? Inafanya kazi vipi? Malengo yake ni yapi? Kitu gani kinaifanya iwe madhubuti? Inayumbishwa na nini? Ni michango ipi anayopaswa kutoa kila mwanafamilia ili familia ifanikiwe? Mafanikio yapimwe vipi? Majibu ya maswali yote haya yana athari ya moja kwa moja katika malezi bora na namna watoto wanavyolelewa. Katika sura hii, tunajaribu kuyachunguza haya na mambo mengine. Pia tutawafahamisha wazazi na wasomaji nafasi kubwa ya kitengo cha familia kwa mageuzi mema ya jamii. Familia sio kwamba inawabadilisha wanafamilia tu lakini hata jamii kwa ujumla. Vile vile tutachunguza kwa vipi malezi yanafanyika katika ulimwengu wa Waislamu na Magharibi.

Katika sura ya kwanza tuligusia wazazi katika masuala yanayohusu malezi bora, kwa vipi watu wanaweza jifunza malezi, na kwa vipi mitindo ya malezi tunayochagua kuitumia inavyoathiri aina ya watu na watoto wetu watakavyokuwa. Kuwa mlezi bora kunaenda mbali zaidi na hufungamana vyema na misimamo thabiti. Malezi yanahitaji ufahamu wa kutosha kuhusu kitengo cha familia na muunganiko wake. Ndiyo kiini kikuu cha sura hii. Sura hii pia itarejelea mara kwa mara kuhusu mapenzi, uangalifu na ulinzi. Familia yenye mazingira mazuri ya mapenzi huongeza katika upatikanaji wa matakwa ya wote watoto na wazazi. Malezi bora yanawaandaa watoto kuwa watu wenye kuwajibika na kujua wajibu wa raia.

Pia tutagusia masuala ya familia ya mzazi mmoja, talaka, mabadiliko ya ukubwa wa familia na masharti ya familia za sasa katika ulimwengu wa Waislamu. Udhaifu unaozikabili familia nyingi za Kiislamu unaweza kuonekana kuwa unatokana na uleaji wa watoto lakini ukweli ni kuwa umadhubuti wa viungo vya familia ni muhimu kwa kuimarisha na kuzipa nguvu familia. Familia endelevu haziwezi kuwepo bila ya viungo imara vya familia, na ukweli huu unadhihirika zaidi kwa ulimwengu wa Waislamu wanaopambana kujinusuru na anguko.

Baadhi wanasema maana ya neno“familia” kuwa ni kundi la watu wenye kuhusiana, wengine wanasema familia ni kama kitengo cha taasisi ya jamii, na wengine wanasema familia ni kama kundi linalojumuisha wazazi, na watoto wenye kuishi pamoja katika kaya. Ingawa kuna mitazamo mingi kuhusu familia, maana ya familia kwa watu wa kale kwa kiasi kikubwa zinahusishwa na ndoa na watoto. Kwa msingi huo kupitia ndoa muungano wa kifamilia huweza kupata mabadiliko, kwa kuwa ndoa si ubia wa watu wawili, lakini ni muungano wa familia mbili tofauti. Muundo wa taasisi ya familia za

kisasa (hususan kwa watu wa Magharibi) zimebadilika mno kwa kipindi cha miaka mingi, mabadiliko hayo ni kutoka familia za muundo wa kijamaa kwenda familia za muundo wa kindugu. Ziada ya hayo, ukubwa wa familia umebadilika (watu wamepunguza kuzaa).

Hata hivyo, familia zilitarajiwa kuwa kubwa zaidi ya jumla ya sehemu zake. Familia ni sehemu ya ukubwa wa tamaduni, na kwa ujumla, ndio utamaduni wenyewe. Ni muhimu kwetu kufahamu ukubwa wa majukumu tuliyonayo katika familia. Familia ni nyumba ndogo ya ibada, ni serikali ndogo, na ni shule ndogo ya wema.

Kuelekea kuwa Mzazi

Tunapofikiria kuhusu familia, kwa kawaida tunafikiri kuhusu wazazi na watoto. Mabadiliko ya mwanzo kwa wazazi ni kutoka wazazi wawili (watu wawili) kuelekea utatu (watu watatu) ni pale anapowasili mtoto wa kwanza. Kutokana na kuwasili kwa watoto wazazi wanaingia katika awamu mpya ya maisha. Wazazi wanapita katika vipindi vya kujiweka sawa kutokana na mabadiliko ya mifumo ya maisha inayoletwa na watoto (ikiwemo shida na fadhaa pamoja na shangwe na furaha). Mtoto anapozaliwa katika familia ya Kiislamu baadhi ya kaida za dini hufanywa kumkaribisha aliyezaliwa (Zaydan, Abdul Kareem, katika Kiarabu, 1993):

❒ **Soma adhana** masikioni mwa mtoto aliyezaliwa. Al-Hakim amesimulia kutoka kwa Abu Rafi kwamba alimuona Mtume (s.a.w) anasoma Adhana (Wito wa lazima wa sala) katika sikio la al-Hasan, mtoto wa Ali, wakati mama yake Fatma alipomzaa. Wito wa Adhana katika sikio la kulia na iqamah (wito karibu na sala) katika sikio la kushoto baada ya kuzaliwa unadhihirisha upweke wa Mungu, unathibitisha ujumbe wa Mtume Muhammad (s.a.w) na kuwakumbusha waumini kutekeleza sala kwa mtoto siku zijazo.

❒ **Mpe jina mtoto** baada ya kuzaliwa bila kuchelewa. Ni muhimu sana kumpa mtoto jina lenye maana nzuri (kwa kuwa unaandaa kupata mtoto bora). Hii hailazimishi kutumia jina la Kiarabu au jina la kihistoria, na linaweza kuwa jina la asiyekuwa Muislamu ambaye ni kigezo kikubwa kwa mtoto kuigiza. Maana ya jina lazima iwe nzuri, na inafaa sana kuzingatia utoaji wa jina rahisi kuandika na kutamka katika lugha zaidi ya moja.

❒ **Andaa aqiqah** (sherehe ya kuzaliwa) kwa mtoto. Aqiqah (katika Kiarabu) inarejelea mnyama anayechinjwa kama kafara ya aliyezaliwa. Mtume (s.a.w) alichinja kondoo dume mmoja kwa ajili ya wajukuu wake al-Hasan na al-Husayn. Hili hufanyika siku ya saba baada ya kuzaliwa kwa mtoto au baada ya hapo. Nyama inaweza kupikwa na watu wanaweza kualikwa kula kwenye karamu (walimah). Nyama ni lazima itumike kulisha familia na wanajamii, wote masikini na tajiri. Mnyama anapaswa awe mwenye siha na afya na asiwe na dosari. Wakati wa kumchinja mnyama husomwa dua ifuatayo, “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa ajili Yako na kutoka Kwako Ewe Mwenyezi Mungu, hii ni Aqiqah ya mtoto [unataja jina la mtoto].”

❒ **Ahmad na al-Tirmidhy** wanasimulia kuwa Mtume (s.a.w) amesema: “Kila mtoto amewekwa rehani kupitia aqiqah yake, ambayo lazima achinjiwe ndani

ya siku saba baada ya kuzaliwa, nywele za mtoto lazima zinyolewe, na mtoto lazima apewe jina." Hii imeshurutishwa na wala si hiari. Kwa kuongezea, Mtume (s.a.w) alimwambia mtoto wake Fatma azipime nywele za mtoto zilizonyolewa na kulinganishwa na vito vya fedha na gharama za vito hivyo itolewe msaada kwa masikini. Wayahudi wana desturi kama hizo lakini kawaida kwa Wakristo waliobatizwa ndio hukidhi vigezo vyao.

Athari za Watoto katika Kuimarika kwa Ndoa

Kitengo cha familia hupata uzito mara tu wanapopatikana watoto. Kuwa mzazi, ingawa ni heshima kubwa, si siku zote huwa tukio lenye kusisimua kama ambavyo baadhi ya wakati hutegemewa kuwa. Katika kuwa mzazi, wanandoa lazima watambue kuwa maisha hayatakuwa kama zamani kamwe, na wajiandae ipasavyo kukabiliana na vikwazo vilivyoko mbele yao. Wazazi watahitajika kutoa baadhi ya vitu wavipendavyo kwa ajili ya mtoto; na uwezekano wa kuwa mama au baba utaibua maswali. Haitakuwa rahisi, hasa kwa mama, kukabiliana na sulubu zisizokwisha za kuitwa na mtoto. Wazazi wa kiume wanaweza wasifike nyumbani ambapo yupo mke mchangamfu, mtoto mwenye furaha, na nyumba isiyo shida, na wazazi wa kiume (baba) wengi, wanaweza kuwaona wake wana kazi nyingi, hawana furaha, na wasioweza kuwahudumia (waume zao) kama mwanzo.

Umama unachosha sana akili, mwili na saikolojia. Kulala kuchache na kudumu kwenye uangalizi wa mtoto kutaathiri uimara wa mahusiano, na hatimaye kunaweza kupelekea ndoa kulegalega.

Masuala ya fedha yanakuwa muhimu zaidi kadri wanandoa wanavyoshughulikia nyumba na majukumu ya kazi katika kumlea mtoto. Hili linaweza pia kuwa na athari mbaya katika maisha ya ndoa. Maisha yanaweza kuwa ya fadhaa tu kwa wazazi waajiriwa. Baadhi ya wazazi wanaacha kuwapeleka watoto wao kwenye mashirika ya kulelea watoto na hufanya kazi kwa zamu ili muda wote mzazi mmoja aweze kuwepo nyumbani na mtoto. Hii haidhuru ni nzuri kwa mtoto, si nyepesi kwa mume na mke, ambao wanakuwa kama meli mbili zinazopishana usiku. Katika hali kama hizi uhusiano unaweza kutetereka kwa ghafla. Wazazi wanaweza kupata madhara madogo au mapambano yenye hitilafu ambayo huwapelekea kufikia tamati kwa kusaidiana kusafisha nyumba au kusafisha vyombo. Wazazi wanaojiona kuwa na hatia kwa kukosa muda wa kukaa na watoto wanaweza kuzidi kuwa na hatia endapo watapunguza "muda wa mahusiano yao ya kindoa" kufidia "muda wa mtoto." Wazazi wengine huwaharibu watoto wao kwa zawadi, pesa, na vyakula vya kipuuzi (kuliko kukaa nao), kuweka zaidi nguvu za fedha na jamii kwao wenyewe.

Nguvu kama hizi zitaitia ndoa kwenye majaribu, hasa ikiwa ukomo wa muda wa kukutana kwa wanandoa unageuzwa kuwa awamu za malumbano badala ya

Wacha familia zilindane zenyewe kwa zenyewe, na jamii itajilinda yenyewe

CONFUCIUS

Mama: Huwezi kuwa Kila Kitu Wakati Wote!
Hakuna Kitu kama Hicho kama Mama asiyekuwa na kazi.

Usijaribu kujifanya kuwa mwenza, mzazi, mfanya kazi za ndani, na muangalizi wa muda wote uliyekamilika, na kuwa na majukumu yote hayo kwa muda mmoja. Unaweza fanya vitu tofauti tofauti katika muda tofauti. Watoto wanabadili mfumo wako wa maisha, kwa hiyo pokea mabadiliko hayo, kuwa rafiki wa familia na kuwa mtu unayeweza kubadilika.

kuliwazana. Migogoro ya ndoa baina ya wazazi inaathiri sana watoto. Wazazi wengi wanakabiliwa na tatizo la kukosa mawasiliano kunakosababisha kukosekana kwa maelewano na migogoro isiyotatulika. Watoto wasihukumiwe kama "wazee wadogo" ambao wanategemewa siku zote kuwa kama watu wazima. Vile vile ni makosa kuwachukulia watoto kama wasumbufu, ni tabia zao kuchagiza na kuuliza maswali. Mahitaji yao ya kimwili, kisaikolojia na kimaendeleo lazima yatimizwe. Zifuatazo ni rai chache za kuwasaidia wazazi kudhibiti kipindi cha mpito kuelekea uzazi. Mabadiliko katika familia yana nguvu sana kutoka kuwa mume na mke na kuwa mama na baba kutatoa matumaini makubwa ya kupunguza fadhaa.

1. Panga ratiba ya siku au wiki ukae pamoja na mwenza wako tu. Hii inaweza kuhusisha matembezi, kufanya mazoezi, au kula chakula cha mchana pamoja. Kuongea naye kwa simu siku nzima au kuamka mapema kwa dakika chache na kusisitizana mambo muhimu inasaidia. Kubadilishana zamu za kulea watoto na wazazi wengine wenye kuaminika pia ni jambo zuri.

2. Badilishaneni matarajio na mwenza wako. Jadilini dukuduku lolote linaloweza kujitokeza kuhusiana na majukumu yenu mapya kama wazazi. Zungumzeni kuhusu athari za kuwa mzazi kwa afya zenu, uhusiano wenu, na kazi zenu.

3. Tenga muda wa kula chakula pamoja, kuabudu pamoja, kujamiiana, na kufanya mazoezi. Kwa kuwa mahitaji ya mtoto yatachukua muda wote, tenga muda wa mawasiliano, na masuala ya usafi wa nguo na vyombo vichafu yanaweza fanywa muda mwingine.

4. Elezea yanayokuchukiza na usiogope mgogoro utakaojitokeza. Chukulia mapambano ndiyo kiashiria kwamba jambo fulani si sahihi kwenye mahusiano, na ombeni ushauri kwa pamoja.

5. Zungumzeni na rafiki anayeaminika au mfanyakazi mzoefu ambaye ameshapitia katika mabadiliko hayo na kuwa mzazi. Hii inasaidia kupunguza fikra za ubaguzi. Hakikisha unazungumza na mtu wa jinsia sawa, na usizungumze jambo lolote kumuhusu mwenza wako ambalo ni la kibinafsi.

Kulea kunahusisha ushirikiano usiotenganishwa baina ya baba na mama – kila mmoja akiwa na kazi tofauti yenye wajibu wa kukamilishana. Hata wanapocheza na mtoto wao, wazazi wanatoa mahitaji tofauti. Mama humkumbatia mtoto, humfariji kwa kumuweka kifuani pake, na humjaza upendo na mahaba. Baba humtoa kifuani pake, humrusha juu angani (baada ya umri wa miaka miwili tu) na kumdaka, humwachia apande mgongoni na kupiga naye mwereka sakafuni. Mazoezi yote haya yanamfundisha mtoto kujiamini na kumwacha huru mtoto kwenye udhibiti mkubwa wa fujo, shari, na hatari. Wazazi wote wanapaswa kutimiza wajibu wao katika kuikuza haiba ya mtoto. Ukiwa kama baba, kulea ni kushirikiana na mke wako; wajibu wako kama baba mlinzi hauna mbadala. Unapaswa kujua wakati wa "kulea" na wakati wa "urafiki" – nayo ni kwamba, ni wakati gani wa kusimama kama mlinzi na wakati gani wa kumpa fursa mtoto wako ya "kupata mafunzo".

Bila kujali namna watoto wanavyoathiri hisia za wazazi kuhusu ndoa, watoto huamsha ari ya uwajibikaji zaidi katika mahusiano ya ndoa. Mchoro Na. 2.1 unaelezea kwa uwazi kwamba kadri wanandoa wanavyokuwa na watoto wengi, inaelekea zaidi kwamba wataendelea kudumu kwenye ndoa. Wazazi wenye watoto wanaowategemea wanailinda ndoa yao kwa pamoja ili kudhibiti upatikanaji endelevu wa maisha bora ya watoto wao. Wazazi (hasa mama) wenye watoto wadogo wanahisi kupata nguvu zaidi za kuishi kwenye ndoa, hata kama hawana furaha. Ingawa watoto hupunguza furaha, lakini kwa yakini huongeza uimara, kwa kuwa nguvu zaidi huwepo ili kuepusha talaka.

Talaka na Takwimu za Watoto

Fig 2.1 (Knox and schacht 1997)



Kiasi cha talaka kati ya wanafamilia wenye watoto ni asilimia 40 ambacho ni kiwango kidogo ukilinganisha na wanafamilia wasiokuwa na watoto (McKinley Irvin Family Law 2012)

- Asilimia arobaini na tatu (43%) ya watoto wanaokulia Marekani leo hii wanakua bila uwepo wa baba zao.
- Asilimia sabini na tano ya watoto wenye wazazi walio achana wanaishi na mama zao.
- Asilimia ishirini na nane ya watoto wenye wazazi walio achana wanaishi ndani ya vijumba huku wakiingiza kiasi ambacho kiko chini ya mstari/ kikomo cha umaskini.

- Nusu ya watoto wakimarekani watashuhudia mvunjiko wa ndoa za wazazi wao. Na baadhi kati ya hawa, wataona pia mvunjiko wa ndoa za pili/ ndoa nyengine za wazazi wao.

(http://www.mckinleyirvin.com/Family-Law-Blog/2012/October/32-Shocking-Divorce-Statistics.aspx)

Asilimia Ya Wanandoa Wanaotalikiana kwa Idadi Ya Watoto

Katika kitabu chake Furaha Kuu ya Taifa (Gross National Happiness), Arthur Brooks anaelezea kwamba katika nchi ya Marekani wazazi wenye watoto wanakuwa na furaha zaidi kuliko wasio na watoto. Sababu moja ni kuwa watoto huchangia kuyapa thamani maisha. Watu wa dini walio kwenye ndoa (ambao kwa kawaida huhudhuria kanisani mara mbili kila wiki) ni bora zaidi kuwa na furaha kuliko wasio kwenye ndoa sio kwa sababu wanaweza kuwa matajiri, lakini kwa sababu maisha yao yametajirishwa (Brooks, 2008).

NANI ANAPASWA KUFANYA NINI

Wazazi: Kutengeneza furaha ya nyumba

Watoto: Jifunze kutoka kwa wazazi wako, na wasaidie.

Bibi na Babu: Kuunganisha familia za vizazi tofauti.

Marafiki: Kusaidia wazazi.

Walimu: Kuelimisha watoto.

Waleta Mabadiliko: Kuwaonesha wazazi namna nzuri ya kulea.

Kuishi na Watoto ni Hatua ya Kupita Tu

Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi! (Qur'an, 94:5-6)

Ingawa wazazi wa mtoto wakati mwingine hudhani kuwa kukesha usiku hakutaisha, kabla ya kulitambua hilo, watoto wao wanakua na kuondoka. Tofauti na uhusiano wa wanandoa, uhusiano wa mzazi na mtoto pasipo kizuizi unaelekea kwenye utengano. Kama ambavyo wanandoa walikuwa peke yao kabla ya kupatikana watoto, watakuwa tena peke yao baada ya watoto kuondoka. Uzazi ni kipindi pekee muhimu katika ndoa na katika maisha. Kwa wazazi, muda wanaoutumia kuishi na watoto unachukua kiasi cha moja ya tatu (theluthi) ya maisha yao na zaidi ya nusu ya maisha yao ya ndoa. Hata hivyo, ukishakuwa mzazi mara moja, basi ujuwe utakuwa mzazi daima. Uhusiano unaendelea hivyo hivyo hata baada ya watoto kuingia kwenye ndoa na kuhama nyumbani. Vile vile, uhusiano lazima uendelee hata kama watoto wako karibu au umbali wa maelfu ya maili. Wazazi hukua na kuingia katika ngazi nyingine ya kuwa babu na bibi.

Ukubwa wa Familia sasa na Baadaye katika Nchi ya Marekani na Uingereza

Kupungua kwa ukubwa wa familia kumeathiri mahusiano ndani ya kitengo cha familia. Kwenye ndugu wachache, watoto wanaweza kupata uangalizi zaidi kutoka kwa wazazi. Kushikana kwa familia kunakuwa na nguvu na imara zaidi. Wakati huo huo, watoto wanaweza kukosa ujuzi unaotokana na kulea ndugu zao wadogo. Kizazi cha watoto wenye uwezo nchini Marekani (Wamarekani Milioni 77 waliozaliwa kati ya mwaka 1946 na 1964), kama wazazi wenye uwezo, walikuza kiasi cha watoto Milioni 80 tu. Wakati kipato chao na elimu yao vikiwa juu, ukubwa wa familia zao ni mdogo. Vyombo vya kudhibiti uzazi na kutoa mimba vinapatikana kwa wingi sana, vinarahisisha kuwa na watoto wachache. Katika siku za uzeeni, wazazi huwaza kuhusu watoto kama vyakula vitamu: vichache vya mwanzo haviwezi kuwa sawa, lakini kila siku unaweza kuandaa vingine!! Hivi sasa familia nyingi zina mtoto mmoja au wawili tu, hivyo wanajishughulisha na wao tu na wanawapatia uangalizi mkubwa mno. Ukubwa wa familia pia umepungua kutokana na wazazi wote wawili kuwa ni wafanya kazi ama familia kuhama hama, na kumekuwa na umbali baina ya wazazi na ndugu. Kwa Uingereza., chini ya kizazi kimoja pamekuwa na ongezeko la wazazi kuwa na mtoto mmoja.Ndani ya mwaka 2012, asilimia 47 ya familia zina watoto mmoja mmoja, asilimia 39 walikua na watoto 2 na asilimia 14 walikua na watoto 3 au watoto zaidi (Ofisi ya Takwimu za Taifa). Asilimia 20 ya wanawake waliozaliwa mwaka 1964 hawana watoto, ukilinganisha na 12% ya wanawake waliozaliwa mwaka 1937(BBC 2010).

Katika mwaka 1960, asilimia 77 ya wanawake wa Kimarekani walihama nyumbani, wakaolewa, na kupata watoto wakiwa na umri wa miaka 30. Mwaka 2000 kwa wale waliozaliwa mwaka 1960 walikuwa wamefikia umri wa miaka 40, asilimia 46 ya wanawake pekee wa Kimarekani, walihama nyumbani, waliolewa na wengine walikuwa na watoto wakiwa na umri wa miaka 30!(Kantrowitz na Tyre 2006). Wakati umri wa wastani wa Wamarekani walio katika ndoa ya kwanza kwa mwaka 2000 ilikuwa ni 26.8 kwa wanaume na 25.1 kwa wanawake, Mwaka 1960 ilikuwa 22.8 kwa wanaume na 20.3 kwa wanawake (Pew Research Centre 2011). Umri kwa ndoa ya kwanza uliongezeka kuanzia hapo kwa mujibu wa Shirika la Sensa la Marekani, katika mwaka 2003 wastani ulikuwa 29 kwa wanaume na 26.6 kwa wanawake. Nchini Uingereza na Wales, wastani wa umri wa ndoa ya kwanza kwa wanawake kati ya mwaka 1930 na 1960, kabla ya kuanza kupanda (Kutoka Ofisi ya Taifa ya Utafiti 2010). Umri wa wastani wa ndoa kwa Uingereza na Wales ilikuwa kubwa ukilinganisha na Marekani. - kwa mwaka 2012 ilikuwa 31 kwa wanume na 29.1 kwa wanawake (Kutoka Ofisi ya Taifa ya Utafiti 2014). Wastani wa umri kwa wanawake walio na watoto uliongezeka tangu miaka ya katikati ya 1970.

Familia ya Mzazi Mmoja

Zaidi ya mtoto mmoja kati ya watoto watatu nchini Marekani wanaishi chini ya familia ya mzazi mmoja (watoto milioni 24.6 - asilimia 35- hiyo ni kwa mwaka 2013 kwa mujibu wa kituo cha kuhesabu kumbukumbu za watoto) ingawa wengi wao ni akina mama, idadi ya akina baba pweke iliongezeka. kati ya mwaka 1960 na 2011. Idadi ya kaya zilizokuwa zikiongozwa na wababa pekee ziliongezeka mara tisa zaidi kutoka 300,000 mpaka kufikia zaidi ya milioni 2.6 mwaka 2011. Wakati kaya zenye mama pekee ziliongezeka mara nne zaidi kutoka watu milioni 1.9 mpaka kufikia watu milioni 8.6 (kutoka kituo cha PEW 2013). Nchini Uingereza asilimia 30 ya watoto wanatoka katika kaya zenye mzazi mmoja. Nyingi ya kaya hizo ziko chini ya akina mama pweke (asilimia 28.1 ya watoto wote wanatoka kwenye kaya za akina mama pweke). Uingereza ndio inayoongoza kwa kiasi kikubwa kuwa na akina mama pweke ukilinganisha na mataifa mengine barani Ulaya –asilimia 18.5 ya kaya nchini Uingereza

zenye watoto basi wako na mama pweke katika kaya hizo, ukilinganisha na wastani wa asilimia 9.1 katika bara la Ulaya. Kwa ujumla asilimia 20.4 ya kaya nchini Uingereza zina mzazi pweke. (kwa mujibu wa European Commission 2014). Familia za mzazi mmoja zinaongezeka na zipo sababu kubwa mbili juu ya ongezeko hilo: Talaka na watoto wanaozaliwa nje ya ndoa. Kwa mwaka 2013, asilimia 40.3 ya watoto waliozaliwa nchini Marekani walikuwa wamezaliwa na wazazi walio nje ya ndoa (1,595,873). (Mfumo Muhimu wa Taifa wa Takwimu 2015).

Ndoa (na masharti yake yote) haipendwi na baadhi ya wenza wanaothamini kuishi bila ya kufunga ndoa (kuishi kinyumba). Kwa mwaka 2009 nchini Marekani, watoto takriban milioni 19.9 wamekuwa wakiishi na wazazi wao wa kike ambao hawakufunga ndoa, asilimia 21 (sawa na watu milioni 4.3) walikuwa wakiishi na wazazi wasiooana. Ukilinganisha na watoto milioni 5.1 waliokuwa wakiishi na wazazi wao wa kiume ambao hawakufunga ndoa, asilimia 54(sawa na milioni 2.7) walikuwa wakiishi na wazazi wa kiume ambao hawakufunga ndoa na wenza wanaoishi nao, kati ya hao milioni 2.4 ni watoto wa kuzaliwa na mama zao wa damu.(Takwimu ya Ofisi ya Sensa ya nchini Marekani,2009). Kwa mujibu wa kituo cha uchunguzi cha Pew (2013) imegundulika akina baba pweke wamebaki wakiwa na wenza wao wakiishi kinyumba kuliko akina mama pweke.(41% kwa 16%). Nchini Uingereza familia za wenza wanaoishi kinyumba bila kuoana zimekuwa zikiongezeka kwa kasi sana kuliko aina nyingine yeyote ya familia- zimeongezeka kwa takriban asilimia 30 kati ya mwaka 2004 mpaka 2014.Inakadiriwa takriban watu milioni 3 wa jinsia tofauti wanaishi kinyumba na watu 84,000 wa jinsia moja wanaishi kinyumba nchini Uingereza hiyo ni kwa mwaka 2014. Kwa pamoja wanafanya idadi ya 16.4% ya familia zote nchini Uingereza (Ofisi ya Taifa ya Takwimu).

Mtazamo wa kuishi kinyumba: kwa mujibu wa CDC , zaidi ya mmoja kati ya wanne katika uzao wa kwanza wa wanawake kati ya umri wa miaka 15-44 ni kati ya wenza wanaoishi kinyumba (asilimia 26 ni kati ya mwaka 2011-2013,mpaka kuanzia asilimia 22 mwaka 2006-2010 na asilimia 12 mwaka 2002.) Kwa Uingereza na Wales, karibu theluthi ya waliozaliwa hai (asilimia 31)waliosajiliwa kwa mwaka 2013, walikuwa ni zao la wenza wanaoishi kinyumba (Ofisi ya Taifa ya Takwimu). Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na chuo cha wataalamu wa wototo waliripoti kwa mwaka 2014 walifanya ulinganishi kwa wenza waliooana baada ya kuzaliwa mtoto, wale waliokuwa wakiishi kinyumba walikuwa ni mara nne zaidi ya wale ambao huachana baada ya miaka mitatu baadaye. Hatari hiyo inapishana mara mbili kwa Wamarekani wenye asili ya Waafrika, na mara tatu kwa Wamarekani wenye asili ya Mexico na kukaribia mara 8 miongoni mwa Watu wa Wamarekani wenye asili ya Ulaya .

Kati ya kaya milioni 123.2 nchini Marekani kwa mwaka 2014

- ❒ Milioni 59.6 walikuwa ni wanandoa
- ❒ Milioni 7.9 walikuwa ni wenza wasiooana wa jinsia tofauti
- ❒ Milioni 34.2 ni kaya yenye mwanachama mmoja

(CPS DATA, U.S CENSUS BUREAU)

Kati ya kaya milioni 26.7 nchini Uingereza kwa mwaka 2014

- ❒ Milioni 12.5 walikuwa ni wanandoa
- ❒ Milioni 2.3 walikuwa ni wenza wasiooana wa jinsia tofauti
- ❒ 61,000 familia ya wenza wa jinsia moja
- ❒ Asilimia 28 ni kaya yenye mwanachama mmoja

(OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU 2015)

Suala la "Talaka Bila Kosa"

Talaka bila kosa ni aina ya talaka ambapo wenza wote wanakubali kusitisha ndoa na hakimu hahitaji kupewa sababu yoyote. Baadhi ya watu wanataka kuondoa aina hii ya talaka. Katika kujibu ongezeko la viwango vya talaka, Ronald Reagan, kisha Gavana wa Califonia, na yeye mwenyewe alitaliki, alisaini sheria ya kwanza mwaka 1969 ambayo iliwaruhusu wanandoa kuwa na talaka ya bila kosa. Baadaye, wanandoa walilazimika kuthibitisha kwamba mmoja wao amefanya kosa ili hakimu avunje ndoa yao (sababu kubwa zilizotolewa sana kuhusu talaka ni zinaa, matusi na kutelekeza). Wanandoa hukata shauri la kuachana kupitia mahakamani au kukodi wapelelezi binafsi ili kumpeleleza kila mmoja. Muswada wa bila kosa uliandaliwa ili kupunguza ukali na makosa baina ya wanandoa wanaotaka kutalikiana. Iliwaruhusu wenza ambao kwa pamoja walitaka kuvunja ndoa ili waweze kuivunja kwa amani; hata kama mmoja wapo alipinga talaka, mwingine anaweza kuipata bila ya kumshitaki mwenziwe kwa kufanya makosa. Kila jimbo, isipokuwa New York, ikifuatiwa na Califonia ziliruhusu talaka bila kosa. Katika miaka mitatu baada ya kuruhusiwa kwa talaka bila kosa, kiasi cha talaka kiliongezeka.

LELAND, 1996

Mzazi mmoja hukosa utulivu wa kutosha na manufaa ya mshauri mwenye moyo wa utiifu:mzazi mwenza

Tunasisitiza kuwa kwa sababu tu mtoto anazaliwa nje ya ndoa, hii haifanyi kila mzazi asiwe mzazi. Kuwakuza watoto kama mzazi pweke kunahitaji bidii ya kutosha na kujitegemea sambamba na akili yenye fikra madhubuti. Kutimiza wajibu wa majukumu ya kazi na usimamizi wa nyumba si mwepesi. Ulezi wa mzazi pweke ni mgumu na wenye kuchosha, akili na hisia. Ulezi wa mzazi pweke ni wenye uhitaji zaidi kuliko ulezi wa wazazi wawili. Mzazi pweke anapaswa kutekeleza majukumu mawili (lile la mama na la baba): Yeye pekee anabeba jukumu la usimamizi na maamuzi yote ya fedha, kusimamia sheria zote za kaya, na kushughulikia migogoro yote ya watoto na tabia chafu, hata pawe na utimilifu wa kiwango gani bado upweke wa kuwa mzazi mmoja utakuwepo tu. Hii haimaanishi kusema kuwa mambo yanakuwa mazuri siku zote kwa familia za wazazi-wawili (mbali na hayo), lakini kazi ni ngumu kwa mzazi pweke, na mahitaji ya hisia zao ni vigumu kutimizwa. Wazazi wote wanapaswa kuwa na akili zenye mtazamo thabiti, hasa mzazi pweke.

Kwa watoto, kulelewa na mzazi pweke ina maana kwamba watakosa matunzo na uangalizi wa mzazi wa pili (baba au mama). Bila shaka mzazi anayekosekana asiwe mzazi ambaye hayupo. Pamoja na kutalikiana, bado wazazi wote wanaweza kutekeleza sehemu muhimu ya maisha ya watoto wao. Watoto wenye mzazi pweke vile vile watakosa mfumo wa msaada wanaoupata watoto wenye wazazi wawili. Wazazi pweke huwapenda na kuwatunza watoto wao, na kila wanapokuwa na elimu kubwa, ujuzi mwingi na mwamko sana, ndivyo wanavyopata maumivu kidogo. Hapa chini kuna taarifa za kweli kuhusiana na athari hasi za nyumba ya mzazi pweke kwa watoto

(HARPER na MCLANAHAN, 2004)

- ❒ Nyumba za wazazi pweke zina uwezo mdogo wa kusimamia ustawi mzuri wa wanawake na ujana wa watoto ikilinganishwa na wanandoa waliooana kisheria.
- ❒ Wasichana wasiolelewa na wazazi wao wawili huwa na ashiki kubwa au hamu kubwa ya jimai kipindi chao cha ujana.
- ❒ Watoto na vijana wasioishi pamoja na baba zao wa kuwazaa wako katika hatari kubwa ya kusumbuka kimwili, kiakili, au kusumbuka kingono.
- ❒ Wanafunzi wa shule za sekondari wanaotoka kwenye nyumba zilizovunjika husababisha matatizo mengi shuleni.
- ❒ Katika baadhi ya jamii, watoto wa mzazi pweke hufanya uhalifu zaidi.
- ❒ Watoto wa mzazi pweke ni rahisi zaidi kukosa heshima au kutengwa, na ni rahisi zaidi kuishia gerezani.

Miongozo ya malezi bora iliyoorodheshwa kwenye kitabu hiki inatumika kama ilivyo kwa familia ya mzazi pweke ni hivyo kwa wazazi-wawili. Wazazi wote wanakumbana na matatizo yanayofanana lakini familia za wazazi pweke zitalazimika kumakinikia zaidi katika mambo yafuatayo:

1. **Kuonesha uwezo binafsi.** Ikiwa wazazi watafarakana, ulimwengu wa watoto hauto tengemaa kwa kuwa hakuna mzazi wa pili atakayeurekebisha. Hivyo, mzazi pweke anapaswa kuitathmini hali hiyo na kujiamini na kujitegemea. Hali za akili na fikra zao lazima ziwe madhubuti.

2. **Kutimiza majukumu mawili.** Jukumu la mzazi anayekosekana linapaswa kutimizwa. Baba, kwa mfano, wanapaswa kuwa karibu zaidi na watoto wao kifikra na kiimani. Viko vitabu vingi vya mtu kujisomea mwenyewe vinavyoweza kuwaongoza wazazi katika hili.

3. **Kuongeza heshima binafsi.** Watoto lazima wasijisikie aibu kwamba wana mzazi mmoja tu, na lazima wajue kuwa ni wazuri kama alivyo mtu anayetoka kwenye nyumba ya wazazi wawili. Wazazi pweke hulazimika kuwapatia watoto wao malezi mazuri na maisha ya familia yenye furaha. Wafundishe watoto kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alifiwa na wazazi wake wote wawili alipokuwa mdogo. Kuwa makini na kuwaendekeza sana watoto kwa ajili ya "kutimiza" kwa namna fulani kukosekana kwa mzazi wa pili, na usiwaruhusu wakuendeshe kwa kukufanya ujihisi kuwa mkosaji.

4. **Mawasiliano mazuri.** Mawasiliano ya kudumu baina ya mzazi na mtoto ni lazima. Maisha ya wote, mzazi na mtoto yatakuwa mepesi kwa kutengeneza upendo, mahusiano yenye moyo wa kupendana, na nyumba yenye mazingira ya kusaidiana. Kwa kusema haya, kuwa mzazi pweke hakumaanishi kuwa tunatakiwa kuwalea watoto wetu pasipo msaada wowote. Inaweza kuwa yenye kufurahia na mafanikio ya kawaida kama yalivyo ya familia za wazazi wawili (au yanaweza kuwa bora zaidi, ikiwa kwamba familia nyingi za wazazi wawili zina kiwango cha juu cha migogoro na mivutano ya ndoa).

Mawasiliano ya kudumu baina ya mzazi na mtoto ni lazima. Maisha ya wote, baba na mtoto yatakuwa mepesi kwa kutengeneza upendo, mahusiano yenye moyo wa kupenda, na nyumba yenye mazingira ya kusaidiana.

KANUNI ZA KUFUATA ILI KUWA MZAZI PWEKE MWENYE MAFANIKIO

Kilichoorodheshwa hapa ni mfululizo wa matendo ambayo mzazi pweke anaweza kufanya ili kulea watoto kwa mafanikio na kupunguza mapambano kati ya mzazi na mtoto.

- ❒ Pandikiza mtandao wa kirafiki na mahusiano. Tengeneza marafiki wazuri na waalike na watoto wao kwenye mikusanyiko ya kijamii na mlo wa pamoja na watoto wako. Zijue familia zingine za mzazi pweke (kumbuka kuwa japokuwa wewe ni mzazi pweke,lakini haupo peke yako). Rafiki wa karibu wanaweza kukupa msaada wa kifikra, mwongozo, msaada wakati wa dharura, utunzaji wa watoto, na sikio la huruma. Kuwa mtambuzi kwa wote unaopanga nao urafiki, chagua watu walio waangalifu, waaminifu, wenye dhamana, na wakweli ambao watakuwa nawe wakati wa shida. Ikiwa una familia kubwa, basi tekeleza masharti haya na mtembelee mmoja baada ya mwingine mara kwa mara. Usijisikie aibu kubadilishana mzigo wako wa kulea na wana familia na waombe msaada unapouhitaji.
- ❒ Andaa siku tofauti za kutembea na kufurahi pamoja na watoto wako. Weka kumbukumbu za matukio ili kukukumbusha wewe na watoto wako nyakati na mambo yenye kufurahisha.
- ❒ Shirikiana na watoto wako katika kufanya maamuzi na kutatua matatizo. Hii itakuza hali ya kujithamini na watajihisi kuwa nao ni sehemu ya wanafamilia wenye thamani. Katika familia za mzazi pweke, msaada na ushiriki wa kila mtoto unahitajika kila siku. Kufanya kazi kwa pamoja na kupeana majukumu sawa sawa kutapunguza uzito unaokukabili.
- ❒ Usiziruhusu hasira zako au wasiwasi wako kuwaathiri watoto wako. Kama unaweza kuuona ulimwengu kama wauonavyo wao, utagundua kuwa watoto wanajihisi kutokuwa salama. Watoto wanahofu kwamba ikiwa jambo litatokea kwa mzazi, watakuwa wapweke ulimwenguni. Kumbuka kumrudia Mungu kwa mahitaji yako yote, na baada ya kufanya yote uwezayo, yawache matatizo yako na woga wako kwenye mikono ya Mungu.
- ❒ Ikiwa umetalikiwa usiwalazimishe watoto katika kuchagua upande (wa kufuata). Usiwaulize watoto wako kuhusu kuchagua baina ya “mzazi mwema na mzazi mbaya”. Watoto wana uaminifu mkubwa mno kwa wazazi wote wawili, na wanajisikia kuwa na hatia ikitokea kumkataa mmoja na kumpendelea mwingine.
- ❒ Juu ya yote, kuwa na hakika na mtegemee Mungu. Kumbuka kuwa mzazi pweke mwenye ujuzi mzuri wa kulea anaweza kuwakuza watoto kwa mafanikio bila ya mwenza. Fanya hivi kwa kutengeneza mfumo mzuri wa msaada – kundi la marafiki, ndugu na jirani. Kukuza watoto wazuri hakuhusiani na idadi ya wazazi, lakini ubora wa malezi na ubora wa mtazamo wa wazazi kuhusu ulimwengu.

ATHARI YA UMAMA PWEKE KWA MITUME

Mussa, Issa Na Muhammad

Baadhi ya mitume mashuhuri waliopelekwa kwa wanadamu wamelelewa katika nyumba za mzazi pweke. Hapa chini tunasimulia kwa ufupi habari za mama wa mitume wanne hawa. Uwezo na busara za wanawake hawa mashuhuri ni mwongozo kwa wazazi wote.

Nabii Mussa

Tulimfunulia mama yake Mussa kwa kumwambia:

> *Mnyonyeshe. Na utakapomkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume (Qur'an, 28:7).*

Alikuwa mama yake Mussa, akimuamini Mungu juu ya kumlea mwanawe, aliyemtupa Mussa kwenye mto. Baadaye alimlea mwenyewe baada ya kukataa kunyonyeshwa na wanawake walioajiriwa kunyonyesha mtoto wa mtu mwingine kwenye nyumba ya Firauni. Maamuzi makubwa ya muhimu aliyoyafanya! Alimuamini Mungu kwa maisha ya mtoto wake, na kupandikiza sifa za uongozi za Mtume huyu mashuhuri!

Nabii Issa

Na angalia pale Malaika waliposema:

> *Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuteua na akakutakasa, na akakutukuza kuliko wanawake wote (Qur'an, 3:42).*

Issa ni mtoto asiyekuwa na baba aliyezaliwa na Bibi Mariam binti Imran. Bibi Maryam alikuwa ni mama pweke aliyepambwa na upendo wa hali ya juu, kujitolea, na uadilifu. Anasimuliwa na Mwenyezi Mungu katika sura nzima ndani ya Qur'an kwamba ni mwanamke msafi mteule na mwenye imani thabiti.

Nabii Muhammad

Muhammad alizaliwa yatima na mama yake, Aminah binti Wahab, alikuwa ni mama pweke. Alimlea kwa miaka sita, kipindi ambacho haiba na tabia zake za kupigiwa mfano zilitengenezwa. Ujasiri, upendo, uaminifu, ubunifu na kujitegemea alisakinishwa navyo na mama yake.

Athari za umama hazipimiki! Ni sifa kiasi gani tunazoweza kuwapa mama zetu kwa mchango wao wa thamani mno katika kulea?

- Watoto wanakuja ulimwenguni wakiwa wanafahamu mama zao ni nani, mama huwaambia watoto baba zao ni nani!
- Imamu Ahmad anasimulia kuwa mtu mmoja alikuja kwa Mtume (s.a.w) na kusema, "Nimekuja kuomba ruhusa kwako ili nifanye hijrah (kuhama) na nimewaacha wazazi wangu wote wawili nyuma yangu wakilia." Mtume (s.a.w) akasema, "Rudi, na njia hiyo hiyo uliyofanya walie, wafanye wacheke."
- Imesemwa kuwa wakati wa mazishi ya mama yake, mara moja Muislamu alilia na kusema, "Kwa nini nisilie wakati moja ya mlango wangu wa kuingilia Peponi sasa umefungwa?"

Je Mzazi mmoja Anaweza kuwa mbadala wa Mwingine?

Mama hawezi kuwa mbadala wa baba, na baba hawezi kuwa mbadala wa mama. Mtoto (mchanga) anayetegemea upendo wa dhati wa wazazi wote hukua vyema. Mama hutoa penzi lisilokoma, wema, kunyonyesha, kuvumilia na kusubiri. Baba hutoa nguvu, kuwajibika, kupaza sauti, harufu tofauti, na busu mashavuni: vishawishi vyote kwa mtoto (mchanga). Kwa ujumla, kukosekana kwa mama ni pigo zaidi kwa watoto kuliko kupotea kwa baba. Mama anaweza kutoa matunzo na upendo, na matumaini yake yanaelekea kuelekezwa zaidi kwa watoto. Mama wanaokaa nyumbani muda wote wanashughulikia zaidi watoto, na watoto kwa namna nyingi wanakuwa karibu na mama. Watoto huwachukulia kama jukumu lake la kila siku. Ana hati miliki na uwezo wa kuwateka watoto kwa upendo na amani ili kuwafanya wafanikiwe katika maisha (George Tremblay na Allen Israel, 1998).

Kuna mitazamo potofu kuwa mtoto wa kiume anamuhitaji baba zaidi kuliko mama, na mtoto wa kike anamuhitaji mama zaidi kuliko baba. Baba ana umuhimu kwa mtoto wa kike kama alivyonao kwa mtoto wa kiume, haidhuru kwa namna fulani kwa njia tofauti. Hivyo hivyo, mama ni muhimu sana katika kuwalea watoto wake wa kiume. Baba huwapa watoto wa kike hisia za kuwa na nguvu, msaada, na ulinzi. Mtoto wa kike anamuhitaji baba kwa kuwa anaweza kufanikiwa kujinasibu kama wanaume. Vinginevyo, wanaume wanaweza kuonekana kwake kama ni watu wa ajabu au wenye kutisha au wenye mvuto sana (wa kimapenzi).

Je, akina mama wanaweza kutekeleza majukumu ya baba kwa watoto wao wa kiume wasiokuwa na baba? Jibu ni kuwa hawawezi na hilo si lazima. Haiba za watoto zinatengenezwa kiasi kwamba haidhuru hawawezi kukumbuka muda wote kuwaona baba au mama zao, wanaweza kujenga taswira za waziwazi jinsi wazazi wao walivyokuwa na kuwaelezea kwa undani kabisa. Watoto wanaweza kuunganisha pamoja baba kamili kutoka kwenye chembe ndogo ndogo na vipande vya haiba za watu wengine. Mama anapokuwepo, anachoweza kufanya kwa mtoto wa kiume asiyekuwa na baba ni kumsaidia kutengeneza taswira ya baba yake kwa kumpatia fursa za kuwa pamoja

na babu zake, wajomba, na binamu (ndugu waliozaliwa na ndugu wa baba na mama). Pia, anaweza kuwatambulisha watoto wake wa kiume kwa rafiki na mwalimu wa kiume wa shule mwenye kuaminika, waziri au Imamu, katika mazingira salama na yenye kusimamiwa. Chini ya mwongozo wake wanaume hawa wanaweza kutoa vigezo vizuri vya wajibu wa mwanamume kwa mtoto wake wa kiume.

Kipi Hasa cha Msingi?

Miaka Arubaini kutoka sasa, haitakuwa muhimu akaunti yako ya benki ina kiasi gani, unaishi kwenye nyumba ya aina gani, au uliendesha gari ya aina gani…Cha msingi hasa ni umekuwa muhimu kiasi gani katika maisha ya mtoto na mjukuu.

UKUMBUSHO KUHUSU UISLAMU NA TALAKA

Moja ya sababu kubwa ya kuibuka kwa familia za mzazi pweke ni ongezeko la kutalikiana. Talaka imekatazwa katika baadhi ya tamaduni na dini (talaka ilikuwa haramu nchini Brazil mpaka mwaka l977, sheria ya Wahindu (Wabaniani) iliharamisha talaka, na talaka kwa Wakatoliki (Wakristo) iliharamishwa Ufilipino). Uislamu unapinga talaka lakini pia unaruhusu (kutokana na kanuni fulani). Kabla ya talaka Muislamu lazima apitie hatua za mapatano na usuluhishi wa kifamilia baina ya wanandoa. Uislamu unataka ndugu wenye hekima na waaminifu ili wafanye jitihada kubwa ya kunusuru ndoa, hasa ikiwa itawaathiri watoto. Mtume (s.a.w) amesema: “Halali kubwa inayochukiza mbele ya Mwenyezi Mungu ni talaka” (Ibn Majah). Kilichosemwa, Uislamu na imani zingine zinatambua kuwa ndoa zinashindwa. Inasikitisha lakini inatokea. Wazazi lazima wafanye kila linalowezekana ili kuzilinda ndoa zao. Talaka inapotokea na watoto kuathirika, wazazi lazima wawe na Imani na wawahurumie watoto:

- ❒ Wanapoachana na kuoana tena, watoto lazima waambiwe kwa uangalifu mkubwa ukweli wa yaliyotokea, pasipo kufunika mambo au kubuni hadithi. Wazazi wanatakiwa kuweka wazi sababu za kutengana, na kusisitiza kuwa si kosa la watoto na kuwa bado wanawapenda watoto wao. Mzazi asije kutoweka ghafla tu pasipo kutoa ufafanuzi. Inaweza kuwapa watoto uchungu. Mzazi anaweza kuamini kuwa anawasaidia watoto ili kuzuia maumivu, lakini watoto hutafsiri kuwa mzazi hawapendi vya kutosha hata kiasi cha kushindwa kuwaeleza kilichotokea na angalau kusema kwa heri.

- ❒ Usiwalazimishe watoto kukubali mtazamo wa mzazi yeyote au kuchagua upande.

Wakati wanapohusishwa wazazi wa kambo na familia za kulelewa, haisaidii sana kujaribu kuwasukuma watoto kuwakubali watu ambao si ndugu zao wa damu kama walivyokuwa wa mwanzo. Wanaweza kuwa na mivutano sana, wachoyo, na washindani kuishi nao kadri uhusiano unavyokuwa. Ni vizuri zaidi kwa mtoto kumkubali mzazi wa kambo kama "mume mpya wa mama yangu" (au "mke mpya wa baba") kuliko kujaribu kuwadanganya kuwa ni mzazi wao mpya.

Athari ya Talaka Kwa Watoto

Athari ya talaka kwa watoto inajumuisha athari mbaya katika mzunguko mzima wa maisha pamoja na mahusiano ya kifamilia, hali ya kiuchumi, hali ya kihisia, msongo wa mawazo, elimu na maendeleo ya kitaaluma, na nguvu ya baadaye ya mapato. Kushuka kwa uwiano wa ndoa na kupanda kwa ongezeko la talaka, kunaleta ongezeko kubwa la watoto wanaoishi chini ya uangalizi wa mzazi mmoja au familia mpya. Kiwango cha umaskini kimeongezeka kwa wanaoishi kinyumba na kwa familia zenye mzazi mmoja kuliko wenza walioana. Marekani ina idadi kubwa ya akina mama pweke masikini miongoni mwa wakwasi waliohuru (Demography 2012). Nchini Marekani watoto wanaoishi na wazazi waliotalikiwa 2009 wengi wao wanaishi katika kaya zinazoongozwa na akina mama (asilimia 75) zaidi ya zile zinazoongozwa na akina baba(asilimia 25). Pia inakadiriwa kuwa wanaishi katika kiwango cha chini cha umasikini takriban (asilimia 28) ukilinganisha na watoto wengine (asilimia19). Na wengi wao wanaishi kwenye nyumba za kupanga (asilimia 53) kuliko watoto wengine (asilimia36). Wanawake waliopewa talaka miezi 12 iliyopita ni mara mbili zaidi ya wanaume walioachana na wenzi wao ambao wanaishi katika umaskini (asilimia 22 ukilinganisha na asilimia 11, kwa mfuatano). (Ofisi ya Takwimu Marekani 2011).

Wazazi na wanandoa wa zamani lazima wawashughulikie wanafamilia wote kwa njia ya huruma, heshima na uvumilivu. Qur'an inatushauri kuwa na tabia nzuri inapotokea talaka:

> Talaka ni mara mbili. Kisha ni kukaa kwa wema au kuachana kwa vizuri. Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlicho wapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kuwa hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu hapo itakuwa hapana lawama ikiwa mwanamke atajikomboa. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiikiuke. Na watakao ikiuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, hao ndio madhaalimu.
>
> (Qur`an, 2:229)

Uvumilivu mkubwa unahitajika kwenye masuala ya talaka. Baadhi ya watoto wanaweza wasiwakubali kamwe wazazi wa kambo; katika hali kama hizi, kinachoweza kufanyika pekee ni kuwa na huruma na upole na kuzingatia muda. Baadaye, watoto wataondoka nyumbani na kutengeneza nyumba zao wenyewe. Ndoa inapokatika baada ya kipindi kirefu cha matatizo, aghlabu ni nafuu kwa watoto. Watoto wanaweza kuzoea hisia za

utiifu. Ingawa inaweza kuwa vizuri pasipo na baba yao, hawawezi kufanya hili ikiwa bado wanampenda na kutamani angelikuwepo. Watoto hutegemea kuwa mambo yangeenda vizuri. Mzazi mlezi wa kambo anaweza kukuza mahusiano mazuri ya urafiki yasiyokuwa na kikomo. Mzazi wa kambo mwenye hekima husema kumwambia mtoto wa kambo: “Mimi si mzazi wako lakini ni mume au mke wa mzazi wako na nitakutunza”.

Mzazi-pweke wa vijana hukabiliana na matatizo tofauti. Mzazi anapaswa kuwa makini ili asiwafanye vijana kuwa tegemezi kupindukia, au kujaribu kuwafanya vijana kutekeleza majukumu ya mwenza asiyekuwepo. Vijana wa kiume wasifanywe kuwa waume, na vijana wa kike wasifanywe kuwa wake. Pia kuna hatari kubwa ya kuwa na tabia mbaya, matumizi mabaya ya mwili na akili. Vijana wana mambo mengi yanayowashughulisha katika wakati ambao wanalazimika kushughulika na kazi za shule. Wazazi pweke wanahitaji kujiandaa ili waweze kutafuta na kuendeleza mambo binafsi wanayoyapenda nje ya nyumbani. Hata kama wazazi wana upweke kiasi gani, hawapaswi kuwa wabinafsi.

Watoto wa nje ya ndoa hawalingani na watoto wa wazazi waliofiwa na mke au mume au wazazi waliotalikiwa na kuishi kwenye nyumba ya mzazi pweke. Tofauti kubwa inayojitokeza ni hali ya kuwa na baba. Baba aliyefariki bado anatoa faraja inayostahiki kwa watoto wake, ambao wanahisi kuwa wanaweza kujinasibisha na kujihusisha naye. Hii humsaidia mama kuwapatia watoto hisia za ulinzi na upendo. Anaweza kuwaongoza na kuwapa mazingira ya urafiki ambayo wanaweza kufanya vizuri zaidi na kuwashinda watoto wenzao ambao wanaweza kuwa na wazazi wote na wenye kuonekana kwa nje kuwa na maisha ya kifakhari. Sambamba na msaada wake endelevu, anaweza kukuza watoto wenye mafanikio ikiwa atawapa watoto changamoto za kukabiliana na vikwazo. Akina mama hawa hutoa fursa kwa watoto wao kujithibitisha wenyewe na kujenga uwezo wa kujitegemea.

USHAURI KWA WAZAZI WALIOTALIKIWA

- ❒ Usitie dosari mtazamo wa watoto kwa mzazi mwengine.
- ❒ Jaribu kuweka mawasiliano hai baina ya watoto na mzazi mwenzio na jamaa zake.
- ❒ Wafanye watoto wajihisi kuwa wanapendwa na wazazi wote.
- ❒ Eleza kwa watoto kuwa kutengana kwa wazazi wao hakuathiri mahusiano yao na wazazi wao.

Umuhimu wa Familia katika Uislamu

Uislamu umeweka umuhimu mkubwa katika kuihifadhi familia. Awali ya yote, Qur`an inasema kuwa wanadamu ndio viumbe wa Mwenyezi Mungu wenye heshima kubwa na waliotukuzwa sana, wenye kuaminiwa na Muumba wao kuwa waaminifu Kwake katika dunia.

Hivyo, wanahitaji kufunzwa na kuandaliwa kwa jukumu la kuchukua dhamana ya Ukhalifa. Haielekei kuwa mtoto (mchanga) ana mzunguko mrefu ikilinganishwa na wanyama wote. Sehemu ya kuanzia ni "familia kama shule ya kwanza yenye kutoa taaluma" ni kuwapo mahusiano hai baina ya mume na mke. Hili lisifanywe kama "patano la kibiashara" au haki na wajibu halali (ingawa "sheria za familia" zinahitajika ziwepo kama kinga ndogo).

Mahusiano ya mume na mke lazima yajengwe kwenye mawaddah (mapenzi) na rahmah (huruma). Bila ya msingi huu, matarajio ya wazazi (yaliyoelezwa kwa ufasaha katika aya ya 25:74 ndani ya Qur'an) ya kuwa na nyumba yenye furaha na mafanikio, watoto watiifu hayatapatikana. Familia za mzazi pweke lazima pia ziwe na huruma na upole kwa watoto wao.

Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wenetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe viongozi kwa wacha Mungu (Qur`an, 25:74).

Familia ni muhimu kwa wanadamu ili kupata makuzi yao kamili ya kisaikolojia. Muumba ametufinyanga kwa njia bora, ikiwemo sehemu za kiwiliwili na zisizokuwa za kiwiliwili. Umbo letu, urefu, rangi, mwendo, na mwonekano, na sehemu za kisaikolojia, imani, na kiakili, zote zimeumbwa katika namna madhubuti. Mungu pia ametubariki kwa makabila, jamii na mataifa.

> Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lililobora kabisa (Qur`an, 95:4)

Katika safari yetu ya maisha, tunakua katika hatua na namna kubwa na za ajabu: kuanzia udhalili na udhaifu wa uchanga, kupitia hatua za kukua na kujifunza, hadi kilele cha ushujaa, na hatimaye kurudi kwenye unyonge wa uzee (karibu ya kupoteza nguvu, maarifa, na kumbukumbu). Wakati wa mchakato huu, wazazi huendelea kukua kisaikolojia, wakichangia mengi kwa watoto wao, wajukuu, na kwa ndugu na jamaa wa familia. Haja ya urafiki wa karibu itabaki kutozibwa ikiwa mtu binafsi hakuwa mwanandoa. Ni ndani ya heshima ya ndoa kwamba wanaume na wanawake wanaweza kuzoea urafiki wa kutosha wa kisaikolojia. Kama Qur'an inavyobainisha,

> ...Wao ni vazi kwenu, na nyinyi ni vazi kwao… (Qur`an, 2:187)

Baada ya ndoa, sababu nyingine ya ukuaji inayofuatia ni : hamu ya kuwa na watoto na kuanzisha familia. Katika hatua hii, mambo manne tofauti yanaweza kutokea, kila moja likiwa na matokeo yake ya kisaikolojia. Ama wanandoa kuwa tasa, au kuzaa watoto wa kike tu, au kuzaa watoto wa kiume tu, au kuzaa watoto mchanganyiko wa kike na watoto wa kiume. Kila moja ya matokeo haya lina athari kwa wazazi na watoto.

> …anamtunukia amtakaye watoto wa kike, na anamtunukia amtakaye watoto wa kiume; Au huwachanganya wanaume na wanawake, na akamfanya amtakaye tasa. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye uweza
>
> (Qur`an, 42:49-50).

Tuzo ya kisaikolojia huendelea kwa wazazi kuzoea furaha ya kuona watoto wao wanakuwa wanandoa, na kisha kuwaona wanakuwa na watoto wao wenyewe (wajukuu zao), kuwafanya wajihisi ni mwendelezo wa kuwepo kwao katika siku za baadaye.

Tunatambua jinsi gani ni tofauti wakati tunapokuwa na mtoto mmoja tu (mvulana au msichana) katika familia. Hisia hazifanani inapotokea mtoto kuwa na kaka na dada. Wala si sawa wakati mtoto anapokosa shangazi, wajomba, babu au bibi.

Watoto wanastawi ikiwa kuna familia ya ndugu na jamaa, na zaidi ya hapo ni kwa familia yenye ndugu na jamaa wengi (kutoka pande mbili za baba na mama). Fursa kwa ustawi wa kisaikolojia hutokea wakati watoto wanapokuwa na mpango mzuri wa mahusiano. Hii hutokea katika mazingira ya majukumu mbalimbali; kwa mwanamke: kama mtoto, dada, mke, mama, shangazi na bibi, na kwa mwanamme: kama mtoto, kaka, mume, baba, mjomba, na babu.

FAMILIA IKIANZA, HUENDELEA!

Ikiwa tutakufa kesho, kampuni au shirika ambalo tunafanya kazi linaweza kujaza nafasi zetu kwa siku chache. Hata hivyo, familia tunazoziwacha zitajisikia hasara katika maisha yao yote. Tunajituma zaidi katika kufanya kazi kuliko kwenye familia zetu wenyewe, jambo lisilostahiki kwa kweli!

— kutoka intaneti —

Familia kwa Mujibu wa Qur'an

Mila nzuri za familia hukuza maadili ambayo watoto wanaweza wasijifunze shuleni

Maisha ya familia yanategemea kuweka malengo sahihi ya familia, ambayo ni zaidi na kushinda lengo la kuwa na watoto tu. Familia haizalishi watoto tu ili kuhifadhi kutoweka kwa ubinadamu.

Utunzaji wa familia kwa ajili ya familia hauleti mantiki, na hivyo malengo ya familia lazima yahusishe mbali zaidi kuliko hifadhi binafsi tu. Qur`an inasema:

> Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni (Qur`an, 4:1).

Wanadamu wameumbwa kutokana na roho (nafsi) moja, kutokana na roho hiyo ndipo kisha akaumbwa mwenza, na kutokana na roho hiyo na mwenza wake wakaumbwa wanaume na wanawake wengi. Ingawa aya ipo katika hali ya umoja, mchakato huo huo umesisitizwa katika hali ya wingi:

> Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu wana na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini upotovu na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?
>
> (Qur`an, 16:72)

Wazo la kuletwa wanadamu katika dunia kutekeleza jukumu fulani linaelezwa katika aya ifuatayo:

> Na pale Mola wako Mlezi alipowaambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa, wakasema: Utaweka humo atakayefanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyoyajua
>
> (Qur`an, 2:30)

Aya inafafanua jukumu la kila mwanadamu hapa duniani: Mwaminifu na mtawala (khalifah). Jukumu la mwanadamu kama mtawala ni kuuendeleza ulimwengu (ímran) na kueneza uadilifu (adl). Qur'an pia inaeleza kuwa maisha ni majaribio, na kwamba tupo hapa ili kumwabudu na kumtumikia Mungu pekee:

> Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi
>
> (Qur`an, 51:56)

Hivyo malengo ya familia yanahusisha: Kumtumikia Mungu, kutawala, kuheshimu riziki za Mungu na ukarimu wake, kudhibiti mahusiano ya damu, na kuhifadhi haki za kila mmoja. Kisha Mungu pia amegawa mahusiano baina ya wanandoa katika aya ifuatayo, yenye kulenga katika utulivu, mapenzi, na huruma miongoni mwa wanafamilia:

> Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri
>
> (Qur`an, 30:21).

Ingawa mapenzi ndani ya familia yanapewa sehemu kubwa sana, si mapenzi ya juu katika maisha. Miongoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu ni Huruma, Haki, na Amani. Mapenzi kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe Wake yamewekwa katika ngazi ya juu:

> Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma, na biashara mnazoogopa kuharibika, na majumba mnayoyapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu
>
> (Qur`an, 9:24)



Msingi wa mapenzi ni upendo kwa Muumba wetu. Kumpenda Muumba ndiyo ngazi ya juu ya upendo. Kwamba, unawapenda wazazi wako, watoto, na ndugu na jamaa zako hata kama wamekukosea, kwa sababu mapenzi yako kwao yanatoka na yanategemea mapenzi yako kwa Mwenyezi Mungu. Ukarimu Wake kwako unaendelea hata unapotenda dhambi. Mapenzi ndani ya familia yanaelezwa ndani ya Qur'an:

> … Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwake mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni
>
> (Qur`an, 4:1).

> Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema… (Qur`an, 17:23)

Katika mtandao huu wa mapenzi na matunzo, mama anakuwa mwanzo kabla ya baba, na yeye ndiye wa kwanza anayestahili kutunzwa kwanza. Mtu mmoja alimuuliza Mtume (s.a.w), "Nani ana haki zaidi ya matunzo yangu na kutendewa wema (birr) kwanza?" Alijibu, "Mama yako, mama yako, mama yako, kisha baba yako" (AL BUKHARI).

Waja wa Mwenyezi Mungu (ibad al-Rahman) wanatarajia kupata matumaini mawili: familia zenye mazingira ya furaha na maendeleo ya viongozi sahihi:

> Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wenetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe viongozi kwa wacha Mungu (Qur'an, 25:74).

Furaha na utulivu ndiyo lengo la kila mtu katika familia (wakiwemo wazazi, bibi na babu, watoto, na wajukuu). Kuzaa viongozi halisi ni lengo la pili. Hili linaweza kufikiwa kwa mtu kuwafundisha watoto wake uaminifu, kumuabudu Muumba, maendeleo ya ulimwengu (Imran), na mapenzi kwa Mungu na Mitume Wake. Kudharau misingi hii muhimu kutainyima familia furaha yake. Furaha ya kulea inakuja kutokana na kuwaona watoto wanakuwa na tabia nzuri na kushikamana na lengo lao la kuishi ulimwenguni.

Chukua mawazo haya, yafanyie kazi, na yaelezee kwa watoto wako kadri wanavyokuwa wakubwa. Hii ndiyo njia ya kupandikiza mbegu ya wema na hisani katika moyo na akili ya mtoto. Hata kama mtoto anakulia katika kumsahau Mungu, siku moja mbegu ya Imani itamea na kuzaa matunda. Kutakasika kwa imani lazima kujazwe kwa ukamilifu na "kutakasika kwa maziwa ya mama kwa mtoto." Simika misingi madhubuti ya tabia njema. Andaa vipaumbele sahihi vya mtoto tangu mapema.

Misingi hiyo ya wema huipa nguvu kinga ya mtoto kuhusu vishawishi vilivyotuzunguka kila upande. Hatuwezi kutegemea moja kwa moja kwenye "sera" za nje za kuikinga jamii. Mifumo ya ndani ya kitabia ya mtoto, hisia za kujiheshimu na nguvu za kujidhibiti ndiyo utaratibu stahiki zaidi wa kuilinda jamii. Wazazi wanatakiwa kuwasaidia watoto ili waweze kunufaika kutokana na hekima za maandiko matakatifu kwa kutilia nguvu imani, ukweli, na huruma tangu mwanzo wa maisha yao.

Kipi kimeenda Kombo katika Familia za Waislamu?

Thamani ya familia imeshuka kwa miongo kadhaa. Ongezeko la viwango vya talaka, familia za mzazi pweke, wachumba wanaokaa kinyumba, (watoto wa) haramu, umasikini na kulegalega (kwa familia) kumeathiri wote watoto na wazazi. Kitengo cha familia ya Waislamu kwa bahati mbaya hakina kinga hata ndogo kutokana na maendeleo haya, kinasumbuliwa na matatizo na udhaifu wake wenyewe.

Familia ya Waislamu inatakiwa kuandaa mipango makini ili ifanikiwe na isiyumbe. Jibu la swali kwanini imeshuka thamani ni tata lakini linaegemea sana kuanguka kwa Umma wenyewe. Kutetereka kwa hali ya uchumi, mifumo duni ya elimu na kuvunjwa moyo kwa wenye imani thabiti – sababu zote hizi zimeathiri vibaya kitengo cha familia ya Waislamu.

Qur'an inawataka Waislamu kusoma (*iqra*'), kutumia mantiki (*ya'qilun*), kutafakari (*yatafakkarun*), kuzingatia (*yatadabbarun*), na kutambua (*yafqahun*). Kwa nini Waislamu wana kiwango kikubwa sana cha ujinga na bado wanazama kwenye ushirikina? Waislamu wameshindwa (kwenye mapambano), wamechinjwa, na wamenyanyaswa katika kipindi cha karne chache zilizopita. Aidha, kuibwa ardhi yao, utajiri, na matumaini, wamekuwa na mtazamo hasi, utamaduni mbovu, na fikra dhaifu ya kujiamini. Wamepoteza sehemu kubwa ya tabia zao na kuchagua fedha na madaraka kuliko maadili na mengine mazuri. Uvivu na choyo vimepewa kipaumbele kuliko hifadhi ya jamii na maslahi ya Umma. Umma unakabiliwa na rushwa, maradhi, umasikini, na njaa.

Kutokuwa na mawazo ya kupata mali na starehe ya mwili, kumeondoa imani na kuwavunja moyo wote wazazi na watoto. Uanzishaji wa jengo la jamii – familia – huanza kushindwa. Badala ya kulea raia wenye thamani kubwa (ambao ni werevu, wabunifu, wenye kujitegemea, na wawajibikaji), familia za Waislamu

zimeanza kuzalisha watoto vibaka na wabinafsi badala yake. Watoto hawa ni wapokeaji zaidi kuliko kutoa, wabinafsi kuliko wanajamii na watumwa, waharibifu na wafujaji zaidi kuliko kusaidia.

Wazazi wengi Waislamu wana matatizo ya kutojua kusoma na kuandika, ujinga, na uzembe. Watoto wengi Waislamu wanakwama kwenye jitihada zao za kupata elimu na ujuzi. Baadhi ya jamii za Waislamu zinasumbuliwa na serikali dhalimu na kandamizi. Waislamu wengi wanakabiliwa na matatizo yafuatayo:

- ❒ Ukomo wa uhuru wa kufikiri, kutokana na ukandamizwaji na nguvu za kidini;
- ❒ Ukomo wa uhuru wa kuhoji, kudadisi, na kuzungumza;
- ❒ Ukomo wa uhuru wa kufanya biashara na kutajirika, kutokana na rushwa na matumizi mabaya;
- ❒ Ukomo wa uhuru wa wanawake, kutokana na ujinga na kukandamizwa na wanaume; na
- ❒ Ukomo wa uhuru wa raia kuchagua viongozi wao, kutokana na ukandamizaji na dhulma.

Waislamu hawawezi kukabiliana na mambo yote haya kwa mara moja. Hata hivyo, wanaweza kuanza na kitu ambacho kimo ndani ya uwezo wao, na huko ndiko kulea vizuri. Kulea watoto wema na wenye mafanikio na hatimaye raia wazuri, Waislamu wanapaswa kubadili mitindo ya malezi ya kimabavu na ukandamizaji inayotumiwa sasa katika nchi zao na kutengeneza mifumo yao ya malezi kwa umakini kabisa.

Maendeleo ya Mtoto na Mifumo imara ya Elimu

Kuna majaribio makubwa ya mageuzi katika kukabiliana na maanguko ambayo ulimwengu wa Waislamu umeanza kuangukia. Mipango mingi imeanza kuwekwa katika utekelezaji. Hata hivyo, elimu ya watoto, kipimo kikubwa muhimu kabisa, hakikuwepo kwenye agenda za wanamabadiliko. Wanazuoni wakubwa kwenye fani zote (ikiwemo

elimu ya dini, falsafa, siasa, elimu-jamii, na uchumi), wakitoa michango madhubuti na imara ili kupindua kuanguka kwa Umma na kuboresha hali yake. Hata hivyo, maradhi yanayozuia kuibuka kwa taifa bora hayakutibiwa. Uwezo mkubwa na kipaji cha Muislamu mmoja mmoja na jamii havikutumiwa inavyostahiki. Mwanya uliopo baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu katika ubunifu, utendaji, na mafanikio (kwenye sayansi na teknolojia) limekuwa likiongezeka kwa karne. Majukumu kwa wanazuoni na walimu ni kugundua kitu kinachokosekana na kutafuta suluhisho. Wanaweza kufanya vyema kuchunguza masuala ya usomaji wa watoto, maendeleo ya watoto, na elimu ya watoto. Ni lazima waanze na malezi katika majumba. Hadi hapo moyo na akili ya mtoto vinakuwa lengo la umakini wa wazazi na walimu, ulimwengu wa Waislamu utaendelea kupungua na kusumbuka kutokana na kushuka kiwango na kudidimia kabisa.

Kihistoria, wanamageuzi wengi wa zamani walijikita zaidi kwenye ibada za dini na vipengele vyake vya kisheria na kisiasa. Mageuzi ya Waislamu wengi wa sasa wa Kimagharibi yameelekea upande mwingine na kujikita kwenye uigaji kwa wavamizi wa Kimagharibi wa awali. Umma uliachwa na ahadi hewa na matumaini ambayo hayakuwahi kutekelezwa. Wanamageuzi wengi wa kidini walikuwa wamejaa jazba na hisia na kupendekeza suluhisho lisilotambulika ambalo liliegemea kwenye uigaji wa zama za ustawi wa Uislamu. Hakukuwa na lengo halisi kuhusu majukumu na wajibu wa wanawake (wake na akina mama) katika kulea watoto. Wanazuoni watambuzi na wanafasihi wenye kushughulikia masuala ya maende-

leo ya mtoto, elimu ya mtoto, na malezi walikosekana. Kulikuwa na majibu hafifu na yasiyohalisika ya Umma kwa maswali halisi ya wanamageuzi, kwamba ni dini za asili au za Kimagharibi zilizotawala dunia ndizo wanazozifikiria. Waislamu wengi walikuwa wasemaji kuliko kuwa watendaji. Hakukuwa na vitendo vilivyoratibiwa vikitumia mbinu bora zilizotokana na ufahamu na uchambuzi wa kina wa tatizo. Wanamageuzi hawakuzishughulikia ipasavyo sheria za Mungu (*al-sunan al-Ilahiyyah*) na sayansi ya asili, jamii na mwanadamu.

Waislamu lazima watambue umuhimu wa kulea watoto wema na athari zake endelevu. Masahaba wa kwanza wa Mtume (s.a.w) walikuwa watu wazima wakati walipolinganiwa na Mtume (s.a.w). Tabia zao halisi tayari zilishajengwa tangu uchanga. Walilelewa kama watu huru na wenye ujasiri na hawakuwahi kunyanyaswa na madhalimu. Mtume (s.a.w) alielekeza kwenye umuhimu wa ujenzi wa tabia za mtoto: “mbora wao kabla ya Uislamu ndiyo mbora wao baada ya Uislamu ikiwa

wataelewa (Uislamu)." Sifa za msingi za mtu tayari zimeshatengenezwa utotoni. Ama kipindi kabla ya Uislamu au baada ya Uislamu. Imani na ujuzi vinaweza kufundishwa baadaye kwa mtoto, wakati tabia njema haziwezekani.

Wakati Mtume (s.a.w) alipoanza kueneza ujumbe wake, alikuwa na miaka 40, Abu Bakar alikuwa na miaka 37, Úthman alikuwa na miaka 30, Umar alikuwa na miaka 26, Ali alikuwa na miaka 8, wakati mke wake Mtume, Bi. Khadija, alikuwa na miaka 55. Malengo ya msingi na maadili yamewekwa na Qur'an, wakati hatua ya kwanza katika kuyafikia ni jukumu la wazazi. Wazazi lazima waanze mapema katika kujenga tabia, kwa kutumia zana za elimu-nafsia (saikolojia), elimu-jamii, mawasiliano, na elimu. Haidhuru maadili ya msingi ya binadamu na mahitaji yake havibadiliki, mbinu za uzazi lazima zitekelezwe ipasavyo, ziendelezwe, na ziboreshwe.

Kutambua umuhimu wa malezi bora na ndiyo nafasi ya mataifa kwa kiasi kikubwa kunabainishwa na namna tunavyolea watoto, kozi kadhaa zimeanzishwa duniani kote ili kutekeleza stadi za malezi, na kulifanya somo liwe wazi zaidi kwa Umma. Kuipuuza sehemu hii ya fursa kuna gharama kubwa sana, na hakuna taifa linaloweza kuhimili hasara kubwa kama hii. Faida kubwa inaweza kupatikana kwa kutoa kozi kuhusu malezi kwa wazazi na wazazi tarajali. Kuanzisha mazoezi ya wanajamii ili kuhamasisha mwamko wa kulea watoto kuna manufaa makubwa sana. Kuunda wizara maalumu ya serikali na/au kuanzisha taasisi maalumu kwa kujenga malezi katika nchi mbalimbali kunaweza kuwa ni huduma kubwa kwa wanadamu.

Uchunguzi wa kina kuhusu Mahitaji ya Mfumo Madhubuti wa Elimu

Ikiwa tunataka kuijenga upya elimu ya watoto wetu, tunalazimika kutazama kwa kina mfumo wa elimu katika ulimwengu wa Waislamu. Baadhi ya shule za Waislamu za sasa zinakosolewa kutokana na kutoeleweka kutokanako na watoto wenyewe, kwa mfano, namna ambayo wanaweza kuichukulia kinyume michezo ya watoto. Mtaala haukujikita kwenye hatua za makuzi ya mtoto, kama vile mara nyingi unalazimisha, mgumu, na usiobadilika. Unadharau udadisi wa watoto na tabia yao ya kawaida ya kufanya mazoezi ya michezo na kucheza. Badala yake, unaegemea zaidi kujifunza kwa ghibu na kukariri.

Kihistoria, aina mbili tofauti za shule zinaweza kubainika katika ulimwengu wa Waislamu. Kwanza, kulikuwa na shule binafsi, halisi, na zenye mfumo wa elimu ya watoto wa tabaka la juu zilizoandaliwa vyema, kama vile za viongozi na matajiri.

Watoto wao wanafundishwa na walimu wenye sifa za juu kabisa na wapole, ambao huitwa (muaddib) kwenye majumba (ya kifakhari) binafsi. Walimu/Wakufunzi hawa wameelekezwa kuwaandaa watoto kuwa viongozi na watu bora. Viongozi kama vile Muawiyah ibn Abu Sufyan, Abd al-Malik ibn Marwan, al-Hajjaj al-Thaqafi, Harun al-Rashid, na wengine walikuwa na walimu wakubwa. Walimu hawa walipewa vitendea kazi vinavyohitajika katika kuwaelemisha watoto katika fani za dini, utamaduni, na fasihi, sambamba na ujuzi na utendaji. Hasara moja ya mfumo wa ufundishaji wa mmoja kwa mmoja ni kuwa watoto wanakosa fursa ya kusoma kwa makundi ya wanafunzi. Hili ni tofauti kabisa na mfumo wa pili wa kuttab, shule za Umma ambapo Qur'an ilifundishwa kwa uchache pamoja na misingi ya hesabu. Si walimu wala vifaa vilitosheleza. Walimu walitumia adhabu kama njia ya kuwaadabisha watoto, waliwazuia watoto kucheza, na walitumia njia ya kuhifadhi kama nyenzo kuu ya kujifunza. Aina hii pacha katika mfumo wa elimu bado inaendelea kwa kiasi kikubwa katika nchi nyingi za Kiislamu. Matajiri wanapeleka watoto katika shule binafsi au za kigeni na makabwela wakiwapeleka katika shule za Umma zilizo na vifaa duni. Shule binafsi zina uwezo wa kutosha kuajiri walimu wenye sifa na hufuata mitaala maalumu na ile ya kigeni, pamoja na kuwa na vifaa bora kama maabara, zana za kuonesha, maktaba, kompyuta na viwanja vya

michezo vyote visivyopatikana katika shule za Umma. Kwa bahati mbaya shule hizi za gharama zinazalisha wanafunzi wenye mtazamo hasi wa tamaduni zao, urithi na dini yao.

Anaeathirika na kutotoshelezwa kielimu ni mtoto. Upotevu huu wa "dirisha la nafasi" katika kulea na kuelimisha Umma ni mgumu kuurekebisha endapo akili na mioyo ya watu itakuwa imetengemaa. Ikiwa tunataka kuurekebisha Umma hatuna budi kubadili mtindo wetu wa malezi na hivyo kuna umuhimu wa kutilia mkazo miaka ya mwanzoni ya utoto. Ili tufanikiwe tuwashughulikie walimu wa kwanza: wazazi. Bila shaka wao ni walimu wa kutengeneza roho na watengeneza tabia za watoto.

Ni haki kusema ya kuwa hakuna kiigizo chema cha ulezi hivi sasa katika jamii ya Kiislamu na ya Magharibi. Jamii yoyote inayotafuta mabadiliko ya jamii wanatakiwa kufahamu ya kuwa ulezi ndio nyenzo kuu

Katika uchunguzi uliofanywa kwa ushirikiano baina ya chuo kikuu cha Havard na gazeti la Washington iligundulika kwamba vipaumbele vya wanaume na wanawake walio wengi ni "kukabiliana na misukumo ya kisaikolojia na kiuchumi;kuimarisha mshikamano wa kifamilia, mawasiliano imara na watoto; na akina mama kupendelea kutumia muda wao mwingi wakiwa nyumbani na watoto." Malezi bora ni lazima yafanywe kuwa ni kipaumbele cha mwanzo.

AL-USRA MAGAZINE 2005

ya kupatikana furaha-kimaadili, kiimani, na kimali. Kwanza kabisa tubadili mtazamo na mwenendo wetu wa malezi. Suala la malezi lijumuishe moyo na akili. Akili inahitaji upembuzi, utambuzi na mbinu. Moyo unahitaji hisia, mapenzi, busara na ushirikishwaji. Uzazi mzuri usikose utaalamu wa sayansi na mguso wa kisanaa.

Ujenzi wa ustaarabu (‘imran) unahitaji taasisi nyingi ambazo zitaongozwa na watu ambao ni waaminifu, wabunifu, wachapakazi, wa kuaminika na wanaoweza kupokea ushauri. Kulea watu ambao ni jasiri kiakili, kimwili, kiroho, na kitabia inakabidhiwa katika taasisi ya familia-wazazi. Jukumu haliwezi kuachiwa shule, mitandao, na serikali japokuwa vinaweza kusaidia sana. Hakuna kitu kinachoweza kufanyia kazi mahitaji ya watoto wao kuliko wazazi, kuna hali ya kujinyima na mapenzi ya ulezi hata kila mtu akatamani kuwa mbora katika dunia, ni wazazi pekee wanaoweza kuombea mema zaidi watoto wao kuliko wao wenyewe.

Kama watashawishika, wazazi wanaweza kujitolea mhanga kwa namna yoyote ile kulea watoto wao kwa njia nzuri iwezekanayo. Wakati mtu atakapozungumzia mambo mazuri ya watoto wao watasikia. Wanatakiwa tu kufahamu namna ya kuyatimiza. Kuwafanya wazazi wakatambua majukumu yao na sehemu ya kuanzia.Ulezi ni mchakato wa muda wote wa maisha si wa miaka mitano tu ya mwanzoni, japokuwa kipindi hiki chaweza kuwa ni kipindi muhimu zaidi. Katika hatua hii ya mwanzo kabisa wazazi ndio wahusika wakuu japokuwa watakuwa na uwezo wa kuendelea kuishikilia katika kurekebisha tabia na mitindo ya maisha ya watoto wao endapo wanajua kuwaongoza ipasavyo.

Familia nchini Marekani

Mimba wakati wa ujana na kiwango cha kuzaa vimeshuka kwa kiasi kikubwa nchini Marekani tangu miaka ya 1990s. Kiwango cha mimba za ujanani kimeshuka kwa asilimia 51 na kiwango cha kuzaa kimeshuka kwa asilimia 57 (Mkutano wa Kitaifa wa Mabunge 2015). Licha ya hivyo hali imeendelea kubaki kuwa kubwa kwa nchi za viwanda. Kwa makisio inakadiriwa kuwa kwa kila binti mmoja kati ya wanne atakuwa na ujauzito kabla ya kufikia umri wa miaka 20. Wamarekani wengi wanapanga mapunziko yao ya kila wiki kwa mpango mzuri kuliko wanavyopanga vizuri familia zao. Katika kitabu chake *It takes a Village to Raise a Child* (1996), aliyekuwa waziri wananchi wa Marekani Hillary Clinton alieleza kwamba kumekuwa na ongezeko la wanaozaa nje ya ndoa kutoka asilimia tano katika mwaka 1960 mpaka kufikia asilimia 25 mwaka 1996. Kwa mujibu wa shirika la sensa la Marekani, katika mwaka wa 2014 ilikuwa ni asilimia 40.6. Asilimia ishirini na moja ya watoto walio chini ya umri wa miaka 18 wanaishi katika dimbwi la umasikini. (kwa mujibu wa Ofisi ya Sensa Marekani 2014). Nchi ya Marekani inaongoza kwa kiwango cha mauaji ya watoto ukilinganisha na mataifa mengine ya Magharibi.Inashika nafasi ya saba katika viwango vya kidunia kwa takwimu ya mauaji kati ya umri wa kuanzia 0-19,ikiwa na zaidi ya vijana 3,000 waliokufa kwa mwaka 2012.(SHIRIKA LA WATOTO DUNIANI-UNICEF 2014). Kwa mujibu wa CDC, mwaka 2013 kujiua ilikuwa

ndIo kisababishi cha pili cha vifo kwa vijana wa umri kuanzia 15-24(idadi ya vifo 4,878) na kisababishi cha tatu kinachoongoza kwa vifo vya watoto wa umri kati ya 10-14 (idadi ya vifo 386). Kati ya vifo 1,659 vilivyosababishwa na kujiua kwa vijana wa umri wa miaka 15-19 kwa mwaka 2010, asilimia 40 walijiua kwa bunduki. Nchi ya Marekani inaongoza kwa raia kumiliki silaha za moto ukilinganisha na nchi nyingine duniani – kwa wastani wa 88 kwa watu 100 (kwa mujibu wa The Guardian 2012). Mwaka 2011, asilimia 5 ya wanafunzi wa sekondari wanabeba bunduki vikiwa pamoja na vifaa vya shule (NASP). Nchi ya Marekani ndio inayoongoza kwa mauaji ya kutumia silaha katika nchi zote zilizoendelea (Washington Post 2012). Pia yako mambo mengine mabaya. Watoto, utajiri umaskini, mahangaiko kutokana na matumizi mabaya, kukataliwa, na matatizo ya kuzuiliwa hisia. Ugonjwa wa unene umeongezeka mara mbili kwa watoto na kufikia mara nne kwa vijana katika miaka 30 iliyopita. Mwaka 2012, zaidi ya theluthi ya watoto na vijana walikuwa na uzito uliopitiliza (kwa mujibu wa CDC)

Asilimia 99 ya wamarekani wanamiliki runinga katika majumba yao na zaidi ya nusu ya watoto wamewekewa runinga katika vyumba vyao vya kulala. Baada ya kulala, kuangalia runinga huwa ndio jambo lenye kuwashughulisha sana watoto. Watoto wa Kimarekani wanatumia wastani wa saa nane kwa siku kuangalia televisheni, hiyo ni sawa na makisio ya saa 28 kwa wiki, ambayo ni zaidi ya saa zinazotumika shuleni. Aidha watoto wa Marekani wanaona vitendo vya vurugu zaidi ya 200,000, vikiwemo vitendo vya mauaji zaidi ya 16,000 kabla hawajatimiza umri wa miaka 18. Program za runinga huonesha zaidi ya matendo 812 ya vurugu ndani ya saa moja; program maalumu za watoto, hasahasa katuni, huonesha matendo yanayofikia idadi ya 20 kwa saa (kwa mujibu wa chuo cha mafunzo ya watoto Marekani na maradhi ya akili kwa vijana). Sinema, video za muziki, michezo ya video, na intaneti vyote kwa pamoja vina ujumbe unaohamasisha vurugu kwa vijana. Tafiti nyingi zimeonesha ya kwamba vurugu nyingi zinazotokana na masuala ya mifumo ya kimtandao ni kama uchokozi, kuumizana na hofu. Baadhi ya tafiti pia zinaongezea kwa kusema kutazama sana runinga hupelekea kufanya vibaya kwenye masomo, tatizo la kutokuwa makini na kupoteza uwezo wa kuwa makini. Uchunguzi uliofanywa na umoja wa kitaifa kati ya mwaka 2008-2009 chini ya mfuko wa familia wa Kaiser ulionesha ya kwamba vijana wa miaka 8-18 wanatumia wastani wa saa 7 na dakika 38 kwa siku kufuatilia mitandao mbalimbali, na kwa sababu wanatumia zaidi ya mtandao mmoja kwa muda tofauti, wanakadiriwa kutumia saa 10 na dakika 45 katika mitandao hiyo.

Kwa nini mtoto anayetazama filamu ya mwaka 1972 ya Janga la Nixon Watergate, akafikiri kuwa si vizuri kuvamia ofisi za Chama cha Democrats wakati atakuwa ameshaangalia uvamizi mwingi katika runinga kila usiku na kuvichukulia ni vitendo vya kishujaa? Watoto wanamalizwa kifikra wanapoona uhalifu mwingi kila siku na inakuwa sehemu ya kawaida katika maisha yao.

Wazazi wanatakiwa kufahamu ujumbe mbaya wanaoupata watoto wao, wawalinde dhidi yake na kupigia kelele kupunguzwa kwa mawazo haya mabaya. Maandiko mengi ya Kimarekani hayajaleta matokeo yanayokusudiwa. Hivyo yatupasa kutathmini ni kwa nini ushauri wote huo na miongo hiyo mingi ya tafiti, suala la ulezi bado linaendelea kuzorota.

Msisitizo mkuu kutoka mashirika ya kutengeneza filamu kama (Hollywood) ni kuonesha maungo ya mwili,badala ya kushughulikia masuala ya ujenzi wa akili na uzuri wa maadili na tamaduni. Kuna

sanamu za wanaume na wanawake walio uchi katika maeneo ya wazi. Mashindano ya ulimbwende yanazingatia uzuri wa maumbile ya kike ambayo yanaondosha maadili na imani. Mashindano haya yamepigiwa chapuo mpaka imefikia hali ya kuwapo mashindano ya mbwa na paka! Mafundisho ya Uislamu kuwa Mwenyezi Mungu ni mzuri na anapenda vizuri yanahusu tabia, mienendo na maadili.

Linapokuja suala la familia na mambo ya dawa za kulevya na zinaa, jinsi tunavyolitafsiri tatizo linaonyesha kiini cha suluhisho, tukilijadili kiuchumi, suluhisho litakuwa la kiuchumi, kama yatapelekwa kama maovu ya kijamii utatuzi utakuwa wa kijamii; kama litakuwa la kimaumbile jibu litakuwa la kimaumbile. Kwa mfano; mara nyingi husemwa kuwa matatizo ya dawa za kulevya ni moja ya kusambaza na sio mahitaji. Hii imepelekea uwekezaji mkubwa wa serikali kwenye vifaa, ikiwemo boti na ndege, ili kuzuia usambazaji. Lengo ni kuhusu uchumi wa jambo lenyewe. Katika uhalisia haidhuru, hili halijatatua tatizo na mizigo ya dawa inaendelea kunufaika kupindukia kwa biashara duni. Ni wakati sasa kwa jamii pia kurejelea mambo haya kama vile imani, kiroho, na kijamii na kuzihukumu ipasavyo.

Hadithi za Malezi Marekani

Mgogoro kati ya dhamira na njia katika jamii za Kimarekani zinazua tafrani katika akili za watoto. William Kilpatrick katika kitabu chake *Why John can't tell right from wrong*, (kwanini John hawezi kutofautisha jema na baya) anaeleza kuwa wazazi wanawataka watoto wao kuwa safi, thabiti, adilifu, wanaojiongoza na wajiheshimu. Ni kipi sasa kinachozuia wazazi kustawisha sifa hizi kwa watoto wao? Sehemu ya majibu imekitwa katika ushawishi wenye nguvu wa hadithi mbalimbali za ulezi. Tutazitazama kwa kina hadithi hizi katika sura inayofuata, hata hivyo hadithi mbalimbali zinazotawala katika familia za Kimarekani zimeorodheshwa hapa chini. William Killpatrick anazikosoa kama ifuatavyo:

1. **Kwa kuwa Marekani** iliundwa katika misingi ya ubinafsi wakati Taifa la Marekani lilivyoasisiwa, watoto walitakiwa kulelewa bila ya mamlaka yoyote. Zamani mwanaume alienda msituni akajenga nyumba yake, akalima mazao ya chakula chake, muda wote akijilinda yeye pamoja na familia yake dhidi ya wanyama wakali, wezi na serikali za kigeni. Alikimbia mamlaka. Mahujaji wa Kikristo kutoka madhehebu tofauti katika taifa lililojulikana kama Koloni la kumi na tatu, walikwenda katika ardhi Fulani ambapo kulikuwa na uchache wa/au hakukuwa na serikali, kuepa udhalilishaji wa serikali za Uingereza, Ufaransa na Ujerumani ambazo ziliwanyima haki zao za kibinadamu na kuwanyima uhuru. Wamarekani wengi walionufaika na wazo la kuwa na mamlaka hafifu ya serikali, walidhani kuwa ni bora kuwalea watoto kwa mamlaka hafifu au bila kuwa na mamlaka kabisa. Hata hivyo watoto wanahitaji mapenzi ya wazazi na mamlaka zitakazo wawezesha kuwa watu wenye mapenzi, wakati watu wazima hawana.

Madhambi Saba Makubwa Kabisa katika Ukristo
Ulafi, Tamaa, Uvivu, Wivu, Hasira, Kiburi na Uasherati

2. **Hadithi ya "kijana mzuri mkorofi".**Vijana "wakorofi" wanachukuliwa kuwa ni wapendwa na wenye furaha.Tom Sawyer na Buster Brown ambao ni vijana maarufu katika vitabu vya hadithi za Kimarekani ni katika mifano iliyopita na Dennis mtishaji, Bart Simpson, mabaradhuli wadogo, na wapendwa wengine watundu wanaoonekana katika filamu na runinga ni mifano ya sasa. Utamaduni huu una nguvu katika hisia mpaka neno utii linakuwa neno baya katika msamiati wa mtoto.
3. **Hadithi ya kuwa mapenzi pekee** yanatosha kujenga "wema asili wa mtoto". Hili ni wazo linaloelezwa na Rousseau kwamba haiba itajiongoza yenyewe endapo tu watoto wataachwa wapevuke kwa namna yao wenyewe. Watakiwacho wazazi kufanya ni kuwapenda watoto wao. Akizungumzia "Mapenzi" Rousseau alikusudia watoto kutoingiliwa na kuwa na uhuru kamili.



4. **Uzushi wa "Ujuzi wa Kitaalamu"** ambao siku zote uko sawa usio na makosa. Wazazi wamejivua majukumu yao na kujigeuza wataalamu katika kulea watoto wao, walio wengi kati ya wataalamu wa malezi wanakubali uzushi wa "wema wa asili", kwa hivyo tuna hali ambayo uzushi mmoja unaunga mkono uzushi mwingine. Wataalamu wanaweka msisitizo zaidi kwenye upekee, ubunifu na hiari ya watoto. Wataalamu wengine wanataka wazazi wajifananishe na watoto wao kuliko kuwafundisha watoto kufuata sheria na kutii mamlaka.

5. **Uzushi wa kuwa** "matatizo ya utu ni matatizo ya kisaikolojia". Matatizo ya tabia yanachukuliwa kama matatizo ya kutojiamini au matokeo ya mahitaji ya kisaikolojia ambayo hayakutimizwa. Wataalamu wengi wa masuala ya watoto wanapingana na dai hili kwamba matatizo mengi ya kisaikolojia yanatokana na ari na utayari upande wa watoto. Vitabu vingi vimeandika kuhusu "kujiamini" na neno "tabia" halipatikani kokote. Ni muhimu kukumbuka kuwa tafiti kuhusu makala za ulezi wa watoto katika jarida la *The Ladies Home, Womens' Home Companion* na gazeti la *Good House Keeping*, kwa miaka ya 1900, 1910 na 1980, imekutikana kuwa moja ya tatu ya machapisho haya yalihusu makuzi ya kitabia.

6. **Uzushi kuwa "Wazazi** hawana haki ya kufunza tabia za watoto". Kuna watu wanadai ya kuwa watoto wanatakiwa kujiundia tabia zao wenyewe. Kiukweli watoto wanao uwezo mdogo sana wa kufanya hivyo, ikiwa watu wengine katika jamii wanataka kuwaingizia tabia zao vilevile.Inaingia akilini kweli wazazi kubaki kuwa watazamaji

tu ambapo kila mtu (wanatamthilia, waburudishaji, watangazaji, mpaka walimu wa ngono) wanang'ang'ana kuuza tabia zao kwa watoto? Njia moja ya kutafsiri tabia ni kufikiria dhambi.

7. **Uzushi wa "Familia ya** mzazi pweke ina ubora sawa na ile ya Wazazi wawili." Kujenga tabia ni kazi ngumu, hata tukijua namna ya kuijenga. Talaka inapelekea ujenzi wa tabia kuwa suala gumu zaidi. Kasi ya talaka ni kubwa na inaathiri karibu nusu ya familia za Marekani. Watoto kutoka familia za mzazi pweke wapo katika hatari ya kutumbukia katika matumizi ya dawa za kulevya, uovu, matatizo ya hisia, na mimba zisizo tarajiwa. Baada ya kuyasema haya, hatukatai kuwa watoto kutoka katika familia za aina zote mbili wana uwezo sawa wa kurekebisha saikolojia zao. Mwanasaikolojia wa Kiingereza D. W. Winicott alibuni msemo usemao "Mama bora tu" akimaanisha ili mtoto aweze kujitambua mama anatakiwa awe mwenye ubora tu ambaye anaendana na mtoto katika " kazi ya awali ya malezi". Hili linajumuisha baba na mama wote katika familia ya mzazi pweke na ile ya wazazi wote. Mzazi pweke anaejali katika familia ya mzazi pweke anaweza kufanya kazi nzuri ya kukuza watoto kuliko wazazi wawili wasiojali katika familia ya wazazi wote. Zaidi kama mzazi pweke atakuwepo na familia pana na wanafamilia wanasaidiana na ana mazingira rafiki ya kufanyia kazi (kama atatakiwa kufanya kazi), anaweza kufanya kazi nzuri ya ulezi kuliko mlezi asiyejua wa familia ya wazazi wawili.

8. **Uzushi wa "familia isiyo ya kidini"** kama mfano bora wa kuigwa. Katika ustaarabu uliopita wa Kiebrania, Kirumi na Kigiriki, na hata Marekani katika karne ya kumi na tisa, wazo la utakatifu wa nyumba lilikuwa ni shuruti si hiari. Tambiko nyingi na usomaji wa vitabu ulifanyika nyumbani. Maisha ya nyumbani yalihusishwa na dhana kubwa kuliko ilivyo, mtazamo na lengo pana. Dira hii pana ya familia kama sehemu takatifu na ikiwekwa katika mfumo mtakatifu iliwapa utawala wa ziada wazazi na kuongezea katika mshikamano wa kifamilia.Familia ambazo zina uzalendo wa watoto wao zina uwezo mkubwa wa kurithisha fikra ya kuwa wanahusika na kazi muhimu: ya kuendeleza imani, utamaduni, ufundi, falsafa au mtazamo wa jinsi mambo yanatakiwa yawe. Kwa bahati mbaya familia nyingi za sasa hazina mhimili wowote (hazisimamii lolote) "Sio serikali ndogo wala Kanisa dogo", zinafanana sana na "hoteli ndogo na migahawa". Maeneo ambayo mtu hukaa kwa muda mfupi bila dhamira yoyote ya majukumu. Kwa kina tamaduni na maadili yamepuuzwa na kusahaulika kufikia hali "Kila kitu ni sawa tu" na si muhimu. Kitu gani kimeibadili familia kutoka katika mkusanyiko wa jumuiya ya watu na kila mmoja kuwa na dhamira yake? Wataalamu wa kileo wa saikolojia

wa Kimarekani wanaweza kulaumiwa. Msisitizo wao haukuwa kwenye familia wala ndoa, bali kwenye kuachana na ubinafsi. Alfred Adler, anaechukuliwa kuwa ni baba wa saikolojia ya binafsia ya Marekani, ameiita nadharia yake " saikolojia ya mtu binafsi" (Utafiti wa vichochezi, miguso, hisia na kumbukumbu za mpango wa jumla wa maisha ya binadamu). Dr Sardar Tanveer (Profesa wa elimu katika chuo kikuu cha Cincinati) anaeleza kuwa dhana ya "mimi" na "binafsi" yanasisitizwa katika madarasa, ambapo walimu huwaambia wanafunzi: "wewe ndie unaamua sio mzazi wako", "fanya upendavyo". Kwa mfano, msichana mmoja alimwambia bibi yake "huwezi kunipa amri wewe si mama yangu". Bibi akamjibu," lakini mimi ndiye mama wa mama yako" (Semina katika kituo cha ADAMS 1997).

Katika mazingira ya kidini, watoto "hawapokei" amri kutoka kwa wazazi,isipokuwa, wanafamilia wote wanapokea kutoka kwa Mungu ikiwa wanaelewa amri za Mungu kutoka katika vitabu vitakatifu.Uwepo wa sheria njema na wazi za kidini zinazoonesha tabia mbaya na njema hufanya ulezi wa kidini kuwa wa kimamlaka zaidi kuliko ulezi usio wa wazazi wa kidini.

Mifano ya familia za kidini. Mifano mingi ya kidini ipo katika tamaduni za watu wa Mashariki ambazo zinazingatia dhana ya familia na ibada za kifamilia. Hakuna ukale uliobaki katika familia za Kimarekani ambapo ibada pekee iliyobaki ikitekelezwa ni ile ya kuangalia runinga. Suala hili linakejeliwa na pongezi zinazomiminwa kwa kipindi cha The Simpsons, ambacho kwa dhihaka nacho ni kipindi cha runinga. Hata hivyo litakuwa ni kosa la kujumuisha na kudai kuwa utamaduni wa Mashariki ni bora kuliko wa Magharibi.

Udugu wa kifamilia Marekani umevunjwa nguvu na kuzuka mfumo wa kifamilia wa "mikataba ya kijamii" ambapo fikra za mahitaji binafsi zimechukua nafasi ya majukumu kamili. Dai letu ni kuwa familia hizi hazifanyi kazi iwapo washirika wake wataichukulia kama ni kampuni fulani ya ubia, iliyoundwa kwa ajili ya mahitaji yake na si kuzingatia majukumu na upendo. Ulezi wa watoto na kudumisha ndoa ni suala linalotaka kujitolea katika maisha ambalo huweza kuonekana ni jambo lisilo na faida likitazamwa katika mrengo wa gharama yenye manufaa.

> Alikuja mtu mmoja kwa 'Umar ibn al Khattab (R.A) akamwambia kwamba anataka kumtaliki mke wake kwa sababu hampendi tena, 'Umar ibn al Khattab' akamwambia "Ole wako! Hivi familia zinajengwa na mapenzi pekee? Uko wapi uchungaji wako na kujali?
>
> (ALHAASHIM, 1999).

Familia yenye msimamo wa Kikristo Marekani huanza mlo kwa sala ya shukurani na kufanya maombi ya usiku kwa kudumisha ibada za kawaida za kifamilia zinazofuata mfumo wa kalenda ya ibada za kawaida za kanisa. Vitendo hivi hudhihirisha lengo na dhima. Kitovu cha maisha ya kidini ni nyumba

ambayo huwa ni mahali takatifu, na kipaumbele huwekwa katika kuendeleza maadili na imani za watoto. Msisitizo huwa katika kuheshimu wazazi na ndugu watu wazima, kama wakina babu/bibi, shangazi na wajomba. Uhusiano wa karibu huimarishwa kati ya ndugu, na sikukuu kubwa za kidini huwa ni matukio ya kujumuika pamoja kwa furaha. Hivyo isichukuliwe ni ajabu kuwa Wayahudi wanaotekeleza mila zao pamoja na kuwa wanaishi katika mazingira yenye watu wengi mijini watoto wao hawatumii dawa za kulevya, ugomvi, na mahusiano holela ya kimapenzi, mabaya ambayo yamezoeleka kwa watoto wengine wa mijini, vivyo hivyo hali hii inakuwapo katika familia za Marekani za Kiislamu.

Mafunzo kutoka katika Mauaji ya Shule ya Columbine

Mauaji katika shule ya Columbine ya Aprili 20, 1999, Littleton, Colorado yalipelekea kuuawa kwa watu 15, kujeruhiwa 26, na mamia wakabaki na kiwewe. Matukio ya aina hii yaliendelea kutokea baadaye mashuleni Georgia, Kentucky, Arkansas, na Virginia. Marehemu Profesa Dilwanaz Siddiqui alijikita katika tatizo la tabia mbaya. Wachambuzi wengi walilaumu kuporomoka kwa mifumo ya familia, wengine wakilaumu vurugu kubwa za vyombo vya habari, wengine wakishutumu urahisi wa umiliki wa silaha pamoja na silaha za mapambano za wafanyakazi kuwa ni kama mkusanyiko wa mabomu. Bado kuna suala muhimu lilisahaulika katika uchambuzi huo, lijulikanalo kama majukumu binafsi na uwajibikaji wa matendo ya mtu. Imani, nia, mienendo pamoja na maneno yetu vyote hivi vina athari. Tunaweza kufupisha ushauri wa Siddiqui kwa wazazi kama ifuatavyo:

- ❒ Mawasiliano ya binadamu, elimu na maingiliano yanakuza maadili mazuri.
- ❒ Watoto lazima wajifunze imani na viwango vya wema na uovu.
- ❒ Tafsiri za waumini juu ya matokeo ya ukweli katika machafuko ya kijamii. Waumini wanadai kwamba wema na uovu vinategemea na mazingira au hali (hakuna kanuni).
- ❒ Mtoto mwenye siha (nzuri) lazima ajifunze kiini cha maadili ya kiulimwengu (kama vile ukweli, heshima, haki na amani).
- ❒ Wema na uovu havipaswi kuwa na nafasi sawa kwa kustawisha sehemu yoyote. Lazima tuwafunze watoto imani nzuri na kuwasaidia kuondosha imani potofu kadri tutakavyoweza.

Badala ya kuwatetea wahalifu kuwa ni wahanga wa mfumo wa jamii, tunataka kumfanya kila mtu ahukumiwe kwa vitendo vyake mwenyewe. Ni lazima kutathimini matendo yetu kulingana na kanuni tulizo jiwekea. Katika mazingira haya, hatupaswi kudhania kuwa kila mtu anaweza kuzifuata kwa namna inavyo takiwa au pengine kuzikiuka kabisa.

Watoto, Mahesabu na Maadili

Watoto hawatazamiwi kugundua mbinu za mahesabu wao wenyewe. Vivyo hivyo katika maadili, tabia na mienendo, wazazi wanatakiwa kuwafunza watoto wao.

Isipokuwa na hadi kama malezi mazuri yatokee, kutarajie nguvu hizi za uhalifu kuendelea, kama si kustawi.

Kufundisha Watoto Maadili: Malumbano ya Ukale na Usasa

Katika ibara isemayo "Njia pekee ya kufundishia maadili: kuwasaidia watoto wajitambue wao" (Chicago Tribune 1998) Eric Zorn amedai kwamba: "njia pekee ya kufundishia maadili ni kuwasaidia watoto wajitambue, ulinzi wa jamii unasisitiza maendeleo ya maadili, fikra za maadili na maadili ya tabia. Watoto hawastaajabu kupata sifa hizi zaidi kuliko wanavyostaajabu kusoma hesabu. Nafasi ya matumaini yote katika tabia za elimu nje ya shule zimegeuka na kuwa nyoofu katika kipindi kilichovunjwa, familia zenye shughuli nyingi na maadili yanarahisisha utamaduni wa watu.

Eric Zorn anaunga mkono elimu ya tabia shuleni, anazungumza kuwa watu wa mrengo wa kushoto wanazuia urudishwaji wa elimu ya tabia mashuleni kwa sababu inazalisha kutokufikiri, na akili-finyu na kutovumilia. Hata hivyo watoto wanaokuwa bila elimu ya tabia wana hasirika kama ilivyo kwa watoto masikini, wagonjwa, wasio na makazi na walionyanyaswa.

Zorn akimnukuu Larry Nucci: "Maelewano yanayofikiwa ni yanayotambua nafasi ya mtoto kuwa hawezi kulishwa ukweli. Wanatakiwa washiriki kikamilifu katika kufikiri na kugundua. Lakini kwa wakati huo huo bado si watu wazima na kuna nafasi mahsusi ya walimu kuwaongoza. Jamii inatakiwa iwe na mwenendo wa pamoja kama sehemu ya kuanzia – sio "iliyo huru kwa watu wote" kama anavyodai Alfie Kohn kuwa jinsi ya kutekeleza azma hii bila kuifanya elimu ya tabia kuwa ni "Mkusanyiko wa nasaha na mawaidha yatakayofanya watoto kutenda kwa bidii na kufanya lile wanaloamrishwa" kwa mujibu wa Alfie Kohn mfumo huo bado ni tatizo. Kohn alidai kuwa mfumo wa Karoti-na-fimbo ambao ndio mashuhuri kwa elimu za maadili unawaacha watoto wakidhani kuwa haiba ni "utii wa ukweli uliopikwa". Aina hii ya ufahamu haikiti mizizi yake katika tabia ya mtu, na haipelekei uelewa, kushukuru na tabia zingine adhimu za kimaadili. Kuanzisha elimu ya maadili shuleni ni wazo zuri na muhimu kwa hakika ni afadhali kuliko kutokuwa na elimu ya tabia kabisa! Jambo muhimu linatakiwa kuwa kutolazimisha maadili kwa watoto lakini pia si vizuri kuwaacha peke yao, kwa kuwa bado ni watoto na wanahitaji mwongozo. Wazazi wana jukumu la kuwaongoza watoto na kuwasaidia kubaini tabia wao wenyewe inapobidi.

Watoto wanaokuwa pasipo kupata elimu nzuri ya kimaadili wanahasiriwa sawa na watoto wanaokulia kwenye umasikini, wagonjwa, hawana pa kukaa, au wenye tabia mbaya.

Mlinganisho wa Familia katika nchi za Waislamu na Marekani

Ujuzi wetu binadamu una mipaka, haujakamilika. Kuna changamoto nyingi ambazo familia zinakumbana nazo, bila ya kujali wanavyoishi. Bado baadhi ya familia zinakumbana na matatizo kuliko familia nyingine. Kukua kwa miji, kukua kwa viwanda, kuipuuza dini, kuna athari kubwa juu ya familia zinazoishi katika miji.Baadhi ya matatizo katika miji mikubwa ndani ya Marekani na Uingereza ni kama zifuatazo:

- ❒ Kujamiiana kwa watu wasio oana kumekuwa kama ni kishawishi, kivutio na pia ni rahisi kupatikana hali ambayo inapelekea uzinzi wa hali ya juu.
- ❒ Mchanganyiko katika kucheza, kuogelea, na muziki unaoamsha hisia za kujamiiana ni mambo ambayo yameenea sana.
- ❒ Makutano, yanayojumuisha kukutana ana kwa ana [kubusiana, kupeana mikono na busu la haraka] ni mfumo waliovumbua wanaume na wanawake ili wajuane baina yao , na haya ni mafundisho ya wazazi kwa watoto wao, kama ni mila inayokubalika .
- ❒ Utupu katika vyumba na sehemu za kukoga hadharani ni jambo la kawaida vyoo vinaweza kukosa milango kwa baadhi ya shule; stara inakosekana katika sehemu za kuogea.
- ❒ Kujizuia kabla ya ndoa ni jambo ambalo haliwekewi msisitizo wa kutosha, kondomu zinagawiwa kwa baadhi ya shule na baadhi ya makanisa kwa vijana wasiokuwa katika ndoa.
- ❒ Baadhi ya walimu huwaambia watoto “wafanye vile ambavyo wanapenda na wanavyohisi”, bila ya kikwazo cha maadili, matamanio na matakwa viachwe huru na si kukandamizwa, vilevile wanajifunza kuwa ni mtu binafsi,na wala sio Mungu, mwenye mamlaka ya mwisho.
- ❒ Kunywa ulevi ni jambo la kawaida na linavumiliwa na kushajiishwa.
- ❒ Matumizi ya dawa za kulevya yameenea. Bunduki na vurugu ni vitu vya kawaida shuleni na kwa watoto wenyewe tena hadharani kabisa. Maonesho ya runinga yanashajiisha vurugu.
- ❒ Utoaji wa mimba ni jambo linalofanywa sana. Familia inataka kuwa na watu wachache, kuelekea familia inayojumuisha baba, mama, na watoto na kupinga familia inayojumuisha zaidi ya baba, mama; na watoto [k.v, babu, bibi shangazi na mjomba].
- ❒ Wanaume wengi huvaa nguo za kubana na wanawake hujipamba na kujipulizia manukato ili wawe kivutio cha uzinzi. Watu wengi hufunika sehemu chache tu za miili yao na kuwa kivutio zaidi cha mabaya. Ndoa za mapema hazishajiishwi, hali inayopelekea kutowajibika kwa tendo la ngono.
- ❒ Kiwango cha talaka ni kikubwa na familia ya mzazi pweke ni jambo linaloongezeka kwa kasi.
- ❒ Mtoto kuwa na mtoto ni jambo la kawaida, na ndoa za vijana hupigwa vita, hali inayopelekea kuwapo na mama wengi wasiofunga ndoa. Profesa Olasky alisema kuwa asilimia 85 ya mama vijana katika miaka ya 1950 waliolewa katika kipindi ambacho tayari walikwisha kuwa na watoto wao. (Olasksy 1994)
- ❒ Kujamiiana kwa watu wa jinsia moja imekuwa ni jambo lenye kukubalika na la kawaida; la sheria. Majimbo mengi yamehalalisha ndoa za jinsia moja.

- ❒ Wazee wengi masikini wamewekwa kwenye nyumba za uuguzi, kuliko kubaki na watoto wao na wajukuu zao.
- ❒ Ubikira kabla ya ndoa ni jambo la nadra. Wasichana bikira wenye miaka 20 na kuendelea wanazingatiwa kama ni wasiovutia na wasiotakiwa. Wengi hushiriki tendo la ndoa kabla ya ndoa, ujane [unafuata misingi ya dini] ni kwa wachache.
- ❒ Familia zinavunjwa hatua kwa hatua na mafungamano ya familia (*silat al-rahm*) na thamani inakua dhaifu.
- ❒ Maridhiano ya ngono kwa makubaliano na mtu mzima yoyote ni jambo linalozingatiwa kuwa hiari ya mtu binafsi
- ❒ Maradhi yenye kuambukizwa na zinaa [STDs] ni jambo la kawaida ukiwemo UKIMWI.
- ❒ Familia kuzihama kazi zao na makazi yao mara kwa mara; kwa kiasi kikubwa wamekua wa kuhama hama.
- ❒ Wanawake wengi wamekuwa wakijitegemea wenyewe na bila ya ndugu anayehusika na kuwajibika kama ni Mlezi na mlinzi kimaadili na kiuchumi.
- ❒ Wanawake na wanaume hawategemeani na wanahamu ya kujitoa muhanga. Familia nyingi za wanandoa wote ni wafanyakazi.
- ❒ Kuna tofauti ndogo baina ya majukumu ya wanawake na wanaume.
- ❒ Kwa upande wa mwingine, familia za mjini za Marekani na Uingereza zina faida nyingi kama zilivyoshuhudiliwa na wahariri.
- ❒ Kuna ushiriki mkubwa wa wananchi na kuheshimu haki za wengine.
- ❒ Wanafaidi maisha bora.
- ❒ Kuna kiwango kikubwa zaidi cha wasomi.
- ❒ Kuna ushiriki mkubwa katika huduma za kijamii na kazi za Umma. Ingawa mshikamano wa kifamilia ni dhaifu, tegemeo kubwa kwenye taasisi za kijamii ni kawaida ndani ya Marekani.
- ❒ Kuna uhuru zaidi na mbinu anuai za kufikia malengo binafsi.
- ❒ Kwa kulinganisha familia katika Ulimwengu wa Waislamu zipo baadhi ya tabia zifuatazo;
- ❒ Ndoa baina ya ndugu ni za kawaida sana.
- ❒ Familia kiujumla zinasimamiwa na zinalindwa. Ikilinganishwa na familia za Marekani ambapo watoto wanakosa kujiamini, ujasiri na ubunifu. Wanaogopa migongano na viongozi na wakubwa wao.
- ❒ Mfungamano madhubuti wa kifamilia unasimama kama mdhamini wa mwisho wa ulinzi katika jamii ambapo kazi za kijamii na hamasa ya upamoja ni duni.
- ❒ Familia ni mfumo wa uongozi wa mtu mmoja, ambapo ushauri unachukua nafasi ndogo. Kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia miongoni mwa wajumbe wa familia ni maarufu sana.
- ❒ Familia zinazofuata dini ya Kiislamu hazialikwi na zina kazi mbaya. Matukio ya kidini yanatokea sana kama kaida za ibada na amri kuliko furaha ya matakwa ya mazingira ya kiroho

Tangu hapo na zaidi familia za Kiislamu sasa zinaishi mijini, ni muhimu kutambua madhila yanayowapata watu wa mjini. Malezi ni magumu kwenye miji.

Hadithi za Waislamu Wanaoishi Uingereza

Bw. Bakry, kutoka Mossul, Iraq alihudhuria katika chuo cha mafunzo ya kijeshi Uingereza. Katika sehemu ya kuogea, kila mtu alioga bila ya nguo, isipokua Bw. Bakry yeye alioga na nguo yake ya ndani; Ofisa wake akamuuliza "kwanini huondoi nguo yako ya ndani?" Bw. Bakry kwa umakini alielezea kwamba Waislamu hawaoneshi utupu wao na sitara kwa mtu ni jambo la muhimu sana.

Bw. Muhammad, yeye anasoma katika chuo kikuu cha Birmingham, Uingereza aliulizwa na mama mwenye nyumba wake. "Kwanini huna rafiki wa kike?" Je wewe ni mwenye kufanya mapenzi ya jinsia moja? Akamjibu kuwa kujamiiana kunaruhusiwa kwa mke na mume tu katika Uislamu.

Majumuisho hayo hayamaanishi kuwa mfumo upi wa familia ni bora. Inalenga kuibua mambo yaliyopo hivi sasa, ili waweze kufikiri na kujifunza na ili kuwe na mifumo mizuri ya utekelezaji kwa wazazi katika pande zote. Kiukweli, kuna ushajiishaji imara kutoka katika utamaduni wa Kimagharibi juu ya familia na wazazi wa ulimwengu wa Kiislamu. Ushawishi huu una matokeo mchanganyiko mengine ni mazuri na mengine ni mabaya. Katika mfumo wa elimu usioendeshwa kwa misingi ya kidini. Mwanadamu anachukua nafasi ya Mungu, kama ndiye mwenye mamlaka yote, na uchaji vitu ndio fikira iliyotawala kwa watu. Ufahamu wa kisayansi kuhusiana na ulimwengu unategemea sababu na athari tu. Ingawa mahubiri ya kisayansi hutupa uthibitisho wa kuvutia sana kuhusu nyanja za uyakinifu juu ya ulimwengu, haitoi nafasi ya ufahamu wa juu ya tunachokiona na vile tulivyotakiwa tuone kabla.

Ulimwengu wa Kiislamu unatambua juu ya umoja wa Mungu, (*tawheed*), uaminifu wa binadamu (*amanah*) na uwajibikaji kwa maendeleo ya dunia (*imran–istikhlaf*) pamoja na kuhesabiwa siku ya kiyama.

Athari za Umagharibi katika Malezi Ya Kiislamu

Kutokana na kuongezeka kwa vyombo vya habari vya Kimagharibi na kudhibitiwa kwa elimu na Wamagharibi, maisha ya familia za kiulimwengu yameathiri wazi wazi familia za Waislamu. Katika kitabu chake (kwa Kiarabu) Kuelekea Elimu Huru ya Kiislamu [tarbiyah] katika Serikali na Nchi za Kiislamu (*Towards Free Islamic Education*) [tarbiyah] *in Muslim Governments and Countries,* Abu al-Hasan al-Nadwi anazungumzia mageuzi thabiti ya mfumo wa elimu. Anaorodhesha athari za mitaala ya Kimagharibi, zinazoyumbisha haiba na kudhoofisha imani. Kizazi cha wahitimu wa vyuo vikuu kimeibuka na kupoteza thamani, kutokana na kuwa na shule zinazozalisha viongozi na watawala wenye kupiga vita dini, kuwanyanyasa waumini, na kuzilazimisha nchi zao kuanguka kiuchumi. Elimu ya Kimagharibi ambayo imefikishwa kwenye jamii za Waislamu huzalisha vijana walio-

changanyikiwa, wasioweza kupambana kwa ajili ya maadili, au kuanzisha mtazamo madhubuti wa pamoja wenye kuunganisha mwili na roho.

Kinachoweza kuwa kizuri kwa tamaduni zingine kinaweza kisifae kwa watoto wa Kiislamu. Wakati wanazuoni wa Kimarekani wakikosoa kuhusu mafanikio makubwa ya shule za Kijapani, wanasisitiza kuwa mengi ambayo ni mazuri kwa Japani hayafai kwa Marekani kwa sababu ni mifumo miwili tofauti ya kiutamaduni. Upofu wa kunakili tamaduni zingine kunapelekea matatizo mengi. Kulea ni kazi inayohitaji uangalifu na lazima ifanywe kwa taaluma na busara.

Mataifa yanaitika Umagharibishaji na Usasa kwa namna tofauti. Profesa Ali Mazrui (Chuo Kikuu cha Taifa cha New York) anaelezea kuwa kunapoulizwa "tunaweza kuendana na uchumi wa kisasa pasipo kuendana na tamaduni za Kimagharibi?" lililoelekezwa kwa Wajapani, Waturuki, na Waafrika, hali tatu tofauti zilijitokeza. Wajapani walijibu: "Ndiyo. Tunaweza kuwa na mbinu za Kimagharibi na kudhibiti imani za Kijapani". Waturuki, wanaochukua urithi wa Mustapha Kemal Ataturk wanaamini hapana: Hapana, Umagharibishaji wa kiutamaduni ni njia tu kuelekea Usasa". Waturuki wafuasi wa Kemal wote wa karne ya Ishirini wamefanya kila waliloweza ili kulazimisha Umagharibi kwa watu wake, ikiwemo kusitisha matumizi ya tahajia za Kiarabu na kuanza kutumia za Kilatini; kupiga marufuku tarbush (vazi la kichwa kwa wanaume); kuwalazimisha wanawake kufuata sheria za mavazi za Kimagharibi; na kuanzisha dola la Kimagharibi. Ukoloni na Ukoloni Mamboleo wa Waafrika ulijibu: Kutekeleza utamaduni wa Kimagharibi pasipo uchumi wa kisasa," ambao kwa kweli ulikuwa ni mbaya kwa pande zote. (Jumuiya ya Jamii ya Wanasayansi wa Kiislamu Bulletin, 2002).

Malezi katika Nchi za Uingereza na Marekani

Ukaguzi wa (Mfuko wa Kimataifa wa Watoto –UNICEF), ambao ulihusisha nchi tajiri 21 ambazo uliangalia vipengele 6 (uwezo wa kifedha, afya na usalama, ,elimu, uhusiano wa kifamilia, tabia na majanga,na vijana wenye hisia za kujitegemea). Ulionesha ya kwamba nchi za Uingereza na ushirika wa nchi za Marekani zilikuwa mwisho kimalezi katika vipengele vilivyoangaliwa (UNICEF REPORT 2007) Watoto wanaathirika licha ya kwamba kuna kiwango kizuri cha mali ya taifa, kwa sababu ya uzorotaji wa uchumi na kutokuwepo uwiano na uduni wa usaidizi kutoka serikalini kwa jamii katika nchi za Marekani na Uingereza na kuwepo kwa huduma mbovu za kijamii ambazo zitasaidia watoto pamoja na familia zao. Hii inaonekana ya kwamba Marekani na Uingereza haziwekezi sana katika malezi ya watoto kama nchi nyengine za bara la Ulaya.

Vipengele Vidogo vya Ukaguzi vya UNICEF

Asilimia ya wanaokula chakula cha siku pamoja na familia zao mara nyingi kwa wiki	Uwiano wa watoto ambao wana utimilifu na msaada au ushirikiano na watoto wenzao
Hali ya afya	Huduma za siku
Kinga kwa watoto	Afya na usalama
Matatizo ya familia za mzazi pweke	Vifo vya watoto
Tabia hatarishi miongoni mwa watoto	Kinga kwa watoto
Unywaji pombe	Vifo kutokana na kuumia au ajali kabla ya umri wa miaka 19
Matatizo ya kujamiiana	Kupigana katika kipindi cha zamani
Kiwango cha watoto wanaoishi na mzazi pweke au wazazi wa kambo	Watoto Walioonewa katika miezi miwili iliyopita

Uhuru au Ukweli?

Tatizo moja wapo katika malezi ya watoto ni uhuru binafsi, katika nchi zenye maendeleo ya viwanda, uhuru umekuwa ni kitu cha msingi kwa mtoto. Wazazi wengi huwapa watoto wao uhuru usiokuwa na mipaka, hali inayochochea matamanio binafsi kwa mtoto. Matamanio yasiyokuwa na mipaka ni hatari kwa sababu unaweza vunja maadili ya Mungu na hali ya kuhurumiana miongoni mwa wanadamu, kuwateka watu katika tamaa za kidunia, starehe na anasa zitafanywa ndio lengo la maisha kwa watoto.Katika Uislamu msisitizo umewekwa katika uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ambao hautakiwi kuondoshwa na tamaa za ghafla “ishi katika dunia kama kesho utakufa” Qur’an inaeleza hali hii kama ifuatavyo:

> Je! Umemwona aliye fanya matamanio yake kuwa ndiye mungu wake, na Mwenyezi Mungu akamwacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi, na akapiga muhuri juu ya masikio yake, na moyo wake, na akambandika vitanga machoni mwake? Basi nani atamwongoa huyo baada ya Mwenyezi Mungu? Hamkumbuki?
>
> Na walisema: Hapana ila huu uhai wetu wa duniani - twafa na twaishi, na hapana kinacho tuhiliki isipo kuwa dahari. Lakini wao hawana ilimu ya hayo, ila wao wanadhani tu. Qur’an 45:23-24.

Uhuru wa kuepukana na matamanio unampelekea mtu kufika sehemu nzuri.

Lau-Tzu-Muanzilishi Wa Taoism, Karne 6).

Ushindi wa kwanza na bora ni kuishinda nafsi.

Plato, Mwanafilosofi Wa Kigiriki

Uhuru ni zawadi kubwa ya thamani ambayo haitakiwi kutumika kwa starehe tu pasi na kuzingatia jema na baya.

Uhuru ni jambo jema kwa kutumia uhuru tunaweza kujua ukweli, kwa kuutafuta na kuuelewa. Swali la msingi la mwanadamu ni kujua ukweli ambalo ndilo lengo la msingi. Wakati uhuru unapotumika kwa busara na kwa lengo tarajiwa hapo mwanadamu huwa ametenda vyema kwa bwana wake na hapo mwanadamu atajua jema na kulifanya na ovu na kuliondosha. Watoto ni lazima wafunzwe kuwa na tabia njema, kufanya maamuzi sahihi na kushikamana na ukweli kwa hali yoyote ile, ukweli unakuja kabla ya uhuru. Kila mfumo katika ulimwengu una mpaka wake na ndio hivyo hivyo uhuru wa mwanadamu ni lazima uwekewe mipaka kulingana na mwongozo wa maadili na vinginevyo. Kwa wazazi wana wajibu wa kuwafunza watoto mtazamo sahihi na imani ambazo zitaendana na vitabu vya dini maandishi na hadithi za mitume amani iwe juu yao.

Ni vyema kutumia uhuru wetu kumridhisha Mwenyezi Mungu, sio kwa kutumia elimu sahihi peke yake lakini na elimu ya uhalisia wa mwanadamu. Tukichanganya hizi elimu zote zitatusaidia tusiwe vipofu na tusiharibu mazingira na sisi wenyewe. Muumba ndiye ajuwaye vyema kuliko sisi na yeye pekee ndiye atakaye tuongoza katika njia sahihi kwa msaada wa utafiti, majaribio ya kitaaluma na ujuzi tutaweza kuwa karibu na mwongozo sahihi na kuelewa jibu sahihi kulingana na muda.

Chukua familia kama ni mfano, wataalamu wa akili na tabia pamoja na wataalamu wa masuala ya kijamii wanatuambia ya kwamba umoja wa kifamilia ni jambo bora na jamii inaweza kuanguka kwa kukosa jambo hili. Kama jamii isingeelewa umuhimu wa mjengeko wa familia kuanzia mwanzo, basi kusingekuwa na jamii hivi leo. Maadili tofauti ya msingi kama ukarimu, uaminifu, heshima, mali, masuala ya kujamiiana, usawa, kuwa huru kutokana na unyanyasaji na vitu vya msingi vya kuishi mwanadamu. Pasi na kuwepo hivi vitu, jamii haiwezi kuwa vyema na hivi vitu vina jengwa na familia. Kwa hiyo, kitu cha msingi kuhusu haya maadili inahitaji jamii ivitengeneze kabla ya ubinadamu kugundua haya. Vitu hivi vikawa vimo katika fikra zetu, katika maumbile yetu au fitra (maumbile) na kama ilivyoelezwa uwepo wa mwanadamu unahitaji ubinaadamu.

Ndio maana, haikuwa katika kipindi cha Adamu ambaye ni baba wa ubinaadamu katika dunia na Hawa ambaye ni mama wa ubinaadamu kuwa walifunzwa haya maadili ya ubinaadamu ambapo wao waweze kuwafunza watoto wao na kuenea katika ulimwengu. Mwenyezi Mungu anaelezea kisa cha Qabiil na Haabil hebu angalia kama Adamu, Hawa na watoto wao kama wangekuwa wanywaji pombe, au waathirika wa dawa za kulevya au masuala ya ngono zembe, matokeo yake yangekuwaje?

Ufunuo unaongoza katika elimu ya mwongozo ambayo inatutoa katika giza, pasina huu mwongozo ustaarabu ungeangamia na kutoweka katika jamii. Uhuru wenye mwongozo sahihi unapelekea

Katika juhudi zao katika kuitoa dini nje ya madarasa, wakatupa maadili nje ya dirisha

kupata watoto wastaarabu na jamii bora, ambayo itaishi vyema kwa vile watajiepusha na tamaa za nafsi, tabia njema na kutunza mazingira vyema. Ulimwengu ni mfumo uliokamilika: chembe hai, atomi, na mfumo wa mpango wa galaxies wenye mpangilio wa hali ya juu na hii mifumo yote inaenda kulingana na sheria na mipaka. Kupuuzia mipaka hii kutapelekea kuharibu utaratibu. Muumba ametengeneza ulimwengu kwa makini na vipimo vilivyosawa na kusisitiza kuhusu ukamilishaji na maingiliano. Dhana ya usawa imeelezwa mara tatu katika aya zifuatazo:

> Jua na mwezi huenda kwa hisabu.
> Na mimea yenye kutambaa, na miti, inanyenyekea. Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani, Ili msidhulumu katika mizani. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.
>
> (Qur'an 55:5-9)

Maadili ya msingi, kwa hivyo, ni lazima yatunzwe kwa gharama yoyote ile, watu wasiharibu maisha na kujiuwa hata kama watakapo ona kujiuwa ni njia mbadala wakati mambo yanapoenda kombo. Watu wasiuane, watu wasinywe pombe, wasile dawa za kulevya, wasijiangamize wao na familia zao na jamii zao. Mwanadamu alipewa mwongozo kupitia ufunuo tangu zama za mwanzo.

Elimu ya mwanadamu ina mipaka yake na inaweza chukua muda watu kuelewa thamani yake na kuelewa matatizo ya ubaguzi wa rangi, kujiua, unywaji pombe, dawa za kulevya na uzinzi. Mwongozo sahihi kuanzia maisha ya mwanzo ya mwanadamu katika dunia ilikuja kuonya matendo haya mabaya kwa ajili ya kushajiisha maadili mema. Lakini kwa bahati mbaya katika juhudi zao za kutaka kuitupa dini nje ya madarasa, wakatupa maadili nje ya dirisha

Mchungaji na mwandishi Dkt. Jerald F.Dirks waziri mstaafu (deacon) katika kanisa la methodist, ambaye aliingia katika uislamu mnamo 1993, wakati alipoulizwa kaika semina ya IIIT kitu gani muhimu kipya ambacho angeweza kukianzisha katika mtaala makanisani alijibu: kujiepusha na matatizo ya kujuana kuhusu maadili na ustaarabu ambayo yanapelekea mabadiliko hatarishi ujumbe wa msingi bado upo na haubadiliki kulingana na kizazi cha sasa. Baada ya hayo yote, mahitaji muhimu ya mwanadamu yatabakia kama yalivyo. Utaratibu wa familia ni vyema ukatunzwa na ukalindwa kwa ajili ya kuepuka mmong'onyoko wa maadili katika familia.

Waislamu waweza jifunza katika mtazamo sahihi, kutokana na uhuru wa Umagharibi kwa ajili ya kuondosha udhalilishaji na ubabe katika kutoa maamuzi na kuongoza watu katika kuwatawala vibaya, na kuwafanya wazorote katika maendeleo. Waislamu wamepoteza nafasi yao ya msingi katika dunia kwa vile wao ndio wajenga maadili.

Mfumo Adili (*adl*) na Kushauriana (*shura*) (mfumo wa uadilifu na ushauri) ambao unatakiwa kuongoza mifumo yote ya Uislamu, kisiasa, kijamii, na mshikamano, wa kifamilia ikijumuisha familia na malezi imeondoshwa na mbadala wake ni kutawaliwa na fikra za kidhalimu.

Wamagharibi wanahitaji kueneza mfumo wao ambao ni potofu, ambapo Waislamu wanahitaji ukombozi dhidi ya udhalilishaji. Kwa maneno mengine uhuru wa mwongozo kwa watu wa Magharibi na uhuru wa Waislamu kutokana na matendo yao yaliyo haribiwa, jamii zote ni lazima zijifunze na kuchunga uelewa wao na matendo yao kwa kuzingatia mwongozo sahihi.

HADITHI YA RONALD KELLER

Tunahitaji imani thabiti na mfumo bora wa maadili kwa ajili ya kuishi kwa furaha.

“Nilizaliwa 1954 katika ardhi ya kilimo kaskazini-magharibi ya Marekani, nililelewa katika familia yenye maadili ya kidini ya Katoliki. Kanisa lilishajiisha imani ya kiroho ambayo haikuibua maswali utotoni mwangu jambo ambalo lilinifanya nifuate mkumbo katika maisha yangu, kuwa kuna vitu vya kweli kuliko vile vilivyo nizunguuka mimi, lakini nilivyoendelea kukua na baada ya kuingia chuo kikuu cha Kikatoliki na kusoma sana nilianza kuielewa vyema dini na kupata maswali ya kujiuliza kuhusu matendo na imani.

Sababu moja wapo ni mabadiliko ya kila siku ya ibada na imani ambayo yalitokea katika Baraza la Vatikani la pili la 1963 lilimpelekea mtu wa kawaida kuamini kwamba makanisa hayana maadili yenye msimamo mmoja. Kwa kila mmoja baada ya mwingine, watumishi wanahubiri kuhusu ubadilikaji na ufanyaji wa ibada lakini kwa Wakatoliki wa kawaida, wanaonekana kama waliotengwa gizani. Mungu habadiliki, hahitaji roho ya mtu, na hakuna ufunuo mwingine (mpya) kutoka mbinguni. Bado tunapigania mabadiliko, wiki baada ya wiki, mwaka baada ya mwaka; tunaongeza, tunatoa, tunabadili lugha kutoka Kilatini kuwa Kingereza, na mwisho tunaingiza magitaa na wana muziki. Mapadri wanaelezea na kuelezea kadri watu wa kawaida wanavyoshangaa kwa kushika vichwa vyao. Kutafuta umuhimu kuliacha idadi kubwa wakishawishika kwamba haukuwepo umuhimu wa kutosha tangu mwanzo”.

NUH HA MIM KELLER 2001

Wapi pa kukuzia Watoto?

Uchunguzi Kuhusu Matatizo ya Kiutamaduni ya Kwenda Baina ya Mashariki na Magharibi

Wakati familia zinapohama kutoka Mashariki kwenda Magharibi au kinyume chake, wachunguzi wameona kuwa utamaduni hubadilika kwa namna yeyote ile, kwa mfano, kuna hadithi ya kweli ya familia moja yenye kusikitisha iliporudi kwenye nchi yake ya Kiislamu, baada ya kuhitimu katika chuo kilichopo Marekani pamoja na watoto wawili wapya.Ingawa walipata nafasi ya kuchagua kufanya kazi katika jimbo moja la Marekani ila familia hiyo iliamua kurejea Mashariki ya kati kwa ajili ya kuwafunza Qur’an na kiarabu. Katika Nchi hiyo watoto walianza kujifunza mabadiliko ya ustaarabu wa Nchi mpya na walitoa mshango kwa kusema: “Yuck, hii ni sehemu chafu sana”. Walipoingia ndani ya vyumba vyao kila kitu walichokigusa kilichafuwa mikono yao.Ingawa wazazi

walihakikisha kuwa vyumba kiukweli vilikuwa safi. Lakini kuta, koridoo, sakafu, sehemu za kukalia na baraza kweli havikuwa safi. Kwa sasa tatizo lao ni kwa vipi watajitoa katika uchafu huo. Ufumbuzi wa tatizo hili ni kuvisafisha vyumba vyao wao wenyewe.

Tatizo la pili ni kwamba, wakati malighafi za kutengenezea zilikuwa ghali, watengenezaji walikuwa hafifu. Milango ya chooni ilikuwa haifungi vizuri, vigae vilikuwa vizuri lakini haviko sawa na vinahitaji uangalifu. Licha ya kuwa na uchache wa maji na maingiliano ya kila siku ya huduma ya maji, mipira ilikuwa inavujisha maji.Katika ghorofa ya tatu msukumo wa maji ulikua mdogo na kila mmoja hujaza maji kwenye ndoo na huyaweka au huyahifadhi kwa ajili ya usiku.

Tatizo lingine ni kuhusu shule. Shule binafsi zilikuwa ghali na shule za kawaida zilikuwa dhaifu kitaaluma. Walimu walikuwa wanahitaji kufunzwa na watoto katika sehemu kubwa walikosa malezi na heshima. Wazazi ndio pekee waliokuwa na uwezo wa kupima faida na hasara ya kuwapeleka watoto wao katika Shule walizozitaka!!!

Usafiri ulikuwa wa polepole sana kwa sababu ya msongamano na ukosefu wa miundo mbinu bora ya barabara. Umbali wa vituo vya kuegeshea magari ya shule yanawasababishia watoto kutumia muda mwingi kwenda na kurudi shule. Mara nyingi ilikua ni rahisi kutembea kwa miguu kuliko kuendesha chombo cha moto. Kutembelea ndugu au marafiki ni lazima upange safari kama unayepanga safari ndefu ya kutoka mji mmoja kwenda mji mwengine. Kuendesha gari kunategemea ujuzi wa hali ya juu na jitihada (ni kama kuingia sehemu ya vita na kukumbana na vikwazo tofauti vya maadui).

Pamoja na kuwepo uchafuzi wa hewa kulikuwa na fujo za makelele zilizo chafua usikivu. Watoto wanapoteza haki zao na utulivu wa akili kwa sababu ya sauti kubwa yenye kuendelea katika mazingira yaliyo wazunguka, mfano shuleni, njiani na kutoka kwa majirani zogo lilivamia vyumba vyao wakati wa mchana. Njia nzuri ya kupata ukimya ni kwenda vijijini. Huu ni kama mfano mmoja wa kuweza kubadilisha utamaduni ambao unaweza kutokea na kuelezea mambo ambayo familia huamua kuhama (aidha kutoka Magharibi kwenda Mashariki au kinyume chake). Sababu hii haiwezi kujumuishwa kwani si kila mmoja anayeweza kukutana na tatizo hilo hilo au jambo hilo hilo.

Hii haina maana ya kwamba familia ni lazima iishi Mashariki au Magharibi. Zaidi ya hayo kila nchi ina vivutio vyake na matatizo yake, na kila familia ina upekee katika mambo yake. Hakuna njia maalumu ya kuonesha sehemu gani ni nzuri kwa kuishi watoto. Familia ambayo inachagua sehemu ya kwenda ni lazima ieleze vigezo vizuri na vibaya ambavyo watakutana navyo. Maisha ni majaribio!!!

Dhana Mbili zinazokosekana katika fikra za Kimagharibi

Katika mijadala kadhaa iliyoendeshwa na watunzi, Dkt. Taha Al-alwani, mdhamini wa IIIT, Virginia, alielezea namna Magharibi ilivyokosa dhana mbili muhimu: **Mungu ni Mkubwa** *(Allahu Akbar)*; na **Mungu anajua zaidi** *(Allahu Aalam)*. Katika dhana ya kwanza, wakati wanadamu wanapodharau hekima na mamlaka ya Mwenyezi Mungu katika mambo yao, wamejiwekea miungu yao wenyewe katika nafasi ya Muumba, Mmoja na Mpweke. Ikiwa watu watakuwa wajinga, wasioongozwa, na kuchukulia kuwa wamesalimika na makosa na ndiyo chanzo pekee cha taaluma, kisha wanaweza kuhalalisha kutenda wapendavyo wenyewe, familia zao, jamii zao, ulimwengu, na mazingira yao. Wanaweza kwa kujua au kutojua kuharibu makundi ya wanyama na makundi ya miti, na kuichafua ardhi, bahari, na anga. Kiburi hupelekea kuharibika kwa mpangilio na usawa wa kimaumbile, na anga na weupe vilivyowazunguka (tabaka la ozone). Kwa sababu wanadamu wamevishusha thamani viumbe vya Mungu, wamevikasirisha, mfumo wa kutegemeana na maumbile (kama vile hewa safi, maji safi, na nyama safi isiyo na kemikali na mboga mboga vimekuwa adimu). Mabadiliko ya tabia nchi ni tishio hasa kwa uwepo wa wanadamu. Bila kujali ni kiasi gani tunaendelea katika sayansi na teknolojia, bado hatuna thamani ikilinganishwa na sehemu kubwa ya uumbwaji wa ulimwengu.

Kwa unyenyekevu tunaweza kusema kuwa Mungu Anajua Zaidi (Allahu Aalam). Ugunduzi wa mwanadamu usiotarajiwa kisayansi na teknolojia mpaka karne ya Ishirini na Moja umewafanya watu wengi kujivunia taaluma ya mwanadamu kwa kiburi. Haidhuru, kinyume chake ni kuwa kila tunavyojua, ndivyo tunavyogundua kiasi gani hatujui. Kusema ukweli kwa wengine na unyenyekevu kwa Mungu ni viambatisho muhimu ili kupata utaalamu wa heshima. Wanazuoni wakubwa wanalifahamu hili. Wanadamu lazima waendelee kuchunguza na kugundua taaluma mpya zaidi. Kumbuka kuwa hamu ya kujifunza ni kutokana na baraka za Muumba, Mfalme wa wote, aliyetujaalia akili na nguvu kuliko viumbe wote ulimwenguni. Qur'an inatupa mwanga katika mada ya taaluma.

> ...Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu
>
> (Qur'an, 17:85).

> …Wala wao hawajui chochote katika vilivyo katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe…
>
> (Qur'an, 2:255)

> Sema: Lau kuwa bahari ndio wino kwa maneno ya Mola wangu Mlezi, basi bahari ingeli malizika kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu Mlezi, hata tungeli ileta mfano wa hiyo kuongezea.
>
> (Qur'an, 18:109).

Inamhitaji mtu hodari kuwa kweli *mnyenyekevu*, na *mnyenyekevu* kuwa hodari wa kweli.

Thamani ya Aqida Dhidi Ya Umuhimu Wake

Familia ndio inayofunza maadili ya familia yake, mfano uaminifu, haki, mapenzi, ukarimu, uwajibikaji, majukumu pamoja na kuthubutu, haya yote yanapatikana katika aqida kabla ya utendaji. Mambo mawili haya (Aqida na Utekelezaji) siku zote si lazima yategemeane. Kwa baadhi ya jamii furaha ndio lengo la mwisho la maisha ya hapa ulimwenguni.Kwa upande wa Waislamu kuweka usawa baina ya maisha ya dunia na matendo ya kufikia kuipata pepo. Hii ina maana kwamba kufanya matendo ambayo yatamfanya mtu kufanikiwa katika maisha ya akhera hayapingani na kuishi maisha mazuri hapa duniani.

Kufanya matendo mazuri ili kufanikiwa katika maisha ya akhera haimaanishi kwamba tudharau maisha ya dunia. Maisha ya dunia ni njia ya kufikia maisha mema ya akhera. Mtume alimshauri bedui mmoja amuamini Mwenye Mungu lakini wakati huo huo afuate kanuni za kimaumbile ya kisayansi na sayansi ya jamii " mfunge ngamia wako (ili asipotee) na mtegemee Mungu (Omba msaada wake pindi utakapoondoka)"Tunatakiwa tuweke usawa baina ya maisha ya dunia na maisha ya akhera.

> **"Tafuta maisha kama vile utaishi maisha ya milele katika dunia hii na uitafute akhera yako kana kwamba utakufa kesho"**
>
> **(ABU-TALIB, 1996).**

Wanachuoni wa Kitalmudic wanasema:"Ishi kila siku kana kwamba ni siku yako ya mwisho, kwani hakuna anayejua kama atafika kesho". Mfano mzuri wa kuzingatia ni jamii zilizopita zilizokuwa zikifuata mfumo wa Ujamaa, wafuasi wa Ujamaa wanajifanya wanajali sana wafanya kazi kuliko mabepari, lakini ukweli ni kwamba wafanya kazi wanaishi maisha duni sana katika jamii zinazofuata Ujamaa.Hata kama jamii zinazofuata Ujamaa zinaonekana kumjali sana mfanya kazi, matokeo yake ni migogoro, ukandamizaji, uvunjifu wa amani katika jamii.

Nchi za Kimagharibi zinaonekana zimefanikiwa sana kupitia ubepari kwa sababu wanatumia mafundisho ya Ukristo ya kupendana, kutoa sadaka pamoja na kuhurumiana. Ndio maana nchi hizi zinawajali sana na kuwasaidia masikini na watu wenye mahitaji maalumu, wakati watu wengine katika jamii za ujamaa (kikomunisti) wanaishi maisha duni.

Ujima ulianguka kwa sababu ya ubinafsi na mtazamo wa dunia kuhusu mfumo huo, imani hii imejikita katika migogoro na huharibu haki ya umiliki mali. Hata kama imani hii imejikita katika kusaidia tabaka la wafanya kazi, kuwarudishia heshima zao na uwezo, tabaka la wafanya kazi limebaki kuwa ni lenye kukandamizana kinyume na malengo yaliyotangazwa na

Itikadi ya ukomunisti. Falsafa ya kikomunisti ilikuwa imekita mizizi, haifanyi kazi na ya kufikirika, ambapo hali katika Magharibi ilikuwa bora zaidi. Ubepari haukutoa mafunzo kwa mfumo wa kufikirika (utopia) duniani. Kulingana na dhana ya uhuru uliokosa miongozo katika umiliki binafsi na falsafa ya maslahi binafsi na faida itokanayo, umeleta baadhi ya mfumo wa kudhulumu hali ya kijamii na kiuchumi kwa wafanya kazi. Ingawa ni

dini iliyojiimarisha na maadili ya Kikristo na upendo kwa upande wa Magharibi ulisaidia kupunguza baadhi ya madhara yenye athari kwa wafanya kazi walio katika daraja la chini, na hivyo kupunguza baadhi ya athari zinazotokana na viwanda.

Hii ni tofauti katika chama cha kikomunisti wasomi hufanya kazi kwa maslahi yao wenyewe kwa njia ya mfumo mkubwa wa urasimu ulioundwa imara katika ufanyaji kazi. Ilikuwa ni kwa tabaka la wafanyakazi chini ya Ukomunisti ambao walikuwa waathirika wa mfumo huu. Wema wa dhati na maadili imara ya kidini ni muhimu kwa faida ya jamii na watu binafsi.

Ingawa sehemu kubwa ya maandishi na utafiti juu ya malezi inapatikana katika nchi za Magharibi, uwezo wa maarifa ya binadamu ni mdogo sana kwa kweli. Watu si tu ni bidhaa "iliyotengenezwa Marekani" au "iliyotengenezwa China" ambao tuna ujuzi mzuri. Sisi tumeumbwa na "Muumba wa Ulimwengu." Ni Muumba wetu na Msanifu wetu anajua kila kitu kuhusu sisi.

Mfano katika kitabu chake kilichoitwa *"Parenting experts: Their Advice, the research and getting it right"* Mwanasaikolojia Jane Rankin alionesha utofauti uliopo baina ya wahubiri wanaohubiri kuhusu malezi na tafiti za wanasayansi miaka 30 iliyopita. Wataalamu maarufu wa nchi hizo za Magharibi wa masuala ya malezi kama vile Benjamin Spock, T Berry Brazil ton, James Dobson, Penelope leach, John Rosemond, na wengineo wametofautiana katika mambo mengi sana kuhusu malezi, mfano kupongeza, kuweka mipaka, mama mfanya kazi, mlezi, mlezi wa nje n.k.

Ingawa tunatakiwa tuzidishe tafiti kuhusu masuala ya malezi, kutumia nyezo zilizokuwepo za jamii, kimaumbile na sayansi ya jamii bado tunapaswa kuangalia matokeo ya tafiti hizo za mwanadamu. Tunatakiwa tufuate mwongozo na malezi kupitia taaluma ya Muumba.

Kiburi + Maarifa → Ujinga
Unyenyekevu + Maarifa → Uerevu

Miaka mia moja iliyopita, bwana mmoja katika shule ya Balliol katika chuo kikuu cha Oxford, Uingereza, aliweka nukuu katika mlango ikieleza kwamba:

"Mimi ndiye bwana wa chuo hiki; kile nisichokijua basi si katika maarifa .Watu ambao huwa wapole kwa wenzao hawafiki mwisho kwa kujikweza

Familia ni mfano wa Kilimo

Watoto kama Mimea, Wazazi kama Wakulima

"Neno Utamaduni (Culture)" limetokana na neno kilimo (cultivation). Watoto na viumbe hai ni kama miti vyote kwa pamoja vinahitaji uangalifu na kutunzwa na kukua vizuri katika mazingira mazuri, ambayo yametayarishwa kwa ajili yao. Mazingira bora kwa mimea midogo midogo ni nyumba ya kioo (greenhouse), kwani miti hiyo inahitaji kufanyiwa jitihada kabla ya kupandwa kwa kuhamishiwa sehemu nyengine, kupitia hifadhi hiyo miti hiyo hupata kuota vizuri na ikipandikizwa, miti hiyo hukua kwa haraka, huwa madhubuti na huepukana na maradhi mbalimbli. Watoto nao wanahitaji kulindwa na kulelewa kwa ajili ya maendeleo ya kiafya na kimaadili. "Wana wetu na wawe kama miche waliokua ujanani. Binti zetu kama nguzo za pembeni Zilizonakishwa kwa kupamba hekalu. (Zaburi,144:12). Mtoto aliyelelewa katika mazingira mazuri atakua mwenye nguvu, afya na kupata kinga dhidi ya maradhi hatari ya kimaadili, yanayozikumba tamaduni nyingi. Mfano huu unadhihirisha kuwa kilimo jamii si kiwanda jamii. Hata hivyo watoto ni zaidi ya mimea, kwani mimea haina hisia wakati watoto ni wenye hisia, wenye akili, wenye kutumia nguvu nyingi wenye matamanio na mapenzi. Watoto pia wanahitaji kutimiziwa malengo yao kwa ajili ya maendeleo na wanahitaji kufunzwa kwa ajili ya kujiwekea mipaka katika mambo yao. Mpaka sasa watoto wanahitaji msaada wa hali ya juu na njia nzuri kwa wazazi ni kuwashajiisha na kuwaelekeza katika maadili mazuri na tabia njema.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI 8: HOFU TATU KUBWA ZA KARNE YA ISHIRINI NA MOJA

Jadili na familia: Ni zipi sababu ya hofu hizi kubwa tatu na vipi zinaweza kuzuiwa?

Katika mwaka 1997, marehemu Willium Buckley (Nguzo isiyotetereka) na Seneta George Mc-Govern (Mwanademokrasia Mpenda Mabadiliko), kwenye mahafali ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Kusini Mashariki, Cape Girardeau, alibainisha hofu tatu kubwa:

Ya kwanza ni kuharibika na kushindwa kufanya kazi vizuri kwa familia za Kimarekani, hali iliyopelekea kuwa na asilimia kubwa ya watoto wa haramu. Ya pili ni uharibifu wa mazingira, ambapo uchafuzi mkubwa wa hewa umepelekea hewa chafu kutapakaa ardhini, angani, baharini, katika mabwawa na msituni. Ya tatu ni unywaji wa mvinyo kunakofifisha afya za watu na familia zao.

ZOEZI 9: MATUMIZI YA TABIA KWA WATOTO (KWA MFUATANO)

Wazazi wanatakiwa wakae na watoto na kujadili kila sifa pambanuzi ifuatayo na kupendekeza njia moja ya kivitendo ili kuifundisha kwa kila mtoto.

Watoto wana ...

Maajabu, wasifie
Waaminifu, waamini
Nguvu, waelekeze
Wema, furahi nao
Furaha, waunge mkono
Moyo wa huruma, jifunze kwao
Mapenzi, watunze
Wema, watunze
Akili iliyo wazi, wafunze
Thamani, wathamini
Maswali, washajiishe
Vitendea kazi, wape nguvu
Hiari, faidika nao
Vipaji, wakuze
Upekee, watamkie kwa dhati
Shauku, weka maanani
Ucheshi, cheka nao

(MEIJI, 1999)

ZOEZI 10: KUJADILI SABABU HALISI ZA UKATILI KWA WATOTO

Jadiliana na watoto wako baadhi ya matukio ya kuogofya kutokana na uzoefu wao. Marekani, mauaji ya kinyama na ya kushtua yaliyotokea katika Shule ya sekondari ya Columbine . Watoto wawili wa kiume, wenye umri wa miaka 18 na 17, waliua watu 15 na kujeruhi 26 kwa kutumia bunduki na milipuko. Kurusha kitu cha hatari huku ukiwa unacheka kama vile wafanyavyo kwenye runinga, michezo ya kuigiza, na michezo ya video, baadaye hujipiga kweli na kujiua .Wameshafanya milipuko 19 majumbani mwao. Matukio kama haya hayakuwa nadra: Matukio kama haya yapatayo 22 Marekani yalitokea katika mwezi uliofuatia. Kwa nini wanafanya hivyo? Nani anahusika? Imekingwa vipi? Nini kifanyike kuzuia matukio kama haya yasitokee tena huko baadaye? Ni mafunzo gani tunaweza kujifunza? Kwa namna gani tunazuia sababu halisi za ukatili huu?

ZOEZI 11: KUSHUGHULIKA NA MATATIZO YA KIJAMII

Jadili pamoja na familia yako juu ya sababu na athari za kuvuta sigara, kutumia dawa za kulevya, mimba zisizo za halali, vilevi, kujiua na talaka. Shauri njia stahiki za kufanya katika kukuza jamii pamoja na familia yako.

KAZI 12: MTINDO WA MALEZI MAREKANI KWA MUJIBU WA DKT. SPOCK (1903-1998): Mafunzo kutoka “fanya kama nisemavyo, siyo kama nitendavyo”

Kaeni pamoja mjadili kwa uzoefu wako katika kulea kupitia mwongozo wa historia ya maisha ya Dkt. Spock kama ilivyodokezwa kwenye makala (Maier, Newsweek-1998) amesema kama ifuatavyo:

Kujua hadhi halisi ya mtoto anayelelewa nchini Marekani kutakuwa hakukamiliki bila ya kuangalia athari ya ushawishi wa Dkt. Benjamini Spock katika malezi ya kisasa. Dkt. Spock, ambaye ni mwanasaikolojia bingwa wa magonjwa ya watoto, alilelewa na mama yake kwa mapenzi, adabu na matarajio makubwa. Baada ya miaka 51 ya maisha ya ndoa, Dtk. Spock, alimtaliki mkewe aliyekuwa mlevi kupindukia. Dtk. Spock, alianza kufanyia utafiti magonjwa ya watoto na kugundua kuwa matatizo mengi ya watoto yalitokana zaidi na ubovu wa tabia kuliko uduni wa afya. Tabia ya kughadhibika, kunyonya dole gumba, kugoma kula, kukataa kulala pamoja na kutotaka kuketi kwenye choo cha kitoto kujisaidia, ni natija ya malezi. Katika usomaji wake, Dkt Spock alivutwa sana na mtazamo wa mwanasaikojia Freud (Sigmund) na akakubali kufanyiwa mara-mbili, uchunguzi wa tiba za kisaikolojia.

Aliwashauri wazazi wasiwakalifishe watoto, bali waoneshe kuwajali na kuwaelekeza vyema. Akiwaambia, “Jiamini. Unajua mengi kuliko unavyo dhani”. Alifundisha kuwa watoto wanahitaji zaidi mapenzi kutoka kwa baba na mama zao. Lakini yeye aliwasikiliza zaidi kwa makini wateja wake kuliko alivyokuwa akiwasikiliza wanawe. Alipoulizwa na mama mmoja kama, “mtoto mdogo anaweza kuwaona wazazi wake wakiwa uchi”, akajibu, “ ni vigumu kutoa jibu rahisi kwa suala hilo”.

Familia ya Dtk. Spock ilitetereka, na haikuweza kuwa kigezo chema. “Daima ni vigumu kufanya jambo bora kwa watoto wako, kama ilivyo rahisi kuandika kuhusu jambo hilo”. Mkewe alikuwa mlevi sugu mpaka akalazwa hospitalini kwa sababu ya ukichaa. Yeye baba wa familia hakuwa mchangamfu kabisa kwa wanawe hata wakahisi kuwa baba yao kawatelekeza.

Dtk. Spock alikiri udhaifu alionao wa kutumia muda mwingi kwenye kazi yake na kusababisha wanafamilia kuanza kukumbatiana wenyewe kufidia waliyo yakosa. “Sijawahi katu, kumbusu yeyote kati ya wanangu wawili wa kiume wakati wakiwa wadogo”, alithibitisha.

Dtk. Spock aliwafunza wanawe kuwaita wazazi kwa majina yao halisi ya awali – ilikuwa hatua kubwa iliyoashiria kupambazuka kwa vigezo vya wakati huo. Baba alitaka na kutamani malezi ya watoto wake kuakisi falsafa ya maisha aliyonayo.

Kujifanya kuwa baba ni sawa na mwanawe ni jambo ambalo kiuhalisia si la kweli. Lilikuwa ni jambo la fakhari kwake kutambulisha ulimwengu wote kwamba, “Huyu ni mwanangu, yeye huniita kwa jina langu la kwanza.” Hata alipokuwa akisemezana na wanawe ilikuwa kama mtihani wa majibizano. Palikuwa na mfanano mdogo sana baina ya ile sauti tulivu inayojitokeza kwenye uandishi wa vitabu vyake na ile sauti kali ya kulaumu aliyokuwa akiitumia nyumbani. Hakuweza kutanabahi athari ya sauti yake kama baba.

Yeye alisisitiza wanawe wasifedheheshe au kuvunja heshima ya utajo wa familia kwa jamii. Kusifiwa na au kukosolewa na watu wa nje ilikuwa ni muhimu sana kwake yeye kama mzazi. Alithamini sana fikra za watu wa kando na mitizamo ya vyombo vya habari. Vijana wake walivalia kiunadhifu na walitakiwa kuwa wenye kauli nzuri na majirani wema. Kama tabasamu la John lilififia au kukosa bashasha, Ben kwa haraka alimchangamsha. " Punguza hasira, jaribu kidogo kuwa mwenye kupendeza kwa watu," alisisitiza.

Dtk. Spock, kimsingi aliyakana matatizo yake ya nyumbani. Vijana wake walijifunza heshima ya kuogopana baina yao. Mgogoro wowote wa Mike na John dhidi ya baba yao ulibaki kuwa jambo la binafsi. Walijizubaisha sana walipotakiwa na majarida ya habari na televisheni kuketi na baba yao kwa ajili ya picha ya pamoja, na kutoa majibu ya mkato yasiyo wazi walipoulizwa kuhusu tabia ya baba yao wakati awapo nyumbani.

Kwa hakika hakuweza kuonesha mapenzi na hisia za upendo kwa wanawe, ambao walikiri hadharani kwamba, "Hatujawahi kumbusu baba yetu." Kimalezi, Dkt. Spock alikuwa alama zaidi kuliko kuwa mtu, alikuwa mtawala zaidi kuliko baba aliye mfano wa kuigwa, na alikuwa ni baba mwenye masharti asiyejali kukidhi mahitaji ya kihisia ya wanawe.

Bwana Spock alilalamikia namna alivyo lelewa, kwamba, "Sikuwahi kuona mvuto wa vitendo (mvuto wa bayana kati ya baba na mwana). Baba yangu alinipenda, na alifanya mambo kadhaa kunikirimu, lakini kwa vitendo najaribu kuvuta kumbukumbu kama alishawahi kunibusu mimi au watoto wengine katika tukio lolote lile, ukweli sikumbuki mimi kubusiwa hata na ndugu zangu."

Mafunzo: Usifuate kibubusa nadharia za wataalamu. Elimu hizo, kimsingi, hubadilika na kuendelea kukua, na tusipoegemeza ugunduzi wa mwanadamu kwenye mwongozo wa Muumba tutapotoka na kupotea, na kuzusha madhara mengi zaidi kuliko manufaa.

ZOEZI 13: MJADALA KUHUSU KUTETEREKA KWA UTAMADUNI

Wazazi wajadili na watoto juu ya uzoefu wao kuhusu kutetereka kwa utamaduni. Kisha amuite kila mtoto aelezee alivyotembelea nchi zingine au tamaduni za wanafunzi wenzake kutoka katika jamii, dini, na makabila mengine.

Ikiwa mtoto hakuwahi kuwatembelea ndugu na jamaa waishio nje ya nchi au nje ya mkoa, inashauriwa sana zitengwe, fedha, ipatikane ruhusa (vibali), ili kutafiti na kupanga mambo ya mbele kuhusu likizo /matembezi ya kifamilia kwa ajili ya kuwatembelea ndugu na jamaa zao mara kwa mara kama inawezekana.

ZOEZI 14: UELEWA WA VIONGOZI WAZURI

Jadili nukuu zifuatazo wewe na familia yako:

"Nimegundua kuwa viongozi wazuri hasa ni mara chache kuwa mashujaa wa ofisi za Umma.Wote kwa pamoja wanaume na wanawake hawana maelezo mengi

kuhusiana na sababu za kuwa mabingwa. Husogea taratibu, kwa uangalifu, na hatua kwa hatua. Hufanya kilicho sahihi" (Badaracco, 2002).

"Viongozi wanaweza kutaka kuendeleza akili za wafuasi wao, lakini wasije wakashindwa kufanya hivyo kwao wenyewe" (Steven B. mfano kutoka katika Mwongozo wa Mkataba wa Uongozi).

Hitimisho: Kufanya jambo sahihi ndicho kinachoangaliwa, sio kipi ni maarufu na mtindo mpya. Jadili nani anaweza kueleza kipi ni sahihi na kwa vipi! Ni wewe, mimi, yeye, au Mungu Muumba?!

ZOEZI 15: KUBADILISHANA MAWAZO YA HISTORIA YA FAMILIA

Kaa chini na watoto wako na kubadilishana nao mawazo kuhusu mnachokijua juu ya wazee wao. Familia nyingi za sasa hazipeani habari za familia zao na watoto wao. Watoto wanahitaji kujua kuhusu maisha, mafanikio, kushindwa, kazi, uzoefu, shughuli na faida juu ya mababu zao na mabibi zao. Nina Abdulla, mtaalamu wa kulea anafundisha wateja wake vipi utachora mti wa familia. Ni Mchoro unaoonesha ndoa, talaka na mahusiano baina ya familia, kama vile shangazi, mjomba, binamu, na babu wa pande zote kwa mama na baba wa familia. Mtume (s.a.w) amewasisitiza Waarabu juu ya mila za makabila kwa kuwatolea habari kuhusu mzee mmoja na kuikariri familia moja kama ni kigezo (Campo 2009). Baadhi ya Wasomalia wanafahamu koo zao za mababu zao na wamekutana katika kabila kubwa kwa pamoja kubadilishana kitu walichokielewa kutoka kwa babu zao.

3

SURA YA TATU

- **MALEZI BORA**

Kuweka malengo sahihi

SURA YA TATU **86**

Malezi bora: Kuweka malengo sahihi **86**

Hatua ya Kwanza katika Kutekeleza Malezi Sahihi 88
Uchambuzi wa kina kuhusu Malengo 90
Kahawa na vipaumbele vya Familia 95
Hitimisho 96
Kazi za kufanya

Tunadhamiria kuandaa vijana wazuri na walio imara,
Ambao watajenga familia nzuri na imara,
Ambao watajenga jamii nzuri na iliyo imara
Ambao watajenga taifa zuri na lililo imara,
Ambao watajenga dunia yenye Amani.

Kuweka malengo sahihi: Hatua ya Kwanza katika Kutekeleza Ulezi Sahihi

Wazazi wajaribu kulea kwa kutumia akili. Japokuwa wazazi wengi huweka mipango katika masuala yao ya kitaaluma na likizo zao za kila mwaka kwa uangalifu wa hali ya juu, wanashindwa kukaa na kuandaa mipango yao kwa pamoja kama kitengo kimoja cha familia. Kiukweli, wengi watashindwa hata kuafiki dhamira yoyote sahihi, azma, matarajio, au mbinu kwa ajili ya familia zao. Bila kuwako malengo ni dhahiri kutakuwa na mafanikio duni.Wanalipuka kutoka kazini, kwenda nyumbani, dukani, shuleni, likizo na kuepa janga hadi janga wakitegemea mambo kuwaendea sawia, si lolote ila ni sawa na mchezo wa pata potea tunaochezea mustakbali wa maisha ya watoto wetu, tukiruhusu muda wenye thamani kuponyoka bila taarifa. Tunahitajika kuweka malengo ya muda mrefu na mbinu ya kuyafikia.

Mtazamo sahihi wa malezi ni ule unaomtazama mtu binafsi na jamii kama mfumo mmoja ulioshikamana. Hatuwezi kujenga jamii imara pasina kuweko watu jasiri na wema. Watu wa namna hii hawatengenezwi katika uwanda uliofungwa, kwa kuwa wanahitaji mazingira ya jamii iliyoshikamana na yenye ushirikiano. Nia ya wazazi iwe ya kuzalisha binadamu ambao ni makhalifa/wajumbe wa Mwenyezi Mungu, ambao ni majasiri na waaminifu, ni raia waliostaarabika, na ambao dhamira yao katika maisha ni maendeleo na mabadiliko ulimwenguni. Bila ya kuwa na ujumbe huu, uwepo wa binadamu hauna lengo wala thamani. Maslahi ya mtu yanapaswa kujumuisha maisha haya na yajayo, ya muda mfupi na ya milele,ya binafsi na ya kijamii. Hili linatakiwa liwe ndio dhamira kuu na mtazamo wa ulimwengu juu ya wazazi katika kulea watoto.

Jedwali la Malengo ya Ulezi: Malengo, Maadili, Njia

Pendekezo la mwanzo: Familia yenye furaha	**Pendekezo la pili: Kulea viongozi wa Wacha Mungu (watu wema)**			
	Siha: Afya na Nguvu	Tabia njema	Maarifa,Busara & imani	Ujuzi: Utaalamu
Mawasiliano Kupongeza/Kukosoa Misimamo Hisia (kujali/kupuuza) Kuhimili/Kuhamaki gusa, busu, kumbatia furaha, utani Uelewano Muda wa familia Mambo m-badala wa kutazama TV Vikao vya familia Mlo wa familia kudhibiti msongo wa mawazo Michezo, Burudani Kushiriki na watoto katika mambo	Kuchagua Mchumba Makuzi ya Mtoto Unyonyeshaji Muujiza wa ubongo Afya Lishe Mazoezi Ulalaji (kulala) Usalama wa jimai Kuepuka Ulevi	Ujasiri/ kuthubutu upendo/ mapenzi Uaminifu Fikra huru Uwajibikaji Kujitegemea Ubunifu Kujiamini Kuaminiana Heshima Uvumilivu Upole/Utiifu	Elimu/Kisomo Kuboresha mazoezi ya masomo nyumbani Kuhamasisha, kuwezesha watoto kufanya Nidhamu na Uadabishaji Imani Utambulisho familia kubwa	Usomaji Uandishi Kompyuta Udereva Kushughulika Kutunza wakati na pesa Kutoa sadaka Kuomba dua Kufanya Uamuzi

Sasa tuanze kwa kuchunguza jedwali hilo hapo juu. Tunaliita ni jedwali la malezi mazuri. Hili linahitimisha malengo tunayotakiwa kuyaweka na linatuongoza jinsi ya kuyafikia kwa kuzitumia kanuni na tamaduni kutoka utoto hadi utu uzima.

Malengo yenyewe kwa ujumla yamechukuliwa kutoka katika (a) Matarajio ya kina ya wazazi yaliyojumuishwa vizuri katika Qur'an 25:74, na (b) Hadithi sahihi ya Mtume Muhammad (S.A.W):

> "Na wale wanao sema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na wanetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe waongozi kwa wachamungu.
>
> (Qur'an 25:74)"

> *Binadamu ni kama madini [au shaba yaani wana tabia zao]; waliokuwa bora zaidi [kabla-ya Uislamu] enzi za Ujinga (jahiliyyah) ndio bora zaidi katika Uislamu kama wataelewa [na kufahamu]. (ALBUKHARI NA MUSLIM)*

Kama ilivyoainishwa katika jedwali, malengo yamegawanywa katika pande mbili kubwa, pande ya pili ikigawanywa zaidi katika vijipande vinne. Wazazi wanahitaji kulizingatia jedwali hili na kujizoesha malengo yake na tamaduni, kuyasoma na kuyakumbuka pamoja na kuandaa mipango ya maendeleo dhidi yake.Hii itahakikisha kuwa hazipuuzwi na kuacha majukumu ya kila siku ya maisha kuchukua nafasi ya kazi za ulezi.

Uchambuzi wa kina kuhusu Malengo

1. MALENGO KUTOKA KATIKA QURAN: SWALA YA WAUMINI

Dua ya kwanza ambayo waumini wanatakiwa kuiomba ni kwanza Mola awajalie kutoka kwa wake zao na watoto wao qurrata a'yun (yafurahishayo macho). Aya hii imerudiwa mara sita katika Qur'ani tukufu na maana yake halisi ni: "Faraja ya macho yetu,furaha kwa macho yetu, na macho ambayo yamefurahishwa na raha za kuvutia" kwa hivyo kiuhalisia hitaji la kwanza lahusu kuwa na nyumba na familia yenye furaha.

Hii haimaanishi familia ndogo pekee bali hata ile iliyopanuka zaidi inayojumuisha mke/mme, watoto, wazee, wajomba, shangazi, na binamu. Mambo muhimu yanayohitajika kwa ajili ya furaha ya familia inajumuisha mawasiliano kati ya wazazi na watoto; kuonyesha mapenzi na upendo, kuwasifia na kukosolewa kwa njia yenye kujenga, sharti la ziada kwa familia yenye furaha inajumuisha kujenga tabia njema, kuhimili hisia katika namna maalumu ya kujali; kutabasamu, kubusu, kukumbatia, kugusa na kupeana mikono na watoto, kula na kufanya kazi pamoja, kutaniana na kukaribishana.

Dua ya pili waombayo waumini kwa mola wao ni kwa wenza wao na watoto wao kuwa "Imam kwa wamchao Mungu". Neno imam na wingi wake a'immah limerudiwa mara tano katika Qur'an. Tafsiri mbalimbali zinaeleza maana ya kundi hili la maneno "Imam wa wamchao Mungu" kama ifuatavyo: Tufanye tuwe

mfano kwa wengine, kiigizo kwa wengine, walinganiaji katika kheri, Mwongozo kwa wengine, viongozi wa waanadamu, wa mwanzo kabisa katika wanaomtambua Mola wao,kiigizo kwa wengine, waanzilishi wa mambo ya kheri kwa wengine, na tuwe wa kupigiwa mfano wa kuigwa kwa tunaowaongoza. Kwa maana hiyo dhima kuu ya familia inalenga kulea viongozi wachamungu na waliobora/ wafanisi na mwangaza kwa wanadamu.

Katika kulitekeleza hili tunapenda kueleza kuwa tunaposema uongozi, hatumanishi uchu wa kusaka madaraka bali ni kukuza watu jasiri,wenye uadilifu, tabia njema, ari na kila sifa zinazostahiki kwa uongozi bora. Kwa maelezo zaidi neno "kiongozi" linaweza kuwa na tafsiri hasi kumaanisha kuwa si jambo zuri kwa kila mtu kupigania nafasi hii moja. Ukweli uliozoeleka kuwa anatakiwa awepo kiongozi mmoja rasmi wa kundi lolote kunazua ushindani usio na tija, na kutengeneza hisia za tamaa isiyotakiwa. Ikiwa kila mmoja akawa na tamaa ya nafasi hii moja nani sasa atakayekuwa ni mfanyakazi au mfuasi? Lengo letu ni kuwafanya wanetu kuwa na hulka zinazomuainisha mtu mwenye misingi ya uongozi.Mwana jamii yeyote anayeshiriki na kutengeneza hali hii ndiye Kiongozi hasa na hivi ndivyo maendeleo yanavyofikiwa.

Wako wapi viongozi? Nyie ndio viongozi.

Sisi ndio viongozi tunaosubiriwa

- **Uongozi si suala la kuwa mtu muhimu, bali ni kutumikia jambo muhimu**
- **Si kwamba umeshika nafasi fulani, bali jinsi gani unaongoza vizuri**
- **Uongozi ni kutenda jambo sahihi ukijua Mungu pekee anakuona**
- **Kila mmoja ni kiongozi kwa mtu Fulani. Mtu huyo awe ni mwajiriwa, mke/mme, mtoto, au binafsi; Wewe ni kiongozi**

Kwa kusisitiza sifa za uongozi hazimaanishi kuwa na uroho wa madaraka, hadhi, nafasi au pesa. Haziimanishi pia mafunzo ya jinsi ya kutawala na kudhibiti. Ni kinyume kabisa. Linalopendekezwa ni kuwa watoto walelewe kwa maana ya ukarimu, uvumilivu, na lengo pana, waweze kujitazama kama wanajamii wenye thamani.Watu wanaoweza kuishi kwa urahisi katika dunia iliyojaa mawazo ya mikinzano na ambao wana uwezo wa kujiwekea malengo ya juu, na hawaathiriwi na kutojiamini. Watoto ambao hawataogopa kutokubaliwa na jamii kwa imani yao au rangi yao hawawezi kuitumikia jamii. Ikizingatiwa jamii tunayoishi, sifa hizi zinatakiwa zipewe kipaumbele.Ikiwa mtu hatafundisha watoto wake kujiamini na kuongoza vizuri wanaweza kupotoshwa kiurahisi.

Katika Urithi wa Waislamu, Neno "Kiongozi", (Qa'id) halikutumika bali lilitafsirika kwa maneno yafuatayo.

Mchungaji, mlinzi *Ra'i.*

Mkufunzi au Muelimishaji, *Murabbi*

Mtu wa kwanza kabisa, Mfano *Imam*

Muadabishaji, Mtengeneza tabia *Mua'ddib,*

Mwalimu *Mua'llim,*

Mshauri, Muongozi *Murshid,*

Kocha *Mudarrib*

Kiongozi ni mtu anaeongoza wengine na kazi zao katika kufikia malengo fulani' wakati Murabbi (mkufunzi - muelimishaji) ni yule anaewaandaa na kuhakikisha watu wanatimiza malengo. Mtume (S.A.W) kwa mfano alimchagua 'Amru ibn al-'As na Ubaydah ibn al-Jarrah kuongoza majeshi, ambapo akamtuma Mus'ab ibn 'Umayr kwenda Madinah na Mua'dh ibn Jabal kwenda Yemen wakiwa kama "wachungaji, wakufunzi, na washauri" kukuza na kulea watu wema na walioelimika.

Haikutokea kwa bahati tu kuwa mitume wengi walikuwa ni wachunga kondoo, akiwamo Shu'ayb, Mussa, 'Issa, na Muhammad,amani iwe juu yao wote kwa pamoja. Kazi yenyewe ya uchungaji ina maana ya wema, kujali, na huruma kwa wafuasi.Vilevile inamaanisha kuwa na unyenyekevu. Hizi ndizo sifa kuu na muhimu zihitajikazo katika kulea watoto; ni mfano mzuri ulioje kuona wazazi kama wachungaji wakihudumia mifugo yao. Kwa maana hiyo kiongozi ni mchungaji, mshauri, kocha, na mwalimu.

Kiongozi au Mchungaji?!

Neno "Kiongozi" *(qa'id)* linatumika katika tamaduni mbalimbali,lakini halijatumika katika Qur'an wala katika Hadith, ila neno "Mchungaji" limetumika katika Hadithi ifuatayo:

Wote nyinyi ni wachungaji na mtawajibika kwa vile mnavyovichunga. Imam (yaani, kiongozi) ni kiongozi wa watu wake na ataulizwa juu yao, na mwanaume ni mchunga kwa familia yake nae atawajibika juu yao, mwanamke ni mchunga juu ya nyumba ya mumewe nae ataulizwa juu yake, Mjakazi ni mchunga wa mali ya bwana wake nae atawajibika juu yake, Mwanaume ni mchungaji wa mali ya baba yake nae ataulizwa juu yake nyote ni wachunga na mtaulizwa juu ya mlivyovichunga.

(ALBUKHARI)

2.MALENGO YALIYOTOLEWA KATIKA HADITH ZA Mtume (S.A.W)

Mtume Muhammad (S.A.W) Anasema:

Watu ni kama madini [au shaba, kwamba wana sifa tofauti]; waliokuwa wabora zama za ujinga (jahiliyya) watakuwa bora zama za Uislamu, kama watafahamu [na kuzingatia].

(Al-Bukhari Na Muslim)

Mambo mengi tunaweza kujifunza katika hadithi hii. Funzo moja likiwa tabia kujengwa utotoni. Jambo hili ni maalumu kwa wanadamu wote, Waislamu na wasio Waislamu (kama ilivyoeleza hadith). Ujasiri, ubunifu, uadilifu, upendo, na uaminifu zimekuwa ni sifa za watu wazima kabla hata ya kuja Uislamu.Watu bora zaidi walikuwa ni wale waliokuwa na sifa hizi.Uislamu unaongezea imani, hekima, maarifa na mwongozo wa Mwenyezi Mungu. Mtume anatueleza kuwa majahili waliokuwa bora zaidi wanaweza kuwa ni Waislamu wenye sifa bora zaidi, ikiwa watauelewa Uislamu.

Mshirikina bora ⟶ Anaelewa na kuzingatia Uislamu ⟶ Muislamu bora

Baadhi ya Waislamu hudhani ya kuwa ujasiri, ukweli na uaminifu wa Waislamu wakubwa (kama Umar ibn al Khattab na Khalid ibn al Waleed) umekuja baada ya kuukubali Uislamu. Ukweli ni kwamba walikuwa jasiri, wakweli na waaminifu kabla ya kuingia katika Uislamu. Uislamu uliongezea katika sifa zao adhimu walizokuwa nazo na hekima, maarifa na mwongozo wa Mwenyezi Mungu.

Hadithi hii inazingatia sifa za tabia. Kuna hali muhimu anazopaswa kuwa nazo Muislamu kama mwili imara na siha njema (hasa wakati wa ujauzito na kunyonyesha). Pombe, uraibu, sigara na uzinzi ni machafu yanayo muathiri mama mjamzito na mtoto ambaye bado hajazaliwa. Kina mama wajawazito wanatakiwa kuepuka kutumia dawa pasi na ushauri wa daktari pia wanahitaji lishe bora na kupumzika (usingizi wa kutosha). Uangalifu na kujilinda dhidi ya maambukizi ya virusi na bakteria unahitajika.

Aina ya sifa za kitabia tutakazo kuzizalisha ni ujasiri, ukweli, ubunifu, uadilifu, upendo, uaminifu na wajibu. Sifa hizi zina nafasi finyu ya kuzalishwa. Hivyo miaka mitano ya mwanzoni ni muhimu. Zaidi wazazi wanatakiwa wawezeshe watoto kuwa na stadi za kusoma, kuandika, kuzungumza, udereva, uogeleaji na kutumia kompyuta. Wanalazimika kuwafunza watoto subira, heshima na utoaji maamuzi. Mtoto akiwa na stadi hizi mapema zitakuwa na tija na kufungua milango ya mafanikio kwa watoto.

Mtume Muhammad (S.A.W) alielezwa na maadui zake kama mkweli na mwaminifu. Hii ilikuwa sifa yake kuu kabla ya kupewa wahyi. Qur'an inatilia mkazo mambo yaliyoelezwa katika Hadithi iliyotajwa (tabia njema) wakati ikiwaelezea Manabii kama Nuh, Yunus, Ibrahimu, Ismail, Mussa, Talut, Issa, Yusuf, Ayyub na Yaaqub (Amani iwe juu yao wote). Mussa anaelezwa kama "jasiri na muaminifu". Nabii Yusuf anajieleza kama ni "mjuzi, mtaalamu na mwaminifu". Sifa hizi ni muhimu katika uongozi: Nguvu

(ya mwili na tabia), utaalamu (ukihitaji maarifa na ujuzi) na uaminifu. Kwa ujumla manabii 25 wanaoelezwa katika Qur'an ni wakweli, wana hekima, wataalamu, rahimu, wana huruma, ujasiri, waaminifu, wana subira na wenye kutimiza ahadi. Sifa hizi ndizo tunazotakiwa kuzisisitiza tunapolea watoto wetu. Zingatia aya zifuatazo za Qur'an takatifu:

> "Na mtaje katika Kitabu Ismail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii.
>
> (Qur'an:19:54)

> "Yusufu akasema: Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi."
>
> (Qur'an:12:55)

> "Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema.
>
> (Qur'an: 28:14)

> "Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu."
>
> (Qur'an: 28:26)

> "Na Nabii wao akawaambia: Mwenyezi Mungu amekuteulieni Taluti (Sauli) kuwa ni mfalme. Wakasema: vipi atakuwa na ufalme juu yetu, na hali sisi tuna haki zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Mwenyezi Mungu amemteua yeye juu yenu na amemzidishia ukunjufu wa ilimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa na Mjuzi.
>
> (Qur'an: 2:247)

> "Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.
>
> (Qur'an: 9:128)".

Kahawa na vipaumbele vya Familia

Mzazi mmoja alichukua mtungi usio na kitu na kujaza vipira vya gofu. Akauliza wanawe kama mtungi umejaa, wakakubali kuwa umejaa. Kisha akachukia sanduku la kokoto akamimina na kutikisa taratibu, kokoto zikaingia katika nafasi zilizoachwa wazi na vipira, akauliza tena iwapo mtungi umejaa, wakakubali kuwa umejaa.Mzee akachukua tena sanduku la mchanga na kumimina katika mtungi ukajaza nafasi iliyo wazi. Akauliza iwapo mtungi umejaa ,watoto wakajibu "Ndiyo".Kisha mzazi akatengeneza vikombe viwili vya kahawa kutoka chini ya meza na kumimina mchanganyiko katika mtungi na kujaza nafasi iliyoachwa wazi na mchanga. Watoto wakacheka. "Sasa" mzee akasema "Nataka mchukulie mtungi huu kuwa ni maisha yenu. Vipira vya gofu ni vitu muhimu- ibada, wenza wenu na watoto wenu, afya, rafiki na shauku zenu-vitu ambavyo vingetimiza maisha yenu iwapo vitu vingine vyote vitapotea, vikokoto ni vitu vingine mnavyojali kama kazi zenu, nyumba na gari zenu. Mchanga ni vitu vingine vyote kama michezo na kadhalika.

Ikiwa utatanguliza mchanga katika mtungi hakutabaki nafasi ya vipira vya gofu wala vikokoto. Vivyo hivyo katika maisha yenu. Kama utatumia muda wako wote na nguvu zako katika mambo ya michezo na kadhalika, hutakuwa na nafasi ya mambo muhimu. Zingatia mambo ambayo yatakuletea mafanikio baada ya maisha ya duniani na furaha yako katika hii dunia. Swali sana, Toa zaidi sadaka,Tumia muda na watoto wako. Angalia afya yako. Toka kwa ajili ya chakula cha usiku na mke/

Zingatia mambo ambayo yatakuletea mafanikio baada ya maisha ya duniani na furaha yako katika hii dunia

mume wako.Tumia muda kujisomea. Daima utakuwa na muda wa kusafisha nyumba yako na kurekebisha sinki la taka.

Kuwa makini na vipira vya gofu kwanza, vitu vya muhimu hasa. Weka vipaumbele vyako. Vinavyobaki ni mchanga tu."

Mtoto mmoja akauliza kahawa iliwakilisha nini. Mzazi akatabasamu "Nashukuru umeuliza.Inamaanisha kuwa hata ikiwa maisha yako yametimia kiasi gani bado unaweza kuwa na nafasi ya vikombe vya kahawa na rafiki".

Hitimisho

Tuliza macho yako kwenye zawadi.

Japokuwa sehemu hii imejadili suala la malengo na dhima/dhamira kwa kina fulani, kama yote yaliyozungumzwa yatatendwa, uwekaji malengo ni chanzo cha kufikia mahitaji, na ndiyo zao la mwisho,suala la uleaji watoto wema linatakiwa kuzingatiwa, litakuwa na athari ya moja kwa moja na jinsi mtu anavyowalea watoto wake na jinsi atakavyowaingizia sifa ambazo mzazi anatamani wawe nazo watakapokuwa watu wazima.

Katika kufikia malengo tunayoweka kwa ajili ya watoto wetu hatuna budi kutazama mienendo na tabia zetu. Tunahitaji:

1. **Kuwa na uwiano katika kuadabisha, kuhamasisha na kuwezesha**
2. **Kufanyia kazi tunayoyahubiri kadiri tunavyoweza na kuyafanya ndio mtazamo wetu wa dunia kwa ujumla na ndio utambulisho na yanatuhusu.Kubali makosa yako na kuomba msamaha kwa makosa hayo bila kujenga hoja.**
3. **Kuchanganya na hayo ni kuwa na imani na kuswali. Mwenyezi Mungu huwajibu watu wakweli katika matendo yao na kuwasaidia kwa Namna yake na Wakati wake.**

Biblia inasema:

> Mfundishe mtoto njia impasayo kuiendea, naye hataiacha hata akiwa mzee (mithali 22:6)

Hatima ya dunia hii na uwepo wake inategemea zaidi vizazi vijavyo. Ulezi unachukua nafasi kubwa katika kuvirekebisha vizazi vinavyokuja na matokeo yake si ya kupuuzwa. Ubinaadamu wenyewe bado unakumbana na hatari pamoja na changamoto na tunahitajika kuwa makini na kazi yetu ya kuwa na stadi za ulezi bora na kuzifanyia kazi. Watoto wetu watakuwa wazazi wajao, ambao watafundisha tabia hizo hizo kwa watoto wao, hivyo kuanzisha mzunguko ambao utaleta amani, haki na ustawi kwa dunia. Uhai haupimwi kwa idadi ya pumzi tunazopumua bali kwa amali zinazomaliza pumzi zetu!

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI 16: MJADALA WA MAZINGIRA YA NYUMBANI

Uliza kila mwanafamilia kujibu maswali haya:

- Unajisikia furaha unapoingia nyumbani?
- Unajisikia furaha unapoondoka nyumbani?
- Utafanya nini kuyafanya mazingira ya nyumbani kwako yawe ya raha?
- Ainisha jambo moja unalotaka kulipata kwa kila mwanafamilia katika kuleta furaha nyumbani.

ZOEZI 17: WAZAZI FUNZENI WATOTO WENU

Tazama mambo yafuatayo na jadili jinsi utakavyoweza kuwafundisha watoto wako, zingatia mambo yasiyo kuwepo wakati wa mafunzo ya watoto

- Namna gani ya kupanda mti wa maua waupendao; (watoto wako wanapenda kuchezea tope, kuchimba,na kuchezea mabomba ya maji)
- Wasichafue
- Jinsi ya kukupigia simu ukiwa kazini
- Jinsi ya kupiga 112 (au namba ya dharura ya taifa) na wakati gani na kwa nini
- Kurudisha walichoazima
- Kuwasifu wengine
- Kutowaumiza wengine
- Kutowaogopa wanyama bali kuwaheshimu na kuwathamini
- Kuyafanya maneno yao ni dhamana
- Kusafisha uchafu wao
- Kugawa na kujali. Furaha ya pamoja ni furaha maradufu na huzuni ya pamoja ni huzuni pungufu

- Kuheshimu mamlaka na sio kuiogopa
- Kufanya urafiki na watoto wa rangi na taifa lolote hata wale wasioweza kuzungumza hata neno moja la Kiswahili
- Wasiogope kujaribu vitu vipya visivyo na madhara
- Jinsi ya kuishi watakapo shindwa
- Jinsi ya kushinda
- Hata kama si hodari kutenda jambo fulani wanaweza kulifurahia
- Watakapokumbwa na tatizo zito wajitahidi na kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu.
- Wasubiri punguzo la bei kabla ya kununua kitu
- Jinsi ya kufua na kukunja nguo zao
- Jinsi ya kuheshimu vitabu
- Wajali muda na kutoa taarifa iwapo watachelewa, mara kwa mara
- Kugawa/ kuwapa wengine
- Jinsi ya kuwa nadhifu na muonekano mzuri

WAZAZI:

- Usimwambie mtoto wako “Acha kulia”;muulize kwanini analia?
- Usimnunulie mtoto wako kila akitakacho hata kama unao uwezo
- Usikashifu makosa ya mtoto wako bali jadili kwa nini wameshindwa
- Usimkashifu mke/ mume wako mbele ya mtoto wako
- Usiweke runinga wala kompyuta chumbani kwa mtoto wako
- Usitumie runinga kama mlezi wa mtoto wako

ZOEZI 18: MAKOSA KATIKA METHALI ZA TAMADUNI ZA WAARABU

Wazazi wanatakiwa wazieleze na kuzikanusha baadhi ya methali ambazo ni mashuhuri katika tamaduni za Waarabu. Methali hizi zinalenga kuchochea dhana za ubinafsi, kutojali na unafiki

- Kama wewe si mbwa mwitu, utaliwa na mbwa mwitu [inahamasisha ubabe]
- Ubusu mkono usioweza kung’atwa [inaonesha unafiki]
- Kwanini nijali! [ubinafsi, uchoyo]
- Nikifa kwa kiu, mvua isinyeshe kamwe [kutojali]
- Jihadhari na ubaya wa watu uliowasaidia [dhana mbaya]

ZOEZI 19: MTAZAMO WA DUNIA KUHUSU URAFIKI

Elezea hadithi hii kisha hadithia hadithi kuhusu urafiki wako ambao haukuwa sawa, si adili na si kwa ajili ya Allah pekee, Mtume(S.A.W) amesema:

"Kuna kundi la waja wa Allah ambao hata Mitume na mashahidi watawahusudu". Wakasema "Ewe Mtume wa Allah, ni watu gani hawa?" Akasema "Ni wale watu wanaopendana kwa ajili ya Allah, si kwa utajiri au undugu wao. Nyuso zina nuru na wapo katika mimbari za nuru; hawaogopi pindi wanapoogopa watu na hawahuzuniki wanapohuzunika watu". Kisha Mtume (S.A.W) Akasema maneno yafuatayo". Kwa hakika walio karibu na Mungu-hawataogopa wala hawatahuzunika"(Abu Dawud)

ZOEZI 20: MAJADILIANO TULIVU YA WANAFAMILIA: AGHALABU

- Kuwa na mkutano wa mara moja kwa mwezi wa wanafamilia kujadili hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi za kila mmoja wenu katika familia.
- Hakikisha hakuna ugomvi wala mzozo unaozuka pengine mjadala unapopamba moto.

SURA YA NNE



- **LENGO LENYE MAANA ZAIDI**
  Kulea Watoto wanaompenda Mungu

SURA YA NNE **100**

Lengo lenye Maana zaidi: Kulea Watoto wanaompenda Mungu **100**

Utangulizi 102
Mbinu za Kisasa za Kuwafunda Imani Watoto Wetu 103
Kukosekana kwa Ushiriki katika Masuala ya Kijamii 104
Kukosekana uwajibikaji wa mtu binafsi 108
Kupitwa na wakati na Ushirikina 109
Mbinu yenye Busara 111
Wafundishe Watoto Upendo wa Qur'an 112
Ukumbusho Endelevu wa Mwenyezi Mungu 115
Wafundishe Watoto Kutubia (Kufanya Tawbah) 116
Wafundishe Kuhusu Muhammad (s.a.w) na Mitume wengine 117
Wafundishe Watoto Maadili 118
Kitu gani umueleze Mtoto wako kwanza? 118
Matatizo ya Elimu ya Kiarabu 119
Kazi za kufanya

Utangulizi

Ingawa katika sura iliyopita tulitazama miongoni mwa malengo makuu na maadili ambayo wazazi wanapaswa kuyaweka katika kuwalea watoto, kuna lengo mahususi moja kubwa ambalo linahitaji msisitizo, nalo ni imani juu ya Mwenyezi Mungu. Kuwalea watoto wamjuaye Mwenyezi Mungu ni tofauti kabisa na kuwalea watoto wanaompenda Mwenyezi Mungu na kujitambua mbele Yake. Kujitambua mbele ya Mwenyezi Mungu ni msingi ambao maadili huchomoza na mafanikio ya kweli yatapatikana. Muda tuutumiao na watoto wetu ni mdogo sana, hivyo tunapaswa kujipanga, kuanzisha ratiba na kutoiacha kwa wakati ujao na kutomtegemea mtu mwingine kutufanyia kazi hiyo tukifikiri kwamba kwa kiasi fulani imani na maadili vitajileta vyenyewe kadiri muda utakapowadia.

Jamii tunayoishi ina hamasisha fikra zisizo sawasawa, namna ya kufikiri kunakomuondoa Mwenyezi Mungu kutoka katika maisha yetu. Kuwa mwangalifu na shule ambazo humsukuma Mwenyezi Mungu nyuma.

Kuwalea watoto wamjuaye Mwenyezi Mungu ni tofauti kabisa na kuwalea watoto wanaompenda Mwenyezi Mungu na kujitambua mbele Yake.

Mbinu za Kisasa za Kuwafunda Imani Watoto Wetu

Kabla ya kutazama kitu gani tunapaswa kukifanya, hebu tutazame kitu gani kinatokea katika familia zetu.

Mbinu za kidini zisizo na mwongozo thabiti ambazo hutumiwa mara nyingi na Waislamu katika maisha ya sasa kama za kufuata mfumo maalumu na kufuata matakwa ya kisheria zinaweza kuelezwa na kwamba jambo hili huathiri namna watoto wa Kiislamu wanavyolelewa. Utamaduni wa kidini uliotawala kama unavyotumika sasa hutenganisha maisha katika shughuli za namna mbili: kaida za kidini (*'ibadat*) na miamala ya kibiashara (*mu'amalat*).

Katika kaida ya kidini, hii inaathiri malezi kwa watoto kwa kuifinya elimu ya dini kwa kuinasibisha na matendo maalumu yanayojumuisha udhu na swala tano, kufunga Ramadhani (*swawm*), na kutoa zaka. Pia kaida hizo, hudhibiti kabisa mahusiano ya kijamii, ikiwa ni pamoja na mkataba wa ndoa (*zawaj*), mikataba ya kibiashara (*'uqud*), maadili rasmi ya mtu (*'adab*) na kukumbuka imani za msingi (*kalimah au shahadah*). Hii ni njia ya kisheria ya kutekeleza imani.

Vile vile, wazazi wa Kiislamu na familia mara nyingi hukwepa majukumu umuhimu ya kijamii na uwajibikaji na kupendelea mafanikio binafsi, kutoa mchango mdogo katika majukumu ya kimaadili kwa wanajamii katika jamii husika. Matokeo yake ni kwamba, watoto wanakosa hamasa ya kushiriki katika masuala ya kijamii, na kwamba

kwa kuwa tu wameshafundishwa misingi ya kuswali na kusoma Qur'an, wazazi huwasifu watoto wao kwa hilo. Hivyo, watoto hukua wakifikiri kwamba kutekeleza matendo hayo ya ibada binafsi ni mhimili muhimu wa maisha ya kimaadili, na kwamba wakifanya matendo hayo ya ibada hizo maalumu, watakuwa wametekeleza majukumu yao yote ya kidini na kimaadili katika maisha. Hii inaweza kusababisha mfumo wa maisha wa kibinafsi na wa kichoyo ambao hauna tija kwa jamii. Kwa bahati mbaya, kaida hii ina madhara makubwa kwani huharibu kabisa maisha ya kushirikiana na ya kijamii, matokeo ambayo kila mmoja katika jamii yanamuathiri.

Katika uhalisia, ibada (*ibadat*) haina maana ya kutekeleza matendo hayo maalumu ya kiibada peke yake, pia inahusisha majukumu na vitendo vyote vinavyohitajika katika maisha ya Muislamu kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu (*Shari'ah*), pamoja na maadili, kama vile kuhamasisha matendo mema na kukataza maovu, kushiriki katika majukumu ya kijamii, na kuwasaidia wengine. Ikiwa sifa hizi haziwekezwi kwa undani katika hisia za mshikamano (*wujdan*) wa watoto wa Kiislamu, kitakachofuata ni kurithisha tabia hii kwa watoto wao na kufanya mzunguko wa hatari. Kwa hiyo, kuna makosa makubwa katika mfululizo wa elimu ya dini ambayo husisitiza zaidi katika utekelezaji wa matendo hayo maalumu ya kiibada kama msingi pekee na kuweka umakini katika maendeleo ya ndani kabisa na matakwa ya jamii. Neno '*ibadat* hasa humaanisha utajo wa Mwenyezi Mungu, ambao humaanisha kukumbuka na kuwasiliana na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kusimamisha haki, maadili, na tabia njema.

Utamaduni wa Ubinafsi: Kukosekana kwa Ushiriki katika Masuala ya Kijamii

Kwa bahati mbaya, kuna mkanganyiko wa kihistoria, kuweka kando na kutenganisha kati ya wasomi wa Kiislamu na wanafikra kwa upande mmoja na viongozi wa siasa wakandamizaji na wala rushwa kwa upande wa pili. Wanasheria wa Kiislamu wametengwa kutoka katika maisha ya kijamii na wao wameegemea sana katika vipengele binafsi vya maisha ya mtu, na kutupilia mbali matakwa ya Umma na ya kijamii. Hivyo, utekelezaji wa masuala ya kijamii, utawala bora, ushiriki katika siasa, ushauri (*shura*), majukumu ya kiraia, kutafuta haki za kijamii, na kuanzisha umoja na mshikamano havikupewa umuhimu wake kama inavyopaswa. Hili limevuruga dira ya Uislamu Ulimwenguni. Tabia ya kutoshiriki kikamilifu katika masuala yanayohusu jamii kumeathiri moyo wa umoja na ushirikiano na kudhoofisha mshikamano wa kimakundi ambao ni muhimu katika kutengeneza matakwa ya Umma. Ustaarabu hauwezi kuendelezwa kwa msisitizo wa fikra finyu

katika kuokoa matakwa binafsi; inapaswa kujumuishwa na msisitizo mkubwa katika matakwa ya Umma na ya kijamii. Kwa maana nyingine, utekelezaji wa dhana ya *istikhlaf* (udhamini wa mwanadamu) unatutaka kutekeleza na kuendeleza kizazi mpaka kizazi, dira ya *imran* (kuanzisha ustaarabu unaoegemea katika matendo mema katika jamii). Ingawa, sheria za

matakwa ya kibinafsi na kifamilia katika elimu ya dini (*fiqh*) ni mahitaji muhimu, haiwezi kutosha kuzalisha wajenzi wa ustaarabu.

Mtazamo kama huo unasaidia kuzalisha mtu mmoja mmoja na jamii iliyo bora lakini ikawa haina msaada mkubwa katika maendeleo ya Umma. Watu wanaokuzwa katika utamaduni wa kale, kimfumo, na kisheria wanaweza kutekeleza matendo hayo maalumu ya kiibada kama udhu, swala, funga, na hija sawasawa, lakini kwa bahati mbaya bado hawawezi kuwa raia bora, kushiriki katika majukumu ya kijamii, na kuisaidia jamii. Wana-Kuwa tegemezi kwa serikali kwa ajili ya kupatiwa huduma zilizo tayari, kuliko kufanya juhudi katika majukumu binafsi na ya kijamii, wanakosa kufikiri kwa faida yao, au kufanya maamuzi kuhusu kesho yao, au kuongeza ufahamu wao, au hata kujihudumia wao wenyewe. Kwa maana nyingine ni kwamba, kutojali huathiri ushiriki ulio imara. Watoto waliolelewa katika njia hii hawawezi kuwa huru, kuwa na maadili, kuwa wabunifu, kushirikiana na wengine, au kuwa waanzilishi wa maendeleo ya kijamii; badala yake wanakuwa katika kaida ya kibinafsi na kichoyo.

Watu wanaoishi katika tawala kandamizi za kisiasa na za kidini huathiriwa na hali mbaya; ambapo mabadiliko ya kijamii yanapohitajika, hutengeneza jamii dhaifu na zenye tabia zisizo na tija, ushahidi wa wazi katika matatizo ya kijamii katika mazingira na uchumi. Wakati wakikwepa akaunti za kibenki zenye riba, wako radhi kufanya udanganyifu katika ulipaji wa kodi pamoja na zaka, hata kama udanganyifu haukubaliki katika Shari'ah. Hujihisi ni washindi wanapoweza kukwepa kukamatwa katika wizi kama huo na kuwadanganya maafisa wa kodi. Kwa sababu wanajua ya kwamba fedha watakazolipa kodi zitatumika vibaya au zitaibwa na maofisa wenye ushawishi mkubwa.

Wazazi wengine husisitiza tabia ya umimi tangu watoto wao wanapozaliwa mpaka wanapofikia utu uzima. Juhudi kubwa huwekwa katika mavazi kuliko kuwafundisha kuwajali wengine na kuwa wema kwa wengine au kupandikiza uwajibikaji kwa watu masikini na hususani, wanaohitaji msaada, na mazingira kwa ujumla wake. Wengi katika sisi huweza kuwanunulia watoto wetu wanasesere (midoli ya kuchezea) wa gharama kubwa wanaoharibika kiurahisi, lakini tunashindwa kumhurumia mtoto anayetaabika barabarani akiomba chakula na nguo.

Mtazamo kama huu katika maisha umeziumiza jamii zetu na maisha ya kijamii. Tunawezaje kuelezea, kwa mfano, kwamba Siku ya Taifa nchini Bangladeshi ina maana sawa na kuwatenganisha Wabangladeshi kutoka Pakistani? Kwa nini sherehe hizo za kutengana zipaziwe sauti tuonapo mataifa ya Ulaya yakiungana na kushirikiana katika kuboresha matakwa yao ya pamoja, wakati walishawahi kuwa maadui? Nchi ya Brazili ina umoja pamoja na kuwa na makabila mengi, imani mbalimbali za kidini, lugha mbalimbali na kila kikundi kimoja kikiwa

na matatizo yake ya kiuchumi na kijamii. Wakati huo huo, pamoja na kuwa na lugha moja, utamaduni mmoja, na matakwa yanayo fanana, mataifa ya Kiislamu na ya Kiarabu, yanaendelea kusambaratika. Mataifa ya Kiarabu yanayo endekeza migogoro na mataifa "masikini" ya Kiislamu yanafanya mambo machache sana kuwasaidia wananchi wao. Idadi ya Waislamu inaongezeka, lakini si hadhi yao duniani.

Je dini inaweza kuwa sababu ya kusambaratika kwa ulimwengu wa Kiislamu, kudorora kwa umoja, kudharaulika na kutengwa? Je, sifa hizo dhaifu zinatekeleza matakwa yake? Je, Waislamu wanaielewa vibaya dini yao? Kuna mgawanyiko katika uelewa wa Umma katika hili. Kila mmoja amejifunza kufikiri peke yake, na kujaribu kuhifadhi matakwa yake au ya familia yake kwanza, wakati huo huo akiyapa kisogo matakwa mapana ya Umma na yale ya wanajamii wengine kama vile ndugu na majirani. Utamaduni wa Kiislamu, unafifishwa na kuharibiwa kwa kutojali ujirani na sifa ya ushirikiano ambayo inapaswa kuwa kipaumbele. Waislamu wanapaswa kushtuka na kuchukua hatua.

Linganisha hali hii na tabia za Abu Bakar, wakati alipokuwa tayari kutoa mali zake zote kwa Umma. Mtume Muhammad (S.A.W) alimuuliza: "Umebakisha nini kwa ajili ya familia yako?" Alijibu: "Nimemuacha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake." Kitendo cha Abu Bakar si tu kwamba ni dalili ya imani kubwa aliyokuwa nayo, lakini pia imani yake kwamba Mtume (S.A.W) na jamii wangeweza kumhudumia yeye na familia yake wakati wa shida. Kama Abu Bakar angefikiri kwamba familia yake ingeathirika na kitendo chake na kupelekea kuomba mitaani, angehifadhi mali zake nyingi na kutoa sehemu ndogo tu ya mali hiyo.

Hali ya sasa ya Waislamu inayosikitisha, haiwezi kulalamikiwa kwa kuzingatia ukweli kwamba jumuiya ya Kiislamu duniani inaundwa na nchi nyingi zenye makabila mengi yanayozungumza lugha mbalimbali, au kwamba zinatawaliwa kimabavu, au zimeathirika na historia ya kutawaliwa na kadhalika. Uislamu unahamasisha amani, kuishi pamoja, na mshikamano katika jamii. Leo hii Waislamu wanafikia robo ya idadi ya watu duniani. Kutengana kwao hakuwezi kunasibishwa na Uislamu kwa sababu Uislamu unafundisha umoja, udugu, mshikamano, na upendo. Pia, hauwezi hata kidogo kunasibishwa na sababu za kiuchumi na za kisiasa kwa kuwa anguko la kiuchumi na kisiasa ni dalili na si sababu. Swali linalobakia ni: Nini kinawajibika? Tunaamini kwamba majibu yanapatikana katika aya za Qur'an:

> Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo naf- sini mwao. (Qur'an 13:11).

Hatuwezi kuweka msisitizo wa kutosha: hali mbaya ya watu inatokana na wao wenyewe. Hivyo basi, njia pekee ni kuielewa vizuri Qur'an na kuamua kubadili tabia zetu za ndani jambo litakalosaidia kubadili hali ya maisha yetu, hii itawezekana kwa kupitia malezi sahihi.

Elimu ni mchakato wa muda mrefu, na mtu anaweza kuipata tangu utotoni mpaka mwisho wa uhai wake. Malezi bora ndio jambo muhimu katika kuasisi msingi bora wa uwajibikaji, kujitolea, na uangalizi juu ya wengine. Mambo haya lazima yasisitizwe katika kipindi cha mwanzo kabisa cha utoto kwa mzazi kupandikiza hisia za kweli, mahusiano ya kijamii na mahusiano ya kiroho yenye maadili ma-

Yapo mahusiano ya moja kwa moja kati ya ibada binafsi na mahusiano ya kijamii.

zuri. Mambo haya lazima yatazamwe tangu hatua za awali kabisa ambapo mambo yanakuwa ni mepesi na ya ufanisi kuliko katika kipindi cha utu uzima. Vitabu vya fiqhi (sharia ya Kiislamu) vinawakilisha mwongozo wa mafundisho ya msingi ya kidini na ya kiutamaduni katika kujenga maendeleo binafsi ya Muislamu na yakawa na ushawishi katika kuimarisha utu.

Kwa hiyo ni muhimu kufanya marejeo katika vitabu vya fiqh kwa kuongeza kila palipopungua ili yapatikane mambo yatakayokuwa na maslahi kwa Umma na jamii yote ya binadamu. Taswira hiyo imeelezwa vizuri katika mafundisho ya Qur'an na hadithi za Mtume (S.A.W).

> Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa. (Qur'an 59:9)

> *Na Mtume (Rehma na Amani Ziwe Juu Yake) anasema: "Yeyote asiye shughulishwa na mambo ya Waislamu basi huyo si miongoni mwao"*
>
> *(Ibn Mas'ud)*

Bila kushughulishwa na mambo ya watu wengine, kama vile masikini, mayatima, majirani na wale wote wanaohitajia hatuwezi kuwa Umma bora kama tunavyofundishwa katika Qur'an:

> "Je! Umemwona anaye kadhibisha Malipo? Huyo ndiye anaye msukuma yatima, Wala hahimizi kumlisha masikini. Basi, ole wao wanao swali, Ambao wanapuuza Sala zao; Ambao wanajionesha, Nao huku wanazuia msaada (Qur'an107:7)"

Yapo mahusiano ya moja kwa moja kati ya ibada binafsi na mahusiano ya kijamii. Ibada za kidini lazima sihusiane na kutazama mayatima, kulisha maskini na kusaidia majirani. Lengo halisi la ibada ni kumuandaa mja kuwasaidia wanadamu wenzake. Kuwapo ombaomba katika mitaa ya Waislamu kunathibitisha kutokuwepo kwa uhusika wa kiuwajibikaji, ambao msingi wake ni hali za wanajamii wa sasa.

Kukosekana uwajibikaji wa mtu binafsi

Watu wengi hawathamini au hawajui wajibu wao na wajibu wa wenzao kwa mustakbali wa baadaye. Kukosekana wawajibikaji na watu waadilifu katika jamii ni jambo linalopelekea kutosaidiana na kupelekea kuomba msaada kwa wengine, kwa kudai kwamba anatimiza wajibu kwa ajili yake, wakati akikanusha kwamba hamiliki chochote kwa ajili yake wala familia yake. Kimsingi kujitolea kwa mtu binafsi kumepotea katika jamii ya Kiislamu. Lakini pia ni matokeo ya moja kwa moja ya maambukizi ya kukosekana umoja kwa jamii ya Kiislamu duniani.

Mtu asije akachanganya baina ya kuwahudumia watu na umoja. Umoja ni kutanguliza maslahi ya kundi dhidi ya mtu binafsi.Ukabila na koo ilikuwa ni mifumo ya umoja ya zamani sana katika jamii za Kiislamu. Hivi sasa mifumo imebadilishwa na kuwa watumwa wa serikali. Kitaalamu umoja hupelekea "fikra mkusanyiko" au akili ya kundi ambayo ni adui wa fikra binafsi (*ijtihad*) na chanzo kikuu cha maendeleo ya binadamu. Kwa dhana za kiuchumi huondoa motisha zote za uzalishaji kutoka kwa watu binafsi na kuwageuza kuwa watumiaji wasio zalisha.

Kisaikolojia inaondoa mtazamo wa mtu mmoja mmoja kama khalifa (kiongozi). Umoja unakuza tabia ya kutegemeana, hali inayofanya mtu asiwe mbinafsi. Kimaadili inapelekea kuwa na hofu ya kuyaendea mabaya. Pia kisiasa inapelekea aidha upinzani wa kupambana na ubinafsi au kuzuia nguvu ya matakwa uliyonayo dhidi ya maslahi ya jamii.

Tofauti na maelezo ya hapo juu, Qur'an inamtaka mtu mmoja mmoja kuchukua majukumu yake kama khalifa (kiongozi) na kujisalimisha kwa Mungu mmoja. Na kuhamasisha kupambana katika kufanya mema kwa ajili yako kisha kwa jamii na hatimaye kwa Umma. Ikiwa kweli tunataka kwa watu kile tunachokitaka sisi, basi tutataka watu wawe makini, wawajibikaji na wawe huru.

Katika nchi nyingi za Kiislamu, watoto wanafundishwa wawe watazamaji na wasioweza kufikiri sawa sawa. Wanajifunza sheria za kimahakama zilizopitwa na wakati. Zaka inafundishwa kama vile ni kodi ya ngamia unaowamiliki. Wanafunzi wanafundishwa kutoa magunia ya shayiri na tende kwa ajili ya maskini wakati

mafunzo hayo yalihitajiwa na jamii za Kiagrariani (jamii za kale), mafundisho hayo yanakuwa hayaendani na jamii za kisasa na zilizoendelea. Vitabu juu ya fiqhi (sharia ya Kiislamu) bado vina maelezo juu ya namna ya kuwashughulikia watumwa na namna nzuri juu ya kununua na kuuza! Vijana wa Kiislamu bado wanafundishwa mambo yaliyopitwa na wakati na kupewa taarifa zisizo na faida kwao. Kwa msingi huo fursa muhimu inapotea: yaani fursa ya kuhurumiana na kuhusika moja kwa moja kuwasaidia wengine. Kukosekana kwa kuhurumiana ni dalili za kuporomoka kwa ustawi wa kizazi cha Umma huu kwa wakati wa baadaye. Sababu za msingi zinazosababisha kuwafundisha watoto zaka si namna ya kukokotoa asilimia kwa ajili ya ngamia, tende na magunia ya shayiri, bali ni kuwapa uelewa wa hali ya juu kuhusu mshikamano, ukarimu, kujitolea, wema pamoja na umuhimu wa kushirikiana na waliokata tamaa na wenye mahitajio. Lililo na umuhimu zaidi si kukusanya rasilimali vitu ukatosheka kwazo bali lililo muhimu ni kuingiza hisia za kuhurumiana na kuelewana, pamoja na kuwahurumia wanyonge/waliokosa msaada hali ya kuwa wanahitajia kutoka katika jamii. Ni utekelezaji wa kuonesha udugu wa Kiislamu na furaha ya kutoa kwa njia ya zaka na aina nyingine ya wema ambao unahitaji kutiwa msisitizo katika kipindi hiki muhimu cha utoto, na si kuwasumbua na ukokotoaji wa mahesabu yanayochosha.

Utamaduni Ulioharibiwa: Kupitwa na wakati na Ushirikina

Tatizo lingine linalowakabili na kuwadhoofisha Waislamu ni suala la ushirikina, uchawi na umajinuni pamoja na ulimwengu wa majini. Ustaarabu wa Kiislamu umejengwa katika misingi ya maarifa, sayansi, usawa na sababu. Jambo la kutia faraja ni kujua kwamba wataalamu wa Kiislamu wanaamini ile nguvu ya kimiujiza ya asili ya mitume wote, wakati huo huo wanaamini ya kwamba muujiza wa hakika kabisa aliouacha Mtume Muhammad (S.A.W) kwa wanadamu ni Qur'an. Ujumbe wa Qur'an unaainisha ya kwamba upevu wa fikra za mwanadamu umeegemea katika kuhoji. Qur'an inawakumbusha watu kufanya utafiti, kutafakari, uvumbuzi na kufikiri. Hizi ndizo fikra kubwa zilizotawala na zinazorudiwa mara kwa mara ndani ya Qur'an. Fikra za aina hii ndizo wanapaswa wazazi wapandikize katika akili za watoto. Kwa msingi huo watazalisha vijana wanaoamini katika kuhoji wakati huo huo wakishikamana kwa dhati kabisa na Imani ya Mungu mmoja na kuamini maisha baada ya kufa. Ustaarabu haujengwi katika misingi ya ushirikina na uchawi. Mtu mmoja ameogopa baada ya kusikia hadithi ya kutisha juu ya watu wanaotegemea nguvu ya uponyaji juu ya roho mtakatifu, majini, nyota na kiini macho katika kushughulikia masuala ya kifamilia, kuliko kutegemea madawa ya uhakika au matibabu ya kisaikolojia. Mazoea haya ni kinyume na kanuni na Imani ya Kiislamu na pia ni sumu kwa fikra za watoto. Jukumu letu kama wazazi ni kuingiza mwangaza wa fikra za kisayansi ambazo zimesisitizwa na Qur'an. Qur'an inathibitisha juu ya *Al-sunnan Al-Illahiyyah* kanuni za asili za kimaumbile ambazo ndizo zinasimamia maisha ya mwanadamu na ulimwengu kwa ujumla.

Kanuni hizi za kiungu ndizo zilizotumika kwa Mtume Muhammad (S.A.W) kama zinavyoelezwa katika aya ifuatayo:

> "Sema: Mimi ni mwanadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi
> (Qur'an18:110)

Malengo haya na fikra hizi za kisayansi zilizalisha ustaarabu wenye nguvu ambao ulimwengu haujapa kushuhudia. Katika kipindi hicho cha dhahabu ni Waislamu pekee ndio walioisaidia Ulaya ikiwa katika zama za giza (kipindi ambacho walizama kwa karne) mpaka kufika katika kipindi cha mwangaza(Al-Hassan 2011).

Kwanza ni jukumu la mzazi na pili walimu wa shule kuzalisha watoto wenye uelewa mpana, wenye kaliba na haiba nzuri, waliokamilika kisawasawa na wenye uelewa juu ya ufunuo na kanuni za asili za ulimwengu, mwanadamu na sayansi ya jamii.

Mwanafalsafa wa Kifaransa Roger Garaudy ameelezea mtazamo wa ustaarabu wa Kimagharibi kama ifuatavyo:

Ustaarabu wa kisasa na uzuri ambao Ulaya inao leo ni zao la mfumo wa sheria kutoka katika staarabu za Kirumi na Kigiriki, maadili yake imeyapata kutoka kwa Wakristo, na fikra za kisayansi imezipata toka kwa Waislamu wa Hispania.

(AL HEWAR MAGAZINE 2002)

Mtazamo potofu wa kilimwengu: Udhaifu na Woga

Mtume Muhammad (S.A.W) amesema:

"Utafika muda ambao mataifa yatawavamia, kama vile watu wenye njaa wanavyoishambulia sahani ya chakula: "maswahaba wakauliza, hii itatokea kwa kuwa tutakuwa wachache kiidadi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Mtume akasema: "hapana, mtakuwa wengi, lakini wingi wenu utakuwa kama povu la wimbi la maji ya bahari. Mwenyezi Mungu ataondoa hofu na heshima yenu kwenye mioyo ya maadui zenu na atapandikiza mioyo ya woga (wahn)". Mtu mmoja akasema: "Nini maana ya wahn, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akajibu: Wahn ni kupenda maisha haya ya dunia na kuchukia kifo."

(Abu Daud)

Njia iliyo ya kati na kati: Mbinu yenye Busara

Tunawaomba wazazi kuwa na mtazamo wa busara juu ya Imani za kidini. Uelewa wenye busara katika utekelezaji na uzingativu wa mambo muhimu ya dini yako yatakuwa na faida zenye athari katika namna unavyolea watoto. Ni muhimu kulea kwa namna ambayo haipelekei kuwa na hofu, ubinafsi, udumavu na kutumia nguvu.

Wasomi wa kale *('alims, fuqahaa*, na *mullahs)*. Walisisitiza mila na ibada (*ibadat)*. Qur'an imetaja *dhikr,* yenye maana ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Yote hayo ni muhimu katika kufunza watoto. Wazazi wana jukumu la kufahamu mtazamo wa Uislamu katika masuala ya dunia na kuwafundisha watoto wao katika umri wa utambuzi.Watoto wanapaswa kufahamishwa kwamba lengo letu ni kuyaendesha maisha ya dunia kulingana na kanuni na sheria ambazo Mungu amewawekea wanadamu, na kwamba ibada ndio njia ya kuyafikia hayo. Hii itawafanya kuelewa kuwa lengo la maisha ni kujitahidi kutenda yaliyo mema.

Sisi wazazi, tabia zetu ndizo zitakuwa kama kioo cha kuigwa na watoto wetu. Hatuna budi kujitahidi kufanya *dhikr* ili itukumbushe jukumu letu na kujirekebisha ili tumfurahishe Yeye. Cha msingi tunatakiwa kufanya juhudi kuishi maisha ya wema katika dunia katika kutunza mazingira, kutafuta elimu, na kusaidia wanaodhulumiwa na kuwakomboa. Watoto wataelewa vyema maana na lengo halisi la ibada endapo watawaona wazazi wakitekeleza kivitendo, na ikiwa wanafundishwa ya kwamba maana ya maisha ni kipimo cha majaribio ya ubora wa binadamu na jitihada zao katika kufanya vitendo vizuri katika hali zote yaani wakiwa peke yao na wakiwa katika jamii.

Aya zifuatazo zinaonesha namna mtazamo wa kilimwengu unavyoweza kujengwa katika akili ya mtoto.

"Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu. (Qur'an 6:162-163)"

"…Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda. (Qur'an29:45)"

"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani (Qur'an 76:8-9)"

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu (Qur'an 24:55)"

Wafundishe Watoto Upendo wa Qur'an

Ili kukuza watoto wenye mapenzi na Muumba wao, wazazi wanatakiwa waipenyeze Qur'an kwa watoto ili iwe mwongozo badala ya kuwa ni kitabu kitakatifu cha kusomwa katika matukio fulani ya kidini na baadaye kuwekwa katika makabati kwa kipindi chote cha mwaka bila kusomwa. Je, msisitizo uwe katika kupata taarifa au katika maeneo muhimu ya maendeleo ya kiroho na kihisia ya moyo na roho ya mtoto? Kupata taarifa na utaalamu huendelea katika siku zote za maisha ya mwanadamu, wakati makuzi ya afya, hisia na saikolojia sharti yatokee katika miaka ya mwanzo ya mtoto hasa kabla ya miaka ya baleghe.

Waislamu mara nyingi wanawaogopesha watoto moto *(Jahannam)* bila kutaja mapenzi ya Mwenyezi Mungu, huruma zake na mapenzi yake, na au uzuri wa pepo (*Jannah*). Tunatilia mkazo jinsi watakavyoungua motoni wasipomtii Mola wao na wazazi au kufanya makosa, wakati huo huo tunasahau kutaja jinsi watakavyolipwa na kuhudumiwa peponi watakapofanya mambo mema, wakamtii Mwenyezi Mungu,wakawatii wazazi wao na kufanya yaliyo mema. Aghalabu tumekuwa tukiwatisha watoto na adhabu endapo watakiuka, wakati mara chache tukiwatia moyo na kutaja mapenzi ya Mungu na jaza wapatayo wakiwa na tabia njema. Katika mazingira haya watoto wanakuwa watu wenye taharuki na woga. Wanajenga tabia hasi na kutojiamini na mbaya zaidi wanavunjika moyo pamoja na kuwatoa katika imani yao.

Walimu siku zote hufundisha Qur'an kwa kuanza na juzuu ya mwisho (*ammah* au juzuu ya 30). Juzuu hii ina sura fupi fupi zilizoteremka Makkah wakati wa mwanzo wa kushuka wahyi. Aya hizi ziliwalenga viongozi dhalimu wa Kiquraysh kama (Abu Jahl

na Abu Lahab). Qur'an katika sura hizi za mwanzo iliwakemea wale waliokuwa wakiwatesa Waislamu, wakiwaua baadhi yao, wakapanga kumuua Mtume (S.A.W), na wakaeneza vita vya kuwateketeza Waislamu. Sura hizi zililenga kurejesha fikra za hawa wajeuri, lakini aya hizi zilipiga masikioni mwao mithili ya radi kwa sababu zilikuwa na maonyo makali. Tazama mifano ifuatayo:

"Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia

(Qur'an 111:1)"

"Ole wake kila safihi, msengenyaji!

(Qur'an 104:1)"

"Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza? Siku hiyo nyuso zitainama, Zikifanya kazi, nazo taabani. Ziingie katika Moto unao waka Zikinyweshwa kutoka chemchem inayo chemka. Hawatakuwa na chakula isipo kuwa kichungu chenye miba.

(Qur'an 88:1-6)

"Ole wao hao wapunjao!

(Qur'an 83:1)"

Sema: Enyi makafiri!

(Qur'an 109:1)

"Pindi dunia itakapo tikisika mtikisiko ulio mkubwa kabisa".

(Qur an 99:1)

Ni kitu cha kuhuzunisha kuona kuwa maonyo ya aina hii hayajakusudiwa kutolewa kwa watoto wasiokuwa waovu, ila hizi ni katika aya ambazo hufundishwa kwa watoto wa aina hii. Sababu kuu ya kufundisha

Watoto wanatakiwa waelezwe kuwa wao ni viumbe wema na Mwenyezi Mungu anawapenda wao kabla hata ya kuanza kuwafunza kumpenda Mwenyezi Mungu.

aya za sura hizi kwa watoto hawa ni kwamba sura hizi ni fupi na huonekana kuwa rahisi kuhifadhiwa. Badala ya kuwatisha watoto wakiwa na umri mdogo kwa kutumia vitisho vya adhabu ya moto na bishara za pepo, inatupasa kuhamasisha watoto wampende Mwenyezi Mungu, wawe na huruma kwa wazazi wao na kuwafunza neema za peponi. Hali hii huendana na mfumo wa fikra zao na kuwajengea wajihisi wako katika hali ya usalama, upendo, ukarimu na huruma tangu wakiwa katika hatua za awali za utoto. Ni bora kuanza na upendo kuhusu Mwenyezi Mungu, huruma Yake kwa viumbe, ukarimu Wake, neema, namna anavyosamehe pamoja na wema wake kwa viumbe ikiwa ni katika sifa zake njema. Watoto wanatakiwa waelezwe kuwa wao ni viumbe wema na Mwenyezi Mungu anawapenda wao kabla hata ya kuanza kuwafunza kumpenda Mwenyezi Mungu. Utaratibu wa kufanya haya uanze kumpenda Mwenyezi Mungu kwanza ukifuatiwa na wajibu wao katika kumpenda Mwenyezi Mungu.

Pindi watoto wanapokuwa wameanza kuelewa wazazi wanaweza kuanza kuwafunza kuhusu adhabu kama malipo ya uovu walioufanya. Sura zilizopo katika Qur'an zenye makatazo na vitisho kuhusu makosa makubwa (dhambi kubwa) zinatakiwa kufundishwa kwa watoto katika kipindi ambacho watoto hawa wanaweza kujifunza kitu fulani badala ya kuwafanya wajenge hisia za hofu. Hii ifanyike katika hatua za mwisho za utoto wao na pale wanapofikia ujana, kipindi ambacho wamekuwa na wanaweza kuelewa mawazo dhahania na athari ya matendo yao.

Umakini unatakiwa kuwepo katika malezi ya kiakili na kisaikolojia hususani wakati wa kuwafundisha Qur'an. Inashauriwa wazazi wachague aya zenye kuendana na hatua mbalimbali za ukuaji wa watoto wao. Wengi katika maswahaba wa Mtume (S.A.W) walifundishwa Qur'an wakiwa watu wazima. Katika wakati huo, Qur'an ilikuwa na athari kubwa sana kwao. Ujasiri wao ulizidi kuimarika na Qur'an iliwafanya waweze kuwa na tabia njema (maadili yanayofaa). Wataalamu katika sayansi ya Qur'an pamoja na wataalamu wa masuala ya elimu na sayansi ya jamii, wanaweza kuwashauri wazazi namna ya kuwafundisha watoto wao, ikiwemo pamoja na aya za kufundisha zenye uhusiano na umri wa watoto wao. Bila shaka, aya zote za Qur an zinatakiwa kufundishwa katika kipindi cha uhai wa binadamu. Hata hivyo kitu cha kujiuliza ni kuwa; katika mfuatano wa aina gani aya hizi zifundishwe? Aya zipi zitiliwe mkazo na katika umri gani wa mtoto? Ni wazi kuwa siyo vizuri kuanza na juzuu ya 30 kwa sababu tu ina jumla ya sura 37 ambazo ni fupi. Uwezo wa kitu kuweza kukikumbuka isiwe kigezo pekee cha kuzingatia.

Wazazi ambao hawazungumzi lugha ya kiarabu wanatakiwa waeleze maana ya aya za Qur'an kwa watoto wao kwa kutumia lugha zao. Kwa sasa, msisitizo umewekwa katika kuweza kusoma kiarabu na kuhifadhi aya za Qur'an bila kujua maana yake.

Wazazi wanasisitizwa wapate tafsiri sahihi ya Qur'an na kuongezea mafunzo yao kwa somo la tafsiri ili waweze kuhusianisha mtazamo wa kiulimwengu na ujumbe wa Qur'an. Kama wazazi hawawezi kufanya hivi, wanaweza kutafuta mwalimu na wao kufanya kazi ya kudhibiti juu ya nini na namna gani watoto wao wanafundishwa.

Rekodi za Qur'an zinaweza kusikilizwa kwa kipindi maalumu nyumbani ili watoto waweze kutambua sauti ya Qur'an. Ni muhimu kuwa na utaratibu pamoja na mfumo maalumu wa kusoma Qur'an ili watoto waweze kujenga mazoea ya kusoma Qur'an kila siku. Kujifunza lugha ya kiarabu kama lugha ya pili pia husaidia watoto katika kujifunza Qur'an na kuielewa katika uhalisia wake bila kutafsiriwa. Vitabu vingi vizuri vya watoto vimechapishwa vikiwa na visa vya mitume mbali mbali kutoka katika maandiko pamoja na mafunzo au mazingatio yake kutokana na visa hivi. Wazazi wanatakiwa kununua au kuazima vitabu vya visa hivi ili kuongezea katika usomaji wa Qur'an ili watoto waweze kufahamu na kuelewa zaidi Qur'an.

Wafundishe watoto kuomba dua: Ukumbusho Endelevu wa Mwenyezi Mungu

Kuna dua nyingi fupi zenye kuhamasisha mazingatio na kujali kuhusu Mwenyezi Mungu ambaye yupo pamoja nasi. Dua hizi ni nyepesi kuzitambulisha kwa watoto na kuwasaidia kuwa na tabia ya kushukuru na kutafuta mwongozo pamoja na ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Pia zinasaidia kumkinga mtu na asimweke nyuma Mwenyezi Mungu katika mambo yake. Wazazi kwa mfano wanatakiwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kabla ya kula na baada ya kula, na kuwataka watoto wao wasome dua zile wanazosoma wao. Pia wakati wa kuingia ndani (nyumbani), wakati wa kutoka ndani/ nyumbani, wakati wa kulala, wakati wa kuamka kuwepo na suala la kusoma dua.

Hali hii hupelekea kuwepo kwa shukrani. Kwa kusema kwa jina la Mwenyezi Mungu wakati wa kufanya jambo fulani, kutaweza kushuhudiwa na watoto kisha kuigwa. Ingawaje inaweza kuonekana jambo hili halina umuhimu sana na siyo sahihi kwa watoto, jambo hili ni bora kulidumisha. Hatima yake ni kuwa tabia hii huchochea watoto kuwa na tabia ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kufanya mawasiliano na Mwenyezi Mungu (mwenye uwezo wa hali ya juu kabisa) sehemu yao halisi ya maisha. Pia watafahamu huruma za Mwenyezi Mungu katika kila kitu.

Katika ibada ya swala, ibada hii ifanywe kuwa muhimu na nguzo asilia ya maisha ya wazazi. Wazazi huwa mfano mzuri kwa watoto. Piga adhana mbele ya watoto wako na utendee haki muda wa ibada ya swala. Runinga inatakiwa kuzimwa na kila mmoja ajiandae kwa swala ili ibada hiyo iweze kutekelezeka katika mazingira sahihi. Wazazi wanatakiwa kuswali mbele ya watoto wao hali ya kuwa wanajielewa na wanautulivu (unyenyekevu). Mara nyingi kuna ukosefu wa subira katika kumaliza swala na hali hii ya kufanya haraka katika swala inaweza kutambuliwa na watoto na bila shaka nao wataiga kwa kuswali bila umakini. Dua inatakiwa isomwe kabla na baada ya swala ili watoto nao wajifunze kufanya hivyo, kwani inakuwa maombi kwa chochote unachokihisi unahitaji kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Wafundishe Watoto Kutubia (Kufanya *Tawbah*)

Watoto wanahitaji kufahamu kuwa matendo yanakuwa na athari. Tabia mbaya ni aibu na inajulikana kwa Mwenyezi Mungu. Wanatakiwa kutubia kwa kuomba pale wanapokosea. Haitoshi kwa watoto tu kusema samahani na kuendelea na mambo yao. Watoto wanatakiwa kufahamu kuwa kitendo cha mtu kujuta kutokana na maovu yake kinatakiwa kutafutiwa ufumbuzi kwa Mwenyezi Mungu. Hali hii pia hufungua mlango wa kuweza kumtambua Mwenyezi Mungu; na kuruhusu ama kutoa fursa kwa wazazi kuweza kufundisha watoto wao mapenzi na huruma ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake. Watoto pia wanaweza kuwa na uhusiano mkubwa na Mwenyezi Mungu.

Wazazi hawatoshukuriwa na watoto wao kwa jitihada zao za kutoa elimu husika kwa watoto na kinyume chake hujikuta wanachukiwa na kuletewa vikwazo na watoto wao. Hata hivyo, kuendelea kutoa maelezo juu ya hali husika kwa sauti ya upole na kuonesha upendo baada ya toba kuwa imefanyika itapelekea watoto kuwa na tabia ya kuendelea kutubia na kujizuia na maovu. Baadaye watoto wanapofikia hatua ya utu uzima, endapo watakuwa wamewadhuru watu wengine au wametenda kosa kwa wenzao, watakuwa wanajua nini cha kufanya ili kusuluhisha kosa lao kwa Mwenyezi Mungu.

Wafundishe Watoto Kuhusu Mtume Muhammad (s.a.w) na Mitume Wengine

Wazazi wanashauriwa kuwekeza kwa kuwa na maktaba za vitabu na kuwa na tabia ya kusoma mara kwa mara na watoto wao. Wazazi wanaweza kusoma au kusimulia visa vya Mtume (S.A.W) kuhusu maisha yake, utoto wake, tabia zake na nasaha zake, simulizi za wajukuu zake na simulizi za maswahaba zake. Hadithi za Mtume huwezesha watoto kuingia katika ulimwengu wa mitume, kuunda uhusiano baina yao na kuwaiga kama vigezo vyema. Simulizi hizi zinatakiwa kuandaliwa na kusimuliwa kwa watoto katika makundi kulingana na rika zao na zilenge katika mandhari ambayo watoto wanaweza kuhusisha. Wazazi pia wanaweza kuwasomea watoto wao simulizi za watu majasiri na viongozi wenye maadili katika kipindi chote cha historia.

Fundisha watoto kuhusu mafanikio ya ustaarabu wa dini ya Kiislamu. Peleka watoto makumbusho kisha waruhusu kujifunza kuhusu sanaa zenye mandhari ya dini ya uislamu, historia na usanifu majengo. Makumbusho ni sehemu nzuri za kuwavutia watoto kihistoria na huwa kuna shughuli nyingi kwa ajili ya watoto, ambapo wazazi wanaweza kutumia vizuri fursa hii. Pia kuna vyanzo vizuri vya mtandao wa kimataifa vyenye kuhusiana na suala hili, kwa mfano "uvumbuzi wa vitu 10001", kuonesha mafanikio ya Waislamu kwa kipindi cha miaka elfu iliyopita:**http:www.10001inventions.com.**

Inapendekezwa pia kwa wazazi kuwekeza katika nakala ya kitabu, *uvumbuzi wa vitu 10001:Urithi wa Waislamu katika dunia yetu.*Hivi inakuwa rahisi kusoma, kitabu kizuri chenye mwongozo kinachoweza kuchukua wasomaji na kuwaelezea miaka elfu ya sayansi na teknolojia na katika kipindi cha wagunduzi wa mwanzo ambao kazi zao za uvumbuzi zimepelekea katika kuunda ulimwengu wetu wa sasa. Tovuti na vitabu/DVD zenye mchanganyiko wa taswira na sauti kuonesha uzuri wa ulimwengu tunaoishi pia huunda sehemu muhimu miongoni mwa vyanzo hivyo. Watoto waoneshwe filamu zenye kuwafanya waweze kujenga taswira fulani, hususani filamu ambazo zinaelezea miujiza ya uumbaji kama vile maajabu ya nyuki.

Kadhalika kadri watoto wanavyokuwa, athari ya ulimwengu wenye dhana ya kutofuata dini huingia ndani ya uelewa/ufahamu wao. Jiandae kujibu maswali ya mada mbali mbali kama "dhana ya mabadiliko". Watoto wanaathiriwa zaidi katika kujihusisha zaidi na mahusiano duniani na wazazi wanakuwa na imani na watoto wao endapo wataruhusu imani ya aina hii iwatawale kupitia mfumo wa uislamu. Pindi utambuzi wa Allah na uumbaji wake wa viumbe unapopandikizwa katika akili za watoto mawazo ya watu wasiofungamana na masuala ya dini itakuwa ni rahisi kukabiliana nayo. Watoto wanahitaji msingi imara na sahihi wenye kuwabadilisha na au wenye kutoathiri mtazamo wa kidunia.

Wafundishe Watoto Maadili

Dhana ya Uislamu kuhusu tabia inajumuisha suala la maadili (adabu). Watoto wanatakiwa wafundishwe kusema "*tafadhali*" pamoja na kusema "*asante*" na kusema "*sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu*", "*Mwenyezi Mungu akipenda*" na "*amani iwe juu yenu*". Mara nyingi salamu hii iliyo nzuri inakubalika kwa kusema "mambo" au "kwa heri". Watoto wanatakiwa wafundishwe adabu za kula na kunywa, kuvaa nguo zenye maadili na kuwa na matendo yanayokubalika katika jamii.

Ni muhimu kuwafanya watoto na mazingira ya nyumbani kuwa safi,na kuwe katika mpangilio mzuri ili watoto nao waweze kupata tabia ya kuwa hivyo. Usiwadekeze watoto wakati mwingine ni bora kuwapikia chakula kisichoungwa kuliko kuwapatia chakula kilichopikwa kwa ustadi mkubwa kwa kusudio la kuwafurahisha ili kuwafunza kujua thamani ya chakula kitamu wanachopewa. Mara nyingi sifa na tamaa za watoto hupelekea kuwa na majigambo pamoja na ujinga. Siyo lazima kuwanunulia watoto kila aina ya sesere (mdoli) wanalohitaji, kama watakuwa wanahitaji kitu basi wakati mwingine wazazi wanaweza kuwaruhusu watoto wao kutafuta kwa kufanya kazi ndogo ndogo. Watoto lazima wakumbushwe kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kuwapatia kitu kilicho bora zaidi. Tafuta njia mbadala, kwa mfano, pindi wanapokosa kitu wanachohitaji, waandae watoto waweze kuwa wenye subira na katika hali hiyo maadili wanayojifunza hapa yatawasidia katika maisha yao yote.

Lipi umueleze Mtoto wako kwanza:Wao wampende Mwenyezi Mungu au Mwenyezi Mungu Anawapenda?

Kama watoto wanafundishwa kusema "nampenda Mwenyezi Mungu", yeye ameniumba mimi na ulimwengu, jua na mwezi"je ni ujumbe wa aina gani hutolewa kwa watoto? Awali ya yote, watoto hawatambui chochote kuhusu Mwenyezi Mungu, ni mawazo ambayo hawatambui. Kitu kinachokusudiwa kwao ni kupenda na siyo tu kupenda wasichojua?

Pia, watoto wanafahamu kuwa kuwepo kwao katika ulimwengu huu pamoja na ulimwengu wenyewe ni jambo ambalo limetokea bila kuwa na sababu nyingine ya ziada. Hata hivyo, endapo watoto watafundishwa kuwa "Mwenyezi Mungu anakupenda, yeye ndiye aliyekuumba na akaumba ulimwengu ili uweze kuishi vizuri", watoto watahitaji kujua ni nani

WAFUNDISHE WATOTO

Mwenyezi Mungu anakupenda amekuumba wewe na amekuumbia dunia ili uburudike ndani yake

Watoto watahitaji kuwa na uhusiano mzuri na Mwenyezi Mungu mwenye upendo, kujali na watataka kufahamu zaidi na zaidi kuhusu Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu hadi awapende, awajali wao pamoja na kuishi kwao kwa uzuri hapa ulimwenguni. Bila shaka, watahitaji kuwa na uhusiano mzuri na Mwenyezi Mungu mwenye upendo na kuwajali wao na pia watahitaji kujua mengi zaidi kuhusu Mwenyezi Mungu.

Kuna uhusiano imara sana kati ya ibada, maisha na kujisalimisha katika himaya ya Mwenyezi Mungu (muumba). Tabia zetu zilizokuwa njema lazima ziendane na hali yenye kumfurahisha Mwenyezi Mungu, aliyekuwa chanzo cha kuleta kila lilio jema. Njia pekee ya kumfurahisha Mwenyezi Mungu ni kufuata yale aliyotuelekeza na kufuata mwongozo wake katika kuboresha maisha yetu yawe mazuri pamoja na wale watu ambao wanatuzunguka. Tunaboresha uhusiano wetu kiroho na Mwenyezi Mungu kwa kufanya matendo mema, kufanya kazi kwa bidii, kuwa wakweli, na kusaidia wengine wenye kuhitaji msaada, hivyo huongeza ukaribu wetu na Mwenyezi Mungu muumba. Huwa tunajisaidia sisi wenyewe kwa kuwasaidia wenzetu, kwa kuheshimu haki zao za kuishi, haki za kumiliki mali, heshima, kutenda haki, kuwa na huruma, haki ya kuwa huru, kuzuia utawala wenye mabavu na kupinga ukandamizaji. Haya yote huhitaji utambuzi endelevu na kukumbuka kuhusu Mwenyezi Mungu pamoja na sifa zake zilizokuwa njema.

Kutazama ibada mbali mbali huimarisha utambuzi huu na upendo wetu kuhusu Mwenyezi Mungu. Kwa namna hii tutapata baraka za Mwenyezi Mungu na mfanya ibada wa dhati atapata umadhubuti wa kufanya yale yaliyokuwa mazuri na mema.

KUJITAMBUA: Matatizo ya Elimu ya Kiarabu

Kuna kilio kikubwa cha kutaka kujifunza, kuwa huru na kufanya *ijtihad* (utafiti). Ripoti ya maendeleo katika jamii ya Waarabu iliyotolewa na Umoja wa Mataifa (2009) imeonesha kuwa hofu imetawala katika jamii ya Kiarabu kuhusu maendeleo ya sayansi na tafiti. Kwa sasa jamii za Kiarabu zimesonga mbele zaidi na kuyapiku mataifa mengine hata katika kulinda na kuendeleza utamaduni wao. Utafiti uliofanywa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1991 ulionesha kuwa jamii ya Kiarabu ilikuwa inaongoza kuwa na nakala chache duniani. Bara la Ulaya lilikuwa linaongoza kwa kuwa na nakala nyingi mara tano zaidi ya zile zilizokuwa katika jamii ya Kiarabu kwa ulinganisho.

Ripoti imeonesha tofauti kubwa iliyopo kati ya jamii za Kiarabu na jamii nyingine duniani. Katika kutaka kukabiliana na hali hii, nchi za Kiarabu zenye mamlaka zikaharibu ubunifu na uwezo wa kujenga hoja. “uhuru wenye kuathiri ulinzi na usalama, uhuru wa kuzuia makala na kujiteua kusimamia maadili ni

miongoni mwa uhuru ambao ulikuwa haukubaliki. Vitu vyenye kuathirika kutokana na hali hii ni ubunifu, jitihada, uvumbuzi na ujuzi" (mchumi mmoja alisema mwaka 2003).

Wazazi hawatakiwi kukwepa majukumu yao waliyokuwa nayo kwa watoto wao kwa kuyahamisha kwa serikali. Wazazi kama vigezo vya kuigwa na watoto wao na walimu waliokuwa muhimu kwa watoto wao, lazima wawe imara katika changamoto hii na waoneshe jitihada katika kubadilisha jamii. Wazazi ndiyo msingi wa mabadiliko (mithili ya funguo katika kuwasha chombo cha moto), dereva ndiyo sawa na mleta mabadiliko ya akili na watoa elimu wanaofundisha wazazi nini cha kufanya na namna ya kufanya. Kama wazazi watashawishika, watafanya kitu sahihi ambacho kinastahili kufanyika. Wazazi huwa wana ushawishi mkubwa wa kimaadili kwa watoto wao na wanaweza kubadili na kuunda tabia za vizazi vya baadaye.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 21: MAENDELEO YA JAPANI NA UJERUMANI DHIDI YA KUSALIA NYUMA KWA NCHI ZA KIISLAMU

Katika kikao cha makundi ya wenza watatu watatu, jadili maswali yafuatayo:

Kwa nini nchi nyingi za Kiislamu hazijaendelea, hali ya kuwa Japani na Ujerumani ambazo ziliathiriwa zaidi katika kipindi cha mapigano ya vita vya kwanza vya dunia, kwa sasa ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa maendeleo duniani?

Kwa nini baadhi ya nchi za Kiislamu bado zinaendelea kutupa uchafu katika mito, bado pia zina mifumo duni ya utoaji elimu na husafirisha malighafi kwa bei rahisi hali ya kuwa baadaye hununua kwa bei ghali baada ya kutengenezwa bidhaa? Kwa mfano, tani za madini ya chuma husafirishwa kwa dola 2000 na baadaye hununuliwa kama Kompyuta na vifaa vingine kwa mamilioni ya dola.

Kwa nini ulimwengu wa Waislamu una kiasi kikubwa cha watu ambao hawana elimu ingawaje kuna aya zinazohusu kusoma (*Iqra'a*)?

ZOEZI LA 22: UHUSIANO BAINA YA WATOTO NA MUUMBA WAO (MWENYEZI MUNGU)- MAPEMA KABISA.

Ingawaje kusimamisha swala kunatukumbusha sisi kuhusu Mwenyezi Mungu kwa utaratibu unaofaa, bado kuna shughuli nyingine nyingi zinatutaka sisi tuzihusishe na Muumba kadri tunapokuwa tunazifanya shughuli hizo.

Watoto wanatakiwa kufundishwa kusoma adhkari za kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Moja kati ya njia nzuri ni kuwafundisha watoto kuhifadhi dua ambayo ilikuwa ikisomwa na Mtume kuanzia asubuhi anapoamka hadi wakati anapolala. Dua hizi hazichukui muda mrefu na huongeza ufahamu wetu na huongoza matendo yote kuwa mema (hususani wakati tunaanza kula na baada ya kumaliza kula). Wazazi wanaweza kuchagua moja au mbili katika dua hizo kila wiki na kuhakikisha kuwa watoto wanazisoma kiufasaha kabla ya kuendelea na dua nyingine. Wafundishe watoto maana ya dua hizi.

Kama lugha ya Kiarabu ni ngumu kwako katika kutamka, inakubalika kutamka dua hiyo kwa lugha nyingine unayoifahamu au hata kwa kutumia Kiswahili.

Tukiamka kutoka usingizini alfajiri au wakati mwingine tutasema:

اَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِىْ اَحْيَانَا بَعْدَ مَا اَمَاتَنَا وَ اِلَيْهِ النُّشُوْرُ

Alhamdullilah lladhii ahyanaa baada ma-amaatana wailayhi nnushuur

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye ameturejesha katika uhai baada ya kutufisha. Na yeye ndiye atakayefufua."

(Bukhari na Muslim).

Baada ya kupambazuka tutasema*:*

أَصْبَحْنا وَأَصْبَحَ المـلكُ لله وَالحَمدُ لله ، لا إلهَ إلاّ اللّهُ وَحدَهُ لا شَريكَ لهُ، لهُ المُـلكُ ولهُ الحَمْـد، وهُوَ على كلّ شَيءٍ قدير

Aswbahana wa-aswbahal mulku lillah walhamdullillah ,laailaha illa llah wahdahuu laashariikalahuu, lahul mulku walahul hamdu wahuwa alaa kulli shayin qadiir.

"Tumeingia wakati wa asubuhi na umekuwa Ufalme ni wa Allah , na sifa njema ni zake Allah, hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki, ila Allah, hali ya kuwa peke yake, hana mshirika. Ni wake Ufalme, na ni zake sifa njema, na Yeye juu ya kila kitu ni muweza,

Dua kabla ya kujitazama katika kioo:

الْحَمْدُ لِلَّهِ , اللَّهُمَّ كَمَا أَنْتَ حَسَّنْتَ خَلْقِي فَحَسِّنْ خُلُقِي

"Alhamdullillah allahumma kamaa anta hassanta khalqii fahassin khuluqi"

Shukran za dhati anastahiki Mwenyezi Mungu, ewe Mola wangu kama ulivyo nipa umbo zuri, kwa hiyo nijaalie niwe na maadili na tabia njema.

Dua kabla Ya Kuvaa Nguo:

الْحَمْدُ للهِ الّذِي كَسَانِي هَذا (الثّوب) وَرَزَقَنِيهِ مِنْ غَـيْرِ حَولٍ مِنّي وَلا قُوَّة

"Alhamdullillah lladhii kasaaniy haadha thawbii warazaqniy min ghayri hauliy minniy walaa quwwa"

"Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amenivisha nguo hii, na kuniruzuku pasina uwezo kutoka kwangu wala nguvu"

Dua ya kuingia msikitini:

اللّهُـمَّ افْتَـحْ لِي أَبْوابَ رَحْمَتِـكَ

"Allahumma iftahlii abwaaba rahmatika"

Ewe Mwenyezi Mungu nifungulie milango ya rehma zako"

Dua ya kutoka msikitini:

بِسمِ الله وَالصّلاةُ وَالسّلامُ عَلَى رَسولِ الله، اللّهُـمَّ إِنّـي أَسْأَلُكَ مِـنْ فَضْـلِك، اللّهُـمَّ اَعْصِمْنـي مِنَ الشَّيْـطانِ الرَّجـيم

"Bismillahir wasw-swalaatu was-salaamu 'alaa rasuulillaahi, Allaahumma inniy as-aluka min fadh-lika, Allaahumma A'iswimniy, minash-shaytwaanir-rajiimi."

"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu na rehema na amani zimfikie Mtume wa Mwenyezi Mungu, Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba katika fadhila Zako, Ewe Mwenyezi Mungu najilinda kutokana na shetani aliyeepushwa na rehma Zako (aliyelaaniwa)

Dua ya kushukuru baada ya kula:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَطْعَمَنِي هَذَا الطَّعَامَ وَرَزَقَنِيهِ مِنْ غَيْرِ حَوْلٍ مِنِّي وَلَا قُوَّةٍ

"Alhamdulillahi lladhii atwaamana haadha twaama warazaqniy min ghayri haulii minniy walaa quwwa."

"Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye amenilisha chakula hiki bila ya uwezo wala nguvu yoyote kutoka kwangu."

Dua ya kunywa maji

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي سَقَانَا عَذْبًافُرَاتًا بِرَحْمَتِه وَلَمْ يَجعَلْهُ مِلْحًا أُجَاجًا بِذُنُوبِنَا

"Alhamdullillahi lladhii saqana adhbaa furaatan birahmatihi walam yajaallahuu milhan ujaja bidhunuubinaa."

Shukran zote anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye amejaalia maji kuwa matamu kwa rehma zake na sio machungu kwa sababu ya madhambi yetu.

Dua kabla Ya Kuingia Chooni:

(بِسْمِ الله) اللّهُـمَّ إِنِّـي أَعـوذُ بِـكَ مِـنَ الْخُـبْثِ وَالْخَبائِث

"(Bismillah) "Allahumma inni a'uudhubika minal-khubuth wal-khabaaithi"

"(Kwa jina la Mwenyezi Mungu) Ewe Mwenyezi Mungu najilinda kwako kutokana na mashetani wa kiume na wa kike"

Dua ya kutoka chooni:

غُفْـرانَك

"Ghufuraanaka."

"Nakuomba msamaha (Ewe Mwenyezi Mungu)

Dua ya kutoka nyumbani:

بِسْمِ اللهِ ، تَوَكَّلْـتُ عَلى اللهِ وَلا حَوْلَ وَلا قُـوَّةَ إلاّ بِالله

"Bismillahi tawakkal-tu 'alallaahi walaahawla walaaquwwata illaabillaahi"

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu (ninatoka) ninamtegemea Mwenyezi Mungu , na hapana uwezo wala nguvu ila vyote vinatokana na Mwenyezi Mungu

Dua ya kuingia nyumbani:

بِسْـمِ اللهِ وَلَجْنـا، وَبِسْـمِ اللهِ خَـرَجْنـاَ، وَعَلـى رَبِّنـا تَوَكّلْـنـاَ .

Bismillahi walaj-naa, wabismillaah kharaj-naa wa'alaa Rabinaa tawakkal-naa.

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu tunaingia, na kwa jina la Mwenyezi Mungu tunatoka, na Mola wetu tunamtegemea"

ZOEZI LA 23: KUSHUKURU NEEMA ZA MUNGU NA BARAKA ZAKE

Kwa kuzingatia dua hizo maalum, watoto wanatakiwa wafanye maombi yao wenyewe kwa Mwenyezi Mungu wakijadiliana pamoja na wazazi wao

ZOEZI LA 24: KUWEKA MAKOSA KATIKA MTAZAMO

Mpe mtoto mmoja asome hadithi hii ya kweli na muijadili, ongezea uzoefu wako. Shukrani juu ya neema ndogo za Mwenyezi Mungu inapelekea kuridhika,wakati huo huo inatuondoshea hali ya wivu, hasira na huzuni. Hii ndio siri ya furaha na ponyo la wasiwasi.

> Kuna mwanamke mmoja alizongwa na matatizo makubwa. Wazazi wake walitalikiana, alikuwa akimuangalia mama yake mgonjwa, wakati huo huo akiwa katika kazi ya kuajiriwa kamili na alikuwa na matatizo ya kifedha. Hata hivyo mtazamo wake wa maisha ulikuwa wa furaha: "Kama nitaweza kuamka asubuhi na kutembea kwa miguu yangu niko sawa"

Kwa maana nyingine zingatia ulichonacho huku ukijitahidi kutafuta matokeo bora zaidi yatakayokujia katika maisha. Hadithi ifuatayo inaeleza zaidi tabia hii:

Mtume (s.a.w) amesema:

> "Yeyote miongoni mwenu atakayeamka asubuhi na kuwa na afya njema na akawa na chakula cha kumtosha kwa siku, basi mtu huyo ni kana kwamba amekusanyiwa ulimwengu mzima."
>
> (Al Tirmidhī na Ibn Mājah)

ZOEZI LA 25: MAMBO SABA YA KUWAFUNDISHA WATOTO

Mpe mtoto asome hadithi ifuatayo, kisha elezea kila kanuni ukihusisha na maisha halisi.

> "Kuna watu saba (7) ambao Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*) atawafunika katika kivuli chake katika siku ambayo kutakuwa hakuna kivuli isipokuwa kivuli chake Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*)": Kiongozi Muadilifu; Kijana aliyekulia katika kumcha Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*); Muislamu ambaye moyo wake umefungamana katika msikiti; Watu wawili wapendanao kwa ajili ya Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*), Kukutana kwa ajili ya Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*) na kuachana kwa ajili ya Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*); Mwanaume aliyeitwa na mwanamke mrembo kwa kutaka kufanya matendo ya haramu na akasema, "La hakika mimi namuogopa Allah (Subhaanahu Wa Ta'ala)". Mtu anayetoa sadaka kwa mkono wa kulia na wa kushoto usijue kitu kilichotendeka (atoae sadaka kwa siri bila ya wengine kujua kwa ajili ya Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*), na mtu anayemkumbuka Allah (*Subhaanahu wa Ta'ala*) kwa faragha na huku macho yake yakatokwa na machozi."
>
> (Al-Bukhaariy na Muslim)

5

SURA YA TANO

▪KUKABILI MATATIZO NA CHANGAMOTO ZA KILA SIKU

SURA YA TANO **126**

Kukabili Matatizo na Changamoto za Kila Siku **126**

Utangulizi 128
Changamoto kubwa zinazowakabili wazazi 129
Masomo ya malezi kutoka kwa Mussa ndani ya Bibilia 135
Hitimisho 136
Kazi Za Kufanya

Unapaswa kuwafundisha watoto wako kwa bidii na uangalifu.
(Kumbu Torati, 6:7)

Utangulizi

Katika sehemu chache zilizotangulia tumejaribu kueleza sifa za mpango mzuri na mpana wa malezi na tumetaja njia maalumu za kuutekeleza. Pia tumesisitiza umuhimu kwa mtu kutumia utaratibu wa asili wa malezi ukijumuisha mpango kama njia au mwongozo mzuri wa malezi ya watoto. Njia tuliyotumia inanyumbulika kiasi cha kuwaruhusu wazazi kuunda misingi yao na kuwa na machaguo yao ya malezi katika familia zao wakiwa na lengo la jumla la kuwalea watoto watakaokuwa wacha-Mungu, wanaowajibika na wenye utambuzi juu ya jamii.

Vilevile tumesisitiza kwamba kumlea mtoto mzuri kuna athari kubwa hata kama si za moja kwa moja zaidi ya ile hali tu ya utulivu wa akili na maisha ya furaha nyumbani; ambapo ni msingi mkubwa wa ujenzi wa jamii na ustaarabu wake.

Ingawa, mpango mzuri licha ya kuwa kunaifanya kazi ngumu ya malezi kuwa nyepesi, sio kwamba utakamilisha kila kitu vinginevyo, mpango huo uwe unaweza kumuongoza mzazi kukabiliana na changamoto za malezi zitakazomkabili. Katika sura hii, tutajikita kuangazia baadhi ya mambo mazito yanayohusu ulezi, na kutoa baadhi ya suluhisho zenye mantiki.

Kwanza, tutaangalia baadhi ya changamoto kubwa, kisha, katika sura inayofuata, tutaangalia baadhi ya mambo makubwa mazito. Ingawa tulishagusa vipengele vya changamoto hizi kwenye sura za mwanzo, inatarajiwa kuzitazama kwa kina zaidi, ambazo zitawasaidia wazazi kuwa na utambuzi zaidi juu ya ulimwengu ambao watoto pamoja na wazazi wanaishi.

ACHENI KULUMBANA

- ❒ Malezi mazuri ni rahisi ikiwa hujui, lakini ni kazi ngumu ukiifanya (ukijua)
- ❒ Watoto wanasema; Wazazi wetu wanatupelekesha
- ❒ Fahamu matatizo
- ❒ Yachambue na yatatue kwa pamoja
- ❒ Huku ukiwa na subra

Changamoto kubwa zinazowakabili wazazi

Maisha yetu yamepambwa na mtiririko wa mitihani migumu, ambapo ulezi ni miongoni mwa changamoto hizo. Hata hivyo, zawadi ya kufaulu mtihani wa malezi haina gharama yoyote. Inasaidia wazazi kutambua kipimo halisi cha changamoto zinazowakabili ili wasitie chumvi au kudunisha kazi iliyo mbele yao. Ikiwa wanafikiri kulea ni kazi rahisi mno, hawatoona haja ya kujitayarisha kwa ajili ya malezi. Ikiwa wanafikiri ni kazi ngumu sana watakufa moyo na kukata tamaa. Tutajaribu kubainisha changamoto hizo, tukiwa na matumaini kwamba wazazi watapata nafuu na kuridhia na kugundua kwamba kumbe si wao peke yao kwenye mapambano ya malezi.

Inashibisha tafakuri za kujadili changamoto hizi pamoja na wazazi wengine, na wazazi wengi watashangaa jinsi changamoto hizi zinavyofanana kila upande. Hapa tumeonesha baadhi ya mifano ya changamoto nyingi zinazomkabili mzazi.

KUKOSA UZOEFU

Hii ndio changamoto kubwa hasa anapozaliwa mtoto wa kwanza. Hakuna mzazi yeyote kati ya wawili anayejua cha kufanya kwenye mazingira mengi. Hata kama wameshasoma baadhi ya fikra, wazazi hawa watakuwa hawana uzoefu. Kuwauliza wazazi wengine kunaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa; ni kama mafunzo ndani ya kazi bila mwongozaji.

Kulea kwa kusikia, kwa maneno matupu!

Mwongozo wa mtoto ulikuwa jambo rahisi mwanzoni, wakati mama yako alipokuwa anasikia

MISUKUMO YA KILA SIKU

Wazazi mara nyingi huwa kwenye msuguano unaosababishwa na mgawanyo wa majukumu unaotokana na jinsia. Wazazi wengi wa kike hutumia muda wa mchana nyumbani ambapo wazazi wengi wa kiume hufanya kazi nje ya nyumba. Inapofika jioni, akina mama hupendelea kutoka na akina baba hupenda kubaki nyumbani. Jambo hili linaweza kusababisha msuguano ikiwa wazazi hawa hawakuelewana.

Kwa kadri tunavyozeeka, ni lazima tutambue kwamba mtu kuwa baba muhimu si kwa kutoa chakula na makazi kwa watoto pekee.

Kuwa baba si kutoa mahitaji ya vitu pekee

24/7 (SAA 24 KWA WIKI)

Hakuna saa maalumu za kazi ya malezi na ni lazima kukubali pamoja na kuukumbatia ukweli kwamba, kazi ya malezi ni ya masaa ishirini na nne kwa siku saba za wiki, wiki hamsini na mbili kwa mwaka, bila likizo. Hakuna dhana ya *kutaliki* au kuacha watoto. Mara mtu anapokuwa mzazi, jukumu limefanywa kuwa ni la maisha yake yote na hakuna yeyote wa kusimamia jukumu hili.

Jambo gani ni gumu zaidi: Kuwa baba au Rais wa Marekani?

> "Naweza kufanya jaribu moja tu kwenye mawili. Naweza kuwa raisi wa Marekani, au naweza kumsimamia mtoto wangu wa kike Alice. Siwezi kufanya yote mawili kamwe".
>
> Theodore Roosevelt
> Rais wa Marekani (1858-1919)
> (Porter na Cervantes 2007)

> "Neno langu moja tu la amri linatiiwa na watu kwa mamilioni...., lakini siwezi kuwaita watoto wangu watatu tu wa kike kuja kunywa chai kwa wakati"
>
> Ofisa wa Kiingereza Wavell
> (1883-1950)
> (Shaw 1998)

MALEZI NI KAZI ISIYOBADILIKA

Mara tu mtoto anapozaliwa ulezi hauwezi kucheleweshwa, kupangiwa ratiba upya au kutelekezwa. Watoto wana mwenendo wao wa saa za kimaumbile, na mzazi lazima atambue makuzi yao. Wazazi hawawezi kupunguza kasi ya makuzi ya mtoto, au kuzidisha kasi yake. Ikiwa watajaribu kuingilia kati mwendo huo, watakuwa na janga kubwa mikononi mwao. Ni kweli kwamba dunia iko kwenye mwendo wa kasi lakini watoto hawako hivyo. Ni jambo la busara kwenda sambamba, na kasi ya maumbile na siri yake ni kuwa na uvumilivu.

MALEZI NI "UWEKEZAJI" WA MUDA MREFU WA "KUWEKEZA MUDA, NGUVU NA FEDHA"

Malezi ni jambo linaloenda taratibu lenye kuhusisha njia mbalimbali. Linaweza kuchukua miaka kadhaa kabla mzazi hajajua kwamba mtoto wake ni mwema au muovu.

WAZAZI NI MIONGONI MWA TAATHIRA PEKEE KATI YA NYINGI ZILIZOPO KWA WATOTO WAO

Wazazi wanapaswa kuujua ulimwengu ambao watoto wao wanakulia ambao kila siku hubadilika. Kwa mfano, maendeleo ya teknolojia yameleta changamoto kubwa (kupitia mfumo wa TV, mitandao, simu, vyumba vya mtandao vya kujadili, mziki, DVDs na gemu kwenye kompyuta). Filamu na "pop star" nazo zimekua kwa kasi. Ikiwa watapona kujiingiza kwenye moja kati ya hivyo, watoto wamezungukwa na vitu vingi vya kuwapoteza. Wazazi hawana uhuru kamili wa kulea watoto wao na hivyo watambue kuwa wanakabiliana na ushindani kutoka kwa waigizaji kwenye TV, mtandao, pamoja na makundi ya vijana. Watoto wamezungukwa na taathira chanya na hasi. Ingawa wazazi mara nyingi hubweteka – na kulaumu-hasa watoto wao wanapoharibika, lakini watambue kuwa wao ndio wahusika pekee kati ya wengi wanaoathiri makuzi ya mtoto.

Kwa mtazamo wa kijamii, wazazi wenye nia njema na wanaowajibika hawawezi kupunguza ubaya wa mtandao, hawawezi kuangalia kwa jicho finyu mihemko na fujo za makundi ya vijana mitaani na pia hawawezi kuvitazama vyombo vya habari kama vitu vyenye ushenzi kidogo. Ingawa wazazi ndio wa kwanza wenye taathira, umuhimu unaongezeka kuangalia pia athari za makundi kwa kadri watoto wanavyokuwa, na kubakia na maisha yao vivyo hivyo katika maisha yao chuoni. Katika kipindi hiki, watoto huangalia thamani na tabia za marafiki zao. Vijana wa miaka kumi hujiweka na vijana wa sampuli yao na wanaweza kujiweka mbali na wazazi wao.

Ndugu wa baba mmoja mama mmoja huwa na athari muhimu na baadhi ya wakati zenyewe hudumu kwenye makuzi baina yao; ni vioo vya jamii na vigezo (kulingana na umri) kati ya mmoja na mwengine. Pia wanaweza kuwa vyanzo vya ushindani na wivu. Tofauti pia za kimazingira zina athari kwa watoto, kwa mfano, maeneo waliyopo, ukubwa wa familia, tabaka la familia kijamii, dini kuu katika eneo husika na mahusiano ya kikabila.

WATOTO HAWAWEZI KUZUNGUMZA

Vuta picha uone ni vigumu kiasi gani kuwasiliana na wanyama, na baadaye fikiria kwa watoto. Hawaongei kabisa, kiasi kwamba ni vigumu kujua mahitaji yao, hisia zao na fikra zao. Tunapaswa kukisia kwa uhakika. Mtoto si mzee mdogo kama ilivyo kwamba mzee si mtoto mkubwa. Ushauri wetu ni kusoma kwa watoto na kuwasomea Qur'an kwa sababu watoto wanakumbuka maneno kabla hawajaweza kuzungumza.

Mawazo yasiyofikirika!

Nilipokuwa kijana wa miaka kumi na nne, baba yangu alikuwa mjinga sana na ilikuwa ni vigumu kusimama na mzee pembeni yangu. Lakini nilipofikia miaka ishirini na moja (21) nilishangazwa na jinsi alivyosoma vya kutosha kwa miaka

MARK TWAIN

Aha! Aha! Sasa naelewa.....

Watoto hukosa heshima kwa wazazi wao mpaka wanapofikia umri wa miaka arobaini (40), kipindi hichi ghafla huwa kama wao- hivyo hudumisha mfumo.

QUENTIN CREWE,

Mwandishi wa Kimarekani

Fikra za watoto hubadilika

Oh, ilikuwa si mtu kamili bali nusu tu kama mawazo ya mwanangu na nilikuwa hivyo kama mwanangu alivyokuwa mdogo, na nilikuwa nusu kama mwendawazimu katika kipindi cha ujana wangu lakini sasa najihisi nimekamilika.

REBECA RICHARDS (BROWN, 1994)

ULEZI NI JAMBO LINALOHUSISHA TAHASUSI NYINGI

Malezi yanahitaji ujuzi makini (ujuzi ambao wengi kati yetu hatuujui). Malezi yanahusisha tahasusi nyingi, kama vile saikolojia, uongozi na sanaa. Malezi ni sanaa na sayansi kwa wakati mmoja. Kama ulimwengu uliotuzunguka unavyobadilika, na kuendelea kutema cheche za changamoto ngumu zaidi katika mwelekeo wetu, ujuzi wa malezi bora unahitajika zaidi. Kuwa na kiwango kikubwa (kwenye sayansi au sanaa) si lazima kutupa maisha ya furaha na familia zilizoridhika. Mawasiliano yanabakia kuwa jambo muhimu katika malezi bora na thabiti.

BABA NA MAMA LAZIMA WAUNGANE

Umoja si jambo rahisi na ndio changamoto kubwa kwa wazazi. Wanandoa wanapaswa kuungana ili wafanye kazi vizuri kwa pamoja. Mwanandoa uliyechagua si tu mke au mume, lakini pia ni mama au baba mtarajiwa wa baadaye. Wangapi kati yetu tunafikiria jambo hili kabla ya kuingia kwenye ndoa? Kufanya kazi kama kitu kimoja kunahitajika zaidi ya mapenzi na ukweli: kunahitaji taaluma, ujuzi na fikra sahihi.

Ni muhimu wazazi kutocheza mchezo wa kulaumiana wakati mambo yanapoharibika, kila mmoja akamshutumu mwenzake kwa kusababisha tatizo au kutotenda ipasavyo. Mtoto wao wa kike au kiume bado anaendelea kubadilika, na kufaulu katika kipindi cha mpito kutoka utoto kwenda utu-uzima kunahitajika ushirikiano mkubwa baina ya wazazi.

ULEZI NI UJUZI UNAOHITAJI USIMAMIZI MZURI WA RASILIMALI

Ni jambo linalowezekana kumuajiri muhasibu kusimamia fedha za familia, mkufunzi kusimamia elimu, na nesi kusimamia masuala ya afya. Ingawa, jukumu la usimamizi wa familia haliwezi kupewa mtu mwengine, hakuna yeyote anayeweza. Usimamizi wa familia unawataka wazazi kuweka mapenzi, kujali, muda na umakini. Hii ni sehemu isiyoweza kutenganishwa katika malezi, ambayo lazima ifanywe na wazazi wenyewe. Mmoja huangalia tu majaribio ya mfuasi wa Marks katika baraza la Kirusi, ambapo watu wengine si wazazi halisi au ndugu ndani ya familia walijibebesha jukumu la ulezi. Vilevile jambo linalofanana na hilo lilijaribiwa mwanzoni kabisa na watu wenye uvumilivu mkubwa kutoka Ugiriki. Matokeo yake ilikuwa ni kushindwa kwa hali ya juu kwa watoto husika. Usimamizi mzuri wa muda na rasilimali ni jambo muhimu zaidi kwa familia zenye mzazi mmoja, ambazo hupaswa kutengeneza ratiba madhubuti kuliko familia zenye wazazi wawili.

MITAZAMO YA WATOTO KWA WAZAZI WAO INAWEZA KUPISHANA NA MATARAJIO YA WAZAZI WAO

Watoto wanaweza kutafsiri msaada wa wazazi wao kama kero, huruma na mapenzi yao kama utoto, na ushauri wao kwao wakautafsiri kama utawala. Ingawa uhalisia ni jambo muhimu kwa watoto, mtazamo ni jambo halisi. Ndio maana ni muhimu kuwauliza watoto juu ya mitazamo, hisia na maamuzi yao ya kiutendaji. Waulize watoto wako: Jee mmependa nilichowafanyia?

NINI CHA KUMUELEZA MTOTO, NA WAKATI GANI?

Ni umri gani hadithi hii inafaa? Simba, mbwa-mwitu, mbweha waliwinda ng'ombe, mbuzi na sungura. Simba alimuambia mbwa-mwitu: "gawa mawindo". Mbwa-mwitu akasema: "ng'ombe huyu ni kwa ajili yako, mbuzi ni kwa ajili yangu, na sungura ni wa mbweha. Simba akamgeukia mbwa-mwitu na akamuua. Baadaye Simba akageuka kwa mbweha: "utagawaje mawindo?" Mbweha akajibu: "Sungura ni kifungua kinywa chako, mbuzi kwa ajili ya chakula cha mchana, na ng'ombe kwa ajili ya chakula cha usiku". Simba akamuuliza Mbweha "Ulijifunzia wapi hekima hii?" Mbweha akajibu: "Kutoka kwenye kichwa ulichokipasua cha mbwa-mwitu". Wakati hadithi hii inapohadithiwa watoto watajifunza khofu, woga, na unafiki. Ingawa, ikihadithiwa kwa watu wazima, watajifunza jinsi ya kuwa na tahadhari na umakini. Muda ni jambo muhimu sana kuliko kutoa hadithi na kuwapa somo watoto. ■

ELEWA CHA KUWAAMBIA WATOTO NA MUDA WA KUWAAMBIA

Mafundisho ambayo wazee wanayapata kwenye visa mbalimbali si lazima yaendane na mafundisho wanayoyapata watoto. Kwa kuongezea, ni jambo linalovutia zaidi kwa wazazi kuitumia fursa ya usafi na ujinga wa mtoto kuathiri matokeo ambayo yanafanya maisha ya mzazi kuwa mepesi. Kwa mfano, watoto wanapokuwa wanakula makomamanga, baadhi ya wazazi huwaambia watoto wao kula pamoja na mbegu zote bila kubakisha hata moja kwenye nguo au samani (kuepuka usumbufu wa kuondoa baadaye). Badala ya kubaki kwenye uhalisia, na kuhakikisha mashirikiano kamili ya mtoto, baadhi ya wazazi hukimbilia kupamba maelezo. Huwaambia watoto kila komamanga moja lina mbegu maalumu kutoka peponi (ili watoto wale kila mbegu kusudi wasikose zawadi maalumu iliyo na baraka).

Vivyo hivyo, kwenye nyumba nyingi, tembe za mchele husafishwa na kuoshwa. Kuhakikisha hakuna punje iliyopotezwa, wazazi wa kike huwataka watoto wao wa kike wawe makini sana ili wasipoteze punje zozote kwa sababu miongoni mwao ipo maalumu kutoka peponi.

Hizi ni mbinu zenye kufaa na za watoto wenye akili na fikra kubwa zinazotumiwa na wazazi kuokoa muda na pesa kwa ajili yao, vilevile kuwafunza watoto adabu, usafi na kuwajibika. Licha ya hivyo, wazazi wanapaswa kuwa makini sana kuelezea jambo kwa watoto mara tu wanapofikia umri wa upambanuzi, kwa sababu mbinu hizi hazitokuwa chochote kwao zaidi ya hadithi za paukwa pakawa, ambazo hufuta kabisa kwenye akili zao fikra za itikadi yoyote. Mzaha mkubwa zaidi ni ule unaojazwa kwa watoto kwamba Santa Claus, ambaye hujitokeza wakati wa sherehe za Kris-mas, na kuwapa watoto zawadi, ni janga kubwa ikiwa watoto wataamini kwamba Santa Claus ni muhimu zaidi kuliko Mungu.

KUPANDIKIZA FIKRA ZISIZOSAHIHI KWA WATOTO BILA KUJUA

Baadhi ya wazazi waliokuwa na nia njema kwa watoto wao wameelezea matukio yafuatayo:-

Tukio la kwanza: Wakati Saleem alipokataa kuingia chooni alipokuwa chekechea, mwalimu alimuuliza kwanini hataki kuingia. Mtoto alijibu, “wazazi wangu wameniambia kwamba vyoo ni makazi ya majini na mashetani. Nahofia kubaki peke yangu pamoja nao.

Tukio la pili: Mtoto mdogo, Hamid, alichanganyikiwa. Aliwahi kuambiwa kwamba Malaika hawaingii chooni, ambapo pia aliambiwa kuna Malaika wawili ambao humuangalia na kuweka kumbukumbu ya matendo yake yote. Jee Malaika wawili hawa wanaingia chooni pamoja naye? Hakupata jibu!

Baadhi ya wazazi huwapa watoto maelekezo ambayo si sahihi kwa lengo la kuwakataza kula nguruwe. Watoto hujumuisha kwamba nguruwe ni wanyama wabaya wanaopaswa kuchukiwa na kufanyiwa ukatili. Wazazi wanashindwa kuwaeleza watoto kwamba wanyama wote wameumbwa kwa uzuri na Mwenyezi Mungu, lakini baadhi yao tu ndio wazuri kwa kula. Wote wameumbwa kwa lengo zuri, na ni juu yetu kutenda wema kwa wanyama na miti.

Baadhi ya wazazi wenye jitihada kubwa na malengo mema hufikisha ujumbe ambao si sahihi wa kuwachukia watu wote wanaofanya makosa. Hawatofautishi kati ya



tendo ovu na mtendaji. Ambapo, huwachukia wavuta sigara na uvutaji wa sigara. Jambo hili huwafanya watoto kuwachukia watu badala ya kuwapenda na kujaribu kurekebisha makosa yao. Matokeo yake ni kwamba watoto hufikiri wao ni bora zaidi kuliko wengine na hujaa kiburi.

CHANGAMOTO YA KUTENGENEZA TASWIRA BINAFSI AMBAYO NI CHANYA

Watoto (hasa wa kike) wanaweza kuanguka kwa urahisi kwenye mtego wa kumeza ulemavu au tabia ya tamaa kupindukia ya mapambo na nguo hasa kupitia hadithi zilizopambwa mwili mzuri na kutangazwa kwa kutumia fasheni za majarida, majumba ya kutengeneza filamu, na miziki ya kuvutia.

Jambo hili lililokuzwa la muonekano huchagizwa na vyombo vya habari vya biashara ambavyo ujumbe wake ni kwamba "wembamba" ndio uzuri. Kwa watoto, kipindi cha mpito kutoka kipindi cha utoto kisichokuwa na hatia kuelekea maisha ya utu-uzima ya kuiga huchomoza kwenye umri mdogo sana pamoja na vitu vyote vinavyomkosesha ulinzi na kufikia hatua ya kutotambua mfumo kamili unaohitajika. Jambo hili huweka kikwazo kikubwa kwa wazazi wanaotaka watoto wao wafaidi kipindi chao cha utoto.

Umuhimu wa kupandikiza maadili mema, kujiamini na tabia nzuri huwa ni jambo linalohitajika kwa haraka zaidi. Wazazi wanapaswa kuelewa waelewe rushwa na mihemko ya watoto ya kufanya ngono katika umri mdogo (kabla ya ndoa) kwa kusoma dhana ya "matumizi ya vitu" (consumerism) (Williams 2002).

Fikra za watoto juu ya kukidhi mahitaji lazima ziambatanishwe na jamii, mawasiliano na mipaka ya familia na sio kwenye vyanzo vya uongo juu ya kukidhi mahitaji vinavyoongozwa na vyombo vya habari (pamoja na pesa, nguvu na utukufu).

Masomo ya malezi kutoka kwa Mussa ndani ya Bibilia: ambacho alipaswa Mussa kukisema

> Sikiliza, Ewe Myahudi: Bwana ndiye Mungu wetu, bwana ni mmoja. (Kumbukumbu la Torati, 6:4)

Somo 1: Weka vipaombele sahihi! Ni jinsi gani wazazi wanawafunza watoto wao jinsi ya kuweka vipaombele? Haijalishi nini tunajua, ikiwahatujui kinachojalisha. Ikiwa tutamsahau Muumba (Mungu), tunakuwa sawa na watumwa papo hapo.

> Ni wajibu kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, na kwa nguvu zako zote. (Kumbukumbu la Torati, 6:5)

Somo 2: Uhusiano ni jambo muhimu kuliko sheria. Sheria si mbaya, kwa sababu zinabadili tabia za ndani, kuliko kubadili cha ndani kwa mwonekano wa nje. Ingawa mapenzi hubadili moyo na nia ya mtu.

> Na maneno haya nnayokuagiza leo lazima yabaki kwenye moyo wako.
> (Kumbukumbu la Torati, 6:6)

Somo 3: Tafakari kwa undani kuhusu maandiko. Ni jambo muhimu kwa wazazi kutafakari kwa undani maneno haya yatokayo kwa Mungu kabla ya kuyafundisha kwa watoto wao. Maneno haya yanapaswa kuwa sehemu ya maisha ya wazazi kabla ya kuwa sehemu ya maisha ya mtoto. Wazazi hawawezi kutoa wasichokuwa nacho, hivyo wana wajibu wa kuyafanyia kazi wanayoyasema. Kama hayafanyi kazi nyumbani, hawapaswi kuyatoa nje.

> Unapaswa kuwafundisha watoto wako kwa bidii na uangalifu.
> (Kumbukumbu ya Torati, 6:7)

Somo 4: Si kiwango cha muda ndio hoja, lakini kiwango cha muda ghali. Wazazi lazima wakaribishe "fursa za kujifunza" na mipango kwa ajili yao wasipojitokeza wenyewe. Wazazi wanaelekea kuwapa watoto wao kila kitu isipokuwa kitu kimoja wanachokihitaji zaidi: muda. Jamii yetu ni jamii ya kufanya kazi, na si jamii ya kifamilia. Hoja si kwamba hatuipi kipaumbele ratiba yetu, lakini kuratibu vipaumbele vyetu.

> Zungumza nao ukiwepo nyumbani, unapotembea, unapolala, na unapoamka. (Kumbukumbu ya Torati, 6:7)

Somo 5: Lililo muhimu ni vyema kulikumbuka, na muhimu kulirudia.Wazazi lazima wazungumze, watilie mkazo, warudie, na waelezee kwa ufasaha manufaa. Ni muhimu kuwa wazi, kufupisha na rahisi kueleweka. Waoneshe na waeleze: Wazazi wanaweza kuwatambulisha watoto wao kwa ndugu, viongozi, mikusanyiko, mchungaji, maimamu, na wageni, ambao huongeza thamani kwamba wazazi wanafundisha.

Hitimisho

Licha ya changamoto zote, Hata hivyo bado, ulezi ni jambo la furaha, la kiutendaji, na lenye malipo mengi kwa wazazi wote wawili. Changamoto ni nyingi (athari za vijana waovu, ngono kwenye vyombo vya habari, mawasiliano mabaya, na uongozi mbovu). Dhana mbaya, ugumu na uongo ni vitu vilivyoenea (kama tutakavyoona kwenye sura ijayo).

KAZI ZA KUFANYA



KAZI 26: KUZUNGUMZIA FIKRA MUHIMU

Waeleze watoto wako (kwa kuwapa mifano yako) kwenye mambo yafuatayo:

- Si hoja kile unachokijua ikiwa hujui nini ni cha muhimu (vipaombele).
- Si jambo la maana sana kuipa kipaumbele ratiba yetu lakini kuvipanga vipaumbele vyetu.
- Ujaze moyo wako mapenzi kwa Mungu ili uweze kuwapenda wengine. Huwezi kutoa usichokuwa nacho.
- Kwa wazazi: Tekeleza unachokizungumza. Picha ina maana sana kuliko maneno 1000. Mfano mmoja kivitendo una maana mara 1000 kuliko picha.

6

SURA YA SITA

- KUEPUKA IMANI ZA KIBUBUSA NA DHANA POTOFU

SURA YA SITA **138**

Kuepuka Imani za Kibubusa na Dhana Potofu **138**

Utangulizi 140

Kukanusha dhana potofu maarufu na changamoto 141

Baadhi ya Uongo wa Malezi uliofichuliwa 144

Kazi za kufanya

"Thamani ya ndoa si kwamba watu wazima wanazaa watoto lakini ni watoto kuzaa watu wazima".

Utangulizi

Kwenye sura iliyopita tumesisitiza kwamba kumlea mtoto mzuri kuna athari kubwa zaidi ya kuwa tu na amani katika akili ya wazazi na maisha ya furaha ya nyumbani. Ndio nguzo kubwa katika ujenzi wa jamii na ustaarabu. Tumetaja umuhimu wa kuwa na malengo na tukaonesha kwa upana baadhi ya changamoto kubwa ambazo wazazi wanapaswa kuzielewa wakati wanapolea watoto.

Katika sura hii tunajikita kukanusha uongo wa baadhi ya dhana maarufu ambazo zinaficha ukweli na kuonekana kama ushauri mzuri katika malezi thabiti, tunaweka wazi pia matatizo ambayo wazazi hujiingiza, kuonesha namna ya kuziepuka. Pia tunadhihirisha ukweli kuhusu uongo maarufu uliopandikizwa katika fikra za watu. Sababu nyengine ya kuangazia changamoto hizi na uongo huu ni kwamba ni mpango mzuri wa malezi, ingawa huifanya kazi ngumu ya malezi kuwa rahisi, si kamili isipokuwa pale unapoweza kuwaongoza wazazi kushinda baadhi ya vikwazo vikubwa katika malezi.

Kukanusha dhana potofu zilizo maarufu na changamoto

KUTUMIA NJIA ZA KURITHI KIBUBUSA

Wengine kati yetu tulijifunza tabia fulani kutoka kwa wazazi wetu. Tabia hizi si kama zinafaa daima, na baadhi huwa zimepitwa na wakati au kuwa na madhara kabisa. Mama mmoja alisema: "kipindi nilipokuwa mjamzito, nilikuwa kama mama yangu". Baadhi ya wazazi kwa kujigamba kabisa na kwa imani kubwa husema kwa uhakika kwamba wazazi wao walifanya kazi nzuri sana kuwalea. Uzoefu kwa wengi kati yetu ni kwamba tumepata mapenzi na matunzo kutoka kwa wazazi wetu wenye matarajio mema, Allah azirehemu roho zao. Ingawa, si wote waliokuwa na nyenzo, taaluma, au ujuzi uliohitajika katika ujenzi wa malezi.

KUIGA WENGINE KIBUBUSA

Kuiga kibubusa ni njia ambayo si sahihi katika malezi. Kila mtoto ni mahsusi katika baadhi ya mambo ambapo kilicho kizuri kwa mtoto mmoja kinaweza kuwa kibaya kwa wengine. Wazazi wanapaswa watafute njia nzuri zaidi kuwashughulikia watoto wao. Wanaposhauriana na wazazi wengine, wanapaswa watambue mitindo tofauti ya malezi wanayotumia, kwa sababu hutofautiana katika kufaa kwake katika utekelezaji kwenye mazingira yao mahsusi. Baadhi ya wazazi ni wazazi 'ruhsa' au 'shirikishi', ambapo wengine huwa wakali na wanaotumia mabavu.

JAMBO JIPYA LA KUSHANGAZA KWA KILA HATUA NJIANI

"Akina baba wapya wasio na uzoefu hujifunza kwa haraka kwamba kulea watoto ni namna fulani inayotengeneza mtu kukata tamaa".

(BILL COSBY, Muigizaji)

"Malezi si jambo ulilojifunza namna ya kulifanya; ni jambo ulilolifanya wakati mtoto alipofika duniani"

(ELKIND 1995)

KUTUMIA WATOTO KUKIDHI MATAKWA YASIYOWEZEKANA

Hichi ndicho chanzo cha tabia mbaya katika malezi. Wapo wazazi wanaohitaji kukamilisha kupitia malengo ya watoto wao waliyoshindwa kuyapata wenyewe, kuwalazimisha watoto wao kuyatimiza na kuyatambua. Kwa mfano, mzazi aliyekuwa na ndoto ya kuwa daktari au mhandisi lakini akashindwa kuitimiza, anaweza akatumia mabavu kwa mtoto wake ili aingie kwenye udaktari au uhandisi, licha ya kwamba mtoto hana hamu ya kufanya hivyo. Watoto si wapanuzi wa ndoto za wazazi wao. Wanamatakwa na malengo yao yanayojitegemea.

Ni jambo la kufurahisha kwa wazazi kuwaona watoto wao ni muendelezo wa wao wenyewe. Wanajaribu kusahihisha makosa yao kupitia watoto wao, hata

kudiriki kusahihisha makosa yaliyofanywa na wazazi wao nyakati zilizopita. Ikiwa wazazi hawakuwahi kuwa wachezaji wazuri wa 'mpira wa gofu' hutaka watoto wao wawe wachezaji mabingwa wa gofu. Ikiwa wazazi ni dhaifu kwenye hesabu, hutaka watoto wao wafanane na Einstein. Ikiwa wazazi walishindwa kuwa wanasiasa, hutaka watoto wao washinde kila mbio ya siasa. Malezi si awamu ya pili ya utoto, watoto si masanamu ya wazazi wao. Tangu mwanzo, huwa ni watu ambao ni lazima kuheshimiwa jinsi walivyo na wanavyohitaji kuwa.

KUWAKILISHA MAJUKUMU YA MALEZI

Ni jambo linalotokea sana kudhani kwamba malezi yanaweza kufanywa na mama au baba. Kiukweli baba hawezi kuchukua nafasi ya mama, ambapo mama pia hawezi kuchukua nafasi ya baba, kama ilivyo mkono wa kushoto hauwezi kuchukua nafasi ya mkono wa kulia. Kila mzazi ana kazi maalumu na muhimu. Si babu wala bibi, ndugu wengine, wala walezi wa muda, wanaoweza kujitwisha jukumu la ulezi. Wote hawa ni wawakilishi wasiotosheleza kwa wazazi.

KUDHANI UJENZI WA HOJA KIMANTIKI UNATOSHA KWA WATOTO

Uhusiano baina ya wazazi na watoto hautegemei ujenzi wa fikra pekee, kwa tabia na hisia ndio hasa panapopatikana ulingano. Wazazi hawawezi kuwashawishi watoto kula tunda au mboga mboga kwa kusema: "Kula, hili ni zuri kwa ajili yako, linakupa virutubisho muhimu na madini vitakavyokufanya uwe na afya njema na kuwa madhubuti". Ingawa, hoja zinaweza kuwa jambo muhimu, lakini haitoshi.

KUDHANI MTU ANAWEZA KUMSHINDA VITA MTOTO WAKE

Ingawa wazazi wanaweza kushinda baadhi ya mapambano ya hapa na pale, hatimaye watoto wanaweza kushawishika kulipiza kisasi na chuki dhidi yao. Wazazi wanaweza kumzuia kwa nguvu mtoto wao wa kike wa miaka kumi (10) ili asijihusishe na tamaa za mihemko, akifikia umri wa miaka kumi na tatu (13), anaweza akakimbia nyumbani na kupata ujauzito, ambapo hushinda vita ambayo wazazi wake waliianza dhidi yake. Mtoto wao wa kiume anaweza akaiba gari na kusababisha ajali mbaya sana. Wazazi huwa na njia moja tu mbadala: kuwashinda watoto wao kuwaleta upande wao. Linafanyikaje hili?

Kwa kuwasikiliza, kujadili, kuwapenda, kubishana nao kwa hoja na kuwaelewa. Ni kazi ya uangalifu mkubwa, inayohitaji uvumilivu na mawasiliano mazuri.

WAZAZI KUTEGEMEA HOJA KWAMBA WAO NI WAKUBWA NA WENYE MAMLAKA

Watoto wanajua kwamba mwishoni nao watakuwa madhubuti. Ikiwa wazazi watatumia nguvu zao kuwatisha na kuwaonea watoto wao; kuwafanya wawaogope, baadaye watoto watatumia mbinu hizo hizo za kitabia wakifika uzeeni. Ikiwa wazazi watawafanya watoto wajihisi kwamba wote wako upande mmoja, baadaye watoto watakuwa na mahusiano mazuri na wengine. Watatambua kuwa nguvu za wazazi wao zimeongeza nguvu zao. Wazazi wanaowalazimisha watoto wao hawatambui kwamba ikiwa wangalijizoesha kuwapenda na kuwashawishi badala ya kutumia nguvu, wangalipata matokeo sawa, na pengine yakawa mazuri zaidi. Ikiwa mapenzi au matumizi ya nguvu yanaweza kutupa matokeo sawa, kwanini basi tung'ang'anie matumizi ya nguvu?

WAHUDUMIE TU KAMA WANA WA KIUME NA WA KIKE

"Hulei mashujaa,
unalea watoto. Na kama
utawahudumia kama watoto,
watageuka kuwa mashujaa,
hata kama bado uko hai"

(SCHIRRA, 2001)

WAZAZI WANADHANI WANAWEZA KUWAHUDUMIA WATOTO WAO KWA NAMNA ILIYO SAWA

Wazazi wanaweza kudhani kwamba watoto wao wote wanafanana. Hivi sivyo ilivyo. Watoto kwenye familia ni sawa na shada la maua; daima mpangaji anaweza kuamua lipi liwe na muelekeo tofauti kulingana na matakwa yake. Watoto wanatofautiana katika uwezo wa kuvumilia shida, uwezo wao wa kujifunza, uwezo wao wa kujiamini katika mazingira ya kijamii, pamoja na mambo wanayoyapenda. Wazazi hujua kwa haraka upekee wa kila mtoto – tofauti za kila mtoto mmoja na mwengine kwamba wanajua kutoka kwa watoto ambao wamewasoma. Inashangaza jinsi watoto wanavyoweza kuwa tofauti. Baadhi ya tofauti zinaweza kuwa ni kwa sababu ya jinsia na majukumu ya kijinsia katika jamii.

KUMUHUDUMIA MTOTO KAMA MZEE MDOGO

Wazazi wanafikiri kimakosa kwamba mtoto anatakiwa kushughulikiwa kama mzee mdogo. Al-Jarajrah (1988), katika kitabu chake kilichoandikwa kwa Kiarabua-naelezea kwamba mtoto si kitu kidogo kama mtu mdogo, kama wanavyoamini Wagiriki na Waroma. Anasema kwamba katika kipindi muhimu zaidi cha maisha yetu ni kipindi cha utoto. Kwa uhalisia, wazazi wanapaswa kuelewa saikolojia ya mtoto, ambayo si rahisi. Ni rahisi kuelewa mahitaji ya kimwili ya mtoto (kwa mfano, ikiwa mtoto ana njaa unamlisha, akichoka unampumzisha). Mahitaji ya kisaikolojia ya mtoto ni ngumu kuyaelewa. Ni vigumu zaidi kwa watu wazima kuelewa saikolojia yao ya kiutu-uzima, hata kama watajijua wenyewe zaidi kuliko watu wengine.

KUWANUNULIA WATOTO KILA WANACHOKIHITAJI

Wazazi wasikimbilie kuwanunulia watoto wao kila wanachohitaji; hawapaswi kujiingiza kwenye kila shida ya mtoto. Wazazi hawapo kusubiri mkono na mguu wa mtoto wao isipokuwa kuwafunza, kuwapa majukumu, na kuwasaidia kuelewa kwamba maisha ni kutoa na kupokea. Tatizo hili mara nyingi hutokea bila kugundua mpaka wazazi wanajenga mazoea ya kumnunulia vitu mtoto na kabla ya kutambua kinachotokea, hujikuta wakijiingiza kwenye mahitaji yasiyo ya lazima ya nguo, CDs, DVDs na vitu vya kuchezea kwa mtoto ambaye ameshakuwa mkubwa.

WATOTO HUWAFUNZA WAZEE WAO

"Thamani ya ndoa si kwamba watu wazima wanazaa watoto lakini ni watoto kuzaa watu wazima".

(Peter Devries, Coloroso 2002)

Baadhi ya Uongo wa Malezi uliofichuliwa

Kulea watoto kunahitaji kuwepo na mvuto wa kutosha kuwavutia idadi ya kutosha ya wanandoa ili wajiingize kikamilifu kwenye jukumu la wazazi, kwa sababu jamii haiwezi kuendelea bila ya kuwepo wanajamii wapya. Baadhi ya wazazi wanaweza kuamini kwamba kulea mtoto ni mchezo mtupu, kwamba wazazi wazuri watatoa watoto wazuri, kwamba mapenzi na uwezo wa fikra vinatosha kupelekea malezi yaliyofanikiwa, kwamba watoto watapenda jinsi wazazi wanavyojitoa muhanga kwa ajili yao, kwamba malezi ni jambo linalokuja tu lenyewe, na kwamba maadili ya familia ni rahisi kuyadumisha. Imani hizi haziakisi uhalisia wa malezi. Chini tumefupisha na kufafanau baadhi ya imani za uongo za malezi zinazotapakaa sana ambazo hazitetewi na ukweli.

Uongo 1: Kulea watoto siku zote ni jambo la mchezo. Wazazi wa baadaye wanaona katika matangazo ya kibiashara wazazi wadogo wakiwa na watoto sehemu za kupumzikia, na wanadhani kwamba namna hiyo ndio njia ya kulea watoto: mchezo usio na mwisho. Ukweli uko tofauti na hivyo. Wazo la kudhani mchezo linamaanisha kwamba mtu anaweza akafanya au akaacha, ambapo wazazi wanalazimika kukaa na watoto na kuendelea kuwahudumia, ikiwa wanapenda au laa! Mara tu wakishaanza, hawawezi kusimama hata kama watahisi hivyo.

Uongo 2: Wazazi wazuri kwa vyovyote viwavyo lazima watoe watoto wazuri. Watu wengi wanadhani kwamba watoto wanaobadilika na kuwa "wabaya" (watumiaji dawa za kulevya, wezi, wahuni, matapeli) wana wazazi ambao hawakufanya kazi nzuri. Tunatupa lawama zote kwa wazazi watoto wanaposhindwa. Ingawa, wazazi wengi wazuri ambao wamejitahidi kufanya vizuri kwa kadri ya uwezo wao wanaweza kuwa na watoto wabaya (kwa mfano fikiria kuhusu mtoto wa Mtume Nuhu alaihi salaam). Kinyume chake, inawezakana mzazi muovu kuwa na mtoto mwema (kwa mfano, fikiria kuhusu kesi za nabii Mussa (A.S), ambaye alilelewa katika nyumba ya Fir-aun, na Ibrahim (A.S), ambaye baba yake alikuwa dhidi yake).

ULEZI UNAKATISHA TAMAA, BAADHI YA WAKATI

Kuna baadhi ya wakati ulezi unaonekana kama vile kujaza kinywa ambacho kitakutafuna.

Uongo wa 3: Watoto ni watu wa kupendezeshwa. Wazazi wengi wanafikiri kuwa ikiwa watawapa watoto vyote wanavyohitaji, watoto watatambua jinsi wazazi wao wanavyojitoa muhanga. Jambo hili sivyo lilivyo siku zote. Wazazi wanaowapa watoto wao mapenzi, huduma, na malezi si kwamba watapendwa na watoto wao. Baadhi ya wazazi hudhani kwamba watoto wao watawapenda ikiwa watawapa mahitaji ya vitu (kama vile nguo, vitu vya kuchezea, kompyuta na gari). Dhana hiyo mara nyingi huwa si sahihi. Baadhi ya watoto hufikiri kwamba ni haki yao kwa chochote watakachopewa na wazazi wao, na hawahisi kuwa na wajibu wa kufurahia walichofanyiwa na wazazi wao.

Uongo 4:Ulezi huja kama jambo la asili. Baadhi ya watu wanaamini kwamba hakuna haja ya mfumo rasmi wa kujifunza malezi. Katika nchi nyingi kuna masomo ya udereva kuliko masomo ya malezi. Zipo tofauti za wazi kabisa kati ya mwanafunzi na mama wajuzi. Mama wanaojifunza kulea, wana uwezo mdogo kuelewa malengo na mahitaji ya watoto wao, na hawajui watarajie tabia gani kutoka kwa watoto wao wanapokuwa wakubwa. Mama wanaojua kulea, kwa upande mwingine, wanaelewa vizuri jinsi watoto wanavyofikiri na tabia zao. Bila ya mafunzo, watu wanaweza kurudia makosa ya wazazi wao.

Mwanadamu hutaka, lakini Mwenyezi Mungu hujaalia

Unaweza ukapanga vizuri kwa mwana wako wa kwanza, lakini linapofika kila kitu kisichopangwa hutokea.

Uongo 5: Hadhi za familia ni rahisi kuzifundisha. Kwa watu wengi hadhi za familia humaanisha yafuatayo:

- Heshima kwa wakubwa na watu wengine
- Kukubali tofauti baina ya watu
- Uwezo wa kujadili tofauti kwa utulivu na kutafuta njia ya pamoja kuzitatua
- Kujikita na jambo zuri, hata kama ni gumu kulifanya
- Kutengeneza na kuendeleza utekelezaji
- Kulinda hadhi ya mtu muda wote
- Kuwasaidia wengine na kuihudumia jamii

Kwa kweli, mambo yote yaliyoorodheshwa juu na mengine mengi hayawezi kufundishwa kwa urahisi.

Uongo 6:Bishara, ujuzi, uwezo wa hisia, na mapenzi yanatosha. Wazazi wanahitaji elimu na ujuzi vile vile. Ulezi ni jukumu lisilo na mwisho linaloundwa na matukio mengi madogo madogo, mizozo ya kipindi, na changamoto za ghafla, ambayo yanahitaji majibu ya muda tu. Majibu yanaleta athari, ambapo kila jibu huathiri utu wa mtoto, kwa namna njema au mbaya. Kukabiliana na mahitaji ya mtoto kwa uzuri ni ujuzi ambao lazima usomwe.

Tabia ya mtoto hubadilishwa na uzoefu unaotokana na watu tofauti na mazingira. Tabia fulani haiwezi kufunzwa kwa bahati nasibu. Hakuna mtu anayeweza kumfunza mtu uaminifu kwa mihadhara, ujasiri kwa njia ya posta, uanaume au uanauke kwa kuhamishiwa vimelea. Ujenzi wa tabia unahitaji taaluma ya saikolojia ya mtoto na hatua za makuzi ya mtoto. Wazazi hupenda watoto wao wawe na huruma, uwajibikaji, na ujasiri. Kufanya hivi, wazazi wanapaswa kujifunza njia sahihi kuweza kutafsiri ndoto walizonazo na kuziweka kwenye mafanikio.

Wazimu na Busara!

"Wazimu ni jambo la kurithi; unalolipata kutoka kwa watoto wako".

Sam Levenson **(Brown 1994)**

"Ufundi wa kuwa mwenye busara, ni ufundi wa kujua lipi ulipuuzie".

William James
(Lazear 1993)

UZOEFU WA KWANZA

Ulezi unaweza kusomwa kwa uzoefu wa mwanzo, lakini uzoefu ni mwalimu mgumu: anakupa ladha kwanza, na kukupa somo baadaye. Jaribu kusoma dua ifauatayo:

"Ewe Mwenyezi Mungu, usinifanye kujifunza kila kitu mwenyewe kupitia uzoefu wa mwanzo"

Uongo wa 7: Ufahamu mbaya juu ya kujitoa muhanga. Baadhi ya wazazi wanaamini (wakiwa na hisia nzuri) kwamba wanapaswa kujitesa kwa ajili ya watoto wao. Zaidi ya hapo hudhani kwamba dini inawataka wafanye hilo tu. Ukweli ni kwamba utajiri na watoto vinapaswa kuonekana kama furaha na mapambo kwa wazazi, na si mfumo wa mateso na maumivu.

> Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini. (Qur'an 18:46)

Wazazi, hasa akina mama, hawapaswi kutoa muhanga kiasi cha mwisho kwa ajili ya watoto wao, wakijifanya kama watumwa wa mahitaji ya watoto. Akina mama lazima wasaidiwe na wahudumiwe vile vile. Wanapaswa kujihudumia wenyewe kwanza, kisha watoto wao.



Uongo 8: Jukumu kubwa la mzazi ni ule uhusiano wake na watoto. Kinyume chake, jukumu la kwanza ni kujihudumia mwenyewe, na si uhusiano na wengine.

> Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye, na mamaye na babaye, na mkewe na wanawe, kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na lake la kumtosha. (Qur'an 80:34-37)

Weka uwiano baina yako, watoto wako, na muumba wako. Mtume (S.A.W) amesema:

> *Mke wako ana haki kwako, mwili wako una haki kwako, Muumba wako ana haki kwako, kwa hivyo kila mmoja mpe haki yake.*
>
> (Al-Bukhar)

Hili linajumuisha wazazi kujihudumia kiafya, kifuraha, kimatamanio ya kisheria, urafiki na likizo.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI 27: UZOEFU WA MTU KWENYE MAMBO MAZITO

Kupitia uzoefu wako kama mzazi, unaweza kuhusisha kwanini ulezi ni mgumu na vipi? Fanya hili kwenye kikao cha familia pamoja na watoto wako. Linaweza kufungua macho yao kuelekea utambuzi wa dhati wa ugumu wa maisha halisi.

ZOEZI 28: MJADALA WA FIKRA ZA MALEZI

Elezea aya hizi kwenye mazingira ya familia, pamoja na watu wote wakiwepo, baadaye jadili mawazo yako, kwa kutoa taarifa za kina juu ya ugumu na furaha ya kulea watoto. Toa baadhi ya hadithi halisi za watu unaowajua!

Baba mmoja alisema: "Watoto wameumbwa kuja kuwaadhibu wazazi wao," ambapo Qur'an inasema:

> Mali na watoto ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.
>
> (Qur'an 18:46)

> Enyi mlio amini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao. Na mkisamehe, na mkapuuza, na mkaghufiria basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu.
>
> (Qur'an 64:14)

> Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.
>
> (Qur'an 64:15)

7

SURA YA SABA

- MAMBO YANAPOENDA KOMBO

SURA YA SABA **150**

Mambo Yanapoenda Kombo **150**

Utangulizi 152
Hasira, Ukaidi, Hamaki na Kulia 153
Uonevu: Mtoto wako na Wewe 155
Ikiwa mtoto wako ameonewa, nini kifuate? 155
Vijana: Uchambuzi kuhusu Dhana ya Baleghe 156
Hasira kwa Vijana wetu na Sisi Wenyewe 158
Tufanye nini kwa kijana wetu na sisi wenyewe? 160
Kanuni chache za mawasiliano mazuri 160
Kazi za kufanya

Tunawalaumu wengine "kwa kuzungumza sana", lakini je, imeshawahi kutokea tukawalaumu kwa "kusikiliza sana?" Kusikiliza ni kujali.

Utangulizi

Hakuna uhakika wa mafanikio kwa mahusiano yoyote na hii inajumuisha yale mahusiano ya mzazi na mtoto. Ulipomuangalia kwa kuridhika mtoto wako mzuri ambaye ndi kwanza amezaliwa, bila shaka ulijawa na matumaini na matarajio mema. Uliomba sana dua mara kadhaa itokee uwe na mtoto wako, na ulitarajia mapenzi, utiifu na heshima na binafsi uliwaza: "Ni mahusiano mema gani nitakayokuwa nayo!"

Miaka kumi na tano baadaye, binafsi utawaza tena: "Jambo gani katika ulimwengu halikuenda sawa?" Ulifanya kila kitu ulichotakiwa kufanya, ulifanya kwa uzuri kwa kadri ulivyoweza, na ulijitahidi kwa kiwango cha juu mno kumkuza mtoto kwa mapenzi, adabu na imani. Lakini imekuwaje kiasi kwamba mtoto amegeuka na kuwa mzimu kwa herufi kubwa M?

Mzazi mmoja alishtushwa kugundua kuwa mtoto wake mwenye uwezo mkubwa kiakili (mwerevu) ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa kiwango cha ufaulu cha daraja A tena mwenye afya njema lakini ana tatizo la mihemko. Alikuwa hajakuwa kisaikolojia.

Baadhi ya wazazi wanaweza kushindwa kugundua kwamba mtoto wao ana tatizo la mihemko, hasa akiwa anafanya vizuri shuleni na yuko sawa kiakili na kimwili. Kwa kweli, anaweza akawa anafaulu sana darasani, lakini akakosa uwezo wa kihisia. Dalili au mapendekezo kwa wazazi yanaweza kutoka kwa walimu, marafiki au ndugu, na lazima yazingatiwe kwa dhati na wazazi, ambao watataka kuchukua hatua za kumrekebisha.

Sura hii inachunguza kitu gani kinaweza kufanywa mambo yanapoenda kombo. Ni vizuri kujikita kuangalia namna ya kuzikabili changamoto kuliko kuzama

Mama mmoja anasema: "Tunaishi pembezoni mwa mji, watoto wetu walikwenda shule nzuri, na tulitumia muda mwingi pamoja nao kama familia: kuwaweka kwenye kambi, kuwapeleka kwenye michezo ya mabarafu, na kuogelea. Mtoto wetu sasa yuko jela, na alipigwa risasi mguuni. Tumeshaacha kujiuliza maswali tulikosea wapi. Ana miaka ishriri na tatu, na alijiunga na mkondo wa urafiki wa vijana ambao waliamua wangaliiba usiku moja". ■

kwenye mambo yaliyopita au kujiuliza wapi tumeshindwa kama wazazi. Sura hii inaangazia mambo yanayohusu hasira, hamaki, ubabe pamoja na tabia mbaya zinazoambatana na ujana. Vile vile inaangazia mawasiliano ya wazi kama nyenzo muhimu katika kutatua changamoto zinazotukabili. Hakuna tatizo, hata liwe kubwa kiasi gani, ambalo haliwezi kutatuliwa.

Wakati mambo yanapokwenda kombo hasa, kiasi cha kutokuelezeka, hali haipaswi kuonekana kama sehemu ya kushindwa kwa upande wa wazazi. Si lazima liwe ni kosa lako au la makusudi litokalo upande wako. Mtoto wako wa kiume au wa kike anapata mabadiliko kila siku, na kipindi cha mpito kutoka utoto kuelekea uzee husababisha misuguano. Hupaswi kujilaumu au kumlaumu mke wako. Wazazi hawahitajiki kuchoshwa na mazito yote yanayojumuisha kazi ya ulezi. Vikwazo vinaweza kutatuliwa kwa ulezi mzuri, na inaweza kuwa na kuendelea kuwa zawadi ya uzoefu. Matarajio na dua za mtu, sambamba na kutafuta elimu, ujuzi na mwongozo kutoka kwa wazazi wengine, ndio msingi wa uhakika wa mafanikio.

Hasira, Ukaidi, Hamaki na Kulia

Watoto wanajifunza na kukua muda wote na moja katika mambo ambayo watayajaribu ni udhibiti wa nguvu za wazazi. Hili linaweza kuwa ni vita vya matakwa. Hakuna kiwango chochote cha hotuba kitakachofanywa na wazazi kitakachosimamisha watoto kutotii, ambapo anaweza kulia kupita kiasi na kuharibu nyumba nzima ikiwa watakuwa na namna yao ya kuishi; au wanaweza kulia kupita kiasi bila ya kunyamaza mpaka wasikilizwe wanachotaka. Wazazi wanaweza kufikishwa hatua ya kulia, na wanaweza kufikiri jambo rahisi ni kujisalimisha [kwenye matakwa ya watoto]. Hili ni jambo la makosa kulifanya, kwa kufanya hivyo kwa muda mrefu baadaye, itakuwa inashajihisha wazo la kutaka wasikilizwe litafanya kazi siku zote. Kuwakaripia, kuwapiga na kuwatenza nguvu watoto vile vile haitotatua tatizo. Suluhisho ni kutumia akili ya kuwatia adabu ambayo itawafunza watoto kuheshimu sheria zako na kubaki kwenye udhibiti wa mkono wako.

NJIA CHACHE ZA KUMTIA ADABU MTOTO MTUNDU

Kumtia adabu kunakuza tabia na kuadhibu kunakomesha tabia

- Zungumza kwa kutumia sauti ya kawaida, ukisisitiza athari za tabia mbaya. Mwelekeo wa mtoto uwe juu ya kumuelewesha athari za kutokuwa mtiifu. Kama njia hii haikufanya kazi, basi jikite kwenye sauti na matumizi ya kumkazia macho. Hii ni hatua ya awali kabla hujachukua hatua yoyote. Tumia sauti madhubuti, sauti tulivu na usipige mayowe.

- Mfanye mtoto ajue kwamba uko makini na angalia moja kwa moja kwenye macho yake. Mkumbushe kila baada ya muda mfupi kwa ufasaha na taratibu. Ikiwa hasikilizi, msogelee uwe karibu yake, endelea na sauti na yakite macho yako kwake. Rudia kwa utulivu mara nyingine.

- Ikiwa njia hii haifanyi kazi, tumia kanuni kuelezea athari yake. Mpe mtoto idadi ya matatizo yatakayotokea kama hatosikiliza. Athari lazima zifuatiwe na azma ya kukuza heshima, vinginevyo watoto hawatoweka umakini kwako unapowaonya. Ikiwa watakuwa wanapiga fujo, manung'uniko, kuonesha hasira, wewe pia usijaribu kufanya hivyo. Mfahamishe mtoto kwa njia ya taratibu kuhusu athari na hakikisha kwamba anaelewa jinsi gani anatakiwa kutii. Mpe muda wa kujiridhisha, na usijaribu kutaka mabadiliko ya papo kwa hapo. Mara tu hili likitokea, achana nalo.

- Zipo "athari" kadhaa ambazo wazazi wanaweza kuzitumia. Wachunguze watoto wako, tafiti jambo gani wanalipenda na kitu gani kina maana sana kwao, na zuia, jambo hili kwa muda hivi. Inaweza kuwa anapenda vitu vya kuchezea au ziara sehemu fulani. Mara tu mtoto akijuta na/au akitulia, mpe zawadi kwa kuwa mtu mzuri. Unaweza kufuatisha athari moja na nyengine kutilia nguvu nukta ikiwa mtoto anaendelea na tabia mbaya.

- Buni "eneo la utukutu" ambapo lazima atakaa wakati unaendelea na kazi yako bila ya wasiwasi mpaka mtoto aombe radhi. Msamehe papo hapo na kisha sahau kuhusu tukio zima ili urudi katika hali ya kawaida. Lengo la "eneo" hili kwa jina lolote utakalochagua kuliita, ni kwamba linaleta uangalifu na kuhisi amekosa hadhi ya kuwa na wengine. Mara hii si kwa ajili ya mazungumzo, mtoto anataka aachwe pekee. Eneo utakalochagua lazima liwe linachosha au sehemu tulivu, na isiwe ni chumba cha mtoto anacholalia. Ikiwa atapelekwa eneo hili, weka kiwango cha muda ambacho lazima akae. Iwapo atajaribu kuzungumza katika namna ya kujitetea au kwa hasira, puuzia hali hii.

- Wape zawadi watoto wanapokuwa na maadili mema. Usiwahonge ili wawe na tabia njema au wakati wanapokuwa na jazba. Kitendo hiki hakifai ambapo watoto hawajifunzi chochote cha maana.

Uonevu: Mtoto wako na Wewe

Uonevu unaweza kumuathiri mtoto wa yeyote na kugundua dalili zake mapema kunaweza kuepusha maumivu mengi kwa mtoto na msongo wa mawazo. Uonevu unatokea wakati mtoto wako anapotukanwa, kubughudhiwa, au kushambuliwa. Wazee wanatakiwa wawe hadhiri sana kwa sababu watoto wengi wanaogopa kuwaambia wazazi wao wanapoonewa. Uonevu mtandaoni (http://www.bullying.co.uk) ni tovuti inayoshughulika na kukabiliana na uonevu. Unaeleza, "takriban watoto 16 wanajiua wenyewe kila mwaka ndani ya UK kwa sababu ya matatizo ya kisaikolojia yatokanayo na uonevu. Shule zao mara nyingi zinasema hazikujua chochote kinachoendelea. Lakini wanaoonea wenzao wanajua fika kinachoendelea – na hata marafiki zao. Inakuwa tumeshachelewa sana kuwa na masikitiko wakati mtu ameshakufa, au amesababishiwa ugonjwa unaohitaji matibabu [ya hospitalini].

Tovuti inayohusu uonevu mitandaoni inaorodhesha baadhi ya ishara zinazoonesha mtoto wako ameonewa

- Kuchana nguo
- 'Kupoteza' pesa
- Kuachana na marafiki wazuri wa zamani
- Kutojielewa na jazba mbaya
- Kuwa kimya na kujitenga
- Kuhitaji kubaki nyumbani siku zote
- Kuwa mbabe kwa kaka na dada zake
- Kufanya vibaya shuleni
- Kulala kwa mashaka
- Kuchanganyikiwa
- Kuja nyumbani na majeraha na vidonda
- Kutaka vitu vilivyoibiwa kurejeshwa

Ikiwa mtoto wako ameonewa, nini kifuate?

Watoto wengi hawataki mazungumzo kuhusu kuonewa. Namna wazazi wanavyolibeba jambo hili inaweza kuwa muhimu, ambapo sio kuchukua hatua zaidi au kutaka majibu ya kina kutoka kwa mtoto wako ndio msingi. Kuuliza maswali kama vile "Ilikuwaje shule leo?" inaweza kusaidia kuchimbua taarifa muhimu. Ingawa, watoto wengi hawatopenda kuzungumzia siku yao ilivyokuwa shuleni na huyaona maswali kama mtego. Kutambua tabia ambayo si ya kawaida ni jambo la muhimu.

Watoto wanahitaji wajihisi raha sana na huru kiasi cha kuzungumza na wazazi wao kuhusu vitu kama uonevu, au vitu vinavyowakosesha furaha katika maisha yao. Mawasiliano ya wazi ni muhimu kuwekwa tangu miaka ya mapema utotoni. Kuwa na mawasiliano huru ya aina hiyo na mtoto wako kutawawezesha kuwa wazi kuhusu wanayoogopa na kuhisi kwamba wanaweza kukukabili kuhusu matatizo yao, ukaokoa muda mwingi na nguvu. Kumlazimisha mtoto wako akuambie "kuna tatizo gani" haitosaidia chochote ikiwa mtoto wako hajihisi amani kujadili mambo haya na wewe.

HATUA KADHAA ZINAZOWEZA KUTUMIWA KUUDHIBITI UONEVU

- Shule nyingi zina sera zinazopinga uonevu. Kuwa karibu na shule anayosoma mtoto wako ambayo hii ni hatua ya awali. Kupanga kuonana na mwalimu wa mtoto wako ni hatua nyengine.
- Usimfunze mtoto kulipiza kisasi, kwa sababu haitokuwa suluhisho na hatimaye itasababisha tatizo zaidi. Kumpiga mwanafunzi mwengine haitarajiwi kuwa mwisho wa tatizo, na inaweza kusababisha mtoto wako kusimamishwa masomo au kufukuzwa.
- Kuwa mtulivu kama mzazi, na wala usikasirike au kukimbilia kuwasiliana na wazazi wa mtoto anayemuonea mwanao. Ingawa, kwa kawaida hii huwa njia ya kwanza kwa mzazi, [lakini] baadhi ya wakati huyafanya mambo kuwa mabaya zaidi. Ni vizuri kwa viongozi wa shule kuwasiliana na wazazi wa mtoto aliyemuonea mwenzake.
- Kuwa na ratiba maalumu ya kuzungumza na mtoto wako na shule kuona kwamba uonevu umeisha. Kama bado, wasiliana na mamlaka ya shule kwa mara nyengine.
- Msaidie mwanao awe jasiri dhidi ya uonevu kwa kujenga uwezo wake wa kujiamini. Mazoezi ya ngumi na mafundisho ya kujihami yanaweza kukuza jambo hili.
- Mfundishe mwanao mikakati ya usalama. Mfundishe jinsi ya kuomba msaada kutoka kwa mtu mzima anapohisi anataka kuonewa. Zungumzia kuhusu yupi anafaa kuombwa msaada na vipi azungumze. Muhakikishie mwanao kwamba kumtolea taarifa mtu muovu si jambo la kujihisi mkosa.
- Waombe walimu watafute vitu vya watoto vya kufanya wakati wa mapumziko na muda wa chakula cha mchana kwenye mazingira salama.
- Tembelea mitandao kama vile (http://www.stopbullyingnow.hrsa.gov) na jifunze jinsi gani wazazi wengine walivyoweza kwenda sambamba na mbinu walizotumia. ■

Vijana: Uchambuzi kuhusu Dhana ya Baleghe

Pengine miaka ya baleghe inaweza kuwa ni ngazi yenye changamoto nyingi zaidi ya malezi ya watoto. Dkt. Imad al-Dean Ahmed anasema kwamba kwenye mazingira yenye uhuru, watoto baleghe wanaweza kuwa viongozi. Ubaleghe unaelezwa kwamba ni “kipindi baina ya kupevuka na utu-uzima”. Ingawa katika jamii za mwanzoni, ujana ulizingatiwa kama mwanzo wa utu-uzima. Dini zote zilizoshushwa zimeelezea ukweli huu kwenye kanuni na sheria zao. Katika dini ya Kiyahudi, kijana katika Baa ya Mitzvah alitangaza “leo mimi ni mtu”. Katika Uislamu, binti anakuwa mwanamke akianza tu kuingia katika hedhi na swala za faradhi kwake ni lazima akishafikia baleghe. Miaka ya baleghe ni muda ambao watu wadogo wanahitaji kupewa majukumu ya watu wazima ili kuwawezesha kufikia makuzi kamili.

Kwa ulimwengu wetu wa leo, mfumo rasmi wa shule kwa wote umebadili mfumo wa malezi wa jamii zilizotangulia. Ili kuwasukuma watu kwa ujumla kuwaingiza katika mfumo rasmi wa elimu, imekuwa ni muhimu kupinga uwezekano wa kuwa kama watu wazima. Hata nafasi za usaidizi haziruhusiwi maeneo mengi mpaka amalize mfumo rasmi wa shule, ujulikanao kama "shule ya kiwango cha juu (miaka 17-18) au chuoni (miaka 19-22)". Kuwalazimisha watoto waingie kwenye mfumo wa shule ambao unafanya kazi kama mfumo wa zamani wa malezi (badala ya wazazi) umepata mwonekano wa 'igizo' na kwamba vijana baleghe wanaonekana ni watoto badala ya kuwatazama kama watu wazima ambao hawajapevuka vyakutosha.

Zaidi imesisitizwa kwenye sharia, wala si kwa bahati tu, ni kujidanganya kwamba watoto wote wanakuwa wakifikia umri wa miaka 18 au 21. Kwa kweli, watoto wanakuwa vya kutosha kimwili wakifikia umri wa miaka 19, licha ya kutangulia kukua kiakili ambapo kihisia, watu wanakuwa kwa umri tofauti tofauti (na baadhi yao hawaonekani kukua kabisa).

Zamani, kuwachukulia vijana baleghe kama watu wazima ilichochea kukuza akili zao na uwezo wa kiuongozi na kupelekea ukuaji wa hisia. Mfumo wa sasa kuwachukulia vijana baleghe kama watoto, kunachochea utegemezi na udhalilishaji wa dhana ya kujitambua. Katika jamii za zamani, vijana wa miaka 15 walishiriki kufundisha, kwenye biashara, shughuli za kijamii, vita, na kuoa au kuolewa. Katika jamii ya leo, vijana baleghe wanaonekana kama watoto wadogo. Wanaopaswa hasa kusubiri ufadhili wa masomo mpaka waingie chuoni, kama hawatomaliza shule.

Kuchelewa huku kuwapa vijana baleghe majukumu ya watu wazima, kumezusha gharama kubwa. Ni sababu ya matatizo mengi ambayo jamii inakumbana nayo kutokana na vijana. Sehemu ya kwanza, si vijana baleghe wote ambao wanapenda kusoma. Baadhi ya vijana wengi wanachukia sana mfumo wa shule ambao unawafunga. Na wale wanaovutiwa na ufadhili wa masomo huonekana kama watoto. Wale wanaonyimwa ruhusa na uhuru wa kufanya biashara kwa sheria maalumu mpaka wafikie umri wa miaka 16 wanaweza kujiingiza kwenye biashara haramu (kama vile kushughulika na dawa za kulevya). Na watakaokosa kujiingiza huko wanaweza kuchukua fursa ya ku-

jiingiza kwenye makundi ya wahuni. Wale ambao watafanya vizuri katika masomo ambayo si rasmi sana au yale ya kiwango cha juu, hubaki madarasani kwenye shule zao wakiwa wamechanganyikiwa. Wengi wanasumbuliwa na "tatizo la kukosa utulivu". Kwa kuongezea, vijana wadogo wa kike na kiume, ambao wamepaleka matamanio yao zaidi kwenye jambo tukufu la ndoa, hawawezi kujizuia na zinaa kwa kisingizio cha kuchelewa ndoa, na badala yake wana watoto nje ya ndoa- au wanazuia kupata watoto kwa kutembelea vituo vya kutolea ujauzito.

Njia halali za kupunguza matatizo haya ziko nje ya lengo la kitabu hichi. Hata hivyo, ni muhimu kwa wazazi kutofanya makosa ambayo jamii yetu imeyafanya. Usiwaone vijana kama watoto. Amiliana nao kama vile unaishi na wafanyakazi wenzako ambao ni wadogo sehemu yako ya ajira. Tambua kuwa wanahitaji mwongozo na uzoefu, sambamba na kutambua pia wanahitaji heshima, kupewa majukumu na ushauri. Washajihishe waendelee kwa kadri inavyowezekana. Wape pia majukumu ya kusimamia fedha, kazi za Jumamosi, pengine, ambapo watajifunza ulimwengu wa kazi na kujipatia kipato.

Hasira kwa vijana wetu na sisi wenyewe

HASIRA (ANGER) NI NENO LENYE UPUNGUFU WA HERUFI MOJA KUTOKA KWENYE NENO HATARI (DANGER)

Hasira kwa vijana inawezekana ndio hisia ngumu sana kwa wazee kuweza kwenda nazo sambamba. Linda Lebelle (Aliyejikita Kwenye Huduma kwa Vijana Baleghe) anaelezea na kuchambua jambo husika, kwa kutumia mifano miwili ifuatayo kutupa picha halisi.

Mfano wa kwanza: Karen ni mwanafunzi wa darasa la tisa amekuwa anawaza hakuna jambo lenye thamani tena. Kwa kadiri alivyokuwa anajaribu, alionekana kutofaa. Siku moja kabla alijaribu kwenye mchezo wa shule, lakini alipofika tu jukwaani, aliganda na kulazimika kusimama katikati ya igizo. Sasa, kila mtu shuleni lazima anajua kuhusu jambo hili na Karen ana hakika wenzake wanamcheka. Asingependa wenzake wajue jinsi gani anavyojisikia vibaya. Anajua kwamba wanafikiria jambo hili na wako sahihi- yeye si mzuri sana na hatofaa kamwe. Karen anawachukia wenzake wote.

Mfano wa pili: Chris alipiga ngumi ukuta wa chumba chake cha kulalia. Hata hivyo haikutosha. Alinyanyua soda yake na kuirusha ukumbini. Maji ya kahawia ya sukari yakaingi kwenye ukuta na kwenye kapeti. "Huwezi kunilazimisha.....!" alipiga mayowe. "Siendi popote pamoja na wewe! Nitafanya ninalotaka!" Chris akashuka chini kwenye ngazi na kutokea mlango wa mbele. Baba yake akamkimbilia, akimpigia mayowe kumuita arudi ndani, lakini alikuwa tayari ameshaingia kwenye gari na kuondoka. Chris alimkasirikia sana baba yake. Alikuwa ana mambo mengi mazuri ya kufanya kuliko kutembelea familia. Yeye pamoja na marafiki zake walikuwa na mipango, na baba yake haendeshi maisha yake. Alijua kwamba huwa anajihisi vyema akivuta sigara.

Watu hawa wadogo wana jambo gani linalofanana?

Wanapambana na hasira. Hawapati wanachokitaka na mambo hayawi kwa namna walivyotaka yawe. Wanahisi kero au chuki dhidi ya mtu fulani au kitu fulani ambacho kinamuelewesha kwamba mambo hayapo kwenye miliki yao siku zote.

Hasira ni hisia, si tabia

Hasira ina mifumo mingi- kutoka uchungu na udhia kufikia ghadhabu na ghadhabu kali- na ni kielelezo cha mifumo ya hasira- ile tabia- tunayoiona. Karen anazuia hasira zake na kuziondoa. Chris ni fedhuli na anavunja vitu. Wataendelea na tabia zao, au watazishadidia zaidi, mpaka waamue katika nafsi zao kwenye mizizi hasa ya hasira zao.

Hasira zinaweza kuleta madhara au afya njema

Hasira ni hisia za kuogopesha. Zikioneshwa katika hali hasi inaweza zikajumuisha vurugu la kimwili na maneno, hisia za chuki, maneno machafu sana, tabia isiyo ya kijamii, kejeli, kukosa subra, kujitenga, na matatizo ya akili. Jambo hili linaweza kuteketeza maisha, kuharibu mahusiano, kuwadhuru wengine, kuharibu kazi, kuharibu mfumo wa kufikiri, kuathiri afya ya mwili na kuangamiza kabisa mustakabali wa baadaye.

Lakini kuna upande mzuri; inaweza kutuonesha kwamba kuna tatizo, kwa vile hasira ni hisia inayokuja baadaye inayosababishwa na woga. Inaweza kutusukuma kutatua vitu hivyo ambavyo havina maana katika maisha yetu na kutusaidia kukabiliana na mambo yetu kwa sababu za msingi zitokanazo na hasira.

SABABU ZINAZOSABABISHA HASIRA

- Matusi
- Majonzi
- Dukuduku
- Matumizi ya dawa za kulevya
- Matumizi mabaya ya utajiri
- Kiwewe
- Huzuni

Kuwa mzazi wa kijana mwenye hasira hutupelekea na sisi kuwa na hasira

Vijana wanakabiliwa na mambo ya mihemko sana. Wanakabiliwa na suala zima la kutambulika, kutengwa, mahusiano na malengo. Pia mahusiano baina ya vijana na wazazi wao ni jambo linaloleta changamoto hasa vijana wanapokuwa huru sana. Jambo hili linasababisha kukata tamaa na kuchanganyikiwa ambalo hupelekea hasira na tabia fulani ya majibizano kwa pande zote mbili baba na vijana. Vinginevyo tufanye kazi ya kubadili tabia zetu, hatuwezi kuwasaidia vijana kubadili tabia zao. Tunahitaji kusikilizana na kushawishiana zaidi kuliko kukurupuka kupambana. Lengo si kukataa hasira, lakini kudhibiti hisia hizo na kuzionesha katika namna njema.

Tufanye nini kwa kijana wetu na sisi wenyewe?

Msikilize kijana wako na jikite kwenye hisia. Jaribu kuelewa matukio kwa namna yanavyotafsiriwa na mtoto wako; kuwa mvumilivu. Kulaumu na kutukana tu kunajenga kuta zaidi na kusimamisha mawasiliano yote. Waeleze unavyohisi, jikite kwenye ukweli, na shughulika na

yanayojiri sasa. Onesha jinsi unavyowajali na jinsi unavyowapenda. Tafuta suluhisho ambapo kila mmoja atapata ushindi. Kumbuka kuwa kujihisi hasira si lazima kusababisha vurugu. Tafuta msaada wa kitaalamu kwa kijana wako, wewe mwenyewe binafsi, pamoja na familia yako pale panapotokea vurugu, uadui wa kupindukia, majonzi, au tishio la kujinyonga.

Kanuni chache za mawasiliano mazuri

Kwenye ulimwengu uliotulia kila kitu huenda sawa na kwa namna ya mipango: kwenye ulimwengu halisi mambo yanakwenda kombo. Malengo ambayo wazazi watayaweka, kanuni ambazo watazitumia,

nguvu watakazowekeza kwenye ujenzi wa familia, yote yatashindwa kufanikiwa ikiwa hakutokuwa na mawasiliano mazuri. Mambo yanakwenda kombo usiruhusu kiwango cha hasira, kukata tamaa au masikitiko kujichomoza. Fikiri kwa utulivu kuhusu mambo husika na namna ya kuwa na mawasiliano mazuri.

Kuna kanuni chache za mawasiliano mazuri ambazo zinaweza kutumika. Kanuni hizi zitaondosha nyingi katika mambo yanayosababisha ghadhabu pamoja na mapambano ya nguvu ambayo yanaweza kuanza mapema pale watoto watakapojiunga na mfumo wa kabla ya shule, umri wa shule, na hata baadaye, kwenye miaka ya ujana.

Waruhusu watoto wako kuzungumza na kuwasikiliza bila kujishushia hadhi au kuwa na pupa. Washajihishe wazungumzie siku yao, kuelezea hadithi au kujadili tatizo fulani. Jaribu kutowakatisha. Mfumo wa kale wa mazungumzo (ambao kutoa hadithi na majadiliano yalikuwa ni sehemu ya mambo yaliyoambatana na jamii na maisha ya familia) kwa sasa umeondoshwa na mfumo wa kuangalia (TV, tamthilia, na programu za video). Mazungumzo yana faida nyingi; yanampa mtoto kujiamini na kujieleza mwenyewe, kuwafanya wazungumze, na inapandikiza uwezo wa asili wa kujadili mambo yanayochanganya au muhimu pamoja na wazazi. Ingawa wewe kama mzazi mnakuwa mara nyingi mmeshachoshwa na wengine wanaweza kuona ugumu kuzungumza, Hata hivyo, mazungumzo yana umuhimu mkubwa mno. Mtoto utakayezungumza naye atakuwa na kuhusiana na wewe kama mwanadamu badala ya kukuona mtu tu unayemlisha na kumtafutia nguo.

Tunawalaumu wengine "kwa kuzungumza sana", lakini je imeshawahi kutokea tukawalaumu kwa "kusikiliza sana?" Kusikiliza ni kujali. Kwa kadri tutakavyoongea kwa sauti kubwa, ndivyo watoto wetu watakavyo nyamaza.

Hali hii itawafanya watoto wajihisi kitu kimoja na wazazi na nyumbani. Mawasiliano mazuri yatamfunza mtoto tabia na heshima inayohitajika wakati akiamiliana na wengine, hasa heshima kwa mzazi. Usiwashushe hadhi watoto au kuwafanya wajihisi wajinga. Kuwa makini na mwenendo wako: lazima uwe mpole, makini na mwenye kujimiliki. Wazo ni kuwafanya watoto wajiamini na salama, (mambo mawili ya utu ambayo watayabeba katika maisha yao ya utu-uzima).

Anzisha mjadala wa kisomi pamoja na watoto wako. Jadili mambo na linganisha mawazo. Jambo hili litawafunza watoto tafakuri ya ndani na kukuza uwezo wao wa fikra. Usijaribu kamwe kudogosha akili za watoto au kukanusha mawazo yao juu ya mada.

Wakati mzuri wa kuzungumza ni wakati wa chakula cha usiku. Ikiwa wazazi wata-

anzisha tabia ya kuzima TV, na kula kwa pamoja kwenye meza au sakafuni, watayafanya maisha mepesi zaidi wakati watoto watakapokuwa wakubwa. TV huondosha umakini na kuzuia uwezekano wa kukuza mahusiano ya ndani, hasa wakati wa chakula, ambayo ni fursa nzuri ya kuanzisha na kukuza umoja ndani ya familia.

Usipoteze udhibiti wa hali kwa kupandisha hasira, au kukimbilia mikakati ya kutengeneza hofu ili udhibiti watoto wako. Ni vyema ukaacha kuzungumza mpaka hasira zitakapopoa.

Bado inaendelea kutokea, hata kwa karne ya ishirini na moja, kwamba baadhi ya akina mama wanawatisha watoto wao wakiwa na jinamizi la kufikirika (kuwazuia kufanya baadhi ya vitu kama vile kutoka nje usiku). Baadhi ya akina mama wamevumbua majinamizi (au kuwawakilisha vibaya majini) kupitia majina tofauti (kama vile dujjerah, su'luwwah au dãmiyyah, kiumbe cha kubuni cha mfano wa jinni kikiwa kwenye gauni nyeusi kikiwa na miguu ya punda) kutumia kitisho kama njia ya kudhibiti. Ingawa mbinu hizi za kutisha zinawaweka watoto nyumbani na kuepukana na madhara ya kimwili yanayowezekana, njia hizi pia zinalipuka kwa kujenga hofu isiyo msingi katika fikra za watoto. Wanaweza wakakua katika kiza cha kuogopa, kuwa wapweke, kwenye vyumba vidogo, wanyama, ngurumo, radi na kwenye wageni. Ingawa baadaye wakishakuwa watu wazima watagundua kuwa habari zote za kutisha hazipo katika ulimwengu halisia, ambapo madhara ya kihisia na kisaikolojia yatakuwa yameshatokea tayari. Moja katika sababu kwanini vitendo hivi vinakimbiliwa ni kutokana na wazazi kutokuwa na uwezo wa kufanya uchambuzi wa ndani, na pia kukosa uvumilivu kupitia kukuza njia mbadala.

Zungumza na watoto kwa kuzingatia rika yao, kuliko kuwakalia juu kama pandikizi la mtu. Kuwa na moyo wa kuwapenda, weka mkono wako taratibu juu ya mkono wao unapozungumza nao, au waguse kwa mapenzi, ili wajihisi wameungana na wewe, na jizoeshe kuelezea hisia zao.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 29: MASWALI NA MAJIBU KWA WAZAZI NA VIJANA

Hatua ya awali kutambua na kuidhibiti hasira ni kujitathmini wenyewe. Wazazi na vijana lazima wakae pamoja na kujiuliza maswali haya kujiletea uelewa binafsi. Nukta muhimu hapa ni kuanzisha mjadala kuliko kutoa majibu sahihi:

- Hasira inatoka wapi?
- Ni hali gani zinazosababisha hisia hizi za hasira?
- Je, mawazo yangu yanaanza na maneno kama vile “lazima”, “sharti”, “siku zote”, “Abadani?”
- Je matarajio yangu hayana msingi?
- Ni mzozo gani usioweza kutatuka unaonikabili?
- Je, narudisha majibu dhidi ya maumivu, upotevu au hofu?
- Je, natambua ishara za wazi za hasira? (kwa mfano kukunja ngumi, kupunguza kupumua, kutoka jasho)?
- Ni namna ipi ninayochagua kuonesha hasira zangu?
- Kwa nani au kitu gani naelekeza hasira zangu?
- Je, natumia hasira kujitenga binafsi, au kutisha wengine?
- Je, nawasiliana na wengine kwa ufanisi?
- Je, najikita kwenye jambo nililofanyiwa badala ya kipi naweza kufanya?
- Je, nawajibika vipi kwa kile nachohisi?
- Je, nawajibika vipi kwa jinsi hasira yangu ijichomozapo?
- Je, hisia zangu ndizo zinazonidhibiti, au mimi ndio nadhibiti hisia zangu?

ZOEZI LA 30: KAZI YENYE MFUMO WA TATIZO-UTATUZI

Kusanya wanandoa wawili au watatu kwa ajili ya kujadili jinsi gani mungaliweza kutatua mambo yanayohusu vijana kwenye mifano ya hapo chini. Kisha, linganisha mawazo yenu na njia za Mtume Muhammad (s.a.w).

Kijana mdogo alikuja kumuomba Mtume (s.a.w) ruhusa ya kuzini. Maswahaba walikuwepo walishtuka na walianza kumkaripia. Mtume (s.a.w) alisema, "mleteni karibu yangu". Baada ya kukaa chini, alimuuliza maswali matano kwa mfuatano: "Je, ungependa hili [uzinifu] afanyiwe mama yako, mtoto wako, dada, shangazi kutoka upande wa baba, au shangazi wa upande wa kwa mama?!" Kwa kila swali katika maswali matano, kijana alijibu: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, Sikubali! Oh, Mjumbe wa Allah, Allah anifanye kinga yako!" Mtume (s.a.w) alirudisha majibu kwa kila jawabu la kijana, "Hakuna watu wanaopenda wafanyiwe hilo kwa mama zao, watoto wao wa kike, dada au shangazi!" Kisha Mtume (s.a.w) aliweka mkono kwenye kichwa chake na kumuombea dua, "Ewe, Allah, msamehe madhambi yake, utakase moyo wake, na zilinde tupu zake"(Ahmad). Kijana hakufikiria tena uzinifu baada ya hapo!

Mtume (s.a.w) alizungumza na kijana mdogo, kwa kuzingatia utu wake na heshima yake, na kamsaidia kukuza jinsi ya kujidhibiti binafsi. Kufikiria, kupiga mayowe au kumtisha kwa adhabu pamoja na moto wa Jahannamu visingalisaidia hali ile.

Tunaweza kuona kwamba njia hii ya kuhudumia inaonesha tofauti iliyopo baina ya taaluma ya kinadharia na uelewa wa ndani wa kisaikolojia juu ya ufahamu wa hisia za mwanadamu. Kijana mdogo alikuwa anatafuta suluhisho wakati akionesha hisia zake za ngono. Mtume (s.a.w) hakumuhubiria kuhusu dhambi ambazo zitampelekea kuadhibiwa na kuingizwa motoni; badala yake, alipambanua uwezo mkubwa wa utu na dhamiri. Alitumia njia ya kisaikolojia kuyafikia malengo ya kitabia na dini. Hii si tukio pekee, lakini dini imekita mizizi katika njia nzuri za kutatua matatizo kuelekea kwenye makuzi ya mtoto.

Sehemu 2

Makuzi na Maendeleo ya Mtoto

- sura ya 8:—:Ujenzi wa Tabia si wa kuakhirishwa 166
- sura ya 9:—:Njia za Afya kwa Watoto 194
- sura ya 10:—:Unyonyeshaji Maziwa ya Mama 236
- sura ya 11:—:Ubongo wa Mtoto 258
- sura ya 12:—:Kulea Watoto wa Kiume na Kike 282
- sura ya 13:—:Jinsia na Elimu ya Jinsia 320

8

SURA YA NANE

- **UJENZI WA TABIA SI WA KUAKHIRISHWA**

SURA YA NANE **166**

Ujenzi wa tabia si wa kuakhirishwa **166**

Hatua za Makuzi 170
Ni kwa kiwango gani elimu ya Saikolojia inaweza kuaminiwa? 171
Hatua za ukuaji wa Mwanadamu ndani ya Qur'an 172
Maajabu ya mimba, ujauzito na kujifungua 175
Makuzi ya Mwanadamu: Kuanzia kuzaliwa hadi utu uzima 176
Kipindi cha kupata hedhi kwa wasichana (Kuanzia miaka 11-13) 183
Miaka 13 – 15 : Pindi wavulana wanapopevuka 183
Kuwaelewa Vijana 184
Kutilia mkazo hatua za Makuzi 189
Kijana wa kiajemi Hafidh mwenye umri wa miaka 6 191
Hafidh wa miaka 4½ kutoka Syria 192
Kuhifadhi: Mashariki na Magharibi 192
Kazi za kufanya

Pindi wazazi wanapoamua kujikita katika malezi mazuri, kwa haraka wanatakiwa kuanza na malezi ya elimu ya tabia, huo ndio msingi wa kila kitu watakachokifanya. Matunda yake yatakuwa yenye thamani kubwa.

Makuzi ya tabia huanza utotoni kipindi cha miaka ya ukuaji wa mtoto. Ni kipindi hiki muhimu cha hatua za ukuaji ambapo vipengele muhimu vya tabia za mtu huanza kuimarishwa. Lakushangaza, pamoja na hayo, uendeshaji wa mafunzo mengi ya uongozi yanayoendeshwa yameegemezwa zaidi kwa watu wazima siyo watoto. Fasihi ya makuzi ya binadamu katika nchi za Kiislamu hasa yameelekezwa katika shule za ngazi ya juu za watu wazima au kwa wale walioko katika ngazi ya chuo na zaidi.



"Nini maana ya ujenzi wa tabia? Tabia za kawaida (kama kujiamini, mapenzi, uhuru, uaminifu, uwajibikaji na ubunifu) huunda vitu muhimu vya ubinadamu wa mtu na huanza kukuzwa mapema utotoni. Mara vinapowekwa, huwa ni vigumu kuviondosha, kuvibadili au kuvijenga katika maisha ya baadaye. Ni tabia hizi ambazo hutengeneza msingi wa maisha ya baadaye ya mtu, kwa hiyo wazazi wanahitaji kutumia muda na nguvu kuzikuza katika kiwango cha juu cha uwezo wao. Ingawa elimu, uzoefu na ujuzi ni nyenzo muhimu katika kufaulu,huja baadaye na huweza kufunzwa kadiri mtoto anavyokuwa mtu mzima kuwa wamelelewa kutoka utotoni hadi ukubwani. Husimama kufanya kama majukumu muhimu, huchangia katika kubadili tabia za kawaida, kusaidia na kuwastawisha watu kuwa na uelewa mzuri. Ikiwa tabia zinakuwa ndiyo "*hadiweya*"(muhimili) wa haiba ya mtu, tunaweza kusema kuwa elimu na imani ndiyo "*softiweya*"(mwongozo) wake. Yule ambaye ni mwoga, ghafla

baadaye hawezi kuwa katika utu uzima kwa kuchukua mafunzo ya kuwa jasiri na mwerevu. Pia, yule ambaye amejaa chuki na ukatili, ghafla hawezi kweli kuwa na mapenzi na huruma kwa kusoma vitabu vya mapenzi na huruma. Muongo kwa vyovyote hawezi kuwa mkweli na muaminifu kwa kusikiliza ushauri juu ya uaminifu. Watu wengi, mara tu tabia zao zinapokuwa zimejengeka (kujua wao ni akina nani na wanatabia zipi) itakuwa ni vigumu kuwabadilisha au kubadili "mianzi yao migumu". Njia rahisi na nzuri ya kutengeneza tabia nzuri ni wakati wa hatua za makuzi wakati wa utoto. Mfano Abu Bakar Swidiiq, Umar ibn al-Khatwaab, Khalid in al-Walid na wema wengine ni maarufu. Wanatufundisha tabia ya ujasiri, uaminifu, huruma na uongozi kwamba tayari walikuwa nazo, kwa kulelewa vizuri kipindi cha utotoni. Uislamu ulikamilisha tabia hizi nzuri kwa kuthibitisha vipengele muhimu vya utu na kuongeza imani, hekima na elimu. Uislamu uliweza kuwavutia kupitia busara ya ujumbe wa kale na kuwajaza maana mpya, mtazamo wa kidunia na lengo la maisha. Uimara wa tabia zao haukupungua baada ya kuingia dini mpya bali ziliendelea kustawi. Qur'an inaeleza haya matukio yaliyotokea kwa Mtume pamoja na viumbe wengine, mara inapoeleza kuhusu ukuaji na zama za utu uzima/umri wa katikati, Mungu alimpa elimu na hekima.

Na Mussa alipo fika utu-uzima barabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema.(28:14)

Mtume (Swallalahu Alayh Wasalam) amesema:

Watu ni kama madini [au chuma, kila kimoja kina tabia zake] mzuri katika watu kabla ya Uislamu, enzi za ujahiliya ni mzuri katika zama za Uislamu kama ni mwelewa. (Bukhari na Muslim)

Afisa mzuri wa askari na mtuhumiwa, wote wanahitaji kuwa na ujasiri na uaminifu

(utiifu) ili waweze kufanya vizuri na kusaidia makundi yao. Pia, afisa askari hutumia tabia hizi kusaidia jamii, ilihali mtuhumiwa huzitumia kwa madhara. Ingawa ujasiri na uaminifu ni muhimu, vinahitaji kuthaminiwa ili viwe msaada, vinginevyo vitakuwa na madhara na uharibifu.

Kwa kawaida Uislamu hutoa usaidizi wa jumla katika mambo mengi, wakati huo huo pia hutoa maelezo ya ziada na mwongozo kuhusu familia. Uislamu unadokeza utambuzi wa mfumo wa familia na kutoa usaidizi katika kuchagua mchumba, kuoa/kuolewa na kuandika mikataba ya ndoa (ikijumuisha umuhimu wa walii na mashahidi). Uislamu pia hutoa usaidizi kuhusu tabia za mahusiano, ujauzito, utoaji mimba, kujifungua, kumpa jina mtoto, nasaba, unyonyeshaji, malezi ya mtoto, utashi na ulezi, elimu na maarifa, tofauti za kijinsia na ufanano, mirathi, haki za watoto na majukumu, uhalifu, kuwalea yatima, kupanga uzazi, ujane, uzazi na makuzi ya mtoto, talaka, eda, kusubiri kipindi cha ndoa (baada ya kupewa talaka au mume kufariki), kuacha, hedhi, mahusiano ya kindugu, familia kubwa, mapatano ya kifamilia, bibi na babu, wajukuu, jirani na kanuni za uvaaji.

Wazazi huchukuliwa kama wafanya jitihada kwa sababu wanajukumu la kuandaa watu wazuri katika jamii pamoja na watu wabunifu, wanazuoni waliobobea, wachapakazi, askari washupavu, wakimbiaji wazuri na viongozi wakubwa mahiri ambao hujali utu. Hatua zifuatazo husaidia wazazi kutilia mkazo katika ujenzi wa tabia na mipango ya maendeleo ya kielimu.

MTOTO NI FUMBO TOFAUTI!

Ulimwengu wa mtoto ni ulimwengu wa ajabu hali inayopelekea watu wazima kushindwa kuufahamu. Ni ulimwengu wa kisasa mno ambapo wazazi , wanafikra, wanafilosofia, wakufunzi hawawezi kuudiriki.

Abu al-Hub 1979

Hatua za Makuzi

Kipengele hiki kitaangalia hatua muhimu za ukuaji ili kuwawezesha wazazi kuangalia taratibu za ukuaji wa watoto wao kutoka hatua moja hadi nyingine na kuelewa vizuri mahitaji muhimu ya kila hatua. Katika muhtasari wa njia za ukuaji wa mwili wa binadamu na ubongo kipindi cha miaka ya ukuaji, wazazi pia wataoneshwa namna watakavyopata faida katika hatua mbalimbali zinazohusiana na matunda ya ulezi.

Mfano, baadhi ya wazazi huwalazimisha watoto wao kula sana lakini hukataa kabisa. Ghafla, baadaye hamu yao ya kula huongezeka na huanza kula sana bila utashi. Hii haitokei kwa uamuzi wa wazazi bali ni hulka ya kimaumbile. Pia ghafla vijana huenda kinyume na wazazi wao pamoja na mazingira, pindi

wanapokua tabia hii hupungua kulingana na hatua halisi za kimakuzi. Madaktari wanawashauri wazazi kuwa na uelewa mzuri wakati wa hatua za makuzi zinapofika. Siyo kufikia hatua hii kama kitu ambacho ni cha ghafla kitakachokuja kama kiashiria kwamba kuna tatizo muhimu la kiafya.

Kibainisho kizuri kwa mzazi ni lazima ajulishwe. Wasiwe na woga kuwauliza wataalamu juu ya familia zao kwa ajili ya kueleweshwa. Wasiwe na woga kama watoto wao hawafikii kila hatua kwa wakati. Watoto husisitizwa juu ya maendeleo yao katika kila hatua. Ingawa maendeleo ya mtoto hufuata njia maalumu za kibinadamu, pia zina upekee kwa kila mmoja. Ili kufaulu, wazazi lazima waweke pembeni ndoto zao kwa ajili ya watoto wao na kuwasaidia watoto wao kutimiza ndoto zao. Watoto sio kama wazazi wao, kwa sababu wana vitu binafsi walivyonavyo. Wanashauriwa wazazi kuuacha ukweli kuwa ukweli na kuukubali uhalisia ambao siri yake ni uvumilivu.

Ni kwa kiwango gani elimu Saikolojia inaweza kuaminiwa?

Ingawa Waislamu wanakubali nadharia mbalimbali za saikolojia zilizoenea katika jamii ya leo, wanahitaji kuwa waangalifu sana kuhusu nadharia juu ya maendeleo ya binadamu na tabia. Kwa namna moja, zinaendelea kubadilika na wanasaikolojia hawakubaliani juu ya mambo mengi. Waislamu hawajapoteza kabisa, kwa sababu wana mwongozo wa dini usiobadilika, ambao unawaweka katika njia sahihi na unawaepusha na kubabaika kutokana na mchanganyiko wa maono.

Mfano ni mjadala usioisha juu ya ulimwengu dhidi ya malezi, hitilafu ya kinasaba dhidi ya mazingira, vinavyowasumbua wanasaikolojia. Anasema Wright (1998)

> "Wanasaikolojia wanaweza kukaa kwa miongo mingi wakitafuta chanzo cha kulea vizuri mtoto – siyo kwa sababu kimepatikana bali ni kwa sababu hakipo. Wazazi hawana malengo muhimu ya muda mrefu juu ya namna ya kuwalea watoto wao".

Judith Harris (1998) anadai karibu nusu ya tofauti za kimaumbile kwa watoto zinatokana na vinasaba. Mbali na mazingira ya nyumbani, mazingira ya nje huchangia sana ambako huiga tabia za wenzake na kupata sehemu imfaayo katika elimu ya kawaida ya saikolojia. Huwa mjeuri au mpole au mpuuzi au mtukutu na tabia huanza kukomaa. Inaaminika kuwa mzazi anaweza kulea tabia katika mazingira ya nyumbani. Hata hivyo katika ulimwengu mtoto ni mtu tofauti na hapo ndipo mwanzo wa ukuaji wake.

Bila shaka fikra za namna ya kurekebisha matatizo ni kwa namna gani mtu anaweza kumkuza vizuri mtoto kwa kutumia njia ya ajabu. Kwa kweli tabia za vinasaba zimefundisha kwamba mapacha wanaofanana waliolelewa pamoja ni nadra kufanana na mapacha waliolelewa tofauti. Uzazi wa mpango pia unaweza kuwa sababu. Labda ndugu wadogo wanaweza kupewa malezi tofauti na wazazi au kukumbana na baadhi ya matatizo ya kimazingira, mfano kukandamizwa na ndugu wengine.

Kijana wa Arkansas alimpiga risasi mwenzake shuleni wakati kaka yake mdogo hakufanya hivyo. Kwa nini? Je, ubaguzi shuleni umefikia kiasi hicho kwa sababu anajihisi nyumbani hapendwi kama kaka yake? Je, kukataliwa kwenda uwanjani kulimfanya ajihisi vibaya kwa hiyo akakaidi malezi ya wazazi wake ambayo alilelewa kaka yake? Hicho kitakuwa ni chanzo cha malezi ambacho kitabadilisha matakwa ya mtoto? Hakuna ajuaye.

Chanzo cha ujumbe wa ushawishi wa Harris' ni kwamba wazazi wanaweza kuathiri na kutumia baadhi ya hisia katika umri huu wa mzazi kuogopwa. Pia inaweza kuwa kinyume chake. Siku hizi tayari malezi ya wazazi yanatengeneza rika moja na mazingira yao.

Wazazi wanaweza kupata utulivu – sayansi bado haijajibu maswali mengi. Ni kwa muda gani wazazi watasubiri ili sayansi iwaeleze namna gani ya kuwalea watoto wao? Mwanadamu anapaswa kuweka matumaini yake katika msingi imara wa kidini kwa msaada wa Mungu na Mtume wake. Huu sio wito wa kupinga nadharia za saikolojia ila utafiti makini unahitajika ambao utaweka misingi ya ufunuo katika matumizi ili kuzisaidia familia katika malezi. Nadharia za wasiomwamini Mungu zitazua matatizo makubwa pasipo faida katika jamii. Jibu sahihi kuhusu malezi linaegemezwa kwa uambatano mzuri kutokana na ufunuo wa muumbaji na mkusanyiko wa elimu ya binadamu. Hizi ni hatua endelevu.

Hatua za ukuaji wa Mwanadamu ndani ya Qur'an

Aya zilizoorodheshwa hapo chini kutoka katika Qur'an zinaelezea hatua mbalimbali za ukuaji wa mwili wa binadamu.

Hebu na ajitazame mwanadamu ameumbwa kwa kitu gani?

Ameumbwa mtu kutokana na maji yanayotoka kwa nguvu.

Maji haya yanatoka baina ya uti wa mgongo na mbavu za mwanamume na mwanamke.

(Qur'an, 86: 5-7)

> Enyi watu! Ikiwa nyinyi mna shaka ya kufufuliwa basi kwa hakika sisi tulikuumbeni kutokana na udongo, kisha kutokana na manii, kisha kutokana na kipande cha damu ilio gandana, kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo na kisicho kuwa na umbo, ili tukubainishieni.
>
> Nasi tunakiweka katika matumbo ya uzazi tunacho kitaka mpaka muda ulio wekwa. Kisha tunakutoeni kwa hali ya mtoto mchanga, kisha mfikie kutimia akili. Na wapo katika nyinyi wanao kufa, na wapo katika nyinyi wanao rudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa, hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua.
>
> Na unaiona ardhi imetulia kimya, lakini tunapo yateremsha maji juu yake husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.
>
> (Qur'an 22:5)

> Na Allah amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.
>
> (Qur'an 16:78)

> Allah ndiye aliye kuumbeni kutokana na udhaifu kisha akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba atakavyo. Naye ndiye Mjuzi, Mwenye uweza.
>
> (Qur'an 30:54)

> Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo.
>
> Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu la uzazi katika kalio madhubuti.
>
> Kisha tukaliumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Allah mbora wa waumbaji.
>
> Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa.
>
> Kisha hakika nyinyi siku ya Kiyama mtafufuliwa.
>
> (Qur'an 23:12-16)

Kuna hatua nyingi za uumbaji na ukuaji zilizoorodheshwa hapa. Zinaweza kuainishwa kama ifuatavyo:

- Vumbi – Mfano wa udongo wa mfinyanzi. Hii ni nyenzo ambayo imetumika katika kumuumba mwanadamu, kama ilivyothibitishwa na ushahidi wa kisayansi, wameumbwa kutokana na udongo na watarudishwa humo na watafufuliwa kutoka humo.
- Nafsi moja – Nafsi moja ni ile ambayo wanandoa wa kwanza, Adam na Hawa waliumbwa kutokana nayo. Inafaa kuangaliwa kwamba neno "*zawj*" limetumika katika Qur'an sawa na mume/mke, jozi na wanandoa.

- Uzazi – Kutoka kwa wanandoa wa kwanza, utaratibu wa uzazi ni kama ifuatavyo; *nutfah:* mayai yaliyorutubishwa (mbegu ya mume + yai) *'aalaqah*: tone la damu *mudghah*: kiinitete (kilichotafunwa – kama kiini) *'izaman*: (mifupa) *lahman*: (pande la nyama) linalofunika mifupa.

- Kiumbe kingine (*kijusi*) – (huwa ni mimba ya miezi 4) sasa inaweza kuwa ni kiinitete ambapo hukua kwenda katika hatua nyingine ya maisha ya ubinadamu. Kwa wakati huu kijusi huwa sio zana tu ila ni mwenza wa nafsi ambayo huwa na ufanano wa tabia za mzazi. Anakuwa ni mwenza na mwenye haki tu hafanyi lolote katika hatua hii.

- Mtoto (*tiflan*) – Mtoto aliyezaliwa asiyejua kitu na mwenye kuhitajia huduma zote.

- Kuacha ziwa (*fisaluhu*) muda usiopungua miaka 2 – mtoto mchanga hunyonya maziwa ya mama kwa muda usiopungua miaka 2. Unyonyeshaji umesisitizwa sana katika aya tano.

- Kupevuka/Kubalehe – Kufikia katika umri (*al-hulum*) wa kujiotea au kupata hedhi unaotokana na ukuaji na maendeleo ya homoni. Katika hatua hii wanaweza kuzaa na kuwa wazazi.

- Ujana (*ashudd*) – Kukomaa kwa mme au mke. Kwa mujibu wa Yusuf Ali, miaka ya ukomavu ni 18 na 32, ingawa Mtume (Swalla Allahu alayh wa sallam) aliwaruhusu vijana wa kiume wa miaka 15 kushiriki katika vita. Kwa wengine kupevuka kunaweza kuwa zaidi ya hapo. Kwa wale waliopevuka, umri wa hekima/busara unaweza kuwa ni wakati wa miaka 40.

- Uzee (*shaykh, shaybah, ardhal al-Umur* na pia *da'f*) Umri wa udhalili, kupoteza kumbukumbu na maarifa na kuongezeka kudhoofu. Inaweza pia kujulikana kwa kupungua kwa maarifa, hadi kufikia mtu kutojua kitu ilihali alikuwa akijua mambo mengi. Katika kipindi hiki, mwanadamu huwa amepitia hatua za udhaifu kisha ushupavu kisha ushupavu zaidi, kisha udhaifu na mwisho umri wa udhalili.

- Kifo – Baada umri aliopewa na Muumba kukamilika, mwili wa mwanadamu ambao ulitokana na udongo hurudi katika udongo, kusubiri siku ya kufufuliwa.

- Kufufuliwa (*ba'th*) – Hivyo mzunguko wa uumbaji hukamilika.

> Kutokana nayo (ardhi) tumekuumbeni, na humo tunakurudisheni, na kutoka humo tutakutoeni mara nyingine.
>
> (Qur'an 20 :55)

- Maisha ya milele – Maisha ya peponi au motoni ni ya milele, yanatokana na matendo yetu pamoja na huruma (rehema) za Mungu. Hatua hii ndiyo ya mwisho katika mzunguko wa uumbaji wa mwanadamu, kutoka tangu kuzaliwa hadi maisha ya milele.

Qur'an imeweka njia hizi tofauti katika mtazamo mpana ambao ni sahihi. Wanadamu hawakuwepo, ndipo Mungu aliiumba nafsi. Kutoka katika nafsi moja Mungu akamuumba mwanamke (haijulikani ni kwa namna gani, Qur'an haielezi juu ya hilo). Hivyo wenza hawa wawili ndipo wakaoana na kuanzisha uzalishaji ambao binadamu hupatikana kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa kuoa/kuolewa kwa kuhifadhi na kulinda mfumo muhimu wa jamii: familia huwa na baba, mama na watoto.

Maajabu ya mimba, ujauzito na kujifungua

D'Oyen (1996) anaeleza kwamba wakati mbegu ya mwanamume inaporutubisha yai la mwanamke, yai jipya lililorutubishwa ni kubwa zaidi ya nukta ya herufi ndogo ya 'i' na kwa muda wa wiki kadhaa hufanana na kitu fulani kilichomezwa na kutemwa. Wakati inapofikisha muda wa wiki nne, huanza kuwa na sura ya binadamu na tayari huwa na moyo mdogo ambao huanza kupiga hadi kifo – wakati inapokuwa chini ya urefu wa inchi moja! Wakati mimba inapofikisha miezi minne, inakuwa karibu na ukubwa wa inchi sita na tayari inakuwa na vidole, nyayo na nyusi. Ingawa inakuwa bado haipumui na macho yake yanakuwa bado yamefungwa, anaweza kusikia mapigo ya moyo ya mama yake, sauti yake na minong'ono mingine ambayo ni sawa na mtu anayesikia sauti wakati kichwa kipo kwenye maji. Kijusi hupiga na kunyoosha na kugeuka kila upande huku akinyonya kidole gumba. Wakati mwingine pia humeza maji ya *amniotic* na kupata kwikwi. Mama huweza kuisikia mienendo hiyo. Wakati mtoto anapozidi kuwa mkubwa, baba anaweza kuweka mkono wake kwenye tumbo la mama na kuyasikio mapigo na kwikwi.

Wakati mwingine mama hushindwa



kulala usiku kwa sababu mtoto anataka kusogea wakati huo wa kwenda kulala. Lazima ale vyakula vizuri vya lishe ambavyo humsaidia mtoto kukua. Pamoja na hayo, wakati wa ukuaji wa mtoto mama hawezi kula sana, kwa sababu ya nafasi ndogo. Mimba inapotimiza miezi saba, mtoto huwa mzito zaidi. Mama mzazi uhitaji uangalizi wa karibu zaidi na usaidizi nyumbani. Baada ya miezi tisa, mtoto huwa na uzito wa kilo 2.71 na 10 na urefu wa kati ya inchi 18 na 21. Hapa hawezi tena kujigeuza ndani ya uterasi (tumbo), ni muda wa kuanza maisha ya nje ya dunia.

Mtoto anapokuwa tayari kuzaliwa, mfuko wa uzazi ambao Allah aliufanya kuwa mgumu, huanza kupanuka kwa kusukuma mtoto nje. Kama walivyo wanyama wengine, mwili wa binadamu umeumbwa kujizalisha bila msaada wa daktari. Mara zote kujifungua ni njia ambayo ni salama na yenye furaha, kinyume na matukio ya kutengeneza yanayooneshwa kwenye TV. Licha ya maumivu makali ya maabara ambayo yanaambatana na kutanuka, akina

mama wengi ni wavumilivu na wajasiri ili kuokoa maisha ya watoto wao. Husahau kuhusu maumivu pindi wanapozaa na kuwabeba mikononi.

Mungu ameeleza hadhi ya saikolojia ya uzazi kuwa ni *wahnan ʻala wahn*, maumivu juu ya maumivu au udhaifu juu ya udhaifu. Kwa kweli wakati mwingine mama hujisikia kuwashwa, kuchoka, maudhi kidogo, huelea katika hisia za huzuni na furaha na kuogopa sana. Allah amempa ruhusa ya kutofunga wakati wa Ramadhani, anaweza kulipa funga hiyo baadaye akiwa mzima. Wakati na baada ya siku 40 amesamehewa kutoswali swala tano kila siku. Hiki ni kidokezo muhimu kwa mume na ndugu kumsaidia yeye kisaikolojia na kimwili kwa kazi za nyumbani. Wahakikishe ana afya nzuri kwa kula chakula chenye lishe, kulala vizuri na asiwe na msongo wa mawazo wakati wa kunyonyesha.

Hatua mbalimbali za makuzi ya mwanadamu: Kuanzia kuzaliwa hadi utu uzima

Hatua za makuzi hutokea kimwili na vile vile kiakili na maeneo yote haya lazima yashughulikiwe kikamilifu. Umri unaotajwa kwa kila hatua huwa kwenye makadirio.

HATUA ZA MAKUZI KWA MUJIBU WA UMAR IBN AL-KHATAB

Ameziorodhesha hatua zifuatazo:

Mtoto hulelewa kwa muda wa miaka saba; na huwasaidia wazazi wake anapokuwa na umri wa miaka saba; ukuaji wake wa mwili (urefu) husimama anapofikia umri wa miaka 23. Ukuaji wake wa akili hukoma anapofikia miaka 35 na zaidi ya hapo ni uzoefu tu. (Tuffah, 1979 kwa Kiarabu).

Maswali mawili muhimu ni: Ni kipindi gani tabia hujengwa? Je kuna jambo lolote linalojengwa baada ya umri huo? Ingawa hakuna anayejua jawabu sahihi lakini kujua kwa ujumla wake ni jambo muhimu.

Hatua kuu za makuzi zimeorodheshwa hapa chini:

KUZALIWA - MIEZI MINNE

Wakati wa kuzaliwa, aya ya (16:78) inaeleza kuwa mwanadamu huzaliwa akiwa hajui chochote, ndipo Mwenyezi Mungu akampa uwezo wa kusikia, kuona na akili kama zana za kupatia elimu ambapo mwanadamu anatakiwa amshukuru Muumba wake.

Tangu siku ya kuzaliwa mpaka miezi minne uoni wa watoto huwa hafifu, baadaye watoto huonekana kuwa makini katika kuwaangalia watu. Huwaangalia zaidi mama zao kuliko watu wengine. Huwa wanashtuka wanaposikia sauti za ghafla na hupepesa macho wanapouona mwangaza, huinyoosha mikono yao na huipeleka nyuma, hugeuza vichwa vyao kila upande, baada ya muda mfupi huanza kuzitambua sauti za wazazi wao, huanza kucheka, kulia na kutoa sauti. Vichwa vya watoto wa kiume huwa vikubwa kidogo kuliko vya watoto wa kike (Spock 1974).

Ratiba ya kinga ya maradhi lazima ifuatwe. Mtoto hatakiwi kutikiswa tikiswa kwa sababu ubongo wa mtoto huwa bado haujatulia, kama mtoto atalia bila ya kunyamaza na joto lake ni la kawaida. Je huo ni wakati wa kubadilisha nepi? Ni wakati wa kula? kulala? Au kubebwa? Mtoto kawaida huwa analia pale anapohitaji mahitaji yake halisi. Kulia, ingawa ni jambo zito kwa wazee lakini huwa ni jambo la kawaida. Wazazi wanahitaji kupata ushauri wa daktari au wanasaikolojia kama kilio kitakuwa cha kupindukia na mtoto hawezi kutulia.

MIEZI 5-18.

Hatua hii ya ukuaji huenda ikawa muhimu sana katika kujenga misingi thabiti ya kimtazamo katika maisha. Watoto huanza kujihisi kama wanatengwa na kujiona wana uwezo wa kujitegemea kama kutaka kushikilia chupa wao wenyewe na si kwa kutaka kusaidiwa kwa muda mrefu. Wanaweka mahusiano ya karibu sana kwa wazazi wao. Ikiwa wazazi watakua na tabia ya ukali, watoto hutarajia pia kuwa jamii nzima ina tabia hiyo. Mapenzi ya wazazi huzidisha upendo kwa watoto. Ikiwa kwa upande mwingine wazazi wao ni wakarimu vivyo hivyo watoto watakuwa katika njia hiyo. Wanaweza kudhani kuwa jamii yote iliyobakia ni wakarimu na hivyo hudumu katika tabia hiyo ya ukarimu. Kulingana na tabia zao, watoto katika hatua hii hujihisi kama wanapendwa au hawapendwi, wema au waovu. Hii ni pale ambapo watoto wanapotaka kuwa na mitazamo mema au mibaya. Ikiwa watoto hawana mahusiano ya karibu sana na wazazi wao, hawatorandana vizuri katika vitu na mitazamo. Unyonyeshaji unafaida kubwa sana kwa ukuaji wa mtoto, kimwili na kiakili.

Wazazi wanatakiwa kuwasiliana na daktari ikiwa mtoto ana matatizo ya kushindwa kutambaa vizuri, kushindwa kusimama mwenyewe hata kwa kujishikiza au kushindwa kutoa sauti au alama kuonesha vitu. Kipindi cha miezi 6, mtoto anatakiwa kuwa na uwezo wa kukaa bila kushikiliwa, kukifikia kitu kwa mkono mmoja na kuhamisha katika mkono wa pili, kucheza na wenzake pamoja na kutambua jina lake. Watoto wengi ingawa si wote wanalala usiku mzima. Mara nyingi jino la mwanzo huota katika kipindi cha umri wa miezi 6. Mtoto anatakiwa aweze kukisimamisha kichwa chake mwenyewe na awe na uwezo wa kutazama, kusikia na kuona vizuri. Wazazi wanatakiwa kujua tofauti ya kilio cha "nina njaa" na kilio cha "nakuhitaji". Kiuhalisia watoto wa kike huwa wepesi sana kufikia mabadiliko ya kimaumbile kama vile uwezo wa kupiga manyanga, kwa haraka kidogo kuliko watoto wa kiume, ingawa watoto wa kiume wanasadikika kukuwa haraka kuliko watoto wa kike.

Katika kipindi cha miezi 9, watoto huwa na uwezo wa kutambaa na huwa watundu sana. Katika kipindi hiki mtoto anakuwa na uwezo wa kutambua sauti mbalimbali na kuanza kuigiza sauti hizo. Mishipa ya fahamu humuwezesha mtoto kukamata vitu vidogo vidogo na kuvigongesha gongesha. Baadhi ya watoto hujivuta vuta na kuanza kutembea kwa kujishikiza kwenye samani. Kitu chochote kile kinachokuwepo karibu na watoto huenda moja kwa moja mdomoni kwa sababu watoto hutumia midomo yao kutambua baadhi ya vitu. Mikono ya watoto hurandaranda mpaka maeneo ambayo wazazi hawakutegemea.

Kwa kipindi ambacho watoto wanakuwa wametimiza umri wa mwaka mmoja, wanakuwa na uwezo wa kutembea na kuzungumza maneno machache pamoja na kujilisha. Wanaweza kujifunza kusema maneno kama vile mama au baba. Ingawa bado hawana uwezo wa kutambua makatazo, mtoto ana uwezo wa kutambua maana ya neno "hapana." Ni vizuri sana kumuelekeza mtoto katika vitu ambavyo havitakikani hali ya kuwa unamkemea. Kabla ya kutimiza mwaka mmoja watoto huwa hawajitambui kama kuna mambo wanakosea. Wanachojua wao ni kwamba dunia ni kubwa, na wapo tayari kujifunza kutokana na ya dunia. Kati ya umri wa mwaka 1 na 2, utembeaji unakua katika kiwango kizuri. Mtoto sasa anakuwa mwenye uwezo wa kujitegemea na kufurahia hali hiyo. Mtoto atacheza mpira, atakimbia, atapanda ngazi kwa kutumia mikono, na kuchorachora kwa kutumia kalamu ya kuchorea au kalamu ya rangi. Watoto huwa na msukumo kwamba hawajui tofauti ya tabia njema na tabia mbaya au kuelewa tofauti baina ya nzuri na mbaya. Wakati ukifika (kumuondoa mtoto kutoka katika hali ya utegemezi katika mazingira fulani) ni njia ifaayo katika malezi, kwa dakika moja tu ndani ya mwaka.Katika umri huu hawajitambui au kujielewa. Wazazi wanatakiwa kuwapa uchaguzi siyo adhabu na kuwapa uhuru kamili. Ni muhimu kuwepo sheria chache kiasi iwezekanavyo ingawa msimamo ni muhimu.

Ni muhumu sana kuendeleza lugha na sehemu muhimu za ubongo wa mtoto kwa njia ya usomaji wa Qur'an, muziki laini, nyimbo za asili, na nyimbo zifaazo, nashidi {nyimbo za dini} na mapigo. Hii itasaidia makuzi ya sehemu mbalimbali za ubongo wa mtoto.

Wazazi wanatakiwa kuwa makini kwa muda mrefu, na wazazi wanatakiwa kuwapa shughuli za kufanya kama uchoraji na ujenzi wa nyumba za tofali. Wanatakiwa kuwajuza matabibu wa familia zao kama watoto wao wataonekana ufahamu wao ni mdogo. Kukasirika hukatisha tamaa ingawa kiujumla hakusababishi tatizo. Usikivu huendelea kwa haraka kuliko kuona, watoto huathiriwa na sauti za ukelele. Haiwezi kuonekana vyema kabla ya miezi sita. Ufahamu huja baada ya usikivu na uoni.

MIEZI 18-36

Katika hatua hii mtoto hupata hisia za kimsimamo juu ya tofauti ya mtu mwingine kama wapendavyo. Yawezekana wanajikuta wakiwa tegemezi juu ya wazazi wao. Mtoto hujihisi katika matatizo mengi: Utegemezi dhidi ya kujitegemea, unadhifu dhidi ya uchafu, ushirikiano dhidi ya kutoshirikiana na upendo dhidi ya uhasama.Tabia ya watoto mwishoni mwa mwaka wa tatu itategemea kiwango cha mlingano au uthabiti, tabia ya kuzaliwa na hatari itokanayo na mahusiano yaliyotokana na wazazi wao katika kipindi cha majaribu.

VITA VISIVYO NA MANTIKI BAINA YA WATAALAMU NA TAFITI ZA KISAYANSI

Brazelton anawaeleza wazazi juu ya kuwazoesha watoto usafi lakini isizidi sana ili kulinda maisha ya furaha. Anasema suala la kuwafundisha usafi wakati ambapo watoto hufuata maelekezo na kuiga wengine, kwa kawaida ni katika umri wa miaka miwili.

Leach anasema:Usijihangaishe kumfundisha mtoto akiwa na umri chini ya miezi 15 na usitarajie watoto wanaweza kutambua kila kitu katika kipindi hicho kabla ya kufikia umri wa miaka mitatu. Usimsumbue. Mchakato unaweza kuchelewa.

Roosemond anaamini kwamba kama mama atakuwa mtu wa sheria na kuacha kuwa mlezi kabisa chini ya umri wa miaka miwili hivyo mtoto hatokua vizuri na pengine atakuwa na matatizo ya kitabia baadaye maishani.

Utafiti unathibisha kuwa watoto tofauti hujifunza kwa wakati tofauti. Kumfundisha mtoto wa kike huchukua miezi tisa (wavulana ni zaidi) na hiyo huwa anakumbushwa mara kwa mara.

(LEMONICK 1999)

Mfano kama wazazi watawalea vizuri na mtoto akawa na tabia ya utiifu, anaweza kuwa pia mnyenyekevu. Wakiwa ni wenye uhasama na uadui, na wakaacha mwanya kwa mtoto kupigana, mtoto anaweza kuwa mwenye uhasama na uadui zaidi. Endapo wazazi walikuwa wakatili na wakajisafisha vizuri, watoto wao wakalelewa katika utiifu wanaweza kuwa wazuri zaidi na waadilifu. Kama wasiwasi wa mzazi utamfanya amwangalie kwa makini na endapo mtoto hatajishughulisha anaweza kuwa mtegemezi moja kwa moja. Unyonyeshaji lazima ukome wakati wa miaka miwili, ili kumuwezesha mtoto kujitegemea mwenyewe zaidi na zaidi. Wanasaikolojia mbalimbali wanadai kwamba tabia ya mtoto inatengenezwa wakati wa umri wa miaka mitatu. Isipokuwa baadhi ya tabia za mtu kubadilika baadaye utotoni na ukubwani kama mazingira yatamsukuma kufanya hivyo.

Pia tabia nyingine nyingi haziwezi kujengwa hadi hatua za baadaye za ukuaji. Mtazamo wa mtoto kwa watu wa jinsia yake na jinsia nyingine utajulikana ni rafiki wa namna gani atakuwanao na aina ya maisha ya ndoa atakayokuwa nayo.

Katika kipindi cha mwanzo wa miaka miwili, mtoto hukua haraka na kubadilika haraka. Kila mwezi huwa anajifunza kitu kipya. Baada ya miaka miwili mtoto huanza kukua taratibu.

Watoto taratibu hukimbia na kuanza kuruka, kupanda, kuchukua vitu na pia kuendesha baiskeli ya magurudumu matatu. Huiga maneno na vitendo. Wanaweza kuchora duara na mraba zinazotambulika kidogo na kufanya mafumbo madogo. Wanaweza kuvutiwa na mazoezi ya kwenda chooni. Kwa hatua hii, watoto wadogo hupenda kuzungumza sentensi fupi na kujua maneno angalau hamsini. Wazazi wanatakiwa kuwa wavumilivu wa mwendelezo wa maswali ya “kwa nini”, ni muhimu kuendelea kuhimiza udadisi bila ya kuwa na papara. Kuimarisha maendeleo na kujali muda ni njia muhimu za nidhamu. Huu ni muda mzuri wa kuanza kufanya kazi za kijamii kama vile kushiriki na kubadilishana na wengine.

Kuongea kwa kuacha baadhi ya maneno, kuonesha mapenzi kidogo kwa watoto wengine na kuanguka mara kwa mara, yote ni matendo ambayo wazazi wanatakiwa kuyaripoti kwa daktari wao wa familia na daktari wa magonjwa ya akili.

Utofauti huanza kuonekana; wasichana huongezeka kwa haraka na wavulana huanza kuelekea mabadiliko taratibu. Wanapotimiza umri wa miaka 3 wote inabidi wawe na misamiati ya maneno yasiyopungua 250.

UMRI WA MIAKA 4-7

Wanapotimiza miaka 4 watoto hula kidogo kulinganisha na walipokuwa na miaka 2 kwa sababu hawakui kwa haraka na wanakuwa siyo wakakamavu sana. Watoto huendelea kukua kwa kasi kila mwaka, kujifunza mambo mapya kila

siku hadi wanapofikia umri wa ujana, pindi wanapofikia mabadiliko mengine makubwa. Nyota ya nishati ndogo ni kati ya miaka 4 na 5 huwa kubwa (hupenda kutembea, kukimbia na kurukaruka), hutumia muda mwingi katika hatua ya kutambaa. Mtoto huweza kurusha mpira na kuendesha baiskeli yenye magurudumu matatu.

Katika hatua hii wazazi wanaweza kueleza kwa nini tabia ni mbaya na kujadili matokeo (pamoja na kwamba maelezo ni mafupi). Tia moyo na wazawadie kwa kuwa na tabia nzuri na waadhibu kwa kuonesha tabia mbaya. Mtoto afundishwe kutokwenda kinyume na mzazi. Mtoto lazima apewe mazoezi ya kwenda chooni kabla ya kutimiza umri wa miaka 5 na atataka aweze akiwa pekeyake au na wengine.

Watoto hujua tofauti kati ya wavulana na wasichana na hutaka kujua majina ya viungo vya mwili. Hatua hii huwa ni ya "maswali" kwa sababu watoto huuliza maswali mengi (yakijumuisha yale ya jinsia). Wazazi lazima wajibu maswali haya, kinyume na hivyo watoto watatafuta majibu kutoka kwa rafiki zao, ambao kwa vyovyote vile watawapa majibu ya uongo. (Jaber 1977, kwa Kiarabu).

Kwa muda mrefu, watoto huwa na tabia ya kubadilika badilika na hisia na hukua kutoka hatua moja kwenda nyingine; kutoka katika kupenda sana na kubadilika kuwa kukasirika au kuchukia, kutoka kwenye furaha kuwa huzuni. Watoto huanza kuogopa na kupelekea kuogopa giza, wanyama, kifo na Mungu. Wanaogopa kutengwa na wazazi na kuwakosa pia. Watoto hujifunza woga kutoka kwa wazazi wao na watu waliowazunguka. Wanawaiga kwa kuogopa buibui, sehemu zenye vitu vya ajabu na sauti kubwa. (Jaber 1977, kwa Kiarabu).

Watoto wanaweza kuwa na wivu kwa wengine kitu kinachoweza kuwapekelea kuwa watu wa shari. Mfano mzuri ni wivu wa kihistoria uliooneshwa na kaka zake Nabii Yusufu, uliwapelekea kutaka kumdhuru.

Jinsi watoto wanavyokuwa, tabia ya mzazi wa jinsia yake inaweza kumuathiri zaidi. Wavulana huwatizama zaidi baba zao kwa ukaribu zaidi wakifanya kazi za bustani-ni na wasichana huwaangalia mama zao wakifanya kazi za nyumbani. Wazazi wa-naweza kupandikiza mapenzi na heshima kwa watoto wao kwa wao kuwa mfano bora wa kuonesha mapenzi ya dhati na heshima kwa kila mtu na kwa watoto wao.

Kufanya mambo kwa pamoja ikiwemo kucheza, kusoma na kuwahudumia wanyama, hii itawasaidia kutengeneza msingi wa uaminifu, kujiamini na mawasiliano ya wazi. Watoto hujifunza dini kwa kuwatizama wazazi na kwa kufanya ibada kwa pamoja. Kama tabia nzuri zitapandikizwa kwa watoto kabla ya kuingia kwenye ulimwengu mwingine, ni wazi kwamba watafanya mambo yale yale watakapokuwa wakubwa.

MIAKA 7 – 14

Huu ndio umri wa mwanzo wa kupata elimu na mwanzo wa kupevuka. Jinsi wavulana na wasichana wanavyozidi kukua ndivyo wanafanana zaidi na zaidi na wanaume na wanawake. Mabadiliko haya yanaanza kati ya umri wa miaka 9 na 13 kwa wasichana, na kati ya miaka 11 na 15 kwa wavulana. Hiki ni kipindi cha ujana, umri wa mtoto hukua na kuwa mtu mzima na kuweza kupata mtoto.

Mabadiliko mengi ya kimwili, kiakili, kihisia na kiimani hutokea kipindi cha ujana. Watoto hugundua kuwa wanaonekana tofauti, hujisikia namna nyingine na kufikiri kwa namna nyingine kinyume na miaka ya nyuma.

Msichana ambaye anaukaribia ujana ghafla anaweza kuongezeka uzito na pia urefu maandalizi ya mabadiliko ya mwili. Nyonga zake na matiti huanza

kuongezeka. Huota nywele za kwapani na sehemu za siri. Mvulana naye huwa na mabadiliko katika mwili na hula sana. Mabega yake huanza kuongezeka. Huota nywele za kwapani, sehemu za siri, kidevuni na kifuani. Sauti huwa nzito kama watu wazima. Wote wavulana na wasichana hugundua kwamba kutokana na kukua sana kila mwezi viatu huwabana. Muda huu mzazi anatakiwa kusisitiza mtoto kuswali tofauti na hapo kabla.

MABADILIKO YAFUATAYO HUTOKEA (UMRI WA MIAKA 7 – 14)

- Watoto huwa na tabia za ukosoaji; kushikwa hasira haraka na kuwa na hisia kali.
- Watoto huwa na mwingiliano na marafiki wao, ambao huiga/huchukua mila na maadili yao. Wakati huu ni vizuri wazazi wawasaidie kuwaelekeza kazi za kijamii.
- Watoto huwa na aibu, hivyo wanatakiwa kutiwa moyo ili waweze kuwasilisha mawazo yao na lazima yaheshimiwe.

- Misuli ya mwili hukomaa kwa haraka na huanza kushiriki katika michezo (mfano kukimbia, kupanda, kuogelea, kucheza mpira wa miguu na kikapu.
- Hujitegemea wenyewe katika kula, kufua na usafi wa mwili. Ni muda wa kuwafundisha adabu za kula, kunywa na kushirikiana na watu. Anza kuwafundisha dua mbalimbali ya kila tendo. Huu ni muda wa kuchanganyikana na jinsia tofauti. Hupendelea kukaa na watu wa jinsia yao. Wasiruhusiwe kuangalia michezo katika TV, magazeti na vitabu vinayoenda kinyume na maadili. Baada ya kufikisha umri wa miaka 10 wasilale pamoja watoto wa jinsia tofauti.

Kipindi cha kupata hedhi kwa wasichana (kuanzia miaka 11-13)

Wasichana wengi huanza kupata hedhi kati ya umri wa miaka 11 na 13 (huanza kuona siku zao). Kwa muda wa siku 3 hadi 7 kila mwezi, kiasi kidogo cha damu hutoka katika uke. Hii ni ishara ya kwamba mwili tayari unaweza kupata mtoto. Kutokwa damu ni jambo la kawaida na halina madhara (hii ndiyo asili ya mwili kwani binadamu ndivyo alivyoumbwa). Damu hii ni sehemu ndogo ya utando wa uterasi. Ovari mbili huanza kupevusha yai moja kila mwezi na kutengeneza damu nyingi katika sehemu laini ya uterasi, sehemu ambapo mtoto anaweza kutunzwa. Bila manii ya mwanaume, yai haliwezi kukomaa na ukuta mwembamba huzeeka, kwa hiyo uterasi huitoa kwa njia ya hedhi. Kati ya siku 27 – 30 tendo hili la asili hutokea kila mara.

KIPINDI CHA MAUMIVU

Wanawake hulalamika juu ya kutojisika vizuri wakati wa hedhi. Tatizo hili linaweza kukaa kwa muda na linaweza kukaa kwa muda mchache au mwingi.

Dalili zake zinajumuisha ; kuvimba, maumivu makali, matiti kuuma, kipandauso, kuvuja damu nyingi, kuwaza na kuchoka. (KALB 2003)

Msichana anapopata hedhi kwa mara ya kwanza, kwake linakuwa ni tukio muhimu. Inamaanisha kuwa amefikia utu uzima na tayari anakuwa ni kijana wa kike. Tangu muda huu analazimika kufanya mambo yote yanayohusu ibada (kama ilivyo kwa watu wazima wengine) kama vile kufunga, kusali na kujisitiri mbele ya wanaume wasiokuwa maharimu wake. Zaidi ya nusu ya wanawake hujisikia vibaya pindi wanapokuwa katika hedhi. Hupata maumivu makali, kuchoka sana na kuwa na hasira. Allah amewasamehe kufunga mwezi wa Ramadhani pindi wanapokuwa katika hedhi ingawa ni lazima kuzilipa siku walizokula baada ya Ramadhani. Pia wamekatazwa kuswali, kukaa msikitini au kugusa Qur'an pindi wanapokuwa na hedhi. Hawatakiwi kulipa swala walizokosa kuswali baadaye. Pedi za kike hutumika kuzuia damu ya hedhi ili nguo zibaki zikiwa safi. Pindi mwanamke anapotoka katika hedhi ni lazima aoge josho la kisheria ili ajisafishe kwa ajili ya swala.

Miaka 13 – 15 : Pindi wavulana wanapopevuka

Wavulana hutokwa na shahawa pindi wanapopevuka na kuwa vijana wa kiume. Mara kwa mara wanapoota usiku uume husimama na kutokwa na shahawa. Huu huitwa usiku wa ndoto kwa sababu shahawa huwa katika hali ya maji maji na kuitwa manii na pindi yanapotoka huchafua nguo ya ndani. Haya ni maji halisi na sio mkojo na hakuna haja ya kuionea aibu. Hii inamaanisha kwamba mvulana amekuwa mtu mzima na kimaumbile

anaweza kuwa baba. Tangu wakati huu ni lazima kwake kufanya ibada za lazima (kama vile zote zifanywazo na watu wazima). Baadhi ya wavulana hawapitii katika tendo la kujiotea, kulingana na sheria ya Kiislamu mara wanapotimiza umri wa miaka 15 wanakuwa ni vijana wa kiume, au pindi wanapokuwa na dalili zote za kimaumbile kupevuka (kama vile kuwa na sauti nzito). Wanapotimiza umri wa miaka 12 kwa vyovyote iwavyo, wavulana na wasichana lazima waswali na kufunga hata kama maendeleo ya dalili za kupevuka zitakuwa zinatoka taratibu.

> Una mtoto mzuri sana, lakini ubaya wake akifikisha umri wa miaka kumi na tatu mazingira mabaya yanamchukua
>
> **Jill Eikenberry (Brown 1994)**

Baadhi ya wavulana na wanaume hushika sehemu zao za siri ili zisisimke na kusimama ili shahawa zitoke kwa kufanya masaji kwa sababu ya kufurahia kumwaga. Hii inaitwa kupiga punyeto. Tabia hii inahimizwa katika baadhi ya jamii na kwao siyo kosa (haramu). Usagaji kwa wanawake na kupiga punyeto kwa wanaume ni vitu vinavyopingwa na Uislamu. Yeyote anayezisisimua sehemu zake za siri kwa makusudi lazima achukue udhu upya kabla ya kuswali. Yeyote aliyepiga punyeto lazima ajisafishe kwa josho la kisheria ili awe tayari kuswali.

MIAKA 14 – 21

Ni katika hatua hii sauti huwa kubwa na nzito kwa wavulana na nyororo kwa wasichana. Kwa wavulana misuli hukomaa na matiti kwa wasichana hukua na mwili kuongezeka. Kwa wavulana miguu na mikono hurefuka, mabega hutanuka na nyayo huongezeka. Huota ndevu, pia nywele huota kwapani na sehemu za siri. Kurefuka kwa miguu na mikono kwa muda usioeleweka husababisha uzito katika kutembea na kubeba vitu. Huhitaji utulivu na kujiweka sawa kimwili.

Kuwaelewa Vijana

Katika kufanya maamuzi, vijana wanaweza kufuata hisia zao bila kutumia busara. Nyoyo zao zinaweza kushinda akili, mihemuko na hisia vinaweza kutawala mawazo na fikra. Vijana ni woga; wanatumia muda mwingi kujiogopa na wanavyoonekana. Katika meno yao wanavaa gango ili kukaza meno, wanaota chunusi usoni na wanaogopa kwamba labda ni warefu, wafupi, wanene sana au wembamba sana. Mabadiliko yote ya mwili yanaweza kuwafanya kuwa na wasiwasi na kutojiamini. Wanaweza kuogopea taaluma yao hapo baadaye na aina gani ya elimu anayopaswa kupata au

shule gani ya kwenda na nani atamuoa/kuolewa. Haya maamuzi yote yanaweza kumfanya kijana audhike na awe na wasiwasi.

Homoni zinazosababisha mwili kukua haraka zinaweza pia kuleta mabadiliko ya hali; wavulana wanaweza kujihisi kuchoka au hasira bila sababu na wasichana wanaweza kulia au kuudhika kwa sababu ya mambo madogo. Wakati mwingine vijana wadogo hutakiwa kushughulikiwa kama watu wazima lakini wanataka kuonekana kama watoto. Ingawa fikra hizi zinaweza kuchanganya, ni za kawaida ijapokuwa haziwezi kuzuiliwa. Watu wenye afya hujifunza namna gani ya kujali afya zao na kufikiria mara mbili mbili kabla ya kuongea na kutenda.

Kwa mujibu wa Avicenna, lazima tuanze kufundisha Qur'an mara tu mtoto anapokuwa tayari kuipokea kimwili na kiakili. Mfundishe herufi na msingi wa dini. Pia chagua mashairi na umfundishe katika somo husika, kusifia elimu na kulaani ujinga, wema kwa wazazi, kuwatendea mazuri wengine na kujali na kuwasaidia wadhaifu na maskini. Pindi mtoto anapomaliza kujifunza Qur'an na lugha, pia ni muhimu aelekezwe katika jambo alipendalo na shughuli ambazo zinaendana na kipaji chake na matakwa yake (**Al-Ibrashi 1976, katika Kiarabu**).

Kwa upande wa faida, kumbukumbu na uwezo wa kufikiri huanza kufanya kazi vizuri kati ya umri wa miaka 13 au 14, na vijana wanaweza kujifunza mambo magumu ambayo ilikuwa ni vigumu kuyaelewa hapo kabla. Ni muda mzuri wa kujifunza ujuzi mwingi ambao utahitajika katika maisha kama vile kupika, kuwatunza watoto, na kuyaweka sawa mambo ya nyumbani. Vijana hujifunza mambo ya kijamii kama vile namna ya kuongea na kushirikiana na wengine na kushirika katika taratibu tofauti. Wanajifunza namna gani ya kubeba majukumu yao wenyewe na ya wengine na wanaweza kufanya kazi za muda wakati wanaendelea na elimu yao au pia kuanza kufanya kazi za ziada moja kwa moja au kujitolea. Uislamu unaelekeza njia mbalimbali kwa vijana za kujikinga katika hatua hii, kama vile :

- Kuinamisha macho unapokutana na jinsia tofauti
- Kufanya mazoezi ili kupata nguvu
- Kufunga Jumatatu na Alhamis na funga na nyengine.
- Kuomba ruhusa kabla ya kuingia katika nyumba ya mtu yeyote
- Kujizuia kukaa mahala pa uficho kwa jinsia mbili tofauti
- Kaka na dada lazima vitanda vyao vitenganishwe (wanaweza kuwa chumba kimoja) baada ya miaka 10. Inapendeza kuona kwamba nchini Uingereza, sheria za nyumba zinawataka watoto walio zaidi ya miaka 10 wa jinsia tofauti wawekwe vyumba tofauti (sheria ya nyumba ya mwaka 1985). Hili linaweza kuulizwa sana, kama sheria hii itafanyiwa kazi kote, nyumba zitajaa ulimwenguni.

Kwa upande wa kinyume na maumbile, mambo muhimu ni vizuri kutazamwa:

- Vijana huonesha utofauti: Vijana wanahitaji muda wa kukaa faragha peke yao. Wanavyozidi kukua huanza kufikiria kuwa; mimi ni nani? Kwa nini niko hapa? Maisha ni nini? kwa nini kuna matatizo mengi ulimwenguni ? Ni muda gani ambao vijana wadogo huuliza kuhusu mambo mengi waliyojifunza na kutafuta majibu na mawazo mapya? Wakati mwingine huu unakuwa muda wa mvutano na mabishano na wazazi. Vijana huwa imara kati ya umri wa miaka 16 na 19. Kipindi ambacho mtoto huwa mtu mzima (11 – 19), ni kirefu na kigumu ambacho kinahitaji uvumilivu na uelewa kwa kila mmoja katika familia.
- Vijana hujenga tabia ya kufikiria. Huanza kubuni na kuwaza. Wanaweza kuwaza tatizo na baadaye kutafuta suluhisho. Kinyume na miaka yao ya nyuma wakati ambapo walikuwa wakifikiria haraka wakati uliopo, wakati huu wanaweza kujishikiza zaidi na uhalisia wa muda: uliopita, uliopo na ujao. Wanatambua maana ya siku, juma, miezi, miaka na karne. Huanza kufikiria kuhusu historia. Hivyo maswali yao yanaweza kupita zaidi kwenye vitu na kuhamia kwenye chanzo cha maisha, uhalisia wa maisha ya baadaye, lengo na maana, ushujaa na maadili, mwanzo na mwisho wa dunia na maisha ya sasa na ya mbinguni.
- Vijana hujenga dhana ya udini: Ujana huitwa kipindi cha kuamka kidini, pindi vijana wanapotetea hoja zao madhubuti kuhusu pepo na moto, dhambi na toba, kufufuka na maisha ya milele, kudra na majaaliwa na uhuru na matakwa. Wakati wa umri wa miaka 20 na zaidi huwa imara zaidi na lengo zaidi la maisha kwa mwonekano.
- Vijana hujiegemeza katika ndoto za mchana na za kushangaza: ndoto za mchana huchukua nafasi katika kipindi hiki. Ni kipindi muhimu ambacho matakwa ya ujana hujionesha. Ni moja ya hulka ya makuzi ya kiakili, ambalo ni tukio la kawaida halifanywi kupita kiasi (ni muhimu kutozidishwa katika maisha ya kawaida na ya kitaifa).
- Vijana hujihusisha na kuwakosoa wengine, wakianza na wazazi wao. Wanaweza kuwakosoa wazazi kwa nguo zao, chakula, ladha, namna wanavyowalea ndugu zao na kuwafananisha na wazazi wenzao. Wanaweza pia kukosoa shule, jamii na serikali na kupigania msingi wa mabadiliko ya jamii.

Je umewahi kujiuliza kwa nini maandamano mengi makubwa yanayofanywa katika nchi mara nyingi yanafanywa na wanafunzi? Sawa yawe yametokea Uturuki , Misri, Malaysia, Indonesia, Irani, au Marekani…..
Hii ni kwa sababu vijana wana nguvu za kutosha, hisia kali, shauku na wanaamin katika maamuzi yao ya kuleta mabadiliko au msimamo mkali. Tuna mengi ya kufanya dhidi ya hatua za maendeleo ya makuzi.

- Vijana huwa waigaji: Uigaji ni miongoni mwa jambo la kawaida kwa vijana linalowagharimu kutokana na kukosa uzoefu wa maisha.

Kudhania + Kukosa uzoefu = Udhanifu

- Kanuni za maisha za ujana hupingana na matakwa ya wazazi na jamii hasa, wakati fikra za ujana na suluhisho zinaendelea kupingwa bila maelezo ya kuridhisha. Vijana wanaweza kukata tamaa na kuchoka na mwishowe hutengwa na kuwafarakanisha. Vijana wadhanifu huonekana hawana msaada wala maana, na wanaweza kupoteza kujiamani na uaminifu kwa wengine.
- Vijana hujihisi kupoteza: vijana hukumbana na uchaguzi mwingi maishani. Pamoja na hayo kwa sababu ya kufanya maamuzi binafsi bila kuwahusisha wazazi au watu wenye uzoefu, hushindwa kufanya maamuzi sahihi. Kinachohitajika katika umri huu ni kutengeneza mazingira ya kuwasaidia kwa namna fulani, ambayo hayawabani ili kufanya uamuzi sahihi.
- Vijana hujenga dhana ya kufaulu: Dhana ya ufaulu inahitajika kuwahakikishia kukamilisha baadhi ya ndoto zao. Majukumu ya wazi yanawasaidia kufanikiwa. Ukosefu wa majukumu huwafanya wajisikie kutengwa na hawana maana. Kuwapa majukumu mengi au magumu huwafanya wajisikie kutoweza na kushindwa. Uzani wa mambo lazima utafutwe.
- Vijana wana uwezo wa kuhifadhi: Kuna njia mbili za kawaida za kuhifadhi; kuhifadhi kwa kurudia rudia na kuhifadhi kwa kuelewa (moja kwa moja au kinyume chake). Njia ya moja kwa moja ya kuhifadhi kwa kurudia rudia ni kusoma kifungu ukiwa na uelewa mdogo au bila uelewa wa mada. Uelewa usiokuwa wa moja kwa moja ni kuelewa maudhui na kuihusisha na maana ya somo jingine pamoja na kuondoa mahusiano mapya na baadhi ya vipengele vya maudhui. Maendeleo ya kuhifadhi kwa kurudia rudia huanza utotoni na huchukua takribani miaka 15 (al-Sayyid 1975). Huanza kupungua uzito wake, kasi na ukubwa. Licha ya hivyo uelewa usiokuwa wa moja kwa moja huanza baadaye, kwa sasa huendelea na kukua na kuendelea kwa kipindi cha umri wa ujana hadi umri wa kati.

Uwezekano: Mtiririko wa Matukio

Jambo moja huzaa lingine kama ifuatavyo:
Fikra za ujana+kukosa uzoefu →Kupingwa na wazazi na jamii →Mgogoro → Kujitenga → Kutengwa→Mfadhaiko → Kutoaminiwa → Kukosa msaada →Kukata tamaa → Kutojali → Kukubali → Kutobadilika

- Kilichofunzwa kipindi cha utotoni hudumu kwenye fikra za mtoto mfano wake ni kama kuandika kwa kunakishi kwenye jiwe na kilichofunzwa ukubwani ni kama kuandika juu ya tabaka la maji (hufifia haraka).

MIAKA 21 – 40: UJANA KATIKA UTU UZIMA

Huu ni umri wa kubalehe, nguvu na kuzalisha kwa watu wengi. Yusufu Ali katika karne ya Ishirini na Umar Ibn al-Khattab katika karne ya Kumi na Saba waliamini kwamba akili inakuwa vizuri katika umri wa miaka 40, baada ya hapo maendeleo huegemea katika ujuzi.

MIAKA 40 – 65 RIKA LA KATI

Miaka ya kati ni wakati wa kuja kwa maendeleo si kwa sababu ya kukuwa kwa uhalisia bali ni kwa elimu, kujifunza na uzoefu. Udhaifu (*da'if*) wa kimaumbile huanza kuonekana.

MIAKA 65 NA ZAIDI: UZEE

Uzee huwa na mwisho wake pindi ambapo huwa ni umri wa kudhoofu (umri wa udhalili), wakati ambapo maarifa na kumbukumbu huanza kupungua. Kama mtu ataishi muda mrefu, ujuzi wake hupungua. Ni kama ubongo wa kompyuta ambao hufutwa mara kwa mara. Ugonjwa wa Alzheimer's huwaathiri wazee kwa kuharibu kumbukumbu zao. Jina lingine la hatua hii ni *shaykhukhah* (utu uzima), *da'fan* (udhaifu) *wa shaybah* (na uzee).

Mzunguko wa maisha huanza kwa kuzaliwa mtoto (ambaye hajui kitu chochote, lakini ana sikia, anaona na ana mapenzi. Allah anamtaka mwanadamu amshukuru. Mtoto hutoka katika udhaifu na kuwa imara kisha hurudi katika udhaifu wakati wa uzee (*shaybah*). Kati ya kuzaliwa na uzee mwanadamu hupata maarifa na Allah humuhimiza kuwa na ufahamu na hekima. Katika hatua ya mwisho ya maisha, mwishoni mwa safari hii, watu lazima wawe wachaMungu na kujiepusha na madhambi makubwa. Katika umri wa miaka 60, watu hawana sababu ya kutenda maovu kama alivyosema Mtume (Swalla Aaahu Alayhi wa Sallam)

"Katika umri wa miaka 60, Allah mwingi wa kusamehe humpa mwanadamu udhuru." (Al-Bukhari)

Jinsi tunavyokuwa wazee, ndivyo jinsi uwezo wa kumbukumbu unavyopungua lakini uwezo wa kufikiri na kutafuta suluhu hubaki imara. Hakika hii ni baraka!

Walio na bahati na baraka ni wale ambao huanza kumtukuza Allah mapema katika maisha na hukua katika maadili ya kujua na kuelewa asili na lengo la kuumbwa mwanadamu katika ardhi hii.

Mtoto hakui kwa mujibu wa saa. Kila mtoto hukua kwa namna yake na kwa sampuli yake. Saa pekee ya mtoto ni pale mzazi atakapomjali.

MTOTO NI WIGO WA FURSA ZETU

Moyo wa mtoto ni mtupu na msafi, kiasili unamuelekeo wa kupokea kitu na unavutiwa na kila kitu (Imam Ghazal).

Mtoto yu tayari kupokea taarifa zote na maelekezo yote yanayoelekezwa kwake (Ibn Miskawayh).

Hii ni fursa adhimu kwa mzazi kushiriki na kumfundisha mtoto kwa kiwango cha juu iwezekanavyo!

Kutilia mkazo hatua za makuzi

KUNYONYA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI YA KWANZA: Hii ni hatua ambapo hatua muhimu za ubinadamu hujengwa. Matokeo yake ni mtoto mwenye afya, kwa pande zote kimwili na kihisia. Wakati wa utoto, sehemu ya kati ya ubongo wa mtoto, sehemu ya muunganiko wa ubongo na sehemu ya kupeleka taarifa katika ubongo (katika mfumo wa trilioni hadi trilioni za nyuroni) hutengenezwa. Ujasiri, ubunifu, mapenzi, uaminifu, mtazamo, lugha na mantiki huanza kuundwa katika hatua hii. Ziada ya hapo faida za kitabibu zisizohesabika wakati wa kunyonya, mama huwapa watoto wao faida nyingi za hisia. Mapenzi, huruma na kuridhika hutengenezwa na uangalizi wa miaka ya kwanza miwili. Pia uangalizi wa mama una faida kubwa kwa saikolojia ya ndani yenye mafungamo na mtoto.

MAPENZI NA KUMUOGOPA ALLAH: Watoto wanatakiwa kuoneshwa mapema mapenzi, matumaini na thawabu kutoka kwa mwenye huruma. Dhana ya woga, adhabu na moto lazima visubirishwe hadi umri wa ujana wakati ambapo mtoto ataelewa dhana ya kufikirika na ya picha. Kuwajibika kwa watoto wao kwani kumbukumbu zao huathiriwa sana katika miaka ya mwanzo, umuhimu wa uhuru wa watoto, ubunifu na fikra vinakoma pindi anapoogopeshwa kuhusu moto. Kuwatisha watoto na kuwaogofya wao huwaondolea ujasiri wao, kubeba majukumu mazito, kufanya mambo ya hatari na maamuzi na kujiamini.

KUHIFADHI: Sheikh Muhammad al-Ghazaly katika *Kayfa Nata'amal Ma'a al-Qur'an* (1992) ameibua swali kwani ni wakati gani wa kusisitiza kuhifadhi Qur'an na wakati gani wa kuzama kwenye kuielewa. Alikuwa akitafuta jibu sahihi. Kwa sasa inaonekana kuhifadhi ni muhimu kusisitizwa zaidi ya kuelewa hadi umri wa ujana na pia kuanzia mwanzo mwa ujana ni muhimu kusisitiza uelewa na kufasiri. Namna hii ubongo utapata manufaa ya kutumika vizuri kwa matunda ya baadaye kwa kuhifadhi mapema na baadaye kuelewa.

NJIA ZA DA'WAH: Hizi ni muhimu zifanywe katika umri wa ujana wakati ambapo watoto wanaweza kupata nadharia za kufikirika kama vile pepo na maisha ya baadaye. Nguvu zao na hisia katika hatua hii ni kubwa na mapenzi yanaweza kupelekwa pahala panapostahili, malezi ya kiroho na kujitolea kwa Mungu mmoja. Hisia za vijana zinahitaji kuwekwa katika usawa kwa busara. Wanatakiwa kuimarisha ibada zao kwa elimu na kukabili hisia kipindi cha matatizo na kujiegemeza katika kumwamini Allah (*tawakkul*).

UMAKINI KATIKA KUWAKOSOA VIJANA KATIKA KIPINDI CHA KUBALEGHE: Vijana lazima wafunzwe kwa hekima ili wasiathiriwe fikra zao na kudhuru heshima zao. Lengo ni kulinda maendeleo yao siyo kuwafanya wapoteze kujiamini. Kutia moyo na nguvu ni vitu muhimu katika hatua hii. Wivu na kufananisha vipo akilini mwao kama vijana, kuanzia hapa kunahitajika kufanya usawa katika kuwalea ndugu zao wote kwa haki na usawa.

UJENGAJI WA UTAMBULISHO NI MUHIMU UKAMILISHWE: Kipindi cha ujana, kwa hili ni pale vijana wanapoanza kujitambua wenyewe, jamii, ulimwengu na metafizikia, ghaibu (mambo yasiyoonekana). Huu ni muda wa kujadili dhana sahihi ya *tawhiid* (Mungu mmoja), *istikhlaf* (Uongozi wa Mwanadamu), *imran* (Ujenzi wa Ustaarabu), mtazamo wa kidunia, lengo la maisha na uhusiano kati yako na watu wengine, mazingira na Muumba.

KUJIFUNZA LUGHA YA PILI: Hili lisisubiriwe hadi umri wa ujana. Inabidi lianze kabla ya umri wa miaka 10. Huu ni wakati ambapo sauti ya lugha huanzishwa katika neva ya ubongo na mahusiano. Ni vizuri kuanza mapema ili aweze kutamka sauti zote za alfabeti kama mzaliwa. Watoto huwa na uwezo mzuri wa kusoma lugha mbalimbali bila ya ugumu wowote kipindi cha mwanzo wa utoto. « Ubongo wa watoto una vipaji vikubwa vya kupokea lugha na yule ambaye anazungumza lugha mbili katika umri mdogo itakuwa rahisi kwake kujifunza lugha ya tatu au ya nne baadaye. Ukilinganisha na watu wazima

au hata wanafunzi wa shule ya juu ya sekondari, vijana wadogo ni wazuri kujifunza lugha ya Kijerumani kwa matamshi yaliyo karibu sawa na mzaliwa (Glod 2006). Hii pia inatokea pia katika kujifunza Kiarabu na lugha nyingine.

Kijana wa Kiajemi Hafidh mwenye umri wa Miaka 6

(Hafidh ni yule ambaye anaweza kusoma Qur'an yote kichwani ; ingawa anaweza kuwa haelewi Kiarabu).

Sayyid Mohammad Husayn Tabatabai, ambaye lugha mama yake ni Kiajemi, alihifadhi Qur'an akiwa na umri wa miaka 6.

Baba yake anasema, alikuwa na miaka 2 wakati nilipogundua kipaji chake'. Mtoto alijifunza kwa kumsikiliza mama yake ambaye pia ni Hafidhwa. Alihifadhi aya kwa kusikiliza mara moja au mbili.

Alisoma Qur'an kila siku ili kulinda kile alichokihifadhi. Sehemu alizozipenda sana ni historia za Mitume, hasa hasa Yusuf. (Muslim News, 1998).

Ni maajabu ya Qur'an kwamba mtu ambaye haelewi kiarabu anaweza kuihifadhi kutoka ukurasa hadi ukurasa! Leo hii, maelfu ya watoto ambao wana chini ya miaka 10 wa jamii tofauti wamehifadhi Qur'an katika asili yake ya Kiarabu.

Hafidh wa miaka 4½ kutoka Syria

Mtoto mdogo katika rekodi (miaka 4½) ambaye alihifadhi Qur'an yote ni Abdullah Ahmad Shghalah kutoka Aleppo, Syria, alizaliwa mwaka 1996. Alianza kuhifadhi Qur'an akiwa na umri wa miaka mitatu na kuimaliza akiwa na miaka minne na nusu. Akiwa na umri wa miaka mitano pia alihifadhi hadith 1000 za Mtume (s.a.w) na zaidi ya mistari 1000 ya mashairi.

Historia ilianzia katika duka la baba yake, alipomgundua mtoto wake wakati akiwa na umri wa miaka miwili akiimba wimbo wa Ummu Kulthum « Zalamuni al-Nas » kwa kuusikia mara moja kupitia sauti ya juu ya redio ya jirani. Wazazi waliamua kumuelekeza katika njia ya kuhifadhi Qur'an. Walianza kumsomesha sura chache Abdullah ambaye alizihifadhi kwa kusomewa mara mbili. Baada ya miezi michache, Abdullah pia alitamka maneno vizuri kwa kuzingatia sheria sahihi za *tajwid*.

Akiwa na umri wa miaka mitano, Abdullah alipata zawadi ya kwanza katika mashindano ya kitaifa ya Syria, ambapo washiriki walikuwa na umri wa miaka 14 hadi 30. Alikuwa ni mtoto mdogo wa kwanza kushika nafasi ya kwanza katika mashindano ya Qur'an. **(Al Usrah Magazine, 2005)**

Kuhifadhi: Mashariki na Magharibi

Jaribio la nchi za Kiislamu kuwasajili watoto ambao hawajaenda shuleni katika vituo vya kuhifadhi Qur'an linaleta faida kubwa. Ingawa Waislamu walio wengi (nne ya tano) hawaelewi Kiarabu, wanaweza kuhifadhi Qur'an bila kuelewa wakilenga kuihifadhi katika ubongo kipindi cha mapema utotoni. Tafsiri inaweza kuja baadaye kipindi cha miaka ya ujana. Siku hizi, kuhifadhi kama mfumo hautiliwi mkazo sana Magharibi, iwe ni kuhifadhi Biblia, mashairi au tamthiliya. Licha ya hivyo, Wakristo wa zamani walikuwa wakihifadhi Biblia. Baadhi ya watoto wa Kikristo wa Arabuni wamehifadhi Qur'an, inawasaidia sana katika mawasiliano hasa katika misamiati, lugha na ubongo kuwa na uwezo wa kutunza vitu na kuvitoa.

Kuhifadhi Qur'an mapema husaidia katika utu uzima wa shule

Dkt. Yusuf Khaleefa (aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sudan) alisema: Ujuzi wetu kuhusu Hafidh kutoka katika madrasa za vijijini na shule za Sudan zilithibitisha kwamba yule aliyehifadhi Qur'an anakuwa na uwezo mzuri kusimulia, kutunza na kufahamu mambo magumu na matatizo. Wanafunzi hawa, ambao hawakuwahi kuhudhuria shule za kawaida, walikuwa wakipewa kozi ya maandalizi ya miaka 2 kwa upande wa sayansi ili wawe na sifa za kujiunga na vyuo. Asilimia tisini yao walifaulu mtihani wa kujiunga na vyuo vya serikali. Walikuwa pamoja na wanafunzi waliohudhuria shule za umma kwa miaka 12 (Abdullah 1994) alikuta kwamba kuhifadhi udogoni kunaweza kuimarisha hifadhi yao miaka ya baadaye maishani.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 31: USHAURI KWA WAZAZI

Baba na mama: Jadili mambo yafuatayo kisha amua namna gani ya kuyafanyia kazi kwa watoto wako.

- Wape watoto zaidi ya walivyotaraji na ufanye kwa uchangamfu.
- Usiamini kila unachosikia au kutumia kila ulichonacho.
- Unaposema 'nakupenda' maanisha hivyo.
- Unaposema 'Samahani' muangalie mtu usoni.
- Usicheke ndoto ya mtoto wako hata siku moja. Mtu ambaye hana ndoto hana lolote.
- Katika kutokubaliana, usiegemee popote. Kutoitana majina mabaya.
- Usiwahukumu watu kupitia ndugu zao.
- Yeyote atakayekuuliza swali ambalo hutaki kujibu, tabasamu na uliza 'kwa nini unataka kujua?'
- Mapenzi makubwa na malengo makubwa huenda sambamba na hatari kubwa.
- Sema Mwenyezi Mungu akurehemu *"yarhamkallah"* wakati utakaposikia yeyote amepiga chafya.
- Utakapokosea, usikate tamaa.
- Jiheshimu; waheshimu wengine na wajibika kwa matendo yako.
- Usikubali ugomvi mdogo ulete madhara katika uhusiano mkubwa wa familia.
- Utakapogundua umefanya kosa, chukua hatua za haraka kurekebisha.
- Tabasamu wakati wa kupokea simu. Mpigaji atasikia katika sauti yako.
- Wakati fulani tenga muda wa kukaa peke yako.

SURA YA TISA

- **NJIA ZA AFYA KWA MTOTO**
  Usafi, Lishe, Mazoezi ya Viungo na Kulala

SURA YA TISA 194

Njia za Afya kwa Mtoto: Usafi, Lishe, Mazoezi na Kulala 194

Afya kwanza 196
Wakati wa ujauzito 197
Baada ya kujifungua: Mjadala kuhusu chanjo 198
Hoja dhidi ya chanjo 199
Usafi na Elimusiha 200
Wanaume, wanawake na usafi 201
Afya: Baadhi ya mifano katika Uislamu 201
Usafi katika vyoo 202
Nywele na kucha 203
Lishe 205
Matatizo ya unene uliopitiliza 206
Maoni ya Imam Al-Ghazali juu ya tabia za kula 207
Ukweli kuhusu watoto na lishe 208
Mfano wa chakula kwa mtoto wa miaka 2 Hadi 10 209
Maswali yanayoulizwa sana 209
Mwongozo wa Qur'an kuhusu chakula 216
Watoto na mazoezi ya viungo 218
Watoto na Viatu 219
Namna ya kukuza juhudi kwa watoto 219
Ratiba za mazoezi zilizokokotezwa 221
Kulala 222
Vileo: Unywaji & uzuiaji wa dawa za kulevya 224
Watoto na vishawishi 225
Alama za awali za kumgundua mtumiaji madawa 225
Vitu atakiwavyo mzazi kufanya ili kuzuia ulevi 226
Ushauri wa mlevi kwa vijana 228
Kuvunja sheria 230
Mwili ni amana: Ni neema isiyo na mbadala 232
Kazi za kufanya

Mgonjwa alibaki akilalamika juu ya maumivu yasiyokwisha kwa daktari. Mwisho daktari mmoja alimwambia "umepoteza muda mwingi na pesa ukilinda rasilimali zako za kibiashara na majengo lakini uliiacha rasilimali yako muhimu – mwili wako!"

Afya kwanza

Kauli ya wahenga "kinga ni bora kuliko tiba" siku zote itakuwa ni kweli na ni kitu ambacho wazazi wanahitaji kukipa kipaumbele. Hawahitaji kusubiri wakati wa maafa na kuanza kuhangaika. Kosa lolote kubwa ambalo wazazi watafanya kuhusiana na afya za watoto wao inaweza kuharibu maisha yake ya baadaye. Wazazi wana majukumu mara mbili kuhusiana na afya zao na za watoto wao. La kushangaza, watu wengi badala ya kushughulikia kinga, hupoteza muda zaidi katika kitengo cha wagonjwa mahututi. Kufanya jambo linalohitajika katika wakati muafaka halina gharama na ni rahisi na matokeo yake huthaminiwa zaidi. Kinyume na hivyo huleta shida na matatizo. Hatari zaidi, pamoja na hayo jambo la kudhuru afya ya mtoto huwa la kudumu. Sio rahisi kufikiri kiasi cha hisia za hatia mtu azipatazo kwa kosa lililofanywa dhidi ya kuacha kushughulikia afya ya mtoto wake, wakati ugonjwa unapotokea ambao ungeweza kuzuilika kwa urahisi. Itakuwa umekwishachelewa kufanya jambo lolote kuudhibiti ugonjwa, haijalishi kiasi gani mtu atajaribu na kiasi gani atakipoteza.

Kwa hiyo afya inabidi ipewe kipaumbele kikubwa. Siyo rahisi kuwa na familia nzuri, kazi nzuri, elimu nzuri au/na wakati mzuri kama mtu hana afya nzuri. Zaidi ya hayo, akili nzuri hutokana na afya nzuri ya mwili na makuzi muhimu ya akili na saikolojia ya mtoto yatatokea endapo mtoto ana afya nzuri ya kimwili.

Wazazi wanahitaji kujitolea kwa ajili ya watoto wao; maji safi, choo safi, chakula chenye lishe, kupata matibabu kwa wakati, mazoezi ya mara kwa mara na kumtembelea daktari. Kumkuza mtoto mwenye afya huanza kabla ya kuzaliwa, mtu inabidi achague mchumba mwenye afya.

Wakati wa ujauzito

Mama mwenye mimba ana majukumu makubwa kwa kijusi chake. Chakula chenye lishe, kulala vizuri, kumtembelea daktari mara kwa mara na mazoezi ni muhimu wakati wa kujifungua. Lazima azuie hatari ya kuathiriwa na bakteria pamoja na kula vitu vichafu (kama vinywaji, chakula kichafu na pombe). Uvutaji wa sigara ni moja ya vitu vyenye madhara ambavyo hatakiwi mama kufanya kipindi cha ujauzito. Kijusi hufyonza kila kitu kutoka kwa mama (virutubishi na oksijeni hupitia kondo la nyuma na kitovu), kwa hiyo kuvuta sigara hakuathiri kijusi tu kupitia uvutaji wa tumbaku bali pia huathiri mfumo wa kondo la nyuma. Soma onyo lifuatalo lililowekwa juu ya pakiti la sigara linalouzwa nchini Marekani.

ONYO LA DAKTARI

Uvutaji sigara husababisha kansa ya mapafu, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa kuvimba mapafu na kupumua kwa shida na inaweza kusababisha matatizo wakati wa kujifungua.

Mazingira yenye uvutaji mdogo: Penye Nia, pana Njia!
Mataifa yanaweza kupunguza sana uvutaji wa sigara kama wataamua kufanya hivyo. Ilifanyika Marekani.

Marufuku kuvuta sigara – Mwaka 1985 nambari ya manispaa ambazo zilikuwa na agizo la utunzaji wa hali ya hewa zilikuwa 202, mwaka 2003 ziliongezeka hadi kufikia 1631.

Pamoja na kuwepo sheria wazazi wanatakiwa kuwaweka watoto mbali na mazingira ya uvutaji sigara, ndani na nje ya nyumba.

Kama mama anataka kuepuka maambukizi ya virusi, ni muhimu awasiliane na daktari ili kuepuka kijusi kudhurika. Hii pia inatakiwa wakati wa kunyonyesha. Maambukizi yanaweza kumsababisha mtoto kuwa kipofu, kiziwi, kudhoofika kiakili, magonjwa ya akili. Kina mama lazima wapimwe damu zao wakati wa ujauzito ili kuzuia ugonjwa wa hemolitiki (ambao unaweza kusababisha ubongo kudhurika au kifo kwa mtoto).

Baada ya kujifungua: Mjadala kuhusu chanjo

Hoja kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa chanjo zinahudhurishwa hapa ili wazazi waweze kufanya uchaguzi.

Baada ya kujifungua, daktari lazima ampime mtoto, hususani macho, masikio na kupiga chafya. Wavulana lazima watahiriwe ili kuzuia maambukizi. Wazazi wengi hutambua umuhimu wa kukinga maradhi na kufuata jedwali la kinga. Pamoja na hayo, 80% yao hawako makini kana kwamba hupewa chanjo kabla ya miaka miwili. Inashangaza kwa namna tunavyokipa kifaranga chanjo ndani ya yai lenye siku tatu kabla ya kuanguliwa.

CHANJO ZINAWEZA KUFANYA MAMBO MENGI!

Magonjwa sita huua "utotoni" – surua, polio, kifua kikuu, pepopunda, kifaduro na dondakoo – huua Mamilioni ya watoto kila mwaka. Waathirika wakubwa ni vijana wenye utapiamlo ambao wana kinga ndogo ya mwili. Chanjo ya kuzuia magonjwa haya ilijulikana tangu miongo kadhaa na imeondoa tishio la magonjwa haya katika mataifa yaliyoendelea.

Karibu kila mtoto Marekani amechanjwa ili kulindwa na magonjwa ya utotoni lakini Mamilioni ya watoto katika nchi zinazoendelea wanabaki katika hali ya hatari kwa sababu hazina uwezo wa kuwapatia chanjo. Asilimia Ishirini ya watoto katika nchi zinazoendelea hawana uwezo wa kupatiwa chanjo na karibu kila mwaka watoto Milioni Tatu duniani hufariki kwa kukosa chanjo ya kukinga magonjwa.

("Kwa ajili ya watoto: Zawadi kwa afya, elimu na matumaini" Jarida la msaada, UNICEF 2003)

Wasimulie wanao kuhusu hadithi ya chanjo: "Alikuwa ni Dkt. Edward Jenner ambaye alileta dhana ya ugunduzi wa chanjo mwaka 1796, ukweli wa hadithi ya kubuni. Katika dawa kuna aina tatu ya dhana nzuri: Iliyowazi, isiyokuwa wazi na ile aina ambayo Dkt. Edward Jenner alikuja nayo. Alisikia kwa rafiki yake wa kijiji cha Gloucestershire, Uingereza, kwamba watu waliokamatwa na ndui ya ng'ombe hawakuweza mara kwa mara kuathiriwa na ugonjwa wa ngozi na aligundua kwamba ugonjwa wa kwanza ulikuwa unaua kinga ya mwili kuliko wa pili. Wazo lazima lilikuwa liwe na mantiki kwa wenzake. Wakati fulani hawakuwa na neno kuhusu "mfumo wa kukinga maradhi" na "kiini cha maradhi" kwa sababu hawakuzama kuhusu wazo hilo" (Carmichael, 2007).

Hata hivyo, Jenner ana imani na dhana yake. Kwa hiyo, je, huyo mama aliyemruhusu kumpima mwanawe wa miaka 8, James Phipps, pindi ambapo ugonjwa wa ndui ya ng'ombe ulipotokea shambani kwake wakati wa masika mwaka huo. Daktari alikusanya usaha kutoka kwa mkama maziwa aliyeathirika na kuiweka katika kiwiliwili cha mtoto huku akisubiri. Baada ya wiki sita alimdunga sindano yenye ugonjwa wa ngozi. Alisubiri tena zaidi hadi alipokuwa na hakika kuwa James hatougua. Kisha alitangaza kuanza kwa zama. Aligundua chanjo. Bila shaka, Jenner hakueleweka wakati alipotoa wazo hili, mara nyingi mabadiliko huwa hivyo.

Chanjo imeibadili dunia nzima kwa kuondoa ugonjwa wa ngozi na kwa kiasi kikubwa na kuondoa ugonjwa wa polio na surua. Chanjo ni moja ya jambo muhimu la uvumbuzi wa dawa kwa miongo miwili iliyopita na ni gharama nafuu zaidi. Chanjo haitibu maradhi, inakinga tu, jambo ambalo ni zuri. Endapo watu 100 watakingwa, hawawekwi kuwa na afya tu bali hukingwa kutokana na maradhi mengi.

Kila mwaka, chanjo huokoa maisha ya wengi. Hata hivyo, Mamilioni ya watu hawawezi kukingwa. Sehemu kubwa katika Afrika, Asia na Amerika ya Kusini, watoto hawapati chanjo yoyote inayopatikana katika nchi zilizoendelea, matokeo yake hufariki. Hakuna yeyote, pahala popote na kwa namna yoyote kuwa ana uhakika wa kwamba kumbe amekingwa dhidi ya maradhi makubwa ya dunia – Virusi vya Ukimwi (VVU), kifua kikuu na malaria, ambayo kwa pamoja huua watu Milioni Sita kila mwaka – kwa sababu pamoja na nguvu kubwa ya dawa za kisasa, chanjo nzuri kwa ajili ya hayo magonjwa haijapatikana.

Hoja dhidi ya chanjo

Watu wengi hawajui madhara ya ndani yatokanayo na chanjo za utotoni. Mjadala kuhusu chanjo umeeleza kuwa mafanikio yanayoelekezwa kwenye mipango ya chanjo kiukweli yametokana na maboresho ya usafi wa jamii (hususani kwa kuzingatia usafi wa maji na vyoo, maeneo ya kuishi yasiyo na mlundikano wa watu, lishe bora na maisha bora).

"Chanjo zote huwa na kemikali za sumu, DNA kutoka katika tishu za wanyama na mimba changa na protini katika mfumo wa uhai au virusi waliokufa na bakteria. Teknolojia ya sasa ya chanjo imeegemea kwenye sayansi ambayo ina zaidi ya miaka Mia Mbili hivyo inasemekana kwamba chanjo 'huchochea kiusalama mwitikio wa kinga' … kemikali za sumu zinaongezwa katika chanjo hutengeneza matatizo ya kinga pamoja na neva kwa sababu siyo rahisi kuondolewa mwilini, hujikusanya katika ubongo na tishu za ogani na huziharibu neva. Protini ngeni na DNA kama havijafyonzwa na kuondolewa na mfumo wa kinga, zinaweza kupenya kwa urahisi kwenye tando za seli za membreni (http:/ /www.know-vaccines.org/parent.html)

(http:/ /www.know-vaccines.org/parent.html)

Mfumo wa kinga ya maradhi huchukua miaka mingi kuimarika na hufanya hivyo kwa kukutana na bakteria na virusi (ambapo mwili hujifunza kupambana kwa kuwa na homa, kupata mafua, kutokwa na jasho na vipele). Chanjo huzuia watoto nafasi ya kupata kinga kutokana na maradhi ya maisha ya kawaida yasiyokuwa na madhara (kama vile surua, matumbwi tumbwi, rubela, tete kuwanga na kifaduro). Baada ya kupata chanjo, mwili hubaki ukiwa na tahadhari juu ya lolote ambalo linaweza lisitokee. Hivyo, mfumo wa kinga ya maradhi unaweza kuwa wa kujihami zaidi na kusababisha mzio.

Wale wanaopinga chanjo wanatoa hoja kwamba afya nzuri ndiyo njia nzuri ya kujikinga dhidi ya maradhi.

Virusi havipo "huko nje" kujaribu kutupata sisi, kama tutakuwa wazima ndani ya mwili, mwili unaweza usipatwe na homa, mafua, surua au chochote kinachotuzunguka. Njia ni KUJIJALI!

(Sinclair, 1995); (Head, 1999)

Kwa kusisitiza tunawaacha wazazi kufanya uchaguzi sahihi wa matabibu kufanya chanjo au la.

Waganga wa watoto wanashauri kwamba watoto wapelekwe mara kwa mara kwa uchunguzi katika umri wa miaka sita, nane na kumi na wanapotimiza umri wa miaka kumi na moja na zaidi wapelekwe mara moja kwa mwaka. Uzuri wa uchunguzi huu wa mara kwa mara ni kwamba matatizo hugunduliwa mapema sana na hutibiwa vizuri, kinyume na kutogunduliwa mapema na kusababisha maradhi kutotibika. Baadhi ya nchi huwafanyia wanafunzi wadogo mara kwa mara uchunguzi wa afya zao mwanzoni mwa muhula, jambo ambalo husisitizwa sana. Maradhi kwa watoto (kama vile matatizo ya kusikia, kuona au kuzungumza) hugundulika wakati wa vipimo vya afya. Wazazi lazima wajikite katika kukinga maradhi. Mbali na chanjo, kiwango cha chini kinachotakiwa ili kuwa na afya nzuri ni usafi, lishe, kulala na kufanya mazoezi.

Chanjo ni mapatano makubwa ya kiulimwengu ya kiafya

Dola 15 kwa ajili ya kumlinda mtoto. Wakati tumepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miongo miwili iliyopita katika kuwachanja zaidi ya asilimia 80 ya watoto duniani, bado zaidi ya watoto Milioni Mbili wanakufa kila mwaka kutokana na ukosefu wa huduma hii ya msingi ya afya katika vituo vya Umma.

Usafi na Elimusiha

Usafi ni jambo la muhimu la kinga kwa wanadamu la kujikinga na bakteria pamoja na maambukizi ya virusi. Kwa kawaida mikono ni zana ambazo maambukizi hupitia na kuingia mwilini (wakati watu wanaposhika macho yao, midomo, pua na masikio). Hivyo, kuosha mikono mara kwa mara kwa siku huua vijidudu.

Mwandishi wa Kimarekani Rose Wilder Lane (1886-1968) alivutia katika kazi yake, *Ugunduzi wa Uhuru*, kwamba "Watu wanamshutumu Mtume Muhammad kwa kuwa mwenye msimamo wa kidini, lakini niliona kwamba alikuwa mtu wa dini sana katika jambo moja – usafi na elimusiha".

Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallam) alisifia kutia udhu mara tano kwa siku kabla ya sala: *"ufanano wa sala tano ni sawa na mto unaotiririka mbele ya nyumba ya mmoja wenu ambapo huoga humo kwa siku mara tano"*. (MUSLIM)

Wanaume, wanawake na usafi

"Linapokuja suala la usafi wa mikono, katika nchi ya Marekani na Uingereza, wanawake ni wasafi zaidi ya wanaume. Utafiti uliofanywa na Chuo cha Michigan katika maeneo ya kupumzikia katika baa, migahawa pamoja na sehemu nyingine za Umma nchini Marekani ilibainika kuwa asilimia 15 ya wanaume hawakuosha mikono yao ukilinganisha na asilimia 7 ya wanawake ambao waliosha mikono yao. Pindi wanapokuwa wakiosha mikono yao, asilimia 50 ya wanaume walitumia sabuni ukilinganisha na asilimia 78 ya wanawake ambao waliosha mikono yao.

Utafiti ulibaini kuwa: Asilimia 5 ya watu ambao walitumia vyoo waliweza kuosha mikono yao ili kuua vimelea vyenye kuweza kusababisha maradhi. Zaidi ya asilimia 33 ya watu wote hawakutumia sabuni na asilimia 10 hawakuosha mikono yao kabisa. Utafiti ya kina uliofanyika nchini Uingereza, asilimia 99 ya watu walihojiwa maeneo ya vituo vya usafiri ambavyo kuna vyoo ambapo walidai kuwa waliosha mikono yao baada ya kwenda chooni. Hata hivyo, vyombo vya kutunzia kumbukumbu vinaonesha kuwa asilimia 32 tu ya wanaume na asilimia 64 ya wanawake ndiyo walikuwa wakiosha mikono yao baada ya kutoka chooni.

Njia pekee iliyokuwa bora dhidi ya kukabiliana na kuenea kwa maradhi ni kuosha mikono vizuri kwa muda wa sekunde 15 hadi 20 kwa kutumia sabuni na maji.

SWALI: Ni kwa namna gani mamlaka ya Hispania kipindi cha "uchunguzi" wa Waislamu na Wayahudi iliwatambua wale ambao walikuwa ni Waislamu kwa kujifanya kuwa Wakristo baada ya kulazimishwa kubadili dini?

JIBU: Kama mtu alikuwa msafi hivyo ilichukuliwa kwamba lazima atakuwa ni Muislamu lakini anajifanya Mkristo.

Afya: Baadhi ya mifano katika Uislamu

Mafundisho ya Mtume kuhusu usafi yanaenda mbali zaidi na kuosha mikono, uso na mikono mara tano kwa siku. Ni lazima kuosha mikono kabla na baada ya chakula na unapotoka chooni. Kuhakikisha afya nzuri na usafi unaweza kuwa ni mchango mkubwa wa Uislamu katika nyanja ya dawa. Bila shaka maji safi na usafi wa afya ya

mtu vimeokoa maisha ya watu wengi zaidi ya kuua vijasumu vikiwekwa pamoja. Walivutiwa na desturi na msemo wa Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallama), mfano "usafi (twahara) ni zaidi ya nusu ya imani" (Tahoor na Iman/ Muslim) na "mwili wa mtu una haki juu yake" (Al-Dahaby, 2004).

Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallama) alitumia matibabu ya asili wakati alipougua na mara chache alifanya matibabu. Alikuwa ni mwenye nguvu na afya ambaye alishiriki katika kazi zenye kuhitaji kutumia nguvu (ikiwemo vita mbalimbali na kuchimba mahandaki wakati ambapo Madinah ilitaka kuvamiwa). Aliweza kupanda katika pango la Hira kila mwaka, kitu ambacho kilihitaji nguvu nyingi.

Wazazi lazima walifanye suala la usafi binafsi ni jambo la kupewa kipaumbele kwa wavulana na wasichana kabla ya umri wa kubaleghe na kwa kufanya hivyo mapema itakuwa ni bora zaidi. Angalizo lazima liwepo kuhusu usafi binafsi kwa watoto. Watoto watatakiwa kusali, kufunga na mafunzo ya lazima ya kidini kama ilivyo kwa watu wazima, kwa hiyo ni muhimu kuwa nadhifu na kuhakikisha miili yao, nguo zao na mazingira yanayowazunguka yanakuwa safi muda wote.

Usafi katika vyoo

Waislamu wanatakiwa kuhakikisha nguo zao za ndani na sehemu za siri ni safi kiasi iwezekanavyo. Pia inatakiwa nguo za ndani, suruali na soksi kubadilishwa kila siku ili kuzuia harufu mbaya. Kama mkojo utaingia katika nguo, ni lazima ioshwe hadi ihakikishwe kuwa hakuna rangi au harufu iliyobaki. Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallama) ameshauri kujisafisha mara kwa mara baada ya kutumia choo (*istinja*), kwanza kwa kuondoa uchafu wote wa mkojo au kinyesi kwa maji au kitu chochote kisafi na kikavu kama vile karatasi laini kwa kutumia mkono wa kushoto. Osha sehemu za siri vizuri hadi uchafu wote utoke usionekane kwenye karatasi laini. Sehemu za siri lazima ioshwe kwa maji na zikaushwe. Nyumba za Waislamu zinaweza kuwa na kinyunyizio maalumu kilichowekwa karibu na choo au kutumia kopo la maji kwa dharura. Mkono wa kushoto unatumika kwa kusafishia na mkono wa kulia kwa kula chakula, ili kuzuia kula uchafu wakati wa kula (hata kama mikono ilioshwa baada ya kutumia choo).

Baada ya kusafisha kwa maji, ni vizuri kukausha (hasa kwa wasichana) ili kuzuia uchafu ambao unaweza kubaki katika nguo za ndani. Wasichana hujipangusa kuanzia mbele kwenda nyuma siyo kuanzia nyuma kwenda mbele. Pia inapendekezwa kuvaa nguo za ndani za pamba ambazo " zina mianya ya hewa" na hukauka kwa haraka kuliko chupi zilizotengenezwa kwa usanisi na nailoni. Mikono ni vyema ikioshwa kwa sabuni baada ya kutoka chooni ili kuhakikisha usafi na pia hakuna harufu mbaya inayobaki ndani ya kucha. Ukataji kucha unahimizwa na Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallam).

Unajua kwamba asilimia 98 ya maambukizi ya watoto yanatokana na watoto kuweka mikono yao katika midomo yao? Zuia kwa kutumia mpira wa mtoto.
(GOOKIN 1996)

Nywele na Kucha

Nywele ambazo huota kwapani na katika sehemu za siri zinaweza kuwa ni chanzo cha harufu mbaya. Uliojumuisha weusi na jasho, nywele hutengeneza mazingira ya bakteria kukua. Zikiondolewa harufu ya mwili hupungua na kunakuwa na uwezekano mdogo wa kupata baadhi ya kero, kama vile kuwashwa au kupata chawa.

> Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallama) amesema: Mambo matano ni tabia za *maumbile* (maumbile halisi au desturi za Mtume): kutahiri, kuondoa nywele sehemu za siri, kunyofoa nywele za kwapani, kukata kucha na kukata sharubu. (AL-BUKHARI)

Nywele za kwapani na sehemu za siri zinaweza kuondolewa kwa njia rahisi na haraka (ikiwemo kunyofoa, kunyoa, kupunguza) kwa kutumia dawa maalumu na mafuta au kwa kutumia wembe mpya za kisasa. Mara moja kila baada ya siku Arobaini ni vyema ziondolewe au wakati wowote zinapokuwa. Usafi wa sehemu za siri ni muhimu hasa kabla ya kwenda katika michezo au shuleni au msikitini ili kutowaudhi wengine. Usafi kwa ujumla unasisitizwa. Viondoa harufu, hata hivyo ni hatari na viepukwe.

Tabia ya baadhi ya wanawake na wanaume kubadilisha rangi za nywele inakatazwa katika Uislamu, pia tabia ya kufuga kucha ndefu au kupaka rangi kucha za mikono na miguu. Kucha ndefu hukusanya uchafu na kupitisha uchafu (hususani wakati wa chakula). Hazifai na mtu hawezi kupata udhu vizuri wakati akiwa amepaka rangi kucha kwani maji hayawezi kupenya na kufikia kucha. Pamoja na hayo inaruhusiwa kupaka kucha hina kwa sababu hazizuii maji kufika katika kucha. Inapendekezwa kwamba wanaume watumie manukato ya asili na uturi kabla ya kwenda msikitini. Wanawake wanaweza kutumia uturi wakiwa ndani ya nyumba zao, wakihakikisha hakuna mtu ambaye siyo maharimu wao (mwanaume ambaye anaweza kumuoa).

Je unafanya usafi ili uishi au unaishi ili uwe msafi? Zuia kupetuka!

- Mwanamke alipewa jina Mama usafi kwa sababu alikuwa msafi sana. Aliishi akiwa msafi. Nyumba yake ilikuwa na mazingira safi yasiyokuwa machafu. Alijitesa kwa ajili ya mtoto wake na kuwanyima furaha ya kucheza na kujumuika na wengine ili kuepuka kufanya fujo yoyote. Nyumba ilikuwa safi kwa ajili ya kuishi. Furaha isingeweza kuingia ndani, ilikuwa safi sana kwa hilo. Hatimaye alipewa talaka kwa sababu mazingira ya ndoa hayakuwa mazuri kwake. Alijitolea kufanya usafi sana ili kupata utulivu wa akili. Watoto waruhusiwe kufanya fujo, baadhi ya sehemu zitasafishwa baadaye. Hofu juu ya jambo lolote ni kawaida, pia katika usafi.
- Daktari alimwambia mgonjwa mwenye matatizo katika mfumo wa neva katika hospitali ya akili aliyenawa mikono yake kwa sabuni kila wakati, alipopeana mikono na watu wengine hata akiwemo mtaalamu wa afya.
- Watoto wafunzwe mapema iwezekanavyo kunawa mikono kabla na baada ya kula hadi wazoee.

Tabia za afya za Uislamu za mwili na nafsi:

- Kunyonyeshwa mtoto (siyo zaidi ya miaka miwili)
- Kutahiriwa kwa wavulana
- Kutofanya tendo la ndoa wakati wa hedhi
- Kuoga mara kwa mara na kutia udhu mara tano kwa siku
- Kuoga josho kila baada ya jimai na kuoga siku ya Ijumaa kama sunnah
- Kuosha mikono kabla na baada ya kula na baada ya kutoka chooni
- Kulinda meno kwa kutumia mswaki
- Kulala wakati wa usiku na kufanya kazi mchana
- Kuzuiliwa tendo la ndoa kwa muda wa siku Arobaini baada ya kujifungua.

Usafi unaaminika kuwa ni «nusu ya imani». Qur'an imekataza kula nyama ya nguruwe au bidhaa zitokanazo na nguruwe, mzoga, damu na vilevi vya aina zote. Kufunga tangu jua linapochomoza hadi linapozama kwa muda wa mwezi mmoja kwa mwaka (*Swaum*, Ramadhan) huupumzisha mwili na hutibu mambo mengi. Mazingatio na sala huleta utulivu wa kisaikolojia.

Kutahiri kwa wanaume hupunguza karibu asilimia 50 ya kupata maambukizi ya HPV (Human Pappilloma Virus) kutoka katika maambukizi ya kizazi cha mwanamke, ambapo kwa mara chache sana inaweza kusababisha kansa ya kizazi katika umri wa miaka 24. HPV imeambukizwa sana kwa njia ya kawaida ya zinaa nchini Marekani.

Zifuatazo ni njia muhimu za matibabu katika Uislamu

- Kunatakiwa kulinda uhai
- Kugawa damu kunaruhusiwa (baada ya kufanya majaribio ya damu)
- Kujinyonga na kujiua au kumsaidia mtu kujiua hakuruhusiwi
- Kumchunguza maiti hakuruhusiwi (labda ikitakiwa kisheria au sababu nzuri za kijamii)
- Utoaji mimba hauruhusiwi (labda ikiwa ni kwa kuokoa maisha ya mama)
- Upandikizaji unaruhusiwa (kwa kufuata masharti na vizuizi kadhaa)
- Uzalishaji asilia wa kisasa unaruhusiwa kati ya mume na mke (wakati tu wa ndoa yao)
- Ushoga na usagaji hauruhusiwi
- Kunahimizwa kuwa na wosia hai na haki ya kitabibu ya uwakilishi
- Uhandisi maumbile kwa ajili ya kutibu ugonjwa unakubalika lakini vipandikizi vinahitaji utafiti zaidi ili kujua kukubalika kwake.
- Kujitolea viungo kunaruhusiwa.

LISHE

Kipindi muhimu kwa yeyote katika lishe maishani ni mwanzoni mwa siku 1000 za kwanza. *(The Economist, Machi 26, 2011*).

Lishe bora ni muhimu kwa afya ya mtoto. Siyo chakula chote kina lishe; chakula ni kitu tunachokipenda kula lakini lishe ndiyo tunayoihitaji. Mwanzoni mwa miaka miwili, kwa vyovyote iwezekanavyo kina mama wanatakiwa kuwanyonyesha watoto wao kwa sababu ya faida za kimwili, hisia, kijamii, kiakili na kisaikolojia. Kabla na baada ya kumuachisha mtoto ziwa, mpangilio wa lishe bora unahitajika.

Mlo wa kila siku lazima ujumuishe vyakula vya aina zote kama vile maziwa, nafaka, matunda, mbogamboga na nyama ambavyo hutoa vitamini muhimu na madini kwa makuzi ya mtoto. Matunda na mbogamboga vinahitaji kuoshwa kwa sababu vinaweza kuwa na bakteria, kemikali na uchafu.

Qur'an imetaja chanzo cha vyakula vyote muhimu vinavyojulikana kuwa ni vizuri. Vinahusisha aina mbalimbali za nyama (ng'ombe, ngamia, kondoo, mbuzi, ndege na nyama ya baharini), ngano, kunde (maharage na dengu), njugu, matunda na mbogamboga (zabibu, tini, zeituni, komamanga, tende, vitunguu maji, vitunguu saumu na tango), maziwa na asali. Asali imetajwa hususani kuwa ni dawa na ni ponya kwa watu. Watoto wanaweza kuhimizwa kula asali mara kwa mara baada ya mwaka mmoja.

KULA SANA

Pindi ambapo watoto wanahitajika kula aina zote za vyakula, kula sana lazima kuzuiliwe. Qur'an inasema:

> *Enyi wanadamu! Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada, na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye hapendi wanaofanya israfu.* (Qur'an 7:31)

Angalia kile unachokiweka katika mwili wako. Kumbuka, *kile unachokula kinakudhuru wewe*. Jifunze namna ya "kula ili uishi" na siyo "kuishi ili ule".

Wazazi ni vyema wakiwapatia maji safi, yasiyokuwa na kemikali. Kuna nadharia isiyokuwa sahihi kuwa mtoto mnene ndiye mwenye afya, hii siyo kweli. Hata hivyo, kinyume na watu wazima, uwiano wa unene kwa chakula cha watoto ni mzuri.

Matatizo ya Unene Uliopitiliza

"Sisi ni taifa ambalo tunakula kwa macho yetu na siyo kwa matumbo yetu. Kadri tunavyoona chakula karibu yetu, ndivyo tunakula zaidi" (DR. SANJAY GUPTA, CNN, 2008)

WAZAZI: mnayo nafasi ya kupatia watoto wenu chakula kizuri chenye kuleta afya katika sehemu salama nyumbani kwenu.

Zaidi ya theluthi (asilimia 35 au sawa na Milioni 78.6) ya watu wazima nchini Marekani ni wanene kupitiliza: Asilimia 36 ya wanawake na aslimia 33.5 ya wanaume. Zaidi ya theluthi mbili ya watu wazima (sawa na asilimia 68.5) wana uzito uliopitiliza au wanene kupindukia: Asilimia 66 ya wanawake na asilimia 71 ya wanaume. Kwa kukadiria, asilimia 17 ya watoto (wenye umri kati ya miaka miwili hadi kumi na tisa) ni wanene kupitiliza, na asilimia 32 wana uzito uliopitiliza (mkubwa sana) au wanene kupitiliza. Zaidi ya mmoja katika watoto kumi wanakuwa wanene sana kuanzia miaka 2 hadi kufikia miaka 5 (Takwimu kwa mwaka 2011-2012; CDC na FRAC).

Tatizo la ongezeko la unene uliopitiliza limeongezeka zaidi ya mara mbili tangu mwaka 1970. Uzito uliopitiliza unaelezewa kuwa ni asilimia 20 au zaidi katika uzito wa kawaida katika mwili wako.

Nchi ya Uingereza ndiyo nchi inayoongoza kwa tatizo la watu kuwa na unene uliopitiliza katika Ulaya Magharibi, ikiwa na ongezeko la tatizo la unene uliopitiliza zaidi ya mara ilivyokuwa katika kipindi cha miaka 30 iliyopita. Uingereza mnamo mwaka 2011 takwimu zilionesha kuwa asilimia 25 ya watu wazima wana tatizo la unene uliopitiliza na asilimia 62 wanaweza kuwa wazito zaidi au wanene sana. Kwa kufaya uchanganuzi kwa kutumia jinsia, asilimia 24 ya wanaume na asilimia 26 ya wanawake ni wanene kupitiliza na asilimia 65 ya wanaume na asilimia 59 ya wanawake ni wazito kupitiliza au wanene zaidi (kupitiliza). Kati ya watu watatu katika wanaume na wanawake (wenye miaka miwili (2) hadi kumi na tano (15) ni wazito zaidi au wana tatizo la unene uliopitiliza na asilimia 16 ni wanene zaidi (NHS 2013).

Tatizo la ongezeko la unene kwa watoto linaongezeka haraka zaidi kuliko ilivyokuwa kwa watu wazima. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na CDC, tatizo la kuongezeka unene utotoni limekuwa kubwa zaidi ya mara mbili na limekuwa kubwa mara nne zaidi kufikia ujanani katika kipindi cha miaka 30 iliyopita nchini Marekani.

Maisha ya kukaa sehemu moja kukiwa na chakula cha kutosha, kula sana vyakula visivyokuwa sahihi pamoja na kunywa vinywaji visivyokuwa sahihi ndiyo chanzo kikubwa cha kuongezeka unene.

Ubora na uwiano wa chakula ni muhimu sana, mtoto anaweza kuwa na kitambi lakini bado anaweza kuwa na upungufu wa lishe. Wazazi wanaweza kuweka jitihada kuwafanya wawe na afya watoto wao kwa kuweka kanuni nzuri za namna ya kula.

Mtoto aliyekataa kusema "Alhamdulillah"

Mgeni wetu alimwambia mtoto wake wa miaka saba, baada ya kula mayai 4, vipande 4 vya mkate na jibini ya kuchoma kwa ajili ya kifungua kinywa "Mwanangu sema *Alhamdu Lillah*", ikimaanisha mwisho wa kula. Kijana alijibu, "Lakini baba, bado nina njaa! Sijamaliza! Sitaki kusema "*Alhamdu Lillah* kwa sasa!" Mgeni aligundua kwa nini mtoto alikuwa hawezi kunyanyuka. Mtoto alikuwa mnene sana!! Wazazi lazima wawe makini na kula sana, *Tukhmah*. Mtume (Swalla Allahu Alayhi wa Sallam) amesema:

Chombo kibaya ambacho mtoto wa Adam anaweza kukijaza ni tumbo. Chakula kidogo kinatosha kuulinda mwili lakini akitaka kula, anaweza kuacha theluthi ya tumbo lake kwa ajili ya chakula, theluthi kwa ajili ya vinywaji na theluthi kwa ajili ya kupumua. (Ahmad, Al-Tirmidhi na Wengineo)

Msomi wa Kiholanzi aliona kwamba vijana katika nchi ya Marekani ndio wenye vitambi sana kinyume na mataifa 15 yaliyoendelea. Karibu theluthi ya watoto nchini Marekani hula chakula kwa haraka kila siku. Lishe mbaya ndilo janga linaloongoza ulimwenguni kwa kuua mamilioni ya watoto na kuwaacha wengine wakiwa wamedhoofika, magonjwa yasiyoepukika na wenye ulemavu wa kiakili. Lishe bora kwa watoto ni jambo la muhimu sana kuanzia umri wa miaka mitatu (UNICEF, 2003). Kuwapeleka watoto katika mazingira ambayo hakuna chakula cha ovyo ni njia muhimu sana ya kuendeleza tabia nzuri ya lishe kinyume na kuwalazimisha kula vizuri kwa mujibu wa maoni yao. Pindi wavulana wanapokula sana, kawaida huonekana katika suruali zao; pindi wasichana wanapokula sana huonekana katika nyonga zao, matiti na makalio.

Maoni ya Imam Al-Ghazali juu ya tabia za kula

Mtu hujichimbia kaburi kwa maneno yake!

Imam Al-Ghazali (1058-1111), mmoja ya watu walioleta mabadiliko katika historia ya Uislamu, amesema:

1. "Muislamu hatakiwi kuwa mtu wa mwanzo kwenda katika chumba cha chakula pia kula kutazama sahani za wengine, chakula cha wengine. Ni lazima atafune vizuri chakula chake na ajizuie na kukipangusa kwa mikono yake na nguo zake".

2. "Chuki dhidi ya ulafi lazima ifunzwe katika akili ya mtoto kwa kuelezea juu ya ulafi na ukaripiwe tabia ya ulafi wakati mtoto yupo na watoto walafi na pia kusifia wale wanaoridhika na kiasi kidogo cha chakula kile kifaa chenye chakula kidogo".
3. "Ni muhimu mtoto afunzwe kutojisifia kwa wengine juu ya kula na kuridhika na chochote kitakachopatikana. Akemewe kwa namna yoyote ya kuchupa mipaka kwa ajili ya hamu ya vyakula vitamu utamu wa chakula, kinywaji na mavazi ya kifahari".



4. "Kula sana kwa watoto wadogo inaweza kuwa sababu inayochangia kuwa na kitambi baadaye na kuwa na kitambi kunaweza kusababisha kupata 'maradhi kwa wingi'"

Ukweli kuhusu Watoto na Lishe

KIPINDI CHA UJAUZITO: Kumpa mtoto mwanzo mzuri, kula na mtoto kifikra hata kabla ya kuwa mjamzito. Wiki 4-6 za mwanzo za ujauzito, wakati ambapo hujajua kuwa wewe ni mjamzito, ni muda muafaka kwa makuzi ya mtoto. Mama na akina mama watarajiwa inabidi wapate micrograms 400 za vitamin B kila siku, ambazo ni muhimu kwa ubongo wa kijusi na kukua kwa uti wa mgongo. Kwa njia hii, asilimia 50 – 70 za dosari za mfumo wa neva wa kawaida zinaweza kuepukwa. Uzito wa paundi 20 – 30 za wakati wa ujauzito huchukuliwa kuwa ndiyo afya. (*Sutherland na Stover, 1997*)

KATI YA KUZALIWA NA KABLA YA UJANA: Maajabu ya makuzi katika mwaka wa kwanza huwa muhimu katika mwaka wa pili pamoja na hamu ya kula. Kwa kawaida watoto hupata paundi 6-8 katika mwaka wa pili na wanaweza kupoteza hamu ya chakula. Watoto hula watakavyo wakati wanapopewa aina mbalimbali za vyakula katika kila mlo. Watoto wengi wanaoanza kutambaa nchini Marekani wanapewa vyakula vyenye mafuta kidogo na hivyo kuwa na utapia mlo. Lazima kuwepo na kutozuia matumizi ya mafuta kwa watoto chini ya miaka miwili. Mafuta huleta nguvu na huongeza mafuta ya asidi kwa afya ya ngozi. Mafuta hubeba na kuusaidia mwili kufyonza vitamin A, D, E na K. Wakati anapokuwa tayari kwa ajili ya maziwa ya ng'ombe, tumia maziwa ya kawaida, siyo asilimia mbili – angalau hadi umri wa miaka miwili. Kula mlo kamili uliokamilika ni muhimu sana. Mlo kamili nchini Marekani huzidi kiwango cha virutubisho vilivyopendekezwa kuliwa au huwa katika sampuli nne tu; Kalori kutokana na mchanganyiko wa vyakula vyenye asili ya fati na sukari ya ziada, punje punje, sodiamu na fati iliyoyayushwa. Wakati huo huo, kiwango kidogo zaidi cha kile kilichopendekezwa katika mboga mboga, matunda, punje punje, maziwa na mafuta huliwa na watu (Baraza la Rais la Afya, Michezo na Ulaji). Ulaji mzuri huchochea ukuaji mzuri na maendeleo ya watoto. Huzuia lehemu na shinikizo la damu na hupunguza hatari ya

kupata maradhi kama vile maradhi ya moyo, saratani, kisukari pamoja na kupunguza uwezekano wa mtu kuwa na matatizo ya unene uliopitiliza, matatizo ya mifupa, upungufu wa madini ya chuma na matatizo ya meno, (CDC).

KABLA YA UJANA NA UJANA: Ingawa watoto wengi wanajua baadhi ya misingi ya kanuni za afya, mara nyingi hawazifuati. Kwa kuwapatia chakula kizuri kwamba watoto ambao hawajafikia ujana na vijana kuwa watakula inaweza kuwa ni changamoto. Mtoto wa miaka nane anaweza kula chochote kitakachowekwa mezani lakini mtoto wa miaka 14 anaweza kukataa chakula alichokula mwezi mmoja uliopita. Baadhi ya ufumbuzi ni kuwasisitiza watoto kuwasaidia na kuandaa chakula na kujiepusha na kukifanya chakula ni jambo la kawaida. Wakati wa mlo lazima uwe ni muda wa kupashana habari za siku, mbali na kula tu. Vijana hukua kwa haraka zaidi kuliko kipindi chochote tangu kuanza siku ya kwanza ya maisha. Wasichana wanahitaji kalori 2,000-2,500 kwa siku kwa ajili kuchochea makuzi yao na wavulana wanahitaji kalori 3,000-4,000, kuna watoto wengine wanahitaji kalori nyingi. Kuongezwa lishe kunahitajika zaidi wakati wa kupevuka, kawaida wasichana ni miaka 15 na miaka 19 kwa wavulana. Wasichana wanahitaji madini ya *kalishiamu* zaidi hadi wanapofikia umri wa miaka 25. Madini ya *kalishiamu* yanaongeza uwezo wa kukua kwa mifupa na huwa akiba baadaye mifupa itakapodhoofu. Ni muhimu watoto wasikose chakula. Kukosa chakula kunasababisha kukosa lishe na kula chakula kidogo siku nzima ni nzuri zaidi ya kuacha kula mchana na kula chakula kingi wakati wa usiku.

MFANO WA CHAKULA KWA MTOTO WA MIAKA 2 HADI 10

Kwa mujibu wa shirika la Marekani la elimu-lishe, mlo wa mtoto kila siku lazima uwe na:

- Vijiko 6-11 vinatakiwa viwe na nafaka
- Vijiko 2-4 vinatakiwa vya matunda
- Vijiko 3 vinatakiwa viwe vya mbogamboga
- Vijiko 2-3 vinatakiwa viwe na nyama, kuku, samaki na maharage makavu
- Vikombe 2-3 vinatakiwa viwe vya maziwa kila siku
- Kiasi kidogo cha mafuta na vitu vitamu. Karanga na mbegu ni vyanzo vizuri vya mafuta.
- Kwa mwaka 1-5 anatakiwa atumie kipimo cha kijiko kimoja cha chakula kwa aina ya chakula kwa mlo kwa kila umri.
- Kwa umri wowote, kula sana ni kubaya.

Wazazi wanawezaje kuwasaidia watoto wao kula chakula chenye aina ya vyakula vyote kila siku? Jibu ni kuhakikisha chakula kidogo chenye lishe mara zote kinapatikana.

MASWALI YANAYOULIZWA SANA

Watoto wengi huacha chakula chenye lishe pamoja na tabia zao za kula bila mpangilio. Wanachukua kile wanachokihitaji katika chakula ambacho ni robo tatu ya chakula cha mtu mzima – kwa mlo mmoja- kijiko kwa umri wa mwaka. Watoto watakula tu kile

chakula ambacho wanahisi ni kizuri kwao. Hizi ni baadhi ya dondoo za kula chakula kizuri (Underwood na Kuchment, 2008):

1. NI UCHAGUZI UPI WANATAKIWA WAZAZI WAWAPE?

Wakati wa mlo, wazazi wanatakiwa wawape vyakula mbalimbali vyenye lishe: protini, maziwa, matunda au mbogamboga, mkate na vyakula vya wanga (kama mchele, tambi au viazi mbatata). Kisha wawaache watoto wao wachukue na wachague katika vile vilivyopo. Wazazi wanapaswa wajue kwamba kujinyima wao kula chakula wasidhani kwamba pia watoto wao wanapenda. Jumuisha angalau aina moja ya chakula wanachokula mara kwa mara – hata kama itakuwa ni mkate au tunda. Upungufu wa vitamin kwa watoto ni mara chache, kwa hiyo katika kadhia nyingi haihitajiki ziada.

2. JE INASHAURIWA KUWA MLA MBOGAMBOGA?

Kanuni ni kula chakula chenye nyama na mbogamboga. Allah ameumba vyakula hivi vizuri vyote kwa ajili ya mwanadamu kwa lengo zuri. Kwa hiyo, ni vyema kula katika vyakula vyote vilivyoruhusiwa kwa kiasi. Namna ya kiasi kikubwa kinavyopunguzwa katika lishe ya watoto, ndivyo uwezekano mkubwa wa hatari ya upungufu wa lishe unavyoongezeka. Kuondoa nyama, kuku na samaki kunamsababishia ugumu mtoto kupata madini ya chuma. Binadamu hufyonza tu karibu asilimia 3 hadi 8 ya madini ya chuma kutoka katika mbogamboga na nafaka, ukilinganisha na asilimia 20 ya madini ya chuma yatokanayo na nyama. Kula vitu vizuri ambavyo ni chanzo cha vitamin C (chungwa au nyanya) kutasaidia kufyonza madini ya chuma katika chakula kiliwacho. Chakula cha mboga mboga kinaweza kuwa na uchache wa mafuta na kalori na hivyo kufanya ugumu kwa watoto kupata mahitaji ya kalori.

3. MWANANGU HAPENDI MAZIWA. JE ANAWEZAJE KUPATA KALISIAMU ZA KUTOSHA?

Ni muhimu hasa kwa ambao hawajafikia ujana na vijana kupata *kalishiamu*, kwa sababu wanapata nusu ya ukuaji wa mifupa wakati wa kubaleghe. Maziwa ni chanzo kizuri cha *kalishiamu*, kwa hiyo mtoto asipoyanywa, anaweza kuyaongeza katika sahani zilizoandaliwa kama vile supu, faluda, njegere na mchuzi mzito. Mbadala mwingine wa kalishiamu unahusisha mtindi, jibini na aiskrimu. Chokoleti za maziwa zina sukari nyingi kuliko maziwa ya kawaida lakini ni chanzo kizuri cha *kalishiamu*.

4. JE NI SAHIHI KUMUACHA MWANANGU ALE KATI YA MLO NA MLO?

Ni kweli hasa watoto wanahitaji asusa. Watoto hawawezi kula sana kwa wakati mmoja kwa sababu ya matumbo yao madogo, pia wanahitaji nguvu nyingi. Wanahitaji kitu chochote cha lishe cha kula kila baada ya saa mbili hadi tatu. Asusa huwasaidia watoto kupata lishe ambayo wamekosa katika chakula kingine. Hata hivyo ni muhimu kwamba hizo asusa wapewe kwa muda maalumu. Kama watoto wanakunywa chai saa moja kamili, kwa hiyo wasipewe asusa hadi saa tatu au nne, hata kama watakuwa na njaa kabla ya muda huo. Kuifuata ratiba inaweza kuwa vigumu, hususani kama mtoto anakula kidogo, wazazi wanakuwa na furaha kuwaona wanakula chochote. Watoto

ambao wanaruhusiwa kula chakula kidogo kiasi watakavyo wanapenda kumaliza nusu ya kile chakula kilichoandaliwa na asusa zaidi. Wakati wa kuandaa asusa, waandaliwe kama sehemu kidogo ya chakula: matunda na mbogamboga, kiasi kidogo cha protini, wanga na mafuta. Asusa nzuri zinaweza kuwa ni biskuti za ogani na maziwa, tufaha na siagi ya karanga, au biskuti, jibini na juisi ya kukamua ya matunda.

5. MATUNDA NA MBOGA NI MUHIMU, NAHOFIA WANANGU HAWAYALI KABISA. NIFANYE NINI?

Kwa wastani, watoto wa Kimarekani hula kiasi cha 1½ cha matunda na 2½ ya mbogamboga kwa siku. Matunda mengi na mbogamboga, watoto wengi hawapendelei. Hata hivyo ni muhimu waendelee kupewa, hatimaye watakula baadhi yake. Kumfanya mtoto avipende vyakula hivi, inabidi:

- Changanya maziwa na matunda ili kutengeneza kinywaji laini
- Kuwapa matunda makavu – zabibu kavu, ndizi, aprikoti na cheri – ya kawaida au iliyookwa.
- Kuongeza mbogamboga katika supu na chakula.
- Ni muhimu rushwa kuepukwa. Watoto huuliza kama wazazi wanahitaji mbinu za kuwafanya wao wale chakula, njia hii haiwezi kuwa nzuri.
- Wazazi wanatakiwa wasifanye kula kila kilichopo kwenye sahani kuwa jambo la muhimu sana kwa watoto wao. Endapo mtoto atakataa brokoli, hivyo apewe maziwa na vyakula vya ogani (kwa ajili ya madini ya kalishiamu).

JARIBIO LA MAMA MMOJA

Pindi nilipokuwa mtoto, tulitarajiwa kula kila kilichowekwa kwenye sahani bila kuchagua. Nilikataa nyama ya mafuta na baadhi ya samaki, kwa mfano, mama yangu:

- Alinihubiria kuhusu wakati wa vita na baada yake
- Alinikumbusha Mamilioni ya watu wanaokufa njaa upande mwingine wa dunia
- Aliandaa chakula kilichokataliwa kwa mlo uliofuata baadaye
- Tulipopatwa na njaa kati ya milo, tulipatiwa mkate wa kahawia na siagi tu. Na kwamba ilikuwa kwamba si kila mtu ana fedha za kutupa.

SLYVIA HUNT, UK

6. JE NI CHAKULA GANI KIZURI UNASHAURI WALE WATOTO NA KWA NINI ?

Wazazi wanatakiwa kuwapa watoto matunda, mbogamboga, mikate, nafaka, mchele na pasta. Baadhi ya mifano ya vilivyofungashwa ni; tufaha, tini, chungwa, pea, stroberi, viazi, maharage, dengu, ngano au mkate, baga, pilau, makapi ya nafaka na mchanganyiko wa nafaka na mbegu. Vyakula vya nyuzinyuzi husaidia kuzuia kansa na kuondoa kula sana, hupunguza ufyonzaji wa mafuta na kalori katika utumbo, kutunza maji na kuupa mwili hali ya kutosheka na kupoza njaa.

7. MUDA WA MAJONZI AU HASIRA KWA FAMILIA ZETU NI ASUBUHI. JE KWELI TUNAHITAJI KIFUNGUA KINYWA ?

Ndio. Ni muhimu kufanya kila uwezalo kuhakikisha familia inapata kifungua kinywa, hata kama ni kuamka mapema kabla ya dakika 15. Watoto wanaokosa kifungua kinywa huwa hawatulii wawapo shuleni na kucheza. Kifungua kinywa huchangamsha ubongo pamoja na kiwiliwili. Kutokula hupelekea kuwa mwanafunzi dhaifu na asiyejiweza.

8. MWANANGU WA KIKE ANATAMANI KUWA MWEMBAMBA. JE NINAWEZAJE KUMFUNDISHA AWE NA AFYA BADALA YA KUACHA KULA CHAKULA?

Utafiti unaonesha kwamba asilimia 78 ya vijana wa kike waliobaleghe wa Kimarekani hupendelea kupunguza uzito. Baadhi huacha nyama kwa hiyo wanahitaji hutumia protini kwa wingi kama mbadala (kama maharage makavu, dengu, peasi, maziwa, jibini, mayai na njugu). Endapo binti wa mmojawapo yuko katika kipindi cha kubaleghe, ni vyema amuelimishe kwamba anahitaji virutubisho vya mafuta kwenye ngozi kama nguvu ya ziada kwa makuzi ya haraka.

9. BAADHI YA MASIKU, CHAKULA KILICHOFUNGWA TAYARI NDIYO CHAKULA PEKEE. UNASHAURI NINI?

Wazazi wazuie matumizi ya soda, chips na baga. Mbadala wake wachagulie kuku waliopikwa, saladi, maziwa yenye mafuta kidogo na mtindi. Tengeneza, ongeza katika piza na kuku wa kuchoma na mbogamboga nzuri.

10. JE MWANAO NI MCHAGUZI WA VYAKULA?



Walezi wanaweza kuchanganua kimakosa kuhusu watoto wenye umri kuanzia miaka miwili hadi mitano kuwa kama ni walaji wa ovyo hali ya kuwa hii ni tabia ya kawaida kwao. Mtoto anaweza kuona chakula walau mara 10 kabla ya kuanza kula kwa mara ya kwanza. Familia kula pamoja ni kitu muhimu sana. Watoto huwaiga wazazi wao namna ya kula na hujifunza mazungumzo yanayohusu chakula. Hata hivyo, tafiti iliyofanywa na Harris Interactive imebaini kwamba asilimia 26 ya walezi wanaokuwepo nyumbani pamoja na watoto wao hukaa pamoja kupata chakula cha pamoja kila usiku (idadi ilikuwa sawa na asilimia 36 ya walezi wanaokuwa nyumbani bila kuwa na watoto). Nchini Uingereza, gazeti la Telegraph (2013) limetoa taarifa kuwa utafiti ilibainisha kwamba zaidi ya asilimia 20 ya familia ndiyo hukaa pamoja kupata chakula japo mara moja kwa wiki hadi mara mbili na asilimia 40 hukaa pamoja kupata chakula japo mara tatu kwa wiki.

Zaidi ya moja katika familia tano hupata chakula chao huku kukiwa na Runinga mbele. Katika nchi zilizoendelea kati ya asilimia 20 hadi 30 ya watoto na vijana huwa hawapendelei kupata kifungua kinywa (Deshmukh-Taskar na wenzake,2010; Coder na wenzake, 2011 alinukuu kutoka katika kitabu cha uelewa katika sayansi ya nyuro za mwanadamu 2013). Hadi kufikia miaka 3, utambuzi ni moja ya sababu za msingi katika kuamuru chakula gani mtoto atakula. Wakati takribani asilimia 92 ya Wamarekani wenye umri kati ya miaka 2 hadi 19 wanakula mbogamboga kila siku (Taarifa fupi iliyotolewa na NCHS 2014), katika mfumo wa vitu vilivyokaangwa kwa utamaduni wa Kifaransa. Mazao yanayotokana na nyanya ikiwemo kachumbari, tambi zenye mchuzi ni vitu maarufu sana kwa watoto. Chakula kinachopendwa na wale waliokuwa wakubwa kiasi hubadilika kufuata mfano wa wale wengine.

Utumiaji wa maziwa umepungua nchini Marekani na Uingereza. Katika utafiti uliofanyika kati ya mwaka 1977 hadi 1978 na 2007 hadi 2008, kiwango cha utumiaji wa maziwa kwa watoto wanaokaribia rika la ujana nchini Marekani kwa wale ambao hawakutumia maziwa kwa siku iliongezeka kutoka asilimia 12 hadi kufikia asilimia 24, wakati kiwango cha utumiaji maziwa kwa wale waliokuwa wamekunywa mara tatu au zaidi kwa siku ilipungua kutoka asilimia 31 hadi kufikia asilimia 18. Kiwango cha utumiaji kwa vijana na watu wazima ambao hawakunywa maziwa kwa siku iliongezeka kutoka asilimia 41 hadi asilimia 54, hali ya kuwa kiwango cha wale waliokuwa

wanakunywa maziwa mara tatu au zaidi ilikuwa imeshuka kutoka asilimia 13 hadi kufikia asilimia 4 (USDA 2013). Nchini Uingereza utumiaji wa maziwa ya maji ulikuwa umepungua takribani asilimia 14 mwaka 2013 kuliko mwaka 2002/2003 (DEFRA-Utafiti wa chakula katika familia uliyonukuliwa mwaka 2013 na Jarida la AHDB, 2015).

Wakati utumiaji wa maziwa ukiwa umepungua, utumiaji wa vinywaji vyenye sukari umeongezeka. Kuanzia mwaka 1989 hadi mwaka 2008, asilimia ya watoto wanaotumia vinywaji vya sukari imeongezeka kutoka asilimia 79 hadi kufikia asilimia 91 (Lasater G, Piernas C na Popkin BM 2011 imenukuliwa na Havard T.H, Shule ya afya Chan). Takwimu kuanzia mwaka 1999 hadi kufikia mwaka 2008 zimeonesha kuwa wakati utumiaji wa soda ukiwa unapungua, utumiaji wa vinywaji vya kuongeza nguvu umeongezeka mara tatu zaidi miongoni mwa watu wazima (jarida la taaluma ya vyakula na taaluma 2013). Hata hivyo, soda bado inabaki kuwa kinywaji chenye asili ya sukari ambacho kinatumika kwa wingi sana. Utumiaji wa vinywaji vyenye sukari umechangia kuongezeka kwa tatizo la watu kuwa wanene kupitiliza. Soda moja yenye onsi 20 inakuwa na jumla ya sukari vijiko 15 hadi 18 na zaidi ya kalori 240. Kinywaji cha kola chenye onsi 64 inaweza kuwa na kalori 700 (Havard T.H, shule ya afya-Chan).

Nchini Uingereza vinywaji vya sukari, ambavyo kwa mujibu wa wataalamu vya lishe kwa watoto wameona kuwa havina umuhimu katika lishe zao, vimeonekana kuwa chanzo kikubwa cha sukari katika lishe ya watoto wa kuanzia miaka 4 hadi 10. Wanatumia asilimia 30 kutoka katika vinywaji laini na juisi, asilimia 29 kutokana na matumizi ya biskuti, keki na vitu vyenye asili ya punje punje wakati wa kupata kifungua kinywa,

"vinywaji vya sukari, kwa mujibu wa wataalamu vya lishe wameona kuwa havina umuhimu katika lishe za watoto... kutokana na pipi, chokoleti, sukari, samli na vitu vingine vyenye asili ya sukari na kutoka katika maziwa mgando, na aina nyingine za maziwa, asilimia 12 ya watoto wenye miaka 3 wamekumbwa na tatizo la kuoza meno ."

asilimia 22 kutokana na pipi, chokoleti, sukari, samli na vitu vingine vyenye asili ya sukari na asilimia 12 kutoka katika maziwa mgando, fromage frais, ice-cream na aina nyingine za maziwa. Asilimia 12 ya watoto wenye miaka 3 wamekumbwa na tatizo la kuoza meno mnamo mwaka 2013 na asilimia 28 ya watoto wote wanasumbuliwa na tatizo hilo wanapofikia umri wa miaka 5 (Afya ya jamii nchini Uingereza ,2015)

Ni lipi linatangulia ? Kazi au kifungua kinywa ? Usifanye kazi kabla ya kupata kifungua kinywa. Endapo utafanya kazi kabla ya kifungua kinywa, pata kifungua kinywa kwanza!!

11. JE VIUNGO NI VIZURI AU VIBAYA KWA AFYA?

Mafunzo yaliyoendeshwa na wanasayansi wawili katika Chuo Kikuu cha Cornel imegundulika kwamba viungo huwa na uwezo wa kuua karibu bakteria 30 tofauti wanaoharibu vyakula. Ikiwemo vitunguu maji, vitunguu saumu, pilipili, limau na miti-shamba na viungo vingi (kama vile kitimiri, mbegu zitokanazo na miti yenye harufu nzuri, karafuu, nanaa na tangawizi) katika chakula (Sherman na Billing, 1998).



12. WANASAYANSI WANABADILI MAWAZO, KWA HIYO TUFANYE NINI ?

Wanasayansi wanatuambia « tusahau kile tukijuacho kuhusu mayai, majarini na chumvi. Mawazo ya busara yamekuwa yakigeuzwa mara kwa mara kwa utafiti mpya; inaonekana wamekosea. Hakuna wiki ipitayo bila baadhi ya wataalamu kutoa taarifa mpya ya kukubali kwamba chakula fulani au vitamini au shughuli au hali itarudisha afya yako ya moyo au kuiharibu – na si mara nyingi, ushauri mpya unaonekana kupingana na wa zamani ». (Lemonick 1999)

Jibu ni lipi? Fuata njia sahihi za Qur'an na Mtume (Swalallahu Alayhi Wasallam) kuhusu chakula na lishe. Lishe nzuri ni jambo la kuchagua tabia ya kula, ambalo ni jambo linaloendana na umri. Kula kiasi kutoka katika aina mbalimbali za vyakula.

Mwongozo wa Qur'an kuhusu chakula

> Enyi mlioamini! Msiharamishe vizuri alivyo kuhalalishieni Allah, wala msikiuke mipaka. Hakika Allah hawapendi wakiukao mipaka. Na kuleni katika alivyokuruzukuni Allah, halali na vizuri. Na mcheni Allah ambaye mnamuamini.
>
> (Qur'an 5 :87-88)

> Enyi wanadamu! Chukueni pambo lenu kwenye kila pahala wakati wa ibada, na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye hapendi wanaofanya israfu.
>
> (Qur'an 7 :31)

> Sema: Ni nani aliyeharamisha pambo la Allah alilowatolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki. Sema hivyo ni kwa walio amini katika uhai wa duniani, na Siku ya Kiyama vitakuwa vyao wao tu. Namna hivi tunazieleza ishara kwa watu wanaojua.
>
> (Qur'an 7 :32)

> « … kisha kula katika kila matunda, na upite katika njia za Mola wako Mlezi zilizofanywa nyepesi kuzipita. Na kutoka matumbo yao kinatoka kinywaji chenye rangi mbalimbali; ndani yake kina matibabu kwa wanadamu. Hakika katika haya ipo ishara kwa watu wanaofikiri.
>
> (Qur'an 16 :69)

> « … hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu aende mjini, akatazame chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni cha kukila. Naye afanye mambo hayo kwa busara, wala asikutajeni kabisa kwa yeyote... »
>
> (Qur'an 18 :19)



Kwa ujumla:

- Kula aina zote za vyakula kwa kiasi. Kula kidogo katika kila kimoja na usile sana katika aina moja.
- Kuwa mla mbogamboga kunahitaji elimu na utaalamu. Zikijumuishwa pamoja na kiasi kidogo cha nyama.
- Epuka nguruwe, damu, mzoga, pombe, dawa za kulevya na kuvuta sigara. Hivi siyo vyakula vyenye lishe bora bali ni vibaya na vyenye madhara.
- Usijaze tumbo. Acha kula wakati bado unatamani kula zaidi.
- Tumia asali katika chakula chako. Kuna tiba na ponyo katika asali.
- Tumia mafuta ya zeituni kiasi (inakupatia HDL, kolesteroli za afya na kupunguza LDL, kolesteroli mbaya).
- Jiepushe na chochote kilichowekwa kemikali, dawa za kuua wadudu na vitu vilivyoongezwa vitu vya bandia.

Daktari wa watoto na dawa ya ajabu

Wakati baba alipofungua bahasha ya dawa iliyofungwa kwa ajili ya mtoto wake, alikuta bili ya dola 10 ikiwa na ujumbe kutoka kwa daktari wa watoto ukisema: “Nunua chakula kizuri kwa ajili ya mtoto wako, ana utapia mlo.”

Hii inaonesha namna gani wazazi wanavyopuuzia mambo muhimu kwa ajili ya makuzi ya kiafya ya watoto wao. Mbio za panya za jamii na maisha ya haraka haraka ya wazazi yanawasababishia kupuuzia kuwapa watoto chakula chenye lishe. Wazazi wanatakiwa kuwapatia watoto wao mambo muhimu kipindi cha miaka ya mwanzo katika makuzi yao kabla hawajachelewa. Kwa pamoja mahitaji ya kimwili na kihisia ni vitu muhimu kwa watoto.

Watoto na Mazoezi ya Viungo

> *"Mpeleke kesho pamoja nasi, ale kwa furaha na acheze; na bila ya shaka sisi tutamhifadhi."* (Qur'an 12:12)

"Rudi hapa!" "Acha kukimbia ndani ya nyumba!" "Nakwambia acha kucheza mpira ndani ya nyumba!" Haya ni mambo ambayo mara kwa mara wazazi huwaambia watoto wao. WANAKOSEA. Ilitakiwa waseme kinyume. "Nenda kacheze mpira wa kikapu". "Nenda kacheze mpira wa miguu na rafiki zako." "Nenda kakimbie na utembee."

Kwanini mazoezi ya viungo ni muhimu kwa mwanangu?

Uongezekaji wa mazoezi ya viungo unaenda sambamba na kuongezeka kwa siku za kuishi na kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo. Mazoezi ya kimwili hutoa manufaa ya kijumla ya kimwili, kisaikolojia na kijamii. Watoto ambao ni dhaifu pia inawezekana ukubwani wakawa wadhaifu. Mazoezi ya viungo husaidia:

- Kudhibiti uzito
- Kupunguza shinikizo la damu
- Kuongeza HDL kolesteroli (Nzuri)
- Kupunguza uwezekano wa kupata kisukari na aina kadhaa za kansa.
- Kuboresha saikolojia ya mwanadamu (ikiwemo kujiamini sana na kujistahi)
- Kujifunza ushirikiano

SHIRIKISHO LA MOYO LA Kimarekani

Karibu asilimia 21 ya watoto wenye umri kati ya miaka 6 – 17 nchini Marekani wana vitambi. Watoto wenye uzito mkubwa wana uwezekano pia wa kuwa na uzito mkubwa wawapo watu wazima. Vitambi kwa watoto huongeza uwezekano wa kupata kisukari, magonjwa ya moyo, kupooza viungo, kansa na maradhi ya kudumu. Njia nzuri ya kuzuia unene na magonjwa mengine ni kwa kufanya mazoezi tangu utotoni. Kufanya mazoezi huleta nguvu, kunyumbulika na ustahamilivu; ni muhimu zaidi kwa watoto wenye miaka miwili na zaidi. Kwa watoto, mazoezi humaanisha kucheza na kuwa mchangamfu muda wote. Mtoto mchangamfu ni rahisi kuwa na misuli na mifupa imara, mwili mwembamba na mwonekano mzuri katika maisha. Mtoto aliyedhoofika ni rahisi kupata magonjwa, kupooza viungo, unene na HDL kolesteroli (nzuri) kidogo. Kufanya mazoezi huwasaidia watoto kulala vizuri na kuwafanya kuwa na uwezo wa

kukabiliana na changamoto za kimwili na kiakili (kama vile kulikimbilia gari wakati wa asubuhi, kuinama kufunga nyuzi za viatu au kusoma kwa ajili ya jaribio). Kukosekana kwa mazoezi ya viungo kwa mtoto mara kwa mara hupelekea kudhoofika mwili wakati wa utu uzima (Kituo cha kudhibiti na kuzuia magonjwa, Marekani).

Watoto na Viatu

Makala ya kuvutia iliyochapishwa katika gazeti la *the Guardian*, mtaalamu wa siha Sam Murphy ameonesha kwamba watoto kutembea pekupeku ni vizuri na kutahadharisha kwamba viatu vya watoto vinaweza kuwaletea madhara katika makuzi ya ubongo wa mtoto. Tracy Bryne (mganga aliyebobea katika kutibu magonjwa ya miguu (nyayo) amesema kutembea pekupeku hukuza misuli na kano za nyayo, huongeza uimara katikati mwa nyayo, inachangia mkao mzuri na kuboresha ufahamu wa mtoto kulingana na mazingira yanayomzunguka. Viatu visiwe ni kwa ajili ya maonesho. Viatu vinaweza kuleta madhara kwa nyayo za watoto wadogo. Utafiti kutoka katika toleo la mwaka 2007 la podiatry journal, *The Foot* limeonesha kwamba baadhi ya viatu vya watoto huwa ni vigumu sana kiasi ambacho sehemu ya kisigino haiwezi kunyumbulika ili kuruhusu kufanyika mazoezi ya viungo (ambapo kunakuwa na uzuiaji katika hatua). Nyayo zinakuwa katika hatari kubwa ya kupata madhara kutokana na magonjwa ya ghafla au viatu vinavyobana. Ni hatari endapo unyayo utabadilika katika umbo lake na kuwa kama la kiatu kinyume na kuruhusiwa kukua kama kawaida yake.

Wazazi wanatakiwa kuifanya hali halisi ya mazingira kuwa mbele kuliko kuiweka mbele mitindo au uvutiwaji wakati wa kuwanunulia viatu watoto na wazazi wanatakiwa kuwahimiza watoto kutembea pekupeku mara kwa mara (hususani karibu na nyumba na popote iwezekanapo). (Murphy, 2010)

Namna ya Kukuza Juhudi kwa Watoto

Wazazi wanaweza kufanya mambo mengi kuwasaidia watoto kuwa na tabia ya kufanya mazoezi. Baadhi ya maoni yameorodheshwa hapa chini:

- Punguza muda wa mtoto kuangalia televisheni na kucheza michezo ya video. Kutokana na umuhimu wa usalama, watoto wengi wanaachwa kuangalia televisheni na kufanya mazoezi ya nyumbani hadi wazazi wao wanaporudi nyumbani. Kimawazo, watoto wanatakiwa kuwa wachangamfu baada ya shule na kusoma tena baadaye.

- Muhimize mtoto kushiriki katika shughuli mbalimbali ambazo zinaendana na umri wake. Watoto chini ya umri wa miaka miwili hawatakiwi kutazama televisheni. (Wataalamu wa matibabu ya watoto wa Marekani)
- Wafunze watoto kwamba kufanya mazoezi ya kimwili ni kwa ajili ya furaha na kwamba mazoezi yanakuwa katika namna mbalimbali tofauti (kucheza mchezo wa kukimbizana na kugusana, mchezo wa vipande/vyumba, michezo). Endapo mtoto anacheza michezo yenye kufurahisha hivyo alazimishwe kuendelea kuicheza.
- Usitumie mazoezi ya kimwili kama adhabu. Ni desturi mbaya endapo mwalimu atawaamuru wanafunzi kukimbia mizunguko mitano ili wapate shida.
- Wazazi ni kiigizo chema kwa watoto wao, na ni muhimu wafanye mazoezi mara kwa mara. Panda ngazi badala ya lifti, atembee badala ya kuendesha gari na atembee pole pole badala ya kutembea kwa haraka.
- Ijumuishwe familia nzima katika mazoezi. Wazazi wasikae kwenye viti na kuwaambia watoto nendeni nje mkacheze.
- Kuambatanisha mazoezi ya kawaida ya viungo pamoja na mlo kamili kwani ni chanzo cha maisha yenye afya nzuri. Watoto wanatakiwa kula matunda, mbogamboga na aina zote za nafaka mara kwa mara.
- Himiza kazi zenye kufurahisha ambazo huongeza nguvu, kunyumbulika na ustahamilivu. Nguvu inaweza kujengwa kwa shughuli ndogo ndogo kama vile kuruka vizuizi, kusimama kwa mikono au mieleka. Himiza mashindano ya kukaa na kusimama, kuvutana na pushapu.
- Wafundishe watoto kuboresha moyo na mapafu. Moyo huenda mbio na kumfanya mtu kupumua kwa shida jambo linalofanya kuimarika kwa moyo na kupeleka oksijeni zaidi katika seli za mwili. Kuboresha moyo na mapafu kunajumuisha mpira wa kikapu, mpira wa wavu, kuendesha baiskeli, kuteleza barafuni, mpira wa miguu, kuogelea, kucheza tenesi, kutembea, kurukaruka na kukimbia.

Ratiba za mazoezi zilizokokotezwa

Ratiba ya mazoezi kwa watoto ni muhimu kwa makuzi yao na kiwango cha chini cha mazoezi inategemea na umri wao. Shirikisho la Taifa la Michezo na Elimu ya Mazoezi ya Viungo (NASPE) limesisitiza:

UMRI	MUDA WA ZOEZI	MAELEZO
Mtoto mchanga	Hakuna hitaji maalumu	Mazoezi ya mwili lazima yahimizwe ili kuongeza mwendo wa ukuaji
Mtoto anayeanza kutembea	Saa 1½	Apangiwe mazoezi ya mwili ya dakika 30, dakika 60 za mapumziko
Mtoto ambaye hajaanza kwenda shule	Saa 2	Apangiwe dakika 60 za mazoezi ya mwili, dakika 60 kwa ajili ya mapumziko
Mwenye umri wa kwenda shule	Saa 1 na zaidi	Afanye mazoezi yaliyogawiwa katika makundi tofauti tofauti ya dakika 15 au zaidi

TAASISI YA MOYO NCHINI MAREKANI INAPENDEKEZA KUWA

- Watoto wote wenye umri kuanzia miaka miwili (2) na kuendelea wanatakiwa kushiriki katika shughuli zenye kuwafurahisha, shughuli zisizokuwa ngumu sana kila siku ambazo shughuli hizi ziwe zenye kuwaletea maendeleo yao.
- Kama mtoto hana muda wa kupumzika kwa muda wa dakika 60 kila siku, basi jaribu kuwa na dakika thelathini au vipindi vinne vya dakika kumi na tano kila kimoja kwa ajili ya kupumzika baada ya kazi yenye kutumia nguvu.

Mtume Muhammad (Swalla Allahu Alayhi wa Sallam) amesema:

> «*Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendwa zaidi na Allah kuliko muumini dhaifu na kuna uzuri kwa wote*». (MUSLIM). (Neno '*qawy*' katika hadithi limemaanisha nguvu ya imani na mwili).

Kanuni « tumia au kosa » imetumika kumaanisha kano za mwili, mishipa ya moyo na seli za ubongo: Mazoezi ya mwili ni lazima (siyo ya hiari) kwa makuzi ya mwanadamu.

Ingawa kupata mazingira yenye afya nzuri ni muhimu, kukaa nayo mbali ni changamoto. Kujiweka vizuri kimwili huwa na athari chanya katika nguvu za mwili, tabia za kiakili na hamu ya kiroho. Kama utakimbia Jumatatu kisha ukaacha hadi Ijumaa, usiongeze mwendo kuwa mara mbili siku ya Ijumaa utakapofanya tena. Usijifanyishe kazi kupita kiasi. Dumu na kukimbia na kufanya mazoezi ya viungo popote pale. Watoto pia huhitaji baadhi ya mazoezi wakati wa kunyonya na kulala. Kwa mtoto aliyezawa hadi mwaka mmoja, unaweza kumbeba mgongoni, zungusha miguu yake taratibu kama vile anaendesha baiskeli, mshike sehemu za tumbo na kumuhimiza kunyanyua kichwa chake na mlaze kwenye blangeti sakafuni ili azungushe mwili wake na kufikia vidude vya kuchezea au kitu kisichokuwa na madhara.

Kulala

Ili kupata afya njema na mwili kufanya kazi vizuri ipasavyo ni muhimu mtoto alale vya kutosha, ambapo kwa kawaida tabia ya kulala utotoni huendelea pia hata baadaye. Taarifa iliyotolewa na Baraza la Lala Vyema (Better Sleep Council) la nchini Marekani linasema takriban nusu ya watu walio kazini wamethibitisha kuwa utendaji kazi wao umeathirika kutokana na kutopata muda wa kulala; asilimia 26 ya wanaume na asilimia 13 ya wanawake wanakiri kusinzia sehemu zao za kazi.

Muda wa usiku ndio muda utakiwao kulala, ambapo miili yetu imeumbwa katika hali ya kuwa macho mchana na kulala usiku, pia, imeumbwa ipumzike kati ya muda wa jioni, jua lizamapo na Alfajiri jua lichomozapo. Yatakiwa kuwepo na mpango mbadala iwapo kutakuwa na hali tofauti ya kawaida; mfano, Ulaya Kaskazini kipindi cha baridi, Usiku huwa mfupi mno, na kipindi cha kiangazi (joto) huwa mrefu zaidi. Nchini Uskochi Kaskazini (Nothern Scotland) jua huzama kati ya saa 4:30 nne unusu usiku na Alfajiri huchomoza kati ya saa 3:00 Asubuhi. Katika kipindi cha baridi jua huzama kiasi cha saa 9:30 Jioni na huchomoza kiasi cha saa 3:00 Asubuhi.

> Hivi hatukukuumbeni ninyi kuwa ni jozi, (Jinsia mbili tofauti),
>
> Na tukaufanya usingizi kwenu kuwa ni mapumziko,
>
> Na tukaufanya usiku kuwa ni vazi (funiko),
>
> Na tukaufanya mchana kuwa wa mishughuliko (kujitafutia)
>
> (Qur'an 78: 8-11)

Usingizi wa mchana hauwezi kuwa ni mbadala halisi wa usingizi uliopotea usiku. Kupata usingizi vya kutosha wakati wa usiku husaidia mwili kuwa na afya na hupunguza hatari ya kupata maradhi.

Kuna baadhi ya Waislamu wana tabia ya kusalia macho usiku kucha na kulala mchana katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani, ambapo hubadilisha usiku kuwa mchana na mchana kuwa usiku. Hali hii huaribu na kusumbua mpangilio wa asili wa miili yetu.

Jua linapozama chembe chembe zilizomo kwenye ubongo huanza kuzalisha aina za kemikali ambazo huziingiza katika viungo na kuvifanya vipumzike na kujiandaa kulala. Unapokaribia muda wa kulala binadamu huanza kupiga miayo, kope

huwa nzito na harakati zote hupungua. Tunapoingia usingizini ubongo huzuiliwa kupokea kutoka mazingira ya nje.

Kitendo cha kulala huendeshwa na homoni ziitwazwo Melatoni na Serotoni ambazo kwa pamoja zikisaidina na giza la usiku huwezesha upatikanaji wa usingizi vyema. Utumiaji kinyume wa usiku na mchana huharibu maumbile ya kibaiolojia ambayo hutusaidia kuwa vizuri, wachangamfu na kushtuka ifikapo Asubuhi. Usingizi huharibiwa na huwa hausaidii mahitaji ya mwili na akili endapo mfumo wa asili utaingiliwa kati.

Kutokana na kutolala sawa sawa ufanyaji kazi na uwezo wa ubongo huharibika, na mwili hushindwa kuakisi. Hili huwa ni hatari mno pale mtu anapofanya kazi au anapoendesha chombo, ambayo ni mambo yenye kuhitaji umakini na utayari. Mwili ukidhoofika kutokana na kuto kulala, husababisha kuharibu kazi, kutotenda kwa mpangilio au makosa na kupelekea ajali. Kutolala ni deni linalojikusanya ambalo ubongo huzingatia kuwa lazima lilipwe kwa kupata muda na masaa ya kulala vizuri. Wanasayansi wengi wanashauri kuwa usiku mtu anatakiwa alale masaa saba hadi nane kwa afya ya akili na mwili. Upungufu wa usingizi husababisa uzalishaji mdogo. Kukosa usingizi kabisa pia huleta tabu na usumbufu pia huharibu uwezo wa kuelewa.

ATHARI ZA KITABIBU ZITOKANAZO NA KUKOSA USINGIZI

Kiwango cha chini cha usingizi pia huingilia kati uboreshaji wa seli za kinga, uamshaji wa seli za kushambulia, hivyo hudhoofisha kinga za mwili na huongeza hatari ya kupata maambukizi na magonjwa. Mfumo mzuri wa kulala huimarisha afya zetu, kumbukumbu, umakini na utendaji wa mwili na akili. Ulalaji sawa sawa hutuwezesha kufanya kazi ipasavyo na uwajibikaji. Ulalaji wa mpangilio huepusha makosa, maamuzi mabaya, upotezaji wa pesa na matatizo mbalimbali yanayoweza kudhuru afya zetu.

Miili yetu na akili zetu vina mahusiano ya moja kwa moja. Ubongo, mfumo wa ufahamu na mfumo wa kinga wa mwili vina mahusiano kupitia kemikali za ubongo zinazotokea kwenye mfumo mzima wa ufahamu. Usingizi kwa kupumzika hutia nguvu ya nishati, tabia, uwezo wa kufikiri na umakini.



Uchunguzi uliofanywa kwa watu wazima 10,000 umegundua kwamba watu walio kati ya umri wa miaka 32 na 49 ambao hulala pungufu ya masaa saba wakati wa usiku wanauwezekano mkubwa wa kupata ugonjwa wa feta(obese) (Stein 2005).

Hatari zaidi inayowakabili watu wanaobaki macho muda mwingi, wanaosinzia ovyo mikutanoni mchana, wanaokosa muda wa kutosha kulala au wanaolala katika muda usiofaa ni kuongezeka hatari ya kupatwa na magonjwa mbalimbali kama vile saratani ya utumbo na matiti, kisukari, matatizo ya moyo

na unene kupitiliza. Uchunguzi wa kisaikolojia unasema ya kuwa kukosa usingizi kunaufanya mwili uwe na wasiwasi, huongeza homoni zinazozalisha msongo wa mawazo, hupelekea mtu kupata shinikizo la moyo ambalo ni hatari kubwa isababishayo matatizo ya moyo na kiharusi. Watu wasiolala vya kutosha hufanya miili iwe na hali ya kuchemka ambayo hiyo ndio hatari kubwa inayoleta maradhi ya moyo, kiharusi, saratani na kisukari. Ulalaji mchana husaidia kushambulia madhara yatokanayo na kukosa usingizi. Usingizi husukuma mpangilio wa ufanyaji kazi katika mishipa yetu ya damu. Hili laweza kueleza kwa nini watu hupatwa na matatizo ya moyo na kiharusi wakati wa Asubuhi mapema. Kemikali za plotoni zinaweza kuzuia seli haribifu zisizalikane, hivyo husaidia kuzuia kansa (amesema hayo Schernmamer wa Shule ya Kitabibu ya Havard). Unapopigwa na mwanga usiku unazalisha plotoni kiwango kidogo na huongeza hatari ya kupatwa na saratani. (Stein 2005).

Matatizo mengine mabaya zaidi yanayohusiana na kukosa usingizi hujumuisha saratani katika mfumo wa kizazi. Watu wanaokurupuka usiku mwingi au kuamka mara kwa mara wanakumbwa na matatizo haya haya. Vile vile kukosa usingizi mwanana huibua homoni za ghrelin na leptine ambazo hushugulika na hamu ya kula.

Kulala mapema, kuamka mapema,
hufanya mtu awe na afya, busara na hekima.

Vileo: Unywaji & Uzuiaji wa Madawa ya Kulevya

Kwa kuendelea na mada yetu ya afya njema ya mwili, wazazi na watoto ni lazima waepuke vileo. Hii hujumuisha sigara ambazo nazo ni hatari mno kwa mama wajawazito, watoto na manii ya baba.

Theluthi ya uzito wa kinga una thamani kubwa kuliko kilo ya tiba.

Sigara ni finyango ya tumbaku iliyokusanywa kwenye karatasi na kuwekwa moto upande mmoja na upande wa pili kuwa na kipisi mpumbavu.

Ulevi au utumiaji wa dawa za kulevya unahitaji weledi wa kitabibu na tiba ya kiakili. Matatizo si lazima kusababishwa na kosa kubwa sana; pia husababishwa na

mjumuiko wa mambo madogo madogo. Endapo wazazi watafanikiwa kutengeza familia yenye furaha na upendo, watoto wao si rahisi kwenda kutafuta starehe nje ya nyumbani kwao.

Ulevi na kutumia dawa za kulevya kama bangi, kokeni na heroini husababisha uharibifu katika seli za ubongo pia uharibifu katika mfumo wa uzazi, mzunguko wa damu na mfumo wa upumuaji. Utumiaji wa madawa haya humfanya mtu awe katili, awe na dhana mbaya na uhalisia na akose mwamko. Uvutaji wa bangi hata kidogo kunapelekea kurukwa na akili.

Watoto na Vishawishi

Watoto wanaweza kualikwa na marafiki au shinikizo rika kujaribu mambo yasiyofaa. Wanatakiwa wawe imara kutoshawishika na kubaki salama bila ya kuathirika na madawa. Ujana wa kati ya miaka (14-20) ndicho kipindi cha changamoto mno katika maisha. Kutafuta elimu na kufahamu ni jambo muhimu mno katika kipindi hiki. Ni vyema kucheza na mazingira ya watoto ili waweze kujua nini wafanye mara tu vishawishi au shinikizo rika vinapojitokeza. Mtu mmoja kati ya wawili nchini Marekani amekwishakunywa au anakunywa pombe au amekwishajaribu aina yeyote ya dawa za kulevya.

Kuzungumzia tu juu ya hatari haiwezi kumfanya mtu aache kunywa pombe au kuvuta sigara- kama mzaha, kuangalia filamu za kutisha juu ya madhara ya uvutaji sigara kwenye mapafu kunaweza kukamfanya akimbilie haraka akavute. Misukumo inabidi ijadiliwe na pia kuangalia namna ya kuizuia.

Yatakikana wazazi wawaelezee watoto malengo yaliyo nyuma ya vishawishi vya utumiaji wa dawa za kulevya, ambapo kwa sehemu kubwa ni kupata athari tamu na kujihisi raha. Hisia hizi bandia za kujihisi raha ni za muda mfupi tu, na hufuatiwa na anguko na kuharibikiwa vibaya kabisa.Endapo wasipoambiwa hili, vijana wanapokutana na wengine wanaoonekana kufaidi na kuburudika na madawa, watadhani kwamba wazazi wao wamewadanganya. Wanahitajika wafahamu kwamba starehe hizi zina malipo makubwa, na furaha ya kipindi kifupi mno na kufuatiwa na maumivu ya muda mrefu. Qur'an inaelezea kwa ufasaha pande zote mbili inapohusisha pombe na kamari. Inasema:

> Wanakuuliza kuhusiana na pombe na kamari, waambie kuna madhambi makubwa kwenye hayo mawili, na kuna baadhi ya manufaa kwa watu, lakini madhambi yake ni makubwa mno kuliko faida.
>
> (Qur'an 2:219)

Kwa mujibu huo, faida kiasi ya unywaji pombe kwenye jamii na uzuri unaodhaniwa, yaweza kuwa nzuri kwenye moyo au ubongo, lakini madhara yake kiujumla ni mazito mno ukilinganisha na uchache wa faida.

Alama za awali za kumgundua mtumiaji madawa: Mzazi Afanye Nini?

Kuna alama nyingi za mtumiaji wa dawa za kulevya, zilizo mashuhuri zaidi ni:

Majani boksi ya sigara yaliyochomwa, mifuniko ya makopo au bakuli zilizounguzwa, vioo na nyembe, rundo la makaratasi, makopo yaliyotapakaa au chupa za vimiminika, maboksi ya sigara, leso, chupa za vidonge, damu kutawanyika bafuni au katika nguo za vijana, kijana kukataa kukunja mikono ya shati lake, kubadilika hamu ya kula, kuchukia vitu vitamu, kuchelewa kwenda kulala, kuchelewa kuamka, simu zisizoeleweka, na tabia za usiri.

Kijana anaweza kuathirika na madawa bila ya kuonekana dhahiri au macho kubadilika, na anaweza kutumia dawa kwa usiri mkubwa. Kama wazazi watatilia shaka mienendo ya watoto wao, ni vyema wakachunguza kama midomo au pua za watoto wao zimevimba au endapo kama wana muonekano wa kilevi au kupagawa. Kama wanaambatana na wavutaji wanaojulikana waziwazi, wazazi wanatakiwa washituke.

Vitu atakiwavyo mzazi kufanya ili kuzuia ulevi

- Katika hali yeyote anatakiwa aimarishe imani ya familia, kwani imani ndio kinga bora. Madawa, pombe, na kamari vimeharamishwa vikali kwa Muislamu. Neno *Khamr* limetumika katika (Qur'an 2:19) likimaanisha kinacholewesha, pia hutumika katika kila kinachoondoa ufahamu na kupoteza kujitambua kwa anayetumia.
- Elimisha familia yako juu ya magonjwa yatokanayo na kuvuta sigara, unywaji pombe na utumiaji wa dawa za kulevya ili wawe na ufahamu na athari zake zenye madhara. Kumuona aliyeathiriwa na dawa za kulevya pia inaweza kusaidia watoto. Watoto wapewe kazi za kuandika kuhusiana na hatari ya dawa za kulevya na pombe kijamii, kiafya na kiuchumi. Watoto pia wanatakiwa waelezee suala hili mbele ya familia. Endapo watahitaji pesa katika kufanyia utafiti ni vizuri wakapata.
- Uangalizi wa wazazi ni kizuizi bora. Vijana wadogo hawawezi kujisababishia madhara kama wazazi wanawachunga kwa umakini. Watoto wasiruhusiwe kuzurura usiku, wasiachwe peke yao majumbani pale wazazi wanapotoka kufurahi. Wazazi wanatakiwa wajenge mazoea ya kuwa karibu na kuzoeana na familia zao, pale inapowezekana, na wajipangie muda mwingi kuwa pamoja na familia ndani au nje ya nyumbani. Zaidi ya hayo, kuwapatia watoto kiasi kikubwa cha pesa kutawaharibu watoto na kuwafanya wanunue vitu haramu.
- Wazazi wanatakiwa wakague vyumba vya watoto wao, mara kwa mara. Pia ni

vyema wakiwaambia watoto kuwa wanafahamu kwamba wanahitaji faragha. Wazazi hawatakiwi kusema "nafanya hivi kwa manufaa yako mwenyewe", bali anatakiwa aseme "nina wajibu kuhusiana na usalama na mustakabali wako". Hii haimaanishi kuwa ni uvamizi wa faragha lakini ni kutafuta sababu ya kweli na ya uhakika na ambayo wazazi wanaweza kuelewa. Wazazi pia wanatakiwa wawe wanapekua mifuko, mabegi, na mapochi ya watoto wao kila baada ya muda bila ya wao wenyewe kujua.

- Faragha iliyopitiliza kwa watoto huweza kuwa na madhara. Wasiruhusiwe kuwa na seti ya Televisheni, simu au kompyuta iliyounganishwa na mtandao vyumbani mwao. Takwimu za utumiaji ulevi zinaonesha ongezeko kubwa la unywaji pombe kati ya vijana wa miaka 11-13 nchini Uingereza (2009).
- Chagua vijana sahihi. Wazazi wanatakiwa wawachagulie marafiki watoto wao katika jamii, ndugu, na majirani. Wazazi wajitahidi kupata aina nzuri ya marafiki kwa watoto wao, ni jambo linalohitaji juhudi.

Licha ya juhudi zote hizi za kuzuia, kuna wakati fulani kijana wa kiume au binti wa mtu huangukia kwenye matatizo. Usifadhaike, kuchanganyikiwa, hasira na kuteseka husababisha uharibifu zaidi. Ushauri wa kitaalamu, ulioambatana na nasaha utamsaidia mzazi kutatua matatizo. Ni muhimu wazazi wakazizuia hisia zao na waweke mazingira katika hali inayotakiwa. Kwa kutumia ushauri wa kitaalamu unaweza kuzalisha tiba kamili au nusu ya tiba katika mambo mengi. Mambo ya tiba na ushauri ni ya kuzingatiwa. Kitu wazazi wasichotakiwa kufanya ni kuficha tatizo au kushindwa kuomba msaada kutokana na kuhisi unyanyapaa kuwa na familia iliyoathirika na madawa au kwa kuogopa hatua za kisheria. Ili kuepuka hasira zilizopitiliza, wazazi wanaweza kuchukulia kuwa si mtoto wao aliyewafuata kwa ushauri bali ni mtoto wa jirani. Hii ni mbinu nzuri itakayomuwezesha kufikiri kwa upole na kutafuta palipo na tatizo. Hakuna aliye pekeyake katika tatizo hili, bali kuna Mamilioni ya familia yanasumbuliwa na tatizo hilo hilo. Wazazi na watoto wanahitajika kuzungumzia yafuatayo:

1. Pombe ndiye mama wa maovu yote

Uthman Bin Affan katika kuhadithia hatari ya kutumia vilevi alisimulia kisa cha: Mtu mmoja alilazimishwa kuchagua dhambi moja kati ya hizi tano ambazo ni; kuchana nakala ya Qur'an, kuua mtoto, kuabudu sanamu, kunywa pombe au kufanya mapenzi na mwanamke (nje ya ndoa). Alichagua kunywa pombe hatimaye akafanya mapenzi na mwanamke, akaua mtoto, akachana Qur'an, akasujudia sanamu. Somo la hapa ni: Pombe ndiye mama wa maasi yote.

2. Kokeni huumiza kiumbe tumboni

Mnamo katikati ya miaka ya 1980, kulikuwa na janga la utumiaji wa dawa za kulevya nchini Marekani. Uchunguzi wa wataalamu wa mambo ya watoto uligundua kuwa watoto wanaozaliwa na wanawake wanaotumia madawa hawakuwa sawa na watoto wengine. Wao walikuwa na uzito mdogo, walitetemeka, wakilia hawabembelezeki, hawataki kukumbatiwa au kuguswa, walikuwa wanastuka hata kwa sauti ndogo.

Ushauri wa Mlevi kwa vijana

■ **Pegi moja ya pombe ni nyingi mno, lakini pipa halitoshi!**

Usijaribu kunywa pombe, hata kwa pegi moja. Uanzapo kujaribu kunywa utaendelea kunywa tu na hata pipa halitakutosha. Utaendelea na vilevi vingine vya hatari zaidi. ■

3. Si kila mtoto ni mkosa hatia: Mnamo mwaka 1987, kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu wa Amerika Kaskazini alimualika Mkuu wa Polisi wa eneo la Herndon, Virginia, aje kuendesha semina juu ya kuzuia ulevi. Mkuu wa Polisi alisimulia stori hii: Nilipokea mashtaka mengi yanayohusiana na upoteaji wa vitu vya thamani katika eneo langu. Nikamtilia mashaka kijana mmoja wa miaka 14, nikaenda kwa wazazi wake nikiwa na waraka unaoniruhusu kupekua chumba chake cha kulala. Kwa hisia kali wazazi wake walisema 'haiwezekani kuwa ni kijana wetu, yeye ni kijana mzuri.' 'Nikawauliza mumeshachunguza chumba chake?' Wakasema 'hatujawahi, ila huwa anasema, hiki ni chumba changu binafsi na sisi haturuhusiwi kuingia, muda wote anakifunga kwa kufuli.' Nilipovunja kile chumba nikakuta vitu vya thamani vilivyoibiwa televisheni, kamera, stereo, saa na vito vya thamani. Nikawashauri wazazi, japo wamempa chumba binafsi, ninyi ndio mnaomiliki nyumba, mna haki ya kuingia, na ni wajibu wenu kuchunguza mara kwa mara.

Hili linaweza kumtokea mwanao? Haliwezi kumtokea kama utafuata ushauri wa afisa huyu wa polisi.

KUATHIRIKA DHIDI YA UHUSIANO MZURI NYUMBANI

Wazazi wajiulize wenyewe maswali ya msingi, "hivi sisi tuna mahusiano mazuri na watoto wetu?" Hivi tunahisi tuko mbali nao? Uhusiano mzuri unaweza kutafsiriwa kama hisia za kufurahi, kuhisi vyema pale unapoona wanao pia wanafurahi na kujihisi vyema wanapokuona. Watu wanapokuwa na wengine huwa wanataka kuwa nao karibu muda wote. Wanafurahi wanapobadilishana fikra na mazungumzo pamoja nao.

Watu hulowea katika matumizi ya vilevi na madawa pindi wanapohisi kutengwa. Nchini Marekani watu wazima kuanzia miaka 18 na kuendelea wapatao Milioni 16.6 (sawa na asilimia 7 ya watu wa rika hili) walikuwa na tatizo la kutumia vilevi kupindukia mnamo mwaka 2013 (Taasisi ya serikali inayojihusisha na masuala ya matumizi mabaya ya vilevi na ulevi).

Nchini Uingereza, asilimia 12 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi ya hapo walibainika kuwa na madhara yatokanayo na utumiaji wa vilevi mnamo mwaka 2010. Unywaji wa vilevi kupindukia kwa watu wenye umri zaidi ya miaka 15 umekithiri nchini Uingereza kuliko nchini Marekani. Nchini Uingereza ni asilimia 23.7 hadi asilimia 30.4 wakati nchini

Marekani ni asilimia 13.4 hadi asilimia 19 (Shirika la Afya Duniani-WHO, 2014). Watu walioathiriwa na vilevi hawapendi kuzungumza au kucheza na watoto wao.

Pindi wazazi wanapotengana na watoto wao, vilevi, dawa za kulevya na uvutaji huwa viburudisho mbadala vya kuwaridhisha watoto. Utumiaji wa vilevi huhusiana na matukio ya kujiua na msongo wa mawazo.

Weka uhusiano mwema na wanao kwa kuwa mfano mwema. Nini wazazi wanachotakiwa kuwaambia watoto wao kama wao wenyewe ni wavutaji, walevi au wanatumia dawa za kulevya? Hakuna mbadala zaidi ya mtu kuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa watoto wake. Hata hivyo, kama wazazi wameathiriwa na magonjwa haya na hawawezi kujisafisha basi angalau wakiri mapungufu yao. Eleza madhara kwa watoto wako, washauri jinsi ya

Mtoto anaweza kuwa salama endapo wazazi wote wawili wanavuta sigara? Au wanatumia dawa za kulevya? Hadithi binafsi.

> Licha ya kuwa wazazi wangu walikuwa ni wavutaji, kamwe mimi sikuvuta. Sababu baba yangu alikuwa akiniambia
>
> "oh Mwanangu, mimi ni muhanga wa tabia hii mbaya, natamani ningeweza kuiacha ila sina dhamira kubwa ya kufanya hivyo. Hili ni tatizo na linadhuru afya yangu."
>
> Nilipokuwa nikisafisha mapovu, na moshi mweusi ulioganda kwenye Shishah (kiko), alikuwa akiniambia
>
> "Oh mwanangu uchafu wote huu umejaa kifuani mwangu!"
>
> Kama wazazi wanajiona wanafanya kosa, wanatakiwa wakiri na wawaeleze watoto wao madhara yake. Huenda watoto wanaweza kuelewa somo na wakajiepusha na mienendo hiyo.
>
> Kanuni kama hii inaweza kutumika kwenye tabia yoyote mbaya: uvutaji, unywaji, kuchelewa kulala, kulala kulikopitiliza, tabia ya ulafi, utafunaji kucha, kuzungumza kwa makelele au kuzungumza sana, kutopenda kusikiliza wengine. Hata hivyo ni vyema wazazi wakachagua umri na mazingira ya kuelezea tabia zao mbaya ili kuepuka watoto kupoteza uaminifu, kujiamini na heshima kwao.

kuepuka makosa kama hayo. Waoneshe jinsi gani pombe na utumiaji wa dawa za kulevya ulivyo ni balaa. Kuwa muongo au mnafiki kutafanya hali kuwa mbaya zaidi, sababu watoto watadhani kwamba mtu anaruhusiwa kuwa muongo au mnafiki.

MPANGO BAADA YA HUDUMA: DINI KAMA KINGA

Huduma katika kituo cha tiba mbadala ndio hatua muhimu na pekee ya tiba kama kijana wa kiume au binti ameangukia kwenye vilevi, tiba mbadala ndio hatua muhimu kama ifuatavyo. Kukosekana kwa tiba mbadala stahiki, juhudi za wazazi, za watoto na huduma za kituoni zitapotea bure. Mpango wa baada ya huduma humaanisha mchakato endelevu uliopatikana katika kituo cha tiba ambapo tiba huwa endelevu.

Wazazi huwa na wakati mgumu kipindi cha kufuatilia tiba ya baada. Huduma ilikuwa ya kutosha na mtoto ameimarika, wazazi hawakuweza kufikiria kama mtoto angelirudia. Hata hivyo, jambo muhimu wazazi waliendelea na tiba. Kijana wao angali bado anakubali kuachana na tabia mbaya, kupigiwa simu ni mara moja, kutokuwasiliana na makundi maovu, kuonja kidogo, kunusa, kupasua au kuachana kabisa na kutumia kemikali! Hatimaye ni kushinda vita au kushindwa katika huduma ya tiba baada.

Scott (1989), anaeleza kwamba huduma katika vituo vya tiba kwa wanaotumia madawa mara nyingi hujumuisha na dhana ya tiba za "kiroho". Japo Mungu hubezwa katika uga wa saikolojia lakini wao hutumia hivyo.

Wataalamu wa mambo ya ushauri nasaha wanajua kwamba programu za kidini zina tija. Hakuna kingine kinachoweza kufanya kazi vyema.

Wazazi wanahitajika wawe na uangalizi makini hasa katika mambo yafuatayo: Kama watoto wanajidhuru (wanataka kujiua), hawashauriki, wanahatarisha wengine, wanahitaji kuondolewa sumu kutokana na kudhurika na madawa, kama anahitajika kupelekwa kwenye kikundi au shule ya kurekebisha tabia au kama anaambatana na makundi movu.

Kama wazazi watahitaji kwenda katika vituo vya serikali watahitajika kupanga ziara za kila wiki kwa mtu wa dini mwenye busara ili kumuweka mtoto wao karibu na Mwenyezi Mungu

Kuvunja Sheria

Utumiaji vilevi humfanya mtumiaji avunje sheria au awe kijana mtukutu. Kijana mtukutu ni yule ambaye yupo chini ya miaka kumi na saba lakini tabia zake zinamuingiza kwenye kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Wazazi wengi hawaamini kama watoto wao wanaweza kufungwa jela siku moja, ni jambo ambalo lipo na hutokea. Jambo hili linawezekana kuzuiliwa kama wazazi watajenga tabia ya kuheshimu sheria mbele ya watoto wao. Kama wazazi hawaheshimu kasi ya kuendesha magari, wanavuka penye taa nyekundu, wanadanganya kulipa kodi, wanawaongopea maafisa forodha, wanaiba ofisini au kiwandani na kwa makusudi wanatoa sababu za uongo kwa maandishi pale watoto wanapotegea kwenda shule, hivyo watoto nao watahisi kwamba uongo si tatizo na hauna madhara. Wazazi

wakiwachukulia polisi kama maadui watoto nao hawatawaheshimu polisi.

Kuna baadhi ya wahamiaji huwa na dhana mbaya kwamba kwa kuwa wao wanaishi kama kundi la watu wachache katika nchi inayoongozwa na mfumo wa sheria za umma basi wako huru kuvunja sheria hizo. Kuondoa ufahamu huu mbovu, Sheikh Taha Jabir Al Alwani, mjumbe wa bodi ya IIIT, anasema: Endapo mtu ataingia nchi ya kigeni, maana yake ni sawa na kusaini "Mkataba" na taifa hilo ya kwamba atatii katiba yao na sheria. Kwa kufanya hivyo Muislamu atatakiwa kuheshimu makubaliano yote ya mikataba kama Qur'an na Hadithi za Mtume zilivyoelezea. Kama hakusudii kufuata sheria za nchi hiyo, basi ajizuie asiingie au atangaze kutotii kwake sheria zao ambapo mahakama itahukumu aondolewe nchini humo.

Kama raia wa nchi fulani hawaitaki sheria fulani, wanaweza wakaibadilisha kisheria na kwa kufuatana na taratibu za kidemokrasia zilizowekwa na katiba. Uislamu unakataza watu binafsi kujichukulia sheria mkononi na kuzifanya wanavyotaka. Bila shaka jambo hili litapelekea vurugu, kutokufuata sheria na dhuluma. Katika hali hiyo hiyo Muislamu hatakiwi atende dhulma katika ardhi ambapo sheria za jamii zimeamrisha pia Muislamu hatakiwi atii sheria inayomtaka atende haramu. Pale sheria inapokuwa ni ya dhuluma upingaji sheria hiyo kwa njia ya amani ndio njia ya kuibadilisha, kama ilivyooneshwa na Thoreau, Gandhi na Martin Luther King.

Muda mrefu kabla ya hao wote Mtume Muhammad (Rehema na Amani ziwe juu yake) alikabiliana na watawala wa Maqureish na akaongoza watu wake kwa amani kwenda kuhiji Makka bila ya vurugu hatima iliyopelekea kupatikana mkataba wa Hudaybiyyah mnamo mwaka 630.CE

Mwili ni amana: Ni neema isiyo na mbadala

Tuna neema zisizohamishika, neema zinazohamishika na neema zisizo na mbadala, miili yetu ni neema isiyo na mbadala. Japokuwa tunaweza kununua magari zaidi, nyumba zaidi, na samani, lakini mwili tunao mmoja tu. Na hii ni amana kwetu iliyotoka kwa Mungu.

Lazima tuitunze kwa kufuata namna ya kuitumia kulikowekwa na Muumba. Jukumu letu ni kama watunzaji tutakaowajibishwa kwa utunzaji wetu kwake.

Hili hutafsirika katika nyanja kubwa zifuatazo:

Usafi, lishe, mazoezi stahiki, kulala, kuepuka ulevi na kutofanya mapenzi nje ya ndoa.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 32: JEDWALI LA RATIBA YA UPIMAJI AFYA

Kaa na familia yako na chora jedwali la ratiba ya uchunguzi wa afya ikijumuisha huduma ya meno. Shauriana na mkutubi wa maktaba, mwalimu, muuguzi, daktari au hospitali. Mwisho wa kukamilika jedwali kila mwanafamilia apate nakala yake.

ZOEZI LA 33 : MPANGILIO WA MAZOEZI YA MWILI KWA FAMILIA

Jadili hali ya mazoezi ya mwili katika familia yako na watoto. Kisha muafikiane familia kiujumla juu ya mpango wa kufanya mazoezi na kuweka ratiba ya kufanya mazoezi mepesi. Jaribu kuongeza kiwango cha mazoezi kidogo kidogo na muda baada ya muda. Jaribu kutembea kwa miguu badala ya kutumia gari, pia wakati fulani kufua nguo kwa mikono badala ya kutumia mashine. Jiwekee bajeti ya kununua vifaa vya michezo, ada ya kujiunga na klabu za michezo na kununua chakula cha kujenga afya.

ZOEZI LA 34 : JENGA UTAMADUNI WA KUTUMIA MAAMKIZI YENYE MAANA

Wazazi wanapokutana na baadhi ya watoto kwa mara nyingine badala ya kuwaambia «MAMBO, INAKUWAJE, HALI YAKO» wajaribu kuwasalimia kwa salamu za upendo na kuonesha kujali, mfano:

- Umekula chakula cha kujenga afya leo?
- Umefanya mazoezi ?
- Umepata usingizi vizuri ?
- Umetabasamu kwa wazazi wako? Marafiki?
- Leo umesoma kitu chochote ?
- Leo umesalimiana na wazazi wako? Umewabusu?

- Leo umemsaidia mtu?
- Leo umetoa swadaka yeyote?
- Umesali?

Si lazima kufuata mlolongo huo wote bali baadhi tu ya maswali yanatosha. Ongezea jambo lolote halisi linalohusiana na masuala binafsi ya watoto.

ZOEZI LA 35 : MWENENDO WA KULALA

Waelezee watoto kulala kiafya na tabia ya kula kiafya:

Hadithi aliyoipokea Ibnu Maajah inasema: Siku moja Mtume (Swalla Allahu Alayhi Wasallam) alipita msikitini akamkuta mtu amelalia tumbo, (kifudifudi). Akamuamsha kwa kumgusa kwa mguu (akimwambia) "usilale kwa namna hii, kwani ni namna ambayo Allah na Mtume Wake wanaichukia". Vivyo hivyo Mtume (Swalla Allahu Alayhi Wasallam) aliwazuia watu kula huku wakiwa wamelalia tumbo.

Kulalia tumbo siyo vizuri kiafya kwa mgongo na viungo vya ndani. Kulalia upande wa kulia ni jambo lenye manufaa zaidi. Kulalia upande wa kushoto husababisha mapafu, tumbo na ini kwenda kinyume na mapigo ya moyo, hivyo kusababisha msongo.

Ni tabia nzuri kufuata ratiba; kulala mapema baada ya sala ya *'Isha'* na kuamka mapema kwa ajili ya sala ya *Alfajir* kabla ya kuchomoza jua.

Tabia ya Mtume (Swalla Allahu Alayhi Wasallam) ilikuwa ni kulala kidogo baada ya swala ya *Adhuhur*. Madaktari wamegundua kwamba kulala mchana husaidia kuongeza nguvu katika ubongo na katika viungo, kuupumzisha mwili wakati katika asili ya maumbile mapumziko hutokea, huongeza uzalishaji na tahadhari, hurekebisha hisia na hasira na kupunguza ajali.

ZOEZI LA 36: KUJENGA MAZINGIRA MAZURI NYUMBANI

Wazazi lazima wakae chini na kujadiliana na watoto wao na kukubaliana njia nyepesi ya kuyaendea yote yafuatayo nyumbani :

Upendo, furaha, ucheshi, uhuru wa mawasiliano, kuaminiana, faraja na pongezi wakati wa mafanikio. Pia kujali maslahi ya watoto wao; kula, kusali na kucheza pamoja, kuheshimu na kuheshimiana, kubusu, kukumbatiana na kutabasamu.

Hata kama hawakuzoea kufanya hivyo, bado hawajachelewa kuyafanya yote hayo hasa kwa dhati.

ZOEZI LA 37 : KUJADILI KWA UMAKINI ALAMA ZA UTUMIAJI DAWA ZA KULEVYA

Lazima wazazi wakae pamoja na kujadili nini wafanye watakapogundua alama kwamba watoto wao wanatumia dawa za kulevya. Lazima zijumuishe njia; kushauriana na wataalamu, kufundishana na kuongea na marafiki na ndugu wenye busara. Kuhamaki, huzuni kubwa, kupiga na kulazimisha havisaidii. (hizi hudhoofisha hisia na kufanya mambo yawe mabaya zaidi).

ZOEZI LA 38 : IGIZA KAMA AFISA POLISI

Wazazi wanaweza kuwashauri vijana wao kujifikiria kuwa kama maafisa wa polisi, mahakama au wafanyakazi wa huduma za kijamii wanaotakiwa kufanya kazi zao. Wanawajibu gani? Ni mambo ya namna gani yametokea wakati wa mchana? Kazi zao ni nzuri au haziridhishi? Wanaweza kufikiria wenyewe kuijali jamii, kuwatambua wahalifu na mengineyo?

Majukumu haya huwasaidia watoto kutambua kwamba Afisa Magereza, Walimu, Zimamoto, Askari Polisi wa kiume na wa kike ni watu wa kawaida ambao wana hisia, nyumba na matatizo kama wengine wowote. Kama vijana wana matatizo katika sehemu hizi, hivyo wazazi inabidi wawatambulishe kwa Afisa wa Polisi halisi au mfanyakazi halisi wa huduma za jamii na kuwaacha wapate habari zaidi kuhusu kazi hizo.

Utembeleaji wa mahakama ni uzoefu wa kukumbukwa. Kuona sehemu inavyofanana na kuelewa nini la kufanya na namna gani unatakiwa uwe inaweza kuwa ni elimu tosha. Ni wazo vizuri kuandaa uzinduzi mdogo wa matembezi kwa watoto.

10

SURA YA KUMI

- **UNYONYESHAJI**
  Maziwa ya Mama

SURA YA KUMI **236**

Unyonyeshaji: Maziwa ya Mama **236**

Utangulizi 238
Unyonyeshaji katika Qur'an 239
Kiwango cha Unyonyeshaji nchini Marekani na Uingereza 245
Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto nchini Marekani 245
Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto nchini Uingereza 246
Maziwa ya Kiwandani, ukuaji duni na maradhi 246
Maoni ya Imamu Ali na Ibn Hazm Kuhusu Unyonyeshaji 248
Muda wa Unyonyeshaji 248
Dondoo Muhimu kwa akina Mama Wanyonyeshaji 249
Mlo unaopendekezwa kwa Mama anayenyonyesha 251
Taifa imara: kimwili 252
Kazi za kufanya

Utangulizi

Unyonyeshaji ni hatua muhimu ya kuwakuza watoto wenye nguvu na afya tele kimwili na kiakili. Inasisitizwa katika Qur'an kuwa unyonyeshaji na uendelezaji wa uhusiano wa kiukoo hutokana na kunyonya maziwa ya mama mmoja. Uhusiano huu huitwa ukoo wa maziwa na watoto huitwa watoto wa maziwa.

Kwa mfano, kwanini Salah mwenye umri wa miaka ishirini (20) kutoka Uturuki hawezi kumuoa Fatimah, msichana kutoka Indonesia? Jawabu ni kwamba, wakati Salah akiwa na umri wa mwaka mmoja, alinyonyeshwa na mama yake Fatimah kwa siku kadhaa. Hii inamfanya Salah kuwa kaka kwa Fatimah na hivyo kutokuwa na sifa ya kumuoa Fatimah. Vile vile, dada zake Fatimah wote pamoja na shangazi zake moja kwa moja wanakuwa dada na shangazi zake Salah na hivyo, kutofaa kuolewa na Salah kwa kuwa ni *mahrim* zake. Hivyo, hakutakuwa na *hijjab* kati yake na ndugu zake hao. Ingawa ni rahisi kuelewa undugu wa damu pamoja na undugu wa kiimani, tunawezaje kufahamu kwamba kiasi kidogo tu cha maziwa ya mama kinaweza kumfanya mtu asiye na uhusiano kuwa kaka au dada? Hii inaonyesha baadhi tu ya umuhimu wa maziwa ya mama. Fikiria kwa mfano, kuongezewa damu. Hata kama damu yote ya mtu itabadilishwa kabisa na damu ya mtu mwingine, kitendo hicho hakiwezi kuwaunganisha watu hao wawili kuwa na uhusiano wa kindugu hata kama tukio hilo likifanyika kwa muda mrefu.

Kuongezewa damu ni hitajio muhimu sana na pia kuwekewa kiungo husaidia kuboresha maisha yetu, bado yote hayo hayawezi kuunganisha undugu wa kisheria hata kama ni makubwa kwa kiwango gani. Wasomi wanakubaliana kuwa hifadhi ya maziwa (benki ya maziwa) imekatazwa katika Uislamu. Hakika undugu kupitia maziwa ya mama umewekwa san-

jari na uhusiano wa familia ya kuzaliwa (Qur'an 4: 23). Hata hivyo, sheria za mirathi hazitumiki katika undugu wa namna hii.

> *Mmeharamishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na khaalati zenu, na binti wa ndugu mume, na binti wa dada, na mama zenu waliokunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu. (Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu. Na kuwaoa pamoja dada wawili isipokuwa yale yaliyokwisha pita. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu.*
>
> (Qur'an 4:23).

Qur'an tukufu inasisitiza unyonyeshaji na kumtunza mama mnyonyeshaji katika kipindi cha miaka miwili. Kukosekana kwa mapenzi na uadilifu kunaweza kusababisha mtindio wa ubongo. Katika mkutano wa habari na waandishi wa habari, Ikulu ya Marekani, ulioandaliwa na Rais Clinton, wataalamu walisisitiza bila shaka kuwa "akili za watoto wachanga ziko vizuri kutoka wakati wa kuzaliwa na huongozwa na matukio ya mwanzo" (Begley na Wingert, 1997).

Miaka miwili ya mwanzo wakati wa unyonyeshaji huchangia sana katika akili ya mtoto. Mahakama nchini Misri ziliainisha sifa tano zinazopaswa kuzingatiwa ili undugu wa maziwa uweze kupatikana.

- Angalau ufanyike mara tano.
- Kila anyonyweshapo mtoto lazima atosheke.
- Kila anyonyweshwapo mtoto unapaswa kuwa wakati tofauti wa kupata chakula, siyo mfululizo.
- Kunyonyesha mara tano lazima kuthibitishwe na mashahidi wa kuaminika.
- Kunyonyesha huko kwa mara tano lazima kufanyike kabla ya umri wa miaka miwili.

Unyonyeshaji katika Qur'an

Qur'an tukufu imeelezea unyonyeshaji katika sura nne tofauti, ikiwasisitiza kina mama kuwanyonyesha watoto wao kwa muda wa miaka miwili. Mama anyonyeshaye hatahusika na majukumu ya kujitafutia riziki akiwa katika jukumu la kunyonyesha hata kama akiwa ametalikiwa ili apate fursa ya kumnyonyesha mtoto ipasavyo. Ikiwa baba atafariki, ndugu zake watabeba jukumu la kumuhudumia mama anayenyonyesha kwa mantiki hiyohiyo. Ibada mbalimali zimefanywa kuwa nyepesi kwa wanawake wa Kiislamu, wakiwemo wanyonyeshao. Wamepewa fursa ya kutoshiriki swala za jamaa za kila siku pamoja na swala za Ijumaa. Hii imefanywa kuwapa kina mama muda wa kutosha wa kuwalea watoto. Pia inampa mama muda wa kutosha wa kuwa na watoto yeye mwenyewe badala ya kumwachia jukumu hilo yaya. Katika kipindi cha miaka miwili,

mtoto humtegemea sana mama yake kimwili, kisaikolojia na kihisia.

Chupa ya plastiki ya kunyonyeshea haiwezi kuchukua nafasi ya matiti laini ya mama pamoja na mapenzi ya mama. Madhara ya kimwili na ya kiakili yanayotokana na mtoto kutonyonya maziwa ya mama yanaweza kuwa magumu kuyatibu mbeleni na kwamba madhara yanaweza kukua na kuwa ya kudumu. Qur'an inafafanua unyonyeshaji katika aya zifuatazo;

1.*Na wazazi wanawake wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili kwa anayetaka kutimiza kunyonyesha. Na juu ya baba yake chakula cha kina mama, na nguo zao kwa mujibu wa ada. Wala halazimishwi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Mama asitiwe tabuni kwa ajili ya mwanawe, wala baba kwa ajili ya mwanawe. Na juu ya mrithi mfano wa hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa kwa kuridhiana na kushauriana, basi si vibaya kwao. Na mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha basi hapana ubaya kwenu mkitoa mlichoahidi kwa mujibu wa ada. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anayaona yote mnayoyatenda.*

(Qur'an 2:233).

2.*Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru mimi na wazazi wako. Ni kwangu mimi ndiyo marudio.*

(Qur'an 31:14).

3. *Na tumemuusia mwanadamu awatendee wema wazazi wake wawili. Mama yake amechukua mimba yake kwa tabu, na akamzaa kwa tabu.*

4. *Na kuchukua mimba kwake hata kumwachisha ziwa ni miezi thelathini. Hata anapofika utu uzima wake, na akafikia miaka arubaini, husema: Mola wangu Mlezi! Niwezeshe nishukuru neema zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na nitende mema unayo yapenda. Na unitengenezee dhuriya zangu. Hakika mimi nimetubu kwako, na mimi ni miongoni mwa Waislamu.*

(Qur'an 46:15).

5. *Wawekeni humo humo mnamokaa nyinyi kwa kadiri ya pato lenu, wala msiwaletee madhara kwa kuwadhiki. Na wakiwa wana mimba, wagharimikieni mpaka wajifungue. Na wakikunyonyesheeni, basi wapeni ujira wao, na shaurianeni kwa wema. Na mkiona uzito kati yenu, basi amnyonyeshee mwanamke mwengine.*

(Qur'an 65:6).

6. *Mwenye wasaa atoe kadiri ya wasaa wake, na mwenye dhiki atoe katika alicho*

mpa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu ila kwa kadiri ya alicho mpa. Mwenyezi Mungu atajaalia baada ya dhiki faraja.

(Qur'an 65:7).

Ikiwa mama hawezi kumyonyesha mtoto kwa kukosa maziwa, basi mama mwingine atatafutwa aweze kumnyonyesha mtoto huyo, hivyo kuwa mama yake kupitia kunyonyesha na hivyo ana haki zote kama mama isipokuwa haki ya kurithi. Watoto wa mama huyu pia watakuwa ndugu kwa mtoto aliyenyonyeshwa na mume wa mama huyo anakuwa baba kwa mtoto aliyenyonyeshwa kwa sababu hiyohiyo. Hakuna ndoa inayoruhusiwa kati ya mtoto kwa kunyonyeshwa na watoto wa mama aliyemnyonyesha mtoto huyo na nduguze. Baba mzazi wa mtoto atawajibika kumlipa mama mnyonyeshaji. Kama baba atafariki, nduguze watawajibika kumuhudumia mama anayemnyonyesha mtoto na mtoto mwenyewe katika kipindi cha miaka miwili cha kunyonyesha.

Unyonyeshaji ulipewa umuhimu mkubwa katika jamii za kale ya Kiislamu. Wakati wa utawala wa Khalifa wa Pili – Omar ibn al-Khattab (karne ya saba), kila mtoto mchanga aliyekuwa akihitaji huduma alilipiwa kiasi cha pesa kusaidia huduma bora katika malezi yake.

Faida za Kunyonyesha kwa Tiba na Kisaikolojia

- Maziwa ya binadamu yanaendana kwa namna ya pekee kwa watoto. Maziwa ya mama yanakuwa na mamia hadi maelfu ya molekyuli ambazo humlinda mtoto dhidi ya maambukizi na husaidia katika kuimarisha kinga za mwili, maendeleo ya ukuaji wa viungo na kuwa na mfumo wa umeng'enyaji chakula wenye afya. Huwa na vitu mbalimbali vyenye kuchochea kukua kwa utumbo, mishipa ya damu, mfumo wa fahamu na mfumo wa homoni. Maziwa ya binadamu hubadilika kimuundo kuanzia hatua ya mwanzo hadi hatua ya mwisho ya unyonyeshaji,na huendelea kubadilika kutegemea chakula na baina ya mama mmoja hadi mwingine (Kliniki ya watoto ya Kaskazini mwa Marekani 2013).
- Makala ya mazingira (2008) imeeleza kuwa;
- "Muundo wa maziwa ya binadamu hubadilika kadri unyonyeshaji unavyoendelea, mabadiliko hayo huendana sambamba na maendeleo ya mtoto. Maziwa ya binadamu huwa na kiasi kikubwa cha protini, wanga, lipidi, asidi ya fati, madini na vitamini ila kiasi kikubwa cha kinga za kupambana na magonjwa hutokana na askari (kinga ya mwili), leukosaiti, homoni, molekyuli yenye amino asidi, protini katika seli ya binadamu, protini za kwenye seli nyeupe na vitu vingine ambavyo ni muhimu katika kuleta ulinzi wa mwili dhidi ya vimelea vya magonjwa katika kipindi cha wiki chache za mwanzo na miezi ya mwanzo katika maisha ya mtoto.
- Al-Bar na Kandil (1986) wametaja faida nyingi za kunyonyesha ikiwemo zifuatazo;
- Maziwa ya mama yanakuwa na virutubisho ambavyo mtoto anahitaji, kwa kiwango sahihi na katika ubora halisi ili kurahisisha mmeng'enyo na utumiaji wa chakula kwa ukuaji wa mwili. Virutubisho vya maziwa hubadilika kila siku kulingana na mahitaji ya mtoto. Watoto wanaowahi kuzaliwa kabla ya muda wa-

nakuwa na kanuni maalumu ya mchanganyiko unaoandaliwa katika maziwa ya mama ili kufanya maziwa hayo kuwa lishe inayomfaa mtoto. Unyonyeshaji husaidia tumbo kuimarika na kupambana na maambukizi/maradhi. Maziwa ya mama hurahisisha zaidi umeng'enyaji katika tumbo la mtoto kuliko mchanganyiko wa maziwa unaoandaliwa kiwandani kwa ajili ya mtoto.

- Maziwa ya mama kwa mtoto huhifadhiwa katika kiwango cha joto kilicho sahihi na hupatikana kadri yanavyohitajika.
- Hakuna chupa zinazohitaji kusafishwa na hakuna mchanganyiko unaoandaliwa kiwandani kwa ajili ya mtoto unaohitajika.
- Uhusiano wa karibu sana kisaikolojia huwepo kati ya mama anayenyonyesha na mtoto wake.
- Unyonyeshaji husaidia mama baada ya kujifungua kupungua uzito.
- Kimiminika cha mwanzo katika hatua za unyonyeshaji husaidia mtoto kutoa haja kubwa kirahisi.
- Maziwa ya ng'ombe au maziwa mengine ambayo hayatokani na binadamu, huhusika sana katika kusababisha aleji.
- Unyonyeshaji hufanya kazi kama vidonge vya kuzuia ujauzito. Mwanamke anayenyonyesha ni nadra sana kupata ujauzito wakati ananyonyesha, hivyo huweza kumpatia kizuizi asilia cha kufanya uzazi wa mpango. Wanawake hawapati ada wakiwa wananyonyesha, kwa hiyo unyonyeshaji huwa kama vidonge vya kuzuia ujauzito. NHS imeeleza, unyonyeshaji huwa siyo njia ya kutegemea kuzuia ujauzito endapo vyakula vingine vinatumika badala ya unyonyeshaji (lazima amnyonyeshe mtoto wakati wote, kwa maana ya kuwa kabla ya kufikisha miezi 6, mtoto anatakiwa anyonye sana maziwa ya mama. Asitumie maziwa ya kiwandani au atumie mara chache sana.
- Maziwa ya mama huwa ni chanzo kizuri cha madini ya zinki yanayopatikana katika mwili wa binadamu.
- Ukilinganisha watoto wanaonyonyeshwa na wasionyonyeshwa, wasionyonyeshwa wanakuwa katika hatari kubwa sana ya kupata magonjwa katika mwaka wa kwanza maishani mwao (Marejeo yaliyofanywa katika jarida la uzazi wa watoto na matibabu kwa watoto, 2009)
- Unyonyeshaji husaidia kuboresha ubongo wa mtoto. Maziwa ya mama huwa na virutubisho muhimu visivyopatikana katika maziwa ya kutengeneza. Watoto walionyonyeshwa kwa kipindi cha mwezi mmoja wanakuwa na uelewa mara nane zaidi kama wanafunzi wa shule ya awali, na uelewa huo huongezeka kadri anavyoendelea kunyonya". (BBC 2002)

- Unyonyeshaji huleta ulinzi wa mwili dhidi ya magonjwa mengi sana. Taarifa iliyochapishwa na taasisi ya serikali kuhusu tafiti za afya na viwango mwaka 2007 ilitazama tafiti mbalimbali na kubaini yafuatayo;
- Kupungua kwa hatari ya kupata saratani ya maziwa na saratani ya uzazi kwa wazazi wanaokuwa wananyonyesha watoto wao
- Kunyonyesha japo kwa miezi mitatu hupunguza hatari ya mtoto kuweza kupata ugonjwa wa sukari unaowapata watoto. Unyonyeshaji kwa watoto pia husaidia kuepusha ugonjwa wa kisukari hapo baade (diabetes type 2).
- Hupunguza hatari ya kupata kisukari kinachoweza kuwapata wazazi wakati wa kujifungua kwa wale ambao hawajawahi kuwa na tatizo hilo wakati wa ujauzito na kwa wale wanaonyonyesha. Na kila mwaka unyonyeshaji unahusiana na kupunguza hatari ya kupata magonjwa ya aina hiyo.
- Unyonyeshaji wa mtoto kwa kipindi cha miezi huhusika katika kupunguza hatari ya mtoto kupata ugonjwa wa saratani ya damu kiujumla, yaani mfumo wa kinga unaohusika na kupambana na seli zinazounda ugonjwa wa saratani kwa asilimia 19 na saratani inayoanzia katika viungo (acute myelogenous leukemia) kwa asilimia 15.
- Pia unyonyeshaji wa mtoto husaidia kupunguza vifo vya ghafla vya watoto kwa asilimia 36.
- Unyonyeshaji wa mtoto husaidia kuepukana na hatari ya kupata magonjwa ya mfumo wa upumuaji (pumu) katika zile familia ambazo hazina historia ya matatizo ya aina hiyo kwa asilimia 27.

Kwa wale wanaotoka katika familia zenye historia ya matatizo ya aina hii, kulikuwa na upungufu wa kupata maradhi hayo kwa asilimia 40 kwa watoto walio chini ya miaka 10.

- Kuna uhusiano wa kunyonyesha na kupungua hatari ya kuwa mzito (kupata uzito uliokithiri) au kuwa mnene zaidi wakati wa ujana na utu uzima.
- Unyonyeshaji wa mtoto hupunguza hatari ya kupata matatizo ya masikio.
- Unyonyeshaji wa mtoto hupunguza hatari ya kupata matatizo ya ugonjwa wa ngozi.
- Watoto wanaonyonyeshwa wanaepukana na hatari ya kupata magonjwa ya tumbo na utumbo (Tafiti iliyofanyika Uingereza ilibaini kuwa asilimia 64 wanaepukana na hatari hiyo).

- Unyonyeshaji hupunguza uwezekano wa kupata maradhi ya mfumo wa upumuaji kwa watoto (ilikuwa ni sawa na asilimia 72 imepunguza uwezekano wa watoto kupelekwa hospitali kutokana na matatizo ya mfumo wa upumuaji kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja ambao walikuwa wakinyonyeshwa kwa kipindi cha miezi minne au zaidi).
- Unyonyeshaji hupunguza hatari ya kupata ugonjwa wa kutoka damu nyingi kwa mama baada ya kujifungua.
- Kuacha kumnyonyesha mtoto mapema au kutonyonyesha kabisa kunahusishwa na matatizo ya kupata msongo wa mawazo baada ya kujifungua.

Maziwa ya mnyama yanawafaa watoto wa mnyama, na viungo vya maziwa hayo vinatofautiana kutoka mnyama mmoja hadi mwingine. Jedwali lifuatalo linaonyesha asilimia za viungo vya maziwa ya mwanadamu, ng'ombe, nyati na mbuzi. Maji huwa ni asilimia 88 na vilivyobaki ni kama ifuatavyo;

MAZIWA	%PROTINI	% FATI	% SUKARI	% MADINI
Mwanadamu	1.5	3.5	6	0.2
Ng'ombe	3	4	4	0.8
Nyati	3	6	4	0.8
Mbuzi	3	4	4	0.8

Idara ya Kilimo ya Marekani, 2010

"Taasisi ya Marekani ya utabibu kwa watoto imependekeza unyonyeshaji wa mtoto uwe kwa kipindi cha miezi 6, na uendelee baada ya hapo kukiwa na vyakula vingine vya kumlisha mtoto vinatolewa, na unyonyeshaji unaweza kuendelea hadi kufikia mwaka mmoja au zaidi kwa matakwa ya mama na mtoto pia.

- Maziwa ya mama yana kinga dhidi ya maambukizi ya bakteria kama vile; uti wa mgongo, maambukizi katika mfumo wa mkojo (UTI) na maumivu ya sikio. Watoto wanaonyonyeshwa kwa kutumia maziwa yanayotengezwa huwa katika hatari ya kupata kisukari, matatizo ya limfu, aleji na maradhi yanayotokana na mfumo wa mmeng'enyo wa chakula.

Kiwango cha Unyonyeshaji nchini Marekani na Uingereza

Kiwango cha unyonyeshaji kimekuwa kinaongezeka nchini Marekani. Katika watoto waliozaliwa mwaka 2012, asilimia 80 ya watoto walianza kunyonya, asilimia 51 waliweza kunyonya walipofikisha miezi 6 (ikiongezeka kutoka asilimia 35 mwaka 2000) na asilimia 29 walikuwa wananyonya kufikia umri wa miezi 12 (ikiongezeka kutoka asilimia 16 mwaka 2000). Kiwango hiki kilikuwa ni kuhusiana na unyonyaji kwa ujumla na siyo kwa unyonyaji wa kutumia ziwa la mama pekee. Unyonyeshaji pekee katika umri wa miezi 6 mwaka 2012 ilikuwa ni asilimia 22, ikiongezeka kutoka asilimia 10 mwaka 2003(CDC). Nchini Uingereza,unyonyeshaji ulikuwa asilimia 81 mwaka 2010 (asilimia 83 nchini Englandi, asilimia 74 nchini Skotlandi, asilimia 64 kaskazini mwa Irelandi na asilimia 71 nchini Wales) ikiongezeka kutoka asilimia 76 mwaka 2005. Hali ya kuwa asilimia 36 ya kina mama walikuwa bado wananyonyesha wakati watoto wakiwa na umri wa miezi 6 mwaka 2006, unyonyeshaji pekee wa watoto kuanzia miezi 6 ilikuwa ni sawa na asilimia 1 (NHS 2012).

Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto nchini Marekani

Moja ya sababu ya kwa nini wanawake hawanyonyeshi watoto wao, inaweza kuwa ni hitaji la kunyonya. Watoto hunyonya hata mara kumi na mbili ndani ya kipindi cha masaa 25, kwa kawaida hutumia dakika 10 hadi 15 kwa kila mara moja wanaponyonya. Kupanga utaratibu wa aina hii wakati wa saa za kazi huwa ni tatizo.

Mwaka 2010, kifungu cha kupatia muda wa kupumzika kilitungwa katika sheria ya kulinda wagonjwa na malezi, ambayo ilihitaji waajiri katika nchi ya Marekani kutoa muda wa kutosha kupumzika kwa mwajiriwa ili kumnyonyesha mtoto wake kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kujifungua mtoto huyo, katika wakati wowote mzazi anapokuwa anahitaji kunyonyesha mtoto wake. Kifungu hiko katika sheria tajwa hapo juu kilimhitaji mwajiri kumpatia mtumishi wake sehemu ya kunyonyesha ya kunyonyeshea (isiyokuwa maliwato), iliyokuwa na stara na isiyokuwa na usumbufu wa watumishi wenzake na watu wengine katika jamii ili iweze kutumika katika kunyonyesha mtoto. Hata hivyo, waajiri hawakuwa wakitakiwa kulipa fidia watumishi wao kwa muda wa kupumzika waliotumia katika kuwanyonyesha watoto wao. Lakini pia, waajiri ambao walikuwa na watumishi

wachache chini ya hamsini hawakuhitajika kutoa mapumziko ya aina hii kwa watumishi wao kunyonyesha kama kufanya hivyo kungeweza kuleta ugumu katika utendaji kazi (Idara ya Kazi Marekani).

Mwaka 1993, tuzo ya UNICEF ilitolewa kwa Kampuni ya Bima ya John Hancock kwa kitendo chake cha kutenga vyumba maalumu kwa ajili ya kunyonyeshea ambavyo vilikuwa na pampu za umeme za kunyonyeshea, viti vizuri pamoja na majokofu. Katika wastani wa mwaka wa wafanyakazi wajawazito 300, kampuni hiyo ilibaini kuwa mpango huo mpya uliweza kuokoa kiasi cha $60,000 tangu kuanzishwa kwake kwa sababu watoto walionyonyeshwa walikuwa na afya na hivyo mama zao waliweza kupata muda mzuri wa kuwajibika ipasavyo kazini. Pia, mpango huu ulifanya kurudi kazini kuwe kwepesi, na kwahiyo, kina mama wengi walipenda kupata muda mchache wa likizo ya uzazi.

Sehemu za Kazi na Unyonyeshaji Watoto nchini Uingereza

Nchini Uingereza, mwanamke anayekusudia kunyonyesha mtoto eneo la kazi anatakiwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mwajiri wake kuwa ananyonyesha. Inashauriwa ifanyike hivyo kabla ya kurejea kazini. Waajiri nchini Uingereza wanatakiwa kwa mujibu wa sheria kuwapatia eneo maalumu watumishi ambao ni wajawazito na wale wanaonyonyesha ili waweze kupumzika pamoja na sehemu ya kulala kama ikiwezekana. Hata hivyo, hakuna hitajio la kisheria kwa mwajiri kumpatia sehemu ya kuhifadhi maziwa mwanamke anayenyonyesha.

Pia hakuna hitajio la kumtaka mwajiri kulipa muda wa mapumziko ili mwanamke aweze kunyonyesha. Maliwato au sehemu za kupumzikia wagonjwa hazifai kwa wanawake wanaonyonyesha kwa sababu za usafi na afya. Waajiri wana jukumu la kupokea na kukubali maombi ya kuwapatia muda uliokuwa tulivu watumishi kwa namna inayofaa na kuwapatia usalama wa afya zao, ulinzi dhidi ya uzalilishaji na ulinzi dhidi ya ubaguzi wa kijinsia.

Maziwa ya Kiwandani, Ukuaji duni na Maradhi

UNICEF (Shirika la watoto duniani) na WHO (Shirika la Chakula) huchukulia mashirika yanayoandaa vyakula vya watoto kama visababishi vya vifo vya watoto na hivyo hushauri serikali kuzuia matangazo ya vyakula vya watoto vinavyotengenezwa. Kwa mfano, UNICEF imekadiria kuwa watoto wanaotumia vyakula hivi, wanaopata maradhi ni mara 6 hadi 25 hufariki kwa kuhara na mara nne zaidi hufariki kwa maradhi ya nimonia, zaidi ya wale wanaokuwa wanatumia maziwa ya mama zao. Watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya viwandani kwa kutumia chupa, mara nyingi hupata lishe isiyokuwa nzuri na iliyokuwa na virutubisho duni na kiasi kikubwa cha vijidudu kwa sababu ya utumiaji wa maji ambayo siyo safi na salama yanayotumika katika utengenezaji wa maziwa hayo. Maji machafu, ukosefu wa mifumo ya kutosha ya maji safi, ukosefu wa kupatikana kwa jokofu na ukosefu wa kuelewa vizuri maelezo ya kuchanganya maziwa huchangia kuleta madhara yatokanayo na utumiaji wa maziwa ya aina hii. Wakati mwingine wazazi huyazimua sana maziwa hayo kwa lengo ya kufanya yakae

sana bila kuisha. Unyonyeshaji wa maziwa ya mama huchangia kumlinda mtoto dhidi ya maradhi. Maziwa ya mama siyo tu kuwa ni chakula kizuri chenye virutubisho unavyoweza kumpatia mtoto, bali pia hupatikana bure.

Lishe duni huchangia vifo takribani vya watoto milioni 3 kila mwaka (ikiwa ni sawa na asilimia 45) kwa ujumla (Lancet 2013). Zaidi ya 2/3 ya vifo hivi hutokea miezi ya mwanzoni katika maisha ya watoto, na mara nyingi huhusiana na ulishaji duni kama vile utumiaji wa chupa kulishia au kutolisha kwa muda sahihi na kumpatia chakula cha ziada (WHO 2010). Lishe duni wakati wa ujauzito hupelekea kuwa na lishe duni pia utotoni (mtoto anapozaliwa). Athari zake huathiri ukuaji wa mwili na watoto waliokuwa na maendeleo duni ya ukuaji, wanakuwa katika hatari kubwa ya kuwa na uzito mkubwa sana na kupata maradhi kama vile kisukari katika maisha yao hapo baadaye. Mkakati wa kupambana na njaa duniani umetoa taarifa kuwa kila mtoto mmoja katika watoto sita sawa na watoto milioni moja katika nchi zinazoendelea wamekuwa na tatizo la uzito kupitiliza na mtoto mmoja katika watoto wanne duniani atakuwa amedumaa. Unyonyeshaji sahihi kwa watoto chini ya miaka miwili ni muhimu katika maisha ya watoto kuweza kupambana na maradhi, na uwezo wa kupunguza zaidi ya vifo 800,000 (asilimia 13 ya vifo vyote) kwa watoto chini ya miaka mitano katika nchi zinazoendelea (ripoti ya Lancet iliyonukuliwa na UNICEF). Taasisi ya mpango wa okoa watoto inakadiria kuwa asilimia 22 ya vifo vya watoto wachanga vinaweza kuzuilika kama unyonyeshaji wa maziwa ya mama unaweza kuanza ndani ya saa moja baada ya mtoto kuzaliwa, na asilimia 16 kama unyonyeshaji ulianza ndani ya masaa 24.UNICEF wameeleza kuwa “watoto walionyonyeshwa wana nafasi kubwa mara sita ya kuishi katika miezi ya mwanzo zaidi ya watoto wasionyonyeshwa. Mtoto aliyenyonyeshwa anakuwa na nafasi ndogo ya kufariki mara 14 zaidi ya

wale wasionyonyeshwa na unyonyeshaji hupunguza maradhi ya mfumo wa upumuaji na kuhara, sababu kuu mbili za kuua mtoto (Lancet 2008)". Hata hivyo,kwa mujibu wa UNICEF, asilimia 39 tu ya watoto waliokuwa chini ya miezi 6 katika nchi zinazoendelea ndiyo huwa wananyonyeshwa na asilimia 58 ya watoto wenye umri wa miezi 20 hadi 23 wananufaika na unyonyeshaji endelevu.

Wakati kukiwa na maendeleo mazuri duniani ya kupunguza vifo vya watoto, kiasi kikubwa cha vifo ni cha watoto wachanga wanaozaliwa. Wakati baadhi ya nchi zimeboresha kiwango cha unyonyeshaji, kama vile Sri Lanka, Cambodia na Ghana, 2/3 ya watoto milioni 92 ambao wananyonyeshwa tu wanaishi katika nchi kumi, katika hizo saba zikiwa hazijafanya maboresho ya kunyonyesha tu: India, China, Nigeria, Indonesia, Philippines, Ethiopia na Vietnam (Taasisi ya Okoa watoto 2013).

Mazao ya maziwa ya watoto yanaunda sehemu kubwa ya soko la chakula cha watoto, kwa asilimia 40. Eneo kubwa linalokuwa kwa kasi zaidi ni soko la Asia, ambalo ndiyo kubwa zaidi (Asilimia 53; Ushauri wa UBIC 2014). Soko la maziwa ya viwandani ulimwenguni kote lina thamani ya mabilioni na linakuwa zaidi. Ongezeko la kukua kwa mauzo ya asilimia 10 hadi 20 hutokea kwa mwaka katika nchi nyingi za kipato cha chini na kati wakati hali kama hii ikiwa haijawahi kutokea katika nchi zenye kipato kikubwa. Katika Asia mashariki na Pasifiki, idadi ya mama wanaonyonyesha imepungua kutoka asilimia 45 mwaka 2006 hadi kufikia asilimia 29 mwaka 2012 (Okoa watoto 2013). Baadhi ya mashirika yanayofanya maziwa ya viwandani kuwa mbadala, wanatumia mbinu za biashara sokoni kuwafanya mama wanaonyonyesha wafikirie kuwa maziwa ya kiwandani ni bora na wanaweza kuwalisha watoto wao, hata kama hawana uwezo huo.

Maoni ya Imamu Ali na Ibn Hazm Kuhusu Unyonyeshaji

Unyonyeshaji wa maziwa ya mama unachukuliwa kama haki ya mtoto kutoka kwa mama yake. Kina mama wanahamasishwa kuwanyonyesha watoto wao. Ibn Hazm alisema:

> "Mama anapaswa kumnyonyesha mtoto wake hata kama ni binti wa mfalme. Haachwi katika jukumu hili labda tu awe hana uwezo wa kufanya hivyo."
> (Ibn Hazm, Juz. 10).

Kama mafundisho ya Uislamu yakifuatwa, matatizo mengi yanayowakumba watoto na mama zao yataweza kuepukwa. Ali ibn Abi Talib alisema:

> "Hakuna maziwa yanayonyonywa na mtoto yaliyo na baraka tele zaidi ya maziwa ya mama."

Muda wa Unyonyeshaji

Pamoja na wanasheria kutofautiana, lakini wanakubaliana kwa pamoja kuwa unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mtoto hauzidi muda wa miaka miwili. Ikiwa mama ana afya njema na maziwa yake yanapatikana vizuri, inashauriwa amwachishe mtoto kunyonya baada ya muda wa miaka miwili. Yusuf Ali anatoa maoni yake katika Qur'an 46:15 kwamba:

Muda wa mwisho wa kumnyonyesha mtoto (miaka miwili) huendana na kukamilika kwa uotaji wa meno ya awali ya mtoto. Meno ya chini (kati) huota katika kipindi cha mwezi wa 6 hadi wa 9 na kisha meno mengine hufuatana kwa kupishana muda hadi meno ya kuraruria yanapotokea . Magego ya mwanzo huota katika kipindi cha miezi 24 na hadi hapo meno ya awali ya mtoto hukamilika. Asili inamtarajia mtoto huyu kuwa na uwezo wa kutafuna chakula na hivyo kujitegemea kabisa kutokana na maziwa ya mama. Kwa upande mwingine, mama huumizwa na mtoto anyonyapo katika wakati huu kwa kuwa mtoto ana meno ya awali yaliyokamilika. Meno ya kudumu huanza kuota kuanzia mwaka wa 6, na magego ya pili huchomoza baada ya miaka 12. Magego ya tatu ni meno ya busara, kwani haya huweza kutokea kuanzia umri wa miaka 18 hadi 20 au hata kutotokea kabisa katika muda huo.

Wengine wametoa maoni yao kwamba kunyonyesha zaidi ya muda wa miaka miwili kunaweza kukamletea mtoto athari za kimwili, kiakili na hata kisaikolojia. Katika mwaka 1997, Shule ya Kimarekani ya Watoto (AAP), ilipendekeza kina mama wawanyonyeshe watoto wao angalau kati ya mwezi wa 6 na mwezi wa 12. Baadaye AAP iliongeza muda na kupendekeza kina mama wanyonyeshe japo kwa mwaka mmoja na zaidi. Shule hii iliainisha faida za kunyonyesha kama; kupunguza uwezekano wa kupata saratani ya kizazi, saratani ya matiti na maradhi ya mifupa.

Mtume (S.A.W.) alizungumzia unyonyeshaji wa maziwa ya mama na mama mwingine. Alisema, ikiwezekana, mama mzazi wa mtoto anapaswa kumyonyesha mtoto wake, ila ikiwa kuna sababu za kiafya zinazomzuia, ambapo mama mwingine anaweza kutafutwa kwa ajili ya kumnyonyesha mtoto huyo. Anasema:

> "Kuweni makini na mtu atakayekuwa ndugu yenu kwa kunyonya! Mtumie mama mwingine kunyonyesha mtoto kwa kukidhi mahitaji ya njaa ya mtoto." (AL-BUKHARI).

Faida mojawapo ya kutangaza ndoa ni kuhakikisha kwamba mwanamke haolewi na kaka yake kupitia kunyonya maziwa ya mama mmoja kimakosa. Hii inatoa fursa kwa Umma kutoa ushahidi wao ikiwa kuna uhusiano wa namna hiyo.

Dondoo Muhimu kwa Akina Mama Wanyonyeshao

(Kutoka kwa: El-Amin, 1998)

Ingawa unyonyeshaji ni njia ya asili, ni ujuzi unaoweza kuboreshwa. Zifuatazo ni baadhi ya dondoo kwa kina mama:

- Jiandae kabla ya kuzaliwa kwa mtoto. Soma vitabu mbalimbali kuhusu unyo-

nyeshaji. Chukua mafunzo kutoka hospitali, mhudumu wa afya au mtaalamu wa unyonyeshaji. Hudhuria mikutano ya taasisi zinazojihusisha na uhamasishaji juu ya unyonyeshaji.

- Namna nzuri ya kumpakata mtoto kwa ajili ya unyonyeshaji ni muhimu. Hakikisha chuchu imeingia kwa inchi 1 au inchi 1.5 kwenye mdomo wa mtoto. Usiiname kumuelekea mtoto; mvute mtoto kwako. Ni vema ukatumia mto.
- Muache mtoto anyonye titi moja mpaka lilainike na mjongeo wa kunyonya wa mtoto unapopungua kutoka katika kasi kwenda hadi taratibu sana. Kisha mpatie titi lingine. Inafaa kulilainisha titi moja kwa kunyonyesha kuliko kumhamisha mtoto mara moja katika matiti yote. Sehemu ya kwanza ni maziwa yanayofanana na maziwa yasiyochujwa, sehemu ya kati ni kama maziwa halisi na sehemu ya mwisho huwa laini, kama yaliyochujwa. Ulaini huu hutoa uwiano mfuatano wa vipindi vya unyonyeshaji na pia huondoa tabia ya mtoto ya kulia kupitiliza.
- Kunaweza kutokea kuongezeka kwa haraka kwa matiti katika siku chache za mwanzo , tukio hili ni la kawaida. Ikiwa mtoto atashindwa kunyonya katika chuchu zilizoongezeka ukubwa, kamua kiasi kidogo cha maziwa kabla ya kunyonyesha mtoto.
- Sawazisha chuchu zilizovimba kwa utaratibu maalumu. Punguza maumivu kwa kuziacha chuchu zikauke, kisha upake mafuta ya mzeituni au lanolini.
- Kunywa maji mengi. Chai /uji wa pilipili manga na kitunguu saumu vinaelezwa kuongeza uzalishaji wa maziwa.
- Ni muhimu mama aanze kumyonyesha

mtoto baada ya saa moja au saa mbili baada ya kujifungua pindi mtoto akishapata fahamu.

- Mara ngapi inatosha? Katika kipindi cha majuma mawili au matatu, utalazimika kumuamsha mtoto kwa ajili ya kunyonya. Kwa kawaida mtoto hunyonya kila baada ya saa tatu au zaidi wakati wa mchana na kila baada ya saa nne wakati wa usiku. Unyonyeshaji wa mara kwa mara ni muhimu sana kwa mtoto na kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa. Mtoto anapozidi kunyonya, uzalishaji wa maziwa huongezeka. Mtoto anapoongezeka uzito vizuri, hamu ya kunyonya mara nyingi huongezeka.
- Kunyonyesha mtoto maziwa ya mama kwa chupa: Usimpe mwanao maziwa yako kupitia kwenye chupa mpaka uhakikishe unyonyeshaji hauna matatizo na unaendelea vema, kwa kawaida kati ya Majuma 3 hadi 5. Mara nyingi inasaidia ikiwa mtu mwingine atampa mtoto maziwa badala ya mama mzazi ikiwa mama mzazi hayupo. Kwa picha ndogo tu, watoto wengi wanaweza kunyonya matiti ya mama zao na kunyonya kupitia chupa maalumu.

- Watoto wengine ni wazuri katika kunyonya tangu mwanzo lakini wengine huchukua muda mrefu kidogo kujifunza. Hili si tatizo, lisikusumbue.
- Usikate tamaa katika kunyonyesha. Mama mmoja alisema, ilimchukua majuma sita mpaka kufikia unyonyeshaji wa kawaida na kufuatiwa na unyonyeshaji wenye furaha na uhusiano mzuri.
- Chuchu za mama zinaweza kuvimba na kuwa na maumivu katika juma la kwanza. Kamua matiti kidogo kabla na baada ya kunyonyesha na kisha pangusia maziwa katika chuchu na uache yakaukie hapo.

Kina mama hufurahia kunyonyesha. Hakuna maandalizi ya chakula yanayohitajika, hisia maalumu za kuwa karibu na watoto huongezeka na imethibitika kuwa mara chache sana watoto wanaonyonyeshwa mara kwa mara hupata homa na matatizo ya kusikia. Kabla ya kujifungua, akina mama wanapaswa kuainisha orodha ya mahitaji na namna ya kuyapata ili watakapopata ugumu waweze kupata wepesi wa kuwasiliana kwa msaada wa haraka.

Mlo unaopendekezwa kwa Mama anayenyonyesha

Ufuatao ni mfano wa mlo unaopendekezwa kwa akina mama:

- Vyakula vitatu vya protini kama kuku na samaki.
- Vyakula viwili vyenye vitamini C kama machungwa
- Vyakula vitano vyenye kalishium kama maziwa na jibini.
- Vyakula sita vya aina ya matunda na mbogamboga kama vile nazi na boga.
- Vyakula sita vyenye mchanganyiko wa kabohaidreti kama mkate.
- Chakula kimoja chenye madini ya chuma kama nyama ya ng'ombe na maziwa.
- Kiasi kidogo cha chakula chenye mafuta (fati) mengi kama jibini na maziwa.
- Bilauri nane za maji.
- Vitamini kwa ajili ya ujauzito au mwanamke anyonyeshaye.

Virutubisha bora humsaidia mama kuwa na maziwa ya kutosha kwa ajili ya mtoto, kumpa mama nguvu na kumrudisha katika hali kabla ya ujauzito. Ni muhimu pia kunywa maziwa mengi vinginevyo anaweza kupungukiwa kalisi hapo baadaye.

Mama mmoja alisema, "Kunyonyesha kunafurahisha sana. Hata usiku wa manane, nikiutazama uso wa mwanangu na kugundua kuwa mwanangu ananihitaji mimi, inawezekanaje nisimnyonyeshe? Faida za kihisia za kunyonyesha ni kubwa zaidi kwangu kuliko kwa mtoto."

Taifa imara: Kimwili

Qur'an na hadithi za Mtume (S.A.W.) zinaeleza jambo hili katika namna zote:

…Nyinyi mmekuwa bora ya Umma waliotolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingelikuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu.

(Qur'an 3:110)

…Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, na wengineo ambao hamuwajui, lakini Mwenyezi Mungu anawajua. Na mkitoa chochote katika Njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumiwa.

(Qur'an 8:60).

Mtume (S.A.W.) alisema: Muumini aliye imara ni bora na anapendwa sana na Allah kuliko muumini dhaifu. Kuna uzuri kwa Waislamu wote. Kumbuka, neno '*qawiy*' katika Hadithi linamaanisha uimara wa imani na mwili. Ufafanuzi wa maneno kama "jamii bora", "andaa uimara na nguvu zote uwezavyo", huhusisha maana ya kimwili pamoja na kiimani na kimaadili. Kutokana na sura zilizopita, mahitimisho yafuatayo yanaweza kufikiwa:

Jamii inaweza kuwa imara zaidi kimwili kupita mataifa mengine kwa kufuata mambo yafuatayo;

- Kuchagua wachumba wenye afya bora.
- Kujiepusha na zinaa, hii inasaidia wazazi na watoto wao kuepukana na maambukizi yanayotokana na vitendo vya zinaa kama vile VVU/UKIMWI na maradhi mengine.
- Kula vizuri. Wazazi, akina mama wajawazito na watoto wanashauriwa kula *azka taaman* kikiitwa pia *altayyibat*, ambacho ni chakula kizuri, chenye virutubisho vingi na chakula halisi. Nyama ya nguruwe, damu, mzoga na wanyama walionyongwa hairuhusiwi kutumika kabisa.

Qur'an inasisitiza matumizi ya maji, maziwa na asali; matunda kama tende, zabibu, zaituni na tini; nyama kama kuku, vyakula kutoka baharini, nyama ya ng'ombe na nyama ya kondoo; pamoja na mbogamboga kama; vitunguu maji, bamia, nafaka, maharagwe na vitunguu saumu.

- Qur'an inasisitiza matumizi ya maji, maziwa na asali; matunda kama tende, zabibu, zaituni na tini; nyama kama kuku, vyakula kutoka baharini, nyama ya ng'ombe na nyama ya kondoo; pamoja na mbogamboga kama; vitunguu maji, bamia, nafaka, maharagwe na vitunguu saumu.
- Kuzingatia usafi. Vimelea vya maradhi huondolewa kwa kuosha mikono tu kabla na baada ya kila mlo. Tumia mkono wa kushoto kwa kuogea msalani na mkono wa kulia kwa kula. Chukua udhu mara tano kila siku.
- Epuka vyakula vyenye kuleta sumu kama; pombe, dawa za kulevya na uvutaji wa bangi na sigara. Maendeleo ya mtoto akiwa tumboni mwa mama yake huwa bora ikiwa mama ataepuka vitu kama hivyo vilivyotajwa.
- Watoto wanaonyonya. Watoto hukua na kuwa na siha njema kimwili na kisaikolojia kunakowawezesha kuwa watu imara na viongozi waadilifu hapo baadaye.

Likizo ya uzazi inapaswa kurefushwa zaidi majuma nane au saba. Likizo inayorefushwa hadi mwaka mmoja itawasaidia kina mama kuwajibika kikamilifu katika kuwatunza watoto wao, yaani kuwaanda viongozi wa baadaye kama alivyofanya mama yake Nabii Musa.

Kwa kuhitimisha, miaka mitano ya mwanzo ni muhimu kwa kujenga siha na tabia njema. Muda huu unaunda dirisha la fursa ambayo haipaswi kupotezwa. Mwongozo huo hapo juu, utaiongoza jamii kuwa watu bora miongoni mwa wanadamu.

Kwa kukuza watoto wenye siha bora, tunaweza kuwafundisha imani, busara, uelewa na ujuzi. Hivi vyote hufuata baadaye katika maisha, kama ilivyoelezwa kwa Mitume kama Yussuf, Musa na wengineo.

Na Musa alipofika utu-uzima barabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyowalipa walio wema. (Qur'an 28:14).

- Unyonyeshaji wa maziwa ya mama una misingi imara kwa kutengeneza mataifa imara kwa sababu zifuatazo:
- Unawapa watoto uimara wa kimwili, kisaikolojia na nguvu za kihisia.
- Umefanywa kuwa na mguso wa moja kwa moja kuliko chakula kinachotengenezwa viwandani.
- Ni njia bora zaidi ya kiasili ya kuwanyonyesha watoto.

Wakati uelewa wa mwanadamu unaendelea kukua na kubadilika, vitabu vitukufu vinasisitiza mambo muhimu ya kufuatwa kwa faida ya wanadamu.

Hakika hii Qur'ani inaongoza kwenye njia iliyonyooka kabisa, na inawabashiria waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa. (Qur'an 17:9).

Sasa hivi waislamu wanakiuka mafundisho ya Mtume katika kuishi maisha yenye afya. Hakuna hata nchi moja ya Kiislamu iliyo katika orodha ya nchi 12 zenye kiwango cha juu cha wastani wa maisha ya mwananchi wake duniani. Afghanistani inatajwa kushika mkia kwenye orodha hiyo duniani ikiwa na wastani wa miaka 43 kwa wanaume na 44 kwa wanawake.

(Umoja wa Mataifa, 2010).

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 39: INANIUDHI…

Wazazi na watoto lazima wajadili vipengele hivi na kukubaliana juu ya namna ya kuzuia kuvifanya.

INANIUDHI WAKATI:

- Pizza, baqlava na keki inapokatwa vibaya.
- Watoto wanapoacha takataka zao na kuwaachia wazazi wao wazitoe.
- Takataka inapotupwa karibu na kikapu cha takataka na si ndani ya takataka.
- Watu wanachelewa kufika katika ahadi zao.
- Mume anarudi nyumbani akiwa amechelewa bila kutoa taarifa kwa mkewe.
- Watu wanasahau kufunga kamba za viatu vyao bila kukumbushwa.
- Watu wanatoka katika nyumba zao bila kunawa mikono yao.
- Watu hawafungi milango ya vyoo wanapoingia kujisaidia.
- Watu wanaacha vikombe vya chai, kahawa au maji katika meza zao usiku mzima bila kumwaga.
- Watu hawatani nywele zao pamoja na ndevu zao.
- Watu wanaacha sindano, vibanio na pini zikizagaa mezani na sakafuni.
- Wazazi hutabasamu pale mtoto anapofanya utovu wa nidhamu nyumbani kwa rafiki yako
- Watu wanasengenya (Qur'an inaeleza kitendo hicho sawasawa na kula nyama ya binadamu).

- Mtoto anaulizwa swali na mzazi anajibu swali hilo kwa niaba ya mtoto.
- Watu huyakatiza mazungumzo ya watoto.
- Mwenyeji anamlazimisha mgeni kula sana chakula.
- Watu wanatoa maoni yanayoonesha ubaguzi wa rangi na kufanya masihara.
- Watu wanaacha chakula kingi na kukitupa.
- Wageni wanakuja bila taarifa.
- Wageni wanaingilia na kuwaadhibu watoto wa mwenyeji wao bila ruhusa.
- Wazazi wanavunja ahadi walizoziweka kwa watoto wao bila kuomba radhi.
- Watu wanaomba ushauri bila kusimulia matatizo yao.
- Vijana wanatumia lifti kuliko ngazi kupanda ghorofani
- Mjumbe hafikishi taarifa kwako kama ilivyo.
- Wageni wanatumia muda mwingi kukaa na mgonjwa.
- Mtu anakerwa sana na wewe bila kukueleza sababu.
- Watu wanatumia vibaya pesa, chakula, karatasi, dawa, nepi na sabuni.
- Madereva wanatuma na kusoma ujumbe wakati wakiendesha (maeneo mengine ni kosa kutumia simu wakati ukiendesha).
- Watu wanakohoa na kupigwa chafya, bila kuziba midomo yao na pua zao.
- Watu hawaondoi milio ya simu zao katika vikao, ibada na maktaba.
- Nguo na viatu vya watu vinanuka.
- Watu wanachafua vyoo bila kusafisha.
- Watu zaidi ya mmoja wanazungumza wakati mmoja.
- Madereva wanapiga honi hovyo.
- Wasemaji wanarudiarudia maneno.
- Mtu anapaza sauti katika mazungumzo, kuwabughudhi wengine wakati mtu mwingine anazungumza taratibu kwa ajili ya wasikilizaji kumwelewa.
- Watu wanaacha taa zikiwaka bila sababu maalumu.
- Mtu fulani anapenya kwenye foleni bila ruhusa.
- Wageni hawafuati mwongozo wa wenyeji wao.

- Mwenyeji anachelewa kutoa chakula kumsubiri mgeni aliyechelewa.
- Watu wanachafua maji ya bomba kama wachafuavyo mikono yao.
- Watu hawatumii vitambaa wakitaka kutema mate.
- Watu hawazoi takataka kutoka katika njia zao.
- Watu wanaziba sebule njia wakizungumza.
- Watu wawili wananong'onezana ndani ya kikao.
- Mtu anafanya kosa na hataki kuomba radhi.
- Watu wanakualika bila kukueleza kuwa kutakuwa na chakula au la.
- Unatoa karatasi za kujifuta nyingi badala ya moja uliyoikusudia.
- Wazungumzaji wanatumia muda mwingi au muda mchache zaidi kuliko uliopangwa.
- Watu wananuniana badala ya kutabasamu
- Unamsalimia mtu haitikii.
- Watu wanakifanya chumba kuwa na kiza sana au mwanga mwingi.
- Watu wanawasumbua wengine kwa kuwapigia kelele, kuwapeleleza na kuwaombaomba.

Kila mjumbe wa familia anaweza kuongeza katika orodha hii mambo yanayoudhi.

SURA YA KUMI NA MOJA

UBONGO WA MTOTO

Kuutumia au
Kutoutumia Ipasavyo

SURA YA KUMI NA MOJA 258

UBONGO WA MTOTO:Kuutumia au Kutoutumia Ipasavyo 258

Utangulizi 260
Wigo wa Fursa mbalimbali 260
Uwezo wa Ubongo kuhifadhi vitu 261
Ukuaji wa Neva na mfumo mzima wa Ubongo 262
Msongo wa Mawazo Unaweza Kuunda Hisia 267
Mfumo wa Utembeaji (Ujongeaji) 268
Msamiati na uwezo wa Kukumbuka Utotoni 269
Jinsi Ubongo Unavyobadilika 269
Wazazi wanatakiwa Wazungumze Vizuri na Watoto Wao 269
Kuanza kwa Masomo ya Awali nchini Marekani 271
Wazazi Wanaweza Kufanya Kitu Gani? 272
Uislamu, Uimbaji na Muziki 273
Avicenna akizungumzia kunyonyesha,na Muziki 275
Picha na Michoro katika Uislamu 276
Kukua kwa Ubongo wa Mtoto Mdogo 277
Je Mafanikio ya mtu huamuliwa kabla ya Umri wa Miaka Mitano? 280
Kazi za kufanya

“Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.”.
(Qur’an 16:78)

Utangulizi

Kitabu kitukufu cha Qur’an kinaeleza kuwa watoto huzaliwa kutoka tumboni mwa mama zao hali ya kuwa hawana elimu wala ujuzi wa kitu chochote. Mungu ndiye mwenye kuwapa ufahamu wa mambo mbalimbali kwa kupitia milango ya fahamu, yaani usikivu kwa kutumia masikio, kuona kwa kutumia macho pamoja na uwezo wa kupambanua kuhisi na kutambua. Elimu ya viumbe hai inaeleza kuwa mfumo wa usikivu upo katika sehemu ya mbele ya ubongo wa binadamu na mfumo wa uonaji upo nyuma ya ubongo wa binadamu. Katikati ya mifumo hii miwili ndipo unapopatikana mfumo mzima wa ubongo wa binadamu. Mifumo hii mitatu kwa ujumla humuwezesha binadamu kutambua na kufanya maamuzi sahihi na stahiki kwa kila jambo linalomkabili.

Ni jambo la kuvutia sana kuona Qur’an ikirudia mara kwa mara kuitaja mifumo hii yote mitatu kwa kufuatana; yaani mfumo unaomrahisishia binadamu kusikia, kuona, pamoja na mfumo wa kuhisi na kutambua.

Tunahitaji kutambua ni jinsi gani ubongo wa mtoto umeumbwa na vipi unaweza kukua. Hivyo ni muhimu kuangalia mazingira ambayo mtoto amepitia na namna gani mazingira hayo yamechangia kuujenga ubongo wake katika uwezo wa kujenga hoja, kufanya hesabu, kujihusisha na muziki, lugha pamoja na kuhisi na kutambua vitu. Tutakapotambua haya, pia itatusaidia kutambua umuhimu wa kumnyonyesha mtoto miaka miwili baada ya kuzaliwa.

Wigo wa fursa mbalimbali

Ili tuweze kufahamu zaidi kuhusu watoto, inatupasa tuelewe elimu ya viumbe kuhusu watoto. Saketi za ubongo hukua na kukomaa katika nyakati tofauti ingawaje

mara nyingi ukuaji wake huanzia wakati wa utotoni. Kwa maana hiyo, saketi za ubongo zina athari kubwa sana katika maisha ya binadamu hususani watoto katika nyakati tofauti za ukuaji wao. Hamasisha watoto katika mambo mbalimbali ya kimaisha katika mazingira ambayo yanahitaji kuhamasishwa, hivyo kunaweza kuleta mafanikio na kama mzazi atashindwa kufanya hivyo watoto hawatoweza kuhamasika na kupata mafanikio (Begley 1996).

Ingawaje ubongo wa binadamu una uzito wa gramu1360, una muunganiko wa seli zaidi ya trilioni na una uwezo mkubwa sana wa kufanya kazi katika kupambanua mambo. Kama hata tukilinganisha mfumo huu na ule wa miji mikuu maarufu duniani ambayo inakutanishwa na barabara moja kubwa na kukawa na barabara nyingine ambazo zimekutanisha miji mikuu tofauti tofauti duniani pamoja na vijiji, bado haitatosha kulinganisha na mfumo huu wa ubongo. Hata kama pia tutaongeza kufananisha na barabara zinazotoka kijiji kimoja hadi kingine duniani hapa pamoja na ukubwa wote wa ardhi tuliokuwa nayo katika ulimwengu wetu pia haiwezi kulingana na ukubwa wa mfumo huu wa ubongo.

Tatizo lililopo katika hatua za ukuaji wa ubongo ni kwamba, kama itashindikana kuandaa mazingira mazuri ya ubongo kukua wakati mwanadamu akiwa angali mtoto wa umri wa mwaka mmoja, basi itakuwa ngumu kuweza kuujenga ubongo wa binadamu huyu atakapokuwa mtu mzima. Khalas (kwisha kabisa)! Hili ndilo tatizo ambalo linakabili wazazi na ndio nafasi pekee ambayo hupotea milele na linakuwa ni janga, huwa ni vigumu kubadilisha ubongo wa mtu ambaye ashakuwa mtu mzima.

Kwa hiyo ni muhimu kujifunza mfumo wa ukuaji wa ubongo na kuweza kujua jinsi gani tunaweza kuandaa mazingira mazuri ya kuwaendeleza watoto kiakili.

Uwezo wa ubongo kuhifadhi vitu

Ni kiasi gani mtoto wa miaka 3 anaweza kuhifadhi vitu katika ubongo wake?

Tukichukulia ubongo kama **Kompyuta,** mazingira anayoishi mtoto yanaweza kuwa sawa na **kinanda chake cha kuandikia kwa vidole. Kompyuta** hii kwa kawaida huwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi vitu kwa kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo inaweza kuhifadhi vitu vingi kuliko hata binadamu wanavyoweza kuhifadhi. Hata hivyo, baada ya miaka 3 au 4, uwezo wake hupungua. **Kompyuta** itaendelea kupokea taarifa lakini uwezo wake hauwezi kuwa sawa kama ilivyokuwa hapo awali. Kwa binadamu pia kama kompyuta, uwezo wake hupungua kadri anavyokuwa mkubwa na seli hai za ubongo huishiwa uwezo wa kufanya kazi na hatimaye hufa kidogo kidogo. Hivyo inatulazimu kutumia vizuri ubongo au akili kabla hatujapita umri wa miaka 3.

(Kotulak 1993).



Rycus na Huges 1998

Kwa kusisitiza, Qur'an inaeleza kuwa wakati binadamu anazaliwa huwa hana ujuzi au utambuzi wa kitu chochote.

> "Na Mwenyezi Mungu amekutoeni tumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.)". (Qur'an 16:78)

Ukuaji wa neva na mfumo mzima wa ubongo

"Ubongo umepitiwa na neva seli zaidi ya bilioni. Baadhi ya neva seli hizi hufanya kazi ya kudhibiti mfumo wa upumuaji, mapigo ya moyo, joto la mwili au matendo yote ya hiari na yasiyo ya hiari. Wakati wa kuzaliwa, neva seli hizi ambazo ni zaidi ya trilioni huwa bado hazijaanza kutumika, zinakuwa kama kibanzi cha pentiamu (kipande kidogo) kinachohifadhiwa katika **Kompyuta** kabla ya kuanza kufanya kazi kutoka kiwandani ilipotengenezwa (factory pre-loads the software).

Neva seli hizi zilizopitia katika ubongo, zinakuwa sehemu ya ubongo katika mfumo wa ufanyaji kazi wa ubongo endapo

zitaweza kutumiwa mapema na kinyume chake ni kwamba endapo hazitumiki zinaweza kufa na kutoweka. Mazingira ya mtoto aliyekulia ndio hutumika kuamuru neva seli gani zitumike na zipi zisitumike

katika mifumo mbalimbali ya mwili wake pamoja na mfumo wa saketi za ubongo kama ilivyo katika mpangilio wa kinanda cha Kompyuta inavyofanya kazi katika Kompyuta. Kibao kipi cha kinanda kimepigwa na mazingira gani mtoto yamemzunguka husaidia sana kumjenga mtoto kiumbile na kiakili kama vile kuwa na akili za kutosha kujifunza haraka au kinyume chake, kuwa muoga, kujiamini sana, kuwa mzungumzaji ama kuwa mkimya. Mazingira yana mchango mkubwa sana ya kumjenga binadamu na kumuweka katika hali fulani." (Nash 1997)

Binadamu anapofikia hatua ya utu uzima, ubongo wake unakuwa na neva seli zaidi ya bilioni 100, zikiwa zinaongezeka neva seli nyingine zaidi ya elfu na kusababisha ubongo kuwa na muunganiko wa neva katika mfumo wake zaidi ya trilioni 100. Muunganiko huu ambao huwa una neva seli nyingi na mkubwa kuliko hata mkusanyiko wa nyota angani, husaidia ubongo uweze kufanya kazi kwa uwezo wa hali ya juu.

Katika kuelezea vizuri mfumo, inaelezwa kuwa mfumo huanza kujijenga katika hatua ya awali kabisa tangu pale yai au mbegu za uzazi zinaporutubishwa katika tumbo la mama kabla mtoto hakuzaliwa kwa kutumia jeni (genes) au sehemu ya DNA inayorithisha tabia na umbile (kinasaba), kama ilivyokuwa katika mfumo wa uwekaji umeme katika nyumba hauwezi kukamilika isipokuwa kwa kuanza na hatua za awali kwa kuweka utaratibu wa kupitisha nyaya za kusambaza moto. Kwa kuwa nusu ya vinasaba hivi husaidia utendaji kazi wa mfumo wa fahamu wa kati, hivyo vinasaba vilivyosalia havina uwezo wa moja kwa moja kuandaa mfumo wa ubongo wenye uwezo wa kufanya kazi katika hali yake ya kawaida. Hivyo, kuna uwezekano kukawa na kitu kingine ambacho kinasaidia katika kuunda mfumo wa saketi katika ubongo pamoja na muunganiko wake. Kitu hiki kinaelezewa kuwa ni mazingira ambayo mtu anaishi pamoja na ujumbe au taarifa ambazo binadamu anaweza kusikia, kutafsiri na kuelewa.

"Ukuaji wa mfumo wa ubongo hupitia hatua kuu mbili, ya kwanza huwa haihitaji ujuzi au uzoefu wowote kutoka katika mazingira anayoishi mtu na hatua ya pili ambayo huwa tofauti na ile ya kwanza, huwa inahitaji ujuzi au uzoefu ambao mtu huwa anaupata kutoka katika mazingira (Carla Shatz, 1996, Chuo kikuu cha Kalifonia, Nash mwaka 1997).

Mfumo wa ubongo ukishajiunda, huwa una kipindi maalumu cha kukua na kukomaa. Kipindi hiki kitaalamu huitwa "*kipindi muhimu*" ambacho huanza kabla mtoto hajazaliwa. Fursa mbalimbali ikiwemo ya kufunza huwa wazi kipindi hiki. Hii ina maana kuwa ubongo huwa na uwezo mkubwa sana katika kipindi hiki ila uwezo huu huweza kupungua kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi kufikia mwaka mwingine".

Dokezo juu ya hili ni kuamua mara moja kuweza kubaini na kutumia vizuri kipindi hiki. Endapo tutaweza kugundua umuhimu wa kipindi hiki na tukaweza kuandaa vitu vyenye manufaa kwa mtoto na ukuaji wa ubongo wake basi mtoto huyu ataweza kunufaika na kuendeleza ubongo wake. Endapo tutashindwa kufanya hivi basi itakuwa ni madhara kwa mtoto na ukuaji wa ubongo wake. Mfano, kama tutashindwa kutumia fursa iliyopo kipindi hiki kwa kumpeleka mtoto shule mapema katika kipindi hiki ambacho uwezo wa ubongo wake huwa ni mzuri zaidi, hatoweza kunufaika vya kutosha na elimu yake ambayo ataipata. Lakini pia hata katika ufundishaji wa lugha ya pili, ni kosa na tatizo kubwa hujitokeza katika kuifahamu lugha husika endapo mtoto hatofundishwa lugha ya pili au lugha ngeni katika kipindi hiki. Chugani aliwahi kuuliza "Ni ujinga gani unaofanya lugha ngeni isifundishwe mapema mpaka kungojea elimu ya sekondari ya juu? Si sawa muda umeshapita". (Dr. Harry Chugani, hospitali ya watoto Michigani).Mfumo mzima wa kuona, kusikia, kuhisi na kutembea unaelezewa kama ifuatavyo:

Mfumo wa Kuona

Katika mfumo wa kuona, kuna neva seli (nyuroni) ambazo huanza ukuaji wake pindi mtoto anapokuwa na miezi 2 hadi 4, sawa na kipindi ambacho watoto hupata ufahamu kuhusu ulimwengu na ukuaji wa neva seli (nyuroni) hizi hufikia kikomo katika ukuaji wake baada ya miezi 8 ambapo kila neva seli moja (nyuroni) inapokuwa imeungana na nyuroni ama neva seli 15,000. Endapo mtoto atakuwa amezaliwa na tatizo la kutokuona kabisa na akafanyiwa upasuaji ili kutatua tatizo hilo akiwa na umri usiozidi miaka miwili, kuna uwezekano wa mtoto huyu kuendelea kuwa na upofu milele. Tafiti za aina hii zimewahi kufanyika kwa paka na imeonekana kuwa uwezekano wa kupona haupo.

Mfumo wa Kusikia

"Katika kipindi cha miezi 12, watoto wanakuwa wameshapoteza uwezo wa kutofautisha sauti ambazo hazina umuhimu katika lugha zao na huwa na aina yao ya uongeaji ambao huakisi lugha yao", anasema Patricia Kuhl (Chuo kikuu cha Washingtoni). Hali hii inatoa maelezo ya kutosha na kutupa sababu kwanini hawawezi kutofautisha matamshi wanapotamka L na R: kama katika neno *"barabara"* na *"balabala"*. Pia jamii nyingi ambazo watu wake si Waarabu wanashindwa kutofautisha "dh" na "z"kama katika neno *"dhalili"* husema *"zalili"*.

Kujifunza lugha ya pili baada ya kujua lugha ya kwanza ni kitu kigumu sana. "Utambuzi wa lugha ya kwanza huwa ni kikwazo katika kujifunza lugha ya pili" Patricia Kuhl anaendelea kusema. Mfano, ikiwa ubongo umejizoesha Kiswahili kama lugha ya kwanza, neva seli (nyuroni) zilizosalia katika ubongo huo huo zinapoteza uwezo wa kujizoesha kiufasaha lugha ya Kiarabu kama lugha ya pili. Mtoto ambaye amefundishwa lugha ya pili akiwa na umri wa miaka 10 hana uwezo wa kuongea lugha hiyo kiufasaha kama mzawa wa lugha husika. Kutokana na sababu hii, inashauriwa watoto waanze kusikilizishwa Qur'an mapema wakiwa bado wadogo ili waweze kufahamu vizuri herufi za Kiarabu.

Utaratibu huu unapokuwepo, watoto huweza kubadili sauti kuwa maneno. Kadri watoto wanavyosikia maneno katika lugha fulani, uwezo wao wa kujifunza lugha hiyo huongezeka mara dufu. Watoto ambao huongeleshwa mara kwa mara na wazazi wao wanaweza kuyafahamu maneno 131 ndani ya miezi 20 zaidi ya watoto ambao hawasemeshwi mara kwa mara na wazazi wao na inapofikia miezi 24 tofauti huwa ni sawa na maneno 295 kwa watoto hawa. Katika kuwaongelesha haijalishi maneno ya aina gani huwa mama wa mtoto anatumia ingawaje inasadikika kuwa maneno yenye silabi moja huwa yanafaa sana. Sauti ya maneno inayosikika huweza kutengeneza mfumo maalumu katika ubongo **(neuro-circuitry)** ambao huweza kunasa maneno zaidi. Kwa maana hiyo, mtoto anaweza kupata misamiati mingi na hali hii husababishwa na tabia ya kurejea utamkaji wa maneno husika. Ni muhimu kutambua kuwa mtoto anaweza kunufaika kwa kujifunza lugha haraka kadri atakavyokuwa na watu wanaoweza kumuongelesha mara kwa mara ikiwemo ndugu zake.

Muziki

(Elbert na wenzake 1995) anasema kuwa

muziki huandaa mfumo wa neva seli **(neural circuit).** Tafiti ilifanyika duniani ambayo ilihusisha ubongo wa wanamuziki wenye kupiga vifaa (string instruments) kwa kutumia kifaa maalumu kiitwacho **(magnetic resonance imaging)** ambapo ilibainika kuwa wanamuziki wengi walikuwa wakitumia sana ubongo wao katika kukitumia kidole gumba pamoja na vidole vingine vya mkono wa kushoto kuliko wale ambao hawakuwa wakipiga vifaa vya muziki.

Plato alisema kuwa muziki ni kitu muhimu sana katika elimu. Hata wanasayansi kwa sasa wamefanikiwa kufahamu umuhimu wa muziki katika mfumo wa elimu. Wanasayansi wanaamini kuwa muziki unaweza kuongeza uwezo wa ubongo kufikiria. Watafiti mbalimbali wamesoma muziki ili kujua ni vipi Muziki unaweza kuongeza uwezo wa kufikiria kwa kutumia makundi mawili ya wanafunzi wa masomo ya awali. Kundi la kwanza la wanafunzi lilijihusisha na upigaji wa kinanda pamoja na kuimba muziki kila siku wakati kundi la pili halikuwa likipiga kinanda wala kuimba muziki.

Baada ya miezi 8 ilibainika kuwa kundi la kwanza lenye wanafunzi wa umri wa miaka 3 lilikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza mchezo wa kujaza jedwali, kwa kupata alama 80% dhidi ya kundi la pili. Hii ilitokana na uwezo wa kundi la kwanza kuweza kuangalia maneno na kutafsiri haraka haraka zaidi ya kundi la pili.

Uwezo huu pia huweza kuhamia katika nyanja za hesabu pamoja na uinjinia. Kwa kulingana na maelezo yaliyotolewa na mwanafizikia aitwae Gordon Shaw wa Irvine, Kalifonia "mafunzo ya muziki wakati wa mapema (utotoni) humjengea mtoto uwezo wa kujenga hoja". (Begley 2000)

Imedhihirika kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya ubongo, muziki, hesabu pamoja na uwezo wa kujenga hoja. Uwezo mkubwa wa kufikiri pia hutegemea vitu vilivyotajwa hapo juu. Walimu wanaowafundisha watoto wadogo hawafundishi watoto hao hesabu wala mchezo wachemsha bongo.

Hata hivyo, watoto hupenda sana muziki na wanaweza kushiriki katika muziki. Francis Rauscher (chuo cha Wisconsini) aliwahi kutoa somo la kupiga kinanda kwa baadhi ya watoto na baadhi yao aliwapa somo la kuimba. Baada ya miezi 8, aligundua kuwa wale watoto waliokuwa wamepewa somo la kuimba muziki walikuwa na uwezo mkubwa wa kujenga hoja ukilinganisha na wale ambao waliokuwa wanapiga kinanda. Hii ilidhihirika kupitia uwezo wao katika kucheza mchezo wa kujaza jedwali, kuchora maumbo mbalimbali ya kijiometri na kunakili maumbo yenye rangi mbili tofauti.

Pindi watoto wanapotumia neva seli zao kwa kusikiliza muziki, pia huongeza uwezo wao wa kufanya hesabu. Muziki unaweza kuhamasisha mfumo wa ubongo na kuimarisha uwezo wake wa kujenga hoja. (Nash 1997).

Watoto wanatakiwa kuhamasishwa kutumia vifaa vya muziki.

Hisia

Mfumo wa kuhisi kwa binadamu huanza kujiunda kabla ya kuzaliwa kiumbe (mtoto). Hata hivyo wazazi nao wana mchango wao katika kuunda mfumo huu. Wazazi wanaweza kumjenga mtoto aweze kuwa na hisia fulani kupitia malezi wanayotoa.

Mfano, endapo mtoto anakuwa amejenga mazoea ya kufurahi na kumkumbatia paka au kufurahi anapoona ndege angani, hisia hizi huendelea katika mfumo wake na kila anapokutana na vitu hivi huweza kuhisi furaha. Kwa hiyo, ubongo wake huwa na hisia hizi wakati wote na endapo ataondoa mazoea au hisia hizi mfumo wake wa kiumeme na kikemikali pia utaweza kubadilika kulingana na hisia ambazo ataweza kuzipata kila anapokutana na vitu hivi.

Endapo mtoto atakuwa anakutana na hali fulani mara kwa mara basi huweza kujenga hisia fulani kutokana na hali hiyo. Mfano, ikiwa mtoto huwa na tabia ya kujijengea kitu mithili ya nyumba na ikawa mama yake anachukia na kumkataza kila afanyapo hivyo, mtoto huyu hatoweza kuwa na hisia za furaha kila anapokutana na mazingira ama matukio ya aina hii.

Kitu cha msingi katika kujenga hisia za mtoto hutegemea na marejeo ya kutenda au kutokutenda kitu fulani. Kitu cha mara moja bila kujirejea mara kwa mara hakiwezi kuathiri tabia ya mtoto kihisia.

Tafiti moja imebaini kuwa wazazi ambao hawana uwezo wa kufurahisha watoto wao hufanya watoto wakose furaha na msisimko.

Msongo wa Mawazo (Stress) Unaweza Kuunda Hisia

Msongo wa mawazo (Stress) na vitisho pia huathiri hisia za binadamu. Saketi hizi za hisia hupatikana katika amigdala, sehemu ya ubongo ambayo huwa na kazi ya kupokea na kufasiri picha na sauti kwa ajili ya kuleta hisia fulani kwa binadamu. Taarifa ya taswira iliyoonekana kupitia

macho au sauti iliyosikika kupitia masikio huweza kufikia katika eneo hili la ubongo yaani amigdala kabla ya kufika katika eneo la kumfanya binadamu afikiri na kufanya maamuzi **(rational and thoughtful neocortex).**

Kama ikiwa taswira au sauti ama chochote kilichotokea huweza kusababisha mtu ahisi maumivu, mfano kwa mtu aliyelewa na kupigwa akiwa anarudi nyumbani kwake, basi kukabiliana na hali hii eneo la amigdala hutoa kemikali maalumu katika neva seli zake (neuro chemicals) kabla taarifa kuhusu maumivu ya mtu huyu hayajaenda kutafsiriwa na kutolewa maamuzi na ubongo **(rational and thoughtful neocortex).** Hali hii huendelea na kumfanya muhusika apate hofu kwa kipindi fulani. Sehemu ya ubongo huendelea kuwa katika hali ya tahadhari kutokana na hali hii ya hatari. Hapo ndipo utamuona mtu anaweza kuonesha hisia zake kukabiliana na hali hii ya hatari kwa vitendo kama vile kukunja uso, kupiga kelele au kuonesha ishara yoyote ya kuchukia (kuwa na hasira).

Hali hii hudumaza ukuaji wa **(cortex)** na hupunguza uwezo wa kupokea ama kuelewa taarifa (ikiwemo pia kuelewa lugha). Kutokana na sababu hii Mtume alisema kuwa ni bora binadamu akae kimya anapokuwa amekasirika, ili kuzuia maneno yasiyofaa kwa wengine kutokana na hasira alizokuwa nazo.

Mfumo wa Utembeaji (Ujongeaji)

Mfumo wa utembeaji kwa mtoto kabla hajazaliwa huanza katika wiki ya 7 baada ya ujauzito na hufikia tamati kati ya wiki ya 15 hadi 17. Hiki ndicho kipindi ambacho sehemu ya ubongo inayohusiana na utembeaji wa binadamu hujiunda. Hatua ya awali katika uundaji wa mfumo huu hudumu na huweza kuchukua hadi miaka miwili kuandaa seli za ubongo, katika ubongo wa nyuma ambayo ndiyo inahusika katika utembeaji (ujongeaji).

Mfumo huu pia huendelea kujijenga kupitia hatua na utaratibu tofauti tofauti pale mtoto anapokuwa ameshazaliwa na kuanza kujongea. Kwa hiyo, ikiwa mtoto atazuiwa asiweze kujongea athari yake ni kwamba seli za ubongo zinazohusika na ujongeaji (utembeaji) hazitoweza kujijenga vizuri katika sehemu ya ubongo wa nyuma. Pindi mtoto anapotembea taarifa hutumwa katika ubongo **(brain's motor cortex).**Kadri mtoto anavyojongesha kiungo kama vile mkono, ubongo huweza kuamuru mkono huo ujongee kiurahisi.

Kipindi cha utembeaji kina muda wake maalumu na kwa miaka michache. Mtoto ambaye hakupata hamasa ya kujifunza na kuweza kutembea katika kipindi hiki hadi akatimiza miaka 4 ataweza kutembea ila siyo kirahisi sana ikilinganishwa na yule ambaye alijifunza mapema (Carmichael 2007).

Ufanyaji wa mazoezi ni muhimu siyo tu kwa afya ya moyo bali pia kwa afya ya ubongo kwa kuwa husaidia kuupatia ubongo virutubisho muhimu vya glukosi **(glucose)** na kusaidia kuimarisha muunganiko wa neva ambazo humfanya mtoto aweze kujifunza na kuelewa haraka. Watoto ambao hufanya mazoezi hufanya vizuri katika masomo yao shuleni. Watoto pia wanatakiwa wapewe shughuli zenye kuchangamsha viungo vyao shuleni badala ya kuachwa wakae tu katika viti vyao

wakiwa wanasoma hesabu za kuzidisha pamoja na mashairi. Ujuzi huweza kukaa muda mrefu katika akili ya binadamu endapo mtoto atashughulishwa kielimu siyo tu kwa kutamka kwa mdomo kile anachokisoma bali pia inatakiwa ahusishwe kiumbile na kihisia katika masuala ya elimu.

Msamiati na uwezo wa Kukumbuka Utotoni

Ugunduzi uliofanyika kuhusu elimu ya viumbe hai umeweza kubainisha sababu zipi huchangia kwa watoto wasio na asili ya Kiarabu kuweza kuhifadhi Qur,ani wakiwa na umri mdogo. Baadhi ya watoto huweza kuhifadhi Qur'an yote kabla ya kutimiza umri wa miaka 10. Kitendo cha kuhifadhisha watoto wadogo imekuwa ni kitu adimu sana duniani kwa sasa. Mwili wa binadamu siku zote unahitaji chakula ili uweze kukua lakini uwezo wa kukumbuka unaupatia ubongo msingi wa kujifunza na kuelewa lugha fulani. Fursa ya mtoto kujifunza lugha na vitu vingine hudumu hadi kufikia miaka 12. Ubongo unaweza kufanya kazi zaidi kulingana na kiwango cha glukosi ambayo inapatikana. Ubongo wa mtoto huhitaji zaidi glukosi zaidi ya ubongo wa mtu mzima. Inakadiriwa kuwa ubongo wa mtoto hutumia kiwango cha glukosi mara mbili zaidi ya mtu mzima pindi mtoto huyu anapofikia umri wa miaka 4 kuelekea utu uzima (baleghe). Kwa hiyo ubongo wa mtoto mdogo unaweza kufanya kazi kwa haraka na vizuri zaidi ya ubongo wa mtu mzima. Masomo ambayo husemekana na huaminika kuwa ni magumu kama vile hesabu za maumbo ya pembetatu na lugha ngeni ni vema yangefundishwa katika kipindi cha utotoni ambapo ubongo wa mtoto unaweza kuelewa na kujifunza kirahisi. Ni rahisi sana kwa mtoto wa shule za awali kuweza kusikia, kuelewa na kuongea lugha ya pili ingawaje atakosa matamshi yanayorandana na mzawa wa lugha hiyo.

Jinsi Ubongo Unavyobadilika

Mazoezi husaidia kukuza ubongo katika eneo linalohusiana na kumbukumbu na hivyo kufanya ubongo uweze kuwa na ufanisi mzuri wa kazi yake. Watafiti wamegundua kuwa mazoezi huongeza msukumo wa damu katika sehemu ya ubongo inayohusiana na utunzaji kumbukumbu, hivyo kufanya seli mpya kuundwa katika sehemu hiyo (Carmichael 2007)

Wazazi wanatakiwa Wazungumze Vizuri na Watoto Wao

Tofauti kubwa iliyokuwepo miongoni mwetu katika nyumba tunazoishi ni kuhusiana na jinsi gani tunazungumza na watoto. Wazazi ambao wamejaaliwa pesa nyingi na elimu ya kutosha huwa na tabia ya kuzungumza na watoto wao mara kwa mara na hii huchangia watoto hawa kuwa na misamiati ya kutosha katika lugha. Pindi watimizapo umri wa miaka 3, watoto wanaotoka familia za kitajiri (ambao wazazi wao ni matajiri) wanakuwa wameweza kusikia zaidi ya maneno milioni 30, hii huwa ni mara tatu ya yale maneno ambayo watoto kutoka familia za kimasikini kuweza kusikia.

Pia kuna tofauti kubwa katika namna ya kuzungumza na watoto hawa. Wazazi

wenye kipato kikubwa na elimu huongea na watoto katika namna ya makubaliano au maridhiano na huwapa watoto kauli zenye kutia moyo au kuhamasisha kama vile "vizuri sana", "sawa", "nakupenda sana", "umefanya kazi nzuri"). Wazazi ambao wanafanya kazi huwasifu watoto wao mara chache na mara nyingi huonekana kukinzana au kupingana na watoto wao kwa kutumia maneno kama vile "hivyo ni vibaya sana", "umekosea kabisa", "acha kufanya hivyo", "acha kabisa", "nyamaza".

Wazazi ambao ni masikini nao huwasifu watoto wao mara chache na mara nyingi huonekana kupingana na watoto wao.

Wingi wa misamiati ya mtoto katika lugha hutegemea na mchango wa wazazi wao hususani mama zao wanavyozungumza nao. Watoto ambao wazazi wao ni wataalamu katika kada fulani husikia asilimia 75 ya maneno zaidi ndani ya saa moja ukilinganisha na watoto ambao wazazi wao ni wafanya kazi, na mara tatu zaidi ya watoto ambao wanatokea katika familia za wazazi wenye kipato duni. Watoto wa familia tajiri hupewa mtazamo chanya mara mbili hadi mara tano zaidi ya watoto wanaotoka katika familia masikini.

Watoto wa aina hizi mbili walijaribiwa wakiwa na umri wa miaka 3,na ilibainika kuwa watoto waliowahi kusikia maneno mengi na uzoefu chanya waliweza kupata alama za juu sana kuliko wale waliowahi kusikia maneno machache na uzoefu mdogo.

Ifahamike kuwa wazazi wenye kipato cha chini pamoja na wazazi ambao wanafanya kazi pia wanawapenda watoto wao kama wazazi wengine wanavyopenda watoto wao (Begley na Wingert 1997).

Kuanza kwa Masomo ya Awali Nchini Marekani

Mradi huu wa masomo ya awali ulikusudia kuwaendeleza watoto wanaotoka katika familia za wazazi wenye kipato cha chini, tangu mwaka 1965 lakini haukufanikiwa. Hii ilitokana na watoto wengi kutokuwa na uwezo mzuri kiakili na kuhifadhi vitu. Sababu kubwa iliyochangia ni muda wa uandikishaji watoto katika masomo. Mradi huu wa masomo ulihusisha watoto wa miaka 2, 3 na 4. Mwaka 1992, mradi wa Abecerdaria ulianzishwa. Watoto 120 kutoka familia masikini walichukuliwa na kuwekwa katika kundi moja kati ya manne kwa lengo la kujifunza masuala ya elimu katika shule ya watoto (chekechea). Kundi la kwanza lilikuwa na watoto wenye umri kuanzia miezi minne hadi 8, la pili lilikuwa na watoto wa umri wa miezi minne hadi miaka mitano, kundi la tatu kuanzia miezi mitano hadi kufikia miaka nane na kundi la nne kuanzia miezi mitano hadi miaka nane lakini halijakuwa na elimu yeyote iliyotolewa. Je kuna maana gani kumpatia elimu mtoto wa miezi minne? Ni kuwapa tofali na ushanga wachezee, kuzungumza nae au kumpa fursa acheze michezo mbalimbali kama vile **kuokota vidude.** Kila mchezo katika michezo 200 ya kujifunzia umekusudia kuendeleza uelewa wa mtoto, lugha ya mtoto pamoja na kuweza kumuendeleza mtoto kijamii. Watoto walisajiliwa katika mradi wa Abecedaria kama wanafunzi wa masomo ya awali waliweza kupata alama za juu katika masomo ya hisabati na kusoma kuliko watoto wengine na walibainika kuwa na upeo mkubwa wa kuelewa na kuhifadhi. Hii imedhihirisha kuwa kujifunza mapema kuna manufaa sana kwa mtoto. Endapo mtoto ataanza kujifunza akiwa na umri wa miaka mitano, inakuwa ni vigumu kuweza kunufaika ipasavyo katika masuala ya kitaaluma au kukua kwa ubongo wake kwa sababu kipindi cha yeye kuweza kujifunza haraka kinakuwa kimepita.

Je, ikiwa kipindi cha kujifunza haraka kimepita kabla ya kuhitimu mafunzo ya awali mwanafunzi hatoweza tena kupata fursa ya kujifunza? Je na wale watoto wanaotoka katika familia za kimasikini ambazo wazazi hawana uwezo wa kuwapatia japo ushanga wajifunze kuhesabu au kuweza kuongea nao inakuwaje? Fursa bado ipo kwa hawa watoto kujifunza kwa vile ubongo una uwezo wa kujifunza kipindi chote cha maisha ya binadamu. Chukua mfano kwa kutazama baadhi ya watu ambao walikuwa hawajajifunza lugha ngeni kama vile Kifaransa wakiwa vyuoni wanasoma na hatimaye wanajifunza lugha hiyo na kuijua wakiwa siyo wanafunzi muda mwingine wakiwa washastaafu kazi zao. Kwa hiyo bado inawezekana ingawaje kuna tatizo. Watoto wa aina hii ambao hawajakuwa na msingi mapema wakiwa ngazi ya chini kielimu wanakuwa na uwezo mdogo kiakili.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, Ingawaje wote tunazaliwa na uwezo, uwezo huu unaweza kukua kama tutafanya jitihada kujiendeleza. Kwa hiyo wazazi lazima watambue jinsi gani ubongo unaweza kukua na kupokea ujuzi au ufahamu wa jambo.

Kuna taaluma ya vitu vitatu vya msingi vinatakiwa kuwepo katika ubongo wa mtoto ndani ya muda sahihi;

- Ubongo wenye uwezo wa kujenga hoja (kufanya hesabu na kujenga hoja) katika ubongo
- Ubongo wenye uwezo wa kujifunza, kuelewa na kuitumia lugha katika ubongo na
- Ubongo wenye uwezo wa kushiriki katika muziki kupitia ubongo (kama vile kuimba)

Mnamo tarehe 30/9/1997, waziri mkuu wa Uingereza Mh. Tony Blair alisisitiza katika hotuba yake huko (Brighton, England), kuwa mtoto anatakiwa aanze masomo ya awali akiwa na umri wa miaka mitatu badala ya minne, huku akiwa anasisitiza kutazama umuhimu wa kuandaa mazingira ya kuwaelimisha mapema watoto ili kuboresha uwezo wa ubongo wao.

Wazazi Wanaweza Kufanya Kitu Gani?

❒ UBONGO WA MANTIKI

Ujuzi unaohitajika: kufanya hesabu na kujenga hoja

Wakati wa kujifunza: kipindi cha kuzaliwa hadi miaka minne

Ambavyo tunafahamu: Sehemu ya ubongo inayohusika na upigaji hesabu inakaa katika koteksi **(cortex)** za ubongo karibu na sehemu ya ubongo inayohusiana na muziki. Watoto ambao hufundishwa vitu rahisi kinadharia hufanya vizuri katika somo la hisabati.

Hatua ya kuchukua: Michezo ya kuhesabu inaweza kutumika kwa watoto. Mfano, watoto wanaweza kuchora jedwali na kujifunza hesabu za mahusiano huku kila mtoto akipewa sahani moja na uma mmoja ili kuakisi uhusiano uliopo. Pia muziki unaweza kufunguliwa wakati watoto hawa wakiwa wanajifunza.

❒ UBONGO WA MUZIKI

Ujuzi: Muziki

Wakati wa kujifunza: miaka mitatu hadi miaka 10

Tujuavyo: (string players) Wapiga vifaa vya muziki wana fursa kubwa ya kutumia mfumo wa ubongo (**sensory cortex)** wakati wa kupiga vifaa hivyo kwa vidole vyao vya mkono wa kushoto. Watumbuizaji wachache katika matamasha huanza kutumia vifaa hivi baada ya kutimiza miaka 10. Ni vigumu kuweza kuvitumia vifaa hivi vya muziki pale mtu anapofikia utu uzima endapo hakujifunza utotoni. Somo la muziki husaidia katika kumpatia mtu ujuzi.

Hatua ya kuchukua: Wazazi wafungulie Qur'an ikiwa inasomwa (kwa tajwid), adhana, na sauti za nasibu pamoja na ndege zilizorekodiwa. Pia wanaweza kuamua kuimba nyimbo pamoja na nashid (nyimbo za kidini) ama nyimbo laini wakiwa na watoto wao. Watoto nao wapewe vifaa vya muziki ili tuweze kufahamu kama wanaweza kujifunza chochote kuhusu muziki au kama wanaweza kuvutiwa na muziki/nyimbo waliyosikia.

❒ UBONGO WA LUGHA

Ujuzi: Lugha

Wakati wa kujifunza: wakati wa kuzaliwa hadi miaka 10

Tujuavyo: katika mfumo wa kusikia, kuna uwasilishwaji wa sauti katika mfumo wa maneno ambayo huundwa katika umri wa mwaka mmoja. Mtoto huweza kuunda misamiati zaidi kadri anavyosikia maneno mengine akiwa ametimiza miaka miwili. Kwa hiyo kila anavyosikia maneno akiwa na miaka miwili, misamiati yake katika lugha inakuwa mingi zaidi. Tatizo la kusikia huzuia uwezo wa kulinganisha sauti na herufi.

Hatua ya kuchukua: ni muhimu wazazi wazungumze na watoto wao mara kwa mara. Kama wanahitaji watoto wao waweze kuifahamu kiufasaha lugha ya pili kwa kujifunza, wazazi wanalazimika kuwafundisha watoto wao kabla hawajatimiza umri wa miaka 10. Tatizo la kusikia linatakiwa lipatiwe tiba inayoondoa maabukizi yanayozuia masikio kutosikia.

Uislamu, Uimbaji na Muziki

Dini ya Kiislamu inaruhusu kuimba na muziki endapo viwili hivi havihamasishi maovu, hisia za kimapenzi au kukinzana na taratibu za ibada za fardhi. Maswahaba wa Mtume Muhammad (S.A.W) na wachamungu waliofuata baada ya wao walikuwa wanasikiliza nyimbo mbalimbali katika matukio muhimu ya maisha yao ikiwemo harusi, sikukuu za idi mbili, tafrija na sherehe pindi watoto wanapozaliwa. Wao walikuwa wakiimba kwa kutumia vifaa vya muziki kama vile ngoma. Imam Bukhari na Muslim wanahadithia kuwa

baadhi ya watu wa Abyssinia walikuwa wakiimba na kucheza mbele ya Mtume hali ya kuwa Mtume akitazama pamoja na mkewe 'A'ishah kwa muda mrefu kwa dhumuni la kumfurahisha mkewe.

'A'isha[r.a]pia amehadithia kuwa;

Mjumbe wa Allah alikuja katika nyumba yangu ambapo kulikuwa na wasichana wawili wakiniimbia nyimbo ya Bu'ath (kisa kinachohusu vita baina ya makabila mawili ya kiansar, yaani Khazraj na Aws kabla ya uislamu). Mjumbe wa Allah aliingia na kujilaza huku akigeuza uso wake upande wa pili. Ghafla Abu Bakar aliingia na kuanza kunitolea sauti ya ghadhabu akisema "Ala za muziki wa shetani leo zimeingia katika sehemu alipokaa Mjumbe wa Allah?". Mjumbe wa Allah alimgeukia na kumwambia "waache hao". Abu Bakar alipoonekana kuwa hazingatii anachoambiwa, nikawaoneshea ishara wale wasichana waondoke nao walielewa hivyo wakaondoka. Ilikuwa ni siku ya Eid, ambapo wahabeshi walizoea kuchezea mikuki na ngao. Mjumbe wa Allah aliniuliza kama ningependa kuona tena tukio kama lile nami nikasema ndiyo. Mjumbe wa Allah akaniruhusu niinuke na kumkumbatia kwa nyuma huku nikigusisha shavu lake na langu na akawa anasema, "endeleeni tu enyi wahabeshi". Nilipohisi kuchoka Mtume aliniuliza kama nimechoka nami nikamjibu ndiyo nimechoka. Kisha akaniruhusu niondoke

(imepokelewa na Muslim)

Hili ni fundisho kwa wazazi waweze kuruhusu watoto wao wa kiume na wa kike wapate viburudisho. Siku za hivi karibuni, muziki na sanaa hutumika kuhamasisha maovu kama vile zinaa, utumiaji wa dawa za kulevya pamoja na ulevi. Hata hivyo bado tunayo fursa ya kutumia vizuri muziki katika kuelimisha na kuburudisha.

Hakuna hadithi ya Mtume ambayo inakataza kuimba nyimbo ama muziki. Mwanazuoni Al Qaradawi (2007) hakubaliani na hadithi zote ambazo baadhi ya watu wanazitumia kupinga kuimba nyimbo ama muziki kwa kuwa zina mapungufu na shaka katika tafsiri, simulizi na wakati mwingine katika tafsiri na simulizi zake. Hakuna rejea za moja kwa moja katika hadithi hizi zinazoonesha kukatazwa kwa muziki na kuimba nyimbo. Pia kuna ushahidi wa kutosha katika kipindi cha Mtume watu walihalalishiwa kuimba nyimbo na muziki. Kwa mfano;

1. Abu Bakar alipoingia katika nyumba ya Mtume alimkuta 'A'isha akisikiliza wasichana wawili ambao walikuwa wakimuimbia ('A'isha). Abu Bakar aliwakataza kwa kusema "vifaa vya shetani vimekuja katika nyumba ya mjumbe wa Allah?" Hata hivyo Mtume alimwambia: "waache waendelee tupo katika kipindi cha sikukuu za Eid."

2. Pindi mke wa Mtume (s.a.w) 'A'isha alipomsindikiza bi harusi chumbani kwake, Mtume Muhammad alimuuliza bi harusi yule, "je ulishaburudika?"

3. Kipindi Mtume anahama kutoka Makka kuelekea Madina, kuna sherehe zilifanyika na katika sherehe hizo walikuja wasichana kumkaribisha Mtume huku wakiwa wanamuimbia. Mabinti kutoka ukoo wa Banu al-Najjar walikuwa nao wakipiga ngoma na kuimba nyimbo. Abu Bakar aliwakataza lakini Mtume wa Allah alisema "waache waendelee dini yenu haijakataza kufurahi."

4.'Umar ibn Khattab aliingia msikitini siku moja na aliwakuta wahabeshi wakicheza muziki huku wakiwa wamebeba mikuki mbele ya Mtume na mkewe 'A'isha katika siku ya sikukuu ya Eid. 'Umar aliwakataza lakini Mtume wa Allah (s.a.w) alisema "waache waendelee".

Taratibu za kisheria ni kuwa jambo lolote hutegemea nia ya mtu na kila kilicho batili ama chenye kupotosha ukweli lazima kiharamishwe. Nyimbo zenye kuhamasisha ngono, zenye kwenda kinyume na maadili ni haramu. Nyimbo nyingine ambazo hazipo katika makundi tajwa hapo juu yaani hazihamasishi maovu ni halali.

Avicenna akizungumzia kunyonyesha, na muziki

Avicenna alisema kuwa: kuna aina ya homa inayosababishwa na tatizo la kisaikolojia.

Unyonyeshaji: Avicenna alisisitiza juu ya kuwepo kwa uhusiano baina ya saikolojia ya mtu na afya ya mwili wa mtu. Mfano alioutoa ni kuhusu unyonyeshaji wa mtoto. Hivyo ameshauri kuwa makini katika kuchagua mtu wa kunyonyesha mtoto.

Kuhusu muziki: Avicenna amesisitiza umuhimu wa muziki kwa wagonjwa, wenye matatizo ya kimwili na kisaikolojia.

Picha na Michoro katika Uislamu

Picha na michoro katika uislamu ni halali isipokuwa zinakuwa haramu kama zitakuwa zinaonesha utupu, uovu wa aina yeyote ile au zinaenda kinyume na maadili ya jamii husika. Kipindi cha Mtume[s.a.w], picha na michoro mbalimbali ilikuwa ikiabudiwa kama miungu ya watu husika na hii ndiyo ikawa sababu ya picha na michoro kukatazwa. Maneno yanaweza kuwa na maana tofauti kwa mazingira ya sasa ukilinganisha na zama za kale. Mfano, neno sayyarah limetumika katika Qur'ani (surat Yusufu) kama msafara wa wasafiri ambapo kwa sasa neno hili hili lina maana ya gari.

Kanuni na utaratibu kama huu pia unatumia kutoa hukumu juu ya picha na michoro iwe ya rangi, filamu, kielectoniki n.k. Kwa kipindi kirefu kilichopita, picha na michoro ilitumiwa na wapagani kwa ajili ya ibada kama miungu yao. Hali hii inaweza kusaidia kuelezea sababu ambayo ilimfanya Mtume asikataze picha au michoro anapoiona sehemu ikiwa haijakusudiwa kufanywa miungu kwa kuabudiwa. Pia kwa kuzingatia mazingira kama haya tunaweza kutambua kwa nini Mtume hakuwakataza watoto walipokuwa wakichezea masanamu pasipokuwa na lengo la kuyaabudu kama miungu yao.

Katika mazingira ya sasa pia, picha yoyote au mchoro unaokusudiwa kuabudiwa kama Mungu ni haramu. Lakini michoro na picha nyingi siku hizi hazitumiki katika ma-

suala ya kuabudu (yaani kumithilisha na Allah) isipokuwa huwa na matumizi katika masomo ya sayansi, teknolojia, kufikisha habari kupitia vyombo vya habari, kuelimisha, kuburudisha, kuweka katika vitambulisho na kadi za benki. Matumizi ya picha na michoro katika namna hizi haujakatazwa na Mtume wa Allah (s.a.w). Hivyo tunaweza kutumia picha na michoro kama namna hii kwa kuzingatia maslahi yaliyopo bila kuleta madhara ya aina yeyote. Chukulia mfano mwingine wa kisu. Kisu kinaweza kutumika vizuri kikaleta manufaa hivyo ni halali lakini pia kinaweza kutumika vibaya na kusababisha mauaji (isipokuwa katika kuchinja kulikoruhusiwa na Allah, ama kujikinga unaposhambuliwa au vitani) au uvunjifu wa amani hivyo kinaweza pia kuwa haramu. Hivyo ulalali na uharamu wake unategemea na nia pamoja na matumizi ya mtu.

Kukua kwa Ubongo wa Mtoto Mdogo

Watoto wadogo wanapenda sana kujifunza lugha, Mambo mbalimbali pamoja na mahusiano. Huwa hawapendi kutulia tu na kutazama kama walivyokuwa wachanga. Yafuatayo ni mambo ya msingi wazazi wanatakiwa wazingatie katika kuandaa muendelezo mzuri wa mtoto na kukuza ubongo wake.

❒ KUWA MAKINI KATIKA MAMBO MUHIMU YALIYOPO KATIKA MAZINGIRA

Mfuatano wa matukio na hali ambayo ilichangia matukio hayo kutokea ni muhimu sana kwa watoto. Kwa kawaida ubongo wa watoto huhusisha matukio na sababu ya kutokea tukio fulani pamoja na madhara yaliyotokana na tukio fulani. Wazazi wanaweza kuonesha watoto wao mfuatano wa matukio (kama vile athari zitokanazo na mwanga, joto, maji na upepo) na taratibu zilizopo katika jamii (kama vile kugonga hodi kabla ya kuingia ndani, kusema asante). Watoto pia katika umri huu hupenda kujifunza sababu na umuhimu wa vitu ambavyo huviona mara kwa mara kama vile (kwa nini watu wanafanya usafi, kwa nini watu wanapika na kwa nini watu wanavaa).

Kitu kingine ni hali ambayo huchangia kutokea jambo fulani. Watoto huwa hawaoneshi sana kuvutiwa na hali ya matukio kama ilivyokuwa katika mfuatano wa matukio. Hata hivyo, kuanzia umri wa miezi 13 hadi 19, huwa wanakuwa na uelewa wa baadhi ya mambo kwa kujiuliza. Kwa mfano, wanaweza kujua vitu mbalimbali, watu na baadhi ya matukio yanayohusiana na sehemu fulani kama vile mgahawani? Wanapofikia umri wa kwenda shule kwa ajili ya masomo ya awali, wanaweza kutumia ufahamu waliopata hapo awali kukabiliana na mazingira yanayowazunguka. Wazazi wanatakiwa kuwaeleza watoto wao kuhusu “nini”, “nani”na “kwa nini” na “jinsi gani”.wawajulishe taarifa hizo wanapokuwa pamoja na watoto katika mazingira tofautitofauti.

❒ KUHAMASISHA WATOTO KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA SHUGHULI MBALIMBALI

Kujifunza kwa dhana ya kitu fulani kunakuwa rahisi sana kupitia (ushiriki wa umbile la mtu) ama kwa vitendo. Kwa mfano, neno “chini” linaweza kufahamika zaidi kwa mtoto endapo mtoto huyo atapewa fursa ya kushiriki kwa vitendo, yaani aende aka-

kae chini ya kitu kama vile meza. Kitendo cha kumzuia mtoto katika mazingira na vitu fulani humfanya mtoto ashindwe kuendelea kujifunza vitu tofauti tofauti. Uwepo wa mzazi pia ni muhimu katika mafunzo ya mtoto kwa kuwa mzazi anatakiwa atoe mwongozo kwa mtoto na kuhakikisha usalama wa mtoto pindi ajifunzapo kitu fulani pamoja na kuonesha ushirikiano wake kwa mtoto ikiwa ni pamoja na kuhamasisha mtoto aendelee kujifunza.

❒ KUZUNGUMZA NA KUWATAFSIRIA WATOTO KWA YALE WANAYOAMBIWA.

Kipindi ambacho wazazi wanazungumza na watoto wao kwa namna moja au nyingine watoto huweza kupata misamiati zaidi katika lugha. Katika kipindi cha miezi 12 hadi 24, watoto hupenda kufahamu majina ya vitu mbalimbali. Endapo wazazi wanakusudia kuwatajia watoto wao majina ya vitu hivi ni vizuri wakatumia lugha nyepesi yenye kueleweka kwa kila kitu kwa kukitaja. Pia wanaweza kuvigusa vitu wanavyotaja kwa watoto ili kuwasaidia kuelewa lugha. Kadhalika wazazi wanaweza kutumia lugha ya vitendo kama kwa kusema “naenda kuchukua kitabu” huku akiwa anelekea kuchukua kitabu. Wazazi wanapouliza maswali na kisha wakatoa majibu na maelezo ya ziada kutokana na kile walichosikia kwa watoto wao, watoto nao huweza kukuza uwezo wao

wa sarufi katika lugha. Kwa mfano, mtoto akiulizwa "ndege yupo wapi?", yeye akajibu "tunduni" lakini mzazi akatoa jibu kama hili na maelezo ya ziada husaidia mtoto kuelewa zaidi sarufi ya lugha. Kwa mzazi akasema, "ndiyo ndege yupo kwenye tundu", hapa sentensi inakuwa imekamilika na hivyo mtoto anajifunza sarufi katika lugha kupitia mzazi wake.

❒ DUMISHA MAZINGIRA CHANYA YENYE KURIDHISHA NA KUMFURAHISHA MTOTO

Hisia ambazo wazazi wanazionesha huchangia kuathiri ubongo wa watoto wao. Endapo mzazi atakuwa na msongo wa mawazo muda mwingi, basi mabadiliko ya kimwili yatamuathiri hata mtoto wake na kumfanya mtoto aweze kufanana kiakili na mzazi huyu mwenye msongo wa mawazo **(Fields na wengine 1988)**. Mazingira ya furaha kwa mzazi hufanya mtoto nae awe mwenye furaha na mtazamo chanya. Watoto hufuata hisia za wazazi wao na pia hisia zao huweza kuathiriwa na jinsi wanavyopewa malezi na misaada kutoka kwa wazazi na walezi wao. Mazingira mazuri pamoja na malezi mazuri humuandaa mtoto mwenye uwezo mzuri wa kujifunza haraka na humfanya mtoto awe na hisia chanya.

❒ KUHAMASISHA UTENDAJI PAMOJA NA MAREJEO YA MARA KWA MARA

Kutenda kitu na kufanya marejeo katika utendaji wa kitu husika ni muhimu sana. Kitu ambacho mtoto anaweza kujifunza kutokana na hali au kitu ni sehemu ndogo sana ya ujuzi ambao yeye ameweza kupata kutokana na muonekano wa kitu hiko, tukio au mazingira. Kiuhalisia watoto wanaweza kuelewa kidogo sana katika yale wanayosikia, kuona na kuhisi. Ubongo unahitaji muda wa kutosha katika kuelewa uhalisia wa jambo katika mazingira yake. Wazazi hawatakiwi kuwa na haraka watoto wanapojifunza mambo kwa vile watoto huwa na vitu vingi sana vya kujifunza.

JE MTOTO ANAWEZA KUJUA SAUTI YAKO?

Tafiti zimebaini kuwa mtoto huweza pia kujifunza kutambua sauti kipindi anapokuwa katika tumbo la mama yake. Baba wa mtoto nae huweza kuzungumza na mtoto kupitia tumbo la mama mjamzito (rolled up newspaper). Kwa hiyo mtoto anaweza kufahamu sauti ya baba yake. (HENRY BILLER 1993).

Je mafanikio ya mtu huamuliwa kabla ya umri wa miaka mitano?

Je mafanikio ya jamii ni sawa na maendeleo ya kukua kwa ubongo? Mfumo mzima wa binadamu hutegemea vinasaba na vinasaba hivi vinakuwa na idadi maalumu. Mafanikio na uzalishaji wa mtu hutegemea sana ubongo. Kwa binadamu, huwa kuna miunganiko ya mifumo ya neva zaidi ya trilioni ambayo huundwa kabla ya kufikia umri wa miaka 10, na mara nyingi hufumwa/huundwa katika umri wa miaka 3. Mataifa ambayo yanajali watoto yana fursa kubwa ya kufanikiwa. Ila kama mataifa hayo yatashindwa kuwa makini katika kuzingatia mambo muhimu katika malezi ya watoto wao mapema, nao watashindwa kupata mafanikio hayo.

Kumjali mtoto kimalezi katika kipindi cha miaka mitatu ni sawa na kuwekeza kwa mtoto na hivyo huweza kuinufaisha jamii nzima. Miunganiko ya mifumo mbalimbali katika ubongo hufanyika kati ya kipindi cha kuzaliwa mtoto hadi kufikia umri wa miaka 4. Hii ndiyo sababu ya msingi kuifanya Qur'an kuwasihi wazazi wanyonyeshe watoto wao hadi wanapotimiza umri wa miaka 2.

Mchakato huu huanza mara moja pale mtoto anapozaliwa, kipindi ambacho baba yake anapomuadhinia kwa sauti katika sikio la kulia na kushoto. Pia mi-chakato huendelea mtoto anapokuwa ananyonyeshwa na mama yake, kupatiwa upendo na faraja. Baada ya hapo mtoto hupenda awe huru na kujitawala kwa hiyo wazazi wanatakiwa wamuendeleze mtoto kiakili kupitia ushauri uliotolewa kupitia kitabu hiki.



Avicenna alihifadhi Qur'an kabla ya kufikisha umri wa miaka 10. Hii ilimsaidia kuboresha uwezo wa ubongo wake kutumika katika mambo mbali mbali na kuweza kutunza kumbukumbu. Baadhi ya watu huamini kuwa binadamu tunatumia asilimia 5 hadi 15 ya uwezo wa ubongo wetu kufanya kazi yake.

(Morgan 2007)

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 40: ANDAA KITABU CHA MWEZI

Wazazi na watoto wao wanaweza kuandaa klabu ya kusoma vitabu wakiwa na lengo moja. Vitabu hivyo vinaweza kusomwa kwa wiki, kwa mwezi au kila baada ya miezi michache kulingana na ratiba ilivyopangwa. Kila mwanachama atasoma kitabu fulani kisha atawasilisha kitu alichosoma na kuanza kufanya majadiliano na wenzake. Kazi hii inaweza kufanyika wakati kila mtu ameshakula chakula huku kukiwa na hali ya utani. Ili ratiba iweze kufuatwa na kuzoeleka lazima wahusika wawekeane kanuni za kuifuata ratiba hiyo. Kwa mfano, panga usiku wa Ijumaa au Jumamosi kuanzia saa 1 usiku kila mwezi. Kwa utaratibu huu hakutakuwa na haja ya kukumbushana na pia wanachama hawatokuwa na mgongano wa ratiba katika siku hizi.

SURA YA KUMI NA MBILI

▪ KUWALEA WATOTO WA KIUME NA WA KIKE

Kuna tofauti yoyote?

SURA YA KUMI NA MBILI **282**

Kuwalea Watoto wa Kiume na wa Kike kuna tofauti yoyote? **282**

Utangulizi 284
Uhusiano wa Kihisia 288
Hisia 289
Hadhi 289
Lugha ya Alama 290
Kasumba ya Kuwabagua Wasichana na Wavulana 290
Huzuni 291
Tofauti za Kijinsi 291
Busara ya Tofauti za Kijinsia: Majukumu, si kwa Upendeleo 292
Utengano wa Kijinsia Unaanzia wapi? 296
Jike-dume, Dume-jike 298
Malezi kwa Kutazama Jinsia 299
Kwa nini hakuna Usawa? 300
Dhana Potofu na ukweli kuhusu kina Baba 301
Madhara wayapatayo watoto kwa kutokuwepo Baba zao 302
Mahitaji Tofauti ya Wavulana na Wasichana 302
Mahitaji ya Msichana mdogo 302
Mahitaji ya Mvulana mdogo 304
Usawa katika masuala ya tofauti za Kijinsia 305
Kuchanganya jinsia na hulka 306
Wasichana na Wavulana Hujifunza tofauti 307
Malezi na Jinsia: Mtazamo wa Kiislamu 313
Njia ya Mungu ni Njia Bora: mfano wa China, Ujerumani na India 316
Kazi za Kufanya

……Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao.
(Qur'an 2:228)

Utangulizi

Kujadili tofauti baina ya wanaume na wanawake Ni muhimu, Kwa kuwa Inasaidia Kutambua majukumu na mahitaji yao mbalimbali. Pia huathiri moja kwa moja uhusiano baina ya mume na mke pamoja na uhusiano baina ya wazazi na watoto wao. Mahusiano imara hujengwa katika misingi ya maelewano ya ndani kabisa kutokana na kufanana na kutofautiana kwa jinsi. Wazo alilonalo mzazi kuhusu mtoto wa kiume au wa kike huathiri mahusiano ya watoto katika maisha yao ya baadaye. Dhana na nadharia hujenga maneno, maneno huwa vitendo, na vitendo huwa tabia na mwishowe tabia hutengeneza hulka.

Huu si mjadala kwamba ni jinsi ipi ni bora au muhimu kuliko nyingine, kwa kuwa jambo hili lilishabainishwa katika Qur'an tukufu na Mtume (SAW) kama ifuatavyo:

Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao.
(Qur'an 2:228)

Mtume (SAW) amesema:

> *Wanawake ni wenzi "wenye ulingano wa sawa" na wanaume.* (AHMAD)

Hivyo, amewafanya wanaume na wanawake katika daraja moja, wakitekeleza majukumu tofautitofauti kwa kusaidiana na si kama wapinzani au washindani.

Tofauti mahususi: Mantiki dhidi ya Hisia

Smalley (1995), anataja baadhi ya tofauti baina ya wanaume na wanawake ambazo ni:

- Kromosomu za kike (*Kromosomu XX*) zina mfumo mkubwa wa kinga kuliko zile za kiume (*Kromosomu XY*).
- Wanaume wana seli nyekundu za damu nyingi kuliko wanawake, hivyo huwa na nguvu zaidi mwilini.
- Wanaume wana misuli mingi zaidi, mafuvu manene na ngozi nene kuliko wanawake.

Karibu asilimia 80 ya wanaume na wanawake hufuata mfumo huu: Wanawake hutumia pande zote za ubongo, wakati wanaume hutumia zaidi ubongo wa kushoto. Wanawake huwa macho zaidi kuliko wanaume kwani husikia na kuhisi zaidi ya wanaume. Katika utafiti mmoja, ujumbe ulipitishwa haraka katika kioo cha kompyuta. Wanawake waliweza kuandika walichokiona, wakati wanaume waliulizana kila mmoja "Umeona?" Sikuweza kulipata."

Kwa ujumla, wanaume hupendelea kutumia upande wa kushoto wa ubongo, unaosadikika kuwa ndio makazi ya mantiki, uwezo wa kufikiri, ushindi, kufundisha, mahesabu, na uhandisi. Wanawake kwa upande mwingine hupendelea kutumia upande wa kulia wa ubongo, unaodhaniwa kuwa makazi ya hisia, sanaa, ushairi, mapenzi, muziki, na uwezo wa kuzungumza ingawa wanaweza pia kutumia upande wa kushoto wa ubongo. Wanawake si wenye shari kama wanaume, wakati wanaume kwa upande wao hupenda hoja (majibizano), kujitukuza, na huwa na wakati mgumu zaidi katika kuwafundisha watoto. Wanaume ni wepesi katika kusoma ramani kwa kuwa huwa na umakini zaidi kuliko wanawake kwa kuwa hufunzwa mambo yahusuyo anga. Ustadi wa kiakili huchambuliwa zaidi katika ubongo wa mwanaume ikilinganishwa na ubongo wa mwanamke, pamoja na kwamba wote hutumia ubongo. Vilevile, upande wa ubongo ambao unaweza kupendelewa unaweza kutofautiana kati ya wanaume (wanaume wanaopenda sanaa hupenda upande wa kulia wa ubongo wakati wale wapendao sayansi hutumia zaidi ubongo wa kushoto). (Baron-Cohen, 2002; Gilmartin na wengine., 1984)

Wanaume na wanawake wanaweza kutumia pande zote za ubongo ikiwa watajifunza.

Gray (2003) anasema kwamba wanaume hupenda kufanya maamuzi, kuteka, kutoa suluhisho, na kufurahia mafanikio. Wanawake kwa upande wao hupenda kujielezea hisia zao, kujadili matatizo yao, na kuwathamini wale wanaowasikiliza, hivyo hupenda kupendwa na kulindwa.

Wanaume hutafuta na kuelezea ukweli, wakati wanawake huelezea hisia zao. Katika utafiti mmoja, wasichana na wavulana wadogo wa Kimarekani walitakiwa kusema maneno yoyote wanayotaka kusema. Wasichana wote walisema kitu kinachohusiana na mazungumzo, wakati asilimia 60 ya wavulana walikuwa wakipiga kelele tu badala ya kutamka maneno. Mwanaume wa makamo wa Kimarekani hutamka maneno 12,000 kwa siku, wakati mwanamke wa Kimarekani mwenye umri huo huo huweza kutamka zaidi ya maneno 25,000 kwa siku. Misuli ya midomo hujongea sana wakati wa kuzaliwa kwa wasichana kuliko wavulana (Eliot, 2009).

Wanaume hutoa masuluhisho kunapotokea matatizo. Ikitokea mke akimlalamikia mume wake, hujaribu kutoa masuluhisho. Wanawake kwa upande wao, hupenda kuonesha huruma na upendo. Wanaume wamefunzwa kusimamia ukweli na kufikiri zaidi, wakati wanawake wamefunzwa kujijali zaidi. Inapotokea mwanaume anatazama mpira wa kikapu, hashughulishwi kujua maisha ya wachezaji. Kinyume chake, wanawake watavutiwa zaidi kutazama mechi hiyo ikiwa anayajua majina ya wachezaji na familia zao.Wanawake wamefunzwa kutilia umuhimu zaidi katika mahusiano kwa karibu zaidi kuliko wanaume.

Kwa kiwango fulani, wanaume, hujifunza kujitenganisha na mazingira yao. Wanawake kwa upande wao huchukua utambulisho wao kutoka kwa wanaowajua na mazingira yao. Mwanamke hajitengi na nyumba yake, watoto wake, na kazi yake. Akisahau kuosha vyombo, hufikiria kurudi na kuviosha. Nyumba yake ni sehemu yake muhimu. Kwa mwanaume hali ni tofauti kuhusu nyumba yake, kwa kuwa kwake yeye nyumba ni sehemu ya kupumzikia sana, na kuosha vyombo kwa wakati sio kipaumbele kwake.

Wanaume hukumbuka vitu kwa ujumla wake katika masuala ya uhusiano, wakati wanawake hujifunza kujikita zaidi katika mambo kwa undani wake, yaani, wanachovaa na kula katika maadhimisho katika siku ya kwanza ya ndoa zao. Wanawake hutamani zaidi mahusiano mazuri na huwa na uwezo wa kutambua mahusiano mabaya haraka zaidi kuliko wanaume. Baadhi ya watafiti waliwauliza wanandoa kujiuliza wenyewe maswali yafuatayo: Uhusiano wako ukoje katika kipimo cha 0-10? Tufanye nini ili kuimarisha mahusiano yetu ili kukaribia 10?

Wanaume mara nyingi hujibu swali la kwanza kwa pointi mbili zaidi ya wanawake, wakati wanawake mara nyingi huwa sahihi zaidi juu ya ubora wa mahusiano yao.

Mume huhitaji kujisikia anatosheleza, ambayo hutokea pindi mkewe akimsifia na hukwepa kukosolewa labda tu awe amehitaji kufanyiwa hivyo.

Wanawake wanahitaji nguvu zaidi za kihisia ambayo ni muhimu kwa malezi bora ya watoto. Wanaume si wavumilivu sana wakilinganishwa na wanawake katika watoto. Baba mmoja alikaa na mtoto wake wa kiume wa miaka 4 kwa siku nzima bila ya kuwepo mama yake. Mwisho alisema kama angekuwa akimuadhibu mtoto akoseapo siku nzima, haingetosha kumfanya mtoto aache utundu. Ni mara chache sana akina mama wanaweza kusema hivyo.

Kihisia, mwanaume ana wakati mgumu ukilinganishwa na mwanamke. Hii huweza kuchangiwa kwa kiasi fulani na maumbile au malezi na mafunzo kwa mtoto. Wanawake ni mahodari zaidi kuwa na uhusiano na watoto kuliko wanaume.

Dkt. Warren anasema kwamba mteja mpya anapomjia huuliza: "Ni akina nani marafiki wako watatu wa karibu?" Kama mteja ni mwanamke mara nyingi jibu huwa la haraka na anaweza kuwataja hata zaidi ya watatu kama alivyoulizwa na anaweza kupata ugumu kupata hao watatu tu. Kama mteja ni mwanaume, mara nyingi kunakuwa na ukimya kabla ya kujibu na kisha kufuatishwa na swali, "Una maanisha nini unaposema marafiki wa karibu?"

> **Wanaume wengi ni mahodari katika kujenga uhusiano. Hufurahia kuwa pamoja kutazama michezo, kuwinda au kuvua. Lakini je ni marafiki wa karibu? (WOLGEMUTH, 1996).**

Kutokana na namna walivyolelewa wanaume wengi, urembo si kipaumbele katika maisha yao. Wanawake mara kwa mara hukuzwa wakizingatia urembo zaidi ya uwezo wa kiuchumi. Mwanamke huelezwa kwamba anatakiwa kuvutia kumpata mwanaume atakayempatia majukumu ya kifamilia.

Gur na wenzake, (1999) wameonyesha kuwa ubongo hupata joto la juu, kusambaza damu zaidi na kuwa na nguvu za ujumla. Wavulana hubalehe mapema kuliko wasichana (huzungumza na kujongea kwa furaha katika umri mdogo). Ubongo wa wanawake na wanaume huonekana kukua kwa taratibu tofauti pamoja na kuwa hakuna anayeweza kujua sababu. Tofauti hizi si za kudumu, kwani tofauti huongezeka au kupungua kulingana na umri. Msichana mdogo anaweza kutumia maneno kirahisi zaidi kuliko mvulana mdogo, japokuwa miaka ya baadaye wanaweza kufanana.

Tafiti za picha za neva za fahamu huonyesha kwamba tofauti ya kibaiolojia inaweza kukisia aina fulani ya tabia. Wanaume wana tabia ya kugoma kwa vitendo wakati wanawake wakifanya hivyo kwa maneno na hivi ndivyo namna watu huwa na tabia tofauti. Hata hivyo, kupata

tofauti za waziwazi kunaweza kutusaidia kujua utamaduni kama ilivyo baiolojia. Kimsingi bongo zetu zinafanana, hata kama tutazitumia tofauti. Kama tutakuwa na bongo mbili kwa wakati mmoja, tutaona kuwa hata kimaumbo zinafanana na itatulazimu kutumia mbinu za ziada kuzitofautisha. Tofauti zake ni ndogo sana na ni zaidi ya fumbo, kuweza kusema kuwa bongo hizo mbili ni tofauti. Ingawa watu wanaweza kufanya mambo kwa namna tofauti, bado mfumo wa tabia kati ya mwanaume na mwanamke unafanana.

Uhusiano wa kihisia

Uhusiano wa kihisia umekuwa ndio jambo la ubaguzi au kasumba inayozungumzwa sana: wanawake hutafuta namna ya kusisitiza wakati wanaume wakiyakimbia. Wanawake huzungumzia hisia zao wakati wanaume hubadili mada kwenda kwenye mpira wa miguu, wanawake huweza kueleza hisia zao kwa marafiki zao wakati wanaume huchukulia kama kulitoa jambo binafsi kwa watu. Je ni dhana tu? Na kama ndivyo, dhana hii ilianzia wapi?

Matokeo ya kihisia yanayotokea katika ukuaji wa mtoto yanaelezwa kwamba hayatokani na mafunzo au kuiga tabia katika jamii. Katika jaribio ambalo lilihusisha kusikiliza sauti za watoto wakilia, wanyama wakiita, na sauti ya ajabu ya nyuki dume iliyotengenezwa kwa kompyuta – watoto walitambua kiurahisi sauti za binadamu mwingine na kuhuzunishwa nayo. (Cassidy, 1999). Hata hivyo, ni watoto wachanga wa kike waliguswa sana na sauti inayoonesha mtu akiwa kwenye tabu, tabia ambayo huendelea katika maisha yao, kwa kuwa hata katika siku ya kwanza tu watoto



wa kike huonesha huruma. Wanawake wanaweza kuwa wepesi sana kueleza namna gani wanaweza kuhisi pale mtu mwingine anapoumizwa. Kwa muda mrefu, wanawake wamekuwa katika mstari wa mbele kutoa msaada – ulinzi wa mwanzo kabisa anaokuwa nao mtoto mchanga dhidi ya ulimwengu ambao hutazama mahitaji ya wengine.

Hisia

Haishangazi kwamba wanawake ni wazuri sana kwa kutambua hisia. Uwezo wa kunusa kwa wanawake ni zaidi ya ule wa wanaume hasa wakati wa kupevuka na kwamba wanawake wana hisia kali zaidi za kuguswa kuliko wanaume. Uwezo wa kuwasiliana kwa kugusa ni muhimu sana kwa afya ya mtoto. Watoto waliozaliwa kabla ya wakati wakibebwa na hata wakipigwapigwa kidogo, hukua na kukomaa kwa haraka. Hupata uzito kwa asilimia 47 haraka zaidi kuliko wale wanaoachwa wenyewe, hata kama wote watapata chakula kwa kiwango sawa. (Dodd, 2005).

Sauti za akina mama zinarandana na hisia na mahitaji ya watoto. Kwa kucheza sauti za mwanamke zilizorekodiwa kwa watoto, sauti hizo hufuatwa zaidi kuliko kucheza sauti hizo kwa watu wazima. Pia, moyo wa kichanga hutulia, kujiliwaza na kuwa madhubuti na pia kupiga taratibu pindi asikiapo ladha ya sauti ya mama yake. Raha anayoipata mtoto kutoka kwa mama yake akiwa tumboni, humfanya mtoto kuwa sawasawa kimwili na kuendelea na kukua vyema. Ni katika uhusiano huu kati ya mama na mtoto ndipo tofauti za kihisia kati ya mwanamke na mwanaume zinapoanzia.

Hadhi

Wazo la hadhi kwa mvulana huanza kutokea mapema sana. Haitokei mapema sana kwa wasichana. Kiujumla, wasichana huwa hawazingatii kuongoza isipokuwa kwa baadhi ya mambo tu. Utafiti mwingine wa mchezo wa watoto, unaonyesha namna gani watoto wa jinsia moja walipocheza mchezo wa “daktari”. Wavulana wote walitaka kuwa daktari-atakayewajibika kuwaongoza wengine. Wanaweza kubishana kwa muda mrefu kabla ya kumpata huyo daktari. Hali ni tofauti kwa wasichana kwani huulizana nani miongoni mwao anataka kuwa daktari. Kisha hukubaliana, kugawana majukumu ya daktari, nesi na mgonjwa.

Wavulana ni tofauti na wasichana hupenda michezo yenye washindi wa ukweli. Pia huonekana kufurahia kwa kukabiliana, matokeo ya michezo husika. Michezo ya wasichana huwa mifupi ikilinganishwa na ile ya wavulana. Wavulana hujadiliana au pengine kubishana kuhusu michezo yao, kuhusu nani alifanya nini, nani alikuwa na nini na michezo yao haishii katika kubishana. Hata hivyo, wasichana kwa upande wao lawama na migogoro ndio huwa mwisho wa michezo yao. Wavulana hukubaliana kutokubaliana kirahisi kuliko wafanyavyo wasichana; kwa kuwa wasichana wana hisia kali katika migogoro. Wengine huelezea hali hii kuwa hutokana na utamaduni,

kwamba tunawafanya wasichana kuwa na hisia zaidi na kupunguza hisia hizo kwa wavulana.

Hata hivyo, kwa jinsi tunavyojaribu kuwatenganisha, baiolojia na utamaduni haviwezi kutenganishwa hata kidogo. Maswali yetu kuhusu majukumu ya asili dhidi ya yale yapandikizwayo huunda mzunguko ambapo moja hushawishi jingine. Katika kitanzi hiki, baiolojia ni muhimu zaidi kwa kuanzia. Lakini swali ni kwamba unawezaje kujua mzunguko unaanzia wapi?

Lugha ya alama

Wanawake ni hodari sana kutafsiri lugha ya alama kuliko wanaume. Wanawake hutabasamu mara nyingi kuliko wanaume, ambapo pia wanaume huwahamasisha wanawake kutabasamu. Wapo wanaosema tabia hii hutokana na uhusiano wa unyenyekevu uliotawala toka enzi kuhusu jinsia. Wanawake pia ni hodari sana katika kusoma lugha isiyotumia maneno yaani lugha ya alama na mijongeo ya usoni.

Katika kujifunza picha za nyuso, jinsia zote zimekuwa zikifanya vizuri sana katika kutambua mtu anapokuwa na furaha. Wanawake pia huweza kugundua upesi huzuni usoni mwa mtu, ikiwa ni kwa mwanaume au mwanamke na kwa ufasaha wa asilimia 90. Wanaume kwa upande wao pia wanaweza kutambua huzuni kupitia uso wa mwanaume kwa asilimia 90 lakini ufasaha katika kutambua huzuni kwa uso wa mwanamke huwa asilimia 70 tu. Uso wa mwanamke unapaswa kuonekana hasa kuwa na huzuni ili mwanaume aweze kutambua huzuni hiyo sawasawa. Ikionyeshwa kwa kiasi kidogo, inakuwa vigumu kwa mwanaume kutambua huzuni hiyo.

Kasumba ya kuwabagua wasichana na wavulana

Baadhi ya watu hukosea kusoma ukweli wa maumbile yetu. Wimbo wa zamani wa shule ya awali unasema kwamba wasichana wameumbwa kwa “sukari, kiungo cha msisimko, na kila kitu kizuri” wakati wavulana ni “konokono na mikia ya mbwa wadogo”. Mvulana wa miaka mitano alichukizwa na dhana hii: kwanini wasichana wawe viumbe wazuri? Kwanini wavulana wachukuliwe kama wadudu wanaopatikana bustanini na viungo vilivyokatwa vya mbwa?

Tafiti zingine zinasema kwamba wavulana huhitaji umakini wa kutazama kwa karibu, kwa kuwa upendo huwabadilisha

Ulishawahi kushangaa kwanini sura za Qur'an zinaanza na "Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu"? Je unaona dondoo yoyote kwa wazazi kuwa na mapenzi kwa watoto wao?

viwango vya homoni zao za kijinsi katika bongo zao. Tafiti nyingi zilizofanywa juu ya wanaume na wanawake zinaonyesha kwamba wanaweza kuishi vema hata wakisumbuliwa na maradhi makali kama vile; ugonjwa wa moyo na saratani kama kuna ndoa yenye upendo. Kila ugomvi ndani ya ndoa hutuma mitetemo katika mfumo wa kinga, na hii huwa na madhara kwa wahusika na huweza kupata maradhi ya mafua punde baada ya ugomvi huo. Mwanandoa mmoja anapofariki, mfumo wa kinga wa mjane hudhuriwa kwa muda kuanzia miezi minne hadi miezi kumi na minne.

Huzuni

Hakuna aliyewahi kuona kuwa upweke ni mzuri kwa afya, ikiwa ni afya ya kimwili au kiakili. Wanawake hudhibiti huzuni tofauti na wanaume. Hii inaweza kuelezea kwanini waume na wake huhimili kupotea kwa mtoto katika hali tofauti (mume mara nyingi hukata tamaa wakati mke hutaka msaada kwa kila mtu). Hata hivyo, hatuwezi kusema kwamba kila mwanamke huonesha hisia zake kirahisi au si kwamba kila mwanaume huwa mgumu kuonyesha hisia zake. Kuna mahali ambapo sayansi haiwezi kuonyesha vitu vyote vinavyotuhusu.

Tofauti za kijinsi

Baadhi ya wake waliulizwa: "Kama ungeelezwa kuwa hutaweza tena kushiriki tendo la ndoa na mumeo, ungejisikiaje?", wengi wao walijibu kwamba haitawasumbua sana, wao wanahitaji kukumbatiwa na

kupata busu tu. Hata hivyo, wanaume walipoulizwa swali hilo hilo, walisema watajisikia vibaya. (Fisher, na wenzake, 2012.)

Katika mahusiano ya kijinsi, wanawake huwa imara zaidi kuliko wanaume. Wanawake wanaweza kuvumilia kutoshiriki tendo la ndoa kwa muda mrefu na huhitaji kuguswa ili wapate msisimko. Wanaume kwa upande wao, wana wakati mgumu kuvumilia kutoshiriki tendo la ndoa kwa muda mrefu. Neno moja tu huweza kumsisimua mwanaume kwa tendo la ndoa. Wanawake wanaweza kushiriki tendo la ndoa bila kusisimka tofauti na wanaume ambao huhitaji kusisimka kwanza.

Mtu mzima Marekani huweza kuwaza kufanya tendo la ndoa kila baada ya dakika chache.Wanaume wanapaswa kuhifadhi macho yao kwa kuwa wao ni dhaifu katika kudhibiti matamanio ya tendo la ndoa. Kujamiiana ni tendo muhimu sana na watoto ni matokeo yake. Kudhibiti mahusiano ya kimapenzi ni muhimu kwa jamii bora, kijamii, kiafya, kimaadili, kisaikolojia na kijamii.

Busara ya tofauti za kijinsia: Majukumu, si kwa upendeleo

Mwanamke ameumbwa na kufundishwa kuwa na hisia zaidi ili aweze kuwalinda watoto wake dhidi ya tishio lolote. Hii pia inaonekana kwa wanyama wengine. Mama paka kwa mfano huwalinda watoto wake na kuwaficha mbele ya madume ya paka, akiwemo baba yao, kwani bila hivyo wanaweza kuwatafuna kama panya. Homoni maalumu huzalishwa wakati wa ujauzito ambao husaidia wakati

wa kujifungua, kunyonyesha na katika kuwalinda watoto wake.

Ni Katika kipindi cha hedhi, ujauzito, kujifungua na kunyonyesha wanawake huhitaji sana kusaidiwa. Hivyo umakini katika kuwapa huduma unapaswa kuzidishwa katika nyakati hizo. Mamilioni ya wanawake hulalamika kutojisikia vema wakati wa siku zao za hedhi. Matatizo yanaweza kujitokeza na kuchukua muda wa siku kadhaa na kutoka katika hali ndogo kwenda kuwa tatizo kubwa. Miongoni mwa dalili za tatizo ni pamoja na; kuvimba, kukakamaa, matiti kulainika, maumivu ya kichwa, kutokwa na damu kwa wingi au kwa muda mrefu, kubadilika-badilika kwa mawazo pamoja na uchovu.

Mwanaume huvutiwa kimapenzi na mwanamke ili aweze kubeba majukumu ya kumhudumia yeye na watoto wake. Anapaswa kuwa mkarimu katika

kumpatia mkewe na watoto wao mahitaji yote wakati kwa upande wa mwanamke atakuwa akihusika zaidi na kujihudumia yeye na watoto wake. Mwanaume hakupewa majukumu ya vipindi vya hedhi kila mwezi, ujauzito, kujifungua na kunyonyesha. Hivyo ameachwa ili atafute mahitaji kwa ajili ya familia yake.

Tofauti za kiujumla katika maumbile ya asili ya wanaume na wanawake zinaelezea Sheria na miongozo ya kifamilia za Kiislamu. Asili tofauti za kijinsi kati ya wanaume na wanawake zinaelezwa katika dhana ya *'awrah* – sehemu za siri za wanaume na wanawake. Uchi wa mwanaume unaelezwa kuwa ni kati ya kitovu na magoti kwa hiyo ni muhimu kujisitiri maeneo hayo wakati anafanya kazi zinazohitaji nguvu. Wakati huo huo sehemu za mwili wake zinazoachwa wazi haziwezi kumshawishi moja kwa moja kutamaniwa na mwanamke au kumfanya mwanamke ashindwe kujizuia na matamanio ya kimapenzi.

Kinyume chake ni sawasawa kwa mwanamke. Karibu sehemu zote za mwili wa mwanamke ni kivutio kwa mwanaume kumtamani. Wanaume wanashawishika kirahisi kwa maumbile ya mwanamke, hivyo mwili wake wote unaelezwa kuwa ni uchi isipokuwa uso, vitanga vya mikono na miguu. Kwa msingi huo hakuna haja kwa mwanamke kuonesha mwili wake kwa wanaume. Uso wake ni tofauti, kwa hiyo una kazi nyingine pia kama kuonesha haiba yake na utambulisho wake. Hayo yote yanaelezea taarifa za msingi juu ya dhana pana ya *"awra"*kama jambo muhimu na imara la stara ya familia na sera ya kinga madhubuti dhidi ya uasherati, ambao huharibu familia na jamii kwa ujumla.

Hata hivyo, katika mahusiano ya mume na mke hakuna kiungo kilichokatazwa kuonekana kama inavyoelezwa katika Qur'an:

> *…Wao ni vazi kwenu, na nyinyi ni vazi kwao...*
>
> (Qur'an 2: 187).

Kama walivyo wanajamii wengine, wanaume na wanawake wana sifa na haki zinazofanana lakini wanatofautiana kwa ujumla kutokana na majukumu yao kutokana na tofauti zao za kisaikolojia na kimwili. Familia ni taasisi maalumu ya kibinadamu inayofanya kazi vema na kutoa faida kwa wanaume, wanawake na watoto.

Wanawake wenye umri kuanzia miaka 20 hadi 40 ni msingi wa familia. Ni watulivu na walezi wazuri ili waweze kuzipatia familia zao amani na utulivu. Mume anahitaji utulivu, hasa arejeapo nyumbani kutoka katika mikikimikiki ya siku ya kutafuta riziki. Utulivu ni kipaumbele cha asili katika umri huo. Hata hivyo,

hii haimaanishi kuwa wake hawawezi kufanya mambo mengine mengi au kwamba waume wanasamehewa katika majukumu yao ya kuhakikisha kuna amani ndani ya nyumba zao. Sifa hizi zisitafsiriwe kama udhaifu wa wanawake na ukatili wa wanaume. Lakini zinasawiri kwa kila jukumu kwa kila mmoja. Sheria ya Kiislamu inampa majukumu kisheria ya kutafuta riziki mwanamke bila kujali hali yake kiuchumi, kwa sababu suala ni majukumu na maandalizi kwa ajili ya majukumu hayo. Uamuzi kama mke atoke nje kufanya kazi ni yake mwenyewe. Hapaswi kulazimishwa kufanya kazi, kwa kuwa mahitaji yake na watoto wake ni jukumu la moja kwa moja la mume wake. Ikiwa mke atachagua kwenda kufanya kazi, hakuna tatizo katika hili. Kama anaweza kutekeleza majukumu yake yote kama mama nyumbani na majukumu ya kikazi basi anayo haki ya kutafuta riziki na kuwa mama.

Tofauti za kimaumbile na kisaikolojia kati ya jinsi wakati wa hatua mbalimbali za maendeleo hazipunguzi haki na majukumu yao. Sifa fulani, kama sauti nyororo, inaweza kuwa kivutio kwa mwanamke lakini isivutie kwa mwanaume na hali kadhalika kwa upande wa pili.

Kiislamu haikubaliki mwanaume kumtazama mwanamke kwa matamanio. Kama mwanamke amevutiwa na mwanaume, madhara ni kwa mwanamke, ikiwa atatenda dhambi, basi ni madhara makubwa zaidi kwake kwa kuwa anaweza kupata ujauzito. Inapaswa mume awajibike kumuhudumia mkewe na kukaa naye. Mume analazimika kumsaidia mkewe na mtoto. Ikiwa atashindwa majukumu yake hayo, atakuwa amewanyima haki zao za msingi walizopewa na Mwenyezi Mungu.

Vipaumbele vya Wanaume na Wanawake wa Kimarekani: Utafiti

Utafiti uliofanywa na gazeti la *Washington Post* na Chuo Kikuu cha Harvard, uliohusisha wanaume na wanawake elfu moja, ulihitimisha kuwa vipaumbele vya wanaume na wanawake nchini Marekani ni kama ifuatavyo:

- Kupambana na misukumo ya kisaikolojia na kiuchumi katika maisha ya kisasa.
- Kuimarisha mahusiano ya kifamilia.
- Kuwasiliana na watoto ipasavyo.

Siku hizi, kwa bahati mbaya, wanawake katika nchi za Magharibi na hata nchi za Kiislamu wamekuwa wakiingizwa

katika majukumu makubwa. Mbali na harakati za kiuchumi, wanawake katika nchi za Magharibi wanatarajiwa kutoka kwenda kufanya kazi na watachukuliwa kama chombo cha kutumia katika matamanio yao ya kimwili, burudani chee, na chombo cha biashara. Katika baadhi ya nchi za Kiislamu, wanawake hawapewi fursa ya kusoma na kutoandaliwa vema katika majukumu makubwa ya malezi ya familia. Wengi wao hawajiamini, hutegemea hekima za waume zao na katika nchi nyingi hubaguliwa na kunyanyapaliwa.

Marehemu Sheikh Muhammad al-Ghazali anasema katika kumbukumbu zake kwamba katika kipindi cha utoto wake huko kijijini kwao, wanawake waliweza kuonekana sehemu zote, isipokuwa msikitini.

Inasikitisha kuona kwamba katika nchi nyingine hakuna sehemu ya wanawake katika misikiti. Wanafunzi wengi wa elimu ya dini nchini Uturuki sasa ni wanawake. Hata hivyo wataalamu wa ujenzi hawakutilia maanani kuhusu nafasi ya kufanya ibada kwa wanawake. Hivyo, katika mji wa Istanmbul, sehemu ya eneo kuu la kuswalia limewekwa kwa ajili ya wanawake na hata kujengewa msikiti mahali tofauti kwa ajili ya swala za jamaa. (MURAD, 2009). Tunatarajiaje akina mama kuwalea watoto bila kuwa na mwongozo thabiti wa dini na elimu inayotolewa kila juma katika hotuba za Swala ya Ijumaa ambazo ni elimu muhimu sana itolewayo na taasisi hiyo? Wanawake wamekuwa wakinyimwa haki yao hii ya msingi tangu enzi, pamoja na Hadithi ya Mtume (s.a.w.) inayosisitiza kuwa:

Mtume (S.A.W.) alisema:

Msiwakataze watumishi wa kike wa Allah kwenda katika Misikiti ya Allah.
(MUSLIM).



Wanawake wanaotekeleza majukumu yao na zaidi katika familia zao wameruhusiwa kusali msikitini au nyumbani kutokana na majukumu yao hayo. Hakika, ni majukumu ya waume kuhakikisha wake zao wanafika misikitini kwa kuwasaidia katika kazi zao.

Wakati wanaume wakiwaruhusu wake zao kufanya kazi nje na nyumbani, wanaume wengi wanapenda kina mama wanaotumia muda wao wote kwa kuwahudumia watoto na nyumba. Wengi wanaamini kuwa sababu kubwa ya wanawake wa Kimarekani kufanya kazi ni kutafuta kipato zaidi kutosheleza mahitaji katika maisha, (al-Usra, Toleo 61, 1419 H.).

Miaka Kumi na Sita, umechelewa

Shairi la Kiarabu lilisema:

Je unamlilia binti yako Lubna,
baada ya kumshambulia?
Lubna ameondoka, sasa utafanyaje?

Wazazi wengine huwanyanyasa mara kwa mara watoto wao na kisha kujutia vitendo vyao. Huruma hiyo inaweza kuwa imechelewa kwa miaka 16!

Utengano wa kijinsia unaanzia wapi?

Watoto wengi wanaanza kuingia kwenye tofauti za kijinsia mwaka mmoja baada ya kuzaliwa. (Beal, 1993). Wakishafikia umri wa miaka miwili au mitatu, wanakuwa wameshatambua sifa zao kutokana na jinsi zao. Kwahiyo watoto wa miaka mitatu wanakuwa wamefanya utafiti kuhusu miili yao kwa miaka miwili. Kimtazamo wa kijinsi, watoto huuona ulimwengu katika makundi mawili. Pindi wajuapo jinsi yao, haraka sana hujitambua kama mvulana au msichana na hivyo kuanza kujifunza tabia za jinsi hiyo. Kufikia umri wa miaka mitatu, tabia ya mtoto hujulikana kutokana na kuwa mvulana au msichana. Wasichana huweza kuwa wapole na kuamua kucheza michezo ya "kisichana" kama mama wa nyumbani. Wavulana wao huweza kuwa wakorofi na kutopea katika kucheza michezo ya "kivulana" kama vigari na kuiga matukio ya kishujaa.

Utambuzi wa jinsi hutokana na msukumo wa tezi mwilini, hasa kutoka katika kubalehe na kuendelea na sehemu nyingine hutokana na utambuzi wa tofauti za kimaumbile mapema wakati wa utoto na mapokeo ya kisaikolojia kutokana na utambuzi huo. Kwa ujumla, utambuzi wa kijinsi hutokana na kujitambulisha kwa mambo mazuri yanayotokana na mzazi wa jinsi hiyo. Kwa wanaume wenye sifa za kike na wanawake wenye sifa za kiume, tatizo huenda likatokana na mahusiano yasiyo mazuri na wazazi, pamoja na kuwa na tezi za kawaida.

Kitu kinachomhakikishia mvulana kuwa yeye ni mvulana ni kupenda, kupendwa na kuiga tabia za baba ambaye hufurahia

kuwa mwanaume. Baba anahitaji kujiona kuwa anatosha katika mahusiano ya kiushindani na wanaume wengine katika jamii. Utambulisho mzuri wa kijinsi kwa mwili unaokua hautegemei kama baba yake au wanaume katika jamii yake wanawinda simba au hujishughulisha na kupika chakula cha watoto nyumbani. Kwa kuwa baba hujisikia vema kuwa mwanaume na kuwa na uhusiano mzuri na mtoto wake wa kiume, utambuzi wa kijinsi utakuwa sawa na salama.

Baba ambaye huona hadhi yake kama mwanaume haiko sawa atamuambukiza mwanaye wa kiume tabia hiyo katika njia mbalimbali ndogo ndogo. Hii itaingilia mtoto huyo kujitambua na kuridhika na yeye kuwa mwanaume. Kukataa kwa baba kufanya kazi za nyumbani kama mwanamke kinyume na mazoea ya wanaume ni njia mojawapo ya kuonyesha kukata tamaa na jinsi yake hivyo kumuathiri mwanaye wa kiume.

Msichana anakuwa na kuhitaji kuwa mwanamke na kujiandaa kwa mafanikio, ikiwa ni pamoja na kupendwa na kuthibitishwa na mama yake anayefurahia majukumu ya mwanamke, kila kilicho katika utamaduni wake, ikiwa mama ni mkulima au mwanasiasa.

Hakuna mahitaji ya kuwalea wasichana na wavulana kwa kuwatambua. Nyumbani hakupaswi kuwa na aliye bora na aliye dhaifu. Pamoja na tofauti zao za kijinsi, kuwalea watoto ni kitendo cha kuvutia kama kufanya kazi ofisini, kiwandani au maisha ya kawaida ya kijamii.

Wavulana na wasichana wanapaswa kupewa huduma sawa lakini si katika kila kitu. Wavulana na wasichana wanapaswa kufundishwa kupambana na maisha, lakini wakiwa na uwezo wa kutimiza majukumu yao ipasavyo, bila wavulana kufundishwa kuwa watundu na kutoguswa haraka na hisia na wasichana hawapaswi kufundishwa kuwa wapole, na wanaohitaji msaada kutoka kwa wanaume. Wasichana wanapaswa kuelezwa kuepuka kuwa na mguso mkali wa hisia ambao hufikia kwenye kulia wasipopata wanachohitaji. Wavulana nao wanapaswa kukatazwa kuwa watundu sana na kufanya vurugu wasipopata wanachohitaji.

Kadiri inapowezekana, elimu ni muhimu kwa wasichana na wavulana mpaka watakapomaliza masomo yao. Wasichana na wavulana wanapaswa kupewa mwanasesere asiye na jinsi moja na vitu visivyoonesha kuwafundisha jinsi fulani. Mwanasesere hapaswi kuwa na sifa za mwanaume au mwanamke. Kuwapamba na kuwavisha wasichana hakupaswi kuzidishwa na pia kuwapamba na kuwavisha wavulana hakupaswi

kupunguzwa sana. Baba na mama wanapaswa kuwapa umuhimu katika kuwatengeneza nywele mabinti zao na watoto wao wa kiume. Dhana hiyohiyo inapaswa kutumika katika mavazi. Nguo hazipaswi kumzuia msichana kucheza na wenzake. Wazazi wakimvisha binti sketi na kisha kumkemea nguo yake ya ndani ikionekana, watakuwa hawamtendei haki. Wazazi wanapaswa kuwaruhusu mabinti zao kuvaa suruali safi, zisizobana ili kuwaruhusu waweze kushiriki michezo bila matatizo kama kaka zao. Msichana anapaswa kujifunza kucheza na kuthamini uwezo wake wa kimwili, kama kaka yake. Mtoto wa kiume anapaswa kufundishwa asimpige msichana, hata wakati wa kucheza. Msichana anapaswa pia kufundishwa kutomruhusu mvulana kumpiga na kama mvulana atafanya hivyo ajitahidi kujilinda mwenyewe na si tu kulia au kukimbia.

Jike-dume, dume-jike

Mtume (S.A.W.) alieleza kukarisishwa kwake dhidi ya wanaume wanaojifananisha na wanawake na wanawake wanaojifananisha na wanaume. (AL-BUKHARI).

Mwanaume ni mwanaume, mwanamke ni mwanamke, wote wanapaswa kushukuru kwa walivyo! Hawapaswi kujifananisha baina yao. Katika utamaduni wanamoishi, inapaswa kuwa rahisi kutambua tofauti kati ya wasichana na wavulana, japo siku hizi imekuwa si rahisi sana. Mwenyezi Mungu amewaumba wavulana na wasichana kuwa tofauti kwa kuwa kazi zao ni tofauti lakini zinaweza kujulishwa. Ni neema kuwa tofauti ili tuweze kuvutiana na kuwa na furaha zaidi. Hatupaswi kupuuza tofauti hizo zinazovutia za kimaumbile.

Tofauti za kijinsi haziwezi kushinda “vita” vya jinsia (maumbile). Kuna kufanana kukubwa na “adui”. Wanaharakati wa Kimagharibi wanaotetea haki za wanawake wameathirika na ushawishi wa utamaduni wa Kimagharibi. Miongoni mwao wanasema mwanamke ana sifa sawa na za mwanaume na kwamba anaweza kufanya kila kitu anachoweza kufanya mwanaume. Wengine wanaenda mbali zaidi wanasema, mwanamke hahitaji kuwa na mwanaume na kwamba mwanamke humuhitaji mwanaume kama samaki anavyoweza kuhitaji baiskeli. Kitu chochote kinachohitajika katika jamii, wanawake wanaweza kukifanya bila ya uwepo wa wanaume.

Mtazamo mkuu wa Kikristo unapinga maelezo hayo na kwani Yesu aliwaasa wanaume kutokuwa wapole na wenye huruma sana na kuwasisitiza kuchukua nafasi katika uongozi. “Mjinga yeyote anaweza kuwa mtu imara” lakini yamuhitaji mwanaume wa kweli kumtukuza na kumheshimu mwanamke. Wanaume wanaweza kufanya maamuzi ya kifamilia lakini baada ya kujadiliana kwa kina na wanawake. Waume lazima wawaheshimu wake zao, ambapo wanapaswa pia kuwatendea kwa heshima. Mwenyezi Mungu amemuumba mwanaume kuwa na sifa za kiume na mwanamke kuwa na sifa za kike, na hivyo wasichana wanapaswa wasifananishwe na wavulana katika majukumu yao. Qur’an inaelezea suala la jinsia kama ifuatavyo:

> *Wala msitamani alicho wafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wana fungu katika waliovichuma, na wanawake wana fungu katika waliovichuma. Na muombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.*
>
> (Qur’an 4:32).

UPEKEE WA WANAUME NA WANAWAKE



- Wanaume wapatao mia moja hutumika kutengeneza kambi lakini mwanamke mmoja hutosha kutengeneza nyumba. (Methali ya Kichina).
- Ni nani mwanadamu imara zaidi duniani? Aliuliza Mfalme Themistocles. “Wakazi wa Athens wanawatawala Wagiriki; Mimi nawatawala wakazi wa Athens; wewe, mke wangu, unanitawala mimi, mtoto wangu anamtawala mke wangu, mtoto anawatawala ninyi”.
- Hivi mwanaume anaweza kumuelewa sawasawa mwanamke? Na hivi mwanamke anaweza kumuelewa mwanaume?
- Hivi mwanaume anaweza kuelewa maumivu ya ujauzito na kujifungua? Si rahisi, lakini maumivu makali ya figo yanaweza kukaribia.
- Kama ungepewa fursa ya kuchagua kumfundisha mwanamke au mwanaume, ungemchagua yupi? Ukimfundisha mwanaume unamfundisha mwananchi, lakini ukimfundisha mwanamke, unalifundisha taifa!

Malezi kwa kutazama Jinsi

Siku hizi, malezi katika familia nyingi ni majukumu ya mama na baba anasaidia. Kutokuwepo kwa wazanifu baina ya wanaume na wanawake. Kwa Marekani kina baba wengi hutumia masaa saba kwa wiki na kina mama hutumia masaa 14 kwa wiki katika malezi ya watoto. Kwa nyongeza kina mama hutumia masaa 18 kwa wiki

kufanya kazi za nyumbani na masaa 21 katika kazi kazi ya kuajiriwa , wakati kina baba hutumia masaa 10 kwa wiki kwa kufanya kazi za nyumbani na masaa 37 katika kazi ya kuajiriwa. (kutoka kituo cha utafiti – pew research centre 2013) kwa hesabu isiyo rasmi asilimia 60 ya kaya zenye watoto wenye umri chini ya miaka 18 wana wazazi wawili waliokatika ajira. Katika kaya hizo ambazo wazazi wa kiume hutumia masaa mengi katika ajira zao, na wazazi wa kike hushughulikia nyumba na uangalizi wa watoto. Ingawa katika kaya hizo ambazo kina mama waweza kuwa wanafanya kazi za kuajiriwa kama kina baba lakini bado wameonekana wakitumia muda mwingi kwenye suala la ulezi. Katika chapisho juu ya mahusiano ya kifamilia la mwezi Disemba 2013, lililoangazia juu ya baba na mama ambao wako katika kikwazo cha kazi zinazofanana yaligundulika mambo yafuatayo:

- Pindi watoto wanapokuwa na umri wa miezi 9, mama hutumia asilimia 70 ya muda wao wa kazi kufanya uangalizi wa mtoto, ukilinganisha na asilimia 50 wanayotumia kina baba.
- Kina mama hutumia mara mbili ya muda wao wa ulezi katika shughuli za kila siku za malezi (kuogesha , kulisha, kuvisha nepi) kuliko wanavyofanya kina baba, hata baada ya kuacha kunyonya japokuwa kwa kuwarusharusha na kuwabembeleza.
- Baba hujishughulisha na kutoa msaada kuliko jukumu la msingi la ulezi.

(Kutoka Chuo Kikuu Cha Ohio 2013)

Kazi na majukumu ya kulea mtoto katika karne ya ishirini na moja hazifanywi tena kwa kutazama jinsi lakini kwa upatikanaji na ukaribu wa huduma husika, na kwamba zinafanana na au kuwa sawa na kazi inayojitokeza. Kubadilishwa kwa nepi ya mtoto “hutambuliwa na yule anayenusa harufu yake kwanza” na si “Baba yangu ambaye huwa hafanyi hivyo, kwanini nifanye hivyo? kujilinda kwa zamani.

Kwa kutumia taarifa (*data*) za mwaka 1965 na 2011 shirika la PEW lilitoa taarifa mwaka 2013 kina baba walikuwa wakifanya sana kazi za nyumbani na uangalizi wa watoto tangu mwaka 1965, wakati kina mama wakitumia muda mwingi katika shughuli za kuajiriwa. Majukumu yao ingawa yamebadilika. Katika mwaka 2012, asilimia 64 ya akina mama wamekuwa wakifanya kazi katika nchi ya Uingereza na asilimia 29 wamekuwa wakifanya kazi muda wote (full time)(Idara ya elimu).

Kwanini Hakuna Usawa?

SABABU ZA KINA MAMA KUJIHUSISHA ZAIDI NA MALEZI YA WATOTO

- Wanawake hawahitaji purukushani au migogoro.
- Wanawake wanasukumwa zaidi katika malezi kwa sababu ya namna wanavyotazamwa na jamii kutokana na asili za maumbile yao.
- Kwa kuwa bado jamii inawapa wanawake majukumu ya msingi wakati mtoto anapopatwa na tatizo, wanawake wengi hawako tayari kuyaacha majukumu haya.
- Wanawake wengi hupata kigugumizi kugawana majukumu na mapenzi ya watoto wao, au hawataki namna wenzi wao wanavyoyasimamia majukumu hayo.

SABABU ZA USHIRIKI MDOGO WA WANAUME KATIKA MALEZI YA WATOTO

- Nahofia kitu kibaya kinaweza kutokea nikiwa katika majukumu
- Sitaweza kumpatia mtoto mahitaji yake na huenda nikakasirika
- Mama yao ni hodari katika malezi na mimi kamwe siyawezi majukumu hayo
- Kama nikitumia muda mwingi na watoto, nitapoteza fursa ya kupandishwa cheo kazini kutokana na kukosa muda
- Wanawake wana nafasi ndogo kuhudhuria mafunzo yanayohusu kuwalea au maendeleo ya watoto
- Wanawake wana mifano mizuri ya malezi
- Wanaume hawana msaada wa mfumo katika majukumu ya malezi
- Baadhi ya kina mama hurudisha nyuma ushiriki wa kina baba katika malezi. Hata hivyo, kizazi cha sasa cha kina baba kinatumia muda mwingi katika malezi ya watoto kuliko walivyofanya baba zao, kwahiyo inaonekana kuna mabadiliko katika tabia.

DHANA POTOFU NA UKWELI KUHUSU KINA BABA KAMA WALEZI WA WATOTO

DHANA POTOFU	UKWELI
Wanawake mara zote ni hodari katika malezi.	Watoto hufuata namna wanavyolelewa na kina baba kama ilivyo kwa kina mama.
Wakati wa miaka michache ya kwanza, kina baba si muhimu kwa watoto zao, na kwamba wanapaswa kuhusiana nao pale wanapokuwa wakubwa.	Kina baba huguswa na watoto wachanga kama ilivyo kwa kina mama.
Jukumu muhimu sana la baba ni kusimamia maadili.	Kina baba hutumia muda mwingi zaidi kushiriki michezo, kwa hisia, na kutumia sehemu kubwa ya muda wao kucheza pamoja (asilimia 40 ya kina baba kuliko asilimia 25 ya kina mama. (Parke, 1996; Yogma, 1981)
Kwa kuwa baba ni mtafutaji, hapaswi kutumia muda mwingi na watoto.	Kina baba wanamudu vema malezi; watoto waliopata muda wote wa malezi kutoka kwa baba zao wameonekana kufanya vizuri zaidi katika jaribio
Watoto wanapaswa kuwa karibu na mama zao wakati wote ili waweze kuwa na afya njema.	Namna ya malezi yatokayo kwa baba huwa na ushawishi katika kufuata tabia za jamii. Kina baba wanaotumia upendo, kuwa wa kiasi, na namna imara katika kudhibiti tabia, hutengeneza watoto wenye uwezo mkubwa. Lakini kina baba ambao hawatumii upendo, na njia ya kutoa adhabu na kutoa amri, huandaa watoto ambao hawajiamini, kuwa na aibu na kuwa na woga.
Kama kijana wa kiume sina uhusiano wa karibu na baba yangu, nimekua kwa namna hiyo, hivyo sihitaji uhusiano wa karibu na kijana wangu wa kiume. Siwezi kulaumiwa kwa tabia yangu hii kwa kuwa hivyo ndivyo baba yangu alivyonilea.	Mara zote tunawajibika na vitendo vyetu. Kama wazazi wetu hawakuwa mifano mizuri katika malezi, tunapaswa kutafuta mifano mizuri ya kuiga.
Kufanikiwa kwangu katika kazi yangu ni kitu cha muhimu sana ninachoweza kukifanya kumsaidia mwanangu.	Mafanikio ya familia ni muhimu kuliko kazi.

Madhara wayapatayo watoto kwa kutokuwepo Baba zao

Tafiti mbalimbali zinaonyesha uhusiano baina ya kukosekana kwa akina baba katika kuwatunza watoto wao na tabia mbaya za watoto hao kama ifuatavyo:

1. Matumizi ya dawa za kulevya na pombe.
2. Ongezeko kubwa la vurugu kwa wanaume.
3. Wavulana kuwa na "tabia ya kiume zilizo-pitiliza" ambazo hazitokani na kuwaiga wanaume.
4. Tabia ya uhalifu.
5. Huwa wagumu kuvumilia kurejea nyum-bani wazazi wanapoachana na kurudiana.
6. Hawathamini hisia na mahitaji ya wengine.
7. Kushuka kwa maendeleo yao ya kimasomo na kuacha shule.

Mahitaji Tofauti ya Wavulana na Wasichana

Hakuna ajuaye hasa kama ni asili au malezi yanayowafanya wavulana na wasichana kuwa na mahitaji tofauti. Hata hivyo, wazazi huweza kuchangia nafasi kubwa katika kuwasaidia watoto wao katika mahitaji yao. Katika baadhi ya jamii, majukumu ya kijinsia na tabia zinazoambatana nazo hufafanuliwa wazi wazi, hasa katika jamii ya kimaskini sana. Yeyote anayekiuka taratibu hizi huadhibiwa.

ZIFUATAZO NI DONDOO ZINAZOWAHAMASISHA WAVULANA NA WASICHANA KUTEKELEZA WAJIBU WAO (IMECHUKULIWA KUTOKA KWA FRIEDMAN, 1998)

Mahitaji ya Msichana Mdogo

Kujiamini: Wasichana wanahitaji kuhamasishwa na maneno yanayoelezea tabia ambazo wazazi wao wanataka awe nazo. "Una akili sana wewe kupanda ngazi zote peke yako." Ni muhimu wasichana wakajua kuwa wazazi wao wanawaamini na kwamba wasichana hao ni wenye akili na wana uwezo. Wasichana wanapaswa kupatiwa fursa zaidi kuwa viongozi, kwa mfano kwa kuwapa fursa ya kuchagua kazi, kuweka miongozo, na kutatua migogoro. Msichana aliyejifunza uongozi huwa anaandaliwa vema kuwajibika katika masuala ya elimu na fani inayomuhusu.

Kujitosheleza: Ni vema wasichana wadogo wakajisikia ni hodari kwa kuwaruhusu wamalize chochote wakifanyacho wao wenyewe, kama vile; kubeba bilauri ya juisi, kuchana nywele zao, au kutengeneza mfano wa jengo refu bila msaada. Wasichana

wanapaswa kukumbushwa kwamba wanawake wengi wanaweza kufanya kazi za kupata ujira kwa sehemu kubwa ya maisha yao na hivyo kila msichana anapaswa kujiandaa kwa majukumu hayo. Wazazi wanaweza kutolea mifano ya wanawake wa kuigwa katika jamii ambao wameweza kufanya kazi za kulipwa, za kujitolea na bila kusahau maisha ya nyumbani.

Uhusiano wa mahali na uratibu: Wasichana wanapaswa kupewa aina mbalimbali za wanasesere wa kuchezea, ikiwa ni pamoja na; magari, matofali ya kujengea, mashine za kuchezea maji, aina mbalimbali za mipira, na vitu ambavyo wanaweza kuviendesha au kuvipanda.

Uimara kimwili: Wazazi wanaweza kucheza na watoto wao michezo kama; kutambaa na mieleka. Hata wasichana ambao bado wadogo sana wanaweza kupata faida ya kuupima uwanja, maeneo yanayotumika katika mashindano ya kukimbia na kuruka sarakasi. Wazazi wajiepushe na kumtenga katika michezo hiyo na badala yake wanaweza kumuhamasisha kujichafua na kutokwa na jasho katika michezo hiyo na kumsaidia kujisikia kuwa mwenye furaha. Pia anapaswa kuhamasishwa kuchezea udongo na maeneo mengine ya nje yatumikayo kwa michezo.

Ujuzi wa kufanya maamuzi: Wazazi wanapaswa kumuacha binti yao mdogo afanye maamuzi kwa mambo yanayomuhusu na kuwajibika kwayo. Kama mtoto mdogo, anaweza kuambiwa achague sahani au kikombe gani anataka atumie wakati wa chakula na rafiki yupi angependa kumualika ili acheze naye.

Udadisi: Wasichana wanapaswa kupewa fursa ya kutosha ya kuyafahamu mazingira waishiyo. Wanapokuwa bado wasichana wadogo, mazingira ya nyumbani yanapaswa kuwa salama ili watoto waweze kuwa na uhuru wa kuzunguka wawezavyo ndani ya nyumba. Pia, wazazi wanaweza kutoka naye nje ya nyumba – katika maeneo mbalimbali ili aweze kutambua mambo mbalimbali, mfano; maktaba, hifadhi ya wanyama, duka kubwa, duka la mtaa na maeneo ya ibada, bustani mbalimbali, mahakamani na vituo vingine muhimu kwa kujifunzia.

Taswira ya mwili: Wazazi wanapaswa kutazama sana katika mafanikio na sio umbo la mwili wa mtoto. Ni vema wazazi wamueleze binti yao kuhusu kitu gani anachoweza kukifanya vizuri kuliko urembo wake. Kwa mfano wanaweza kusema, “Umefanya kazi kubwa” badala ya kumwambia, “Umependeza sana leo.”

Uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu: Kama watoto wanatazama televisheni na filamu, wazazi wanaweza kuwafundisha namna ya kufanya hivyo kwa kufanya upembuzi yakinifu. Wanaweza kujadili na binti yao kuhusu walichokiona pamoja na kutazama kazi za kawaida za kipindi au filamu hiyo. Kwa mfano, mzazi anaweza kuanza na taswira ya mwili. Atazame wasichana wanavyooneshwa katika televisheni: Je wasichana wenye maumbile makubwa wanaonyeshwa kama sio maarufu? Je, wanatumika katika vichekesho? Je, wasichana wenye maumbile ya kuvutia wanaoneshwa tu kama burudani kwa wanaume? Je, huonekana kama warembo?

Uwezo wa kumudu hisabati na masomo ya Sayansi: Wasichana wanapaswa kupewa kila fursa katika masomo ya sayansi, hisabati na teknolojia. Ingawa wasichana wako tayari, wana matarajio na hamu ya kuutambua ulimwengu, mara nyingi hawapati fursa ya kutosha au hamasa katika kutekeleza hayo.

Kuwa mfano: Kwa kujiheshimu wenyewe na wanawake wengine, kina mama, kina shangazi na ndugu wengine wa kike, wasichana huweza kupata mfano wa kuiga. Na hivyo, wanaweza kukumbana na kasumba zilizopo katika jamii hiyo ambazo huwahamasisha wasichana kuwa "sukari na viungo na kila kitu kizuri."

Mahitaji ya Mvulana Mdogo

Mfano wa mwanaume wa kuigwa: Wanaume wamekuwa wakiitazama jinsia katika maisha yao binafsi na ya kiweledi na kuacha mambo ya utambulisho, usawa na jinsi. Katika wakati huu ambao akina baba wamekuwa adimu, ikiwa wavulana hawajifunzi kutoka kwa baba zao, ni dhahiri kwamba watajifunza kutoka katika tamaduni za kisasa (kama michezo na televisheni) kwamba uanaume unapambanuliwa kwa vitu vinne: *uwezo wa kujamiiana,ukakamavu, michezo, na umiliki wa vitu*. Kama walezi, wazazi wanaweza kufikiri upya uhusiano kati ya wanawake, wanaume, na wavulana. Wanaume wanapaswa kufanya mambo ambayo kiasili yanafanywa na wanawake kama vile: kutambua hisia, kutoa msaada wa kihisia, na kushughulikia sanaa ya mazungumzo. Ikiwa mvulana atakuja kwa baba yake na kusema kwamba mtoto mwingine amempiga, kisha baba anaweza kupata taswira ya namna gani mazungumzo yangekuwa kwa mfano huo baina ya binti na mama yake, na kutumia baadhi ya miongozo ya msingi katika mjadala.

Upendo wa kimaumbile: Wavulana wadogo huhitaji sana kukumbatiwa kama wahitajivyo wasichana wadogo, hivyo wazazi wanapaswa kumliwaza mtoto wao wa kiume anapolia. Pia wanapaswa kutumia muda kucheza naye na kuendelea na kumbembeleza kadiri atakavyoendelea kukua.

Mbinu za Mazungumzo: Wazazi wanapaswa kuzungumza na mtoto wao wa kiume mara kwa mara, hata angali mchanga. Sauti zao humpatia liwazo na kuhamasisha ukuaji wake wa lugha.

Kuwatambua Wengine: Ni vema wazazi wakamuelezea mtoto wao wa kiume kwamba matendo yake yanaweza kuwaathiri watu wengine. Mtoto wa kike akikosea, huambiwa kwamba atamkosea mtu mwingine, lakini watoto wa kiume huadhibiwa tu. Wanapoadhibiwa, watoto huzingatia zaidi namna wazazi wanapochukia kuliko kujifunza na kwamba tabia zao za ukaidi hutokana na wazazi wao au wenzao wanaocheza nao.

Mbinu za Usuluhishi wa Amani: Wavulana wanahitaji kupewa njia za kujenga katika kutatua migogoro. Kama watakuwa na tabia ya kuwapiga wenzao au kuwang'ata, kama wengi wanavyofanya wakiwa wadogo, wazazi wanapaswa kuelezea kuwa kupiga hakuvumiliki na kupendekeza njia nyingine katika kuonyesha hasira zao.

Kuwajibika kwa Matendo yake: Ni vema kuepuka upendeleo. Kama wazazi wataona tabia isiyokubalika kwa mtoto wao wa kike, kiwango hicho hicho kitumike kwa mtoto wao wa kiume. Hawawezi kutumia kisingizio cha "wavulana watakuwa wavulana" kusamehe utukutu wao.

Kuonyesha Hisia: Wavulana wanapaswa kuhamasishwa waeleze hisia zao, pamoja na kulia. Kama wavulana wanafundishwa kuamini kwamba hisia za huzuni hazihitajiki, watajifunza kuzikwepa hisia hizi ukubwani.

Usawa Katika Masuala ya Tofauti za Kijinsia

Wazazi wanaweza kusaidia kwa kuwafanya watoto wajisikie vizuri katika tofauti za uvulana na usichana.

- Wanaweza kuwapatia mabinti wao mwongozo na ufahamu kuhusu tofauti za kijinsia
- Wazazi wanaweza kuwafunza tabia njema watoto wao kwa tabia zao wenyewe. Kwa mfano, wanaweza kuhakikisha kwamba mtoto wao wa kiume anamuona mama yake akifyeka nyasi katika bustani na kuendesha gari na baba akifuta vumbi, akipika au kuosha vyombo. Katika baadhi ya nchi, wanawake hufanya kazi nyingi zilizo nzito (kama kubeba maji).
- Wazazi wanaweza kuwaondolea watoto wa kiume tofauti za kijinsia. Watoto wadogo hujifunza sana kutoka katika tabia za watoto wenzao kuliko kutoka kwa wazazi wao, hivyo wazazi wanapaswa kushirikiana na wazazi wengine.

Kuchanganya Jinsia na Hulka

Wazazi wengi wanakubaliana na wanasaikolojia kwamba kuwa na tabia ya kuwa mwanaume au mwanamke na kutotaka mabadiliko si njia sahihi. Watoto wa kiume na wa kike wanapaswa kujiamini na kuwa wapole, wepesi katika kufanya mambo na wenye kutathmini. Hata hivyo, wazazi wengi hushituka pale watoto wao wanapokuwa na tabia zinazowahusu watoto wa kiume na zile za watoto wa kike. Baba hushituka mtoto wake wa kiume anapohitaji kuwa na mwanasesere mzuri wa kike na mama hupata tabu pale binti yake anapokataa kuvaa magauni (Kessler na McKenna, 1978).

Lakini, jambo hili ni muhimu kiasi gani? Lina maanisha nini?

Yeyote katika sisi amezaliwa na hulka fulani. Hulka ni sifa ambazo mtu anakuwa nazo katika kukabiliana na mambo yanayomzunguka. Hulka hutufanya, kwa kiasi fulani, tuvutiwe na baadhi ya vitu na tuchukie baadhi ya vitu. Baadhi ya watoto huweza kuvutiwa na kuwapenda baadhi ya watu na kuwachukia watu wengine lakini wengine huwagopa (kumtazama machoni tu kunaweza kusababisha kumvutia na kuonesha tabasamu kwa tabasamu). Watoto wengine wanavutiwa zaidi na vitu vinavyoonekana au vitoavyo sauti (macho yao huganda kwa mwanasesere aliyening'inizwa).

Tatizo linatokea pale wazazi wanapoamini kwamba baadhi ya hulka huwa zinatokana na kuwa mwanaume au mwanamke. Hii huweza kuharibu ukweli. Kwa mfano, mzazi anapomwambia mtoto wake wa kiume aliyepaka rangi ya pinki katika kucha zake, "Unadhani wewe ni nani – u-msichana?" Mtoto huyo anaweza kujumuisha kwa makosa kwamba ikiwa anataka kufanya "mambo ya wasichana" basi anapaswa kuwa msichana. Hivyo anaweza kuanza kufikiria angekuwa mwanamke na kuwa mwanamke haswa! Hii ni tabia iliyoambukizwa kwa bahati mbaya na wazazi. Wasichana wengi hupenda sauti na vurugu za michezo ya watoto hasa ya kukimbizana, mieleka na mingine kama hiyo. Kama msichana anataka kuwa na nguvu na kufurahia michezo kama hiyo, wazazi wanaweza kumuona binti huyo kuwa anakosa "sifa za kisichana", wakati kimsingi ni kwamba mtoto huyo ana hulka ya juu ya kusisimka katika mazingira.

Mkanganyiko wa hulka na matarajio ya majukumu ya kijinsia ni tatizo hasa kwa vijana wa kiume. Wavulana hukaripiwa zaidi wanapojihusisha na michezo ya kisichana kuliko wasichana wanapojihusisha na michezo ya "kivulana". Michezo ya "kisichana" inaepukwa zaidi kuliko ile ya "kivulana". Hii ni kwa kuwa "nembo ya kiuanaume" ni ya kifahari zaidi katika jamii kuliko "nembo ya kike", na kwamba kukataliwa kwa nembo ya uanaume dhidi ya ile ya kike kwa kuwa na hadhi ya chini imepotoshwa kabisa.

WAZAZI WANAPASWA KUWA MAKINI NA MAMBO YAFUATAYO:

- Kuwa mwangalifu ukibaini mwanao ana tabia isiyoweza kudhibitika na kubadilika. Ni jambo moja kwa mtoto (awe msichana au mvulana) kutaka kuchezea mwanasesere wa kike au kuvaa kama mwanamke. Ni jambo jingine kama hicho ndicho pekee anachohitaji mtoto wako au mtoto anacheza kwa kurudiarudia sana.
- Ni mara chache sana, watoto ambao hawana furaha sana wanaweza kutamani miili yao, hasa sehemu zao za uzazi zingekuwa tofauti. Wazazi wanatakiwa kuwa makini kama mtoto wao atajaribu, au hata kuzungumzia kuharibu mwili wake. Katika hali hiyo, ni vema kutafuta usimamizi wa kitaalamu.
- Wazazi hawapaswi kubadili aina za hulka kuwa maradhi. Kama kijana wao au binti yao ana huzuni, kusononeshwa, au kuwa na tamaa anapaswa kupelekwa kwa mtaalamu wa kisaikolojia wa watoto ambaye amebobea katika tasnia hiyo.
- Tiba ya dawa ni hatari.Kumpatia dawa mtoto haishauriwi wakati tiba ya mazungumzo inapatikana.
- Si sawa kumlaumu mtu yeyote. Ni kama mahitaji yasiyo ya kawaida ya mtoto hayaendani na kitu chochote mahususi walichokifanya wazazi.

Wazazi wanapaswa kuwapenda watoto wao wa kiume na watoto zao wa kike. Watoto hujisikia vema wanapokuwa na malezi imara yenye uhusiano bora na wazazi, na pindi wazazi wanapotaka watoto wao kujali, kujihusisha na uzalishaji, kuwa na afya, na kuwa binadamu wenye furaha.

Wasichana na Wavulana Hujifunza Tofauti

"Toka kipindi kabla ya kuanza shule, wavulana na wasichana huchukua taarifa kwa viwango tofauti, kwa sababu tofautitofauti, na kwa vipimo tofauti vya mafanikio" (Gurian 2001).

Wavulana wadogo wanaweza kuvutiwa zaidi na vitu wakati watoto wa kike huvutiwa zaidi na watu na mahusiano. Katika shule za msingi, wakati watoto wa kiume wanaweza kuipata ramani ya Ufaransa mapema zaidi, wasichana hutumia muda kidogo kujifunza kifaransa. Mtoto wa kiume atakuwa mwepesi kujibu kwa usahihi

wakati mtoto wa kike atakuwa bora katika kusikiliza swali na kulijibu kwa maandishi. Kwa bahati mbaya, wavulana na wasichana huchukuliwa kama vile wote wanajifunza kwa namna moja, ambayo husababisha utukutu na kufeli.

Wanafunzi wenye matatizo (wazito) katika kujifunza wanaweza kubadilishwa ikiwa tu tutatambua tofauti kati ya wavulana na wasichana na kujifunza wenyewe namna ya kuwasaidia wapate msukumo. Mikakati iliyofanikiwa ya Michael Grian imetumika kuwabadilisha wanafunzi wanaofeli kuwa wanafunzi bora. Mikakati hiyo ingeweza kuyafaidisha madarasa yote kwa kuwa alisisitiza katika ubora wa wavulana na wasichana na hivyo kukamilisha udhaifu wao.

Kwa wasichana: Wazazi wanatakiwa kuboresha majukumu yao ya kiuongozi, kucheza michezo inayohusiana na mijongeo, kutumia mbinu za uandishi; kuwawezesha kutumia kompyuta na kuzimudu sawasawa; na kuwahamasisha watoto wa kike kushiriki katika mashindano ya hesabu na sayansi.

Kwa wavulana: Wazazi wanatakiwa wawahamasishe watoto wao wa kiume kutumia nguvu zao katika usafi, kusaidia na kuvisogeza vitu karibu; kuwasaidia watoto wa kiume kutambua hisia kama hasira, huzuni, na furaha; kuwafanya wasimulie hadithi mbalimbali, kutengeneza dhana na kukuza uwezo wa ubongo katika mazungumzo na fikra; kuwafanya kuwa na mijongeo ya kimwili, kuwafunza ujuzi wa vyombo vya habari, na kuwashirikisha katika usuluhishi wa matatizo na mafunzo katika jamii.

Suala la elimu ya kuwatenganisha wavulana na wasichana ni lenye utata. Hata hivyo, kwa kuwa wasichana na wavulana hujifunza tofauti, inaweza kufanya umuhimu wa kuwepo kwa mikakati tofauti ya kufundishia madarasani, kwanini tusitumie madarasa na mbinu tofauti zisitumike kwa mafanikio bora ya kielimu? Tutawezaje kutumia mbinu mbili tofauti za ufundishaji katika darasa moja kwa wakati mmoja? Hilo linawezekana? Na kama ndivyo hivyo, gharama zikoje katika muda, fedha, na mafanikio ya matokeo?

Michael Gilbert (2007) anapendekeza kuwepo kwa shule za jinsi moja. Makala yake ya mtandaoni imefupishwa kama ifuatavyo:

> Wavulana wanaanguka na kuacha shule kwa idadi kubwa kuliko wasichana. Wavulana waliofanikiwa kuendelea na masomo na kujikuta ni kundi dogo, wakizidiwa kwa idadi karibu mara tatu ya idadi ya wanawake. Katika miaka ya 1960, kwa kuhofu kuwa kuwatenganisha hakutaleta usawa, na katika kutafuta njia ya kuzuia kasumba za kijinsi, wataalamu waliamua kuwachanganya wote pamoja katika umri mdogo kabisa. Katika mwaka 1965, idadi kubwa ya madarasa ya Shule za Umma nchini Marekani zilikuwa za jinsi moja; kufikia mwaka 2000 chache sana katika hizo zilibakia.
>
> Shule zinazojumuisha watoto wa kiume na wa kike zinahitaji mbinu za vifaa vya kufundishia visivyozingatia jinsi za wanafunzi na majaribio yanayofanana na viwango vya tabia. Kitendo hiki, katika jitihada za kuwa na usawa katika ulimwengu wa jinsi katika shule zetu, kimesababisha "sawa na" kubadilishwa kuwa "sawa kama". Lakini pana shida: wavulana na wasichana hawafanani. Hawakui pamoja na kwa wakati mmoja. Wazazi wengi wanaoishi nao wanajua kwamba wavulana hujifunza taratibu katika kila kitu kutoka katika msamiati mpaka kuwa mwandishi, hata uwezo mwepesi tu wa kukaa tuli.
>
> Wakati wavulana wadogo nchini Marekani wanapofika shuleni leo, wanaingia katika ulimwengu uliotawaliwa na viongozi wa masuala ya utawala ni wanawake na walimu wao pia ni wanawake . Asilimia ya idadi ya walimu wa kiume katika shule za Umma nchini humo imefikia idadi ndogo kwa kipindi cha miaka 40. Wasichana wanaowazunguka hujifunza kwa haraka, hudhibiti hisia zao haraka na wana furaha zaidi na mfumo wa elimu wa sasa unaosisitiza mafunzo kwa ushirikiano na kueleza hisia. Wavulana wanapendelea vitu vya kuonekana na hawana kitu cha kuwadhibiti kama ilivyo kwa wasichana waliopata mapema wakati wa utoto wao. Ni nadra sana kwa vitendo, mashindano, au mifumo wanayotengeneza wavulana. Wavulana wangependa kufanya vitu tofauti ambavyo vitaelezea hisia zao.
>
> Wavulana wana tabu katika kusikiliza kwa makini wanapokuwa madarasani. Mara nyingi hupuuza maelekezo na hivyo kuishia kufanya kazi vibaya. Wanaweza kuathirika mara tatu au mara nne zaidi katika matatizo ya kimaendeleo, na mara mbili zaidi ya wasichana wenye matatizo ya kujifunza. Wengi wao huadhibiwa kwa makosa yanayoonekana. Wavulana wanadhibitiwa na kufanywa wawe na tabia za kiume (mvulana mmoja mpaka watano wa kizungu hutumia pombe kali). Wanaweza wasiruhusiwe hata wakati wa mapumziko. Hii inamaanisha wavulana huanza na tabia ya utukutu, kushindwa kuendana na kasi ya masomo na mwisho kuacha shule.

Wavulana wa shule za awali huwazidi wasichana kwa asilimia 50 katika kukariri (kurudia) madarasa na wavulana hao huacha shule mara tatu zaidi ya watoto wa kike. Wavulana kutoka katika familia zenye uwezo duni wa kiuchumi na jamii za wachache huteseka zaidi. Mwishowe, mfumo wa elimu wa Kimarekani husababisha matabaka ya wavulana walioshindwa kuandaliwa vema au kutokuwa na hamu ya kujiendeleza kimasomo, pamoja na kwamba matokeo yake makubwa katika mapato yao ya mbeleni yameandikwa sana. Hii ni mbaya kwa wanaume, wanawake, na ustawi wa kiuchumi wa nchi.

Margaret Mead, miongoni mwa wanahistoria wa mazingira, anasema kwamba karibu utamaduni wote umewafunza na kuwaandaa wavulana na wasichana katika namna tofauti.

Katika shule 90,000 za mchanganyiko wa wavulana na wasichana nchini Marekani, shule chini ya 250 za Umma zimechagua kuwa na shule za jinsi moja katika majimbo 33.Uamuzi huu umekuwa maarufu katika shule za binafsi na za kidini.

Shule za jinsi moja za binafsi zilipata mafanikio makubwa kwa muda mrefu. Wanafunzi wa darasa la nne kutoka shule ya awali ya Florida walihamishiwa katika darasa lenye wanafunzi wenye jinsi moja. Wasichana na wavulana hao waliongeza mafanikio yao mara dufu katika majaribio ya kuandika. Mafanikio mengine yalionekana katika majaribio yaliyofanyika Marekani, Kanada na Ireland. Wasichana na wavulana hufanya vema katika masomo wanapoongezewa mashindano na msukumo wa kijamii katika shule za mchanganyiko, na matatizo ya kinidhamu hupungua.

Kuna matokeo chanya kutoka katika shule za jinsi moja kwa pande zote: wavulana na wasichana ikiwemo pamoja na kusoma sana na mafanikio makubwa katika lugha za kigeni, muda mwingi hutumika kwa kazi za kufanya nyumbani, na kuwa na ndoto za kufika elimu ya juu. Ripoti ya Jumuiya ya Kitaifa ya Bodi za Elimu nchini Marekani (NASBE), 2002, inaonyesha dhahiri kwamba katika shule za jinsi moja “matokeo chanya ni makubwa miongoni mwa wasichana na wanafunzi wa kundi dogo kwa jinsi zote.” ■

Kuwatenganisha Wavulana na Wasichana katika Shule na katika Madarasa

Katika shule ya Wilaya ya Greene, Georgia, Marekani ilipania kuwa ni shule ya kwanza ya Wilaya kuwa na wanafunzi wa jinsi moja pekee, ambapo wasichana na wavulana wangewekwa katika madarasa tofauti. Maamuzi hayo yalitokana na muda mrefu kuwa na ufaulu mdogo, takwimu mbaya za watoto wanaoacha shule pamoja na visa vingi vya wasichana wanaopata ujauzito. Wazazi wengi na walimu walipinga mabadiliko hayo kwa kuwa hawakuhusishwa na mwishowe mpango huo ulifutwa.

Muhudumu wa shule ya McCollough alisema kwamba wavulana na wasichana hujifunza tofauti na kwamba kuwatenganisha kungetoa fursa kwa walimu kupanga ufundishaji wao. Pia, wavulana wasingeweza kuwa watukutu kwa kuwa hawangeweza kufanya kwa ajili ya kuwavutia wasichana, na hali kadhalika wasichana wataweza kuzungumza darasani kwa kuwa hawataogopa kuhusu utanashati mbele ya wavulana. (*India Times*, 2008).

Madarasa tofauti huwezesha masomo kutokana na uimara na mahitaji ya kila jinsi. Wavulana na wasichana hujifunza tofauti na watapata mafanikio zaidi kama madarasa yao yakiandaliwa kwa mahitaji yao. Sax (2006) anasema, sisi kama taifa hatutambui tofauti za kijinsia na kuifanya kuwa si sahihi kisiasa kujadili hilo. Matokeo yake ni kwamba shule haziwasaidii wanafunzi kufikia malengo yao. Bila kutarajia tunasukuma nje wasichana katika

fani za sayansi ya kompyuta na kuwasukuma wavulana nje ya fani ya sanaa na lugha. Gurian (2001) anaonyesha kwamba wavulana hawasikii sawa na wasichana na kwamba wasichana huogopa sana mwanga. Wavulana mara zote, huzungukazunguka na kufanya mijongeo kuwa na tahadhari, wakati wasichana hutulia na kusikiliza. Mbinu tofauti za ufundishaji zinatumika katika tofauti kama hizo (Chandler and Glod 2008). Tunapendekeza mfumo ufuatao uanzishwe kwa mafanikio na Chuo Kikuu Cha Kiislamu Cha Malaysia, (IIU), katika shule zake za awali, za kati, na za juu:

1. Kutoka shule za awali mpaka darasa la tatu: kusiwe na ukuta wa kuwatenganisha wavulana na wasichana, na walimu wawe ni wanawake.
2. Kutoka darasa la nne mpaka la sita: wavulana na wasichana wawe katika darasa moja lakini lililotenganishwa, upande mmoja wakae wasichana na mwingine wavulana, ndani ya shule hiyo hiyo. Kuwachanganya pamoja kunaruhusiwa katika shughuli mbalimbali na wakati wa mapumziko. Hata hivyo, wavulana na wasichana wanaweza kukaa pamoja katika darasa moja lakini kwa kutenganishwa katika safu, kama inavyoonekana katika mchoro ufuatao:

Mpangilio wa Darasa unaopendekezwa kwa Darasa la Nne mpaka la Sita



3. Kutoka daraja la saba mpaka la nane: kuwe na shule tofauti kwa wasichana na wavulana na walimu wanapendekezwa kuwa wa jinsia sawa na wanafunzi husika. Kundi hili la wanafunzi wenye umri kuanzia miaka 13 mpaka 14 ni kipindi ambacho watoto wanaathirika sana na mihemko itokanayo na baleghe, na watoto hushuhudia na kujifunza taratibu, mabadiliko yao katika ukuaji. Ni hatari kuwachanganya pamoja kabla hawajaelewa hatari ya zinaa na masuala mengine yanayohusiana na mabadiliko yao ya kimwili.

4. Kutoka darasa la tisa mpaka la kumi na mbili kuwe na shule tofauti na walimu wa jinsia husika tu.

5. Elimu ya Chuo Kikuu: wavulana na wasichana wawe katika darasa moja lakini wakae katika safu mbili tofauti. Katika umri huu, vijana hujiheshimu zaidi. Wanaweza kuchagua wachumba wao hususan Kitivo au wazazi watakapowasaidia na kuwashauri. Hili linafanyika vema katika IIU, ambapo kozi juu ya malezi hutolewa kwa wanafunzi wote.

Malezi na Jinsia: Mtazamo wa Kiislamu

Uislamu ulipokuja mnamo mwaka 610 baada ya Kristo, jamii ya Kiarabu ilitawaliwa na mfumo dume na kuwa na uzalendo pofu kwamba kuzaa msichana ni mkosi na aibu.

> Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki!
> (Qur'an 16:58).

Majibu ya Qur'an ni kwamba ni Allah aliyetoa zawadi ya uzao, kama wote ni wasichana, wavulana, au mchanganyiko. Mtume (s.a.w) alifundisha kufanyiwa wema wazazi waliowalea mabinti zao katika maadili mema aliposema:

> *Yeyote mwenye mabinti au dada watatu, au mabinti au dada wawili, na akawafundisha maadili mema, na kumuogopa Allah, ataingia peponi. (Al-Bukhari na Muslim).*

> Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamungu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari. (Qur'an 49:13).

Wanadamu wote ni watoto wa mwanaume mmoja (Adam) na mama mmoja (Hawaa). Linapokuja suala la majukumu mahsusi ya kila jinsia, Mtume (s.a.w) aliweka wazi fikra na matendo katikati ya jamii ya Kiarabu iliyotawaliwa na mfumo dume kwa kusema:

> *Aliye bora miongoni mwenu ni yule aliye bora katika familia yake na mimi ni mbora kuliko ninyi katika familia yangu.*
> *(Al-Tirmidhi na Ibn Majah).*

Mtume alifanya kazi za ndani kama inavyoelezwa katika hadithi ifuatayo:

> *Aisha na Umm Salama walimzungumzia Mtume (s.a.w) kwamba amekuwa akirekebisha viatu vyake, akishona na kurekebisha nguo na*

> *kufanya mengine yanayofanywa na wanaume wengine majumbani mwao. (Ahmad).*

Mtume (s.a.w) hakugawanya majukumu katika makundi mawili, yaani: "kazi za wanawake" na "kazi za wanaume". Linapokuja suala la majukumu ya kimaumbile ya mama, ujauzito, na kunyonyesha, Qur'an Tukufu imeweka bayana nafasi ya baba katika kumsaidia mkewe na mtoto kwa kila kitu , yawe mahitaji ya vitu au ya kihisia. Vilevile, Mtume (s.a.w) aliwapa akina mama heshima kubwa, na si baba aliposema:

> *Pepo ipo chini ya nyayo za kina mama.*
> *(Ahmad, Al-Nasa'I, na Ibn Majah).*

Mtume (s.a.w) alisisitiza usawa wa kijinsia na kuweka mfano katika kufanya kazi za nyumbani katika maisha yake mwenyewe ambazo zinaweza kuelezwa kama za kimabadiliko katika mfumo uliokuwepo enzi za ujahilia katika jamii ya Kiarabu na utamaduni wa Kipagani.

Katika jambo nyeti la jinsi, Uislamu uko imara na wazi kuhusu kukataza ngono ya aina yoyote nje ya ndoa kati ya mwanamke na mwanaume. Kanuni hii inalenga kuikinga familia na jamii dhidi ya maradhi na migongano. Uislamu hauna mjadala katika mambo haya, na kufunga njia zote zinazoelekeza katika ngono inayokiuka sheria kama vile: pombe, dawa za kulevya, shubha, na ushawishi. Watoto wanapofikisha umri wa miaka kumi, wanalazimika kutenganishwa katika vitanda, kuzuia hatari yoyote inayoweza kutokea.

> *Mtume (s.a.w) anasema: watoto wenu wanapofikia umri wa miaka saba, wafundisheni kuswali, na wanapofikia umri wa miaka kumi, wapeni adhabu kama hawafuati maelekezo [ili waweze kuswali];na kuwatenganisha katika vitanda vyao. (Ahmad na Abu Daud).*

Uislamu unawaandaa wasichana katika majukumu ya kuwa kina mama na walezi wa watoto, pamoja na kufanya kazi nje na nyumbani na majukumu ya Umma ikiwa ni pamoja na kushiriki vitani). Enzi za Mtume (s.a.w), wanawake walipigana bega kwa bega wakishirikiana pamoja na Mtume. Baada ya watoto wao kufikisha umri fulani, kina mama wanapaswa kushiriki vilivyo katika majukumu ya kijamii, katika kazi zote za msimu na za kudumu, za malipo au za kujitolea, harakati za kisiasa au zisizo za kisiasa. Kitu chochote kinachowezekana katika hali zao, weledi wao, mafunzo yao, uzoefu wao, na mahitaji ya kiuchumi yanasisitizwa. Haya si majukumu ya mwanamke, lakini ni yote haya ni katika hiyari zao. Kinyume chake, majukumu ya mwanaume ni kuisadia familia yote.

Baadhi ya majukumu ya kijinsia kwa undani yameachiwa utamaduni wa kisasa. Kwa mfano, wakati wa Mtume (s.a.w), wanaume walikuwa na nywele ndefu. Katika nchi za Magharibi, katikati ya miaka 1900, nywele ndefu zilimkosesha mwanaume kupata ajira. Wakati huu wa karne ya ishirini na moja, kuwa na nywele ndefu, kunakubalika. Kipindi cha nyuma, kazi ngumu na zinazohitaji uchapakazi mkubwa zilipewa kwa wanaume. Hata hivyo, wakati huu, miongoni mwa kazi hizo ngumu hazihitaji misuli kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, vifaa vya umeme, na kompyuta. Tasnia kama ujenzi, uhandisi, na usafirishaji zinaweza kufanywa vema na wanawake. Kwa namna hiyo hiyo wanaume na wanawake kufanya kazi katika maeneo kama kufundisha, mgahawani, uhudumu hospitalini, teknolojia ya habari, na uongozi wa hoteli. Pia, linapokuja suala la mavazi, wote, wanaume na wanawake, wanaweza kuvaa *jinzi* na mavazi mengine ili mradi zinatunza heshima, utu na hadhi yaani; isiyobana, isiyoangaza, yenye kufunika mwili na isiyoshawishi matamanio. Katika nchi za Kiislamu, kama Pakistani, suruali ni sehemu ya mavazi ya kiasili kwa wanawake.

Wanaume na wanawake wana vitu vingi vya kujifunza kutoka kwa pande zote. Inaweza kuelezwa kwamba kuna sifa za kike katika kila mwanaume na sifa za kiume kwa kila mwanamke. Wote wanaume na wanawake, huwa na vichocheo vya aina tofauti. Hii haishangazi kabisa kama tukiitathmini aya ifuatayo katika Qur'an:

> … Wao ni vazi kwenu, na nyinyi ni vazi kwao.
> (Qur'an 2:187).

> Mola Mlezi wao, akayakubali maombi yao akajibu: Hakika sipotezi kazi ya mfanyakazi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi…
> (Qur'an 3:195).

> Amekuumbeni kutokana na nafsi moja.
> (Qur'an 39:6).

Nafasi ya mwisho baina ya jinsia ni:

> Wala msitamani alichowafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wana fungu katika waliovichuma, na wanawake wana fungu katika waliovichuma. Na muombeni

> Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. (Qur'an 4:32).

Qur'an Tukufu inawaelezea wanadamu wote. Katika baadhi ya aya wanaume au wanawake wametajwa pale kunapokuwa na jambo mahsusi linalowahusu. Katika hali zote, hata hivyo, Qur'an inawaelezea wanaume na wanawake kwa heshima kubwa.

Njia ya Mungu ni Njia Bora: Mfano wa China, Ujerumani na India

Muumba wa ulimwengu ameweka kila kitu katika kipimo sahihi na kutuzawadia mazingira yaliyo na uwiano sawa. Tunapochezea sheria tukufu, tunasababisha matatizo. China ni mfano katika hili. Katika juhudi zake za kukabiliana na ukuaji wa idadi ya watu, ilianzisha sera yenye utata ya mtoto mmoja. Wanandoa walipaswa kujizuia kuwa na mtoto zaidi ya mmoja katika familia vinginevyo watakosa msaada. Hii ilisababisha jamii iwe na wanaume wengi, kwa kuwa watu wengi hupendelea mtoto wa kiume kuliko mtoto wa kike kuwasaidia majukumu ya familia. Kwa miongo mingi sana, wazazi wamekuwa wakipenda kuwa na watoto wa kiume na kuwaangamiza watoto wa kike. Matokeo yake ni upungufu mkubwa wa wanawake katika idadi ya watu, hivyo kusababisha uhalifu, utekaji, na ukahaba pamoja na madhara makubwa ya kutoa mimba. Mgawanyo huu hatari na usiyo sawa, umeilazimisha serikali kuifuta sera hiyo isiyozingatia maumbile ya mwanadamu, uhalisia wa kijamii na kuzifanya familia kurudia katika asili yao. Qur'an Tukufu inaeleza bayana sheria tukufu ya maumbile kama ifuatavyo:

> Ni wa Mwenyezi Mungu peke yake Ufalme wa mbingu na ardhi, kwa kuumba, kuudabiri, na kuusarifu. Yeye anaumba atakacho. Humtunukia amtakaye wana wa kike, na akamtunukia amtakaye wana wanaume bila ya wanawake, au huwachanganya wanaume na wanawake, na akamfanya amtakaye tasa: Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye uwezo.
> (Qur'an 42:49 – 50).

Toka enzi za Adam na Hawaa, usawa wa kijinsia ulikuwepo kiasili kwa mujibu wa mpango wa Muumba Mkuu. Wanazi walijaribu kufanya utafiti kwa sifa za mtu mmoja mmoja. Mipango yao ya udhibiti imelenga kuzalisha "binadamu imara", kwa kila njia ya utambulisho, kutenganisha, na mafunzo. Pia, matokeo yalikuwa kufeli kuliko kukubwa.

Agnivesh na wenzake. (2005) ameonyesha kwa namna gani utoaji wa mimba kwa kuzingatia jinsi (kuwatoa mimba watoto wa kike) imesababisha pengo la kutisha la kijinsia la milioni 50 zaidi la wanaume dhidi ya wanawake. Kwa kejeli, teknolojia ndio iliyorahisisha hili. Hapo zamani, watoto wadogo wa kike wamekuwa wakiuawa baada ya kuzaliwa. Sasa hivi ni rahisi kwa wazazi, na yenye faida sana kwa madaktari kutoa mimba kwa kutambua jinsi ya mtoto kwa kutumia *ultra-sound* bila kufungwa na sheria za adhabu kwa makosa kama hayo. Katika jitihada za kukabiliana na tatizo hili, serikali imefanya juhudi za kutambua jinsi ya mtoto aliye tumboni kuwa ni kosa kwa kutumia kipimo cha *ultra-sound*.

Vitendo hivi viliendelea kushamiri katika jamii za kimaskini na zile zisizoelimika, na kiasi kikubwa hali hii inasababisha kuongezeka kwa kiasi kikubwa cha mahari kitolewacho kwa mwanaume, pamoja na kasumba nyingine. Hata hivyo, kwa sasa, vitendo vya kutoa mimba kwa watoto wa kike, vimeshamiri pia katika familia za kitajiri na wasomi, pamoja na kupanda kwa kiwango cha elimu kwa wanawake ambapo kiwango cha chini huwa darasa la tano na cha juu miongoni mwa wanawake hufikia shahada ya Chuo Kikuu.

Wasichana wamekuwa wakisafirishwa kutoka katika familia za kimasikini kutoka nchini Bangladeshi na Nepali au kutoka katika maeneo ya makabila madogo nchini India na kuuzwa katika ndoa kwa takriban dola za Kimarekani 200 – wakati fahali hugharimu dola za Kimarekani 1,000 (Hughes, na wenzake. 1999). Kwa bahati mbaya, karibu kutoka kila utamaduni nchini India, kuzaliwa kwa mtoto wa kiume husherehekewa wakati kuzaliwa kwa mtoto wa kike huombolezwa.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 41: MAZUNGUMZO YA WAZAZI

Wakusanye kina baba na kina mama kadhaa wajadili "Namna gani ya kumlea mtoto mwema", na kuwafanya wabadilishane uzoefu katika mambo mazuri na mabaya.

Baada ya hafla ya chakula cha usiku nyumbani kwetu, wazazi wote waliketi na kuanza kujadili namna gani ya kumlea mtoto mwema. Uzoefu mzuri wa namna tofautitofauti ulionyeshwa. Mwishowe, mzazi mmoja mwenye busara alisema, "Yote yaliyosemwa ni muhimu, lakini hayatoshi kwa kuwa hata kama utafuata taratibu zote, bila Baraka za Mungu katika familia yako, kijana wako hatajisikia vema." Wazazi walikubaliana yafuatayo:

Haijalishi utatumia juhudi kiasi gani, unapaswa wakati wote kuoanisha ujuzi na mbinu zako katika kutafuta Baraka za Mungu ili aweze kukusaidia katika majukumu haya adhimu na yenye changamoto, majukumu ya malezi.

Inahitaji familia, inahitaji kijiji, inahitaji Umma, na inahitaji Baraka za Mungu kumlea mtoto. Ushirikiano wa wadau wote katika majukumu haya ndio jawabu.

ZOEZI LA 42: NAKUSHUKURU MWENYEZI MUNGU

- Shukran zote ziende kwa Mungu "Al-Hamdu Lillah"
- Mfundishe mwanao kutamka yafuatayo mara kwa mara:
- Namshukuru Mungu kwa vitu vyote vizuri alivyonijalia.
- Namshukuru Mungu kwa kuniumba mimi kuwa mwanadamu.
- Namshukuru Mungu kuniumba mimi kuwa msichana, au
- Namshukuru Mungu kwa kuniumba mimi kuwa mvulana.

  Namshukuru Mungu kwa kuniumba mimi kuwa mweusi, mweupe, maji ya kunde, au wa manjano.

Namshukuru Mungu kwa kuniumba hivi nilivyo!!

ZOEZI LA 43: BARACK OBAMA: MFANO WA MALEZI RAHISI

Wazazi wanashauriwa kuketi na watoto wao na kujadili kunyanyuka kwa Wamarekani-

Waafrika mpaka kufikia katika ngazi za ofisi kubwa katika dunia. Haijalishi ni kwa namna gani Urais wake unavyoendeshwa, mafanikio ya Barack Obama yatatumika wakati wote kuonyesha mfano katika uwezo wa mwanadamu wa kukabiliana na matatizo. Waeleze watoto wako wasome vitabu viwili vya Obama: *Ndoto kutoka kwa Baba Yangu: Kisa Cha Rangi na Urithi*, na *Ujasiri wa Matumaini*. Wazazi wanaweza kuwaeleza watoto wao kuhusu uwepo na busara za mipango ya Mungu, namna inavyoweza kuendelea kutoka kwa kizazi kimoja mpaka kizazi kingine, kusafiri umbali mrefu, na pamoja na vikwazo njiani, mara zote hufika kuliko kusudiwa. Obama alilelewa na mzazi mmoja, wazazi gani wanaweza kujadili ni mzazi yupi. Wanapaswa pia kujadili akina mama waliowalea Mitume Mussa na Issa (amani iwe juu yao), na mjomba aliyemlea Mtume Muhammad (SAW). Kuhusu Obama na mpango wa Mungu, inapendeza kutambua kwamba hali ingekuwaje tofauti kama hatua mojawapo ingeachwa katika maisha yake. Zingatia "ingekuwaje kama:"

- Ingekuwaje kama baba yake Obama (Barack Hussein Obama, Mkubwa) asingekuwa Muislamu mwenye asili ya Kenya na asingekwenda masomoni Marekani?
- Ingekuwaje kama asingemuoa mwanamke wa kizungu (Ann Dunham) kutoka Kansas? Ingekuwaje asingemuacha mke wake Ann wakati Barack akiwa na umri wa miaka miwili na asirudi tena? Ingekuwaje mama yake, Ann asingeolewa na Muislamu kutoka Indonesia (Soetoro) na kuishi kwa miaka minne Jakarta, mahali ambapo Obama alisoma na watoto wa Kiislamu?
- Ingekuwaje kama mama yake asingefariki kwa saratani na wazazi wake wa kizungu (Madelyn na Stanley Dunham) wasingemlea katika jiji la Hawaii, aliposomea? Fikiria athari na neema za familia kubwa!!
- Ingekuwaje kama asingesoma Chuo Kikuu cha Harvard na kuwa Mwafrika wa kwanza kuwa Mhariri wa Jarida la kifahari, Harvard Review?
- Ingekuwaje asingeishi Chicago kama Mkristo na kusali katika Kanisa la Utatu wa Kikristo kwa miongo kadhaa? Ingekuwaje asingemuoa Michelle, mwenye asili ya watumwa wa Kiafrika, ambaye pia alisomea Harvard?

Mwanadamu anapendekeza lakini Mungu anapanga.

Ni mafanikio makubwa kwa ubinadamu kupambana na ubaguzi wa rangi na uhafidhina na kuzidisha usawa, kukubali tofauti zetu, na kuvumiliana. Ikulu ya Marekani ilijengwa na watumwa wa Kiafrika kati ya mwaka 1792 na mwaka 1800, na sasa kukaliwa na mmoja wao; familia ya baba, mama, na mabinti wawili ni mabadiliko makubwa. Kitu chochote anachokifanya Obama, hakika anatengeneza historia!

Katika muktadha huohuo, wazazi wanaweza kusimulia visa vyao wenyewe kuhusu mipango ya Mungu, na kubadilishana maamuzi yaliyofanyika katika changamoto za maisha yao, na kwa namna gani zimefanya kuoa au kuolewa, kuwa na watoto, na kuwa walipo leo!

Ni Mpango Mkuu wa Muumba: Huwezi kufanikiwa, mpaka Mungu atake liwe!

18

SURA YA KUMI NA TATU

- **JINSIA NA ELIMU YA JINSIA**

Je tunawaeleza nini watoto wetu?

SURA YA KUMI NA TATU 320

Jinsia na Elimu ya Jinsia: Je tunawaeleza nini watoto wetu? 320

Elimu ya Jinsia ni Nini? 322
Ukimwi na vifo nchini Thailand 327
Kwanini Profesa Mmoja aliamua kuhama nchini Marekani? 327
Maadili na Jinsia: jana na leo 329
Kwanini Elimu ya Jinsia? Ni lazima Kufundisha? 331
Kitu gani wafundishwe Watoto? 333
Muingiliano wa Kimwili Usiokubalika Kisheria! Jinsi Ulivyoenea! 334
Hikima ya Hukumu ya Kisheria kuhusu Uzinzi 337
Maradhi yanayoenea kwa njia ya Kujamiiana 338
Watoto Wenye Watoto 343
Utoaji Mimba 344
Uleaji wa Kunasibisha Mtoto 345
Mahusiano ya jinsia Moja na Wazazi 346
Elimu ya jinsia kwa Mujibu wa Uislamu 350
Jukumu la Wazazi kwa Watoto 352
Jinsia na Usafi wa Mwili 353
Vijana na Kujizuia 354
Mwongozo wa Kufuata Kuzuia Matatizo 356
Kuwa na Haya kwa jinsia tofauti 359
Utaratibu wa mavazi 364
Hakuna Kuchanganyika na Kukutana Faragha 365
Vishawishi Rika (makundi) na Sababu nyingine 366
Ndoa za mapema 367
Kuwalinda watoto dhidi ya ukatili wa kijinsia wa watu wazima 371
Umri unaofaa kwa Watoto Kuwatahadharisha kuhusu Ukahaba 373
Pindi Mtoto Anapokuwa Mhanga wa Kubakwa na nduguye 374
Mtaala wa Elimu ya Jinsia kwa Mujibu wa Uislamu 376
Kazi za Kufanya

"Wala usiikurubie zinaa; hakika ni kitendo kiletacho aibu na kiovu chenye kupelekea utendaji wa maovu mengine"
(Qur'an 17:32)

Utangulizi

Muingiliano wa kimwili na elimu ya jinsia ni mada zenye umuhimu mkubwa. Wazazi wengi hukosa hali ya kujiamini wanapokuwa wanajadili kuhusu muingiliano wa kimwili na hivyo huwafanya waache elimu ya jinsia kwa watoto wao iwe inafundishwa shuleni na watu wengine katika jamii. Ili watu wawe sawa kimwili na kiafya, kiakili, kimaumbile, katika mioyo na kiroho wanatakiwa wajihusishe vizuri kabisa katika masuala ya mahusiano na muingiliano kimwili. Ngono isiyo katika misingi ya sheria huleta athari na madhara ya muda mrefu. Madhara makubwa yanayofahamika ni pamoja na magonjwa. Siyo kwa watu ambao wanajihusisha katika mahusiano ya aina hii pekee ndiyo wenye kupata maradhi bali hata wenza wao na watoto huweza kuathiriwa na maradhi hayo. Maradhi haya huwa mabaya sana na hushindwa kutibika.

Mwenyezi Mungu ambaye ndiyo muumba wetu amekataza zinaa. Kuwa na mahusiano ya kimwili zaidi ya mtu mmoja huleta madhara na kanuni mojawapo ya kuepukana na hili ni kudhibiti mahusiano ya aina hii nje ya ndoa. Maradhi yenye kuenea kwa njia ya zinaa huenea kupitia njia ya zinaa. Pindi binadamu wanapokuwa na tabia yenye kukinzana na asili yao, maradhi mapya huibuka. Wazazi wanahitajika kushiriki kikamilifu katika masuala ya elimu ya jinsia kuhusu wao wenyewe pamoja na watoto wao.

Elimu ya Jinsia ni Nini?

Watu wana uelewa tofauti kuhusiana na elimu ya jinsia. Je, huwa inahusiana na muundo na muonekano wa mwili wa binadamu, au muingiliano wa kimwili, au inahusiana na namna binadamu wanavyozaliana na kuishi maisha yao katika familia au namna ya kuzuia maradhi na mimba zisizotarajiwa? Je, kuwaelimisha



watoto kuhusiana na elimu ya jinsia ni sawa na kuwapa ruhusa kushiriki katika mahusiano ya kimwili? Mwalimu aliwahi kusema "sikusudii kuwaeleza watoto wenu kuwa washiriki katika mahusiano ya kimwili (zinaa) au la na wala siwaelezi namna ya kuendea tendo hilo. Lakini kama wataamua wenyewe kujihusisha na mahusiano ya aina hiyo, lazima wafahamu namna ya kujiepusha na maradhi pamoja na mimba". Elimu nyingi zinazotolewa kuhusu masuala ya jinsia zinakuwa na mapungufu na hazizungumzi kuhusu maadili, kukosa uwezo wa kushiriki kikamilifu katika tendo, kukiuka mipaka ya tendo hilo na masuala ya ndoa.

Kuna vitu viwili vya msingi. Kitu cha kwanza ni kuhusu uhalisia wa maumbile kibaiolojia. Hii inahusiana na hofu wanayokuwa nayo vijana kutokana na kutoandaliwa na wazazi wao kuhusu ada yao/siku zao (kwa wanawake) na ndoto nyevu (kwa wanaume). Kitu kingine ni kuhusu kuwapa dondoo za kutosha vijana ambao wanaweza kushiriki katika mahusiano ya kimwili (zinaa) namna ya kuzuia mimba zisizotarajiwa na madhara ya kutoa mimba hapo baadaye. Dondoo husaidia kuwaepusha na hatari zitokanazo na tendo hilo.Baadhi ya shule hufundisha namna binadamu wanavyozaliana na majukumu ya kijamii. Katika shule nyingi elimu ya jinsia huwa ni sehemu kubwa ya mtaala wa elimu ya maadili na jamii. Hushiriki kwa kiasi kidogo sana kumtoa katika makundi haya, kutokana na masomo haya pia huweza kujadiliwa katika masomo ya kiingereza, historia, elimu ya maumbile, sanaa au vipindi vya dini mashuleni au kuweza kuonekana katika somo lingine lolote. Maingiliano ya kimwili (kujamiiana) yamekuwa sehemu muhimu katika maisha yetu.

Kiasi kikubwa cha elimu itolewayo kuhusu jinsia haipelekei kuwepo na maisha ya ndoa yenye furaha na kuridhisha. Kwa hiyo wanandoa wengi huwa na maisha ya ndoa yenye kukatisha tamaa, mara nyingi kutokana na kukosa elimu na ujuzi. Dhana potofu iliyopo ni kwamba "uwezo wa mwanaume katika kumridhisha mke wake ni jambo asilia, hutokea bila kujifunza". Utambuzi wa namna ya kuunda maisha ya ndoa yenye furaha ni sehemu muhimu ya elimu. Kitu cha kusikitisha ni kuwa, elimu ya aina hii haitolewi sehemu yoyote katika maisha ya vijana.

Kama kijana wako amekuwa na ana uwezo wa kushiriki katika tendo, huenda wewe ukawa ni mtu wa mwisho katika kufahamu hali hiyo. Kijana atajaribu kufanya siri suala hilo katika nafsi yake. Vijana wana tabia ya kufanyiana siri miongoni mwao, ambapo hujua mengi kuhusu makundi yao ila huficha kwa wazazi wao.

Jibu la yote haya ni kigezo chema Mtume Muhammad (s.a.w). Namna elimu ya jinsia inavyoelezewa na kufundishwa shuleni inakuwa na faida na madhara mengi. Kwa hiyo, wazazi lazima wachukue nafasi yao katika jukumu la kuwaongoza watoto wao. Dondoo tunazopewa na jamii

kuhusu jinsia, ikiwemo shule, runinga, mtandao wa kimataifa na makundi mbalimbali huwa na faida na madhara mbalimbali.

Mazingira ya Marekani

Athar (1990) anasimulia namna watoto wanavyopewa elimu ya jinsia isiyozingatia maadili katika shule zao na namna watoto hao wanavyopata taarifa isiyo sahihi katika vyombo vya habari kuhusu elimu ya jinsia. (Tazama elimu ya jinsia: mtazamo wa Kiislamu, imeharirwa na Shahid Athar, D.M. http://www.teachislam.com/dmdocuments/33/BOOK/Sexeducation). Katika shule nyingi, elimu ya jinsia hufundishwa kuanzia darasa la 2 hadi 12 kwa kutumia mabilioni ya dola. Walimu huelezea kuhusiana na maingiliano ya kimwili bila ya kuwaeleza watoto maadili ya msingi katika hilo au namna ya kufanya uamuzi ulio sahihi. Baada ya kuelezea elimu ya maumbile ya binadamu na namna binadamu wanavyoweza kuzaliana, mada kuu huwa ni jinsi gani wanaweza kujizuia na maradhi na mimba za mapema katika maisha yao ya ujana. Kutokana na kuongezeka kwa maradhi ya Ukosefu ya Kinga Mwilini (UKIMWI).

Jambo linalotiliwa mkazo ni “maingiliano salama/ngono salama” kwa kutumia mipira ya kujikinga (kondomu). Dola za kodi hulipwa shuleni kwa kutoa bure mipira hii ya kujikinga na kuzuia maradhi (kondomu) pamoja na dawa za kuzuia ujauzito kwa watoto wanaokwenda katika vituo vya afya shuleni mwao. Mashine za kuuzia kondomu pia zimekuwa zikipatikana katika kumbi za shule pamoja na vyuo vikuu.

Majukumu ya wazazi yanapuuzwa na wakati mwingine hubezwa. Pindi watoto wa kiume wanapouliza kuhusu kujamiiana, wazazi wao (baba zao) huwakemea na kubadili mada. Kwa hiyo watoto wa kiume hujifunza mahusiano haya kutoka kwa watu wengine wa nje. Mambo maovu yenye kuhamasishwa na wasambazaji elimu (waelimishaji) hayawezi kukubalika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za dini. Kwa mujibu wa maelezo ya Shahid Athar, imani za baadhi ya waelemishaji waliopotoka ni kama zifuatazo;

a) Kukaa mtupu bila nguo (bafuni au chumbani) ni jambo zuri na njia nzuri ya kuwaelewesha watoto chini ya miaka 5 kuhusu maingiliano ya kimwili, kwa kuwa inawapa fursa ya kuuliza maswali. Hata hivyo, kwa mujibu wa tafiti ya mwaka 1997, asilimia 75 ya matukio ya kulazimisha watoto kuingiliana kimwili na watu wazima (sawa na matukio 500,000 kila mwaka) husababishwa na watu wa karibu yao (ikiwemo wazazi, rafiki zao katika familia jirani) katika mazingira ya kuizunguka familia (Abel na wenzake 2001).

b) Kitendo cha mtoto mmoja kuchezea tupu za mtoto mwenzake ni sehemu ya kujifunza, inaruhusiwa na isiwe sababu ya kumkemea au kumuadhibu. Muelimishaji huyu pia anafahamu kuwa watoto wa kiume wakiwa na umri wa miaka 12 huwabaka watoto wa kike wenye umri wa miaka 8. Muelimishaji huyu hafundishi wakati gani kujifunza kwa watoto hawa hubadilika na kuwa zinaa.

(c) Watoto wanaokamatwa wakiwa wanasoma makala zenye maudhui yasiyofaa wasifanywe kujihisi wakosefu, lakini wazazi wanatakiwa kutumia hii kama fursa ya kueleza vitu vya msingi kwa mtoto wa kiume au mtoto wa kike kuhusu mtazamo wake katika mahusiano ya kuingiliana kimwili, maadili na kutumika kwa miili katika kujamiiana. Huu ni ukosefu wa ujuzi. Makala nyingi hufikisha ujumbe kuwa jinsia ni sawa na bidhaa na kuwa wanawake ni sawa na wanasesere/midoli wa kuchezewa na wanaume. Ukweli ni kuwa, kujihisi mkosefu siyo vibaya endapo hisia hizo huweza kuwafanya watu wajutie makosa yao na kujirekebisha. Kujutia baada ya kutenda kosa (kwa lengo la kutafakari na kujirekebisha) ni njia mojawapo ya kujifunza ili kuelimisha watoto kuweza kupima matendo yao na majukumu walionayo.

d) Kama mtoto tayari ameshaanza kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na mwenzake, badala ya kumkemea mtoto aweze kuacha tabia hiyo mzazi anakuwa na wajibu wa kumlinda mtoto kiafya kwa kumpatia taarifa na njia za kuzuia kupata ujauzito pamoja na kuepukana na maradhi. Watoa elimu kama hawa huwa hawana imani kuwa kumuelimisha mtoto kuhusu masuala ya mahusiano ni sawa na kumaanisha kumruhusu mtoto aweze kufahamu vizuri mahusiano na aendee kudumu katika mahusiano ya aina hiyo. Endapo mtu ataelezwa umbile, rangi, harufu na ladha ya tunda ambalo hajawahi kulila, kwa hali ya kawaida hawezi kupata shauku ya kutaka kujaribu kula tunda hilo? Wazazi wanatakiwa wafanye majadiliano yaliyo sahihi na watoto wao kuhusiana na mahusiano ya kimapenzi yasiyo sahihi miongoni mwao. Majadiliano hayo yanaweza kuwa kama vile yanayohusu upataji wa mimba zisizotarajiwa katika jamii, matangazo yenye kuashiria uasherati, muziki au vipindi vya runinga vyenye kuhamasisha uzinzi.

Ni ukweli au uongo?

Kadri wanavyopata kufahamu ndivyo wanavyohamasika kutenda

Utoaji wa elimu ya jinsia katika shule za serikali nchini Marekani haujafanikiwa kupunguza kuenea kwa magonjwa ya zinaa kwa vijana, upataji wa mimba za utotoni wala haujabadili tabia za vijana katika kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi. Pia hata kuhamasishwa kwenda kanisani kufanya ibada hakujasaidia kuondoa matatizo hayo (Athar 1990). Mzazi usipompeleka mtoto wako katika shule ambayo haitoi elimu ya maumbile ya viumbe hai, basi lazima mtoto wako nae atakuwa amepata elimu ya jinsia na wazazi pia watakuwa wakihusishwa katika hili. Shule hutakiwa kutoa kiasi kidogo cha elimu ya maumbile pamoja na njia za kujizuia kupata ujauzito ambazo huwa ni muhimu na zenye kuhitajiwa kwa vijana wanapokuwa watu wazima. Wazazi wengi ambao ni Waislamu, wakiwa kama wazazi wenye imani nyinginezo wanaguswa kutokana na kuwepo kwa utoaji wa elimu ya jinsia katika shule za serikali ambazo hairandani na kiwango au ubora unaotakiwa kulingana na imani zao na huamini kuwa kuwapa ushauri watoto wao kuhusu njia za kuzuia ujauzito kutawapelekea wajihusishe zaidi katika mahusiano ya kimapenzi. Hofu hii ni dhana ya uongo, kwa kuwa elimu na taarifa wanayopewa watoto ni muhimu kwao.

Watu wengi, walio Waislamu na wasio Waislamu hushangazwa kubaini kuwa wake zao hawatosheki kimwili. Hali hii hutokana na wanaume wengi kuelezwa kuwa ni rahisi sana kwa mwanamke kuweza kumridhisha mwanaume kimwili wakati wanapoingiliana na kitu ambacho mwanamke anachotakiwa kufanya ni kuwa tayari na kumruhusu mwanaume wake aweze kumuingilia kwa kipindi cha sekunde kadhaa. Hata hivyo wanaume

hawakuelezwa kuwa ni swala lenye kuhitaji ujuzi na jambo la wajibu kwa mujibu wa dini kujifunza namna ya kumridhisha mwanamke kimwili. Wanatakiwa wajifunze kutokuwa na aibu katika kukabiliana na tupu za wake zao, jinsi ya kuwaandaa wake zao kabla ya kuliendea tendo la jimai na waelimishwe kuwa kujiridhisha wao pekee pasipo kuridhisha wake zao hupelekea ukosefu wa haki ya msingi ya ndoa kwa wake zao na hali hii ni katika mambo ya ukatili kwa wake.

Wazazi wengi hawapendi kuona watoto wao wakiwa wanajihusisha na uzinzi. Hata hivyo katika kipindi ambacho vijana huanza maisha ya kujitegemea hukaa mbali na uangalizi wa wazazi wao, hali hii hufanya wazazi washindwe kudhibiti watoto wao ipasavyo. Ingawaje, kutojihusisha na jambo lolote kuhusu mahusiano ndiyo njia pekee ya kuwalinda vijana, hali hii hutoweka katika kipindi ambacho watoto huanza kushiriki michezo katika viwanja vya michezo wakiwa na umri wa miaka 10. Watoto siku hizi wanaweza kujifunza kila kitu kupitia mitandao, runinga, tamthilia na kama watoto hawa wanaweza kutazama mambo mbalimbali kupitia **DVD** wanaweza kufahamu vizuri zaidi kuhusu mahusiano ya kimwili kuliko hata mzazi anavyofahamu.

UKIMWI NI MIONGONI MWA VISABIBISHI VYENYE KUONGOZA KATIKA KUSABABISHA VIFO NCHINI THAILAND

Hadi kufikia mwaka 2001, ukimwi ulikuwa chanzo kikuu cha vifo nchini Thailand, baada ya kupiku ajali, magonjwa ya moyo na saratani kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na waziri msaidizi wa masuala ya afya nchini humo Surapong Suebwong-lee. Waziri huyo hakuweka bayana idadi kamili ya watu waliofariki kutokana na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi kutokana na kuwepo kwa uhafifu wa kutoa taarifa kuhusu maambukizi sababu walio wengi hususani ndugu wa waathirika wanaoishi maeneo ya vijijini hawapo tayari kutoa taarifa hizo.

"viongozi wa serikali za vijiji wameripoti vifo vingi ambavyo havihusiani na ajali, yaani vingi vikihusishwa na moyo kushindwa kufanya kazi ipasavyo. Hali hii imepelekea kuwa na dhana potofu miongoni mwa watu kuwa watu wa Thailand hufariki kutokana na magonjwa ya moyo". Lakini tumefanya tafiti na kubaini kuwa vifo vingi sana katika maeneo ya vijijini vinatokana na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi", Waziri huyo alisema baada ya kurejea katika mkutano wa Shirika la Afya ulimwenguni uliofanyika huko Maldives. Mpango wa umoja wa mataifa wa kudhibiti maambukizi ya ukimwi wenye ofisi zake Bangkok ulieleza kuwa vifo vitokanavyo na ukimwi vitaendelea kuongezeka kutokana na watu wengi wa Thailand walishapata maambukizi hayo tangu ugonjwa huo ulipoanza kuingia miaka 10 iliyopita na wengi wao wameshaanza kuugua na kufariki. Inakadiriwa kuwa kati ya watu milioni 60 wa Thailand, takribani watu milioni 10 watakuwa wameshaathiriwa na ugonjwa wa ukimwi na takribani theluthi kati ya hao watakuwa wameshakufa kutokana na maambukizi hayo.

(AIDS EDUCATION GLOBAL INFORMATION SYSTEM 2001)

Kwanini Profesa Mmoja Aliamua Kuhama Nchini Marekani?

Profesa mmoja katika chuo cha Kiislamu cha kimataifa, Malaysia (IIUM) aliwahi kusimulia kuwa: mtoto wake ambaye anasoma darasa la tatu katika shule moja ambayo ni ya serikali huko Michigan siku moja alirejea nyumbani na kumueleza kiundani kuhusu mwanafunzi mwenzake (wa kiume) ambaye alimuona akiwa anamuingilia mwanafunzi mwenzake (wa kike) darasani. Simulizi hii ilimshawishi profesa huyu kuhama nchi ya Marekani pamoja na familia yake ya watoto watano. Elimu ya jinsia isiyozingatia maadili imepelekea vijana wengi kujiingiza katika mahusiano ya kimwili bila hata kujali athari zake. Tamaduni hii iliyokomaa inachangia kufanya vijana wadogo kuvutiwa kujihusisha na kufurahia vitendo vya uzinzi. Kuzuia vitendo vya uzinzi imekuwa ni jambo geni kwa kuwa masuala ya mahusiano na uzinzi yamekuwa ni mambo ya kawaida yaliyozoelewa.

Uelewa wa kina Mama na Watoto nchini Marekani

Vijana huchanganyikiwa sana kuhusiana na masuala ya **tabia za kimaumbile (sexual behaviour)** na hukosa mwongozo kutoka kwa wazazi na walimu wao. Ifuatayo ni baadhi ya mifano katika maneno ambayo vijana wengi husema;

- Selma mwenye umri wa miaka 16 anasema: "siwezi kumuuliza mama yangu kitu chochote kuhusu kujamiiana. Endapo nikiuliza mama hushangaa na huniuliza kwanini nimeuliza swali kama hilo. "kwanini unahitaji kufahamu?" Anasisitiza labda hadi……"
- Juliet mwenye umri wa miaka 14 anasema "mama yangu anaamini kuwa kutofahamu kabisa kuhusu mahusiano hupelekea mtu asiweze kujihusisha na mahusiano. Hupatwa na huenda wazimu pindi ninapouliza kuhusu kujamiiana. Mama yangu husema "mume wako atakufundisha kila kitu unachohitaji kujua juu ya kujamiiana".
- Louis mwenye umri wa miaka 18 anasema kuwa: "nilikuwa nikipata taarifa tofauti toka kwa wazazi wangu. Taarifa moja ilikuwa inasema "usijihusishe katika mahusiano ya kimapenzi utaingia katika matatizo! Nyingine ilikuwa ikisema "andaa njia ya mafanikio yako ukiwa bado mdogo." Natamani wazazi wangelikuwa na uelewa sahihi katika hili. Kama kuingiliana kimwili ni katika mambo bora kwetu, basi waache waseme hivyo. Ila kama siyo katika mambo mazuri kwetu, basi nawe usithubutu kufanya hivyo".
- Joshua mwenye umri wa miaka 15 anasema; "baba yangu anapenda sote tuwe wakweli. Ila ukweli na uwazi kwa upande wake huishia pale ninapoanza kudadisi kuhusu masuala ya mahusiano ya kimapenzi. Nami hushindwa kuwa mkweli katika hili mbele ya baba yangu.
- Jonathan mwenye umri wa miaka 22 anasema kuwa; "kwa watoto wa kiume waliofikia elimu ya chuo, kuingiliana kimwili ni ishara ya kupevuka au kubaleghe. Ila kwa upande wa watoto wa kike huwasaidia kupata umaarufu, kupendwa na kuwatoa katika upweke.
- Sintofahamu kuhusu kuingiliana kimwili huelezewa na kijana katika mtindo huu: " kama nitaona ucheshi bila shaka nitacheka, kama nitaona kitu chenye kuhuzunisha nitaweza kulia, nikikutana na kitu chenye kunikasirisha nitalia, lakini kama nikiona tamthilia yenye kuamsha hisia za kimapenzi sijui nifanye kitu gani?"

Mijadala ya aina hii inaashiria kuwa elimu ya jinsia inahitajika kwa kiasi kikubwa ili kuondoa tatizo la ujinga. Jamii haiwezi kuachwa huru ili iruhusu mitaala kuonesha na kupanga viwango vya elimu ya jinsia na maadili.



Maadili na Jinsia: Jana na Leo

Kumekuwa na ukinzani mkubwa katika suala la maadili miongoni mwa watu kwa sasa. Baadhi ya watu wanakiri kuwa muda umefika kukubali ukweli uliopo. Watu hawa wamepatwa na hofu juu ya magonjwa yaenezwayo kwa njia ya kujamiiana, mimba zisizotarajiwa na kupoteza heshima zao. Watu hawa wanatarajia kuepukana na matatizo haya kupitia elimu sahihi ya jinsia. Baadhi yao watawapatia vijana wao elimu ya jinsia pamoja na mbinu za kuzuia ujauzito. Baadhi ya wazazi wanakataa kutumia utaratibu wa wazazi hao. Sababu kubwa ni kuwa na imani kwamba utumiaji wa njia za kuzuia ujauzito utahamasisha vijana kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi kabla ya ndoa yaani uzinzi. Wazazi wanatambua kuwa jamii haiwezi kuhamasisha masuala ya mahusiano ya kimwili kwa vijana kwa kuwa hali hii inaweza kuhatarisha mahusiano katika jamii na ustaarabu wao.

Jukumu kubwa kwa vijana ni kupata elimu na kujiandaa kuwa watu wema na kuwa tayari kuwa katika maisha ya kifamilia. Baadhi yao huona mijadala ya mahusiano ya kimwili inapingana na maadili ya jamii na hivyo huchukuliwa kuwa ni kitu kibaya. Baadhi ya wazazi huhisi kuwa mijadala ya aina hii inaweza kuchangia kuongezeka kwa vitendo vya kujamiiana ingawaje mijadala hii huenda ikawa inakusudia kumtambulisha kijana jinsi ya kujizuia na vitendo vya kujamiiana. Mzazi mmoja aliwahi kuzungumzia namna ya kuwa kigezo chema kwa watoto kwa kutumia maneno haya “ni pale tunapofikia hatua ya utu uzima ndipo huwa tunajiweka katika hali ya kuigwa kama mfano kwa watoto na kuwataka wao waoneshe tabia nzuri, watoto wataweza kuwa na tabia kama tunavyohitaji.”

Katika maisha na riwaya, hakuna maadili ya kutosha kuhusu mahusiano ya kimwili. Nchini Marekani pamoja na nchi nyingine, ,somo la mahusiano ya kimwili limekuwa likifundishwa bila kukatazwa, somo hili linafundishwa shuleni na kujadiliwa nyumbani.

Katika jamii somo hili pia linakubalika na vijana hujifunza. Kwahiyo, watoto wa kiume wamekuwa wakishutumiwa wakati watoto wa kike wanasimamiwa. Watoto wa kiume siku hizi wanaweza kumiliki gari na watoto wa kike wamekuwa na uhuru zaidi. Vishawishi vinapoongezeka bila kuwepo usimamizi kwa vijana, je kwa namna gani vijana hawa wataweza kufuata maadili?

Katika kipindi cha nyuma, watoto wa kike walikuwa wakihamasishwa kujihifadhi dhidi ya watoto wa kiume, hivyo kuwafanya wasiweze kujihusisha

na vitendo vya kimapenzi bali walikuwa wakishikana kimahaba, kubusu au kukumbatiana tu. Hali hii ilitokana na uelewa na ridhaa ya watoto wa kike pamoja na jamii husika. Kwa sasa vijana wengi wamekuwa wakihoji mbinu hii. Kwa sasa vijana wa kiume hawapo tayari kwa hili kutokana na kugubikwa na hisia zaidi kupitia wanachokiona katika runinga, tamthilia na majarida wakati watoto wa kike nao hawapo tayari kwa hili kwa kuhofia kuongopewa na kupata matatizo kwa upande wao. Watoto wa kike waliofikia elimu ya chuo kikuu hujikuta wanapata ugumu kutunza ubikira wao. Watoto wengi wa kiume hukataa kuwaposa na huwaona kama watu wa zamani. Wale ambao wanakuwa na msimamo wa kujihifadhi mpaka waolewe hujikuta wanatengwa na jamii. Katika hali hii, yule aliye bikra hujihisi hayupo sawa na wengine. Hali hii hupelekea wachache sana wenye maadili kuweza kuendelea kujitunza. Kikubwa cha kusikitisha, watoto wengi wa kike huanza kuingia katika mahusiano ya kimwili kwa kuzini siyo kwa ajili ya kuhitaji kufanya hivyo isipokuwa ni kwa ajili ya shinikizo. Katika kipindi cha nyuma, watoto wa kike waliweza kujihifadhi kwa hofu ya kupata ujauzito. Kwa sasa hali hii haipo tena. Dawa za kuzuia maradhi na ujauzito zinauzwa hadharani pamoja na baadhi ya shule na makanisa hugawa mipira ya kuzuia maradhi na ujauzito bure kabisa.

Baada ya kurejea katika safari ya chuo, Jason mwenye umri wa miaka 18 alimwambia baba yake kuhusu maisha na mapenzi kuwa “nimegundua tofauti iliyopo kati ya watoto wa kiume na watoto wa kike. Watoto wa kike hutumia mbinu ya kutofanya mapenzi na watoto wa

kiume ili kushawishi wapendwe wakati watoto wa kiume hutumia mbinu ya kuwa wamewapenda sana ili waweze kupata fursa ya kuwaingilia watoto wa kike kimwili. Filosofia yangu ni kuwa wapende watoto wa kike kisha waache.” Baba yake akauliza “kitu gani kinatokea endapo wewe na mwingine mkampenda mtoto wa kike kisha baada ya muda mkamuacha?” “Mimi hilo halinihusu na wala sihitaji kulifikiri”, Jason alisema.

Fikiria jambo hili, katika Bara la Asia kuna msemo unaosema kuwa “ukinusuru mtu kutoka katika kifo basi unahusika katika kuokoa maisha yake”. Kama ukimshawishi mtoto wa kike ajiingize katika mapenzi, hisia zake juu yako zitakuhusu” baba yake Jason alisema.

Baba yake Jason akakiri kuwepo kwa kanuni: ukweli, uwajibikaji katika mahusiano ya binadamu. Katika hali zote ngumu au rahisi, kijamii au kimapenzi uwajibikaji unahitajika.



Kwanini Elimu ya Jinsia? Ni Lazima Kufundisha?

Vijana wanatamani wajifunze kila kitu kuhusu jinsia. Wamekuwa wakishangazwa na kuwa njia panda hivyo wanahitaji majibu binafsi yenye uhalisia. Wanapopata fursa ya kujadili masuala ya jinsia, vijana huzungumza kiuhuru na kujifahamu zaidi. Huhitaji kujua kuhusu maadili, maana kuhusu jinsia zao.

Swali la msingi la kujiuliza ni: je elimu ya jinsia ifundishwe kwa vijana? Muda umeshapita wa kujiuliza swali la aina hii. Suala la jinsia limeshakuwa likifundishwa katika mitandao, shuleni na hata mitaani. Kwa kutumia maneno na picha, watoto hujikuta wanafundishwa kuhusu masuala ya jinsia na mahusiano ya kimwili bila kuzingatia maadili. Runinga pamoja na watu wa rika tofauti mitaani hueneza taarifa isiyo sahihi katika hili. Wafanya biashara wanaojihusisha na vitu vyenye kuonesha picha za ngono wanahusika katika kueneza uhalisia na kuamsha hisia kuhusiana na vitendo vya kujamiina bila kificho. Watu waliowatangulia vijana umri nao huwaeleza vijana hawa uzoefu wao katika masuala ya kujamiiana kiuhalisia na hata kinadharia wakati mwingine.

Ni wazazi na walimu pekee ndiyo wanaokuwa na hofu ya kuwaeleza vijana kuhusu mahusiano ya kimwili na kujamiiana katika wakati husika. Elimu ya jinsia imegawanyika katika sehemu kuu mbili; taarifa na maadili. Maadili huweza kufundishwa vizuri zaidi nyumbani. Wataalamu wanaweza kutoa taarifa kuhusu elimu ya jinsia kiufasaha zaidi. Siyo kila swali linalohusiana na masuala ya kujamiiana linatokana na hitajio la kutaka kuelewa. Baadhi ya vijana huhitaji kuwafedhehesha wazazi wao ambao hawapendi kutoa majibu mabaya yenye kuwaudhi. Wazazi hawawezi kujua ukweli wote, au wakawa wanajiamini asilimia zote na kujua masuala yote juu ya mahusiano ya binadamu. Taarifa inayohitajiwa na vijana ni vizuri ikatolewa na maswali mengine yaelekezwe kwa wataalam husika wa masuala hayo kulingana na maswali yaliyoulizwa. Wazazi wanatakiwa kuhamasisha watoto wao kushiriki katika mijadala inayohusu mahusiano ya kimwili ama jinsia siyo pale tu kunapokuwa na ufadhili wa shule bali hata pale kunapokuwa na ufadhili kutoka katika kanisa, msikiti, na vituo vya kijamii. Taarifa inayotolewa kwa malengo na ukweli inaweza kusaidia kupunguza uhasama na kuongeza uaminifu

kati ya vizazi. Watu wazima wanaweza kuaminiwa na vijana na vijana wanaweza kuwaamini watu wazima japokuwa kuna tofauti ya umri kati yao. Watu wazima hujali sana kuwaona vijana wakiwa katika hali nzuri na hupenda kubadilishana nao mawazo kuhusu utu.

Kwa upande mwingine, mtu anaweza kusema kuwa: je watoto wanahitaji kupata elimu ya jinsia? Je unafundisha mtoto wa bata kuogelea au unamuweka katika maji na kumuacha aogelee mwenyewe? Kwa kipindi takribani cha miaka zaidi ya elfu, watoto wa kike wamekuwa wakijihusisha katika mahusiano ya kimwili na watoto wa kiume bila kupewa elimu rasmi kuhusu kufanya hivyo. Katika ustaarabu wa kizamani, elimu ya jinsia na kujamiiana ilianza kwa kujaribu na kubaini makosa baada ya kufunga ndoa. Hata hivyo kuwa na idadi fulani ya watoto siyo ishara ya upendo. Elimu ya kujaamiiana na jinsia inayofaa ni muhimu katika kuleta ndoa yenye furaha.

Je, nani afundishe elimu ya jinsia? Kila mtu anayo nafasi yake katika jambo hili. Wazazi wanatakiwa watambue ukweli na matatizo yaliyopo na kufanya mambo yao ya wajibu. Baba anao wajibu wa kumjibu mtoto wake wa kiume maswali yake anayouliza kama ilivyokuwa kwa mama kwa mtoto wa kike. Hatuwezi kutegemea elimu ya jinsia itolewayo shuleni pekee au ile inayotolewa katika vyombo vya habari. Ni jukumu letu kuongezea elimu hii kwa kuongeza maadili yanayofaa kuwepo ndani yake. Walimu wa shule za Kiislamu/Kikristo, matabibu wa familia, maimamu na viongozi wa dini kanisani na msikitini wana kazi ambazo nao wanaweza kuzifanya. Ndani ya familia, dada anakuwa na jukumu kwa wadogo zake na kaka pia anakuwa na wajibu dhidi ya wadogo zake. Wazazi hawatakiwi kuwa kimya kuhusu elimu ya jinsia. Ukimya hutoa ujumbe ambao siyo sahihi kwa watoto. Watoto huchanganywa na mambo yenye kukinzana ambayo wanasikia kutoka kwa watu wasiowafahamu. Wanaweza kuwa na mtazamo hasi kuhusu mahusiano ya kimwili ambayo huweza kuwaathiri hata wanapofikia utu uzima. Kuzuia kutoa elimu ya jinsia siyo kitu sahihi kwa sasa. Lazima tuwe wakweli na wawazi. Wazazi ambao wanazuia watoto wao wasipate elimu ya jinsia ni sawa na kuwa wanapiga vichwa vyao ukutani. Ni vyema watoto wao wakajifunza kutoka kwa watu wazima ambao wana maadili katika utoaji wa elimu ya jinsia, wenye uwezo wa kuondoa mikanganyiko na vishawishi hasi kutokana na mazingira.

Qur'an pamoja na hadithi za Mtume zinaelezea elimu ya jinsia kiufasaha na kwa hekima ya hali ya juu. Kuingiliana kimwili (Jimai) siyo neno baya, bali ni kitu muhimu katika maisha ya binadamu. Qurani imejadili katika lugha ya heshima zaidi: kuzaliana, uumbaji, maisha ya familia, ada (hedhi) na kukohoa ama kutoa mbegu za uzazi wakati wa jimai. Hata Mtume Muhammad (s.a.w) amekuwa akijadili na maswahaba wake kuhusiana na jimai katika mazingira tofauti ya maisha yao. Sababu inayowazuia wazazi wasiweze kujadili jimai na watoto wao kunatokana na namna wao walivyolelewa. Wazazi wanaweza kuwa hawana ujuzi kuhusu jimai au wanashindwa kujiamini na kuwa huru katika swala hili au kushindwa kulielezea.

Kitu Gani Wafundishwe Watoto?

Wazazi wengi huwaandaa watoto wao wa kike pindi wanapoingia katika kipindi cha ada zao na watoto wa kiume pindi wanapoanza kupata ndoto nyevu. Baadhi ya wazazi huwa hawawaandai watoto wao kabisa na hali hii hupelekea watoto kuwa na hofu. Kutokwa na damu sehemu za siri au kitu chochote hupelekea mtoto kujihisi kuwa amepata maradhi fulani au jeraha hususani kama alianza tabia za kujichunguza au kujichua, vijana hujihisi kama wakosefu kwa kujiletea matatizo wao wenyewe. Utokaji wa damu uliokithiri au ute huwafanya waweze kuamini kuwa kuna viungo katika maumbile yao havipo sawa ama vimedhurika na huwa na aibu pamoja na hofu kueleza bayana. Mtoto mmoja wa kike aliwahi kuvumilia hali hii ya kutokwa na damu nyingi huku akiwa anatumia kitambaa kwa kipindi cha miezi kadhaa kwa kudhani kuwa ni mgonjwa na alikuwa na hofu kueleza kwa watu. Mwisho wake, mwalimu aligundua baada ya kuona madoa ya damu katika nguo zake na baadaye aliweza kumsaidia. Alikuwa akiziosha huku akiwa na hofu ya mama yake kuweza kumuona.

Baadhi ya kina mama wanatakiwa wafikiri vyema mitazamo yao mibaya kuhusu hedhi, kabla ya kuanza kuzungumza kwa watoto wao wa kike juu ya masuala hayo. Ni muhimu pia watoto wa kiume wakafahamu kuhusu ada ya watoto wa kike. Hii itaweza kumsaidia kijana baadaye aweze kuendana na mkewe pale anapokuwa anapata maumivu, ishara pamoja na hasira katika kipindi cha ada. Haifai kuchukulia kuwa ni jambo lisilofaa au lenye kufedhehesha na kuwatenga watoto wa kike.

Mtume Muhammad (s.a.w) anatuasa kuwa tusiwafanye watoto wa kike waliokuwa katika ada zao wajihisi wachafu. Kitu ambacho hakiruhusiwi kwao ni kuwaingilia kimwili tu. Lakini kwa kuwa wanaweza kujisitiri katika tupu zao na kuzuia damu zisiweze kuwapata waume zao,wanandoa bado wanaruhusiwa katika kipindi hiki kukidhi haja zao kwa namna nyingine pasipo kuingiliana.

Katika mazingira machache yasiyo ya kawaida, elimu ya jinsia katika shule nyingi za serikali nchini Marekani imekuwa miongoni mwa masomo yafundishayo namna ya kutumia mipira ya kondomu, jinsi ya kujikinga na maradhi na namna ya kutoa ujauzito. Imani iliyoenea nchini Marekani ni kuwa vijana wanahitaji kujamiiana kwahiyo ni bora wafundishwe namna ya kujizuia kuepukana na matatizo yanayoweza kusababishwa na jimai. Maadili mara chache sana huzingatiwa na mara zote huwa hawazingatii mitazamo ya dini, kiroho wala njia ambazo zinamridhisha Mungu. Elimu ya jinsia hutolewa katika madarasa yenye mkusanyiko wa watoto wenye jinsia tofauti, hivyo husaidia kuondoa aibu miongoni mwao. Hata

katika madarasa ambayo hayana mchanganyiko wa jinsia, walimu huwashawishi watoto wajifunze kwa vitendo ikiwemo namna ya kuingiliana, kubusu na kujichua. Watoto wa Kiislamu ambao hawakuwa wakifahamu lolote katika masuala haya hujikuta wanashindwa kujua nini cha kufanya na hupatwa na fedheha na kushindwa hata kuuliza kwa wazazi wao.

Muingiliano wa kimwili usiokubalika kisheria! Jinsi ulivyoenea!

Kwa mujibu wa dini ya Kiislamu, tendo lolote la jimai pasipo kuwa na ndoa (zinaa) ni kosa kimaadili na kidini. Baadhi ya watu husema kuwa zinaa inaposababisha kupatikana mtoto huwa na madhara makubwa sana kuliko hata kosa la mauaji ya kukusudia. Zinaa ina athari kubwa sana katika familia na vizazi vinavyokuja. Athari zake ni kama vile: kupata maradhi, kutoa mimba, kuzaa mtoto mwenye matatizo ya kiafya (kama maradhi yanayoenea kwa njia ya kujamiiana yatakuwa yamemuathiri mama wa mtoto), kupatikana mtoto wa nje ya ndoa, familia ya mzazi mmoja, kuvunjika kwa familia, kutofahamika baba wa mtoto (nasaba), kukosekana kwa uaminifu na kuongezeka ukahaba (kujiuza kimwili).

Zinaa hushusha heshima ya mtu katika jamii pamoja na ushirikiano katika jamii husika. Jamii ambayo inaruhusu kuvunjwa kwa mila za miingiliano ya kimwili hujikuta inakuwa na mila mbaya zaidi (ikiwemo biashara za kujiuza kimwili) ingawaje ni kosa kisheria. Mila zinapokiukwa kwa kiasi kidogo hupelekea kukomaa kwa ukiukwaji wa taratibu hadi kufikia katika kiwango kikubwa. Uzinzi ni kosa kubwa kisheria ambalo mtu akitenda anaweza kuadhibiwa na Mungu Muumba hapa duniani na baadaye huko akhera.

Dini ya Kiislamu haijachukulia kosa la uzinifu kama dhambi ya mtu pekee isipokuwa pia ni kosa dhidi ya jamii mtu anayoishi. Kama uzinzi ukiruhusiwa basi huweza kuathiri msingi wa jamii kuanzia katika ngazi ya familia. Adhabu ya kosa la uzinzi katika Qur'an ni bakora 100 na adhabu hii hutekelezwa hadharani kila mtu akiwa anashuhudia. Kosa la uzinzi limekithiri sana na ndiyo maana hapo zama za kale ilihalalishwa kupiga mawe mtu aliyezini hadi kufa (Biblia, kumb. la Torati 22:23-24).

Hata hivyo adhabu hii haijatolewa katika Qur'an na wanazuoni wengi wameonekana wakiikosoa. Kutokana na ukubwa wa kosa hili na athari zake hususani katika kuondoa heshima ya mtu, ni lazima mashahidi wapatikane wanne ambao ni wakuaminika, waliokuwa na uelewa sahihi waweze kutoa ushahidi wao kuhusiana na tuhuma za uzinifu zinazomkabili mtu.

Kuhitajika kwa idadi hii ya mashahidi ni kwa lengo la kulinda wadhifa binafsi wa mtu, heshima ya mtuhumiwa pamoja na kuashiria kuwa kosa hili siyo la mtu pekee bali pia ni kosa la jamii nzima.

Watu hawana hatia katika kosa hili hadi pale mashahidi wanne wapatikane kutoa ushahidi dhidi yao. Kama mashahidi waliopo ni chini ya wanne basi ushahidi huo ni batili na wanazuoni wanakubaliana kuwa ushahidi wa vinasaba unaweza kutumika kuthibitisha kosa la uzinzi. Uzinifu unaofanyika waziwazi mbele ya mashahidi wanne au zaidi ni sawa na kulingania maovu katika jamii na ni mbaya zaidi ya lile kosa la uzinzi linalofanywa kwa siri na mtu ili akidhi matamanio ya nafsi yake.

Uzinzi kwa wanandoa ni ukiukaji wa mkataba wa ndoa.

Uzinzi kwa wanandoa ni ukiukaji wa mkataba wa ndoa. Takribani nusu ya ndoa ambazo zimefungwa nchini Marekani zimeshavunjika (CDC 2012). Nchini Uingereza, katika jiji la Uingereza na Wales kwa kila saa moja kuna talaka 13 zinatolewa, hiyo ni kwa mwaka 2012 (jumla ya talaka 11,840 zilitolewa) na kwa kila talaka moja kati ya saba wanandoa hao hupeana talaka na sababu kubwa ni kuwa wanandoa wengi wamekuwa na mahusiano ya kimwili nje ya ndoa zao (Utafiti Kutoka Ofisi ya Taifa 2014). Watu wameonekana kutofuata maandiko ya Biblia wala Qur'an. Biblia inasema kuwa "usizini" na Qur'an pia inasisitiza kuwa "usiikurubie zinaa", hii inamaana kuwa siyo tu tusizini bali tujiepushe na kila kitu chenye kupelekea zinaa.

Vitu vyote vyenye kushawishi zinaa kama vile kujihusisha katika mahusiano na kuwekeana ahadi za mapenzi, uvaaji wa nguo fupi zenye kubana au kuonesha maumbile, kutojihifadhi tupu,na kutazama filamu za ngono vyote ni miongoni mwa vishawishi vya zinaa hivyo haviruhusiwi. Mavazi ya kike na kiume yote yamewekwa kisheria ili kuepusha vishawishi na matamanio kwa yule mwenye kuyatazama. Baadhi ya watoto wa kiume hushindwa kujizuia na hatimaye hutenda dhambi na wakati mwingine hufikia hatua ya kubaka kabisa.

Katika masuala ya kuingiliana kimwili, mitazamo huwa na nguvu zaidi ya maneno. Nini mtazamo halisi wa jamii kuhusu kuingiliana kimwili? Nini maana ya maadili? Kama jamii tunakosa mtu ambaye tunaweza kumfanya kigezo chema katika maadili. Tunachukulia vijana kuwa wanachanganywa na maelezo tofautitofauti yaliyopo katika jamii, kwa upande mwingine jamii imetawaliwa na mawazo ya mahusiano ya kimwili na kushawishika kwa pesa. Kwa lengo la kujifurahisha na kupata manufaa ya kiuchumi, filamu za ngono huoneshwa, hutangazwa na hutumiwa katika matangazo ya kuvutia biashara. Kwa upande mwingine, jamii inajielezea kuwa ina imani katika kujizuia na mahusiano ya kimwili kabla ya ndoa. Hali hii huchochea mgongano na mgogoro wa mawazo. Kama jamii inaruhusu vishawishi wazi wazi, haitoweza kuzuia miingiliano ya kimwili isiyozingatia sheria na taratibu. Vijana wengi wana mitazamo huru inayohusu mahusiano ya kimapenzi, katika kuingiliana kimwili na mtu yoyote. Hali hii hupelekea kuenea kwa uzinzi na ongezeko la talaka.

Natalia mwenye umri wa miaka 19, mwanafunzi wa chuo mwaka wa pili anaelezea sintofahamu yake kuwa; (Faber na Mazlish 1982).

Mimi na wazazi wangu tunaishi pasipokuwa na sheria ya mazungumzo. Hakuna maswali wala majibu. Huwa hawahitaji kujua nini kinaendelea kuhusu mimi na mimi wala siwaelezi chochote. Mimi ni msichana mzuri mwenye maadili. Ni vigumu sana kwangu kupata rafiki ambaye anaweza kunipenda kama rafiki. Napenda sana mahusiano ya kimapenzi. Mwanzo wapenzi mnapokutana huwa ni furaha. Pia vishawishi hufuata pale unapoalikwa katika tafrija huku kukiwa na vinywaji pamoja na vilevi. Ni rahisi sana kuweza kuishia kulala na mtoto wa kiume kwa wakati huu. Na wao huwa wanasema " ukifanya hivyo dunia itakuwa na furaha pamoja na wewe, ukikataa utalia peke yako". Kwa hiyo mimi nimejawa na ukarimu na pia nina mrundikano wa machozi.

Kitu kibaya ni kwamba baadhi ya watoto hawawezi kusema kilicho sahihi katika mabaya yaliyopo. Nchi ya Marekani inakabiliwa na tatizo la maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi, matumizi ya dawa za kulevya na vurugu. Matatizo haya hayawezi kuisha hadi pale shule zitakapoanza kufundisha tabia njema. Mtaala wa shule lazima uandae misingi ya maadili ambayo pia inahitaji miongozo ya wazazi. Shule ambazo zinaweza kujenga na kusimamia maadili ni bora sana katika jamii yenye afya kuliko kundi la madaktari, washauri, askari polisi au watoa huduma katika masuala ya kijamii.

Mila za Ibrahimu zinakataza Uzinzi

Mfuatano ufuatao wa matukio kiujumla au kwa kiasi fulani hutokea kwa kizazi cha vijana
Rafiki wa kiume — rafiki wa kike → kishawishi na kutongoza →kuingiliana kimwili kabla ya ndoa → kupoteza ubikira na heshima →mimba zisizotarajiwa → kutoa mimba au ndoa za utotoni au mtoto haramu na kulelewa na mtu wa nje → umasikini na ugumu wa maisha →kuvunjika kwa familia kupata na maradhi →kifo.

Mtu ambaye ameanzisha mahusiano ya kimwili na watu wengi anaweza kupata kaswende, kichocho au ukimwi na kuweza kueneza ugonjwa kwa mpenzi wake ambaye ametulia. Kama mke atapata ujauzito, ugonjwa unaweza kumuathiri mtoto milele. Mtoto anaweza kuzaliwa akiwa kiziwi au mlemavu wa viungo. Kama atakuwa amemuambukiza ukimwi basi mwanaume huyu atakuwa anahusika na vifo vya watu watatu, kifo cha mkewe na mtoto wake pamoja na kifo chake mwenyewe.

Zinaa inasababisha uharibifu wa mtoto. Mzazi wa kiume anaweza kupata mtoto kwa mwanamke fulani na kisha akakataa kuwajibika kwa kuwa hajamuoa mwanamke huyo. Kwa udanganyifu wake, anamkosesha mtoto wake haki ya kupata malezi mazuri kutoka kwake. Kadhalika mwanamke ambaye amezini na mtu ambaye sio mume wake anaweza kupata ujauzito. Kama atakuwa msiri katika hili, kamwe hawezi kuficha ukweli huu dhidi ya nafsi yake. Mtoto naye hatoweza kumfahamu baba yake wala ndugu zake.

Baba halisi wa mtoto hatoweza kuchukua nafasi yake kama baba wa mtoto na mume halali aliyesalitiwa na mkewe anachukua nafasi na wajibu ambao siyo wake kwa mtoto. Kwa udanganyifu wa mwanamke huyu, huweza kuzuia haki ya kila mtu kati yao kuweza kujua familia yake. Baba wa mtoto aliyesalitiwa pamoja na mtoto wake wanaweza kufahamu ukweli wa mambo kutokana na mfanano wa damu zao au vinasaba. Mwanamke huyu pia anaweza kupata ukimwi na kuhatarisha maisha ya mumewe na mtoto wake. Kwa kawaida mwana ndoa mwenye mahusiano nje ya ndoa huweza kubainika na hii hupelekea kutalikiwa kitu ambacho huathiri watoto, familia na jamii kwa ujumla.

Katika sheria ya Kiislamu, adhabu kwa wazinifu hutolewa na mahakama tu ambayo inatumia sheria ya Kiislamu. Watu hawana mamlaka na hivyo hawawezi kuchukua sheria mikononi mwao isipokuwa wanatakiwa waende katika vyombo husika vyenye mamlaka wakiwa na ushahidi unaokubalika. Kwa bahati mbaya baadhi ya kina baba wamekuwa wakiwaua watoto zao wa kike ambao wamepata ujauzito kabla ya kufunga ndoa pamoja na wapenzi wao. Baadhi yao wakati mwingine huhisi tu kuwepo kwa tabia zisizokubalika na mara nyingi watoto wa kiume hufanikiwa kuwatoroka.

Kuna shinikizo kubwa kwa vijana kuwataka watulie kuwasikiliza wakubwa zao pamoja na kusikiliza vyombo vya habari. Kama wangekuwa wanafanya hivyo, basi matatizo ya aina hiyo yangeweza kuepukika. Watu wasio katika ndoa ambao wanafanya uzinzi huweza kugundua kuwa hakuna ulazima na umuhimu wa kuingiliana kimwili. Kwa ajili ya kuridhishana ndani ya muda mfupi, hujikuta wameingia katika matatizo makubwa na majonzi mazito. Haya huwa ni maamuzi mabaya ambayo wamewahi kuyafanya katika maisha yao. Na siku ya hukumu (Qiyama) watu hawa watakuwa wenye kuwajibishwa kwa walioyatenda mbele ya Mungu Muumba.

Hikima ya hukumu ya kisheria kuhusu Uzinzi

Ingawaje inaonekana ni kitu kigeni kwa sasa kuzingatia uzinzi kama kosa la jinai, bado katika uislamu ni kosa la jinai huku ikiwa inaelezewa jinsi gani uzinzi unavyoweza kuleta athari katika maisha ya binadamu na jamii yake. Jambo hili linahitaji uelewa wa kina juu ya asili ya wanadamu. Tutaangalia vitu vikuu vinne katika kuelezea hili; navyo ni Wahyi, akili, asili na matendo.

Lengo la sheria ya adhabu ni kuleta amani na usalama katika jamii. Pindi kosa linapofanyika likawa linahusiana na mali za watu au mauaji, sheria ya Kiislamu inahitaji kuwepo kwa mashahidi wawili waweze kuthibitisha. Hata hivyo,

kosa linalohusu uzinzi, mashahidi wanaohitajika ni wanne. Je hii ni kwa nini? Sababu kubwa siyo kuwa kuna utendaji wa dhambi kwa mtu binafsi, bali pia kosa hili limetendeka katika jamii na kuna madhara katika jamii hiyo ndiyo maana sheria inahitaji wawepo mashahidi wanne. Kutenda kosa la aina hii bayana ni chanzo cha kueneza uovu katika jamii.

Pia kuna mahitaji ya kuzuia maovu na kudumisha wadhifa wa mtu na heshima. Kuna tofauti kubwa ya kutenda kosa kwa usiri ili kukidhi matamanio ya nafsi ya mtu na kutenda dhambi hadharani kila mtu akafahamu na kuona kwa lengo la kulingania uovu na kushusha heshima na usalama wa watu. Mfano mzuri unapatikana katika kipindi cha khalifa wa pili 'Umar ibn al-Khattab wakati akiwa anapita katika nyumba moja alisikia watu wakiimba na wakinywa vilevi ambapo yeye (Khalifa) alipanda juu ya ukuta na kuwachunguza.

Ingawaje alikuwa na nia ya kuwafungulia mashitaka na kuwahukumu kisheria, watuhumiwa walipinga kitendo hicho na kudai kuwa Khalifa hana haki ya kupanda ukuta na kuwachunguza. Khalifa alikiri kuwa amekosa na hivyo hakuweza kuwahukumu kwa makosa yao waliyotenda. Katika masuala ya uzinzi, kama kuna mashahidi chini ya wanne, basi hawatakiwi kusema chochote kuhusu watu fulani kuwa wamezini kinyume na hapo watakuwa na makosa ya udhalilishaji katika jamii. Uislamu unakemea uhamasishaji maovu na tabia mbaya kwa kuwa kuhamasisha kunaweza kufanya maovu yakafahamika kwa watu hali ambayo inaweza kupelekea yakaonekana kama ni mambo ya kawaida na kukubalika na kuvumiliwa katika jamii.

Maradhi yanayoenea kwa njia ya Kujamiiana

Vijana wanaweza kupata magonjwa aina ya (**mononyukleosis**) kutokana na kubusu, ugonjwa huu hushambulia ini na humfanya muathirika aweze kupata matibabu akiwa amelazwa kwa majuma kadhaa. Magonjwa mengine pia ni kama vile;

- Kaswende, ambao huathiri na kufanya mume na mke washindwe kupata watoto
- Kichocho, ambao huweza kuathiri karibu kila sehemu ya kiungo cha binadamu
- Ukimwi (upungufu wa kinga mwilini) ambao husababisha kifo chenye maumivu polepole. Matumizi ya dawa husaidia kupunguza ukali wa maambukizi kwa miongo kadhaa.

Kuwa wanandoa waaminifu ambao hawana mahusiano nje ya ndoa yao hawawezi kupata maambukizi ya magonjwa kama haya. Magonjwa ya zinaa huenezwa na wasiokuwa katika ndoa ambao huweza kuwa na wapenzi wengi au hata wanandoa wasio waaminifu katika ndoa zao wenye mahusiano nje ya ndoa. Katika miaka ya 1940 magonjwa maarufu yenye kuenea kwa kujamiiana yalikuwa ni kichocho na kaswende. Kwa sasa magonjwa mengine yamekuwa yakijitokeza karibu kila mwaka na ni vigumu sana kuyatibia. Mfano ukimwi na **herpes** hakuna tiba inayofahamika.

Magonjwa haya yamekuwa hayana kizuizi kwa sababu wanajamii wamekiuka misingi ya asili ya ubinadamu kutokana na kukithiri kuliko dhahiri kwa vitendo viovu/ vitendo vya dhambi katika jamii.

Mtume Muhammad rehema na amani ziwe juu yake amesema kuwa;

"Endapo uchafu wa zinaa utakithiri katika jamii na watu katika jamii hiyo wakawa wameridhia, basi magonjwa ambayo hayajawahi kuwepo yatajitokeza na kuenea miongoni mwao." (Ibn Majah)

Matatizo mengine ya kuingiliana kimwili kabla ya ndoa ni pamoja na kupata msongo wa mawazo kutokana na kuumizwa kihisia katika mapenzi, saratani ya mfuko wa uzazi na mimba zisizotarajiwa utotoni. Majeraha pia yanaweza kupatikana pale viungo vya uzazi vinapokuwa havijawa tayari na kukomaa vizuri. Baadhi ya majeraha haya huweza kudumu kwa muda mrefu. Saratani ya mfuko wa uzazi inasemekana kuwa inatokana na tabia ya mtoto wa kike kuwa na mahusiano ya kimwili na wanaume wengi katika umri mdogo.

Mapinduzi ya jinsia yaliyowahi kutokea nchini Marekani miaka ya 1960 imeongeza gharama za huduma za afya. Kwa mujibu wa umoja wa wataalamu wa afya ya jinsia Marekani, katika mwaka wa 2008 ilikadiriwa kuwa magonjwa ya zinaa yalienea kwa watu takribani milioni 110, wakiwemo wanaume na wanawake nchini Marekani na kila mwaka kulikuwa na kijana mmoja kati ya vijana wanne alipata maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Umoja huo unaeleza kwamba "takriban asilimia 15 ya wanawake wa Kimarekani ambao wana matatizo ya uzazi yaliyopelekea kuharibika kwa mirija ya uzazi itokanayo na homa ya viungo vya uzazi, ambayo ni matokeo ya kutotibika kwa magonjwa ya zinaa.

Mwaka wa 2012 ziliripotiwa kesi takriban 1,422,976 za ugonjwa wa klamidia na kesi za ugonjwa wa kisonono katika nchi ya Marekani., badala ya magonjwa ya zinaa (CDC). Pigo la upungufu wa kinga mwilini limekuwa nyongeza katika hofu zetu. Katika nchi ya Uingereza kuna makadirio ya watu takriban 440,000 ambao wamegundulika na ugonjwa wa ukosefu wa kinga mwilini kwa mwaka 2014. Ugonjwa hatari kabisa katika magonjwa ya upungufu wa kinga mwilini ni klamidia. Katika karne zilizopita, ugunduzi juu ya kisonono, kaswende, magonjwa ya viungo vya uzazi, malengelenge katika viungo vya uzazi, yameongezeka kwa kiwango kikubwa hususani kwa wanamume. Wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja na wanaume wenzao wameendelea kuwa waathirika wakubwa wa magonjwa ya zinaa: kati ya mwaka 2013 na 2014 kumekuwa na asilimia 46 % ya wagonjwa wa kaswende na asilimia 32% wagonjwa wa kisonono miongoni mwa hao wanaume. Hali iliyochangia 81% ya waliogundulika na kaswende na 52% ni ya wale waliogundulika na kisonono. (Kwa Mujibu wa Kituo Cha Afya Uingereza 2015-Public Health England 2015).

Sababu hatarishi zenye kupelekea saratani ya mfuko wa uzazi: ni kuwa na wapenzi wengi na uvutaji wa sigara, bangi. Wanawake ambao wapo katika mazingira hatarishi zaidi wanatakiwa wafanyiwe vipimo mara kwa mara. (Tafiti ya saratani nchini Uingereza).

Marekani ni nchi inayoongoza kuwa na magonjwa ya zinaa yanayotibika kwa nchi zenye maendeleo ya viwanda. Kuna takribani kadhia milioni 20 ya ugonjwa unaosababishwa na zinaa kwa kila mwaka (CDC) magonjwa ambayo yanaweza kupelekea mtu kupata ugumba na hata kufa (Ofisi ya Afya kwa Vijana).

Mahusiano ya Mtoto wa Kiume na Mtoto wa Kike

Watoto wadogo huwa hawajali ni mtu wa aina gani wanacheza nae ingawaje kuanzia umri wa miaka 8, watoto wa kike hupenda kucheza na watoto wa kike wenzao na watoto wa kiume hupenda kucheza na watoto wa kiume wenzao. Watoto mara nyingi huunda urafiki madhubuti kuanzia umri wa miaka 10 na 12 na hudumisha urafiki wao katika kipindi chote cha ujana wao (D'Oyen 1996). Pindi mtu anapokuwa mkubwa, urafiki wake na watu wengine huendelea kuwa ni kitu muhimu. Endapo kila kitu kinaenda sawa katika familia, anakuwa na uhusiano wa kirafiki na baba yake, kaka zake, wajomba zake, binamu zake na baadaye watoto wake waliofikia utu uzima. Mtoto wa kike nae hujihisi faraja katika urafiki wake na watu fulani kama vile mama yake, dada zake, ndugu zake, jirani zake na hata wanawake wengine.

Urafiki wa kawaida unaruhusiwa ingawaje unatakiwa uwe na mipaka. Mtoto wa kiume na mtoto wa kike ambao hawana uhusiano wa damu (mahram-mtu ambaye hamruhusiwi kuoana) hawatakiwi kukaa pamoja faragha kwa muda; lazima pia wavae nguo zenye kuwasitiri vizuri na kuwa na tabia nzuri na wawe wanazungumza mada zenye maadili. Mahusiano ya mapenzi yaliyoshamiri katika jamii nyingi kwa sasa hayakubaliki katika dini ya Kiislamu. Mikusanyiko ya wanafamilia, shughuli mbalimbali msikitini na ziara za kirafiki husaidia kuleta fursa za kubadilishana mawazo baina ya watoto wa kiume na watoto wa kike katika hali ya maadili inayokubalika.

Katika jamii nyingi ni kitu cha kawaida kwa watoto wa kiume na watoto wa kike kutoka pamoja kwa kujifanya kutokana na ahadi zao kama wapenzi na kila mmoja kati yao huwa na wapenzi wengi kabla ya kufunga ndoa. Huamini kwa mtazamo potofu kuwa wanaweza kuwa na fursa nzuri ya kupata ndoa njema endapo watajihusisha katika kuingiliana kimwili kabla ya ndoa. Au huamini pia ni bora kujaribu mahusiano ya kimwili na wapenzi tofauti tofauti kabla ya kupata mwenza ambaye ni sahihi kufunga nae ndoa. Au hutaka tu kujiburudisha. Wakati mwingine huishi pamoja kama mume na mke hali ya kuwa bado hawajafunga ndoa; kitendo hiki huitwa "kuishi pamoja". Wanaweza pia kupata watoto kabla ya kufunga ndoa. Tabia hii hukatazwa na dini mbali mbali kutokana na matatizo yanayojitokeza. Cha kusikitisha ni kwamba tabia hii imekomaa miongoni mwa vijana. Runinga, matangazo ya biashara, filamu, mitandao na vitabu vimekuwa vishawishi vikubwa katika kuhamasisha vijana kuingia katika mahusiano kabla ya ndoa, vitu hivi vina dosari kubwa sana. Baadhi ya watoto wa shule wakiwa na umri wa miaka 9 tu hufanya mambo kama watu wazima kwa kuhadithia vitu walivyowahi kufanya na watu wa jinsia tofauti na yao kama vile vitu hivyo huwafanya waishi maisha mazuri sana. Hujaribu kuwafanya watoto wengine wajisikie kuwa hawaendani na wakati wa sasa au wapumbavu wanaposhindwa kuungana nao. Nini hutokea kwa watoto hawa pindi wanapokuwa watu wazima?

Vijana ambao wanakuwa na mahusiano na watu wa jinsia tofauti na yao wakiwa na umri mdogo mara nyingi huwa wanatoka katika familia zenye matatizo. Wazazi wao

huwa wamepewa talaka au wamekosa mapenzi na usimamizi nyumbani kwao. Huwa wanatafuta urafiki na watu wa jinsia tofauti na zao, ambao wanaweza japo kuwabusu na kuwagusa na kushirikiana nao. Hii ni hatari kwa kuwa hisia zao zinaweza kuwapelekea wakaingia katika masuala ya kuingiliana kimwili kabla ya wao wenyewe kuwa tayari kwa hilo na kuongeza matatizo kwao.

Pindi mtoto wa kiume anapokuwa katika mahusiano na mtoto wa kike au kinyume chake kabla ya ndoa, katika jicho la uislamu huwa tayari washatumika kama nguo iliyovaliwa. Wanapoenda kuingiliana kimwili kabla ya ndoa hupoteza ubikira wao. Tamaduni nyingi ulimwenguni husisitiza vijana kutunza ubikira wao (hususani watoto wa kike) hadi wanapofunga ndoa na wale wanaokosa kuwa makini katika jambo hili hupoteza heshima zao na inakuwa vigumu kwao kupata mume mwenye heshima. Hata hivyo, uislamu umeweka msisitizo na thamani katika kujitunza na kujihifadhi kati ya watoto wa kiume na watoto wa kike. Wazazi wengi katika tamaduni hizi hukataa kufungisha ndoa watoto wao wa kike kwa mtoto wa kiume ambaye anajulikana kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanawake wengi. Kufungisha ndoa na mtu wa aina hii anaweza kupelekea kumchoka mkewe mapema mno na kumuacha ili apate mwanamke mwingine au anaweza kushindwa kumheshimu mke wake na kumkarimu.

Zinaa inaweza kusababisha ujauzito kwa kuwa njia ya uzazi wa mpango wakati mwingine hushindwa kusaidia. Kama msichana atapata ujauzito kupitia uzinifu, huwa ni janga kwake, mtoto wake na huwa laana kwa familia yake. Kuwa mama ni jukumu zuri hata kwa wanawake ambao wana familia. Inakuwa ni vigumu sana kwa mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 11 katika kulea mtoto ambaye baba yake ana umri wa miaka 14 akiwa hayupo tayari kumlea kama baba, hususani wote wakiwa hawana misaada kutoka katika familia zao. Mara nyingi sana huwa hawajapata elimu ya kutosha, hawajakuwa imara kihisia na hata kiuchumi pia. Kwahiyo hawana uwezo wa kuwa na maisha mazuri kwao na kwa mtoto wao. Hii siyo haki kwa mtoto ambaye hana kosa. Mara nyingi mtoto wa kiume hupata uoga na hukataa kuwa yeye ndiyo baba wa huyo mtoto na wala hawezi tena kuwa na mahusiano mazuri na binti wa kike aliyemzalisha. Kwahiyo mtoto huyu aliyezaliwa husalia mpweke na mama

yake kwa kukosa mapenzi na msaada kutoka kwa baba wa mtoto. Watu wa aina hii huwa na wakati mgumu sana. Huwa hawawezi hata kuhitimu masomo yao na huwafanya wazazi kulazimika wakati mwingine kufanya kazi wasizoridhia ili wapate fedha za kulipa madeni.

Katika jamii za kiliberali, wazazi wanaweza kufanya kitu gani kwa watoto wao wa kike na wale wanawake wanaofikiria watoto wa kiume? Kadri watoto wao wa kike wanavyokuwa wakubwa,wazazi wanaweza kufahamu kuwa mtoto wake anapata ufahamu kuhusu wavulana. Wanasikia watoto wao wa kike wakizungumzia kuhusu mvulana fulani. Kwa mara ya kwanza pindi wazazi wanaposikia watoto wao wa kike wakizungumzia mahusiano yasiyo katika misingi ya kisheria hupata hofu. Mawazo juu ya mvulana huwepo katika akili ya msichana aliyempenda na hatimaye huanzisha mahusiano na hali hii huwaudhi wazazi wa msichana. Ni muhimu kutambua kuwa moyo wa binti wa kike huwa na upendo sana wa baba yake na hufundishwa namna ya kujiheshimu, uwajibikaji na tabia njema ili pindi atakapokutana na mvulana mwenye mapungufu ya kimaadili asiweze kuathiriwa na tabia hiyo. Kwa kuwa wazazi wake wamemfundisha namna ya kuzungumza nao, nae ataweza kuwaeleza wazazi kuhusu wavulana. Pindi usiri utakapoisha, hofu waliokuwa nayo wazazi itapungua. Kuwafundisha watoto wa kike namna nzuri ya kuzungumza kutawalinda kimwili dhidi ya wavulana, kwa kuwa mtoto wa kike atakuwa amepata hali ya kujiamini na utambuzi hivyo ataweza kusema “hapana hiyo haikubaliki”, kuliko kukubali ombi la mvulana.

Wazazi wanatakiwa wawaeleze watoto wao wa kike madhara ya kuingia katika mapenzi na wavulana. Wavulana wengi huwarubuni wasichana na baadhi ya wasichana huwarubuni wavulana. Msichana mzuri anaweza kudhihirisha hisia zake za kuingiliana kimwili kwa kuingia katika mahusiano ya kimapenzi na mvulana. Hii ndiyo sababu kwa wasichana kuweza kuathirika na mapenzi pamoja na maneno matamu ya wavulana. Maneno matamu ya mapenzi yanaweza kumhalalishia aweze kufanya mapenzi na mvulana. Msichana huwa anafikiria kuwa kitu ambacho ni kweli kwake pia ni kweli kwa mvulana. Mvulana yupo tofauti kiumbile na kisaikolojia na hulelewa tofauti. Mvulana anaweza kumuingilia mwanamke hata kama hajampenda na akahisi furaha katika kitendo hicho hata kama mwanamke hayupo. Kisha anaweza kutafuta faraja na kwake mwanamke anaweza kuwa mtu yeyote. Mvulana anaweza kufanya mapenzi bila hata kushiriki kimwili. “Furahi nae ila usimlete nyumbani” ndiyo ushauri wenye kupotosha kwa upande wa wavulana.

Ni jukumu la mwanamke kuhakikisha kuwa hatumiki kama chombo cha starehe na ni jukumu la mvulana kutomtumia msichana kama chombo cha starehe. Wavulana na wasichana wanatakiwa kufahamu kuwa kuna kanuni na taratibu za mahusiano ya kimapenzi pamoja na namna ya kuingilia kimwili. Ni kosa kwa msichana kumshawishi mvulana . Pia ni kosa kwa mvulana kumshinikiza msichana. Mvulana huweza kupotoshwa na matamanio yake kwa kufanya kitu bila kufikiria na anaweza kufanya chochote kadri atakavyoruhusiwa na msichana, bila kuhoji kama msichana yupo tayari kwa hilo au kuhusu wajibu wake.

HATIMAYE AMEKIRI KUWA…..

Wakati nilipokuwa nasoma katika chuo kikuu cha Liverpool nchini Uingereza katika miaka ya 1962, nilikuwa na rafiki yangu muislamu ambaye alikuwa akipenda sana kuwa na uhusiano wa kimapenzi na watu ambao siyo Waislamu. Nilimueleza madhara ya kufanya hivyo lakini hakufuata ushauri wangu. Baada ya miaka mitatu akiwa anaendelea na tabia yake hiyo aliniambia kuwa "unajua, unaweza kuwa na furaha ukishaoa kwa kuwa wewe na mkeo mtakuwa bikira katika ndoa yenu, kwa hiyo ndiyo mara yenu ya kwanza kuwa katika mahusiano na zawadi yake itakuwa nzuri na yenye kuridhisha. Kwa upande wangu mimi nikioa mke wangu atakuwa kama mmoja kati ya wanawake wengi ambao nishawahi kuingiliana nao. Kwa upande wangu uhusiano wa aina hii siyo maalumu wala hauna heshima sana."

Watoto Wenye Watoto: Kutoa mimba na Uleaji wa Mtoto kwa kunasibisha

Kuingiliana kimwili kabla ya ndoa ni kosa lenye kuweza kusababisha ujauzito. Ingawaje kuna njia za kudhibiti ujauzito zinazotumiwa na vijana, kuna idadi kubwa ya wasichana wamepata ujauzito kabla ya kuolewa. Ni jambo lenye kuwaathiri wasichana ambao bado hawajaolewa. Mbali na kuwasumbua kisaikolojia, anatakiwa achague moja kati ya makosa haya mawili; kutoa mimba au akubali kuwa na mtoto haramu wa zinaa bila ya kuolewa na aishi nae milele mtoto huyo. Kadhia hizo bado zimekuwa ni nyingi, ingawa kiwango cha mimba za utotoni kilipungua kutoka kileleni nchini Marekani mnamo mwaka 1991, mwaka 2013 takriban asilimia 89 kati ya watoto 273,105 walizaliwa na mabinti walio kati ya umri wa miaka 15-19 nchini Marekani, kwa waliokuwa nje ya mafungamano ya kindoa.(CDC taarifa hizi zimepitiwa na Ofisi ya Afya za vijana barobaro).

Maisha yanakuwaje kwa wasichana waliopata ujauzito nchini Marekani? Shirika la NCSL linatoa ripoti kama ifuatavyo: " Ni asilimia 40 pekee ya akina mama vijana ambao wamefanikiwa kumaliza sekondari, theluthi mbili ya walioanzisha familia basi ni maskini, na takriban mmoja kati ya wanne hutegemea msaada kutoka ustawi wa jamii kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuzaliwa mtoto. Watoto wanaozaliwa na wazazi wa namna hii wanafanya vibaya katika mambo yanayohusu masomo, zaidi ya silimia 50 hurudia darasa, na kuacha shule, ukilinganisha na watoto waliozaliwa na wazazi watu wazima." Pia watoto waliozaliwa na vijana ambao wapo katika baleghe hukumbwa na matatizo ya kiafya, kupata kifungo baadhi ya wakati katika kipindi cha ujana wao, kuzaa wakiwa bado vijana sana, na kukabiliwa na tatizo la kukosa ajira pindi wanapokuwa. (kwa mujibu wa Hofman akinukuliwa na CDC). Dola bilioni kadhaa hutumika kila mwaka katika kuwasaidia wazazi vijana kuhusiana na afya zao nchini Marekani.

Hakuna watoto wa zinaa isipokuwa kuna wazazi wazinifu wenye watoto wasiokuwa na hatia!!

Utoaji Mimba

Muda umeshapita: wazazi wamegundua kuwa mtoto wao amepata ujauzito. Je ni kitu gani wanaweza kufanya kukabiliana na hali hiyo? Busara inaonesha kuwa Vinasaba vinaweza kutumika katika kutambua baba wa mtoto. Anachotakiwa kufanya mvulana ni kuoa msichana aliyempatia ujauzito ili awe mkewe.

Msichana mwenye ujauzito hali ya kuwa hajaolewa akifahamu kuwa hawezi kulea mtoto peke yake, anaweza kuamua kutoa mimba. Atakachofanya ni kutafuta mganga (daktari) ambaye atamtoa mtoto kutoka katika mfuko wa uzazi kabla ya kuwa mkubwa. Baadhi ya watu huamini kuwa utoaji mimba unaruhusiwa na kuamini kuwa mtoto ambaye bado hajazaliwa siyo binadamu katika kipindi cha miezi michache akiwa katika tumbo la mwanamke wakati wa ujauzito.

Hata hivyo, kichanga huwa hai pindi mbegu za uzazi za mwanaume zinapoungana na yai la mwanamke na kama yai lililorutubishwa halifanywi kitu chochote, linaweza kuunda kiumbe hai (binadamu) aliyetimia. Inaelezewa katika Qur'an na Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa kichanga hakipuliziwi roho hadi kifikie miezi minne katika tumbo la mama yake. Kama mtoto huyu hakuzaliwa na akafariki akiwa na umri wa miezi minne au zaidi ya hapo kwa sababu yeyote au ujauzito ukaharibika, mtoto anatakiwa apatiwe jina, aombewe dua na azikwe kwa heshima.

Uislamu unafundisha huruma na heshima kwa maisha ya binadamu. Kila binadamu ana haki ya kuishi (isipokuwa pale atakapokuwa ametenda makosa makubwa sana kama vile kuua nafsi iliyoharamishwa kwa kukusudia). Hii huitwa haki ya kuishi na ni haki ambayo kila mtu kapewa na Mungu Muumba. Kwa hiyo utoaji mimba bila kuwa na sababu ya kisheria ni sawa na kuua nafsi iliyoharamishwa kwa kukusudia kwa maelezo yaliyotolewa na wanazuoni wengi wa Kiislamu kwa sababu kunakatisha uhai wa kiumbe (binadamu) asiyekuwa na hatia.

Mazingira ambayo mwanamke anaruhusiwa kutoa ujauzito ni pale atakapotakiwa kufanya hivyo ili kunusuru uhai wake na baadhi ya wanazuoni wanasema kuwa endapo kama ujauzito ulipatikana kwa kuingiliwa kilazima yaani mwanamke alibakwa au kuingiliwa na ndugu yake wa damu.

Baadhi ya wanazuoni wanakataza utoaji mimba baada ya kipindi cha miezi minne kupita na kuruhusu kutoa kabla ya miezi minne kutimia kwa vile mtoto anakuwa hajapuliziwa roho. Hata hivyo uislamu hauungi mkono utoaji wa mimba kwa kipindi chochote katika hivi na bila kificho umekataza utoaji mimba kuanzia miezi minne. Utoaji mimba unaruhusiwa ili kuokoa uhai wa mama mjamzito, au kulinda heshima ya familia, kuzuia matatizo ya kisaikolojia na kijamii kwa upande wa mama mjamzito, mtoto pamoja na familia yake. Ingawaje utoaji wa mimba unaruhusiwa katika mazingira kadhaa katika baadhi ya madhehebu, kitendo hiki hakiruhusiwi kutumika kama njia ya kupanga uzazi wa mpango au kuepukana na matatizo ya kiuchumi katika mimba isiyotarajiwa. Kama mwanamke mwenye ujauzito ataamua kumtunza mtoto atakuwa mzazi pekee wa mtoto wa nje ya ndoa hali ambayo inaweza kusababisha ugumu zaidi kwa mwanamke huyo na mtoto wake pia ambaye hana baba.

Uleaji wa Kunasibisha Mtoto

Baada ya kutumia kila njia inayowezekana kudhibiti kuingiliana kimwili kabla ya ndoa, kama wazazi wataendelea kukaa na wajukuu zao nyumbani kwao, je wanaweza kufanya kitu gani? Wazazi wengi ambao mabinti zao wamepata ujauzito kabla ya kuolewa hujisikia aibu kutokana na tabia walizoonesha watoto wao na huwa hawahitaji kuwatunza watoto wa nje ya ndoa. Uislamu umeruhusu mama wa mtoto kupeleka mtoto wake akalelewe na mtu mwingine ili mtoto apate matunzo. Njia hii imeruhusiwa na Uislamu katika kulea na kutunza watoto yatima. Hata hivyo mali za yatima lazima zihifadhiwe pamoja na utambuzi wa mtoto juu ya asili yake (ukoo). Wazazi wanatakiwa wawapeleke watoto wao wakalelewe pasipo kuwaona tena. Watakuwa wakishangazwa nao na watoto pindi wanapokuwa wakubwa wakigundua kuwa walilelewa na mtu wa nje huwa wadadisi juu ya wazazi wao na ndugu zao. Siyo watoto wote wanaokubali kulelewa na watu wa nje hupata makazi mazuri. Baadhi ya watoto hawalelewi. Wengi wao hupelekwa katika vituo vya watoto yatima na baadhi yao huamishwa kutoka kituo kimoja hadi kingine ambapo hukosa malezi mazuri. Katika baadhi ya jamii endapo ikibainika kuwa mtoto ni wa nje ya ndoa atatengwa na wenzake. Watoto hawa ambao hawaafikiani na matunzo wanayopata mara nyingi huwa watoto wenye kuleta matatizo. Je mtoto wa kumlea bila kuwa na uhusiano wa damu anaweza kupewa jina la baba anayemlea? Qur'an inachukulia kuwa ukoo ni kitu kikubwa sana na inakataza kuficha ukweli kuhusu ukoo au asili ya mtu.

> "…Wala hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa. Hayo ni maneno ya vinywa vyenu tu" (Qur'an 33:4)

Kila binadamu anatakiwa aitwe jina halisi la mzazi wake wa kiume:

> "Waiteni wao kwa majina ya baba zao; hivyo ni sahihi zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Lakini kama hamuyajui majina halisi ya baba zao basi waiteni kaka zenu katika imani au marafiki" (Qur'an 33:5)

Kama majina halisi ya baba zao hayajulikani Qur'an inaelekeza kuwa waiteni wao kaka zenu katika imani, dada zenu katika imani na rafiki zenu katika imani na waweza kuwapa jina la familia yenu. Tatizo kubwa siyo uitaji wa jina

kilugha bali kukubalika na kuzingatia heshima ya watoto. Katika kuthibitisha zaidi kuhusu undugu, Mtume Muhammad alituonesha mfano kwa kumuoa binamu yake Zaynab baada ya kuachwa na mtoto aliyelelewa na Mtume aitwae Zayd Ibn Harithah.

> "Kisha zayd alipovunja ndoa yake kwa kufuata misingi ya kisheria, tulikuamuru wewe umuoe yeye (Zaynab) ili kuondoa ugumu kwa waumini baadaye kuhusu uhalali wa ndoa baina yao na wale walioachwa na watoto wao waliowalea kwa kufuata taratibu na misingi ya kisheria nao waweze kuwaoa".
>
> (Qur'an 33:37)

Mtu anaweza kulinganisha mfanano uliopo baina ya tabia chafu ya kuficha nasaba au ukoo kabla ya kuingia Uislamu (kipindi cha ujinga) na ile hali ya karne ya 21 ambapo kumuita mtoto wa kumlea bila kuwa na uhusiano wa damu kwa jina la mzazi aliyemlea kuwa ni kitu cha kawaida. Tabia hii inatakiwa isitishwe mara moja na kama jina halisi la mzazi wa mtoto linajulikana basi liwekwe bayana. Sababu kuu ya kufanya hivyo ni bora kwa mtoto huyu yatima na kulinda haki zake. Mbinu nyingine hutegemea tamaduni za jamii husika kwa wakati huo.

Mahusiano ya Jinsia Moja na Wazazi

Mtu mwenye kuwa na uhusiano na mwingine mwenye jinsia kama yake ni mtu ambaye amevutiwa kimapenzi ama kimwili na mtu mwingine mwenye jinsia sawa na yake na huamini kuanzisha mahusiano naye badala ya kufanya hivyo na mtu mwenye jinsia tofauti na yake. Mtu mwenye matamanio ya kuanzisha mahusiano na mwingine mwenye jinsia tofauti na yake huzuia matamanio yake ya kimapenzi kwa watu wenye jinsia tofauti na yake.

Wanawake ambao huanzisha mahusiano na kuingiliana kimwili wenyewe kwa wenyewe huitwa wasagaji. Shoga ni neno lisilo rasmi lenye kuwa na maana sawa na mwanaume mwenye uhusiano na kuingiliana kimwili na wanaume wenzake. Tumekusudia tangu hapo awali kujadili mambo yenye msingi mkubwa na muhimu kimaadili na kwa upande wa ubinadamu. Tukiwa tunapingana kabisa na mahusiano ya kimwili ya watu wa jinsia moja, hatupingani na watu wanaohusika na vitendo hivi kwa kuwa binadamu wanastahili kuchukuliwa hatua bila kuathiri heshima zao au kuwasababishia chuki. Lengo kuu ni kutaka kusaidia wazazi ambao watoto wao tayari wamekuwa wana mahusiano ya aina hii ambao kwa mujibu wa maandiko ya dini yamekatazwa lakini yameruhusiwa katika taratibu za sheria za nchi. Qur'an kitabu kitukufu kimekataza mahusiano ya kimwili ya watu wa jinsia moja;

> "Je! Katika viumbe vyote
> mnawaingilia wanaume? Na mnaacha
> alicho kuumbieni Mola wenu Mlezi
> katika wake zenu? Ama kweli nyinyi
> ni watu mnaoruka mipaka!".
> (Qur'an 26:165-166)

Hili ni tatizo lenye kuwakosesha ujasiri wazazi kukabiliana nalo. Baada ya kufanya wanachotakiwa kufanya kiusahihi kwa nafasi yao kama wazazi, baba na mama

wanaweza kufanya kitu gani endapo watabaini kuwa mtoto wao (Wa kiume) anajihusisha na uhusiano wa kimwili wa jinsia moja (Ushoga)? Kama mtoto wa kiume anakuwa na uhusiano wa kimwili wa jinsia moja ni vyema akafuatiliwa kwa makini na kumtafutia msaada unaomfaa. Uhusiano wa jinsia moja ni suala zito sana. Baadhi yao huamini kuwa ni bora wasiwe na uelewa wa kutosha kuhusu uhusiano wa aina hii. Wazazi hujivunia kuona watoto wao wakiwa na muonekano wa kiume kila nyanja kama mtoto wa kiume na kwa mtoto wa kike akawa na muonekano pamoja na sifa za kike. Hata hivyo ukweli wa mambo lazima tukabiliane nao. Kwa mujibu wa Gallup poll waliofanya uchunguzi wao mwaka 2015,waligundua asilimia 3.8 ya watu wazima wa Marekani wanaweza kuwa ni mashoga, wasagaji, au watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja. Nchini Uingereza kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2010 uliofanywa tume ya taifa ya utafiti juu ya mtazamo wa masuala ya ngono na mitindo ya maisha ambayo hufanyika kila baada ya miaka kumi tafiti ilionesha ya kwamba, 1% ya wanawake na 1.5% ya wanaume wanajidhania wao wenyewe kuwa ni mashoga au wafanyao mapenzi ya jinsia moja, na 1.4% ya wanawake na 1% ya wanaume walijidhania wao wenyewe kuwa wanavutia kimapenzi baina ya wanaume na wanawake (kwa umri kati ya miaka 16-74) (kwa mujibu wa Guardian 2015).

Watu wenye uhusiano wa jinsia moja wamekuwa mstari wa mbele katika kudai haki zao. Wamekuwa wakikusanyika na kutaka sheria zenye kuzuia uhuru wao kufanyiwa mabadiliko. Ni kawaida sasa kuona mwanaume anambusu mwanaume mwenzake au kumuona mwanamme kavaa mavazi ya mwanamke hadharani. Katika baadhi ya nchi pamoja na Marekani wanaume wanaweza kuoana wenyewe kwa wenyewe na wanawake pia wanaweza kuoana wenyewe kwa wenyewe. Watu wa aina hii wanataka wapewe haki sawa kama wanandoa wa kawaida. Ingawaje hawana uwezo wa kupata watoto, wakati mwingine hulea watoto wa wenzao. Mtu yeyote mwenye kukemea uhusiano wa aina hii huitwa “muoga wa mahusiano ya jinsia moja (homophobic)”

Maendeleo yaliyotokea nchini Marekani katika kupanga uzazi wa mpango kupitia matumizi ya vidonge mwaka 1960, uhalalishaji wa kutoa mimba, na ufundishaji wa masomo ya saikolojia umepelekea kuwepo kwa mapinduzi ya mahusiano ya kimwili. Watu katika jamii ambazo zipo na mitazamo ya kiliberali wameanza kudai kuwa wanastahili kuwa huru kuingiliana kimwili na mtu yeyote wanayemtaka, awe kaoa, kaolewa au vinginevyo na awe mwenye jinsia sawa na wao au kinyume chake. Watu wengi wameanza kukubaliana na mawazo ya aina hii na hatimaye ikawa kinyume cha sheria katika nchi nyingi ulimwenguni kumtenga mtu anayejihusisha na uhusiano wa jinsia moja. Swali la kujiuliza ni kwamba, ni jambo gani linalosababisha mtu kuwa na mahusiano ya kimwili na mtu wa jinsia yake? Kuna nadharia tofauti zimependekezwa. Nadharia moja inasema hilo ni suala ambalo mtu anaamua na kuwa hivyo na nadharia nyingine inasema mtu huzaliwa akiwa tayari yupo hivyo na hujibaini kadri anavyokuwa mkubwa? Hadi kufikia miaka ya 1970, uhusiano wa jinsia moja ulikuwa ukitazamwa na wataalamu kama aina ya tatizo la ubongo.

Wataalamu wa masuala ya tiba wanaeleza kuwa baadhi ya watoto wa kiume ambao mama zao ni dhaifu, wakatili hukua na kuchukia wanawake na baadhi ya watoto wa kike ambao wametendwa vibaya na baba zao huchukia wanaume na ndiyo maana hupenda kuwa katika mahusiano ya jinsia moja. Katika miaka ya 1990 wataalamu wa tiba na tabia za binadamu walieleza kuwa kujihusisha katika mahusiano ya jinsia moja ni jambo la kawaida linalotokana na mabadiliko katika mfumo wa jinsia. Wanaendelea kueleza kuwa mahusiano haya huanzia katika mfumo wa vinasaba na huweza kurithishwa (huku mfano ukitolewa katika familia ambazo zina vijana wengi wenye mahusiano ya aina hii, ingawaje hii inachangiwa na namna watoto walivyokuwa wakipata malezi katika familia). Zaidi ya hapo, baada ya kubaini uhusiano wa jinsia moja kwa wanyama walihitimisha kuwa hali hii ni kawaida kwa binadamu; ni dosari katika ukuaji wa mfumo wa ubongo kuweza kutafakari kwa kuwa mtu anaweza kujiuliza "je mambo wanayofanya wanyama yanaweza kutumika kama kipimo kuelezea mila za matendo ya binadamu au kufikiria baadhi ya matendo kukukubalika kijamii? Je watu hufikiria kuwa wanyama wanafaa kuwa mfano wa kuigwa na binadamu katika utendaji wa mambo yao? Matendo mema ya binadamu hayawezi kutokana na kuiga tabia za wanyama. Watu ni tofauti na wanyama na Mwenyezi Mungu kamjaalia binadamu utukufu awe juu ya viumbe wengine wote.

Baadhi ya sababu zinazochangia kuwepo kwa uhusiano wa jinsia moja zinajadiliwa chini kama ifuatavyo. Somo la vinasaba ni moja ya sababu itakayoelezwa. Hata hivyo uzoefu, sababu za mazingira na masuala ya kujenga mahusiano pia ni miongoni mwa sababu za msingi zenye ushawishi na umuhimu mkubwa.

Kuchanganywa kuhusu urafiki; vijana wenye hisia kali juu ya rafiki zao wa jinsia moja huchanganyikiwa wanaposikia mazungumzo kuhusu mahusiano ya jinsia moja. Huanza kushangaa kama nao ni miongoni mwa mashoga au wasagaji. Mwanamke anaweza kuwa na furaha kuwa na rafiki yake ambaye anaweza kumbusu na kumkumbatia. Anaweza kujihisi kuwa yupo katika makosa kwa kusikia maneno fulani na kuchanganya na mahusiano ya kimapenzi. Kama ataweza kuaminishwa kuwa yeye ni msagaji, anaweza kumshawishi rafiki yake waweze kuingiliana kimwili. Suluhisho la tatizo hili linaweza kuwa ni majadiliano endelevu na mawasiliano ya wazi juu ya masuala ya elimu ya ngono kati ya watoto na wazazi kipindi cha kati na kipindi chote cha ujana.

Ukosefu wa mapenzi kwa watoto; Mtu anaweza kuwa hana mtu ambaye anaweza kumpatia mapenzi. Vijana ambao hawana mahusiano imara na wazazi wao au ndugu zao wanahitaji kuguswa na kupendwa na mtu mwingine. Kama rafiki pekee aliyekuwa anafanana nae jinsia, hisia za kumgusa huwa imara zaidi na stara hutoweka hatimaye wanafikia hatua ya kuingiliana kimwili. Suluhisho katika jambo hili ni kuwapenda na kuwajali watoto tangu wakiwa wadogo wananyonya. Mapenzi yaendelee kuwepo miongoni mwa wanafamilia milele. Kwa hali hii, mtu anaweza kupata mapenzi ndani ya nyumba yao kwahiyo hawezi kwenda kuyatafuta nje.

Kulazimisha kumuingilia mtoto; Baadhi ya vijana huchukua mwanya wa kuingiliwa bila ridhaa yao kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi ya jinsia moja hadi wanazoea. Katika tafiti ya wanaume 2881 ambao wamewahi kuingiliana na wanaume wenzao, iliyofanywa na Paul na wenzake (2001) imebaini kuwa moja ya tano ya wanaume wote wanojihusisha na mapenzi ya jinsia moja wamewahi kuingiliwa bila ridhaa yao walipokuwa watoto. Suluhisho ni wazazi kuwatazama watoto wao kwa karibu zaidi katika kuhakikisha watoto wao wanakuwa na marafiki wazuri. Tambua kuwa matendo haya ya kuingiliwa bila ridhaa hufanywa na watu wa ndani ya familia na mara nyingi huendana na hali ya kulipiziana visasi.

Hitilafu za kimaumbile; baadhi ya watu huzaliwa na maradhi au hupatwa na maradhi hali ambayo hupelekea upungufu wa homoni za kike au kiume zinazowafanya kuwa na tabia za kike au kiume katika hali yao ya kawaida. Homoni ni aina ya kemikali zinazozalishwa katika mwili wa binadamu zenye kazi ya kumfanya mtu awe na tabia fulani kulingana na jinsia yake (kama mtoto wa kike kuwa na matiti). Pia husaidia kuunda tabia za mtoto wa kiume kama vile mtoto wa kiume kuwa na mustachi, upara, kuwa na misuli imara, hamu ya kupigana na kujionesha au kwa mtoto wa kike kuwa na hamu ya kulea watoto. Mtoto wa kiume mwenye upungufu wa homoni za kiume hatoweza kuwa na upara, sauti yake haiwezi kuwa nzito kama wenzake na hawezi kuwa na misuli imara kama wenzake. Suluhisho katika tatizo hili ni kupata matibabu ya daktari.

Kuchelewa kuoa au kuolewa; wanaume na wanawake ambao wanakosa kufungishwa ndoa katika umri unaotakiwa huwa nao wanahitaji kukidhi matamanio yao ya kimwili. Kama fursa ya ndoa haijatumika vizuri kuwaoza, vijana watapata mawazo ya njia mbadala katika akili zao. Ndoa za mapema zinatakiwa kuhimizwa katika umri unaoruhusiwa kisheria, kwa kuwa kuoa katika wakati huo ni haki kwao watoto. Ni jukumu la wazazi kurahisisha ndoa kwa watoto wao.

Wazazi ambao wamegundua kuwa watoto wao wana uhusiano wa jinsia moja wanatakiwa wawe wavumilivu na waelewa na pia wanatakiwa wapate ushauri wa kitaalamu. Hawatakiwi kuondoa upendo wao kwa watoto. Ingawaje ni vibaya kwa mujibu wa sheria kuwatenga watu wenye uhusiano wa jinsia moja, sheria pia hairuhusu kuvikubali vitendo vya uhusiano wa jinsia moja japokuwa vinaweza kutokuwa maarufu kwa kuvikemea kwa kuwa sote tuna uhuru wa kuvipinga. Kama ilivyo kwa sharia za kulinda haki za watu walio katika uhusiano wa jinsia moja, ndivyo ilivyokuwa katika kulinda uhuru wa imani na dini.

Wazazi wanatakiwa wafahamu matatizo ya kisheria kuhusu uhusiano wa jinsia moja; sheria ya nchi ya Marekani inakataza kuwatenga watu kutokana na jinsia, rangi, lugha au utaifa. Jamii nyingi hutuma ujumbe kwa watoto kuwa uhusiano wa jinsia moja unaruhusiwa. Jamii hizi zinaficha kitu gani ni cha kawaida na kipi siyo cha kawaida.

Tunawahamasisha wazazi waweke mambo bayana kwa watoto wao kuwa uhusiano wa jinsia moja siyo sahihi. Wazazi wanatakiwa waingilie kati kama mwalimu atakuwa anahamasisha tabia zenye kuhamasisha uhusiano wa jinsia moja.

Wanaume waoneshe tabia zao za kuwa wanaume
(wawaheshimu wanawake, wainamishe macho yao, wawalinde waliodhaifu siyo waoneshe tu miili yao).

Wanawake wanatakiwa kuonesha tabia za kike
(wavae nguo zenye kuhifadhi miili yao,walinde heshima zao dhidi ya wanaume wasiokuwa na tabia njema)

Elimu ya jinsia kwa Mujibu wa Uislamu

Uislamu unatambua kuwa Mungu Muumba ameumba matamanio ya kimwili. Suala la jimai limezungumziwa katika Qur'an na Hadithi za Mtume zimeeleza katika muktadha wa ndoa na maisha ya familia. Uislamu hauwatazami wanawake kama chombo cha kumstarehesha mwanaume kimwili isipokuwa huwatazama wanawake kama muktadha wa uhusiano ambao hukidhi mahitaji ya binadamu na kumridhisha Mungu Muumba. Wakati kitendo cha maingiliano ya mwili nje au pasipokuwa na ndoa hutazamwa kama kosa na dhambi yenye kuhukumiwa, maingiliano baina ya wanandoa wao kwa wao ni suala lililo sahihi na hulipwa kwa thawabu kama sehemu ya ibada. Sheria za Kiislamu kuhusiana na jimai zipo wazi na zinazingatia asili ya binadamu, huwa hazibadiliki kuendana na msukumo wa tamaduni zinazobadilika katika jamii. Wakati huo huo hali ya kuwa bikira katika ndoa ni jambo zuri kwa mujibu wa Uislamu, siyo kama katika baadhi ya jamii ambazo huona kama tatizo. Uhusiano wa kimapenzi kati ya wanaume na wanawake unaoneshwa katika aya zifuatayo hapa chini:

"Kwani hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa? Kisha tukayaweka mahali pa utulivu madhubuti? Mpaka muda maalumu?Tukakadiria na Sisi ni wabora wa kukadiria".
(Qur'an 77:20-23)

"Na wala usikurubie zinaa, jiepushe nayo hakika (zinaa) ni uchafu na njia ya uovu"
(Qur'an 17:32)

Yafuatayo ni marejeo kutoka katika sunnah za Mtume kuhusu mahusiano ya mume na mke;

Mtume anayatazama mahusiano ya ndoa kuwa ni sehemu ya ibada yenye ujira (thawabu). Mtume amesema kuwa;

"Endapo mmoja wenu atalala na mkewe basi hupata thawabu kwa kitendo". Maswahaba wake walishangaa na kusema, "ni vipi sisi tunakidhi matamano ya nafsi zetu na tukawa tunapata

thawabu?" Mtume akajibu, "kama mmoja wenu atafanya katika misingi isiyoruhusiwa kisheria itakuwa ni dhambi na kama atafanya katika misingi inayoridhiwa kisheria atapata thawabu kwa hilo" (Muslim)

Mtume amesema kuwa maingiliano ya wanandoa ni siri baina yao na asiambiwe mtu mwingine yeyote:

"atakayekuwa na hali mbaya katika siku ya hukumu (Qiyama) miongoni mwenu ni yule ambaye atakayetoa siri baina yake na mkewe kwa yale wayafanyayo kuwaeleza watu wengine"(Muslim)

Aishah anasimulia kuwa;

"Wakati nikiwa nalala na Mtume wa Allah nikapata ada, hivyo nikaamka na kuvaa nguo hali ya kuwa bado nipo katika ada. Mtume akauliza "je umepata ada"?. Mimi nikajibu "ndiyo". Mtume akaniita na nikaenda kulala nae pamoja kitandani. (Al-Bukhari na Muslim)

Aisha (mke wa Mtume) anaeleza jinsi alivyotoka kitandani na kumuacha Mtume alale peke yake usiku mmoja. Lakini Mtume alipobaini kuwa mkewe amemuacha kitandani kwa kuwa yupo katika siku zake (hedhi/ada), Mtume alimueleza ajizuie na nguo kisha alale nae pamoja katika kitanda hicho. Mtume na mkewe Aisha walikuwa wanalala pamoja kwa mujibu wa hadithi nyingi zilivyoelezea. Mume na Mke wameelezewa katika Qur'an kuwa kila mmoja ni nguo (Vazi) kwa mwenzake. Nguo au vazi ni mahususi kwa mtu na linamhusu mtu binafsi, kwa hiyo hata wanandoa nao wanatakiwa wawe karibu pamoja. Vazi hulinda tupu zetu, hivyo na wanandoa wanatakiwa wahifadhiane na kulindana tupu zao. Mavazi huvaliwa wakati wowote mtu anapohitaji, kwahiyo wanandoa nao wanatakiwa wawe karibu muda wote na waweze kupatikana kwa kusudio la kustareheshana wakati wowote. Vazi huongeza uzuri wa mtu, hivyo wanandoa wanatakiwa wapendezane wawe wazuri.

Jimai ni namna ya kuelezea upendo na kila kimoja hutegemea kingine. Upendo bila jimai ni sawa na bure na kinyume chake pia ni sahihi. Jukumu la mume kwa mkewe ni kutoa elimu kuhusu namna ya kufanya jimai, hususani kwa vitu apendavyo na asivyovipenda na wala hatakiwi kumlinganisha mkewe na wanawake wengine. Wake nao wanatakiwa kufanya kama waume zao wanavyofanya ili kuweza kupata burudani katika jimai. Wake wanastahili kufahamu kuwa hisia za kimwili za wanaume ni tofauti na zao. Badala ya kujiweka katika hali ya upokeaji bila kushughulika katika jimai, anatakiwa ajishughulishe na ashiriki kikamilifu katika tendo. Wote waume na wake hukutana na vishawishi vingi nje ya nyumba zao, hali ambayo huwafanya wawe katika ushindani mkubwa wa kukabiliana na vishawishi hivi. Kwa hiyo kwa manufaa ya wote, mke anatakiwa apatikane kumridhisha kimwili mume wake ili asiwe na shinikizo au fursa ya kuchagua baina ya mke wake na wanawake wengine ambao wanaweza kupelekea kuharibika kwa familia na kumghadhibisha Allah. Pia mwanaume anatakiwa apatikane kwa mkewe ili aweze kumtimizia na kumridhisha matamanio ya kimwili mke huyo.

Mtume anaendelea kueleza namna ya kufanya jimai ili wanandoa waweze ku-

furahia na kuridhika. Uislamu umekataza liwati lakini hakuna makatazo katika Qur'an wala Sunnah kuhusu kufanya jimai kwa kutumia mdomo. Tupu za wanandoa zinatakiwa kuwa safi na wanandoa wanatakiwa kuoga baada ya kutokwa na ute au baada ya tendo la jimai.

Mtume anaeleza kuwa

"yeyote kati yenu asimuendee mke wake kama "mnyama". Lazima kuwa na mjumbe kati ya wanandoa. Mtu akauliza "unamaanisha nini kwa kusema mjumbe?". Mtume akajibu "mjumbe ni kubusu na kuzungumza (kwa lengo la kumuandaa) .(Imesimuliwa na Al-Zubaydi na Al-Iraqi)

Mtume pia amesema kuwa:

"Ukiwa unamuingilia mke wako lazima umhurumie. Utakapokuwa umeridhika kabla yake, usimkimbie hadi naye awe karidhika"
(Imesimuliwa na Abu Ya'la)

Kila mtu ana jukumu la kumchunga mwenza wake. Kama mume atatarajia mke wake kuwa mwaminifu kwake, basi ni jukumu lake kumpatia muda wa kutosha kufurahia jimai. Kwa kawaida huchukua takribani dakika 15 hadi 20 kuweza kumridhisha mwanamke. Mwanaume hatakiwi kumuendea mke wake kama mnyama bila hata ya kumuandaa. Kitendo hiki hakikubaliki katika Uislamu na wanaume wanatakiwa kuwa na huruma kwa wake zao. Wanatakiwa wafahamu maumbile ya wanawake katika masuala ya jimai, wajifunze mbinu za kuwaridhisha wake zao ili waendelee kuishi maisha ya kuridhisha na yenye furaha. Mwanaume ambaye hawezi kumhurumia mke wake katika kipindi hiki cha jimai husababisha kero pamoja na kushawishi mke kutokuwa mwaminifu katika mahusiano.

Jimai siyo tendo ovu wala siyo uchafu; ni tendo safi likifanyika kwa kuzingatia mipaka iliyopo kwa mujibu wa imani (dini) na maadili.

Jukumu la Wazazi kwa Watoto

Ni muhimu kwa wazazi kuwafundisha watoto wao mitazamo chanya kuhusu jimai. Tendo la jimai halikuumbwa na shetani na wala siyo uovu wala uchafu (kama litafanyika kiusahihi katika misingi iliyowekwa). Ni zawadi na neema kutoka kwa Allah mwingi wa rehema na mfano wa miongoni mwa raha za peponi hapo baadaye.

Ingawaje jimai ni tendo lenye raha na pia ni tendo zuri, linaweza pia kuhamasisha na kutumika katika misingi ya kishetani isiyokubalika kubadili lengo lake na kusababisha madhara. Madhara zaidi yanaweza kusababishwa na jimai zaidi ya kitu kingine chochote ulimwenguni, ikiwemo njaa na vita. Madhara huwa makubwa zaidi kwa kufanya jimai kinyume na taratibu za kisheria, mtu huweza kuishi maisha ya tabu pasipokuwa

na kikomo. Jimai ni tendo linalotakiwa kuendewa kwa mujibu wa amri za Allah bila kuzidisha au kupunguza kitu na kuleta madhara.

Mtume alikuwa muwazi na mkweli katika kuelewa mahitaji ya wanaume na wanawake. Mtume hakuwahi kuwa mgeni katika mahusiano na alionekana kufurahia ndoa yake. Huu ndiyo uliokuwa mtazamo wa Aisha ambaye alikuwa akimfahamu vizuri Mtume zaidi ya mtu mwingine. Kuridhishana kimwili kunahitaji kuzingatia maadili. Kuruhusu kuingiliana kimwili kunaweza kupelekea kuvunjika kwa familia na jamii kutokana na uongo na ulaghai, kukosekana kwa hali ya kuwajibika na wakati mwingine kupelekea kutokea kwa uhalifu kama vitendo vya ubakaji, matumizi ya dawa za kulevya, wizi na mauaji ya kukusudia. Kama mtu anampenda Mungu, basi mtu huyo anatakiwa ajiepushe na vishawishi na kutambua kilicho sahihi dhidi ya kisichokuwa sahihi. Watu wengi wanajihisi aibu na kujizuia kujifunza namna ya kufanya jimai katika namna inayoridhisha.

Jinsia na Usafi wa Mwili: hedhi (ada), nywele za sehemu za siri, kutahiri na utoaji wa ute sehemu za siri.

KUINGILIANA KIMWILI WAKATI WA HEDHI (ADA): Tamaduni za kiyahudi hapo zamani wakati mwanamke anakuwa katika ada zilikusudia kuzuia kuonana au kuwasiliana na wanawake kiujumla. Mtume aliwaeleza maswahaba kushirikiana na wake zao wakiwa katika ada zao, ingawaje walitakiwa wajizuie kuwaingilia na kugusa sehemu zao za siri.

Wasichana wanatakiwa wapewe ushauri namna ya kutumia pedi za kujisafishia na namna ya kuzitupa bila ya kuharibu vyoo. Njia mbadala ni kutumia vitambaa laini/pedi ambazo zinaweza kufuliwa, kukaushwa na kutumika tena baadaye. Ada kwa wanawake ni kitu cha asili kwao na wala isichukuliwe kuwa ni jambo la siri au kufedhehesha hususani mtoto wa kike anapohisi maumivu.

NYWELE ZA SEHEMU ZA SIRI: Mtume amependekeza kuwa nywele za sehemu za siri za mwanaume na mwanamke ziondolewe ndani ya kipindi fulani yani mara moja kwa mwezi ili kufanya mwili uwe safi kwa ajili ya kuwa tayari kumridhisha mwenza. Nywele za sehemu za siri ni asili ya binadamu, ishara ya afya na kitendo cha kuziondoa ni katika kupata amani kiakili na ni katika miongoni mwa usafi.

Mtoto wa kiume hatojali kuwa na kifua chenye nywele, au nywele miguuni au ndevu za sharubu. Wanawake wengi hata hivyo huwa hawapendi. Wanawake hupatwa na hofu wanapoona kuwa wanaota nywele katika matiti yao na huchukizwa zaidi wanapoona miguu pamoja na mikono yao ikiwa imezunguwa na nywele. Kina mama wanaweza kuwa na msaada mkubwa sana kwa watoto wao kuwaeleza watumie vipodozi au mbinu nyingine zitakazowafanya wawe nyororo na kuvutia. Wanawake hawatakiwi kuwa na hofu kuwa wanabadilika na kuwa wanaume kwa kuota ndevu za sharubu au

ndevu nyinginezo chini ya kidevu. Ndevu zinaweza kuondolewa kama zitaonekana kuwa tatizo. Wanawake wanastahili kujiamini na miili yao na wasiwe na fikra za kutaka kuwafurahisha wanaume hadharani.

KUTAHIRI: Mtume amesisitiza kwa wanaume kutahiriwa (kuondolewa ngozi katika sehemu ya uume) katika umri mdogo. Hali hii huimarisha usafi kwao na huleta furaha zaidi wakati wa tendo la ndoa wanapokuwa katika ndoa. Sunnah hii kwa watoto wa kiume husaidia kupunguza maambukizi ya saratani, kupunguza maambukizi ya magonjwa mengine mbalimbali na kupunguza maumivu wakati wa kujisaidia haja ndogo. Wanawake hawatakiwi kufanyiwa sunnah hii (kukeketwa). Uislamu umekataza kukata sehemu yeyote katika sehemu za siri za mwanamke.

Kutokwa na ute na ndoto nyevu kwa Wavulana

Baadhi ya vijana hupata fedheha sana wanapoona nguo zao zikiwa zimeloa kwa ute na huogopa sana wazazi wao kuona. Ni muhimu kuwaeleza kuwa kiasi fulani cha kutokwa na ute ni suala la kawaida. Kama ute huo utakuwa na rangi fulani au damu au harufu au nguo zao za ndani zitakuwa zinahitajika kubadilishwa zaidi ya mara moja kutokana na hali hiyo basi ushauri wa kitaalamu unahitajika. Ute usichanganywe na haja ndogo yani mtu asidhani kuwa ute ni mkojo. Mkojo ni najisi (uchafu) na lazima usafishwe. Ute ni msafi hauhitaji kusafishwa kama mkojo, kusafisha kidogo kwa kutumia matone machache ya maji na kusugua nguo kunatosha.

Vijana na Kujizuia

Watoto wengi katika nchi zilizoendelea ikiwemo Marekani, Kanada na Uingereza hufikia umri wa baleghe mapema mno. Kwa wastani wasichana huingia baleghe kati ya umri wa miaka 8 hadi 13, hali ya kuwa wavulana hufikia wakiwa na umri wa miaka 9 hadi 14. Kwa kawaida kuanza kupata ada, huanza katika kipindi cha mapema zaidi ndani ya miezi sita kuliko

ilivyokuwa katika kipindi cha miaka 40 iliyopita, lakini utokaji wa chuchu huwahi miaka miwili mapema zaidi na ilivyokuwa miaka ya nyuma. Dalili nyingine za kuwahi kufikia baleghe ni pamoja na kuwa na harufu ya mwili na kuota nywele sehemu za siri zimekuwa zikijitokeza mapema zaidi ya ilivyokuwa awali (Chuo kikuu cha Berkley California, 2014). Kubaleghe mapema kunaweza kuwa kunatokana na utumiaji uliokithiri wa mazao ya wanyama, ambao wengi wao hukuzwa kwa dawa na homoni zenye kupandikizwa katika kuhamasisha ukuaji wao.

Kwa upande mwingine, wastani wa umri wa kufunga ndoa umepanda. Nchini Marekani ni miaka 29 kwa wanaume na miaka 27 kwa wanawake mnamo mwaka 2013 (kwa mujibu wa kituo cha Tafiti

cha Pew, 2014) na nchini Uingereza ni takribani miaka 31 kwa wanaume na miaka 29 kwa wanawake mnamo mwaka 2012 (kwa mujibu wa ofisi ya taifa ya takwimu 2014).

Watu ambao wanakuwa na imani ya kuweza kujizuia kuingiliana kimwili kabla ya ndoa wanawaeleza watoto wao wazuie matamanio ya nafsi zao hadi watakapofunga ndoa, subira ya miaka ipatayo 16. Hiki ni kipindi ambacho matamanio huwa ni makubwa sana na mtoto huwa na nishati ya kutosha. Hii ni changamoto kwa watu wanaoelekea katika utu uzima.

Hadi kufikia miaka 100 iliyopita watu wengi wamekuwa wakioana mara tu baada ya kubaleghe. Jamii zilikuwa zikipigania kuweza kuishi. Kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya vifo vya watoto na vita vya mara kwa mara, ilikuwa ni muhimu kwa wanaume na wanawake kuweza kufunga ndoa mapema katika kipindi ambacho wanakuwa na matamanio ya kutosha na nguvu za kutosha.

Baadhi ya jamii zimeamua kufuata taratibu za kuchelewa kufunga ndoa kwa vijana kwa kuruhusu kuwepo kwa njia za kujizuia kuiendea jimai. Watu walioshikamana na dini hawana uwezo wa kufanya hivyo, hata hivyo bado wanaweka msisitizo mkubwa sana kwa vijana waweze kuyashinda matamanio yao (kujizuia). Inaonekana kama ni ngumu kwa binadamu kuweza kuzuia matamanio yao ya mwili kuanzia katika baleghe hadi kufikia hatua ya kufunga ndoa (takribani miaka 20 ijayo). Kijana mwenye homoni kali anapata tabu katika mazingira ya kawaida yenye vishawishi kila sehemu.

Jamii za Kiislamu zinatakiwa kufuata taratibu za kufunga ndoa mapema kukabiliana na hali iliyopo. Njia hii mbadala pia inaweza kuwa na tatizo. Hata hivyo wazazi wanatakiwa wawaeleze vijana wao sababu zipi zinapelekea kuingiliana kimwili nje ya ndoa, kukatazwa kwao japokuwa wanahitaji kufanya hivyo kukidhi mahitaji ya nafsi zao. Familia kubwa zinaweza wasaidia kuwapa miongozo vijana wenye kulea watoto hususani kama uzazi wa mpango unafanyika kwa ufasaha.

Baadhi ya wanachuoni wa Kiislamu wametoa hukumu ya kwamba kujichua (masturbation) hakufai hivyo lazima kukemewe isipokuwa pale inapokuwa mtu hajaoa akazidiwa kupindukia na kuamua kujichua ili kujifariji na hata hivyo kitendo hicho kisifanywe kuwa ndio mazoea. Kipindi hisia za mwili zinapokuwa ngumu kuzizuia, kujichua inakuwa ni kosa dogo. Katika kitabu chake kinachoitwa "***rududun 'ala abatil***", marehemu sheikh Muhammad al-hamid ameelezea kuwa wanazuoni wamekataza kujichua kama kitendo hicho kitatumika katika kuamsha hisia za kimwili.

Hata hivyo, endapo hisia za kimwili zitakuwa zimetawala akili ya mtu kiasi kwamba akawa anashindwa hata kujidhibiti na kujikuta anashawishika kuelekea katika uzinzi basi kujichua imeruhusiwa kwa mtu huyo ikiwa tu kufanya hivyo kutasaidia kupunguza hamu yake. Kujichua ni kitendo cha kati na kati kisichokuwa na thawabu wala hukumu, lawama wala pongezi lakini pia siyo dhambi wala siyo kitendo kizuri. Kujichua ni kitendo cha mtu mmoja. Wakati kijana akiwa yupo peke yake badala ya kuwa na mtu katika uhusiano, kijana huyu anaweza kujiridhisha haja zake kwa nadharia kuwa yupo na mtu. Ingawaje kitendo hiki husaidia kwa muda, hata hivyo pia huwa ni njia mbadala ya ndoa. Pindi kijana anapokuwa anadumu kujiridhisha peke yake kwa kujichua huwa ni tatizo kwake.

Wazazi wanatakiwa wafahamu kama vijana wanatumia mbinu ya kujichua kujiridhisha kimwili. Kwa kawaida tabia hii huisha pale mtu anapokuwa na kuamua kufunga ndoa. Kitu cha msingi ni kuwa wazazi wanastahili kuwabana watoto wao kwa vitu mbali mbali ikiwemo michezo au kuwajengea mazoea ya kufunga siku mbili kila wiki na kuwashirikisha katika shughuli mbali mbali katika makundi. Wazazi wanatakiwa kuwaeleza watoto wao kuwa kujichua kuliokithiri kunaweza kuleta matatizo ya kiafya na wajitahidi kuyashinda matamanio ya nafsi zao. Kwa namna hii vijana wanakuwa wanazuiliwa kuweza kufikia kujichua.

Wazazi wanatakiwa wawe wakweli kuwaeleza watoto wao namna ya kuishi na miili yao. Jimai huchukua sehemu kubwa sana katika fikra za vijana wanaoelekea utu uzima lakini bado suala hili hujadiliwa kwa uchache sana baina ya wazazi na watoto wao na wanapojaribu kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili wazazi huwa hawasemi ukweli kwa watoto. Wanazuoni wa Kiislamu wanaweza kuwaeleza watoto kuwa kujichua ni haramu na kumekatazwa kisheria, ingawaje baadhi yao wamehalalisha suala hili katika mazingira fulani. Vijana walio wengi wataendelea kujichua na kuishi kwa kujisikia aibu au kujihisi wakosefu. Uwiano lazima utafutwe na kitendo hiki kiweze kutumiwa kama njia ya mwisho na katika kiasi kidogo sana bila kuathiri mwili kiumbo au kihisia.

UFUMBUZI WA KIISLAMU KATIKA MATATIZO YA KIJINSIA: MWONGOZO WA KUFUATA KUZUIA MATATIZO HAYO

Njia ya msingi ni kujizuia:"*Laa takarabu zinaa*" kuwa mbali, usikaribia kitu au mazingira yeyote yenye kuhamasisha utendaji wa dhambi ya zinaa.

> "Wala usiikurubie zinaa; hakika ni kitendo kiletacho aibu na kiovu chenye kupelekea utendaji wa maovu mengine"
>
> (Qur'an 17:32)

Neno muhimu hapa ni "usikurubie", maana yake jizuie, jikinge kutokana na zinaa na hii inaashiria kuwa mtu analazimika kujiepusha na vyote vyenye kupelekea zinaa hadi kufikia katika hali ambayo mtu atakuwa hana uwezo wa kutenda dhambi hii ya zinaa. Mbinu ambayo jamii inaweza kuitumia ni kuzuia kwa kutumia njia ambazo zinaweza



kuondoa mianya yenye kupelekea zinaa kuwepo. Kwa kuondoa biashara za ngono, kuzuia usambazaji wa huduma za aina hii na kupunguza mahitaji yake jamii inaweza kurekebisha tabia za watu na kufanya ndoa ziwe safi na salama. Aina hii ya maadili siyo ngeni wala tofauti katika Uislamu, na ilikuwa ikifundishwa na imani za dini nyingine ikiwemo (Ukristo, Uyahudi na Uhindu). Hakuna mtu mwenye akili timamu anaweza kufikiria kuwa ni vizuri kwa vijana au wazee kujihusisha zaidi na vitendo vya uzinifu na kuwa watumwa wa matamanio ya miili yao. Watu ambao wana imani thabiti kuhusu Mwenyezi Mungu wanatambua kuwa sehemu nzuri ya kuweza kukidhi matamanio ya mwili ni ndani ya ndoa zao. Tatizo ni kuwa katika jamii nyingi, mawazo haya yamekataliwa na vijana wa sasa.

Zama za leo vitu vinavyopelekea kuenea kwa magonjwa ya zinaa vipo wazi na vingi sana. Ili kuepukana navyo, kunahitaji mtu ajitoe sadaka. Matunda ya kujizuia ni mengi lakini pia madhara ya kujihusisha na zinaa ni makubwa. Pindi mfumo wa Uislamu unapotathminiwa, unaonekana wazi kuwa umekusudia kutunza na kulinda heshima ya familia. Msisitizo mkubwa unawekwa juu ya kuwa na haya katika mavazi, kutokidhi matamanio ya mwili nje ya ndoa, kujizuia kutotumia vilevi na dawa za kulevya, kutokuwa na mawasiliano yasiyokuwa na maadili baina ya watu wenye jinsia tofauti, kutokaa pamoja baina ya mwanaume na mwanamke bila kuwa na msimamizi, kutojihusisha na filamu za ngono wala kusikiliza muziki wenye kuhamasisha mapenzi. Hizi ni katika jitihada za kuondoa vishawishi vyenye kumuelekeza mtu kuendea zinaa. Wazazi pia wanatakiwa wawaeleze vijana wao hatari ya kuingiliana kimwili pasipokuwa na malengo. Mbinu za kuzuia zinaa zinatakiwa kutumika kuanzia kijana anapokuwa bado mdogo. Mtu binafsi na kwa ushirikiano wa watu wengine kwa pamoja katika kudhibiti vishawishi kwa vijana.

Hata Qur'an inatambua kuwa matamanio ya kimwili yanakuwepo kwa binadamu. Nabii Yusufu (a.s) anasema katika shinikizo la matamanio mtu anaweza kushindwa kujizuia isipokuwa kwa huruma ya Muumba pekee ndiyo mtu anaweza kunusurika katika hali hiyo ngumu.

> "Na yule bibi wa nyumba aliyo kuwamo Yusuf alimtamani kinyume cha nafsi yake, na akafunga milango. Akamwambia: Njoo! Yusuf akasema: Audhubillahi! Najikinga na Mwenyezi Mungu. Huyu bwana wangu kaniweka maskani nzuri, na hakika wenye kudhulumu hawatengenekewi. Na hakika yule

> mwanamke alimtamani, na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi. Hayo hivyo ili tumuepushe na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa" (Qur'an 12:23-24)

Mwenyezi Mungu ameweka vishawishi vikubwa kwa wanaume kuliko wanawake. Matamanio haya ya mwili yanatakiwa kukidhiwa katika ndoa tu. Kama vishawishi ni vingi, matamanio hujionesha mapema na huwa vigumu kuyadhibiti.

Hata hivyo hisia za kimapenzi kwa wanaume zipo karibu sana kuliko wanawake na huwa ni vigumu kujidhibiti na katika kipindi ambacho mwanaume anafikia baleghe hisia hizi huanza kujidhihirisha. Wanawake wana uwezo mkubwa wa kudhibiti hisia zao na tabia zao kuliko wanaume. Mazingira yenye kuruhusu muingiliano wa kimwili yapo wazi sana katika jamii nyingi katika karne ya 21. Jamii haifanyi jitihada za makusudi kusaidia vijana bali huwatupa vijana katika ziwa hali ya kuwa wamefungwa mikono na kuwaeleza "kuweni makini mtaroa". Vishawishi huchochea hisia za mapenzi hali ya kuwa jamii inatarajia kuwa vijana watajizuia wenyewe. Hii ni sawa na kumuweka samaki mtamu mbele ya paka mwenye njaa halafu ukamwambia "usimle huyo samaki". Kujizuia huwa rahisi sana kama hakuna vishawishi.

Mwanaume anapata hisia za kimwili haraka zaidi kwa kugusa, kutazama, kusikia, kunusa au hata kwa kufikiria. Ni muhimu kuwa vitu vyenye kushawishi, kurubuni na kuamsha hisia za kimwili kuondolewa haraka iwezekanavyo. Ni vizuri kuchukua hatua salama za kujilinda ili kuepuka matatizo kuliko kujiweka katika matatizo na kuanza kupambana kujinusuru. Wakati watu wanakuwa wamepata hisia za kimwili, uwezo wao wa kujikinga unakuwa dhaifu na uwezekano wa kuingia katika vishawishi huongezeka.

Mbinu inayopatikana katika Qur'an ni yenye kuzuia na kufanya ufafanuzi. Swali la kujiuliza ni: namna gani vijana wanaweza kuwa na maadili yanayokubalika katika jamii inayoruhusu mahusiano ya kimwili? Je inawezekana kiubinadamu? Kwa mujibu wa sheria ya Uislamu, kitu chochote chenye kupelekea kutenda kosa ni haramu.

Alimfunga mikono yake na kumtupia katika mto, kisha akamwambia; kuwa makini! Kuwa makini! usiroe

Kwa hiyo kitu chochote chenye kumzuia mtu ashindwe kudhibiti matamanio ya mwili wake na kuzuia uwezo wake wa kujidhibiti katika hali hiyo hakiruhusiwi katika Uislamu. Zifuatazo ni hatua ambazo huzuia vishawishi vinavyopelekea uzinzi. Kupunguza vishawishi ni mchakato wa muda mrefu katika maisha kunakohitaji ushirikiano wa wazazi, familia, shule, vyombo vya habari na jamii.

Kuwa na Haya kwa Jinsia Tofauti

Ni muhimu kutambulisha suala la aibu (Haya) tangu mtoto anapozaliwa kwa kuheshimu sehemu za siri za mtoto. Wazazi hawatakiwi kugusa sehemu za siri za mtoto isipokuwa wakati wa kumuogesha tena akiwa anatumia mikono yake pamoja na nguo ndipo afanye hivyo kwa kipindi kifupi tu. Pia sehemu nyeti za watoto wenye umri wa miaka 3 na zaidi zinatakiwa zihifadhiwe kwa kutumia nguo hata wakati wa kuwaogesha. Epuka kuziweka wazi sehemu za siri za mtoto.

Nini maana ya haya? Haya imefafanuliwa kuwa; Ni kuhisi aibu kutokana na kitendo chochote chenye kushusha heshima ya mtu. Kwa lugha ya Kiarabu ina maana kuwa;

Tabia au mtazamo wenye kusababisha kufedheheka (kupata aibu) au hofu ya kitendo chenye kushusha heshima.

Wanazuoni wamefafanua haya kuwa ni tabia ambayo humzuia mtu kufanya maovu (matendo machafu) au matendo yenye kuleta aibu. Kuona haya ni tabia ambayo inatakiwa kuandaliwa na wazazi ili iwe tamaduni katika familia na jamii. Hata katika mazishi, wakati wa kuosha maiti waoshaji hawatakiwi kumtazama maiti katika sehemu zake za siri wala kuzishika kwa mikono isipokuwa wanaruhusiwa kutumia nguo kusafisha sehemu hizo. Katika kutambua uzito wa haya (aibu), Mtume Muhammad (s.a.w) amesema yafuatayo:

> *"imani ina zaidi ya matawi 70. Bora kuliko yote ni kutamka kuwa "hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah pekee". na dogo kati ya matawi hayo ni kuondoa kitu chenye madhara katika njia. Na haya ni katika tawi la imani".* (Muslim)

Kuwa na Haya ni katika Imani!

Kitu ambacho watu wamerithi kutoka katika utume: ni kuwa kama hauna aibu (haya) basi unaweza kufanya kitu chochote utakacho (Abu dawud)Mtume anasema kuwa:

> *"Ukosefu wa maadili (kimavazi,vitendo) hufanya mtu kuwa mbaya. Haya humfanya mtu awe na uzuri". (Ibn Majah)*

Al-jurjan amegawa haya katika makundi makuu mawili yafuatayo;

a) Katika sehemu ya kisaikolojia, hii huwepo kwa kila binadamu kama vile kutozionesha sehemu zao za siri au kutoweza kuingiliana kimwili hadharani wakiwa wanaonekana na watu wengine. Aina hii ya haya huwepo kwa binadamu na huwa ni asili ambayo mtu huzaliwa nayo.

b) Haya inayopatikana kutokana na imani ya mtu, ambayo humuhifadhi mtu kutokana na utendaji wa maovu kwa ajili ya kumpenda Mwenyezi Mungu na kuwa na hofu ya adhabu zake.

Watoto wanatakiwa wafundishwe vitendo vifuatavyo katika masuala ya haya;

1. Kuinamisha macho yao wanapotazama binadamu mwenye jinsia tofauti na yao au kitu kisichokuwa na maadili
2. Kutembea kwa aibu bila kuhamasisha matamanio ya mwili kwa wengine au kuiga mwenendo wa jinsia kinyume na jinsia yake
3. Kuzungumza vizuri na kwa upole bila kuzungumza sauti yenye kuamsha hisia za kimwili
4. Kuwa na aibu katika mavazi, kwa kuvaa mavazi yenye kusitiri mwili mzima vizuri

Katika mazingira 3 yafuatayo haya haitakiwi kuwepo

1. Katika masomo; kutafuta elimu ya dini hususani inayohusu masuala ya jimai katika ndoa, ada kwa wanawake, masuala ya ujauzito na ndoto nyevu kwa wanaume. Wanazuoni wana msemo usemao "hakuna aibu katika kujifundisha dini". Tunaweza kutumia msemo huu kuwa "hakuna aibu katika kutafuta elimu (kujifunza)".



SHAIRI

Kama hauna hofu kuhusu madhara ya tabia yako na ukashindwa kuwa na *haya* katika matendo yako, unaweza kufanya chochote utakacho.

Lakini kwa Mwenyezi Mungu hakuna wema katika maisha yasiyokuwa na *haya*(aibu)! Mtu huishi kwa kujiamini ikiwa ana *haya* (aibu), kama shina linavyolindwa kwa kuzungukwa na gome la mti.

Shairi la lugha ya Kiarabu

2. Katika kuleta mabadiliko (maboresho); katika kuamrisha mambo mazuri na kuzuia maovu ni jukumu linalotakiwa kutimizwa kwa ukamilifu na busara.

3. Katika ndoa; hakuna aibu baina ya wanandoa katika uhusiano wao nyumbani kwao. Mtume amesema kuwa;

> *"ficheni tupu zenu isipokuwa kwa wenza wenu" (Abu dawud ibn Majah na Al-Hakim)*

Wakati jimai imekatazwa kwa wasiokuwa wanandoa, tendo hili limeruhusiwa kwa wanandoa katika vyumba vyao. Kama mzazi atapuuza kuandaa misingi ya haya kwa watoto wake, basi jamii itaathirika. Haya ni msingi wa kinga dhidi ya vishawishi na urubuni. Yafuatayo ni baadhi ya madhara yaliyobainika kutokana na kutokuwepo kwa haya miongoni mwa mataifa.

- Kwa kutumia kivuli cha sanaa na uhuru wa kujieleza, sehemu za makumbusho katika nchi nyingi kumekuwa na mabango yaliyobandikwa kuonesha tupu za wanaume na wanawake pamoja na michoro ya picha zenye kuonesha tupu za wanaume na wanawake. Hali hii pia imeonekana kuwepo katika baadhi ya hekalu nchini India

Kwa wengi kuna tofauti kati ya kile kinachodhaniwa kuwa ni sanaa na picha za ngono. Vitu vyenye kuonesha utupu katika tamaduni za sanaa za magharibi ni miongoni mwa maendeleo yaliyopiga hatua sana kwani ni ishara ya mambo yaliyoonekana mazuri na kufaa (maadili), heshima na utukufu wa mtu. Mfano mzuri ni picha ya David (Mtume) iliyochorwa na Michael Angelo, ambayo huchukuliwa kama ni picha nzuri ikiwa imechorwa na kuonesha utupu.

Baadhi ya hekalu duniani (mfano nchini India) pia huonesha utupu wa watu katika sehemu za kufanya ibada za dini fulani. Bila shaka picha ya David ni yenye

kuashiria mtu aliyekuwa na malengo au ndoto za kutimiza na uelewa mkubwa lakini haiashirii Mtume David mwenyewe.

Kukubalika kwa tafsiri ya utupu katika jamii ni jambo ambalo wazazi wanatakiwa walifikirie kiundani zaidi, hususani kwa kuwadhibiti watoto wao.

- Katika makumbusho moja huko Santiago, Chile kuna michoro ya mwanaume na mwanamke wakiwa wanaingiliana kimwili imewekwa wazi inaonekana.
- Msichana mmoja nchini Marekani alikuwa akijirekodi chumbani kwake na bafuni kisha kusambaza picha moja kwa moja kwa watu ambao wanaweza kutazama kupitia mtandao kwa masaa 24 ya siku.
- Katika nchi ya Marekani watu elfu hamsini huingia mtandaoni kutazama moja kwa moja namna mtoto anavyozaliwa katika mtandao.

(Gazeti la Time, Juni 29,1998)

Ifuatayo ni orodha inayoonesha baadhi ya kanuni katika masuala ya haya

- Watoto wanapokuwa kiumri, wanatakiwa wapishe hodi kabla ya kuingia katika vyumba vya wazazi wao pamoja na ndugu zao wengine (ili wasiweze kuwaona kama wakiwa hawajajisitiri).
- Wazazi na ndugu wavae mavazi yenye heshima ndani na nje ya makazi yao. Matumizi ya urembo na vipodozi vyenye kuweza kuleta mvuto lazima yazuiliwe na uturi usitumike. Wazazi pia wanatakiwa kuwa makini katika matumizi ya lugha zao wanapokuwa na watoto wao, wasizungumze kuhusu masuala ya mapenzi. Na wala wasijihusishe katika matendo yanayohusiana na mahusiano ya kimwili mbele ya watoto wao kama vile kubusu na kushikana sehemu za siri.
- Wakati watoto wanapokuwa wametimiza umri wa miaka 10, wanatakiwa walale katika vitanda tofauti kila mmoja na chake.
- Wavulana na wasichana wanatakiwa wafundishwe kushusha macho yao wanapowatazama watu wa jinsia tofauti na wao.

> “Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za wanayo yafanya. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipokuwa unaodhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, au wafwasi wanaume wasio na matamanio, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyo khusu uke. Wala wasipige chini miguu yao ili yajulikane mapambo waliyo yaficha. Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa.. (Qur’an 24:30-31)

Kuinamisha macho ni muhimu. Mtume anasema;

> *"Yeyote mwenye kushusha macho yake kuepuka kile kisichokuwa halali kwake, Allah humpatia furaha katika moyo wake"*

- Wanawake wanatakiwa wafundishwe kutembea kwa heshima kuepusha mvumo wa kimapenzi. Hawatakiwi kuinua au kupandisha nguo zao ili waweze kuonesha miguu yao wakati wanatembea. Pia wanatakiwa kujizuia kuzungumza kwa namna ambayo inahamasisha mahusiano ya mapenzi;

> Kama mnamcha Mungu basi msilegeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema (Qur'an 33:32)

Wanaume na wanawake wasiruhusiwe kukaa pamoja faragha muda wa usiku nje ya makazi yao. Muda wa kutembea udhibitiwe kwa makubaliano baina ya wazazi na watoto.

Baadhi ya aina fulani ya muziki una madhara (zile zenye kuamsha hisia za mapenzi na zenye kutumia maneno machafu). Suala la mapenzi ni jambo la kawaida katika muziki unaosikilizwa na vijana na huwa muziki unaohusu mapenzi, burudani na kufikia katika muziki wenye kuharibu. Tafiti zimegundua kuwa vijana wanaosikiliza muziki wenye kuhusu mapenzi wanaweza kuingia katika mahusiano ya kimapenzi mapema zaidi (kwa mujibu wa tafiti za tiba kwa watoto, 2007). Muziki unaohusu mapenzi huamsha hisia za kimwili. Baadhi ya muziki hutumia maneno yanayohusu mahusiano ya kimwili (ngono) hivyo watoto wanatakiwa wazuiliwe kusikiliza muziki wenye maneno sampuli hii. Pindi watoto wanaposikiliza muziki wa aina hii huzoea maovu na kuona kitu cha kawaida.

Filamu za ngono ni hatari kwa watoto kwa kuwa huamsha hisia za mwili na kufanya watoto washindwe kujizuia. Filamu hizi zina madhara ya muda mrefu katika fikra za watoto na kuwafanya waweze kutizama na kuanza kuota hata mchana ndoto zinazohusu kuingiliana.

Filamu za ngono hupunguza thamani ya wanawake ambao huwepo kwa ajili ya kukidhi haja za wanaume. Kama mwanaume atapata hisia kutokana na filamu za ngono au kitu chenye mithili yake anatakiwa aweze kujiridhisha haja yake kwa mke wake. Wale ambao hawajaoa hawawezi kufanya hivyo na hii inaweza kuwa sababu ya kufunga ndoa mapema. Mtu hawezi kuhukumiwa kwa kuwa na matamanio ila atalaumiwa kama ataruhusu matamanio haya kuweza kuathiri watu wengine. Kwa hiyo wanaume wengi huwaumiza wake zao bila kujua kwa kuwatazama wanawake wengine kwa matamanio.

Taswira za watu maarufu na nyota wa filamu katika mabango, majarida huleta tatizo. Taswira hizi hukaa katika fikra za mtu milele hali ya kuwa hazizeeki na zikiwa bado nzuri ukilinganisha na wake zao halisi ambao huzeeka, huwa wanene na huweza kuchoka. Wanandoa wanatakiwa kuwa na huruma baina yao na kufanyiana ukarimu, mmoja wao anaweza kuwa mzee lakini bado akawa na mvuto kutokana na kupanga uzazi, kula vizuri na kufanya mazoezi ya kutosha. Kwa sasa wazazi wanatakiwa wawe makini na wajue hatari ya filamu za ngono katika mtandao, picha

za utupu na mazungumzo yanayohusu mapenzi. Lazima wawasimamie watoto wao kwa umakini na kuweka vinakilishi katika maeneo ya wazi katika nyumba zao badala ya kuziweka katika vyumba vya watoto wao.

Utaratibu wa Mavazi

Wasichana na wavulana wanatakiwa wawe na tabia nzuri na wavae vizuri. Wasivae nguo za uchochezi na wala wasiwashughulishe watu kwa maumbo yao. Wasivae nguo zinazobana kwa lengo la kuonesha maumbo yao au kuvaa vito vya thamani zenye kuchochea uzinzi. Nguo zenye kuonesha hadi mwili kwa wanaume na wanawake haziruhusiwi na wanawake lazima wafunike vichwa vyao. Watoto wa kiume wasivae nguo za kike na watoto wa kike wasivae nguo za kiume. Hadithi ifuatayo inaelezea vizuri zaidi kuhusu hili;

> *"Abu Hurayrah amesema: Mtume amempa laana mwanaume anaevaa mavazi ya kike na mwanamke anaevaa kama mwanaume ili aonekane mwanaume". (Abu Dawud)*

Kufuatilia wanachovaa watoto ni kitu muhimu kuna msemo unaosema "matendo huendana na mavazi" una maana kuwa watoto wanatakiwa wavae kwa heshima. Watu huvaa mavazi tofauti kulingana na matukio tofauti: katika ibada kila wiki, usaili, maadhimisho, tafrija au michezo. Watu hupenda kujichanganya, kuvutia na kuongeza fursa za kuweza kukubalika zaidi katika jamii. Mavazi, mitindo ya nywele na vito vya thamani vivaliwe kwa stara (aibu). Kwa ujumla wazazi hawapendi kuvaa hadi wakapendeza zaidi. Kama nguo nzuri

hutumika katika kila hali, basi mwenye kuvaa atapendeza kila mahali. Aina ya mavazi, tabia na mitindo ambayo haizidi mipaka ni katika kuonesha haya ya mtu.

Kadri iwezekanavyo wazazi wanatakiwa wawachagulie watoto zao mavazi yenye kukubalika. Itakuja kufikia kipindi mtoto wa miaka 2 au 3 wazazi wanakuwa wanatoa mitazamo yao kwa kile mtoto huyo anachovaa. Na katika hali isiyo ya kawaida, mtoto atakataa kuchaguliwa na mzazi mavazi ya kuvaa. Suluhisho katika hili itakuwa kuandaa baadhi ya nguo kama mbili au tatu za kumchagulia, ili mtoto aweze kuhisi kuwa yupo huru kuchagua atakayo.

Shuleni ambapo wanafunzi huvaa sare ya aina moja, huwa hawapendi hali hii hapo awali lakini punde husahau namna ya uvaaji wao na hivyo tatizo lao la mavazi huisha. Hii huondoa mijadala kuhusu nguo ya kuvaa kila siku asubuhi. Wasichana wanastahili wafahamishwe kuwa ingawaje wakati mwingine muonekano wa kiuchochezi unaweza kuwafanya waonekane wamependeza, hali hiyo inapelekea tafsiri mbaya kwa wavulana na inaweza kuwaathiri wao.

Hakuna kuchanganyika na kukutana faragha baina ya mvulana na msichana

khalwah ni makutano baina ya mtoto wa kiume na mtoto wa kike katika sehemu maalumu iliyo na kificho ambapo hakuna mtu anaweza kuwaona (kama vile ndani ya chumba cha hoteli). Ni muhimu kupambana na kuzuia khalwah kwa gharama zote. Mtume anatupa onyo kwa kusema;

> *"Mahali popote mwanaume na mwanamke wanapokutana peke yao, basi wa tatu wao anakuwa shetani" (Al Tirmidh)*

Hali ya mchanganyiko baina ya wanaume na wanawake lazima izuiliwe lakini mchanganyiko unaokuwa chini ya usimamizi wa wazazi kwa ukaribu katika misingi ya maadili inaruhusiwa. Mvulana anaweza kuvutiwa na msichana fulani kutokana na kumuona mara kwa mara msikitini, shule, maktaba au sokoni. Anaweza kumrubuni na kuanza kuongea nae ili afahamu kama nae amevutiwa kuwa pamoja nae. Baada ya mazungumzo wanaweza kupeana ahadi ya kukutana faragha sehemu fulani kama vile katika maegesho ya gari au katika makazi yao. Kwa kuwa hakuna anaewaona mvulana anaweza kuthubutu kumshika au kumbusu mtoto yule wa kike. Kama mtoto wa kike atamruhusu mvulana kufanya hivyo bila pingamizi, mvulana anaweza kupata ujasiri wa kufanya mengine zaidi ya hayo. Hatimaye wawili hawa huishia katika uzinifu bila hata kuwa na mpango wa kufanya hivyo hali ambayo inapelekea matatizo.

Mtego!

Kutazamana kwa macho → tabasamu la ukarimu → salamu → kuwasiliana Kukutana → kugusana → kupata hisia za kimwili → kutobadili uamuzi Dhambi ya uzinifu → matatizo!! matokeo yake yanaweza kuwa kupata magonjwa yanayoenezwa kwa zinaa, kupata ujauzito, kutoa ujauzito au kupata mtoto wa nje ya ndoa.

Kanuni za hapo juu zisipuuzwe kwa kuwa ni maelezo ya janga kuweza kutokea. Hata kwa watu wenye msimamo wa dini, huweza kuingia katika uovu kupitia hali hiyo. Watu wote wameumbwa kwa pande la nyama na hisia hata Nabii Yusufu aliwahi kukutana na hali hii;

Kukutana na kutoka pamoja; huu ni mlango wa zinaa kwa vijana. Huweza kusababisha maumivu na tabu kwa wahusika, familia zao na jamii. Katika tafiti ya mwaka 1999 nchini Marekani, asilimia 25 ya wanaume ambao walitafitiwa walisema kuwa, siku wanapokutana na mwanaume akalipia chakula kisha msichana akakataa kwenda kumridhisha mvulana, mvulana anakuwa na haki ya kumlazimisha msichana akubali kuingiliwa. Matukio mengi ya aina hii hayatolewi taarifa (Norris na wengine 1999, bohmer 1993).

Kitu chochote ambacho kinapelekea kumfanya mtu ashindwe kujizuia hisia zake kama vile vilevi, dawa za kulevya, muziki wenye kuchochea uzinzi, khalwah (makutano ya faragha kwa watu wa jinsia tofauti) haziruhusiwi. Kubusu na kushikana huuandaa mwili kuweza kuingiliana ambapo mtu hushindwa kujidhibiti.

Kukutana faragha pamoja, kutoka pamoja na kuwepo kwa uhuru wa kuingiliana kimwili huathiri ndoa. Nadharia iliyopo kuwa wanandoa wameanza kujaribiana na hivyo watajuana zaidi haina msingi. Jamii yeyote inayoruhusu kuwa na uhuru wa aina hii huwa na familia zinazoyumba na huwa na kiasi kikubwa cha utoaji mimba, vizazi vya nje ya ndoa na kutalikiana.

Vishawishi rika (makundi) na sababu nyingine

- Kuna sababu nyingi zinazopelekea watoto kujiingiza katika zinaa na mojawapo ni vishawishi na makundi. Sababu yao kuu ni kuwa kila mtu anafanya kitendo hiki. Sababu nyingine ni kutaka kujionesha kwa wakubwa wao kuwa nao wanaweza na ni watu waliondelea kijamii. Kwa baadhi yao inatokana na kutojua thamani yao ambapo huhisi kuidumisha kwa kuwa wazazi. Wakati mwingine ni kutokana na kukosa njia mbadala za kuzuia hisia zao. Ukosefu wa upendo na kutothaminiwa nyumbani pia huwa ni sababu ambapo mtoto hutengana na familia na kuanza maisha sehemu nyingine. Vishawishi vya ngono vipo kila sehemu, hususani katika majarida, makundi na hata katika runinga. Kiasi kikubwa cha maudhui ya mada za mapenzi kimeongezeka. Kwa mujibu wa tafiti ya mwaka 2005, 70% ya vipindi vya runinga nchini Marekani vilikuwa na maudhui kuhusu mapenzi, ikiwa imeongezeka kutoka 64% mwaka 2002 na 56% mwaka 1998. Kiasi kikubwa cha vipindi vyenye maudhui ya mapenzi kurushwa katika vituo vya utangazaji kimeongezeka, kufikia sawa na vipindi 8 kati ya 10 (sawa na 77%) mwaka 2005, ikilinganishwa na 67% mwaka 1998 na 71% mwaka 2002. Miongoni mwa vipindi 20 vinavyoongoza kutazamwa na watoto, 70% vinahusisha maudhui ya mapenzi na 45% vinahusisha mambo mengine yanayohusiana na mapenzi (Taasisi ya Henry J.Kaiser, 2005). Tafiti iliyofanyika mwaka 2010 katika nchi 25 za Ulaya ilibaini kuwa 23% ya watoto kuanzia miaka 9-12 wamekutana na vipindi vyenye maudhui ya mapenzi, katika mtandao au vinginevyo na katika sehemu hizo zote mtandao wa kimataifa ndiyo unaongoza kuonesha maudhui haya (sawa na 14%) kama ilivyo runinga, filamu au video (kwa 12%) (kwa mujibu wa mtandao wa watoto, jumuiya ya nchi za Ulaya mwaka 2014). Wazazi kwa hiyo lazima wajaze mapenzi kwa watoto wao, watumie muda wa watoto wao kwa kuelekeza vitu vizuri na kufanya nao mawasiliano yaliyo wazi.
- **Vilevi**; pombe na dawa za kulevya vina madhara kwa sababu hupunguza uwezo wa mtu wa kujidhibiti na huondoa uwezo wa mtu kujiepusha na kuingia katika uzinifu.
- **Kucheza muziki** (huhusisha kuchanganyika na watu wengi na kugusana kati ya wavulana na wasichana) na kugusana katika nyeti lazima kuepukwe, ikiwa pamoja na kubusu, kusugua mwili na kukumbatiana. Hivi vyote huamsha hisia za mwili na kuhamasisha watu wakaribie uzinzi.

Maana moja ya kucheza muziki na mtu wa jinsia tofauti ni:
Kucheza ni muonekano wetu tukiwa wima,juu ya hisia /matamanio yetu yaliyo katika ulalo

Nini cha Kufanya

Wazazi wanatakiwa wawashauri vizuri watoto wao. Wazazi wasifanye wajibu wao kuwa ni kuwapatia malazi watoto

wao pekee, kuwapa chakula pekee ila pia wanatakiwa watoe mwongozo wa kiroho na maadili.

- Wazazi wanatakiwa kufanya ubongo wa mtoto uweze kufikiria vizuri na awe na maadili pamoja na uelewa wa kutosha. Mfano wa ushauri ni ule unaoonesha namna gani Mtume alizungumza na kijana aliyeomba ruhusa kwa Mtume ili aweze kuzini kwa vile hakuweza kudhibiti hisia zake. Mtume akatoa sababu za kumkatalia na kuuliza kama yeye angekubali endapo mtu angehitaji kuzini na mama yake, dada yake, mtoto wake wa kike, shangazi yake au mke wake. Kwa kila swali kijana yule alisema "hapana". Kwahiyo, Mtume alimwambia yule kijana kuwa yule aliyetaka kumzini ni mama wa watu, dada wa watu, mtoto wa watu, shangazi au mke wa watu. Kijana yule akaelewa na kutubia na Mtume akamuombea dua asamehewe na Allah.
- Ni muhimu kuimarisha uelewa na kuzuia mtu kufanya uamuzi kwa kufuata makundi. Wazazi wanaweza kufanikiwa katika hili kwa kuwafundisha watoto wao mifumo tofauti ya maadili, mitazamo na mfumo wa maisha. Katika mazingira haya watoto wanaweza kukumbuka kutokunywa pombe, kutokula nguruwe, kutotumia dawa za kulevya na kujihusisha katika zinaa. Wazazi nao wasiwe na mahusiano nje ya ndoa kwa kuwa wao ni mfano kwa watoto.

Ndoa za Mapema

Hakuna umri maalumu kwa ajili ya ndoa. Imekuwa ni mtindo kwa vijana kuoa baada ya kupata shahada ya kwanza katika masomo yao, kupata kazi au baada ya kufikia umri wa miaka 26 au zaidi ya hapo. Wasichana nao husema kuwa wanataka kufunga ndoa baada ya kutimiza miaka 24 huku wakisema "sipo tayari kwa ndoa". Ingawaje wanakuwa na maumbile na hisia za kawaida kuhusu kuingiliana kimwili; lakini vijana lazima watambue kuwa kuna jambo moja kati ya haya mawili ambayo wanaweza kuchagua: kufunga ndoa au kujizuia hadi watakapofunga ndoa. Qur'an inasema kuwa;

> "Na wajizuilie na machafu wale wasio pata cha kuolea, mpaka Mwenyezi Mungu awatajirishe kwa fadhila yake." (Qur'an 24:33)

Mtume anasema;

"Mbele ya Allah, hakuna mcha mungu zaidi yangu kati yenu lakini mimi nafunga na kufungulia, nina swali na kulala usiku na pia nimeoa wake. Mwenye kukataa sunnah yangu hayupo pamoja na mimi". (AL-BUKHARI). **"Ndoa ni nusu ya dini, nusu iliyo salia ni kumuogopa Allah"** *(Al Tabaran na Al-Hakim)*

Mtume amesema;

> *"Enyi kongamano la vijana wenye uwezo miongoni mwenu basi waoe, kinyume na hapo wasioweza wafunge kuzuia matamanio yao" (Al-Bukhar)*

Pindi mtoto wa kiume au mtoto wa kike anapokuwa anatamani ndoa na hana uwezo wa kusubiri zaidi, wazazi wanatakiwa kufanya jitihada kuhakikisha ndoa inapita. Wazazi wasipofanya hivyo itakuwa wanalazimisha watoto wao kuingia katika maovu kwa namna moja au nyingine. Moja miongoni mwa wajibu wa wazazi unaelezewa na Mtume (s.a.w) kuwa;

> **yule aliyepewa neema ya mtoto, anatakiwa ahakikishe mtoto wake anapata haki za vitu vitatu; jina zuri, elimu na anapofikia umri wa utu uzima wazazi wanatakiwa wahakikishe anaoa/ anaolewa.**
>
> **(Tibrizi 1985)**

Kama wazazi watashindwa kutimiza maombi ya mtoto katika kuandaa kupitisha ndoa, dhambi atakazochuma mtoto pia zitaenda kwa wazazi pia. Hata hivyo ni muhimu kufahamu kuwa hakuna ulazima wa kutumia nguvu kutaka vijana wafunge ndoa. Baadhi ya wazazi hufanya makosa kwa kulazimisha watoto kufunga ndoa. Wazazi huamua katika miongoni mwa wanafamilia mtu wa kuoa mtoto wao badala ya kuwapa fursa watoto nao

wachague. Kwa kufanya hivi wazazi huwanyima watoto haki yao ya msingi katika kuwaona na kuwatambua wenza wao wa baadaye. Kwa upande mwingine, ndoa iliyoandaliwa kwa ushirikiano wa wazazi na ridhaa ya watoto ni jukumu la wazazi kuiandaa kuwa hivyo kwa sababu hii itapelekea maisha ya kudumu yenye furaha kwa wanandoa na familia zao.

Mipango ya ndoa ya aina hii inatakiwa izingatie misingi ya furaha kwa wanandoa na siyo maslahi ya wanafamilia. Jamii ina kazi nyingi za kufanya katika kurahisisha ndoa;

- Kuandaa mazingira mazuri ya kuwakutanisha wavulana na wasichana ili waonane na kufahamiana, na kuzuia kukutana faragha bila kuwepo mtu wa kuwatazama mwenendo wao.
- Kutoa elimu kabla ya kuingia katika ndoa kwa wavulana na wasichana na kuweza kuwaandaa kuwa wazazi yaani baba, mama na wake katika ndoa.

Uamuzi mzito: Kuchagua Ndoa ya Mapema na Elimu

Mfumo wetu wa elimu uliopo sasa umepelekea kuwa na tatizo kubwa la maingiliano ya kimwili. Kufikia hatua ya elimu ya juu(Chuo) au shahada inaashiria kuwa ndoa itabidi isubiri hadi kufikia umri wa kuanzia miaka 20. Lakini bado vishawishi vya kuingiliana kimwili kwa upande wa wanaume hushika kasi zaidi katika hatua za mwisho wa ujana wao na watoto wa kike katika hatua hii huwa na hitajio kubwa la kutegemea kutoka kwa watoto wa kiume, hivyo kuwafanya wawe wepesi wa kurubuniwa. Zinaa huchangia vitendo vya utoaji mimba, kupatikana kwa kina mama ambao huwajaolewa, kuenea kwa magonjwa ya zinaa na watoto kuwa na watoto wa nje ya ndoa.

Suluhisho kutokana na hali hii ni kuoa mapema wakati kijana akiwa bado anasoma au kujizuia hadi baada ya kuhitimu masomo ya chuo. Ndoa ya mapema huwa ni suluhisho zaidi endapo jamii itakuwa imewaandaa vijana kuwatunza wenza wao, watoto na kuweza kukabiliana na majukumu yao.

Katika jamii za sasa, kuhitaji vijana wawe wavumilivu na kutunza ubikira wao hadi kufikia katika umri wa miaka 20 ni vigumu sana kutokana na kuwepo kwa vishawishi vingi na vichochezi vya zinaa. Historia hutupatia fundisho zuri. Katika kipindi cha nyuma tatizo hili halijakuwepo sababu kufunga ndoa mapema ilikuwa ni mila na jamii iliandaliwa kukubali na kusaidia katika hilo. Katika kipindi cha Mtume na karne nyingi baadaye, mifumo ifuatayo ilikuwepo na kufanyiwa kazi;

a) Kusisitiza ndoa za mapema.

b) Familia zilitoa msaada mkubwa katika kulea watoto na wajukuu. Ilikuwa kitu cha kawaida kuona vizazi vitatu kutoka familia tofauti katika ukoo mahala pamoja, mara chache sana kuona familia moja ikiishi yenyewe. Familia zilikuwa hazihamihami sana kama ilivyokuwa sasa.

c) Uislamu umeruhusu uzazi wa mpango kwa kuwasaidia wanawake wenye umri mdogo kuchelewa kupata ujauzito, yaani waweze kupata ujauzito katika wakati wakiwa tayari kufanya hivyo. Hali hii inategemea sana ushirikiano na uelewa wa mume na mke wake.

Miongoni mwa maswahaba wa Mtume rehema na amani ziwe juu yao, kulikuwa na vijana wengi kama viongozi. Usamah Ibn Zayd alishiriki katika vita vya koo tofauti (Al-ahzab) akiwa na umri wa miaka 15. Akiwa na umri wa miaka 18 aliongoza jeshi likiwa na maswahaba wakubwa zaidi yake. Katika vita vya Uhud vijana wengi wenye umri wa miaka 15 kama vile Samrah Ibn Jundub na Rafii Ibn Khydayj nao walishiriki. Katika vita vya koo, Abdullah Ibn Umar, Zayd Ibn Thabit, Al-Bara Ibn Azib, Amr Ibn Hazm na Asid Ibn Thahir wote walikuwa na miaka 15. Qutaybah Ibn Muslim Al-Bahily aliongoza jeshi la Waislamu kuelekea China akiwa na umri wa miaka 18. Mfano kama huu pia unaweza kutolewa kwa maswahaba wanawake.

Kwa sasa, kina mama wenye taaluma au shahada wanaweza kulea watoto wao muda wote na wanaweza pia kufanya kazi kwa muda fulani hadi wakifikia umri wa miaka 30, na pia wanaweza kufanya kazi muda wote au kwa muda fulani baada ya watoto wao kufikia umri wa utu uzima, iwe kufanya kazi huko kwa kujitolea au kwa kupata ujira. Hakuna madhara kwa watoto na jamii haiwezi kunyimwa fursa ya kunufaika na ujuzi pamoja na busara kutoka kwa kina mama hawa wenye ujuzi. Siyo sahihi kumtazama mtoto mwenye umri wa miaka 13 na 19 kama mjuzi wa kutosha na kumfanya awe mtumiaji wa mwisho bila kuwa na majukumu pamoja na uzalishaji. Mwenendo wa sasa unaonekana kupanua umri wa utotoni hadi kufikia miaka 20. Kijana huwa tegemezi kiujumla badala ya kuwajibika, kuwa huru na kuzalisha.

Qur'an inazungumzia mitume ambao walikuwa vijana kama vile Ibrahimu, Yusufu, Musa, na Issa (rehema na amani ziwe juu yao) na wengineo ambao ni kiigizo kwetu na walitimiza wajibu wao kwa kufanya kazi nzito na nzuri katika vipindi vyao vya ujana. Pia kuna kisa cha watu wa pangoni (As hab al-Kahf) ambao nao walikuwa vijana walifuata mwongozo mzuri na wakapata mafanikio yaliyo makubwa.

Utaratibu wa sasa wa kuchelewa kufunga ndoa hadi kufikia miaka 20 hauridhishi. Utaratibu wa kufunga ndoa mapema wenye mafanikio ulikuwa ukitimizwa kipindi cha nyuma takribani kila sehemu ya ulimwengu huu. Tukizungumzia kidaktari, kubebea ujauzito na kujifungua ni rahisi sana katika umri mdogo kuliko kufikia umri wa kuanzia miaka 20 kuelekea 30 (na wanaopata ujauzito kwa mara ya kwanza wakiwa na umri mkubwa hupata tabu zaidi).

Tatizo hili ni kubwa, kweli lipo na linahitaji ufumbuzi wa haraka. Lazima tushughulike ipasavyo juu ya sintofahamu hii ya ugumu wa kujizuia kuingiliana kimwili, ulazima wa ndoa za mapema na umuhimu wa kuwa na familia katika ujana (na kupanga kuwa na watoto au kutokuwa na watoto).

MADHARA NA MANUFAA : ULINGANISHO WA JAMII YA KIFUSKA YENYE MAADILI

Njia ya Ufuska		Njia ya Maadili	
Zinaa Uhalalishwa	Madhara yake	Zinaa Uharamishwa	Manufaa yake
Uzinifu ni kitu rahisi, kinachovutia na kipo ukijisikia unafanya	▪ Magonjwa ya zinaa (STD) ▪ Mimba za utotoni ▪ Utoaji wa Mimba ▪ Watoto wasiofunga ndoa nao wanapata watoto ▪ Umasikini ▪ Talaka ▪ Kuvunjika kwa familia ▪ Kuibuka kwa familia ya mzazi mmoja ▪ Kuongezeka kwa uhalifu ▪ Kuongezeka kwa vitendo vya ubakaji	▪ Usikurubie zinaa ▪ Inakuwa ngumu kutenda zinaa ▪ Zinaa inakuwa haina mvuto na tabu sana kutenda kwa kuwa mianya ya utendaji haipo wazi ▪ Maingiliano sahihi huwepo ▪ Maingiliano huwepo katika ndoa (kwa wanandoa) ▪ Maingiliano salama huhamasishwa	▪ Wazazi wenye afya ▪ Watoto wenye afya ▪ Wazazi wa pande mbili huishi pamoja ▪ Kiongozi wa wachamungu ▪ Kupungua kwa uhalifu ▪ Familia yenye furaha ▪ Watoto wenye furaha ▪ Kupungua kwa vitendo vya ubakaji katika jamii

Kuwalinda Watoto dhidi ya Ukatili wa Kijinsia wa Watu Wazima

Ni asili ya watoto kuwaamini watu wazima na watoto wa Kiislamu wamefundishwa kuwaheshimu wakubwa wao. Watoto wanapata hofu endapo watakuwa hawajafanya walichoambiwa kufanya na wakubwa. Wengine huwaogopesha watoto ingawaje wanaojua kujilinda hufanya hivyo ili wasifanyiwe ukatili wa kijinsia. Ifuatayo ni habari ya kuwaeleza watoto dhidi ya watu waovu kwao;

▪ Kama mtu haumjui anakufanyia vitu ambavyo siyo vya kawaida, anakusogelea karibu, anakutazama sana na kukuzuia njia au kukufuata unaweza kukimbia na kuomba msaada. Kama una uhakika kuwa anakufuata unaweza kupiga kelele ya “moto! Moto! Kwa sababu watu wataweza kuja na yule anayetaka kukushambulia atachanganyikiwa.

▪ Usipande katika gari la mtu usiyemfahamu au kwenda sehemu na mtu ambaye humfahamu. Hata kama mtu huyo ataonekana kuwa rafiki kwako na kufahamu mengi kuhusu wewe na wazazi wako au anuani yako, usisite kusema kwa nguvu “Hapana”.

▪ Jiepushe kwenda sehemu na mazingira ya jirani yasiyokuwa salama na usitembee pekeyako kama unaweza kuepukana na hali hiyo hususani katika miji mikub-

wa. Ni bora kwa watoto wa kike wakaenda shule katika kundi au kusindikizwa na wakubwa wao.

- Hifadhi namba za dharura za askari polisi na fahamu namna ya kuzipiga hata katika giza. Tembea na pesa za sarafu, tokeni na simu za mkononi muda wote ili uweze kuwapigia wazazi wako au hata askari polisi.

- Kama itakulazimu usubiri ndani ya gari au nyumbani pekeyako, hakikisha umefunga milango na madirisha. Kama mtu usiyemfahamu atakuita mlangoni au kupiga simu, usiwape fursa ya kubaini kuwa upo pekeyako. Usimpe anuani yako mtu yeyote usiyemfahamu au taarifa yoyote kuhusu simu yako. Mueleze kuwa wazazi wako hawawezi kwenda kufungua mlango au kupokea simu kwa sababu wana kazi nyingi au hawataki kusumbuliwa. Jifanye kuwa unaongea na mtu mwingine chumbani.

- Kama haujiamini kutokana na mtu alivyokuwa anakutazama au kuongea na wewe, mueleze hali hiyo mtu mwingine mkubwa unayemuamini.

- Jifunze michezo ya kujilinda. Haihitaji mtu kuwa madhubuti sana kuweza kujilinda isipokuwa fikiria vizuri na fanya maamuzi sahihi haraka. Kuna mafunzo kwa ajili ya kujilinda ambayo hufundishwa mbinu za kujilinda na siyo kupigana.

- Kuwa makini na filamu za ngono kwa watoto. Watoto hawatakiwi kuonekana wakiwa hawajahifadhi tupu zao kwa wengine. Sheria zilizopo katika nchi nyingi zinakataza filamu za ngono na filamu za ngono kwa watoto pia zinakatazwa karibu kila sehemu duniani kote.

- Kama unamuogopa mtu, soma Qur'an suratul Fatihah, ayatul kursi, suratul falaq na suratul al-nas kuomba ulinzi kwa Allah. Rudia mara kwa mara na soma dua nyingine kwa kuomba msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Allah ni rafiki yako, kiongozi kwako na mlinzi wako.

Umri Unaofaa kwa Watoto Kuwatahadharisha kuhusu Ukahaba

Ukahaba ni mada ya elimu ya jinsia ambayo wazazi wanatakiwa waieleze kwa watoto wao, kwa kuzingatia umri wao. Watoto hawafahamu uhalisia wa maisha ya watu wanaojiuza kimwili na wanaweza kuwa wanajiuliza maswali mengi kuhusu wao. Hali hii pia iwe kikwazo kuwazuia wale wote wanaofikiria kuondoka nyumbani kwao kwa ajili ya kujikwamua kimaisha hapo baadaye. Wazazi wanatakiwa kutumia utaalamu na maadili yao. Ni muhimu kwa wazazi kuwaeleza watoto wao athari za maisha ya wanaofanya biashara ya kuuza miili yao ili kuzuia mitazamo waliokuwa nayo kuhusu mahusiano ya kimwili kwa kuzingatia maadili ya mtoto. Mwanamke anaweza kulazimika kuingiliwa na wanaume zaidi ya 20 kila siku, kupata magonjwa hatari ikiwemo ukimwi na kufariki mapema katika umri mdogo. Kwa kawaida hulazimishwa kufanya hivyo na watu wabaya na mazingira magumu waliyokuwa nayo.

Mara nyingi huwalazimu kuhama nyumba zao kutokana na kupigwa mara kwa mara au kufanyiwa ukatili wa kijinsia au wameathirika na matumizi ya dawa za kulevya, hivyo wanahitaji kupata pesa ili waendelee kutumia dawa hizo. Baadhi yao walitekwa wakiwa wanasafiri pekeyao na kufungiwa katika nchi nyingine ambazo huzungumza lugha tofauti na zao na wanashindwa namna ya kujisaidia. Hawataweza kuonana na familia zao tena. Wengine wamewekewa dawa za kulevya wakati wa usaili ili waweze kupatiwa kazi ya uhudumu au ulezi. Kisha wakachukuliwa mali zao zote, wakipelekwa nchi nyingine na kufungiwa. "Takribani ya watu 4,000 ambao wanafanya biashara ya ngono nchini Uingereza walipelekwa kwa kuuzwa. Watu wanaopinga biashara ya binadamu wanasema kuwa idadi kamili ni zaidi ya watu 4,000" (Morris 2008). Katika mazingira mengine, watoto wa kike hulazimika kuyakimbia makazi yao kutokana na matatizo wanayoshindwa kuvumilia na kuelekea kutafuta sehemu nyingine wanayoweza kuishi kwa amani. Kwa hali hii wale wanaomiliki biashara za ngono huwachukua na kuwalazimisha waingie katika biashara ya kuuza miili yao. Kiasi kidogo cha pesa huenda kwa anayeuza mwili wake wakati pesa nyingine huenda kwa anayemiliki biashara hiyo. Wazazi wanapoandaa maisha magumu kwa watoto wao, huandaa mazingira kwa watoto wao kukimbia maisha hayo kuelekea kuhangaika mtaani. Mtoto mwenye matatizo nyumbani na hafahamu nini cha kufanya katika hali hiyo anashauriwa kuomba msaada kwa mkubwa wake aliyekuwa mwaminifu kama vile ndugu, imamu, mwalimu, mshauri au askari polisi. Kukimbia au kuanza kutumia dawa za kulevya ili kuepukana na tatizo huongeza tatizo.

Kama watoto hawana ufahamu kuhusu biashara ya ngono wataanza kufikiria jinsi ilivyo. Wanaweza kufikiria kuwa ni nzuri na inamfanya mtu aridhike kimwili. Au anaweza kuhisi kuwa ni taaluma yenye faida, watakuwa na vipodozi vyote wanavyofikiria kuwa navyo, wataweza kuvaa nguo zenye kuvutia na kuwafanya wanaume wengi waweze kuwafuata au hata kuishi katika hoteli zenye hadhi. Mawazo haya yanaweza kuwepo

katika akili zao kama wazazi hawawezi kuwaeleza watoto wao mapema ukweli kuhusu biashara hiyo. Kwa bahati mbaya vyombo vya habari vimekuwa vikitetea maisha ya watu wanaofanya biashara ya ngono ambao wanaishi maisha ya kifahari kutokana na kuchuma pesa kwa wanaume waliokuwa matajiri. Emma Hamilton, mke wa Horatio Nelson ni miongoni mwa mfano wa watu hawa.

Pindi Mtoto Anapokuwa Mhanga wa Kuingiliwa na Ndugu yake au Kubakwa

Ni vigumu kwa wazazi kukubali kuwa mtu kutoka familia nyingine ametumia mwanya wa mtoto kuwa mdogo na kumuingilia. Wakati mwingine inakuwa vigumu kuthibitisha na huwa hataki kabisa kuamini katika hili. Katika mazingira kama hayo, ni bora kwenda kwa imamu, mshauri au askari polisi. Kama uhalifu umeshafanyika, askari polisi lazima apewe taarifa. Kila mtu anayo haki ya kuwa salama na kulindwa na siyo kulazimishwa kufanya kitendo cha zinaa chenye dhambi.

Ubakaji ni kitu cha kawaida kwa sasa, tafiti iliyofanyika kitaifa ilibaini kuwa takribani mtu mmoja kati ya wanawake watano (sawa na 18.1%) ya wanawake na mmoja kati ya wanaume 71 (sawa na 1.4%) ya wanaume nchini Marekani walitoa taarifa ya kubakwa katika kipindi cha maisha yao. Tafiti pia ilibaini kuwa 13% ya wanawake na 6% ya wanaume walikuwa wamelazimishwa kujiingiza katika mahusiano ya kimwili kwa kutumia nguvu katika maisha yao na 4.8% ya wanaume walitoa taarifa ya kusababishwa waweze kuwaingilia wanawake bila ridhaa yao (kwa mujibu wa CDC 2012). Nchini Uingereza na Wales, katika mwaka 2015 mwezi wa 3, makosa ya kuhusiana na mahusiano ya mwili yalikaririwa na polisi kuwa yameongezeka kwa 37%, matukio 29,265 yakiwa yanahusiana na ubakaji wakati matukio mengine 58,954 yakiwa ni makosa yanahusiana na mahusiano ya kimwili pasipokuwa na ubakaji (kwa mujibu wa ofisi ya takwimu za taifa 2015). Kwa mujibu wa taarifa ya takwimu iliyotolewa na wizara ya sheria, ofisi ya mambo ya ndani na ofisi ya taifa ya takwimu mwaka 2013, takribani wanawake 85,000 na wanaume 12,000 wamebakwa nchini Uingereza na Wales pekee ndani ya kila kipindi cha mwaka mmoja. Hata hivyo ubakaji na makosa ya utumiaji nguvu katika mahusiano ya kimwili huwa hayatolewi taarifa kwa kiasi kikubwa. Kuanzia mwaka 2010-2012, tafiti inayohusu mitazamo ya mahusiano ya kimwili na mfumo wa maisha ilibaini kuwa mwanamke mmoja kati ya wanawake 10 na mwanaume mmoja kati ya wanaume 70 walishawahi kuhusika katika mahusiano ya kimwili bila ridhaa zao na nusu kati yao hawakuwahi kutoa taarifa kuhusu matukio hayo kwa mtu yeyote (kwa mujibu wa *Welcome Trust, 2013*). Ikumbukwe kuwa wahanga wa vitendo vya ubakaji ni watoto wa jinsia zote, miongoni mwao wakiwa bado wadogo sana. Wanawake ambao wamefikia utu uzima pia hubakwa na watu wanaovamia katika makazi yao.

Ifuatayo ni mifano miwili: “Mahakama nchini Saudia imeamuru kuwa mtu mwenye kupatikana na hatia ya kubaka watoto watano atahukumiwa kwa kukatwa kichwa.” Mhanga mdogo kabisa katika tukio la ubakaji alikuwa ni mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 3, huku

akitelekezwa jangwani ili aweze kupoteza uhai wake (kwa mujibu wa BBC,2009).

Askari polisi wa jiji la London walimkamata mtu akiwa amefanya zaidi ya mashambulizi 100 kwa watu wazima (wenye umri kuanzia miaka 68 hadi umri wa miaka 93). Akiwa anafahamika kama mtukutu wa usiku, wahanga wengi katika matukio yake walikuwa wanawake na matukio yake mengi yalikuwa ya utumiaji nguvu katika kuingilia kimwili na ubakaji (kwa mujibu wa BBC 2009).

Kama msichana amebakwa, anaweza kuhisi maumivu, hujihisi hana nguvu, huhisi hasira na kuhisi kuchanganyikiwa. Anaweza pia kujihisi mwenye hatia kama amefanya jambo baya lenye kupelekea mvulana kuhitaji kumbaka kitu ambacho huwa siyo kweli. Au pia anaweza kuhisi aibu sana na kupata hofu ya kumueleza mtu yeyote. Msichana aliyebakwa anatakiwa awasiliane na askari polisi, apate matibabu na kuomba ushauri wa kitaalamu. Kufanya hivi ni muhimu kwa sababu kama atapata ujauzito au kupata maradhi mganga ataweza kuthibitisha kuwa ni kweli msichana huyo alibakwa na wala hajaingiliwa na mpenzi wake kwa ridhaa yake. Hii ni njia sahihi ya kuweza kujiepusha na tuhuma za uzinifu. Kama msichana ameshambuliwa basi ajaribu kukimbia au kujaribu kujitetea kwa kuparua na kucha zake. Baadaye askari polisi wanaweza kumtafuta mhalifu kwa njia ya vinasaba kutokana na vipande vya ngozi ya mhalifu kusalia katika kucha za yule msichana. Kupiga kelele hakushauriwi katika kufanya hayo yote kwa sababu kutasababisha mhalifu kupata ghadhabu zaidi na kuthubutu kumzuia mdomo wake asipige kelele, wanawake wengi pamoja na watoto ambao wamewahi kupoteza maisha walikuwa wakizuiwa wasipige kelele. Ingawaje kupiga kelele kunaweza kusababisha watu kuja kutazama tukio, haina maana kuwa wao watakuwa watetezi. Ni bora kuwa na saa kengele na kukiwasha kama itawezekana kumrushia mwilini (au hata kutumia kifaa chochote) kupitia dirisha. Uharibifu lazima ufanyike ili wakazi waweze kupiga simu kuwataarifu askari polisi. Pia inawezekana kabla ya kutoroka, anayeshambuliwa anatakiwa ajitahidi kupata kitu chochote kutoka kwa anayemshambulia hata kama ni kitu kidogo ikiwemo nywele ili kusaidia askari polisi katika kumbaini mhusika. Vijana wanatakiwa wafahamishwe kuhusiana na vitendo vya ubakaji kwa njia ya kawaida na ubakaji kwa kutumia dawa za kulevya. Dawa hizi zinaweza kutumika kwa kuwekwa katika vinywaji vyenye kulewesha na pia huweza kuwekwa katika vinywaji visivyoweza kulewesha.

Ushauri unatakiwa kutolewa kwa mhanga wa vitendo vya aina hii. Mshauri anaweza kumsaidia mhanga kurudi katika hali ya kawaida yaani kutokuwa na mshituko, hasira, huzuni, hofu au hali ya kukosa furaha.

Mtalaa wa elimu ya jinsia kwa mujibu wa Uislamu



Elimu ya jinsia kwa mujibu wa Uislamu ni muhimu ifundishwe nyumbani, kuanzia mtoto anapokuwa bado mdogo. Kabla ya kufundisha elimu ya mifupa/umbile la mwanadamu na fiziolojia, elimu ya imani kuhusu Mungu Muumba inatakiwa ianze kufundishwa. Bila ya kuwa na imani ya kumuogopa Mungu, baadhi ya tabia hufikiriwa kuwa zimeruhusiwa katika kukidhi matamanio ya mwili. Baba anatakiwa amfundishe mtoto wake na mama pia amfundishe mtoto wake. Kukosekana kwa mzazi mwenye kuweza kufanya hivyo, chaguo la pekee liliosalia ni kuwepo mwalimu wa kiume kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo kwa watoto wa kiume na mwalimu wa kike kutoa mafunzo kwa watoto wa kike katika shule za Kiislamu. Mtalaa unatakiwa upangiliwe kulingana na umri wa mtoto na watoto wa kiume wafundishwe sehemu tofauti ambayo watoto wa kike watakuwa wanafundishwa. Majibu yenye kuhusiana na maswali ndiyo yanatakiwa kutolewa. Kwa mfano, kama mtoto wa miaka sita atauliza “niliingia vipi katika tumbo la mama?” hakuna haja ya kuelezea kila kitu. Pia hauna haja ya kumueleza mtoto mwenye umri huu namna ya kuvaa kondomu. Vitu vingine vinaweza kufundishwa katika darasa maalumu kabla ya ndoa.

Mtalaa wa elimu ya jinsia kwa mujibu wa uislamu unakuwa na vitu vifuatavyo kwa mujibu wa (Athar 1990):

Aya za Qur’an na hadithi za Mtume

Ukuaji wa jinsia na kupevuka

- **Utaratibu wa kubaleghe**
- **Mabadiliko ya mwili wakati wa baleghe**
- **Hali ya kiakili, kihisia na kijamii wakati wa kubaleghe**

Fiziolojia ya mfumo wa uzazi

- **Kwa wanawake: Viungo vya mwanamke, hedhi, dalili za awali kuelekea katika hedhi**
- **Kwa wanaume: viungo, vishawishi vya kujamiiana**

Ubebaji mimba, kukuwa kwa mtoto na kuzaliwa kwake

Magonjwa yanayoenea kwa njia ya kujamiiana

Maadili ya jamii na dini

Namna ya kuepukana na vishawishi rika



Ni muhimu kutoa elimu ya jinsia kwa watoto; kinyume na hivyo wataweza kujifunza taarifa zisizo sahihi kutoka katika makundi na vyombo vya habari. Hata hivyo elimu hiyo isitolewe moja kwa moja. Maelezo ya waziwazi kuhusu elimu ya jinsia kati ya wazazi na watoto haitoleta manufaa. Mfundishe mtoto tofauti ya maumbile kulingana na jinsia, maadili yanayofaa na jinsia ya kuingiliana katika hali ambayo itapelekea kuwepo na maisha yenye kuzingatia misingi ya Uislamu.

Majukumu na malengo ya wanaume na wanawake yanatakiwa kuelezwa bayana kutokana na hatua ya ukuaji wa mtoto. Ni muhimu kwa wazazi kuwaeleza watoto wao kuhusu athari za kujihusisha na makundi yaliyopotoka. Lazima waoneshe kutoridhishwa na tabia mbaya na kukemea watoto wao kwa tabia za aina hiyo. Wazazi lazima wawatambulishe watoto wao namna ya kubaini na kujiepusha na tabia mbaya na kuwaelekeza watoto kwa vitendo kuhusu afya kijinsia (mahusiano ya kimwili yasiyokuwa na madhara)

Ni jukumu la mzazi kuhakikisha na kurahisisha kuwa mtoto anakuwa na mahusiano na vikundi vyema. Wazazi wasiwaache watoto wao wakiwa hawafahamu mahusiano ya kimwili yanayofaa. Wazazi wanatakiwa kuzuia watoto wao kuwapo nje ya nyumba zao nyakati za usiku mkubwa na kuwazuia kulala pamoja wanapokuwa katika jinsia tofauti isipokuwa pale tu kunapokuwa na mtu mzima mwenye kuaminika na kuweza kuwasimamia. Umri unaopendekezwa kwa watoto kufanya majadiliano na wazazi wao kuhusiana na mahusiano ya kimwili ni kama ifuatavyo:

- Umri wa miaka mitano; jadili tofauti ya maumbile kati ya mwanaume na mwanamke
- Umri wa miaka kumi;jadili kuhusu kubaleghe, kutokwa ute na kuingia katika mzunguko wa hedhi (ada)
- Umri wa miaka 15; namna ya kuzuia mimba
- **Zingatio**: Dkt Mohamed Rida beshir na Dkt Ekram na watoto wao Sumayah na Huda wameandika jumla ya vitabu 15 kuhusu namna ya kulea na mambo mbalimbali ya familia katika lugha ya iingereza na lugha nyinginezo. Pia wanatovuti ambapo wasomaji wanaweza kunufaika ;www.familidawn.com]

KAZI ZA KUFANYA



KAZI ZA KUFANYA 44: TAJIRISHA UBONGO WA MWANAO

Benjamin Franklin alikuwa anakaribisha wageni chakula cha mchana nyumbani kwa familia yake na kuanza kuzungumza masuala yenye kuhitaji kushughulisha akili ili watoto wake waweze kusikia na kunufaika kutokana na mazungumzo hayo bila ya watoto wenyewe kufahamu kuwa ni hadhira (Franklin 1909). Wazazi wanaweza kualika wageni hao nje au katika jamii yao na kuwaomba wazungumzie mada fulani ili kuwanufaisha watoto.

KAZI YA KUFANYA 45: MFUMO WA JEDWALI LA MATENDO MEMA KWA WATOTO

> ***"Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanao kumbuka"*** (Qur'an 11:114)
>
> Mtume amesema ***"Muogope Allah popote ulipo na unapotenda kosa basi fuatanisha jambo jema ili kufuta baya (kosa) hilo na kuwa na tabia njema kwa watu" (AL-TIRMIDHI)***

Wazazi wangeweka chati juu ya friji likiwa na jedwali lenye jina la kila mtoto likiwa na mgawanyo wa pande tatu; "vizuri zaidi", "vizuri" na "vibaya". Pindi watoto wanapokuwa wamefanya kile walichoelezwa alama ya tiki iwekwe katika upande wa "vizuri" na kama kutakuwa na makosa yamefanywa alama ya kosa iwekwe katika upande wa "vibaya". Kama watakuwa wamefanya kitu kizuri bila hata kuambiwa wanatakiwa wapate zawadi mara mbili au alama mbili za tiki katika upande wa "vizuri zaidi". Sifa itolewe hata kama watoto watakuwa wamefanya vizuri bila kuwepo wazazi wao (kama katika mazingira ya shule, au nyumbani kwa ndugu na rafiki zao); watoto watoe taarifa za matendo mazuri waliyotenda kwa wazazi wao ambao nao wanatakiwa kuamini. Alama zinatakiwa kutolewa kila juma na kila mtoto apate alama zake kulingana na matendo yake.

Kama alama za kosa zitakuwa chache, basi mtoto apewe zawadi. Ila kama alama za kosa ni nyingi mtoto asipatiwe zawadi yoyote. Endapo mtoto atapatiwa zawadi hakika atahamasika kuwa na matendo mazuri baadaye. Inaweza kuchukua zaidi ya juma moja kupata zawadi. Ni muhimu kutazama upande wa matendo mema, hata kama kitendo chema kilichofanywa ni kidogo, ili kuhamasisha na kufundisha watoto kuwa hata tendo jema dogo linaweza kuleta tofauti. Ingawaje haitakiwi kwa watoto kufundishwa wafanye mema kwa ajili ya kupata zawadi, utoaji wa zawadi husaidia kuwajengea kuwa na mtazamo chanya na kuridhia zawadi wanazopatiwa kuliko kupewa pongezi kwa dhahania. Wazazi pia waeleze kwa watoto wao kuwa tabia zao ni "nzuri" au "mbaya". Watoto wenyewe hawapewi jina la "wazuri" au "wabaya" isipokuwa tabia zao.

MFANO WA JEDWALI LA MATENDO MEMA/MATENDO MAOVU MTOTO WA KWANZA (HIBA) MTOTO WA PILI (HALA)

	HIBA			HALA		
SIKU	**MAALUM**	**NZURI**	**MBAYA**	**MAALUM**	**NZURI**	**MBAYA**
J-Tatu	▪ Kamsaidia dada yake mzigo ✓✓	▪ Kaondoa uchafu ✓			▪ katandika kitanda chake ✓	
J-Nne		▪ ameswali ✓	▪ amepiga makelele ✗			▪ amempiga dada yake ✗
J-Tano			▪ ametupa takakata sakafuni ✗	▪ amemsaidia bibi kuvaa soks ✓✓		
Al-Misi		▪ amemsaidia mwalimu kugawa vitu ✓			▪ amepanga nguo zake ✓	
Ij-Maa	▪ Kaleta ripoti nzuri ✓✓					
J-Mosi					▪ Kamaliza chakula chake ✓	
J-Pili		▪ Amehifadhi Qur'an ✓				
Jumla	8 ✓		-2 ✗	5 ✓		-1 ✗
Salio	**6 ANAPATA ZAWADI**			**4 ANAPATA ZAWADI**		

Sehemu 3

Kujenga Tabia na Haiba ya Mtu

- sura ya 14 —: Tabia na haiba 382
- sura ya 15 —: Kukuza ujasiri 392
- sura ya 16 —: Kupandikiza Mapenzi 410
- sura ya 17 —: Kufundisha ukweli na uaminifu 430
- sura ya 18 —: Kufundisha uwajibikaji 444
- sura ya 19 —: Kufundisha kujitegemea 462
- sura ya 20 —: Kustawisha Ubunifu 490
- sura ya 21 —: Watoto wa Kudekezwa na Kujitambua 512
- sura ya 22 —: Kumchagulia mwanao marafiki wema 520
- sura ya 23 —: Madhara ya TV, Video na michezo ya kompyuta 532

14

SURA YA KUMI NA NNE

- TABIA NA HAIBA

SURA YA KUMI NA NNE **382**

Tabia Na Haiba **382**

Utangulizi 384
Tabia Ni Nini? 385
Ujenzi wa Tabia 387
Tabia si muonekano wa nje, ina mizizi mirefu 388
Kuharibu Tabia Ya Mtoto 389
Haiba ni nini? 389
Ua la waridi, Mtoto, na Wazazi 389
Kazi za kufanya

Watu ni kama madini (yenye sifa tofauti); waliokuwa bora zama za ujahiliya pia ni wabora katika zama hizi za Uislamu, ikiwa wataelewa na kufahamu.

Utangulizi

Mtume (s.a.w) alisema:

> *Watu ni kama [madini au vyuma, vyenye sifa tofauti]; waliokuwa bora zama za ujahiliya kabla ya Uislamu pia ni wabora katika zama hizi za Uislamu, ikiwa wataelewa na kufahamu. (Al-Bukhari na Muslim).*
>
> *Ee Allah! Upe nguvu Uislamu na kipenzi chako baina ya wanaume wawili, Abu Jahl au Omar ibn al-Khatab. Na Omar alikuwa kipenzi zaidi. (Al-Tirmidhi).*

WANAUME HAWA WAWILI walikuwa na tabia njema toka utotoni mwao na kuweza kuwa viongozi katika koo zao za kipagani. Walikuwa na sifa bora kabla ya kuingia katika imani na elimu. Lengo kuu la kuwalea watoto ni kuwajengea tabia njema, kuwafundisha dhana sahihi, na kuwajenga katika maadili yanayokubalika ili iwe kawaida kwa watoto. Watoto huiga tabia za wazazi wao, na hivyo wazazi wanapaswa kuwa makini sana katika maendeleo ya kisaikolojia na kihisia. Kwa mfano, kama wazazi watashindwa kutimiza ahadi na wakubwa wenzao, msamaha utasaidia kuweka sawa kosa hilo. Kosa kama hilo likifanywa kwa mtoto lina madhara makubwa kwa kuwa watoto huhisi kwamba kuvunja ahadi si kosa kubwa. Hisia zao katika jambo hili linaweza kuwa kubwa na wanaweza kuhisi wanakatishwa tamaa. Katika umri wao mdogo, matendo ya wazazi wao yanaweza kuhamasisha kutoaminiana.

Matarajio ya kwanza ya kitabu hiki ni kutengeneza watumishi wenye huruma, na upole. Viongozi hawa wanapaswa kuwa bora kimwili pamoja na kuwa na tabia sahihi. Hizi ni sifa binafsi za uongozi. Sifa hizo ni viungo muhimu katika ujenzi wa misingi ya haiba ya mtu. Kama viungo hivyo havitakuwa sawa au kuwa dhaifu, basi mfumo mzima wa kibinadamu hushindwa kufanya kazi sawasawa.

Vijenzi vya tabia ni pamoja na vitu vingine mbali na imani na elimu. Malezi hutokana na ujuzi, imani, na hekima. Watu ambao hawakupata fursa nzuri ya malezi, lakini wenye sifa nzuri wanaweza kuongozwa kirahisi kwa ushawishi wa kimantiki, kwa kuwa wao ni tayari imara. Kwa upande mwingine, wale wenye sifa na haiba zilizo dhaifu hawawezi kuwa viongozi waasisi katika jamii, hata kama wana sifa bora za kiroho. Hivyo, malezi bora yanahitaji kutilia umakini katika kujenga viungo vya tabia kwa watoto katika umri mdogo kwa kuwa itakuwa vigumu sana kuwarekebisha baadaye.

NJIA TATU ZA UJENZI WA TABIA

Fahamu →Penda→Tenda

Moyo: Unapenda kizuri

Kichwa: Kinajua kitu kizuri

Tabia: Inatenda kizuri

Tabia ni nini?

Ufafanuzi wa kamusi kuhusu tabia unasema: ni sifa bora ya kipekee; mojawapo katika sifa inayounda na kumtofautisha mtu mmoja na mwingine; ujumla wa sifa za kiakili na kimaadili zinazomfanya mtu, kundi la watu au nchi; mtu anayetambulika kwa sifa za kuvutia; utu; heshima; na ubora katika maadili na kuwa imara.

Lengo la kulea watoto ni kuandaa watu imara, wenye tabia njema na wenye kuwajibika.

Maana ya tabia kwa lugha ya kiarabu ni haiba – tabia njema – nidhamu – heshima – adabu – mafanikio – utambulisho – tabia njema.

Malezi yanahusisha kuwajenga watoto na tabia za uongozi kutoka utotoni. Wanasaikolojia kadhaa na wanafalsafa wamesisitiza sifa za ujasiri, uhuru, ubunifu, mapenzi, uwajibikaji, uungwana, uaminifu, kujiamini, kujitegemea, uvumilivu, ucheshi, haki, ukweli, utiifu, na ushirikiano. Katika kitabu hiki, msisitizo umewekwa katika sifa zifuatazo:

Ujasiri, Ubunifu, Ukweli, Uaminifu, Mapenzi, Uwajibikaji, Kujitegemea, na Uhuru.

Viongozi maarufu duniani, kama wazuri au wabaya, wana sifa hizo zilizoainishwa hapo juu. Zingatia viongozi wakubwa wa kuigwa, kuanzia kwa Adam, Hawaa, Nuhu, Ibrahim, Sara, Hagari, Mussa, Maryam, Issa, na Muhammad (s.a.w). Fikiria pia viongozi wengine kama, Napoleon, George Washington, Mao Tse-Tung, pamoja na Maswahaba wa Mtume (s.a.w) kama: Sumaiya, Khadija, Aisha, Abubakar, Omar Ibn Khatab, Othman bin Affan, Ali Ibn Abi Talib, Fatima, Khalid Ibn al-Walid, pamoja na shujaa wa Ottoman, Muhammad al-Fatih. Wote walikuwa werevu, wabunifu, na wenye kuwajibika, vinginevyo, wasingeweza kufanikiwa katika uongozi wao.

Mafunzo yafuatayo kutoka kwa Mtume Mussa na Wana wa Israeli ni muhimu sana. Baada ya Mussa kuwaokoa Waisraeli kutoka utumwani mwa Firauni huko Misri, hakuwategemea sana kizazi cha waliookolewa kutoka utumwani kuweza kupata mafanikio, kwa kuwa walikosa sifa zilizohitajika kama vile ujasiri, uhuru, na ubunifu. Wameishi kwa vizazi hata vizazi kama watumwa wakisumbuliwa na uoga na mateso. Hakuweza (Mtume Mussa) kuwabadilishia tabia zao za msingi kwa imani na elimu kwa kuwa muda wa kuwafundisha ulishapita kama watu wazima. Chuma kilishapinda! Alisubiri kizazi kipya kilicho huru kizaliwe katika jangwa la Sinai, ambao angewalea na kuwafanya wawe watu imara, wenye ujasiri, uhuru, waaminifu, na wenye sifa ya kuwajibika. Mchakato huu wa kujenga tabia njema ulichukua miaka 40. Mussa na Haruni walitumia jangwa lililo wazi na huru la Sinai kuwajenga Wayahudi walio imara na waaminifu waliozaliwa baada ya kukimbia kutoka Misri.

Wazazi wanapaswa waanze kujenga tabia mapema angali watoto bado wadogo, kwa sababu kutoa mihadhara na kuhubiri kuna sehemu ndogo sana katika kufanya mabadiliko wakati wa utu uzima, wakati sifa nyingi za haiba huwa zimeshajengeka katika vitu vingi vinavyowaongoza wazazi. Hata hivyo ni vema njia hizo zikatumika kirafiki na mazingira ya furaha nyumbani. Pamoja na ukweli kwamba ujenzi wa tabia ni mchakato endelevu, unakuwa na mafanikio makubwa ukisisitizwa sana kwa watoto wadogo.

Tabia ndio inayomtambulisha mtu, siyo matukio wala mazingira.

Ujenzi wa Tabia

Ingawa ujenzi wa tabia huanzia utotoni na kuendelea, miaka michache ya mwanzo ionyeshe kuwa na mafanikio makubwa. Ujenzi wa tabia huwa wa siku hadi siku, mawazo kwa mawazo, na kitendo kwa kidendo.

Tabia inajengwa wakati gani? Je kitu chochote kinaweza kufanyika baada ya muda huo? Hatujui hasa majawabu yake ya msingi. Dkt. Spock anafikiri muda huo ni kati ya umri wa miezi mitano mpaka mwaka mmoja na nusu, kwamba pengine huo ndio muda muhimu kabisa wa kutengeneza tabia msingi za watu maishani. Muda huo ni ule ambao watoto wanapoanza kujitambua na kuonyesha tabia ya kujitegemea kama kutaka kushika wenyewe chupa zao na kutopakatwa muda mrefu. Wanakuwa wanajenga uhusiano wao wa kweli na wa mwanzo kwa wazazi wao. Kama mzazi ni mcheshi wanatarajia na watu wengine watakuwa hivyo. Mapenzi ya wazazi yatajenga mapenzi ndani yao. Kama, kwa upande mwingine, wazazi wao wenye aibu na woga, watoto watajifunza tabia hiyo hiyo wao wenyewe. Watatarajia ulimwengu mzima kuwa hivyo hivyo. Kuhusu dhana juu yao wenyewe, watoto hujifikiria kama wao ni wenye kuvutia au ni wenye kuchukiza, wenye thamani au wasio na thamani. Hii hutokea pale wanapotaka kuwa na mtazamo chanya au hasi kuhusu mambo mbalimbali. Kama watoto wangepata uhusiano mzuri kutoka kwa wazazi wao wasingeweza kufikiri kuhusu vitu au fikra. Kuanzia umri wa mwaka mmoja na nusu mpaka miaka mitatu, watoto huweza kujitambua wenyewe. Mtoto huvutwa na vitu vingi: kujitegemea dhidi ya kuwategemea wengine, kuwa msafi dhidi ya kuchafuka, ushirikiano dhidi ya kujitenga, na kupenda dhidi ya kuchukia. Tabia za watoto mwishoni mwa mwaka wao wa tatu zinategemea namna uhusiano wao na wazazi wao ulivyokuwa bora. Pia, ujenzi wa tabia, unategemea wazazi na watoto kutatua migogoro katika wakati huu.

Kufikia umri wa miaka 18, ujenzi wa tabia kwa mtu unakuwa umekamilika na kuwa imara. Ujenzi wa tabia hutokea wakati wa hatua ya chekechea, shule ya msingi, na sekondari. Elimu ya juu kuanzia miaka 20 na zaidi ni hatua ya maarifa na maendeleo ya elimu.

Kuwalea watoto sawasawa, kila katika haiba zifuatazo lazima zitiliwe maanani: kiroho, kimaadili, kimwili, kiakili, kisaikolojia, na kijamii.

Katika kila eneo, wazazi wanapaswa kuimarisha mahusiano na watoto wao. Mathalani, kama wazazi watakuwa ndio wenye maamuzi katika kila kitu na watoto wao wakafuata, watoto hao wanaweza kuwa wanyenyekevu. Ikiwa wazazi watakuwa wakali na kukosa mbinu nzuri za malezi, lakini wakawaachia watoto wao kugombana nao, watoto hao watakua na tabia ya kuwa wakorofi. Ikiwa wazazi watakuwa wasafi, na kuweza kuwa makini katika kufanya usafi, na kama watoto wao ni wapole, nao wataishia kuwa wasafi na wenye kuwa waangalifu sana. Kama wazazi wa watoto watawalinda katika tabia zao na kuwatazama ipasavyo, na kama watoto watakuwa wanaweza kushawishika, wanaweza kujitegemea.

Ingawa wanasaikolojia mbalimbali wanaeleza kwamba tabia ya mtoto mara nyingi hujengwa ndani ya umri wa miaka mitatu, haiba zingine zinaweza kuboreshwa ukubwani kama mazingira au msukumo utabadilisha. Tabia zingine hazitaweza kujengwa mpaka umri wa baadaye sana wa utoto, kama vile, tabia kuhusiana na watu wa jinsi zao na jinsi nyingine.

Walio imara hutaka amani wakati walio dhaifu hutaka haki

Rais Theodore Roosevelt aliwaonya Wamarekani juu ya kuwa warahisi na wenye kusubiri ridhaa: Vitu ambavyo vitaiangamiza Marekani, ni utajiri kwa gharama yoyote, amani kwa gharama yoyote, usalama kwanza badala ya majukumu kwanza, na nadharia ya kupenda kuishi kirahisi na kupata utajiri kirahisi maishani." Alionya, hakuna mtu aliye juu ya sheria, na kufaa kwa jambo fulani si sababu ya kukubali matendo yasiyokubalika. Maadili ambayo Wamarekani wameumbwa kwayo ni: Ujasiri, heshima, haki, ukweli, na utii.

Tabia si muonekano wa nje, ina mizizi mirefu

Tabia si kitu wanachoweza kupewa watoto kirahisi kwa kusoma au kwa uzoefu. Ujenzi wa tabia unapaswa kuandaliwa mapema wakati wa ujenzi wa haiba. Inachukua muda kwa wazazi kuimarisha tabia, yaani kama mizizi ya mti mkubwa inavyochukua muda kukua ardhini. Tabia njema huhifadhi heshima ya mtoto, na kutoyumbishwa na matukio ya kila siku. Tabia iliyojengwa vema haitikiswi kirahisi au kufuata mkumbo. Tabia ina uimara ambao hukua kama mizizi iliyozama sawasawa ndani ya watoto. Kama wazazi watapanda mbegu hizo kwa mtoto wakati wa kuzaliwa mbegu hizo (tabia) zitakua haraka.

"Zawadi iliyo bora ambayo mzazi anaweza kumpatia mwanawe ni tabia njema." (Tawfiq, 1967).

Kuharibu Tabia Ya Mtoto



‘wewe ni mpumbavu’

Haiba ni nini?

Kwa ujumla, kuna nadharia tatu kuu kuhusu haiba:

1. Nadharia ya kiutamaduni inaundwa na mambo matatu: akili, mwili, na roho.
2. Nadharia ya kisasa inasema kwamba haiba inaundwa na akili pekee. Shaykh al-Nabhany, mwanasheria wa Kipalestina, anaamini hili na kusema kwamba mwili hauna uhusiano na haiba.
3. Nadharia baada ya nadharia ya kisasa inasema haiba inajumuisha vitu vingi. Wataalamu wengi wa elimu na wanasaikolojia wanaamini ya kwamba vipo vipengele vingi vinavyounda haiba kama vile: vipengele vya kimwili, kiakili, kijamii, kihisia, na kiroho.

Msisitizo hapo ni katika misingi ya haiba, yaani: ujasiri, ukweli, uaminifu, kujitegemea, na uhuru.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa masula ya maadili, Michael Josephson (katika Ferguson na wenzake 1999), misingi sita ya tabia ni: ukweli, heshima, uwajibikaji, haki, kujali, na uzalendo.

Sifa zingine zimeelezwa na wasomi mbalimbali kama vile: busara, subira, uvumilivu, kujizuia, upole, kuwa na kiasi, kufanya mambo kwa urahisi, kujiamini, kujitolea, na uungwana. Tabia ni kitu cha ndani na inahusika na misingi ya haiba, ambapo vitendo vya mtu ndivyo vinakuwa matokeo yake. Tabia ni vitendo vinavyofanywa kwa kurudiwa rudiwa na kufanywa bila kupangiliwa baada ya muda fulani.

Sura zinazofuata zitagusa sifa mahususi za tabia: Ujasiri (Sur. 15), Mapenzi (Sur. 16), Ukweli na Uaminifu (Sur. 17), Uwajibikaji, (Sur. 18), Kujitegemea (Sur. 19), Ubunifu (Sur. 20), na Kujitambua (Sur. 21).

Ua la waridi, Mtoto, na Wazazi

Tunaweza kumfananisha mtoto na waridi. Lina chanua na kutoa harufu ya kuvutia, na kuonyesha uzuri. Hata hivyo, kikonyo chake kina miba mingi. Mzazi mwenye huruma hulikumbatia waridi taratibu na kwa uangalifu na kulipa fursa ya kuchanua, pamoja na kwamba anaweza kuchomwa na miba wakati mwingine. Mzazi asiye na subira, hujaribu kujiepusha na miba na kulishika ua katika sehemu yake laini, na hivyo kuliua. Anaweza kukwepa maumivu lakini akaliumiza ua. Wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao kwa uangalifu mkubwa na subira kama kulitunza ua la waridi.

KAZI ZA KUFANYA



KAZI 46: KUHIFADHI DUA

Hifadhi dua ifuatayo na familia iwe kwa Kiswahili au Kiarabu:

اللهم إني أعوذ بك من الهم والحزن، وأعوذ بك من العجز والكسل، وأعوذ بك من الجبن والبخل، وأعوذ بك من غلبة الدّين وقهر الرجال

> Mtume (s.a.w) amesema: Ee Allah! Najilinda kwako dhidi ya wasiwasi na majonzi, najilinda kwako dhidi ya udhaifu na uzembe, najilinda kwako dhidi ya uoga na ubahili, na najilinda kwako dhidi ya kudaiwa na kutukuzwa na watu wengine. (Abu Dawud).

Jadili na bainisha sifa zilizotajwa katika hadithi hii. Kwanini sifa hizi mbaya ziondoshwe katika utengenezaji wa haiba ya mtu? Je wazazi wanaweza kuchelewa kuwafundisha watoto wao kupambana na sifa hizo mbaya mpaka kufikia utu uzima? Vitu gani vinapaswa kufananishwa na kusimuliwa kwa watoto wako? Angalia mambo yaliyobainishwa katika hadithi hii:

- Wasiwasi na mfadhaiko au majonzi
- Kutokuwa na msaada na uzembe
- Uoga na ubahili
- Kuwa na madeni kupindukia na kudharauliwa na wengine

15

SURA YA KUMI NA TANO

- KUPANDIKIZA UJASIRI

SURA YA KUMI NA TANO **392**

Kupandikiza Ujasiri **392**

Utangulizi 394
Kanuni za Msingi za Ujasiri naWoga 396
Kufahamu Kujengeka kwa Woga kwa Watoto 398
Watoto Wanahitaji Kujifunza Hisia Pamoja na Ujasiri wa Kimwili 400
Baina ya Ujasiri na Utii 400
Msukumo wa Makundi Rika 401
Wazazi, Ushupavu, na Utamaduni 403
Kazi za Kufanya

Mtu imara si mwana mieleka mzuri, lakini ni yule anayejidhibiti anapokuwa na hasira.
(Al- Bukhari).

Utangulizi

Ujasiri ni uwezo wa moja kwa moja wa kupambana na kila kitu kilicho hatari, kigumu, au kiumizacho, badala ya kukikimbia. Kutokuwa na uoga au ushujaa kuna sifa zifuatazo: jasiri, imara, madhubuti, thubutu, na shujaa.

Ujasiri lazima uhamasishwe kwa watoto wadogo. Tunaweza kuwafundisha watoto sifa hizi kwa kuwajaza matumaini, kutarajia mafanikio, na kuhamasisha ndoto walizonazo watoto kuhusu wanachotaka kuwa. Tunaweza kuwafundisha watoto kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa kuwa watulivu na kusaidia na si kuwa na jazba. Wazazi wanaweza kuwafundisha watoto wao ushujaa, inavyoelezwa kama ujasiri unaokuzwa na heshima kwa, kuwajali, kuwaokoa, na kuwaheshimu watu wengine. Zifuatazo ni maelezo ya ujasiri kitabia au sifa:

1. Kusimamia kilicho cha haki, hata kama ni peke yako.
2. Kataa msukumo mbaya wa makundi rika.
3. Jaribu kufanya kitu hata kama unahofu hutafanikiwa au utafanya makosa.
4. Jielezee, hata kama baadhi ya watu hawatakukubali.

Baadhi ya changamoto zinazofahamika sana ambazo watoto huhitaji ujasiri katika kukabiliana nazo ni kama zifuatazo:

1. Kusema ukweli hata kama ukweli huo unakusababishia matatizo.
2. Kukabiliana na waovu.
3. Kukabiliana na msukumo wa makundi rika.
4. Kuanza shule.
5. Kuwa tofauti na wengine, kama; kuvaa hijabu (kwa wasichana wa Kiislamu, au kofia kwa mvulana wa Kiislamu.

6. Kufikia malengo ya juu zaidi.
7. Kuelezea maoni yasiyo maarufu.

Hata hivyo, kuna mazingira ambapo ujasiri unakuwa wa kidharau, kama vile, kutowatii wazazi, walimu, na sheria. Inakemewa kufanya mgomo bila kufikiri na kukataa kufuata utaratibu bila sababu za msingi ni kinyume na utamaduni na dini pia. Ni muhimu sana kuwa makini ili kuepuka kuchanganya utamaduni wa nchi na dini, hii ni kwa kuwa baadhi ya tamaduni hupingana kabisa na Sheria za Kiislamu. Mathalani, ndoa za lazima, kumpa baba jukumu la malezi ya watoto hata bila kujali tabia yake, kuwanyima watoto haki zao – hususani mabinti haki yao ya elimu, na kuwanyima wanawake haki yao ya kurithi, ambavyo vyote hivyo ni ukiukaji ya Sheria ya Kiislamu. Kuwatenga wanawake na wasichana, wakati wanaume na wavulana wanapata fursa ya kwenda popote, wakati wowote, na yeyote wanayemuona kuwa hawezi kuwachunga, na adhabu kwa wanawake na wasichana hutolewa kwa wasiwasi mdogo tu utakaojitokeza, jambo ambalo kimsingi, limekatazwa katika Uislamu. Tamaduni nyingi zilizobuniwa na watu na kupitishwa kimakosa huwa zinadhaniwa kwamba zimepitishwa na "dini". Ni vibaya pia kwa wazazi kuwalazimisha watoto wao kusema uwongo na kuwa na tabia mbaya.

Kauli juu ya Ujasiri

Mtume (S.A.W) amesema: "Kiongozi wa waliokufa mashahidi ni Hamza Ibn Abd al-Muttalib (Mjomba wake Mtume), na mwanaume aliyesimama katika utawala wa kidhalimu, akasema ukweli, na mtawala akamuua" **(al-Nisaburi, 1990).**

Hamza alipoingia katika Uislamu, alipambana na waabudu masanamu na waliotaka kumpiga Mtume. Alipata sifa ya "Kiongozi wa Waliokufa Mashahidi" alipouawa katika vita kwa shambulizi la kiuoga kutoka nyuma yake. Alikuwa mtu hodari sana.

- "Ujasiri ni kitu cha kwanza katika sifa za watu bora kwa kuwa kama huna ujasiri huwezi kupata fursa ya chochote cha wengine" Samuel Jackson.
- Thomas Jefferson alisema, "Mtu mmoja mwenye ujasiri ni kundi la watu wengi."
- Huwezi kugundua mabara mengine bila kupoteza kuona ardhi.
- Uovu utaendelea kumea ikiwa watu wema hawatakuwa na ujasiri.

Kanuni za Msingi za Ujasiri naWoga

Kinyume cha ujasiri ni woga, miongoni mwa vitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Woga unaweza kuwa matokeo ya kujifunza au unaoweza kuwa wa kutoka ndani kama njia ya kujilinda. Wazazi wanapaswa kuwa makini na woga wa aina zote mbili, yaani ule mdogo na wa kupita na ule wa kudumu alionao mtoto. Woga mwepesi ni ule unaotokea mara moja moja na kupotea, mara nyingine huweza kubakia kwa muda fulani na kisha kuanza kuondoka.

Hii inachukuliwa kuwa kawaida. Kwa upande wa woga wa kudumu, ni kwamba, huu hubakia au kuongezeka. Si kawaida kwa watoto kuwa na woga katika kuruka hewani, kujinyoosha, kuogopa mbwa, buibui, na sehemu zenye watu wengi. Woga au hofu ya kudumu inaweza kuhitaji subira isiyo na kikomo kukabiliana nayo, na pia huweza kuhitaji tiba ya kiuweledi. Hofu ya afya ni sehemu ya maisha ya kila siku, kwa kuwa huwasaidia watu wazima na watoto kuwa wepesi kukabiliana na hatari inayowakabili. Baadhi ya hofu katika afya ni kama kuogopa nyoka wenye sumu kali, moto, na asidi kali. Hofu huwa mbaya kiafya pale inapomzuia mtu kufanya majukumu yake ya kila siku. Zifuatazo ni baadhi ya mapendekezo ya kumsaidia mtoto kupambana na woga:

- Wazazi wanapaswa kupongeza kazi za watoto wao. Watoto wafanyapo jambo zuri, wana haki ya kupongezwa kwa juhudi zao, bila kutazama mafanikio katika kazi hizo. Ni muhimu sana kupongeza ujasiri wa kimaadili – kutotembea na wengine ambao wamekuwa wakitenda makosa, au kusema ukweli

wakati uwongo ungekuwa rahisi zaidi kwao.

- Mhamasishaji mkuu wa ujasiri ni tabia za wazazi. Wazazi wakiishi katika ujasiri, watoto watafuata. Watoto hupenda kuiga, kwa kufanya mambo kama watu wazima, hususan, wazazi wao. Mara nyingi hofu za watoto huwa sawa na hofu za wazazi.

- Wazazi wanapaswa kuonesha tofauti kati ya ujasiri na kuwa msemaji sana au kujionesha. Wazazi wanapaswa kutochanganya kati ya kukosa ujasiri, aibu na kuonyesha staha. Watoto wanapaswa kufundishwa wasimamie haki zao wenyewe pamoja na haki za wengine.

Wazazi wanaweza kuwaeleza kuhusu "ujasiri wa kimya", ujasiri wa kusema "Hapana" kwa kisicho sawa.

- Wazazi wanapaswa kutengeneza mazingira ya kukubalika na kuheshimika nyumbani. Watoto wanahitaji sehemu salama kuelezea mawazo yao kwa uhuru. Hofu yoyote ni ya kweli kwa watoto, bila kujali ni nyepesi kiasi gani kwa watu wazima. Wazazi wanapaswa kukwepa kuwakejeli na kuzidharau hofu za watoto wao. Mtoto aliyejaa woga asichekwe, kuadhibiwa au kulindwa kupita kiasi.

- Utaratibu endelevu wa kila siku huwapa watoto nguvu na uhimili. Mara nyingi hofu za watoto huchipukia kutoka katika kukosa taarifa kuhusu kitu kinachotokea katika maisha yao. Ikiwa mabadiliko katika utaratibu ni muhimu, mjadala kabla ya mabadiliko hayo na watoto ufanywe ili kuwaandaa watoto kwa tukio husika. Safari, wageni, au zima moto, vinaweza kusababisha hofu kwa watoto kwa sababu hawajui kitu cha kutarajia. Wanaweza kuulizwa wanafikiri nini kinaweza kutokea baada ya tukio, wanaweza kujumuishwa katika mjadala kuhusu tukio na matarajio yao. Maneno kama "kuogopa", "hofu" na "kutishika" yanaweza kutumika kuzungumzia namna watoto wanavyojisikia.

- Usiwalazimishe watoto kukabiliana na jambo wanaloliogopa kwa kuwa tayari wana hofu nalo. Wanapoonekana kuweza kulikabili, wanaweza kushawishiwa kukabiliana na woga polepole kwa kuliendea jambo hilo. Mathalani, kama watoto wanaogopa sauti ya mashine ya kuondoa vumbi ndani, wanaweza kuigusa wakati ikiwa imezimwa au mtu mwingine anaweza kuiwasha wakati wazazi wameshazungumza na watoto. Kuwapa fursa watoto kuamua wakati gani wanaweza kuzamisha vichwa vyao wakati wa kuogelea kunawapa fikra za kuweza kujiamulia cha kufanya na kupunguza woga.

- Usioneshe kuwa kinyume nao wakati watoto wako wanapohitaji kuliwazwa. Unaweza kuzizidisha hofu zao bila kukusudia, na kuonesha kwamba kuna mazingira ya kuwa na woga. Watoto wanaweza kupewa taarifa muhimu katika umri wao kwa utulivu na sauti ya upole. Mathalani, mzazi anaweza kusema, "Hiyo ni sauti kubwa sana, sivyo? Ni gari la wagonjwa, litakuwa likienda kutoa msaada."

- Watoto wanapaswa kukumbushwa kwa wema na kwa upendo kwa vitu ambavyo si hofu tena kwao. Hii itawapa na itasaidia kupambana na hofu zao pia.

- Wasaidie watoto kufahamu woga. Mathalani, "Sauti kubwa, kama milipuko na radi, inaweza kuwa ya kutisha", "Mbwa hubweka kwa sababu hivyo ndivyo wanavyozungumza na wakati mwingine hubweka sana wanapokuwa na furaha kumuona mtu fulani." Usitarajie hofu ya mtoto itaondoka mara moja, kuwa na subira.

Watoto huchukua kile wanachokisikia kawaida, kama vile, “Polisi atakukamata kama hutaingia ndani ya gari na kuketi”, au mgeni anaposema “Wewe ni mzuri sana, nitaondoka nawe leo kwenda nyumbani.” Kifo kisielezwe kama usingizi, kwa sababu watoto wanaweza kuogopa kwenda kulala. Pia watoto wasielezwe watakuwa wakubwa wakiacha woga wao. Hii humpa msukumo mkubwa juu ya utoto.

Kufahamu Kujengeka kwa Woga kwa Watoto

UMRI	WOGA ULIOZOELEKA UTOTONI
Miezi 6	Wageni
Miezi 8	Kuwa mbali na wazazi, kuanguka
Mwaka 1	Kuwa mbali na wazazi, kelele, wanyama, madaktari, kuoga
Miaka 2	Kuwa mbali na wazazi, mafunzo ya chooni, wakati wa kulala, madaktari, kuoga
Miaka 3	Kupoteza wazazi, mafunzo ya chooni, wakati wa kulala, mizimu, yeyote atakayekuwa tofauti na wanafamilia kama vile; mlemavu, mwenye ndevu, rangi tofauti ya ngozi au mavazi mengine
Miaka 4	Kelele, wanyama, mizimu, watu wanaoonekana tofauti na familia, wakati wa kulala, kupotea, kwenda shuleni, kuumia, kupotea, kufariki au kuachana kwa wazazi.
Miaka 5	Kelele, wanyama, mizimu, wakati wa kulala, kupotea, kwenda shuleni, kuumia, kupotea au kufariki au kuachana kwa wazazi.

Ni kawaida kwa watoto wote kuwa na woga na kitu fulani wakati mmoja au mwingine, haijalishi iwe ni radi, mbwa, nyuki, kiza, au vitu vya kufikirika kama mizimu ya kutisha uvunguni mwa kitanda. Kadri mtoto anavyojifunza mambo mbalimbali ya ulimwenguni, idadi ya vitu anavyoviogopa huongezeka. Utafiti mmoja uliofanywa umeonesha kwamba asilimia 43 ya watoto kati ya umri wa miaka 6 mpaka 12 huwa wana wasiwasi na woga kwa kiwango kikubwa (kwa mujibu wa Jarida la Marekani katika masuala ya elimu ya akili 2004 na kunukuliwa toka Jumuia ya Afya ya Watoto 2015) Moja ya hofu kubwa kwa watoto wa umri huu ni kiza, hasa hasa wanapoachwa pekeyao mahala penye kiza. Silika ya baadhi ya watoto huwafanya kiasili wawe waoga sana kuliko wengine. Wakati wazazi wanapowaliwaza watoto wao walio katika hofu, wanawasaidia kujisikia salama. Kujisikia huku kuwa salama huwapa ujasiri wanaouhitaji kukabiliana na woga wao.

Watoto wachanga huogopa kelele za barabarani, wageni, na kuwa mbali na wazazi wao. Wakikua kidogo huogopa wageni, kuwa mbali na wazazi wao, na wasiyoyajua. Kadri wanavyokua kifikra, kwa wale ambao bado hawajaanza shule na wale walio katika umri wa kwenda shule huogopa kiza, kuumizwa, wanyama, kuachwa peke yao, na kifo. Zaidi ya hofu hizi, wale walio katika umri mkubwa kidogo wa kuweza kuwa shule huogopa kutoishi vile wanavyotaka wazazi wao au walimu wao. Wakati wa kubaleghe, vijana mara nyingi huogopa vita vya kinyuklia, majanga ya kiasili, na ugaidi.

Watoto wanaweza kuogopa kitu ambacho hakifikiriki kabisa. Mathalani, watoto wanapoanza kutembea na kutambua kwamba wanaweza kwenda mbali na mama zao, hutambua kwamba mama zao pia wanaweza kuwaacha hata wao. Au maji yanayoingia mtaroni, hutambua kuwa hata wao wanaweza kutumbukia humo, hivyo wanaweza kutumbukia humo. Mazingira yanayomzunguka mtoto, kama maeneo asiyoyafahamu, yenye watu wengi, na vivuli kutokana na mwanga wa taa za usiku yanaweza kuongeza hofu.

Woga wa watoto unapozidi na kuwasumbua katika maisha yao, wazazi wanapaswa kumtafuta mtaalamu wa kuwasaidia. Wakati wa kufanya maamuzi kama haya, wazazi wanapaswa kujiuliza maswali yafuatayo:

- Hofu hizo zimedumu kwa muda gani?
- Je, hofu hizo zina madhara kwa mtoto?
- Je, hofu hizo zinaingilia tabia za kawaida au mahusiano?
- Je, hofu hizi zinamzuia mtoto katika michezo yake au katika kulala?

Watoto Wanahitaji Kujifunza Hisia Pamoja na Ujasiri wa Kimwili

Ujasiri wa kihisia hutokea pale unapokuwa huna hofu ya kusema kitu fulani, kuandika kitu fulani, au kufanya kitu chochote kwa hisia, kama kulia. Ujasiri wa kihisia ni ujasiri wa kiukweli, ni namna ya ujasiri ambao ni chanzo cha uimara katika maisha. Filamu maarufu zinazolengwa kwa wavulana zinaonesha kusisitiza aina moja ya ujasiri: kuwa mpinzani mwenye nguvu. Utayari wa kupambana na adui, kukabiliana na mnyama mkubwa, kumshinda mzimu, na kukabiliana na jambazi mwenye bunduki, ni miongoni mwa njia ambazo vyombo vya habari vinavyoonesha aina ya ujasiri wa kiume. Wavulana wanahitaji watu wa kuwaiga katika ujasiri wa kihisia. Wanahitaji kuona ujasiri katika familia zao na katika maisha ya watu wanaowazunguka.

Jamii inapaswa kuwa na mifano ya kuigwa katika ushujaa ambao unaenda zaidi ya mtu wa miraba minne. Ingawa watu wazima wengi huonesha ujasiri wa kihisia kazini mwao au katika maisha yao binafsi, ni nadra sana kuwaonesha watoto wao kushuhudia nyakati hizo za kujitambua na ushujaa. Watu wanapaswa kuzungumzia hilo.Wazazi wanapaswa kuwapongeza watu ambao huonesha ujasiri wa kihisia hasa wale ambao huamua kuzungumza, kuwa timamu pamoja na kwamba wamesongwa na changamoto, kujifunza lugha mpya, na kusaidia kama ingekuwa rahisi kuchukua hatua mbadala. Pindi ujasiri wa kihisia unapotolewa moja kwa moja, huwa na mafanikio chanya kwa watoto.

Kigezo kingine cha ujasiri wa kimaadili ni ujasiri wa kudhibiti hisia na kauli wakati wa hasira. Hii ni kinyume na nguvu ya kimwili kama ilivyobainishwa na Mtume (s.a.w).

Mtu imara si mwana mieleka mzuri, lakini ni yule anayejidhibiti anapokuwa na hasira.(Al- Bukhari).

Baina ya Ujasiri na Utii

Watu wazima wengi wameeleza namna mrejesho wao katika hofu ulivyopatikana kipindi cha utoto wao kutokana na wazazi au walimu walipotumia mbinu za vitisho au kuaibisha. Watoto walifundishwa kwamba ni vema wakatii “au vinginevyo!”, na walikuwa wakinyanyaswa, kutishwa, na kuabishwa hadharani kutii kile wengine wanachotaka wafanye. Watoto wanakuwa hawana budi kufuata kibubusa matakwa ya watu wazima. Walielezwa kwamba: “Watoto wanapaswa kuonekana si kusikika!” Kauli hizi hujenga hofu na kuangamiza ujasiri.

Watoto wenye hofu na kutojiona salama hutafuta “usalama” kwa kubaki katika kazi au mahusiano yasiyowastahili. Kutokana na hofu zao za kutokuwa na uwezo wa kupata mafanikio, hawawezi kupata kazi

nyingine iliyo bora zaidi. Wanakuwa na hofu ya kukataliwa. Wanajijengea kuwa wakosaji, wenye aibu, na wenye udhaifu. Hawajiamini, hawaoni kama wanastahili kupata vyenye thamani, na hawapambani kutafuta uhuru. Inahitaji ujasiri kuwa huru. Hawa watu wamekuwa wakifundishwa tangu utotoni kwamba hawakuwa salama wao wenyewe na kwamba walihitaji msaada wa wengine. Hawakufundishwa ubunifu, lakini hukaripia mara kwa mara katika ubunifu wanaoufanya, na badala yake, huelezwa kutii utaratibu.

Msukumo wa Makundi Rika

Watoto wanapokuwa wadogo, wazazi au walezi wao huwafanyia maamuzi muhimu watoto wao. Hata hivyo, wanapokua, watoto wanapaswa kujifunza kufanya maamuzi yao wenyewe. Vijana wamekuwa wakitumbukia katika changamoto mbalimbali za kijamii inapokuwa ni lazima kufanya maamuzi yao. Ndugu na jamaa huwapa msukumo kujaribu kunywa pombe, kutumia dawa za kulevya, au kufanya uasherati. Ni vigumu kusema "Hapana" na kwenda kinyume na kikundi rika.

Kuiga → Kuhusiana na jamii → Kujitawala

Hatua tatu za ukuaji zinaweza kubainishwa: hatua ya kuiga kutoka kwa wazazi – kutoka kuzaliwa mpaka miaka 7; hatua ya kuhusiana na jamii – kutoka miaka 7 mpaka miaka 14; hatua ya kujitawala – kutoka miaka 14 mpaka miaka 21.

Watoto wanataka kuingia na kuwa sehemu ya makundi, na hupenda kuonekana kuwa na utaalamu kuliko walivyo kiuhalisia. Hawataki kuonekana kama wao ni "watoto". Si rahisi kwao kujitegemea wao wenyewe na kufanya wanachofikiri ni kizuri, hasa pale marafiki wanapowahamasisha kujaribu kunywa pombe, au kuvuta sigara. Kikundi kinaweza kumchukua mtoto mmoja, au kumuacha mwingine katika jambo hilo. Mara nyingine watoto huhusika katika harakati za kutafuta madaraka katika kundi dogo la marafiki. Mtoto anaweza akaambiwa na rafiki yake "Sitakuwa rafiki yako mkubwa kamwe" ni silaha maarufu inayotumiwa na watoto wadogo dhidi yao.

Hata watoto wadogo hutaka kuwa sehemu ya kikundi fulani, na wazazi wanapaswa kuwaelezea kuhusu jambo hili la msukumo wa makundi. Wazazi wanaweza kuzungumza na watoto wao kuhusu mambo yanayojiri katika makundi. Kama kikundi cha watoto kitakuwa kikicheza kombolela (mchezo wa kujificha), kwa mfano, ni vema kila mmoja wao akazingatia utaratibu, vinginevyo, mmoja wao anaweza kuvuruga mchezo. Hata hivyo, kama kikundi kinataka kufanya kitu cha hatari, kukataa kuwa miongoni mwa kikundi hicho ni jambo jema. Kukataa kwa mtoto mmoja kukubaliana na maamuzi ya kikundi, yanaweza kuwapatia wengine fursa ya kusema "Hapana" kwa kikundi hicho vile vile.

Wazazi wanaweza kujadili tofauti za mtu mmoja mmoja na watoto wao. Je, kila mtu anapaswa kufanana na mwingine katika kikundi? Kama watoto wataheshimu tofauti za kila mmoja, watakuwa na maisha mazuri katika ujana na utu uzima wao. Wazazi wanaweza kujadili juu ya kuwa kiongozi au mfuasi. Wanapaswa kuwasikiliza watoto wao kwa makini ili waweze kutambua changamoto za kuiga makundi rika. Kama wazazi wanaweza kuwasikiliza watoto wao na kujadiliana nao kuhusu mambo mbalimbali bila kuhukumu, ni dhahiri kwamba watoto hao wataendelea kuzungumza na wazazi wao kadiri wanavyokua.

Makundi yanaweza kuwa mazuri, lakini bado msukumo wa makundi unaweza kuwa mbaya. Hata hivyo, watoto wengine watawashawishi wenzao katika afya, katika hali chanya na yenye kusaidia. Pindi wazazi wanapowaheshimu na kuwa marafiki wakarimu kwa watoto wao, watoto wao watakuwa wakiona na kujifunza mambo muhimu kuhusu namna na kuwaheshimu wengine.

Pindi wazazi wanapovumilia tofauti walizonazo na dhidi ya wengine na kumthamini mtu mmoja mmoja, ambaye anaweza kuonekana kama mgeni na wa tofauti, watoto wao pia hujifunza kuwavumilia wengine. Pindi wazazi wanapokuwa hawatoi hukumu juu ya watu kulingana na kipato chao, nguo zao, dini yao, au kabila zao, watoto wao watagundua kuwa hakuna kitu kitakachosumbua kwa watu kuwa tofauti. Ingawa makundi huweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa mtoto anayekua, wazazi wanaweza kuwa na ushawishi mkubwa zaidi.

Marafiki ni wa muhimu katika maisha ya kila mtu, na kujifunza kuwa na ushirikiano katika jamii na wengine ni sehemu ya maendeleo ya kawaida ya watoto. Watoto wote wanapaswa kujifunza namna ya kushabihiana na makundi yao wakiwa bado wanashikilia

tabia zao na utambulisho wao. Pindi wazazi wanapowasaidia watoto wao kujiamini na kuwa majasiri, watoto hao watakuwa wazuri sana katika kukabiliana na misukumo ya makundi. Watakuwa na uwezo wa kusema "Hapana" kwa mambo yanayowafanya wajisikie vibaya au yale ambayo wanaamini hayako sawa.

Wazazi, Ushupavu, na Utamaduni

Ujasiri ndio unaomtengeneza kiongozi. Kuwawezesha watoto katika ujasiri huanza mapema kwa mtoto. Inaweza kuwa rahisi kuliko inavyodhaniwa kwa ujumla wake, kwa sababu utafiti unaonesha kwamba watoto huzaliwa wakiwa hawana woga kwa mazingira yao, na kwa kawaida wazazi ndio wanaopandikiza hofu katika fikra zao. Wanawafanya watoto waogope wanyama, nyoka, kiza, vitu virefu, mizimu, mbwa, na maji. Namna watoto wanavyolelewa ndivyo wanavyojengwa katika ujasiri. Ni kawaida Katika baadhi ya tamaduni, kuwafundisha watoto kwa kutumia vitisho na utesaji katika kuwafanya watoto kuwa wapole na watiifu. Njia hii inaathiri namna watoto wanavyofundishwa imani, dini, kuhifadhi Qur'an, na majina mazuri ya Allah. Njia nzuri ni ile ya kuanza na Aya zenye Upendo na Ukarimu, majina na sifa za ukaribisho za Mungu. Mwanzoni, msisitizo lazima uwekwe katika upendo na Pepo, si katika adhabu na Moto.

Wasimulie visa vya ushujaa wa Mitume. Nabii Ibrahim, aliingia katika nyumba ya ibada, kuwavunja masanamu kwa shoka lake, kisha kulining'iniza shoka hilo shingoni mwa sanamu kubwa kuliko mengine; Mussa na kaka yake Haruni bila woga walipambana na Firauni; na Muhammad (s.a.w) aliswali Katika Ka'aba ya Makka, ingawa wapagani walikuwa wakimtishia na kumrushia mawe na taka. Tumia visa vya kweli katika maisha yako. Ni muhimu watoto wafundishwe kujihisi kama wanaishi wakiwa wanamuona Mungu au Mungu anawaona wao. Wafundishe watoto kuwa mashujaa, kujijali na kuwa na maadili yanayofaa, kutomhofia yeyote isipokuwa Mungu wa kweli, anayewapenda kwa mapenzi ya dhati.

Kwa bahati mbaya baadhi ya wazazi hawawafundishi watoto wao kujichanganya na kucheza na wengine, na huwatenga kabisa. Huwaeleza namna kuogelea kunavyoweza kuhatarisha maisha yao, namna kuondesha farasi kunavyoweza kuwajeruhi, na namna michezo inavyoweza kuwavunja miguu na mikono yao. Wazazi huwafundisha woga wanapowazuia watoto kuweza kuchagua wanachotaka kufanya na kuwanyima haki yao ya kufanya maamuzi. Hii inawafundisha watoto kwamba wazazi ndio pekee wanaofahamu na kwamba wazazi wanapaswa kuamua na kufikiri kwa niaba yao. Wanawaharibu watoto kwa kuwapatia kila kitu kwa ajili yao na kufanya juhudi zote kwa ajili yao. Wanawazuia watoto kuthubutu katika kitu chochote katika maisha, na kuwafundisha wasifanye juhudi zozote. Wazazi pia hufanya juhudi za kuwalinda sana watoto wao na kuwa na hisia; hawawaruhusu watoto watoke nje ya nyumba zao, wakiogopa wataugua na kupatwa na mafua. Wanawafundisha watoto kwamba watoto hawawezi kuaminiwa na kuruhusiwa kuthubutu kwa namna yoyote. Suluhisho ni kuwafundisha watoto kuwa wajasiri kwa kuwaweka katika mazingira ambayo huhitaji ujasiri

na kuwa na uthubutu. Wafundishe watoto namna ya kuwa salama katika mazingira yasiyokuwa salama. Waeleze watoto, msituni, kiwandani na kwenye meli kukoje; kitu gani ni salama, kipi si salama, na namna gani ya kuelezea tofauti hizo. Ushujaa unapaswa kuwa sehemu ya utamaduni wetu. Kumbuka: Allah huwasaidia wale walio mashujaa.

Mjomba wake Mtume (s.a.w) aliitwa Hamza, lenye maana ya "Simba"

Kutokana na ujasiri na uwezo wake, alipewa jina la utani la "Asadu Allahi wa Rasuluh" lenye maana ya Simba wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake!

Tunaweza kuwasimulia watoto visa mbalimbali vya ujasiri katika wanyama kama vile:

Katika nyumba ya simba kuna harufu ya kunukia, ambayo mbweha huogopa kuisogelea hata kama simba yuko mbali na nyumbani kwake. Kuna hulka ya ndege kuwa na hofu hata wakiwa wanaruka. Pia kuna ushujaa na heshima kwa vipanga hata kama wanakufa.

"Tunapaswa kujenga mfereji wa kurudisha mtiririko wa hofu."
Martin Luther King, Jr.

AIBU AU HAYA?

Tunachokihamasisha ni haya, siyo kuwa na aibu. Aibu ni kuwa na woga kutoka ndani ya nafsi na kuogopa kukutana na watu wengine. Haya ni kuwa na umakini, upole, na kuwa na heshima. Vile vile ina maana ya mtu asiye na makuu.

KAZI ZA KUFANYA



KAZI YA 47: KUPEANA UZOEFU JUU YA WOGA

Zungumza na watoto wako juu ya baadhi ya hofu ulizowahi kuzipata katika maisha yako na ulichokifanya ulipotishwa. Watoto wanaweza kueleza maoni na uzoefu wao pia.

KAZI YA 48: NJIA TISA ZA KUMLEA MTOTO MWOGA

Jadiliana na familia yako kuhusu malezi mabaya na kusimulia mifano na visa kutokana na uzoefu wako. Kama makosa haya yanatokea unawezaje kukabiliana na madhara yake?

- Kutokukubalina na mwanao na kumdhalilisha, hususani, mbele ya marafiki zake.
- Kumuita majina mabaya mwanao. Kumwambia kwamba hana faida yoyote.
- Kutomuamini mwanao na kila mara kutoamini asemacho. Kumwambia hawezi kuwa mkweli na kwamba wengine wanajua zaidi kuliko yeye.
- Kukataa kila kitu kizuri kutoka kwake. Msisitizo kuwa katika makosa yake tu.
- Kuwapendelea kaka zake, dada zake, na binamu zake. Kila mara kumlinganisha na wao – kwa namna gani yeye ni mbaya na mzembe na kwa namna gani wenzake ni wazuri na wachapakazi.
- Kila mara kumuweka mwanao karibu yako ili ajisikie yuko salama.
- Kumharibu mwanao na zawadi lukuki.
- Kutomruhusu mwanao kuzungumza mbele ya mtu yeyote. Anapaswa kuwa kimya mbele ya wengine wakati wote.
- Kutompatia jukumu lolote mwanao, hata kama ni dogo kiasi gani. humfundisha kutegemea wengine na kutothubutu.

KAZI YA 49: UJASIRI NA IMANI

Jadiliana na wanao kisa cha Makurayshi walipojaribu kumzuia Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) alisema:

> Mjomba wangu mpendwa, kwa Jina la Allah, kama Makurayshi wataweka jua katika mkono wangu wa kulia na mwezi katika mkono wangu wa kushoto, ili niache kutoa ujumbe wa Allah katika nuru na uongofu, sitaweza kuliacha mpaka litoke, au nitakufa nikiwa ninalilinda.

- Ni sifa gani za ujasiri unazoweza kuzibaini katika kisa cha Mtume (s.a.w) alipokuwa akimueleza mjomba wake Abu Twalib kwamba hawezi kuanza kutoa ujumbe kwa Makurayshi?
- Simulia visa vingine vya kijasiri kutoka katika maisha ya Mitume.
- Simulia visa vingine vya kijasiri kutoka kwa Maswahaba wa Mtume (s.a.w).
- Simulia hali ilivyo sasa kuhusu ujasiri kwa kutaja mashujaa mbalimbali kutoka katika imani duniani kote.

Elezea tukio ambalo ulionesha ujasiri. Jambo gani lilikuwa gumu katika tukio hilo? Lilitimiza lengo gani? Je ni namna gani watu waliitikia ujasiri uliouonesha?

Waeleze watoto wasimulie visa vyao wenyewe.

KAZI YA 50: UJASIRI: MTIHANI KWA VIJANA

Je, Wewe ni Mtu Mwenye Ujasiri? Toa mifano kadhaa.

KWELI ✓	SIKWELI ✘	
☐	☐	Ninasimamia kilicho cha haki, hata nikiwa peke yangu.
☐	☐	Sifuati maamuzi mabaya ya msukumo wa kikundi.
☐	☐	Hofu ya kushindwa hainizuii kuthubutu.
☐	☐	Siogopi kujielezea mwenyewe wakati wengine hawakubali.

Nadhani mimi siyo mtu jasiri kwa kuwa:.....

KAZI YA 51: KUPUNGUZA WOGA KWA WATOTO KATIKA VITA NA MAJANGA

Jadiliana na wanao vipengele vifuatavyo na kuvifanyia kazi baadhi ya vipengele hivyo.

Watoto wengi wanaingizwa vitani na katika majanga mbalimbali siku hizi. Wazazi wanaweza kufanya yafuatayo kupunguza hofu zao dhidi ya majanga:

a) Zima habari katika televisheni. Hata hivyo, wapatie muhtasari wa matukio.

b) Fuatilia ratiba za kila siku za watoto wako (kama vile; muda wa kulala, kujifunza mpira wa miguu, muda wa chakula, na muda wa swala).

c) Lenga katika kuwalea wanao. Wabebe na kuwakumbatia, kuwa nao, na kuwapa umakini na faraja zaidi. Sisitiza mawasiliano kwa kuwasikiliza na kuzifanyia tathmini hisia zao.

d) Toa majibu au mrejesho wa kirafiki kwa matukio ya kutisha: usitishike au kuhuzunika na epuka kutekwa na habari.

e) Waruhusu wanao wapate ufahamu mzuri wa vita kwa kutumia michezo, (kama: kutengeneza hospitali kwa ajili ya kuwatibu wanajeshi na raia waliojeruhiwa vitani; kutengeneza mahali kwa ajili ya mateka wa kivita; kuamua wapi, kwa namna gani, na nini cha kuwahifadhi na nini cha kula kwa wakimbizi; kutengeneza mashirika ya msaada wa kibinadamu kwa wahanga; na kufanya maombi maalumu kwa watu walio kwenye matatizo).

f) Wasiliana kwa barua-pepe au barua na watoto kutoka katika nchi nyinginezo zilizowahi kupata majanga, na kubadilishana ujumbe na zawadi baina yao.

g) Andika barua kwa mtu fulani, (ikiwa ni pamoja na kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu): Raisi wa nchi iliyoharibiwa kwa vita, maadui, au aliyenusurika katika janga. Chora picha ya amani kwa mwanajeshi, tengeneza chakula kwa ajili ya aliyejeruhiwa, au kusanya fedha na kuzituma kwa taasisi inayokusanya fedha kwa ajili ya kuwasaidia walionusurika.



KAZI YA 52: NAMNA GANI YA KUSEMA "HAPANA" NA KUENDELEA KUWA MARAFIKI

Fanya mkakati huu wa hatua nne na wanao ili wajisikie huru kusema "Hapana." Unaweza kutafuta idadi yoyote ya matukio, yanayoendana na umri wao. Mathalani: Rafiki wa mwanao anamshauri mwanao ajaribu kuvuta sigara au kunywa pombe, au kutumia dawa za kulevya, au kufanya uzinifu.

- Kusema "Hapana: Sihitaji kufanya hilo"
- Mkakati wa kwanza wa kukataa msukumo kutoka kwa marafiki na jamaa ni kusema "Hapana, Sihitaji." Mara nyingi, hapo ndipo huwa mwisho wa tukio. Umechagua na wengine lazima waheshimu chaguo lako.
- Rudia rudia "Hapana Ahsante"
- Wakati mwingine, mtoto mwingine anaweza kuendelea na msukumo, akikushauri tena na tena kujaribu angalau mara moja. Mjibu kama ulivyomjibu mara ya kwanza tena na tena. Mwambie "Hapana, Sihitaji" mara nyingi iwezekanavyo. Kwa mazingira ambayo siyo sahihi, mwambie "Ni kinyume na dini yangu." Usijisikie mnyonge kwa kurudiarudia jibu lako na usijaribu kutetea maamuzi yako. Moja kwa moja, mtoto anayekupa msukumo atachoka kusikia majibu yako ya kurudiarudia na kukata tamaa. Kama mkakati huu bado umeshindwa, sasa eleza sababu za maamuzi yako kwa sauti ya ufasaha na ya kujiamini.
- Geuza Msukumo: "kwa nini unanilazimisha!?"
- Kama bado mtu anaendelea kukusumbua, mgeuzie msukumo. Mwambie, "Kwanini unanichokoza." Hii hugeuza msukumo, kumlazimisha mtu mwingine aeleze tabia yake. Inaonesha kwamba ni mtu mwingine, na si wewe, uliye na tatizo. Unaweza kupendekeza mbadala kwa kudumisha uhusiano mwema.
- Samehe na Uondoke: "Samahani, naondoka."
- Katika sauti ya kirafiki, mwambie, "Samahani, naondoka", kisha ondoka zako bila maelezo. Huna haja ya kutoa maelezo kwa vitendo vyako tena, au kuendelea kustahimili msukumo ambao unakufanya usiwe na utulivu.
- Wahamasishe wanao kufikiria njia za kusema "hapana" pindi marafiki au wanadarasa wenzake wanapotaka kufanya kitu fulani ambacho hakikubaliki. Watoto wanapojifunza kwamba kumbe wanaweza kusema "hapana" na bado wakaendelea kuwa marafiki, inawaondolea misukumo mingi.

(Imetolewa kutoka katika ushauri katika mtandao wa www.ehow.com)

KAZI YA 53: UJASIRI NI …

Watolee mifano na uwasimulie visa kuhusu mistari ifuatayo:

Ujasiri ni:

- Kufuata matakwa yako badala ya "kufuata wengi."
- Kukataa kushiriki katika tabia ziumizazo au zenye kuaibisha.
- Kutoa kafara mafanikio binafsi kwa faida ya wengine.
- Kusema mawazo yako hata kama wengine hawakubaliani nawe.
- Kuwajibika moja kwa moja kwa matendo na makosa yako.
- Kufuata taratibu-na kusisitiza wengine wazifuate pia.
- Kufanya unachoona ni sahihi-bila kuzingatia hatari na madhara yake.
- Kukabiliana na waovu na kushirikiana na wema.

16

SURA YA KUMI NA SITA



- KUPANDIKIZA MAPENZI

SURA YA KUMI NA SITA **410**

Kupandikiza Mapenzi **410**

Utangulizi 412
Misingi ya Kuwezesha hisia 414
Upendo: Dhana ya Akili ya Kibunifu na Qur'ani 415
Dondoo Muhimu kwa Wazazi 417
Itakuwaje Mwanao Akikwambia "Nakuchukia" 418
Mtoto Wa Kwanza 419
Kwanini Wazazi Huwapenda Watoto Wao? 420
Upendo na Kujiamini kwa Wazazi 422
Njia za Kivitendo za Kujenga Mapenzi 422
Je, Wazazi Wanapaswa Kuwafundisha Watoto Chuki! 427
Kazi za Kufanya

Ondoa uovu kwa lililo jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.

Utangulizi

Watoto huzaliwa na uwezo wa kupenda, ambao wazazi wanapaswa kuuendeleza. Ndani ya majuma sita, watoto wanaweza kuitika sauti za wazazi wao. Uwezo wa mzazi katika mapenzi kwa mtoto wake ni kigezo kikubwa katika maendeleo ya uwezo wa mtoto katika kupenda. Uwezo huu unaanza kufanya kazi mtoto anapofikisha umri wa miezi sita.

Ni jambo jema kwa wazazi kuonesha mapenzi, si tu yale ya ndani lakini pia yenye kuonekana. Kumekuwa na utamaduni wa baadhi ya Wazungu katika jamii ya Wamarekani kutojali kigezo cha upendo cha kimwili hususani baina ya baba na mtoto. Hii inaweza kuelezea kwa aina fulani kwa nini watoto wa Kimarekani huvutiwa na jinsia nyingine mapema sana, kutokanana na kukosa upendo wa kimwili wakati wa utotoni. Mtaalamu wa malezi, Dkt. Spock amekosoa ukosefu wa upendo baina ya watoto wa kiume na baba zao. Yeye mwenyewe alilelewa katika namna hiyohiyo na kwa bahati mbaya akafanya hivyo hivyo kwa watoto wake mwenyewe. Katika utamaduni wa Uislamu na tamaduni nyinginezo, kusalimiana kwa kushikana mikono, kubusiana, na kukumbatiana unasisitizwa.

Watoto hujifunza kwa mara ya kwanza namna watu wengine walivyo kutoka kwa wazazi wao. Kama wazazi wana mapenzi makubwa, hali hiyo itawafanya watoto wao kuwa na uwezo wa kuwa na mapenzi. Watoto watafahamu kwamba watu wote ni marafiki, na hivyo hawawezi kuwaogopa watu wengine. Wazazi wanapaswa kuepukana na migogoro isiyo na lazima na watoto wao hata katika umri wa mwaka mmoja. Kuwazuia watoto kugusa vitu hatari na vile vyenye sifa ya kuvunjika kama; dawa, chupa, na visu, inawapasa wazazi kuviondoa karibu na watoto. Hii itapunguza idadi ya matukio

ya kuwakemea “Hapana”, “Hapana”. Nyumbani kunapaswa kuwe na mazingira salama na rafiki kwa watoto, kimwili na kihisia. Ujenzi wa mapenzi huanzia katika unyonyeshaji. Kupakata, kutabasamu, kushika, kubusu, na kuwakuna taratibu ni muhimu kwa mtoto. Watoto wanapaswa kupewa maneno ya upendo, kuwakubali, na kuwaridhia. Kadiri watoto watakavyokuwa wakikua, watagundua ni kwa namna gani wazazi wao walivyokuwa wakiwaheshimu wengine. Je, wazazi hao walikuwa na mapenzi na bashasha au walikuwa wakatili na wenye chuki? Hii itawaathiri watoto kuhusu kuuelewa ulimwengu na pia tabia yake kwa wengine.

Watoto pia hugundua namna wanavyohusiana na wanyama wa nyumbani, wanyama wengine, mimea, na mazingira. Wazazi wanapaswa kuonesha uthamini kwa mvua, theluji, jua, mwezi, na nyota, badala ya kuvilaani pindi vitakapokuudhi. Tunapohusiana na mazingira ya asili, tunapaswa kuonesha hali ya mapenzi na kujali.

Miongoni mwa zawadi kubwa kabisa mzazi anaweza kumpatia mwanawe katika maisha yake ya raha na karaha ni mapenzi. Nguvu ya mapenzi ya mzazi ni miongoni mwa vishawishi muhimu sana.

Kuwahudumia kwa bashasha na kuwakubali watoto, ni mambo muhimu kwa afya ya maendeleo ya kihisia. Katika miaka miwili mpaka mitatu haiba ya watoto inaongozwa na wazazi na walezi. Watoto yatima walioishi bila usimamizi wa kutosha au wale ambao huwa wametelekezwa katika vituo vya kutunzia watoto, wanaweza kuwa na majeraha katika maisha yao yote. Hii imeonekama katika Jamhuri ya Muungano wa Kisovieti wa zamani. Watoto wanapopuuzwa, kiakili na kihisia wanaathirika moja kwa moja, wakati watoto ambao wanapata matunzo mazuri na mapenzi kutoka kwa wazazi wao hufanikiwa katika maisha yao.

Misingi ya Kuwezesha hisia

Wazazi hukuza nguvu za kihisia wanapowapatia watoto wao mapenzi ya dhahiri. Mpe moyo mwanao kwa kumsifu na kufurahia kazi anazofanya, michezo, na majawabu kwa maswali. Wape uhuru wa kucheza lakini kwa kuzingatia usalama wao, wasomee na kuwaonesha picha mbalimbali. Watoto hufahamu kuwa wako dhaifu, si wazoefu, na kuwa ni wategemezi, hivyo huwategemea wazazi wao kuwapa mwongozo, mapenzi, na ulinzi.

Watoto huendelea kuwatazama wazazi wao na kujifananisha nao wenyewe kupitia kwao. Hivi ndivyo wanavyopata haiba zao, tabia njema, na uwezo wa kuendana na mazingira. Wanajifunza utotoni namna ya kuwa watu wazima, wafanyakazi, wanandoa wapenzi, na wazazi kutoka kwa wazazi wao.

Wazazi huonesha mapenzi katika njia nyingi zisizohesabika: kuwa na nyuso za furaha, kuonesha mapenzi ya dhahiri kimwili, furaha katika kazi za watoto wao, kuwafariji wanapoumia au kufadhaika na usalama wanapotishwa. Ni mapenzi ya wazazi yanayojenga mapenzi kwa watoto wao. Ni kutokana na mapenzi haya kwa wazazi, watoto huendelea kujenga mahusiano bora katika maisha na marafiki, walimu, wenza na watoto wao, majirani, na jamaa wengine.

Watoto hupata uaminifu kwao wenyewe kutokana na kupendwa na kuheshimiwa na wazazi wao. Kujitambua huku kunawasaidia kuwa na faraja wao wenyewe na watu wote katika maisha yao yote. Heshima na mapenzi kutoka kwa wazazi, ndizo zinazowafanya watoto kuwa na heshima na mapenzi kwa wazazi na watu wengine.

Katika jamii yenye vurugu, watoto wanapaswa kufundishwa mapenzi katika njia iliyo imara zaidi, ili iwe mbadala wa mazingira ya vurugu. Kama wazazi hawatawafundisha watoto wao mapenzi, wanawezaje kujifunza sehemu nyingine?

Upendo: Dhana ya Akili ya Kibunifu na Qur'an

Qur'an Tukufu inaelezea moyo (*fuad*), kama makazi ya uwezo wa kuelewa, ufahamu, bashasha, na huruma. Taasisi ya Hesabu ya Moyo katika mji wa Boulder Creek, California, nchini Marekani, inaonesha kwamba moyo ni kiungo chenye nguvu sana katika kutengeneza mitazamo, kutatua matatizo, na kushughulikia mambo mbalimbali muhimu. Kuushirikisha moyo na ubongo na mapenzi ni jambo ambalo linaweza kuongeza ujuzi, kujitambua kuliko kamilika. Nafsi (*fuad*) na moyo (*qalb*) ni vituo vya kiroho na kihisia vya mwili.

Kwa kutumia moyo, watu hutaka kutafiti, kujifunza, na kuwa wabunifu. Watoto huwa na muitikio na kusikiliza vizuri zaidi wakiwa "moyoni". Wakiwa "nje ya moyo", kuchanganyikiwa, hasira, kuchoshwa, kujihurumia, au hofu huweza kuchukua nafasi, na tatizo huonekana kuwa kubwa. Watoto waliojifunza kupenda hubaki kuwa timamu na wenye kujitambua, huendeleza zaidi mtazamo wa kimaisha, wanaweza kufanya maamuzi yenye busara zaidi, wanaweza kujijali na kuwajali vyema wenzao, na hurithisha uelewa wa namna ya kupenda kwa watoto wao.

(Bradly na wenzake. 2009) Katika kitabu chao, *Emotional Intelligence* (Akili ya Kihisia), Goleman anaonesha kwamba mafunzo ya kihisia anayojifunza mtoto humjengea utimamu wa ubongo wake. Watu wanaofanikiwa katika maisha mara nyingi ni wale wenye akili iliyo sawa sawa, lakini pia huwa na akili nyingi za kihisia.

Akili ya kihisia inajumuisha kudhibiti shauku, tabia katika nidhamu binafsi, uungwana, na upendo. (Goleman, 2005).

Dhana kwamba uwezo wa kiakili wa watoto haufungamani na uwezo wa kutoa na kupokea upendo si sahihi. Fahamu ,tabia za kiakili na kihisia, nyakati za vitendo, na uwezo wa kufanya maamuzi zinahusiana moja kwa moja na afya ya mioyo yetu. Mahali pa juu kabisa kifikra katika ubongo panafanya kazi ikiwa mitetemo inayozalishwa katika moyo inapokuwa sawa sawa. Mapenzi, kujali, kuthamini, na ukarimu huunda mitetemo yenye utulivu na yenye kuwa sawa sawa. Kwa kuweka sawa kichwa na moyo, watu hujenga busara, nguvu na utu katika kuchagua na kuwasiliana. Kupitia mapenzi, umakini unaendelea, mawasiliano yanaboreshwa sawasawa, na uelewa unaendelea. Mapenzi, bashasha na kuthamini huongeza ubunifu, huboresha usuluhishaji wa matatizo, na kuboresha uwezo wa kufanya uchaguzi sahihi.

Wanafunzi wanapokosa mapenzi, na kuwa daima ni waoga, hupata mfadhaiko na hivyo kudhoofisha uwezo wao wa

kukabiliana na mazingira hupotea. Kadiri wanavyokumbwa na mfadhaiko, mpangilio wa mishipa ya fahamu katika ubongo hufanywa kuwa na muundo wa kukabiliana na mfadhaiko: hivyo, watoto wanaokosa mapenzi wanakuwa na wakati mgumu wa kujifunza. Katika mazingira ya malezi mazuri na huduma kwa watoto, watoto hupenda kujifunza.

Moyo huitikia katika upendo na hii inaweza kupimwa kwa kipimo cha ECG (eletrocadiogram) na katika HRV(Heart Rate Variability) - kipimo cha tofauti ya mapigo ya moyo. Hisia za hasira, woga, hofu na mfadhaiko husababisha mapigo ya moyo kutokuwa sawa na kuvurugika. Ili kuhimili hisia chanya na za matumaini kuhusu wakati ujao, watoto wanahitaji mapenzi.

MOYO KATIKA QUR'AN

Qur'an Tukufu inaelezea moyo wa mwanadamu katika namna nyingi; zote hizi zikiwa na dalili kwamba moyo ni zaidi ya mashine ya kusukuma damu. Maelezo muhimu zaidi ya moyo katika Qur'an ni kwamba ni kitovu cha:

A. MAMBO MEMA	Iman: *imani* Taqwa: utukufu, *kujitoa* Yahdi: *ulezi* Ya'qilun: *utambuzi* Lin: *ulaini*	*Takhsha*: Ufahamu wa Mungu *Khayr*: Wema *Yarbit*: Nguvu *Mutma'in*: kujitosheleza	*Yutahhir* : usafi *Munib*: kutubu *Yafqahun*: uelewa *Sakinah*: amani *Rahmah*:Huruma
B. MAMBO MAOVU	Marad: *maradhi* Athimun: *dhambi* Nifaq: *unafiki* *Ru'b: vitisho, hofu* *Qasiyah:Ukatili* *Yazigh:Kukengeuka*	*Munkirah*: kukataa *Ta'ma*: Upofu *Ghill*: uchungu/ chuki *Tartab*: mashaka	*Ghamrah*: ujinga *Kal Hijarah*: Kususuwaa *Lahiyah*: shughulisha

Kuna maeneo 145 katika Qur'an Tukufu yanayoutaja moyo. Utafiti zaidi unahitajika kupanua uelewa wetu kuhusu moyo.



Dkt. Ilham Altaib (ADAMS Center seminar, 2008) anaelezea ile misemo ya "Nakupenda kwa moyo wangu wote" au "Nakupenda kutoka katika sakafu ya moyo wangu" kwamba ni sahihi kabisa, kwa kuwa moyo ndio kitovu cha hisia na mapenzi kwa mwanadamu.

WATOTO HUWA WASIKIVU NA WENYE MUITIKIO WA HARAKA MNO WAKIWA *"MOYONI."*

Dondoo Muhimu kwa Wazazi

Watoto wamezaliwa ili wapende. Ni juu ya wazazi kuchunga thamani hiyo na kuiweka sawa. Kama wazazi wataonesha mapenzi kwa watoto wao, itawahamasisha wao kuonesha mapenzi. Zifuatazo ni hatua za kivitendo za kuwasaidia watoto kupata haiba ya mapenzi.

❒ ANZA WAKIWA BADO WADOGO

Waingize mapenzi. Kuwabeba watoto wadogo wakati wa kuwanyonyesha kunafundisha mapenzi. Kuwabeba, kuwakumbatia, kuwabusu, na kuongea nao kunawafundisha usalama na mapenzi.

❒ KUWAFUNDISHA WATOTO "WATENDEE WENGINE KAMA UNAVYOPENDA WAO WAKUTENDEE WEWE"

Wafundishe watoto wako namna ya kuishi na watu wengine bila choyo na ubinafsi.

Kwa kuzingatia namna gani wangependa wahudumiwe, watoto huweza kufikiri kabla ya kutenda. Wanagundua kwamba wanavyowatendea wengine ndivyo watakavyotendewa baadaye. Kanuni ni kujibu kwa "namna nzuri" ambayo itatengeneza urafiki badala ya uadui.

> *Na mnapo amkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuhisabu kila kitu.*
> (Qur'an 4:86).

❒ MAPENZI HUTENGENEZWA KWA MIFANO

Kilicho cha muhimu kwa watoto ni kwa namna gani wazazi wao huonesha mapenzi, kwa kila mmoja wao, na kwa wanafamilia wote.

❒ THAMINI HAIBA YA KILA MMOJA WAO

Kila mtoto ana haiba yake tofauti na mwingine. Si jukumu la wazazi kubadilisha haiba za watoto wao, lakini badala yake wawasaidie kuonesha mapenzi katika njia sahihi. Wazazi wanapaswa kuwafundisha mapenzi ya subira kwa wale wasio na subira, mapenzi ya kijasiri kwa watoto wenye aibu, na mapenzi ya kiungwana kwa watoto walio wabinafsi.

Itakuwaje Mwanao Akikwambia "Nakuchukia"

Baada ya mapenzi yote uliyowapatia watoto wako, pamoja na kuwakumbatia na kuwabusu, kuwapatia zawadi, kwenda pamoja kwa daktari, na mambo mengine ya kuwaliwaza uliyowapatia, watoto hao wazuri wenye mapenzi wanaweza kusema: "Nakuchukia" Je, ni kweli wanawachukia wazazi wao? Bila shaka sivyo! Wanachukia ukweli kwamba wazazi wao hawatawaruhusu kula peremende kama kifungua kinywa au kwenda katika sherehe. Wanazungumza hivyo tu kwa sababu ya hasira za mfadhaiko na chuki. Watoto hujifunza mapema na ndio sababu ya wao kuwa wachokozi sana wasemapo "Nakuchukia", kwa sababu mrejesho wa wazazi wao huvuta umakini ingawa si mzuri. Pia, wazazi hukasirishwa sana, huchukizwa sana, huumizwa sana kiasi kwamba mwishowe hulazimika kutimiza matakwa ya watoto, ikiwa tu wakisema kwamba hawakuwa wakimaanisha walichokisema. Watoto hujaribu kusukuma mipaka na kuvuta umakini wa wazazi wao. Ni muhimu wazazi kujizuia kukasirika. Ingawa wanaweza kuchukiwa kwa muda mfupi au mara mbili, watoto hukusudia kupata mrejesho wa haraka wa matakwa yao. Watajifunza kwamba,

kumbe kusema "Nakuchukia" hakutaweza tena kuwashawishi wazazi kupata wanachokihitaji kutoka kwa wazazi wao hapo baadaye. Wazazi wanapaswa, kutambua hisia za watoto wao nyuma ya maneno hayo badala yake. Wanaweza kuwaeleza watoto wao "Unaonekana kama umechanganyikiwa kidogo", wakati wakikwepa kusema neno linaloweza kuwaumiza watoto. Inapendeza wazazi wakijitahidi kujiondoa katika mazingira hayo, kwenda sebuleni, kukaa katika viti, na kupumua kidogo. Muite mwenzi wako akupatie matumaini na utulivu. Jiandae kwa mjadala zaidi pamoja na watoto baadaye wakati kukiwa na muda tulivu kabisa, waeleze watoto: "Tutalizungumzia hili baadaye tutakapokuwa hatuna hasira."

Mtoto Wa Kwanza

Wazazi wenye matarajio makubwa hutaka watoto wao kuwa na matarajio makubwa pia. Wazazi wote waliofanikiwa, hupenda mtoto wao wa kwanza kufanikiwa kama wao walivyofanikiwa. Katika vitu vyote walivyovifanyia juhudi na vile ambavyo hawakuweza kufanikiwa, wazazi huamini kwamba mtoto wao wa kwanza atakuwa mwenye mafanikio zaidi. Makosa yoyote waliyoyafanya na kusababisha kuwa na mashaka yanaweza kufanywa na mtoto wao wa kwanza. Kwa kuwatofautisha, wazazi hawa wenye matarajio makubwa kwa mwana wao wa kwanza, ni dhahiri kwamba hawawezi kuwa na mtazamo huo huo kwa mtoto wao wa pili. Hivyo mtoto wa pili atakuwa huru kidogo kutokana na matarajio ya wazazi wake kwake.

Ni rahisi kuwaeleza wazazi wapya "Tulieni na mtoto wenu wa kwanza. Muacheni ajitegemee." Hiyo ni kama kuwaeleza wanafunzi wakati wakiendesha farasi au gari kwa mara ya kwanza. Inasaidia kuwapeleka watoto wa kwanza kwenda kucheza na wenzao. Michezo ni fursa kubwa sana kujifunza namna ya kuishi na wengine, pamoja na kutoa na kuchukua. Kuwatembelea watu wengine na kuwakaribisha watoto wengine kuzuru nyumbani kuna faida kubwa. Kuwa na wakati mzuri pamoja ndio msingi wa kuhuisha mapenzi.

Wanasosholojia wengine hushauri wazazi wapate watoto kwa kufuatana, yaani wasiachane sana. Hii inawasaidia watoto kuwa na maisha ya kijamii baina yao, kuliko kulelewa peke yao na kukua wakiwa pekee yao. Ni rahisi kwa wazazi wengi kulea kizazi kizima kwa wakati mmoja, na kisha kwenda hatua nyingine katika maisha yao. Ikiwa kipindi kati ya mtoto mmoja na mwingine kitakuwa kirefu, wanaweza kuishia kuwa na watoto, vijana na watu wazima, hivyo kufanya wazazi kulea vizazi vya aina tatu kwa wakati mmoja, kitendo ambacho, kimsingi ni jukumu zito kwa wazazi, ambao watatumia muda mwingi wa maisha yao katika malezi kwa watoto. Watakuwa na muda mdogo sana kwa ajili yao wenyewe wakati wa kustaafu.

Husuda ni kupambana na mapenzi, kwa sababu ni kitendo cha kutaka neema walizonazo watu wengine ziwatoke kisha zije kwako. Ni tatizo kubwa, ambalo wazazi wanapaswa kuliondoa katika umri mdogo wa maisha ya watoto wao. Mtume (s.a.w[1]) ameliona tatizo hilo kama uovu wa kijamii. Mtume (s.a.w) amesema:

> Watu wataendelea kuwa vema kama tu hawatafanyiana husuda.(Al-Tarabani).

Mara nyingi mtoto mpya katika familia huwavutia wazazi wote. Watu huja kuwatembelea na kuwaletea zawadi, na kila mmoja humsifia namna mtoto alivyo mzuri. Mama anaweza kuwa amechoka sana, na baba akawa na mishughuliko mingi, katika kuwahudumia watoto wengine. Kaka wakubwa na dada wakubwa wanaweza kujisikia kama wametelekezwa, hususani wale wadogo sana, ambao wanaweza kuchukizwa au kuchanganyikiwa, kwa sababu wao si wadogo tena. Ni hali ya asili kuona husuda wakati mtoto mdogo akipendelewa sana. Wazazi wanaweza kufanya yafuatayo kuzuia au kupunguza husuda:

- Wafanye watoto wote wajisikie kwamba wanapendwa na kuthaminiwa.
- Mtoto mwingine akiwasili, hakikisha mwingine hahisi kama hapendwi na kuthaminiwa sana. Ni muhimu kuendelea kuwapatia umakini wa kutosha ili kuwafanya wote waonekane ni wa muhimu.
- Epuka kuwashindanisha au kuwalinganisha baina ya wavulana na wasichana.
- Uvumilivu, zawadi, na maadili lazima yafanywe kwa usawa.
- Watoto wote wana haki ya kubusiwa na kukumbatiwa mara kwa mara, kadiri itakavyokuwa ikiwezekana.
- Wazazi wanaweza kuwapatia watoto wakubwa hisia za kugawana majukumu katika kumhudumia mtoto mdogo, na pia washirikishwe katika maamuzi.

Kwanini Wazazi Huwapenda Watoto Wao?

Kwa mujibu wa Euripides, hapa wanadamu wote ni sawa: matajiri na masikini wanafanana. Watawapenda watoto wao." Rabindranath Tagore yeye akasema "Simpendi kwa sababu ni mzuri, lakini kwa kuwa ni mtoto mdogo."

Ni jambo la kuhuzunisha kwamba watoto wengi hawapendwi kwa sababu:

- Wao ni matokeo ya "ajali", msukumo wa kijamii au ubakaji.
- Wanaonekana kama sababu ya kifo cha mke wakati wa kujifungua.
- Ni mtoto wa mtu aliyekuwa muhalifu.
- Mtoto ni wa kike katika jamii ambayo thamani huwekwa kwa watoto wa kiume.

(Katika nchi nyingine, wazazi hupongezwa ikiwa tu mtoto atakuwa mvulana).

Kwanini watoto wanyanyaswe kwa makosa yasiyowahusu?

Usifananishe mapenzi na utiifu. Bila mazingira yoyote, inaweza kuchukuliwa kwamba wazazi wanaweka masharti katika mapenzi yao. Wazazi hawapaswi kusema: "Nitakupenda zaidi ikiwa tabia yako itabadilika."

Watoto wanahitaji mapenzi, hususani pale wanapoona kama hawayapati sawasawa. Wazazi wanapaswa kuwashawishi watoto wao kwamba mapenzi kwao hayatokani na utendaji kazi wao na kwamba mapenzi yako huru. Wanawapenda kama walivyo. Mafanikio ya wazazi hupimwa kwa kiwango cha watoto kujisikia salama, kuhitajika, na juu ya yote, kupendwa. Japokuwa kusifiwa na kupewa zawadi kunapendwa na watoto, watoto wanapenda upendo kuliko kitu chochote. Mark Twain alisema: "Sifa ni nzuri, zawadi ni nzuri, lakini bashasha, Mapenzi ndio mwisho wa yote na ni zawadi yenye thamani zaidi ambayo mwanadamu yeyote anaweza kushinda."

Wapende Watendaji Lakini Chukia Matendo Maovu!

Uhusiano wa kimapenzi kati ya watoto na wazazi unapaswa kutokuwa na masharti. Wanapaswa kuthaminiana bila masharti. Watoto wanapaswa kuthaminiwa kama walivyo, pamoja na hofu zao, tamaa zao, na ujinga wao. Bila masharti kuna maanisha bila kuwa na upendeleo au hukumu. Watoto wako wanaweza kuwa au wasiweze kuwa ni wenye kuvutia sana, wasomi sana, au watoto maarufu. Hata hivyo, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, wameweza kuletwa ulimwenguni, ni hii ni sawasawa na kutowapa mapenzi bila masharti.

HAITOSHI KUWAPENDA WATOTO KIMYAKIMYA: YAFANYE MAPENZI YAKO KUWA NA SAUTI KWAO

Mtume (s.a.w) aliwafundisha Maswahaba zake kutamka mapenzi yao baina yao.

Siku moja wakati Mtume (s.a.w) ameketi na Maswahaba zake, mtu mmoja akapita mbele yao. Miongoni mwao akasema, "Nampenda huyu bwana". Mtume (s.a.w) akamuuliza, "Je Umemueleza?" Yule Swahaba akamjibu Mtume (s.a.w), "Hapana" Mtume (s.a.w) akasema, "Nenda kamueleze." Yule Swahaba aliamka na kumuwahi yule mtu aliyekuwa akipita, kumshika na kumueleza, "Nakupenda kwa ajili ya Allah" Yule mtu mwingine akamjibu "Namuomba Allah akupende kama ulivyonipenda mimi kwa ajili yake."
(Abu Dawud).

Upendo na Kujiamini kwa Wazazi

Kujiamini kwa wazazi ni jambo la msingi katika mahusiano ya kimapenzi kati ya wazazi na watoto wao. Kama wazazi watashindwa kuwashawishi watoto wao kwamba wanajua waliposimamia, na wapi wanapotaka watoto wao wasimame, watoto wao watawapa majaribu mbalimbali. Majaribu haya yenye kudumu yanayotikisa wazazi huweza kukuza kiwango cha mfadhaiko katika mahusiano yao. Mfadhaiko huumiza mapenzi. Upunguzaji wa mfadhaiko unaachia mtiririko wa mapenzi katika mahusiano. Bila uwepo wa mapenzi, mamlaka huwa ya kidikteta au ya kutokuwa na mahusiano. Wazazi wanaojiamini huonesha vyote, mamlaka na mapenzi. Mapenzi yenye mamlaka na mamlaka yenye mapenzi vile vile, hulindana vyenyewe katika usawa. Katika kufanya hivyo, wanawasilisha ulinzi wa kiwango kikubwa kwa watoto wao na watoto wenye ulinzi huwa na utulivu na furaha. Hawatakuwa na sababu tena za kuwasumbua wazazi wao, pamoja na kuonesha changamoto chache sana za kimaadili. Pindi watoto wakikosea, ukumbusho mdogo tu wa nani anayepaswa kuhusika hujitokeza.

Njia za Kivitendo za Kujenga Mapenzi

Wazazi wanawapenda watoto wao, ambayo ni msingi wa uhusiano wa kimapenzi baina yao. Wazazi ambao hawazungumzi kuhusu mapenzi yao mara kwa mara hushitushwa wanapogundua kwamba watoto wao hawaoni kama wanapendwa.

Upendo unaweza kujengwa na kuendelezwa kwa matendo. Inajumuisha nia na matendo. Nia ni kuwa na hamu ya kufungua moyo wa mtu kwa ajili ya wengine, na kuonesha kwamba wanawajali. Kitendo ni kufanya kitu fulani kuhusiana na nia ya mtu. Mathalani: wazazi wanaweza kuchangia fedha kidogo au muda wao kidogo au vyote kwa kikundi kwamba wanapenda au kutabasamu na kusalimu kutoka ndani ya moyo kwa watu wanaokutana nao mtaani. Haijalishi namna gani wazazi wanatenda, angalau tu kwamba wanafanya kitu. Mama Teresa alielezea kwamba: “Hatuwezi kufanya mambo makubwa hapa duniani. Tunaweza tu kufanya mambo madogo kwa mapenzi makubwa.”

Zifuatazo ni miongoni mwa njia wanazoweza kutumia wazazi kujenga na kuendeleza mapenzi kwa watoto wao:

- Kulenga katika vitu vikubwa na kuacha vitu vidogo.
- Upendo huendeleza shukrani. Unapotoa mrejesho kwa zawadi kubwa katika maisha
- kama vile zawadi kama unaweza kusoma kitabu hiki unaweza kujenga mapenzi.
- Kuwa na mapenzi ya pamoja na watoto kwa kuwa kupenda ni kuwa pamoja na kujali. Kuleni chakula pamoja; tumieni fedha, kalamu, karatasi, compyuta, magari, viti, na vitabu pamoja; na kufanya safari na kubadilishana mawazo pamoja na watoto.
- Waeleze wanafamilia kwamba unawapenda, hususani, kabla hujaondoka kama unasafiri.
- Tunga wimbo maalumu na watoto wako unaosema “Nakupenda”.

MAPENZI NI KUFANYA MAMBO PAMOJA

Mtoto anapaswa kuwa na mapenzi katika moyo wake kwa wengine, anapaswa kuwapendelea wengine anachokipenda yeye. Mtume (SAW) anasema:

Hutakuwa muumini mpaka umpendelee ndugu yako unachokipenda wewe. (Al- Bukhari).

Mapenzi ni …

Kushirikiana … matumaini yetu mema, hofu zetu nzito, vicheko vyetu vikubwa, machozi yetu laini, njozi zetu tamu, matatizo yetu machungu, udhaifu wetu mkubwa, mapenzi yetu yanayokua, kuwa mara zote macho, kadiri tunavyozidisha ushirikiano, tunazidisha kuthaminiana.

Njia nzuri ya kusahau matatizo yetu ni kuwasaidia wengine kutatua matatizo yao. Unaweza kusahau ulicheka na nani, lakini huwezi kusahau ulilia na nani.

Kisa kutoka katika kitabu cha John Gray: *Mars and Venus*

Ndugu yangu ambaye afya yake ilikuwa ya mgogoro alinieleza kwamba alikuwa hazungumzi na kijana wake kwa muda wa miaka mitatu kwa kuwa walitofautiana naye katika suala la mkewe na kwamba aliamua asingethubutu kuzungumza naye mpaka kijana wake yeye huyo atakapoanzisha mazungumzo. Nilimshauri yeye ndiye awe wa mwanzo kumzungumzisha akasisitiza kwamba hawezi kufanya hivyo na kwamba kijana wake huyo anapaswa kuomba radhi kwanza. Alikuwa tayari kufa bila kuzungumza na mwanawe huyo. Baada ya mazungumzo ya upole ya kumpa moyo, alikubali kuwa wa mwanzo kuanza mawasiliano. Cha kumshangaza ni kwamba, mwanawe alijisikia furaha sana kwa kupigiwa simu na mama yake, na kumuomba radhi yeye mwenyewe. Mtu akichukua fursa na kujirudi, kila mmoja anakuwa mshindi.

Chuki ni kama asidi/tindikali. Inaweza kuharibu mishipa inamowekwa pamoja na kuharibu chombo ilimohifadhiwa.

Ni muhimu kujifunza upendo. Ingawa kutoa vitu halisi ni vizuri si sawa na upendo halisi.

Je ni kiasi gani cha mapenzi kinatosha? Wazazi huweza kuwekeza akiba ya kutosha katika hifadhi ya mapenzi kwa kuonesha mapenzi kwa watoto wao. Hakuna anayejali kupokea akiba ya kuzidi.

Kadiri wazazi wanavyotoa mapenzi, ndivyo watakavyopokea mapenzi kutoka kwa watoto wao. Kuwa mtu wa kupenda ni sifa ambayo inaweza kumiliki, lakini kupokea mapenzi ni nje ya miliki ya mtu yaani huwezi kuidhibiti. Wazazi hawawezi kutegemea mrejesho wa mapenzi kutoka kwa watoto wao, kwa kuwa mapenzi ni zawadi tosha. Watoto hawawezi kuelewa ni kwa namna gani wazazi wanawapenda mpaka wao waje kuwa wazazi.

Wazazi wanapaswa kuwa wa kwanza kusuluhisha wanapotofautiana na watoto wao. Watu wengi sana hughadhibika kwa mambo madogo tu, na kuhitaji mtu mwingine atumike kufanya suluhu, wakidhani hii ni njia pekee ambayo kosa linaweza kusamehewa au urafiki au udugu unaweza kurudishwa.

Watu wakighadhibika, wanakuwa wadhaifu katika mambo ambayo ni mepesi kwao na akili zao. Hufikiri kwamba nafasi zao ni muhimu sana kuliko furaha. Watu wenye amani hufahamu kwamba kuwa sawasawa hakuzidi kuwa na furaha. Watu wanapaswa kuhimili hasira zao na kusaidia amani kuwepo. Kuwawezesha watu wengine kuwa sawasawa hakumaanishi kwamba mtu anakosea. Watu hujisikia vizuri zaidi wanapopata amani ya kuondoa hasira zao, pamoja na faraja ya kuachana na hasira kama ilivyo faraja yakuwafanya wengine kuwa na furaha. Mrejesho wake ni kwamba, watu wengine wataondoa dhana ya kujihadhari nao na kuongeza mapenzi zaidi kwa mahasimu wao wa zamani.

> Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lililo jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako na yeye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.
>
> (Qur'an 41:34).

- **Kujitolea muda wako na fedha yako kwa ajili ya watoto kuna thamani kubwa sana. Upendo ni kama jumla ya mfano wa mrejesho chanya wa kamba iliyofungwa. Kadiri wazazi watavyozidisha mapenzi kwa watoto wao, ndivyo wanavyozidisha kujitoa; na kadiri wanavyojitolea, ndivyo mapenzi yanavyoongezeka.**
- **Kila asubuhi, wazazi wanaweza kujiuliza wao wenyewe: Je nimpe nani mapenzi yangu maalumu katika familia yangu leo? Wanaweza kupanua swali hili kwa kumjumuisha mtu mwingine wa nje ya familia. Kila siku mapenzi huondoa bughdha katika familia.**

Utafiti: Njia Mbalimbali za Kuwafanya Wanao Wajisikie Kupendwa

Samon (1999) aliuliza akina mama na akina baba wapatao 55 wenye watoto kuanzia umri wa mwaka 1 mpaka miaka 16 kwamba kwa namna gani waliweza kuhusiana na watoto wao. Katika kila kisa kimoja, jawabu lilikuwa kuwa na muda wa kukaa na watoto wao na kufanya kitu fulani. Hii ni pamoja na; kutazama filamu, kusoma kitu fulani, kupika kitu fulani, kuzungumzia kitu fulani, kushirikishana kitu fulani, na kuwa pamoja. Tumia muda pamoja katika shughuli za pamoja na watoto wako. Ifuatayo ni orodha ya shughuli ambazo wazazi wanaweza kuzifanya na watoto wao, ambazo zitaongeza mapenzi baina yao:

- Kutembea pamoja.
- Kuonesha maumbo katika mawingu/ kusoma anga la usiku.
- Kutazama filamu za nyumbani/ kusikiliza vipindi vya redio pamoja.
- Kuwaruhusu watane nywele zako.
- Kupigana mieleka.
- Kujaza kijitabu cha kumbukumbu kwa picha na vibandiko vingine.
- Kwenda nao sokoni, na kuwaacha waamue wanataka kununua nini kwa ajili ya chakula cha usiku.
- Cheza pamoja na watoto wako michezo ya kielektroniki. Michezo hii ni rahisi, rafiki wa mazingira kwa kuwa haihitaji umeme isipokuwa betri tu, husisimua akili, inaweza kuchezwa kwa lugha yoyote, na huvutia machoni kuliko kutazama katika skrini ya video.

- Kufanya kazi za shuleni, za kufanyia nyumbani nao, lakini isiwe kuwafanyia.
- Kusoma Qur'an, kusikiliza kaswida, muziki na nyimbo pamoja.
- Kufua na kukunja nguo pamoja.
- Kuchora pamoja.
- Kukumbatia, kubusu (lakini sio mdomoni), na kushikana mikono.
- Kwenda makumbusho pamoja.
- Kuswali pamoja.
- Kuvaa nguo za zamani pamoja.
- Kwenda nao kazini kwako.
- Kupiga sufuria na vikaangio pamoja, bila kuwabughudhi majirani.
- Kwenda na watoto wako katika matamasha, michezo, filamu, mechi, kuendesha baiskeli au farasi, riadha, katika hifadhi, na kutembelea maeneo mbalimbali kama msituni, jangwani na ufukweni.
- Kuwa nyumbani na kuwasikiliza kwa umakini, bila kupokea simu au kufungua barua pepe.
- Kuwatembelea akina babu na bibi na ndugu wengine.
- Kusafisha nyumba pamoja.
- Kupika chakula pamoja.
- Kutazama picha za familia pamoja.
- Kumenya matufaha, machungwa, mapea, na zabibu pamoja.
- Kusafisha bustani pamoja.

Je, Wazazi Wanapaswa Kuwafundishwa Watoto Chuki! Huweza Kutokea!

Pamoja na kwamba msitititizo uko katika mapenzi, chuki haipaswi kusahaulika, kwani zote ni muhimu. Kama watu wakimpenda Mwenyezi Mungu, Mitume, wazazi, ndugu, wanadamu wenzetu, wanyama, mimea, mazingira na ulimwengu, kunapaswa kuwa na chuki dhidi ya Shetani, maovu, rushwa, kuongopa, kudanganya, ubaguzi, wizi, unyanyasaji wa kijinsia, dawa za kulevya, kunywa pombe, wivu, ubaguzi wa rangi, ubinafsi, na hasira. Hata hivyo, pamoja na kwamba vitendo viovu vinapaswa kuchukiwa, wanaovitenda wanapaswa wasichukiwe. Chukia uovu, si anayefanya uovu.

> Hakika Shet'ani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni. (Qur'an 35: 6).

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 54: UTARATIBU WA MAPENZI YA KILA SIKU

Mtoto mwenye umri wa miaka 17 anasema: “Bado mimi huwa napenda mama yangu akija chumbani kwangu kabla hajaenda kulala.”

Wazazi: Jadilini utaratibu wenu wa mapenzi kwa watoto wenu. Msisahau kufanya *du'a* kila siku!

17

SURA YA KUMI NA SABA

- KUFUNDISHA UKWELI NA UAMINIFU

SURA YA KUMI NA SABA 430

Kufundisha Ukweli na Uaminifu 430

Utangulizi 432
Wazazi wanapaswa kuwaamini watoto wao lakini wajue walipo! 434
Kanuni za Msingi 435
Kufanyia Kazi Tabia na Mtazamo wa Ulimwengu Mzima 437
Kwanini Watoto Hudanganya: Namna ya Kutibu Uwongo 438
Waeleze watoto visa vyenye malengo 440
Kazi za Kufanya

Ukweli huzaa wema na wema huzaa Pepo. Mtu atasema ukweli mpaka atakaporekodiwa kama muaminifu. (Al-Bukhari na Muslim).

Utangulizi

Wazazi wengi hupata hofu wanapowaona watoto wao wanadanganya kwa mara ya kwanza. Lakini kwa watoto wengi, kudanganya ni kipindi cha mpito tu ambacho kinakuwa ni sehemu ya maendeleo ya mtoto katika kukua, sehemu moja ikisababishwa na kuogopa adhabu na pili tabia ya kujifunza kutokana na mazingira. Wakati kudanganya kukiwa si chochote cha kuhofia, juhudi lazima zifanywe kuwafundisha kuwa wakweli. Kudanganya ni mrejesho wa mtoto kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya kujitetea.

Watoto huchanganya uhalisia na vitu wavipendavyo, ndoto na matarajio. Ni muhimu kwa wazazi kutowakatisha tamaa na wavipendavyo. Ndoto za mchana na matarajio ni vitu vya msingi katika utu hata kwa watu wazima. Kuwa na uwezo wa kujifanya kwamba mtu fulani yupo mahali fulani huwa kama ukombozi na kuondoa msongo wa mawazo. Usihoji sana. Kama watoto watajihisi kwamba ni lazima watoe maelezo mbele ya wazazi, hili linaweza kuongeza kiwango cha kutokuwa mkweli kukwepa kuhojiwa.

Mapagani wa Kikurayshi walimuita Mtume (s.a.w) tangu utotoni kama “Mkweli na Mwaminifu” (al-sadiq al-amin). Kuaminika katika Kiarabu kuna maana nyingi: Uaminifu, kujiamini, kuwajibika, kujali, na kuwa mlezi.

Ukweli na uaminifu ni sehemu muhimu ya tabia ya kiongozi mwadilifu. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao, kutenda, na kuishi katika “ukweli na uaminifu” mpaka tabia hiyo imee kwa watoto. Watoto huwa waaminifu wakiwaona watoto wengine wakiwaamini wazazi wao na kuhisi kwamba fedha zao, mali zao, na siri zao zitakuwa salama. Wazazi waaminifu, mara nyingi

huchaguliwa kuwa viongozi katika jamii zao. Ukweli ni kwamba, moja kati ya sifa bora za Muislamu zilizofundishwa na Mtume (SAW) ni uaminifu.

> Muislamu ni yule ambaye watu watajisikia kuwa salama kutokana na ulimi wake (mazungumzo) na mikono yake (vitendo) na waumini waliobarikiwa (wahamaji) ni ambaye huepukana na makatazo ya Mwenyezi Mungu. (Al-Bukhari).

Uaminifu baina ya wazazi na watoto ni kitu cha muhimu sana. Hakikisha uaminifu unapatikana, kudumishwa, na kuendelezwa. Hata kama kuwaamini baadhi ya watoto ni changamoto, wazazi wanapaswa kufanya kama wanawaamini. Kama watoto hawasemi ukweli, wazazi wanapaswa kuwa makini na si kuwalaumu. Kukiwa na misuguano, watoto wanaweza kuwauliza wazazi wao: "Hamniamini?"

Wazazi wanaweza kujifanya kwamba wanamuamini mpaka watakapopata njia nzuri na yenye mafanikio ya kudhibiti tabia hiyo ya kutokuwa mkweli. Watoto wanapaswa kufundishwa kwamba kutokana na kuwajibika uaminifu hujengeka. Ili watoto waweze kujenga uaminifu kwa wazazi wao, wanapaswa kujifunza ni kwa namna gani wengine wamefanikiwa kuaminika kwa wazazi wao na tabia gani zinaondoa uaminifu.

Kupata uaminifu ni mchakato endelevu. Pamoja na kwamba watoto wanaweza kupata mafanikio katika mahusiano na wazazi wao, wakati mwingine mambo huenda kombo. Hili huwafanya wazazi washindwe kuwaamini watoto wao tena. Hata hivyo, ni muhimu wakabakia kujiamini! Wanapaswa kuwa wavumilivu.

Wazazi wanapaswa kuwaamini watoto wao lakini wajue walipo!

Wazazi wanaweza kuwaamini watoto wao wanapotoka nje, wakati huo huo, wanapaswa kujua walipo watoto wao. Wazazi wanapaswa kujua walipo watoto wao pamoja na watu waliokuwa nao. Hii inaweza kufanywa bila kuondoa uaminifu na kuwafuatilia sana. Wazazi wanapaswa kuacha kutoamini kirahisi kwamba wanapowaacha watoto wao shuleni asubuhi, watabakia shuleni wakati wote. Watoto wengine hutoka shuleni bila walimu na wazazi wao kuwa na habari. Wazazi wanapaswa kuwatazama watoto wao mara kwa mara, kupitia shuleni, rafiki zao, na majirani, moja kwa moja au vinginevyo. Watoto wengi wameingia katika matatizo kwa kutoka mapema shuleni na kujiingiza katika vitendo viovu. Ni vema kukagua vyumba vyao na nguo zao mara kwa mara ili kuwa na uhakika kwamba hawajihusishi na dawa za kulevya, wizi wa fedha na vitu vingine vya thamani. Waeleze watoto wako unachokifanya na kwanini unafanya hivyo.

> Wachukulie watu kama unavyodhani wanavyotakiwa kuwa kwa kuwa kufanya hivyo kutawasaidia kuwa wanavyotakiwa wawe.
>
> (Johann Wolfgang Von Goethe).

> Waamini watu, na watakuwa halisi kwako; wafanye waonekane wazuri, na wao wataonesha uzuri wao. (Ralph Waldo Emerson).
>
> (Exley, 1997).

Kanuni za Msingi

Zifuatazo ni dondoo muhimu za kuzingatia unaposhughulika na watoto:

MAADILI YA KIFAMILIA

Watoto wanapaswa kuelewa kwamba kudanganya si katika maadili mazuri na hakukubaliki kijamii. Waoneshe kwamba kudanganya kutakuwa na madhara makubwa sana. Wafundishe ukweli na uadilifu kwa maneno na vitendo. Wazazi wanapaswa kujadili pamoja na watoto wao imani yao juu ya ukweli. Toa mifano kwa kushirikiana kuhusiana na kutokuwa na uaminifu unaoendana na umri wao. Hakikisha sera ya ukweli inakuwepo katika orodha ya maadili ya kifamilia. Wapatie watoto maana ya uaminifu na waamini kwamba wanaweza kukuelewa na kutekeleza.

KUPIGIWA MFANO

Wafundishe watoto wako ukweli. Usiwadanganye kuhusu ulipo, usiibe katika ghala au kwa muajiri na usifanye udanganyifu katika kodi na mwenzi wako.

Wazazi wanapaswa wajiulize wenyewe, "Ujumbe gani tunaowapa watoto?" Ni muhimu kukwepa kutokuwa muaminifu, hususani mbele ya watoto. Wazazi hawapaswi kuwadanganya watoto wao. "Tiketi ya mtoto tafadhali, ana umri wa miaka 11 tu." Wazazi hawapaswi kuwaagiza wadanganye kwa sababu yao. "Mwambie bibi yako, niko bafuni." Wazazi wanapaswa kufanya kila juhudi kujali kila wanachofanya, kwa wakati, kutenda wanachokisema, na kuahidi mambo yanayowezekana kutekelezeka tu, hususani, yanapowagusa watoto. Kama mazingira yatabadilika mbali na uwezo wa wazazi, wazazi wanapaswa kutoa maelezo, na kuepuka kutoa sababu zisizokuwa na mashiko au kuwalaumu wengine. Usiwadanganye watoto kwa maneno ya mzaha, kama mwanasiasa asemaye: "Niliahidi, lakini sikuahidi kuitimiza ahadi."

WAFUNDISHE TOFAUTI KATI YA UONGO MDOGO, UONGO WA HATARI NA AINA NYINGINE YA UONGO

Ni muhimu kuwaelezea watoto tofauti iliyoko baina ya uongo wenye hatari kubwa na ule wa kiupole. Ingawa watu hukataa kwamba husema uongo, kila mmoja hufanya hivyo. Kuna mantiki gani kusema kwamba majirani ni wabaya? Au kumueleza mtumishi wa posta, anapouliza mmoja anachofanya, kwamba anafanya vibaya na kwamba anahitaji msaada wa kisaikolojia? Wakati mwingine, tunadanganya bila heshima kabisa. Wafundishe watoto kutofautisha baina ya uongo, kuongeza chumvi, kuhadithia, na sitiari.

WAFUNDISHE WATOTO TOFAUTI KATI YA VITU WAVIPENDAVYO NA UHALISIA

Bainisha utofauti kati ya kitu kilichokuwa halisi na kile kisichokuwa halisi. Jadili ndoto pamoja na watoto baada ya kuamka. Jadili kilichomo katika filamu na kilichokuwa katika maisha halisi. Jadili visa ni nini na matukio halisi ni nini.

UKWELI WA ZAWADI

Kama watoto wako katika wakati mgumu waeleze ukweli, ni vema kuwapongeza wakati wote watakapoonesha uaminifu. Watoto wanapenda kuona wazazi wao wanawajali. Hivyo, ukweli unapaswa kupongezwa na kuhamasishwa hata kama kufanya hivyo kunaweza kusababisha matatizo. Wazazi wanapaswa kuwasifia watoto wao kwa juhudi wanazofanya za kuwa wakweli na kuwaonesha mifano mizuri, kadiri itakavyowezekana wakati wa kuelezea kutoridhishwa na kutokuwa wakweli.

OMBA KABLA YA KUCHUKUA

Wazazi wanaweza kufanya kuwa sheria nyumbani kwamba kila mmoja anapaswa kuomba kabla ya kuchukua kitu chochote kisichokuwa chake. Hii huwafundisha watoto kuheshimu vitu vya wenzao. Pia itawafundisha kwamba kumuibia mtu yeyote ni kosa.

SULUHISHA MATATIZO KABLA YA KUWA NA MATATIZO

Starehe ya haraka imekuwa tatizo kubwa, kiasi kwamba, watu wengi wanashindwa kuweka akiba, wanakuwa na uzito uliopita kiasi, na hawawezi kusema “hapana” kwa manunuzi yasiyokuwa ya lazima. Hususani, huwa ni vigumu kwa mtoto kuahirisha matakwa yake na kuacha mabaya yake. Wafundishe watoto kukubali makosa na kuahirisha starehe.

Watoto hawapaswi kuiba kabla ya kujifunza madhara ya kufanya hivyo. Jadili tabia zisizokubalika na watoto kabla hawayajayatenda.

WATOTO WAKUBWA

Kama wazazi wana watoto wakubwa ambao wanaendelea kudanganya na pia sio wakweli, hapo msaada wa kitaalamu unahitajika. Watu wazima wengi wamedanganya sana wakiwa vijana, na mara nyingi bila kukusudia kwa ajili ya kuficha siri. Vijana huwa hawapendi kutoa siri zao kwa wazazi wao, na hii inaeleweka. Ni muda ambao wanabadilika sana kuanza kupata fikra za kiutu uzima, wakati wakiendelea kuchukuliwa kama watoto. Ni wakati ambao kuficha siri ni kawaida. Usiri lazima uheshimiwe. Hata hivyo, matarajio ya wazazi vile vile yanapaswa kutarajiwa na watoto wao, madhara ya kudanganya yanaweza kufafanuliwa sawa sawa na kukubaliana.Vijana wanapaswa kufahamu madhara ya kutokuwa waaminifu. Kama watoto wako wapo katika kundi la wenzao wanaosema uwongo, watoe katika kundi hilo na waonye kuhusu kuwa na marafiki wa namna hiyo.

Ni suala la msingi vijana kufundishwa umuhimu wa kuwa waaminifu katika mahusiano, ikiwa ni pamoja na ukweli ambao wanapaswa kuwa nao mioyoni mwao. Hivyo, watoto wasiwekwe katika mazingira ambayo uwongo na kuongeza chumvi kunaweza kutokea, kwa mfano; kamari, michezo, biashara za kimataifa, na biashara zenye msukumo mkubwa. Pia wasilaumiwe kwa kudanganya mpaka kuwa na uhakika kwamba wanahusika kwa hali iliyotokea. Mjadala kuhusu watu kutokuwa wakweli uendeshwe kwa siri, yaani kila mtoto awe na wakati wake ili wasipate woga kueleza ukweli.

Kufanyia Kazi Tabia na Mtazamo wa Ulimwengu Mzima

Enyi mlio amini! Kwa nini mnasema msiyo yatenda? Yanachukiza vikubwa mno kwa Mwenyezi Mungu kuwa mnasema msiyo yatenda. (Qur'an 61: 2-3).

Onesha maana mbalimbali za ukweli, uaminifu, na kutimiza ahadi

Ongeza maadili kama ukweli na uaminifu katika mijadala katika mada mbalimbali kama; siasa, dini, historia, sayansi, fasihi, lugha, na hisabati. Mathalani: Je uwezo wa kimahesabu wa karani wa benki kuficha wizi unaweza kujadiliwa katika maadili? Je, wanasayansi wanabanwa na maadili yao katika matokeo ya tafiti zao kwa faida ya wanadamu wote? Je, watu wote walio katika maandiko ni watu wa haiba?

Kudanganya ni tatizo kubwa, kitu ambacho hakiwezi kupuuzwa na kukatazwa kikamilifu lakini kwa busara. Kudanganya ni hatari sana kiasi kwamba Mtume (s.a.w) alisema:

Mtume (s.a.w) aliulizwa, "Je, inawezekana kwa muumini kudanganya?" Alijibu, "Muumini hawezi kudanganya kamwe." (Kanz Al-Ummal).

Uzuri zaidi ni kwamba ukweli wote usemwao duniani hivi sasa hufanywa na watoto. (Oliver Wendel Holmes kukatazwa Brown, 1994). Mtoto wa miaka tisa alisema: Ni vigumu kudanganya unapomtazama machoni mama yako).

Ingawa watoto wengi huzaliwa wakiwa wakweli, mara nyingi, hujifunza kudanganya kadiri wanavyokua, kwa kufahamu au kutofahamu, kutoka kwa wazazi, ndugu na watu wengine. Ukweli ni tabia ya kujifunza, si sifa ya kurithi. Kadiri muda unavyoenda watoto hujifunza kudanganya na kuwa tabia yao. Vijana hulazimika kudanganya, kujilinda kutokana na makosa, kuficha siri zao, na kukwepa mazingira ya kubughudhiwa. Kadiri mtoto anavyoendelea kuongopa, ndivyo hivyo tabia ya uongo inavyozidi kushamiri. Kuongopa huzaa kuongopa, kama ilivyo kwa ukweli kwamba huzaa ukweli kama ilivyoelezwa na Mtume (s.a.w) aliposema:

> Ukweli huzaa wema na wema huzaa Pepo. Mtu atasema ukweli mpaka atakaporekodiwa kama muaminifu. Kuongopa huzaa kutokuwa na uadilifu na kutokuwa mwadilifu huzaa Moto. Mtu atasema uwongo mpaka atakaporekodiwa kama muongo. (Al-Bukhari na Muslim).

Kwanini Watoto Hudanganya: Namna ya Kutibu Uwongo

Hizi hapa ni miongoni mwa sababu zinazofanya watoto wadanganye:

- Wanataka kukwepa adhabu.
- Wanataka kuwaaminisha watu waamini kuwa vitu vya watu wengine kuwa ni vyake.
- Wanahisi kupuuzwa, kukataliwa na kutelekezwa.
- Wanataka kujisifu kwa wenzao, kwa kueleza sifa zisizokuwa zao.
- Wanataka waheshimike katika vitu ambavyo hawajahusika.
- Wanaweza kufikiri kwamba wanaruhusiwa kudanganya kwa kuwa wazazi wao wanafanya hivyo.

Sababu kubwa inayowafanya watoto waongope ni kuogopa kuadhibiwa. Wao huhamasishwa na raha au karaha. Kwa namna itakavyowezekana, wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kukiri makosa yao na kuomba msamaha. Kama watoto wao wakichukua kitu fulani kutoka dukani bila kukilipia, wazazi wanapaswa kuhakikisha kwamba watoto wao wanarudisha na kumkabili muuza duka moja kwa moja kwa kumuomba msamaha. Kama watoto watatumbukia katika dimbwi la kupenda kudanganya, wazazi wanapaswa kutafuta sababu za kutokea hali hiyo. Mara nyingi watoto hufanya kazi mbalimbali, ambazo pengine hawawezi kuzimudu sawasawa na kwamba kunakuwa na msukumo mkubwa katika kuzifanya. Wanaweza kuwa wanadanganya kwa kuwa wanashindwa kumudu vishindo hivyo. Watoto wengine

huweza kudanganya kwa sababu ya kukatishwa tamaa na kwamba hawapewi kipaumbele. Watoto ambao wamepewa kipaumbele kutokana na kuhadithia visa na uongo wanaweza kuendelea kufanya hivyo ili waendelee kupewa kipaumbele au kuthaminiwa.

Kufuatilia tabia ya watoto, ikiwa ni pamoja na muda na mahali ambapo hudanganya sana, inaweza kusaidia hasa kunapotokea tatizo. Pengine watoto hudanganya wakati wakiwa michezoni tu, au pengine ni wakati wakitenda kosa, au pengine ni wakati wakiwa na rafiki zao na hivyo kujaribu kuvuta umakini kutoka kwa wenzake. Mazingira yote haya yanaweza kuhitaji mrejesho tofauti tofauti.

Kuongopa kunapaswa kuzuiwa toka watoto wanapotenda kosa hilo kwa mara ya kwanza. Mtu anayekua akiwa anaongopa ataishi maisha magumu sana. Watoto wanapaswa kufundishwa kwamba kutokuwa wakweli hakukubaliki kabisa. Usimuadhibu mtoto kwa makosa ikiwa atakiri kuyatenda. Hata hivyo, kunapaswa kuwa na madhara kutokana na makosa aliyoyafanya mtoto. Mathalani: kama akimpiga mtoto mwingine wanapaswa kuchukuliwa na kupelekwa kwa wazazi wa mtoto aliyepigwa ili aombe radhi; kama wakikamatwa wakiwa wanafanya udanganyifu katika majaribio ya shuleni, wanapaswa kufelishwa hapo hapo. Hata hivyo, wanaposema ukweli, kusiwe na adhabu ya moja kwa moja kwa watoto. Zawadi mojawapo kwa ajili ya watoto kusema ukweli ni kwa wazazi kutowakaripia. Wazazi wanapaswa kuwa na mrejesho unaotazama mazingira na athari ya mrejesho kwa kutumia busara. Kufanya hivyo kunakamilisha malengo mawili muhimu.

Kwanza, inahakikisha kwa mipaka ya mawasiliano kati ya wazazi na watoto itakuwa mipana. Watakuwa wakizawadiwa wakiwa waaminifu, kwa kuwa kuongopa hutokana na kuogopa adhabu.

Pili, kwa sababu ya mahusiano mazuri yaliyowekwa baina ya wazazi na watoto wao; kwa mazungumzo, ukweli, na bashasha, watoto watakwepa kuwaudhi wazazi wao. Mahusiano ya kimapenzi baina yao yataimarika na kuboreka sana na hivyo kuziathiri tabia zao. Wazazi hawapaswi kuogopa kwamba kanuni ya kutowaadhibu watoto ili waseme ukweli itageuka kuwa tatizo baadaye. Mapenzi ya pamoja yatajenga udhibiti mkubwa katika familia.

- Njia ya muongo ni fupi.
- Kuongopa kutakufanya watu wasikuamini, na kutawafanya waone wamesalitiwa na kuchakachuliwa.
- Ukisema ukweli, huwezi kuchanganya mambo, huna kazi ya kukumbuka ulichokisema, na husahau ulichokisema.
- Uaminifu utajengeka, ambao utakuwa nguvu itakayokusaidia usonge mbele kwa mafanikio makubwa. Ukiongopa, kunakuwa na nguvu kubwa pia za kukunyima mafanikio.

Hatua zifuatazo juu ya kutibu tabia ya uwongo zimeelezwa katika kitabu cha, *al-Khuluq al-Kamil* (Tabia iliyokamilika) cha Muhammad Jad Almawla (2002 kwa Kiarabu):

- Ikiwa mtoto anaongopa na kusema sana, basi mwambie anyamaze.
- Ikiwa mtoto anaongopa kwa kuwa anaogopa adhabu ya kikatili, basi kuwa na huruma kwake.
- Ikiwa mtoto anaongopa kwa kutamani au kutaka kupata kitu fulani, basi usimkubalie kumpatia kitu hicho.
- Ikiwa mtoto anaongopa kwa kuwafanyia mzaha wenzake na kuwapuuza, basi muadhibu.
- Ikiwa mtoto anaongopa kwa kutaka kuwashawishi marafiki wabaya, basi mtafutie marafiki wazuri.
- Kabiliana naye kwa kutumia kinyume cha anachokihitaji kutokana na kuongopa kwake.

Vijana wanapaswa kufundishwa kwamba kuongopa ni kitendo cha aibu na kinyume cha maadili mema, uaminifu, haki, na heshima. Ibn Khaldun atushauri kwamba: Kumfundisha muongopaji kuhusu vipengele vinavyoenda kinyume na maadili ya kuongopa, na namna vinavyoenda kinyume na tabia njema za wanadamu. Wanadamu wana mapenzi katika ukweli, haki, na uaminifu.

Kutoa elimu kwa kutumia nguvu ni hatari kwa wanafunzi, hususani, watoto. Wakati mtoto anapokuwa amelelewa katika mazingira ya kugombezwa, au mazingira ya kikatili, au ya kukandamizwa atakuwa na msongo wa mawazo na mfadhaiko ambao humsababishia uzembe na kupendelea kudanganya au kutenda makosa. *Al-Muqaddimah*, sehemu ya 32, 1992).

Jaza maisha ya watoto kwa mapenzi na kuwajali. Pindi wengine watakapogundua kutowepo kwa uaminifu, watapoteza uaminifu wao kwako na kutokukupenda tena. Pindi wazazi wanapowaeleza watoto wao kusema ukweli, katika mazingira yoyote, basi wazazi wao wenyewe wanapaswa kusema ukweli, ili waweze kuonekana kwamba ni waaminifu, na kuheshimika kwa utu wao. Wananchi wakweli na waaminifu hupata heshima, ushirikiano, na ukweli kwa watu wengine.

Waeleze watoto visa vyenye malengo

Shaykh 'Abd al Qadir al-Jaylany wa Baghdad alisimulia:

"Niliapa kwa mama yangu kumwambia ukweli mara zote. Niliondoka Makka na kwenda Baghdad kusoma. Mama yangu akanipatia *dinari* 40 kwa ajili ya safari. Genge la wezi wakanishambulia njiani karibu na Hamdan. Mwizi mmoja aliniuliza, 'fedha kiasi gani ulizonazo?' Nikamjibu: 'dinari 40.' Akaniacha, akidhani nilikuwa nikimtania. Kisha mwizi wa pili aliniuliza, nikamueleza kwamba nina dinari 40. Akanipeleka kwa mkubwa wao, ambaye aliniuliza: 'Kwa nini unasema ukweli?' nikamjibu kwamba "Niliapa mbele ya mama yangu kusema ukweli mara zote na sitaki kuvunja ahadi yangu.' Mkuu wao alishtuka. Akakasirika na kupiga kelele akisema; 'Unaogopa kuvunja ahadi uliyoiweka mbele ya mama yako, nani

siko tayari kuvunja ahadi yangu kwa Mwenyezi Mungu?' Aliwaarimsha wezi wote kunirejeshea mali zangu zote na kusema, 'Naenda kutubia kwa Mwenyezi Mungu mbele yako.' Wafuasi wake wakamwambia, "Ulikuwa kiongozi wetu katika wizi, na leo umekuwa kiongozi wetu katika kutubia.' Wote walitubia kwa Baraka za kusema ukweli."

Wazazi: Hiki ni kisa chenye malengo, bila kuangalia chanzo chake. Maadili yaliyoonekana katika kisa hiki kwa watoto ni kwamba uaminifu unaweza kukunusuru na kuwanusuru wengine pia.

Njia ya Kitume ya Kutibu Uwongo

1. Kijana mmoja alikuja kwa Mtume (s.a.w) na kumwambia: "Ee Mtume wa Allah, mimi siswali, ni mzinzi, na ni mwongo. Nitubie kwa kitu gani?" Mtume (s.a.w) akasema, "Tubia kuongopa." Kwa hiyo kijana huyo aliahidi kutoongopa tena. Muda haukupita, alipoondoka, akataka kufanya uzinzi, akajisemea mwenyewe, "Mtume anaweza kuniuliza kama nimefanya dhambi. Ikiwa nitasema hapana, nitakuwa naongopa, na nikisema ndiyo, nitakabiliana na adhabu kwa ajili ya dhambi zangu." (Tibris, 1991).

Unapoepukana na kusema uwongo, ambayo ni dhambi kubwa, wakati huo huo, unaepukana na dhambi na makosa mengine.

2. Kusema ukweli ni jambo kubwa, hata kwenye mazingira yanayoonekana kuwa na changamoto kubwa. Mtume (s.a.w) alitoa mwongozo ufuatao:

> Yeyote atakayemueleza mtoto kuja na kuchukua (mshumaa) huu kwa kuficha katika mkono wako na asimpatie chochote, atakuwa amedanganya. (Ahmad).

Mtume (s.a.w) pia alisema:

> Watu wabaya kabisa ni wale wenye sura mbili: anaonesha sura moja kwa baadhi ya watu na kuwaonesha wengine sura nyingine. (Al-Bukhari).

Ukweli na uaminifu, kwa kuongezeana sifa za mapenzi na ujasiri, ni sifa za tabia ambazo hupatikana kwa watoto waliotosheka kwa wazazi wao. Hebu, tutazame upande wa wajibu, uhuru na ubunifu katika sura zifuatazo.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 55: KUBADILISHANA UZOEFU

Shirikiana na watoto wako katika mazingira ambayo ulisema ukweli, ambapo pia ingewezekana kuongopa. Kulikuwa na matokeo gani, au tiba gani, na mafunzo yatokanayo na kudanganya? Watoto pia wanaweza kuelezea visa vyao wenyewe.

ZOEZI LA 56: MOJA KATI YA TABIA MBAYA SANA UNAYOTAKA WATOTO WAACHANE NAYO

Ni tabia gani iliyo mbaya zaidi ambayo watoto wako waachane nayo? Jawabu: Kuongopa.

- Wasimulie watoto unataka visa vya kweli kuhusu watu ambao waliharibu maisha yao kwa kuongopa. Wangekuwa wakweli wangepata mafanikio na kuishi maisha yenye furaha.
- Wakumbushe watoto wako na kujadiliana nao ukweli kwamba wapagani wa Makkah walimuita Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa ni “Mkweli na Muaminifu” kabla ya utume wake.

18

SURA YA KUMI NA NANE

- KUFUNDISHA UWAJIBIKAJI

SURA YA KUMI NA NANE **444**

Kufundisha Uwajibikaji **444**

Utangulizi 446
Tabia na Mtazamo wa Kiulimwengu 448
Fursa katika Hatua Mbalimbali za Maendeleo ya makuzi 450
Kanuni za msingi za kuimarishwa 451
Jenga uwajibikaji taratibu 453
Kataza tabia ya mtu kusema 'lile si jukumu langu' 454
Ushauri wa kutekelezwa 454
Unganisha Hadhi na Uwajibikaji: Mifano 456
Kazi za Kufanya

Basi anaye tenda chembe ya wema, atauona! Na anaye tenda chembe ya uovu atauona!
(Qur'an 99:7-8).

Utangulizi

Maana ya kuwajibika ni kufanya kazi kwa busara bila kuelezwa, kulazimishwa au kutishwa. Ni uwezo wa kufanya maamuzi na kuwajibika kwa vitendo. Mtume (s.a.w) anasema:

> Yule ambaye hajishughulishi katika mambo ya Waislamu, si miongoni mwao. (Ahmad).
>
> Si katika waumini ambaye analala akiwa ameshiba kupita kiasi wakati jirani yake ana njaa, wakati anaijua hali hiyo. (Al-Tabarani).

Kufundisha uwajibikaji ni muhimu sana. Watoto wanapaswa kufundishwa kutekeleza wajibu wao bila kusimamiwa au kukumbushwa. Watoto wanaowajibika hujitolea kufanya kazi za jamii, bila kulizwa au kupangiwa kazi hizo. Watoto wanaowajibika pia huwa na kiu ya kutimiza kazi zao kwa mafanikio. Njia mojawapo ya kuhamasisha uwajibikaji kwa watoto ni kuwafundisha namna ya kujisimamia wao wenyewe. Watoto wanaowajibika hutambua umuhimu wa tabia zao na madhara ya vitendo vyao. Tabia nzuri kwa mtoto kuichukua ni ile ya kuwajibika katika mambo yote aliyoyatenda siku nzima kabla ya kulala usiku. Wajengee watoto mfumo wa sera hii na kuifuatilia. Wazazi wanapaswa kuwajaza watoto wao upendo na kumuogopa Mwenyezi Mungu katika mioyo yao na fikra zao ili kuwafanya wajitambue kila wakati. Kuwaeleza watoto kwamba Mwenyezi Mungu yupo pamoja nao mahali popote kunawaimarishia moyo wa uwajibikaji.

Uwajibikaji ni zaidi ya kukumbuka kufanya majukumu yako au kuwa mtiifu. Inajumuisha kujali lipi tendo zuri na lipi ni baya, namna gani kitendo cha mtu kitaathiri watu wengine, na kutambua kwamba ni kanuni ni muhimu. Ili Kuwafundisha watoto kuwajibika, wazazi wanapaswa kuwa wawajibikaji pia.

Mfano mzuri: Baba na mwanawe wa kiume wanawahi dukani kabla halijafungwa. Wanasimama kumsaidia mwanamke kupandisha kigari cha mtoto ghorofani. Mtoto anajifunza kwamba ni vema kutoa msaada, hata kama utakosa baadhi ya thamani za kifedha.

Pindi watoto wanapowajibika katika majukumu, wazazi wanapaswa kutambua na kueleza kufurahishwa kwayo. Kuwapa pongezi watoto kwa tabia nzuri kunawahamasisha wawe na tabia nzuri zaidi. Mara nyingi watu hawatilii maanani watoto wanapokuwa na tabia ya kuwajibika au huchukuliwa kama kawaida tu. Kibaya zaidi, wazazi wengi husema pale wanapowaona watoto wao hawawajibiki. Matokeo yake sasa, watoto hujisemea: "Nikiwa nafanya kitu kizuri hakuna anayekumbuka, na pindi ninapokosea hakuna anayesahau." Wazazi wanapaswa kusema, "Shukran, huo ni msaada mkubwa." Wanapaswa kuwa waangalifu kutambua tabia za watoto wao, ambazo ni muhimu kwao, lakini hiyo inaweza kuonekana si muhimu kwa watoto, kama: "nimegundua kwamba umeweka vitabu vyako chumbani kwako badala ya sebuleni. Nzuri sana, sasa naweza kuandaa meza kwa ajili ya chakula cha jioni." Au "Nafurahi kuona unaning'iniza jaketi lako mahala husika pindi ukiingia."

Kufanya maamuzi mazuri ni sifa mojawapo ya tabia ya uwajibikaji. Watoto wanaoelezwa cha kufanya kila wakati ni mara chache sana huweza kufanya maamuzi yenye tija. Hawataweza kufundishwa kuwajibika. Ni vema watoto wapewe fursa ya kufanya maamuzi, kwa kuwa katika utu uzima, wataweza kufanya maamuzi kati ya jambo moja na jingine kuwa ni kitu cha kawaida. Badala

ya kuwagawia majukumu wanafamilia, orodhesha kazi zote zinazopaswa kufanywa nyumbani, kisha jadili na wanafamilia kuhusu nani atafanya kipi. Kwa pamoja watagawana majukumu, hivyo kila mmoja atakuwa amepata kazi ya kufanya ambayo ataifanya kwa bidii kwa kuwa ni chaguo lake, na pia ni vema kubadilishana majukumu ili kuwasaidia wanafamilia ambao wanaweza kukwama katika kazi ambazo zingine zinaweza kuwa ngumu. Kuwajumuisha watoto katika mchakato huu kunaonesha kwamba wazazi wanawajali watoto wao na kuthamini mawazo yao, na hii huwafanya kuwa marafiki wenye kuzingatia uwajibikaji. Pia huwafanya kuwa sehemu ya timu, ambayo kila mjumbe atakuwa akiwategemea wengine katika majukumu ya kifamilia bila matatizo. Hii ni njia ya kivitendo ya kuwafundisha watoto namna ya kufanya maamuzi, kufanya ushauri (kushauriana kwa pamoja), na kuwajibika.

Kuweka Msingi: Tabia na Mtazamo wa Kiulimwengu

Kama sisi ni wazazi tunaowajibika, nusu ya kazi imeshafanyika. Kazi iliyobakia ni kuwasaidia watoto kufuata nyayo zetu.

Watoto wanahitaji elimu ya kutosha, pamoja na tabia njema ili kuwaandaa na utu uzima. Uwajibikaji ni miongoni mwa sifa muhimu katika tabia njema. Uwajibikaji unaanza na utayari katika akili, au imani ambayo wazazi huwarithisha watoto wao. Kama mtazamo wa kiulimwengu wa wazazi ni kwamba watoto wanapaswa kucheza na kuwaliwaza wao, watoto watapata uzoefu huo lakini watalalamikia kazi zao. Kama wazazi wanaamini kwamba watoto watakuwa wachoyo wakati wote, basi matarajio hayo hudhihirika kwa watoto hapo baadaye. Hata hivyo, kama mtazamo wa kiulimwengu wa wazazi ni ule kwamba, kila mtu bila kuzingatia umri wake na uwezo wake, anapaswa kuchangia katika maisha ya wote, kisha maamuzi yao, tabia zao, na matarajio yao yatasawiri hayo, na kwamba watoto wao watajifunza thamani ya uwajibikaji.

Tunataka kuwalea watoto wenye mafanikio katika maisha. Watoto wanaojifunza uwajibikaji mara nyingi hujitegemea na kuwa na uwezo wa kuwajibika kwa matendo yake mwenyewe wakati wa utu uzima. Uwajibikaji ni weledi wa kujifunza, na kwamba watoto wanapaswa kufundishwa toka wangali wadogo. Watoto ambao wamekulia katika mazingira ya uhuru katika changamoto wanakosa fursa ya kujifunza uwajibikaji. Wazazi wengine wanaenda mbali zaidi wanapojaribu kuwatengenezea maisha mazuri watoto wao. Wazazi hawa huwakataza kuthubutu katika changamoto mbalimbali zinazoweza kuwakabili. Watu kama hawa huwa msaada wa karibu kwa watoto, tabia ambayo huwafanya watoto kuwa tegemezi na kutokuwa wawajibikaji. Watoto hawa hukua wakiwa na fikra za hadhi fulani ya juu. Wanatengeneza mazoea mabaya ya: 'naudai ulimwengu' badala ya tabia tija ya: 'ulimwengu utanifanya mimi kuwa mtu mwenye kuwajibika kama nitawajibika kwake.'



Watoto hawawezi kuwa wawajibikaji ikiwa hawatambui, na pia wanaweza kujifunza tu pale wanapofundishwa. Kufundisha na mafunzo ni sehemu muhimu sana ya uhusiano baina ya wazazi na watoto. Kuwa muwajibikaji ni tabia na weledi. Watoto hawawezi kuwaondoa wanasesere mpaka wafundishwe. Watu wazima wanaweza wasijue namna ya kurejesha vitu walivyoviazima au kufika kazini katika muda uliopangwa mpaka wawe wamepewa mafunzo. Namna nzuri ambayo wazazi wanaweza kuwafundisha watoto wao uwajibikaji ni kwenda nao taratibu, siku baada ya siku.

Usikubali kuwatengenezea vijana wadogo tabia ya uzembe. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuwapatia watoto majukumu. Hata hivyo, unapaswa kuwapa watoto majukumu zaidi ya kufua nguo, siku mbili kwa juma na kutupa taka. Pindi vijana wadogo wasiowajibika wanapolazimika kuendana na mazingira ya kufanya kazi za nyumbani kwa saa 40 kwa juma (au kutumia muda mwingi chuoni na kufanya kazi za muda nje ya chuo.) watakuwa hawajajiandaa. Uchapakazi na uwajibikaji ni muhimu sana kwa mtu mzima mwenye kuzalisha na mwenye mafanikio.

Anza nao katika umri mdogo, kabla hawajaanza shule. Watoto wanapaswa kufundishwa pindi kunapokuwa na matarajio ya kupata mtoto mpya kwamba: "Tutafurahi kumlea mtoto pamoja." Watoto watafurahishwa na wazo la kuwajibika katika mradi huu maalumu. Hapo basi watoto wanaweza kuwasaidia wazazi wao katika malezi ya mdogo wao kwa kumpa nepi safi, kuhifadhi nguo chafu za mtoto mdogo, na kumuokotea mwanasesere wa mtoto anapoanguka. Ujanja uliopo hapa ni kuhakikisha watoto wanajishughulisha katika majukumu yao. Badala ya watoto kuwatazama wazazi wao, watoto wanapaswa kusaidia katika majukumu.

(SHAIRI LA KIARABU)

Anza Mapema

Matawi madogo yatanyooka, ikiwa utajaribu kuyanyoosha.

Lakini hayatanyooka kama yatakuwa na kukomaa.

Fursa katika Hatua Mbalimbali za Maendeleo ya makuzi

MTOTO MCHANGA NA ANAYEANZA KUSIMAMA

Katika hatua hii watoto huanza kujaribu mipaka ya wazazi wao. Mathalani, mtoto wa miaka miwili huanza kujifunza kumtupa mwanasesere wake ili kuvuta umakini, kisha atajifunza kumtupa mwanasesere kuonesha hasira zake, na kisha atajifunza namna ya kumuudhi mtu mzima. Katika wakati huu, wazazi wanapaswa kuweka mipaka kwa watoto wao kuliko kuwaacha kuweka mipaka. Mtoto anapomtupa mwanasesere wake kwa mara ya kwanza, basi wazazi wanaweza kumuokotea na kumpatia. Hata hivyo, ikiwa mtoto atafanya hivyo kwa kukusudia na kurudiarudia, basi ni wakati wa kumuondoa huyo mwanasesere mbele ya mtoto. Hapa mtoto atatambua kuwa kumbe tabia mbaya haitunukiwi. Umri huu huitwa "Hatari mbili."

Kadiri watoto wanapokua na kufikia hatua ya kusimama na kuanza kujifunza kutembea, hapa watajifunza kwamba ni matendo gani yanaweza kujaribu uvumilivu wa wazazi wao. Ni katika umri huu, mtoto anapaswa kujifunza kwamba kuna madhara katika tabia mbaya. Ikiwa wazazi watawaeleza watoto wao, "kama hutaacha, tutaenda nyumbani" hivyo wanapaswa kusimamia vitishio vyao. Kama wazazi watawafundisha watoto wao kwamba wanawapa vitisho vikubwa, maneno yao yatachukuliwa kwa uzito mkubwa. Ni muhimu wazazi wote wakafanya hili.

KIPINDI CHA UTOTO

Katika umri wa utoto, watoto wanapaswa kujifunza kujijali. Wanapaswa kutana nywele zao wao wenyewe, kupiga mswaki wao wenyewe, kufunga kamba za viatu na kuwa nadhifu wakati wote. Kuwapatia watoto wako kazi ndogo ndogo kutawasaidia kukuza kujiamini kwao na hisia zao katika mchango wa familia. Watoto wanaokataa kufanya majukumu yao wanapaswa kutambua kwamba kutakuwa na madhara. Ikiwa Kazi hazitaweza kukamilika, basi watoto wanaweza wakazuiwa kwenda kucheza na rafiki zao, au kutazama televisheni, au kufanya kitu chochote ambacho ni cha furaha kwao. Pindi wanapozimaliza kazi walizopewa, basi watoto wanaweza kuruhusiwa kufanya wanachotaka.

UMRI WA SHULE NA KUELEKEA KATIKA UJANA

Kadiri watoto wanavyokua, majukumu yao huongezeka. Kuwapatia watoto ruhusa au zawadi mara kwa mara wanapomaliza kazi zao kutawafanya waongeze hisia kwamba walichokifanya kinathamani kwa wazazi wao. Wapongeze watoto kwa uwajibikaji wao. Mathalani: kadiri watoto watakavyojitahidi kumtunza paka wa nyumbani, zawadi maalumu inaweza kuandaliwa kwa ajili yao, kama kadi ya ripoti ya mafanikio, kuwaandikia ujumbe kuwapongeza uwajibikaji wao na kwamba wazazi wanajisikia fahari sana kwa uwajibikaji wao.

Ikiwa watoto hawafanyi vema shuleni, au hawana msaada nyumbani, basi ni vema wazazi wakatafuta mzizi wa tatizo.Watoto hufanya vema wanapowekewa mipaka. Wale watoto ambao hawahamasishi kufanya vema, iwe nyumbani au shuleni, watashindwa kutimiza ndoto zao. Kuwapatia watoto moyo wa uwajibikaji kwa matendo yao huhitaji mazingira ya kimalezi. Watoto wanapaswa kuruhusiwa kufeli pamoja na kufanikiwa.

Watoto wadogo, huwa wakali sana wanapokabiliwa na ushawishi wa makundi. Watoto ambao wamelelewa katika nyumba ambazo zimewafundisha uwajibikaji wataweza kuepukana na ushawishi wa tabia mbaya kirahisi zaidi. Kuweka wazi mipaka ya mawasiliano, kunawapatia watoto fursa ya kujadili hofu zao pamoja na wazazi wao na kuwapatia uhalisia wa vilivyomo mioyoni mwao.

VIJANA

Vijana wanakabiliana na fursa nyingi sana za kufanya maamuzi mabaya. Kijana anayetambua lipi zuri na lipi baya anajua kuwa vitendo vibaya huwa na madhara, basi atajitahidi kufanya maamuzi sahihi.

Endelea kuwafundisha wanao moyo wa uwajibikaji. Kama msingi wa uwajibikaji umekwishawekwa, basi wazazi watakuwa na fursa nzuri sana kujadili kesho ya watoto wao pamoja nao.Watoto wanahitaji kujua maana na faida ya kuwajibika. Wasaidie watoto kuendeleza malengo yao ambayo yanaweza kufikiwa.

KIJANA ANAYEELEKEA UTU UZIMA

Kama umewafundisha watoto wako moyo wa kuwajibika, basi wao wanajitosheleza na wanaelekea kuishi kwa kujitegemea. Wazazi waliowafundisha watoto wao kuwategemea wengine watagundua kwamba watoto wao hawawezi kuondoka nyumbani. Watu wazima ambao hawakuwahi kujifunza madhara ya matendo yao mabaya, watajikuta wakitumbukia katika matatizo, lakini bado watatazama sehemu nyingine ya kupeleka lawama zao kwa matatizo yao. Daima mahusiano yatakuwa na changamoto kwa watu wazima ambao wasiowajibika.

Kanuni za msingi za kuimarishwa

IFANYE KAZI KAMA SEHEMU YA FURAHA

Watoto wadogo huamini chochote kisemwacho na wazazi wao, kwa hiyo wanaweza kufundishwa kwamba kazi inaweza kuwa sehemu ya furaha.Wazazi wanaweza kufanya mchezo wa kuondoa wanasesere na vinywaji. Kama vijana, watoto hawa watakuwa wachapakazi na kuwa na msaada nyumbani. Wazazi wanapaswa kuwa makini sana na wakisemacho mbele ya watoto wao. Ikiwa watoto watasikia, “Mama angependa kufurahi nanyi, lakini ana kazi anaifanya” hapo wazazi wanatuma ujumbe kwamba kazi ni kitu kibaya na kisichopendwa. Badala yake, unaweza kusema “Mnaweza kufurahi nami wakati nikiwa nasafisha sakafu. Mnaweza kunishikia kizoleo cha taka. Hili halitakuwa zuri?”

Wafundishe watoto kwamba hakuna kazi yoyote ya nyumbani au bustanini isiyowahusu, kwani kazi zote hizo zinatambulika. Ni vema kufikisha ujumbe kwamba kazi ile ina heshima, na wala siyo haki. Wazazi wanapaswa kushirikiana na watoto katika mazuri ya kazi zao. Itakuwaje kama hawataweza tena kufanya kazi zao za kawaida kwa sababu ya kupata ajali au kuachishwa kazi au kuumia? Kila mmoja anapaswa kutambua neema ya afya njema. Wazazi hawapaswi kupoteza muda katika kuwapatia watoto wao faraja katika kazi zao na majukumu yao.

Wazazi wanapaswa kujitahidi kufanya kazi kuwa sehemu ya furaha zao, kwa nyimbo za furaha, ucheshi, au mazungumzo ya pamoja. Mazingira ya ucheshi huwasaidia watoto kuboresha tabia zao kuelekea katika uwajibikaji. Kama ratiba ya familia ya kufanya kazi na kufurahi au kucheza inaweza kuwekwa katika muda mmoja katika siku, itasaidia mazingira ya kuleta umoja na usawa katika familia, ili watoto wengine wasijisikie kufanyakazi wakati wengine wakicheza. Kama kuna kazi inapaswa kufanywa bustanini, itakuwa vema familia nzima ikafanya kwa pamoja.

KUFANYA KAZI PAMOJA

Wazazi wanaweza kuona kwamba inafaa kutumia neno “sisi” katika kuwapa mafunzo. Mathalani: wanaweza kuwaambia watoto wao, “Huwa tunaweka nguo zetu zilizo chafu katika jamanda, kama hivi, badala ya kuweka sakafuni.” Watoto wanapenda kushirikishwa na kutumia neno “sisi” kunawahamasisha tabia njema bila kuwapeleka darasani. Badala ya kumwambia mtoto “safisha chumba chako!” Mzazi anaweza kusema, “Hebu tusafishe chumba chako pamoja.”



Watoto husoma vitu vizuri na kujenga tabia njema wakifanya kazi pamoja na wazazi wao. Hujiona wanapendwa na kuzinasibisha kazi na uwajibikaji pamoja na mapenzi ya wazazi wao. Hii inawapatia sifa njema zaidi kuhusiana na kazi hapo baadaye.

“KANUNI KUMI” ZA KUWAJIBIKA BUSTANINI

Pindi watoto watokapo nje, wanapaswa kufanya kazi kumi kabla hawajaanza kucheza. Miongoni mwazo inaweza kuwa ni kukusanya mawe kumi au majani, kuokota maua kumi yaliyokauka, kuweka majani makubwa kumi yaliyokauka katika kikapu cha taka, kuchuma majani ya miti kumi yenye kuleta madhara. Au mtoto anaweza kufanya kazi moja kubwa kama ya kusafisha bustani kwa kutumia reki au kumwagilia maji bustani. Hii inawafundisha watoto kulinda mali.

> Wazazi wanapaswa kuwahamasisha watoto wao kupata mazao yao wenyewe inapowezekana.

Mlibya mmoja alinieleza kwamba namna gani alivyoigawanya bustani yake katika sehemu sita, na kumpatia kila mtoto mmoja sehemu yake, ambaye anaweza kupanda chochote akitakacho. Kama mkewe angehitaji mboga mboga basi angewauliza watoto kama anaweza kupata nyanya au pilipili au chochote kinachoweza kupatikana. Bustani zilihudumiwa vema sana na njia hii ilisaidia katika mgawanyo wa kazi zote katika bustani. (Silvia Hunt).

Watoto wadogo ambao bado hawajaanza shule wanapaswa kuruhusiwa kuchagua katika baadhi ya mambo. Pia kuna wakati ambao mtoto anahitaji kusikia, “Hiki ndicho utakachokifanya.” Usithubutu kufanya makosa kuwafundisha watoto kuwa wavivu kwa kushindwa kuwaruhusu kufanya wanachotaka kukifanya. Sehemu ya muhimu katika uwajibikaji ni kujifunza kinachopaswa kufanywa. Kwa wakati mmoja hakikisha kuwa upo madhubuti na mwenye mapenzi kwa watoto.

Jenga uwajibikaji taratibu

Kosa mojawapo wanalofanya wazazi ni kuwaacha watoto wao kucheza bila kufanya kazi mpaka wanapofikia umri wa “kuwajibika”. Hapo ndipo kunapokuwa na kazi nyingi za kufanya na majukumu mengi yakuyatenda. Wasaidie watoto taratibu kufanya kazi nyingi na kuwajibika kila mwaka. Katika baadhi ya nchi zinazoendelea, watoto, hususani wasichana, wanatarajiwa kuwatunza watoto na kubeba mafuta na maji pamoja na kuwasaidia wazazi wao kazi za nyumbani. Watoto katika umri wa miaka 8 wanaweza kutumwa kufanya kazi kama wahudumu wa nyumbani.

Mtoto huanza bila kazi, afikishapo umri wa miaka 19 hufanya kazi kwa saa 40 katika juma. Kazi ya wazazi ni kujenga uwajibikaji taratibu. Watoto ambao wanaongeza uwajibikaji wao wataweza kumudu kazi wakifika katika utu uzima.

Ratiba inaweza kuanza kabla ya kuanza shule, wakipewa kazi kama kuweka nguo katika jamanda na kuokota wanasesere. Kazi nyingine zinazofaa kwa watoto zinaweza kuongezwa taratibu kadiri umri unavyoongezeka. Watoto wa miaka sita wanaweza kupewa jukumu la kupanga meza kila siku, kutandika vitanda vyao, kusaidia kukausha vyombo, kuwalisha wanyama, kusafisha meza baada ya chakula, na kuondoa mashine ya kufulia kwa kusaidiwa. Majukumu mapya yanaweza kuongezwa taratibu kadiri atakavyoendelea kukua. Vijana wanaweza pia kufanya kazi za kulipwa au za kujitolea katika jamii.

Kataza tabia ya mtu kusema 'lile si jukumu langu'

Watoto wanapaswa kufundishwa kwamba kuwajibika kunapaswa kutendwa na wanafamilia wote. Watoto wanaoruhusiwa kuleta ubishi katika haki hukosa jukumu la kuwasaidia wengine. Kama kipaumbele kikiwekwa mara kwa mara kwa mtoto anayechuma majani mengi au watoto wawili waliokausha idadi sawa ya vyombo, watoto wanaweza kujenga tabia za kibaguzi ambazo si nzuri katika utulivu wa kifamilia. Tengeneza tabia ya kufanya kazi kwa pamoja katika fikra zao. Wazazi wanaweza kuwaeleza watoto wao, "Pindi meza inaposafishwa na kupanguswa, sote tunaweza kutazama video au kwenda mbugani," au, "Kama tukifanya kazi za bustanini leo, tunaweza kupata Barafu tamu (ice cream) au *Bisi* usiku." "Baada ya kumaliza kufanya usafi tusafiri pamoja tukasherehekee." Zawadi za pamoja huhamasisha umoja, ushirikiano, na uwajibikaji. Watoto wanaweza kuulizwa kusaidiana wakati mmoja wao ni mgonjwa. Ni muhimu kuwahamasisha kusaidiana katika kazi na kuvumiliana katika matatizo. Watoto ambao umri wao ni mkubwa wanapaswa kuwasaidia wadogo zao pamoja na rafiki zao wa shuleni, na watoto wadogo wanapaswa pia kuwasaidia kaka na dada zao katika kazi zao.

Ushauri wa kutekelezwa

- **Usiwazidishie watoto kazi.** Wazazi wanapaswa wazingatie uwezo na mienendo ya watoto wao, na kuwapatia majukumu wanayoweza kuyafanya kwa mafanikio. Mafanikio na pongezi zitawahamasisha kuongeza juhudi zaidi, ambapo kuwazidishia kazi kunaweza kuwafanya kushindwa na kuharibu hamasa yao katika kazi.

- **"Tarajia" watoto wawajibike.** Matarajio ya wazazi huwahamasisha watoto. Wanapowapatia kazi, wanaweza kujadili muda unaokubalika wa kufanya jukumu hilo. Kisha wanapaswa kuwaacha watoto wafanye na kutegemea kwamba kazi itafanyika. Waruhusu watoto wamalize kazi kwa namna yao wenyewe bila kuwasimamia au kuwakumbusha mara kwa mara juu ya majukumu hayo. Kama hawataweza kuyamudu majukumu hayo, wazazi wanaweza kuwasaidia.

- **Usimuite mtoto "mzembe".** Hata kama mtoto atafanya kitu cha kizembe, kama vile kwenda kutazama filamu wakati waliwaahidi rafiki zao kusoma ili wajiandae na jaribio, wazazi wanapaswa kuacha kuwataja vibaya. Badala yake, ni vema kuwahamasisha kulitenda lile alililoliacha haraka iwezekanavyo. Na ikiwa mtoto anakuwa msahaulifu

sana, wazazi wanapaswa kukwepa kutamka maneno kama, "kama kichwa chako kisingeunganishwa na mwili wako, ungekisahau pia." Maneno kama haya yanaumiza na kukatisha tamaa. Unaweza kukemea tabia lakini si mtu.

▪ **Watoto wanahitaji msaada katika utengeneza ratiba zao**. Waoneshe namna ya kukadiria muda gani unaweza kutumika kufanya zoezi la mwalimu na kulipangilia sawasawa. Wasaidie watoto kutengeneza ratiba baada ya shule. Waoneshe namna gani kuna muda wa kutosha wa kukamilisha kazi zao, kuoga, na bado wakabakiwa na muda mwingine kwa ajili ya kupumzika na kucheza nje.

▪ **Gawanya kazi kubwa katika kazi ndogo ndogo.** Watoto wanapopewa kazi za kuandika ripoti, wazazi wanapaswa kuwasaidia kujadili muda utakaotosha kwenda maktaba kutafuta taarifa au kutafuta katika mitandao ya kielektroniki na kuandika sehemu tofautitofauti za ripoti. Watoto wanahitaji msaada wa kuivunjavunja ripoti ya mradi katika sehemu mbalimbali ili kurahisisha upangaji katika kufikia malengo ya kila sehemu.

▪ **Wazazi hawapaswi kufanya kazi za shuleni za watoto wao.** Inashangaza namna wazazi wengi wanavyokamatwa katika mtego wa kuwasaidia watoto wao kufanya kazi za shuleni. Watoto wanapaswa kuelezwa kwamba kazi za shule za kufanyia nyumbani ni jukumu lao, sio jukumu la wazazi, ikiwa kazi hizo zinaendana na uwezo wa mtoto. Hata hivyo, watoto wanahitaji msaada wa kiwango fulani sasa na baadaye, na wanahitajika kujaribiwa katika uwezo wao katika kuandika kwa usahihi hususan mpango wa herufi au misamiati.

▪ **Watoto wanapaswa kujifunza kuchukua majukumu kwa makosa yao wenyewe.** Wazazi wasikimbilie kuwasaidia.

▪ **Watoto wanapaswa kufundishwa namna ya kutumia fedha kwa busara.** Watoto hawapaswi kutumia fedha kuzidi walizo nazo, haijalishi ni posho, zawadi kutoka kwa wazazi au ujira kutokana na kazi walizozifanya. Haikubaliki kuwakopesha fedha wakati hawana ili wazilipe watakapokuwa na fedha za kutosha. Haya ni mafunzo duni. Badala yake, wanapaswa kusubiri mpaka watakapopata fedha zao wenyewe na sio kuwa na madeni. Watoto waliopata kazi za kufanya wanapaswa kujifunza namna ya kutenga fedha kwa ajili ya sadaka au akiba. Kadiri watoto watakavyokua, wazazi wanaweza kujadiliana nao namna watu wazima wanavyotunza fedha na aina ya kupanga kwa ajili ya akiba na miradi. Hii ni fursa ya kipekee kuwaelezea watoto kwamba riba imeharamishwa katika Vitabu Vitukufu na kuwafundisha katika utaratibu wa kuweka akiba katika Uislamu.

- **Wape moyo watoto watafute kazi.** Hakuna tabu kama itakuwa ni kazi ya kujitolea au kazi inayoweza kufanyika baada ya muda wa masomo au katika msimu wa kiangazi. Watoto ambao wazazi wao wanafanya biashara, kama vile; duka, hoteli, mgahawa, shamba, au sokoni, wanapaswa kuwasaidia wazazi wao katika kazi hizo tangu utotoni mwao. Watoto watajifunza kujali muda, kuwa na tabasamu kwa hali yoyote watakayokuwa nayo, na kuhakikisha kwamba kazi zao zinafanyika.

Ushauri wa ujumla

- Watoto hawapaswi kufundishwa wakiwa na njaa au wakiwa wamechoka.
- Ukosoaji ni sumu pindi unapounganishwa katika mafunzo ya watoto.
- Uwajibikaji unahitaji Uvumilivu.

Kama ilivyo katika nguvukazi ya ukweli…

Lakini wazazi hawawezi kumfukuza mtoto wao!

Tabia ya uzembe haikubaliki kabisa kazini. Wafanyakazi wote wanajua wajibu wao na wanahitajika kuyatimiza kwa muda fulani au kufutwa kazi. Ingawa wazazi hawawezi kumfuta kazi mtoto wao, wanaweza kuwapatia miongozo na kuwafundisha ili wawe wawajibikaji.

Kuna siku zingine, wakati watoto hawawezi kufanya kazi, kwa kuwa wanaweza kuwa wanatumia usiku wao nyumbani kwa rafiki zao au kuwa safarini. Hata hivyo, kama ilivyo kwa mfanyakazi wa kweli, watoto wanaweza kuomba ruhusa kwa siku moja au mbili pamoja na kwamba lazima wafikishe maombi hayo mapema. Hawawezi kuja kazini siku ya kwanza na kusema: “Nahitaji kupumzika leo kwa sababu nilikuwa katika sherehe usiku uliopita.

Unganisha Hadhi na Uwajibikaji: Mifano

Watoto wengi huamini kwamba wana haki katika chochote katika fursa walizo nazo, kama vile wazazi wao waliumbwa ili wawatumikie wao. Watoto kama hawa hupata tabu kukubali majukumu wakati wa utu uzima wao. Familia moja ina kaida ya kila mwaka. Kila mwaka, kila mtoto anapewa fursa mpya na majukumu mapya. Moja linakuwa si la kutarajiwa.Watoto hujadili na wazazi wao kuhusu machaguo yao ambayo huyachukua na kuyafanyia kazi.

Mfano 1: Binti yako amekuwa akihitaji kununuliwa paka kwa miaka mingi. Amekubali kumpakata mdogo wake mara moja kwa juma, kwa kitendo hiki, atapata fursa ya kushawishi kununuliwa paka, ingawa anapaswa kumtunza paka yeye mwenyewe. Na anapaswa kukumbushwa kwamba kama atamsusa mnyama huyo, ataondolewa!

Wazazi wanapaswa kutoa adhabu inayofaa, ambayo ina maana kwamba itawasaidia watoto kuwaokoa haraka wanapokosea. Mara nyingi wazazi huwasumbua watoto wao na baadaye kuwatuliza. Moja katika njia ambazo watoto hujifunza uwajibikaji ni kutokana na madhara ya adhabu zinazostahili. Kama madhara yake ni sahihi, itakuwa vigumu watoto kusahau wajibu wao wakati mwingine. Kwa mfano, kulipa faini ya kuegesha kimakosa ni kosa, wazazi hawatakiwi kufanya hivyo!

Mfano 2: Kijana wako alitaka kuchukua katoni ya maziwa kutoka shuleni na kuipeleka nyumbani akaisahau. Badala ya mama kukimbilia dukani yeye mwenyewe, ataandaa chakula cha usiku bila maziwa, na asubuhi ya siku ya pili, hakutakuwa na chochote cha kuweka katika mkate wake.

Mfano 3: Binti huchelewa mara nyingi kuondoka nyumbani kwenda shule jambo linalosababisha kukosa basi la shule, pamoja na juhudi za mama yake za kumuamsha kwa wakati. Hali hiyo ilimlazimu kila mara mama amsindikize kwa gari lake shuleni, akimsisitiza kuhusiana na kujali muda katika safari.

Hata hivyo, binti huyo atabadili tabia yake ikiwa mama yake akiacha kuzungumza naye na kumuacha atembee kwa miguu kwenda shuleni. Kama usalama ni mdogo, mama anapaswa kumueleza binti yake kwamba atampeleka baadaye, akimaliza kazi zake. Binti hatapendezwa na kuchelewa kufika shuleni wakati vipindi vimekwishaanza, na hali hii itamfanya arekebishe makosa yake kwani makosa yanaweza kuwa fursa ya kujifunza. Hakuna sababu ya wazazi kukasirishwa na kufeli kwa watoto wao, kwa kuwa kukaripia mara nyingi kunashindwa kuwa suluhisho na badala yake kunaweza kuongeza tatizo. Badala yake, wanapaswa kutafuta njia ya kuboresha hali hiyo, kwa kuwa watoto watajifunza zaidi kuliko katika kukaripia, na wazazi watajisikia vizuri pia.

Mfano 4: Ni zamu ya kijana wa kiume kuandaa chakula cha usiku. Anasahau, anachelewa kurudi nyumbani kwa kucheza mpira, kufika nyumbani akiwa amechelewa. Badala ya kumgombeza, au kuanza chakula cha usiku yeye mwenyewe, mama anaweza kujaribu kusema, “Tumepata tatizo sasa. Unadhani tunaweza kufanya nini sasa katika hili?” Anaweza kuamua

kuchemsha mayai na mikate, na kutengeneza chakula cha haraka, au akubali kukubaliana na mwenzake mwenye zamu ya usiku katika siku inayofuata. Kufanya hivyo ni muhimu zaidi kuliko kuweka chakula mezani, ataweza kuwajibika kutekeleza majukumu yake kwa umakini.

Watoto wengine hujengeka kwa kuwa na tabia ya kuwalaumu watu wengine au mazingira yaliyosababisha wafanye makosa. Hata hivyo, hii inaweza kuwanyima fursa ya kuwa wazuri baadaye. Wazazi wanaweza kufikiria mazingira ambayo, kama watoto, wanaweza kukataa kuwajibika. Mara nyingi, hali kama hizi, huwakatisha tamaa sana wazazi wao juu yao kwa sababu ya kutowajibika kwao.

Watoto wanaweza kujisikia kwamba wazazi wao watawaeleza kila mara kitu cha kufanya. Pengine ni kwa sababu watoto hawakuchukua hatua za kukubali kuwajibika. Watoto wanapaswa kuchukua hatua na kubadilisha kilicho hasi kuwa chanya, na kisha wazazi wataacha kuwaelekeza cha kufanya.

Qur'an Tukufu inaelezea vitendo na madhara yake:

> Basi anaye tenda chembe ya wema, atauona! Na anaye tenda chembe ya uovu atauona! (Qur'an 99:7-8).

Uwajibikaji ni kanuni ya msingi ambayo tunapaswa kuifundisha kwa watoto wetu. Katika sura inayofuata, tumetamalaki na dhana ya uhuru, ambayo ni muhimu katika kujifunza uwajibikaji.

Waagize watoto wako kufanya wajibu wao katika kazi za nyumbani na kuwafanya wawajibike. Wanaweza kutopendezwa kama hawatafanikiwa, lakini watakwisha kabisa kama hawatajaribu.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 57: MWENYEZI MUNGU ANAYATAZAMA MAKUNDI YOTE

Waruhusu watoto wasome visa hivi kisha kila mmoja atoe maoni yake.

a) Katika kambi ya kiangazi ya watoto, katika mstari wa kupata chakula cha usiku, kuna alama inayosema “Chukua tufaa moja tu, Mwenyezi Mungu anakutazama.”Mwishoni mwa mstari kulikuwa na vyakula ambavyo havikuandikwa, mtoto mmoja aliandika alama moja na kuiweka katika vyakula hivyo, “Chukua vingi utakavyoweza kwani Mwenyezi Mungu anajishughulisha na kutazama matufaa.” (MCHUNGAJI PETER MARTIN KATIKA UFUNGUZI WA RAMADHAN WA IIIT, OKTOBA, 2007).

b) Wakati Omar Ibn Khattab alipokuwa Khalifa na akamuona mfanyabiashara akifanya ulaghai, alimueleza “mtoa matangazo wake” kutangaza rasmi, “Yeyote anayefanya ulaghai si miongoni mwetu. Ni kinyume cha sheria kuchanganya maji na maziwa kabla ya kuyauza.”

   Baadaye, majadiliano yafuatayo yalitokea katika nyumba moja huko Madinah:

Mama: Binti yangu, amka na uongeze maji katika maziwa tupate fedha nyingi.

Binti (kwa upole): Hukujua kama mtangazaji wa Omar amesema hakuna maji yanayopaswa kuchanganywa katika maziwa?

Mama: Fanya ninachokwambia, si Omar wala mtangazaji wake watakaotuona!

Binti: Nawezaji kumtii mtawala hadharani na kumkhalifu faraghani? Kama Omar hatuoni, Bwana wa Omar anatuona! Wakati wote!

ZOEZI 58: MAFUNZO KATIKA AJALI NA UWAJIBIKAJI

Jibu maswali yafuatayo, kisha fikiri kuhusu maoni yanayofuata.

Kijana wako wa kiume wa miaka 12 anacheza mpira wa magongo katika yadi ya nyuma, anapiga mpira na kuvunja dirisha la jirani yako, wewe sasa:

a) Wapigie simu majirani zako kuwaeleza kwamba utalipia dirisha lililovunjika, kisha, muadhibu mwanao.

b) Mwambie kijana wako aende mwenyewe kwa majirani zako na kuwaeleza kwamba kwa bahati mbaya amelivunja dirisha na kwamba atalilipa. Unamlipia na kumkata katika posho yake.

c) Mwambie kijana wako aende mwenyewe kwa majirani zako na kukiri kwamba amevunja dirisha kwa bahati mbaya na kwamba atalipia kulikarabati kutokana na akiba zake (kama zitakuwepo) au atatafuta fedha kulipa gharama yote kwa ajili ya ukarabati.

MAONI: Huu ni mfano mzuri kwa ajili ya kijana wako katika kumfundisha kukubali kuwajibika kwa vitendo vyake bila kuwa na hasira au kuwa na ulazima wa kumuadhibu mtoto, kama utakuwa umejibu:

a) Utakapomuita jirani yako, mwanao hatajifunza chochote, isipokuwa kwamba yupo mtu wa kumsaidia katika makosa yake. Kwa nini umuadhibu? Ni bahati mbaya.

b) Hatua nzuri ya kwanza, yaani, kumtuma mtoto akamtaarifu jirani kuhusu kuharibika kwa dirisha.

c) Safi sana! Sasa mwanao anabeba majukumu yote katika vitendo vyake. Njia hii inafaa zaidi kuliko (b).

na
weza

19

SURA YA KUMI NA TISA

- KUFUNDISHA KUJITEGEMEA

SURA YA KUMI NA TISA **462**

Kufundisha kujitegemea **462**

Makuzi binafsi ndani ya Amerika 464
Kuna kejeli za kutisha kama utaifanyia kazi nyanja hii 464
Je, tunamaanisha kujitegemea ama kutegemeana? 466
Umri –kipindi cha kukamilisha majukumu 468
Naweza fanya mwenyewe 468
Waache watoto watafute suluhu wao wenyewe 469
Hofu ya kutengana: kukabiliana na tabia ya ung'ang'anizi. 470
Ujana – Hali halisi 471
Athari za mitindo ya malezi 473
Ujuzi katika Kumuandaa Mtoto Kujitegemea 476
Vidokezo kwa wazazi 481
Ushauri na Uhuru: Binti na Mama yake 483
Je, unalazimisha uvaaji hijabu kwa binti yako? 485
Kama wazazi hawawapendi marafiki wa watoto zao. 486
Kuwasaidia watoto kufanya maamuzi huwajengea kujitegemea 486
Hatua za kufuata katika kufanya maamuzi 487
Kazi za Kufanya

Makuzi binafsi ndani ya Amerika

Wazazi ndani ya Amerika hulalamika ya kwamba watoto wengi huwa tegemezi kwa wazazi wao kwa muda mrefu, Amerika kama jamii imefeli kuandaa watoto wao kuishi nje ya nyumbani na kuweza kujitegemea.

Kuna kejeli za kutisha kama utaifanyia kazi nyanja hii

Ingawa katika zama za leo wazazi wanahitaji watoto wao kuwa na furaha, lakini njia zinazotumika ni kuwaandaa watoto kutokuwa na furaha. Watoto hawajifunzi namna bora ya kutumia uhuru wao, kwa sababu hawategemei kuwa hivyo. Wazazi wanatumia kila aina ya gharama za fedha na kihisia kwa ustawi wa watoto wao. Wako tayari kujitolea, wanajaribu kufanya kazi nzuri ili kuonesha ile ghera waliyonayo kwa ajili ya kuwasaidia watoto wao. Wazazi bora hutambuliwa kwa mambo makubwa mawili: kwa yale wayafanyayo kwa watoto wao, na kwa yale wanayowapa watoto wao, kikawaida hufanya kila waliwezalo kuhakikisha watoto wao wanapata kila kitu. Wanapamba vyumba vya watoto wao kwa rangi maridhawa, wanawanunulia kila aina ya kifaa kinachoweza kuwasaidia

katika taaluma yao, na wanawapa watoto wao kila aina ya kizuri wanacho kihitaji. Wanafanya kwa watoto wao yale yote

ambayo wameshauriwa na wataalamu wa masuala hayo ya malezi. Wanawasajili watoto wao katika kumbi za kufanyia mazoezi, huwapeleka shule ghali na kuwasajili katika timu za watoto wadogo wa miaka minne. Wanajitolea muda wao, urafiki wao na vitu vya maslahi binafsi na hata mahusiano yao ya ndani. Wanawaruhusu watoto wao waingingilie chochote kuhusu wao ikiwa ni sehemu ya wao kujifunza.

Zaidi ya yote wanatumia kila aina ya fursa kujenga heshima ya watoto wao (kwa kuwasifu juu ya utanashati, umadhubuti, uwezo, akili, na muonekano wao mzuri). Wanawaandalia sherehe maalumu za kuzaliwa kama vile ni watoto wa kimalkia au kifalme. Hata ikitokea mtoto amepotoka kiasi gani mzazi huendelea kumpatia zawadi na kumtekelezea kila aina ya hitajio lake. Wazazi hawa hawapendi kuwahuzunisha watoto wao kwa namna yoyote ile, ghafla jambo hili husababisha mahangaiko. Ukweli ni kwamba walilo likosa wazazi ni kudhani ya kwamba vijana wao watabaki chini ya milki ya wazazi wao na wazazi kutowaruhusu kuanza maisha ya kujitegemea.

Wazazi wengi wa kizazi cha watoto wa sasa ndani ya Amerika walilelewa tofauti sana.Katika kipindi chao hicho, watoto walilelewa katika namna ya kuchanganyika wao kwa wao na mchanganyiko wa wazazi ilikuwa ni vivyohivyo. Baadhi ya wazazi walifikia hatua ya kuwaambia watoto zao wasiwasumbue labda ikifika mahali mtu ameumizwa na anavuja damu, kipindi hicho michezo ilikuwa baada ya vipindi vya darasani na si siku za mwisho wa wiki, wazazi waliwaacha vijana wao wacheze wenyewe. Watoto waliachwa shuleni chini ya uangalizi wa walimu wao. Kimsingi, wazazi hawakuwa na hofu sana juu ya watoto wao katika kufurahika kwao, bali walikuwa na hofu juu ya furaha zao wenyewe.

Kama wazazi wa sasa wangekuwa ni watoto ndani ya Jamhuri ya Amerika, familia zingekuwa kubwa, nyumba zingekuwa ndogo na huduma zingekuwa na mipaka maalumu. Vijana wengi wanafanya kazi

Je tunamaanisha kujitegemea ama kutegemeana?

Kufundisha kujitegemea kwa watoto haimaanishi kuzuia mahusiano ya jumla na wazazi. Ni lazima pawepo na uhuru pamoja na kutegemeana baina ya wanafamilia wote

za muda mfupi wakati wakiendelea na masomo, ili kumudu gharama zao za maisha. Wanapata magari kama wataweza kuyalipia wao wenyewe. Wote wazazi na watoto wanachukulia ya kwamba pindi mtoto anapohitimu elimu ya juu ama chuo na akapata ajira, basi ataweza kujikimu kwa kipato akipatacho, dhana hiyo ndiyo inasababisha watoto kujitegemea.

Wazazi wa leo wapo makini dhidi ya watoto wao kuhakikisha wanapata furaha, na kusahau kuwafundisha wawe watoto wema. Haitoshi kuweka msisitizo kuwa watu asilia tunaofikiria watu wengine kuliko sisi wenyewe. Watoto ambao wanapendwa sana, huwa si wepesi kwa shida za wenzao na hujitazama wao kwanza.Watoto waliotengwa huwa na marafiki wabaya na kuwa na wenza wabaya pia. Watoto hawa wakikua jukumu la mzazi katika malezi linakuwa bado linamuhusu. Kunakuwa na hitajio kubwa na mzazi hasemi hapana au anaweza kukubali lakini asisimamie, wazazi wa namna hiyo wanahitaji watoto wao wawe na furaha pasi na kujali inapatikanaje furaha hiyo. Wazazi hawa pia hudhani ya kwamba kuwawezesha ama kuwapa zaidi watoto wao ndio msingi wa furaha zao. Wasichojua ni kwamba kufanya hivyo ndio kuwazorotesha na kuwafanya wawe wazazi tegemezi zaidi kwa baadaye na kuongezeka maradufu. Wazazi wa aina hiyo wamekuwa wagonjwa na wamechoka kabisa na hawajui nini cha kufanya.

Hali hii haiwezi kuzuilika kwa namna yeyote kwa familia nyingi. Kuna watoto wengi wa Kimarekani katika kila hatua ya kuhitajia kipato hudhani kwamba wazazi wao wapo pale kama chanzo cha kipato chao. Wazazi wengi wanaishi maisha ya kawaida wakati huo huo wakichangia zaidi katika matumizi ya watoto wao. Wanachojifunza watoto ni matumizi mabaya na kuendelea kuwa tegemezi.

Ikitokea mtoto amepata mafanikio ya kutosha husababisha wazazi kuingilia kati mafanikio yake. Kizingiti muhimu kati yake na wengine hujitokeza na uwezo wa mtoto kujifunza hudumaa. Msaada stahiki wa malezi huhitajika na ni muhimu. Hata ikitokea amepata tatizo la mwili ama akili, ni kosa kumpa msaada mkubwa sana na kumshughulikia kijana ama binti kama anavyoshughulikiwa mtoto mchanga. Wakati mwingine mtoto huelekezwa zaidi mpaka inamsababisha kuwa na hofu katika kufanya maamuzi, kutoka katika hali ya “kutojua kipi naweza vaa” mpaka hali ya “je naweza kufanya kazi hii?” au “naweza kumuoa/kuolewa na huyu?” Wale ambao wamepewa kupita kiasi wanafikia utu uzima wakiwa wanawategemea wazazi wao katika kutekeleza wajibu wao.

Endeleza kujitegemea binafsi na kujiamini.
Na si kuwa tegemezi na kuhofia kufanya maamuzi

KISA: Kadhia ya watoto walizi

Kwa mujibu wa mwanasaikolojia Jeffry Simpson: ukikosa ulinzi salama katika umri wa mwaka mmoja, kuna kila dalili ya kutokea tatizo la kihisia ukiwa katika mahusiano na mwenza wako miaka 21 ijayo.(Gazeti la Washington Post, 2007)

Simpson na wataalamu wenzake walifanya uchunguzi kwa muda wa zaidi ya robo karne, walianza kuwatazama watoto walivyokuwa wadogo, mama zao waliwaacha katika chumba cha maabara na waliombwa wawaache kwa utaratibu mzuri, watoto wale walibaki wanasikitika. Wazazi wao waliporudi baadhi ya watoto waliwang'ang'ania mama zao, kwa kuhisi utulivu na baada ya muda mfupi walinyamaza, baadhi hawakunyamaza hata baada ya kubembelezwa kwa muda, na kundi la tatu walikataa kabisa kurudi kwa mama zao.

Baadhi ya wazazi wa kike(akina mama) huwa wanapanga kufanya mambo yasiyowezekana, baadhi ya akina mama huamua kuwakinga watoto wao wapendwa kwa kila mtu ama kwa kila kitu ambacho, kinaweza waletea madhara au kuwakatisha tamaa, hili ni jambo lisilowezekana.

Mtoto aliye salama anapata funzo ya kwamba “wazazi wangu wako tayari kunisimamia” na anajifunza kuwakimbilia wengine. Mtoto asiye salama anapata funzo ya kwamba, “wazazi wangu wananipuuza” au “wazazi wangu hawanijali” au lazima nigome ili nipate uangalizi”. Mtoto anapokosa usalama katika kipindi cha umri wa mwaka mmoja anaweza kukua akiwa dhaifu na kuwa tegemezi. Watoto wanaopata uangalizi mzuri wanakua wakiwa salama. Watoto waliotengwa ama kupuuzwa wanakosa usalama, na baadaye husababisha kutoweza kujitegemea. Watoto wanaolia na kukimbilia kwa wazazi wao ili kupata msaada ni lazima wakidhiwe. Mara tu wapatapo faraja wanaendelea na shughuli zao za utafutaji. Vivyo hivyo kwa wapenzi wa dhati wanakuwa wanategemeana ikitokea mahitajio yao ya kihisia wametoshelezana. Ni rahisi sana kwa watu kukubali kubeba majukumu na changamoto ikiwa wanaamini ya kuwa nyuma yao yupo anayeweza kuwasaidia na kuwafariji pindi mambo yatakapokwenda kombo.

Kadri mtu anavyokuwa na uhakika wa usalama wake na hakika ya watu wa kumpa faraja ndivyo anavyoweza kukabiliana na majukumu.

Kwa hakika wanaoweza kutegemeana ni wale ambao wanajiamini vya kutosha kuwakabili watu wengine ili wasaidiane nao na kuweza kutoa msaada kwa wengine.

Umri –kipindi cha kukamilisha majukumu

Fikra za vijana wadogo ni kwamba wao wenyewe wanao uwezo wa kujitegemea ikiwa wazazi wao watawafundisha namna ya kujitegemea. Watoto wanajifunza namna ya kutumia uhuru ikiwa wazazi wanawaonesha upendo na kuwasaidia. Kumfariji mtoto katika uchunguzi na udadisi humfundisha mtoto ujuzi mbalimbali na kumpa mtoto uwezo wa kufanya uchaguzi. Shauku ya mtoto juu ya uchunguzi wake itatoa taarifa kwa mtoto juu ya thamani ya kile akifanyacho.

Naweza fanya mwenyewe

Kazi binafsi zenye usimamizi husababisha kujitegemea. Jitihada za mtoto mchanga za kunyanyua na kuchezesha kichwa chake, kuzungusha shingo au kukaa ni hatua muhimu kuelekea kujitegemea. Malezi bora, upendo na huruma husaidia katika kufikia malengo.

Mazingira salama yana mchango mkubwa katika maendeleo ya makuzi ya mtoto. Mtoto mdadisi ana maamuzi mepesi juu ya usalama wake. Kujitegemea kunaweza kuimarishwa kwa mtoto kupewa machaguo madogomadogo. Mtoto apewe uangalizi wenye mipaka juu ya maisha yake, uangalizi kama vile hadithi ipi asome, mchezo upi acheze, au nguo ipi avae. Watoto ambao bado hawajafikia umri wa kwenda shule wana uwezo mkubwa wa kueleza hisia zao, fikra zao na mahitaji yao na wako tayari kupiga hatua kubwa kuelekea kujitegemea. Hamasisha watoto kupanga vizuri nguo, vifaa vyao vya kuchezea, kuweka vizuri meza pamoja na kusaidia katika maandalizi ya chakula. Jambo hili linaimarisha hali ya ustadi na kujitegemea. Mara tu mtoto afikiapo umri wa kwenda shule huwa kuna fursa nyingi za kumsaidia mtoto kuelekea kujitegemea. Maamuzi kuhusu marafiki, shughuli za shule na michezo ni machaguo muhimu katika maisha ya kila siku.

Maamuzi kuhusu fedha ni muhimu kufundishwa kwa vijana ili kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi (mfano mzuri unaweza kumpa jukumu la kuwa mhazini wa familia au kumpa jukumu la kusimamia matumizi ya kila wiki). Ni muhimu kuheshimu machaguo ya watoto kadri iwezekanavyo. Hii ni kwa kuwaonesha kuwa tunajali hisia zao na kutambua yale majukumu madogomadogo wanayoyatekeleza. Wazazi wawasaidie watoto katika kujitawala kwao katika yale mambo yanayowazunguka hapa ulimwenguni hii itakuwa ni namna nzuri ya kuwaandaa watoto kupata ustawi mzuri na kujitegemea katika maisha.

Waache watoto watafute suluhu wao wenyewe

Watoto wanataka kujaribu vitu wao wenyewe. Unaweza ukaona ni vigumu kuendana na hali ya watoto wako kubadilika kutoka kwenye hali ya kutaka kufanya wenyewe kwenda kwenye hali ya kukung'ang'nia na kuogopa kukuachia.

"Fanya kila uwezalo kujenga hisia za ulinzi kwa watoto kwa kuwapa upendo wenye dhamira ya dhati"

Zifuatazo ni dondoo zinazosaidia katika malezi ya watoto

- Utovu wa nidhamu na kukosa utii (kukataa kukubaliana na matakwa ya wakubwa) ni sehemu ya hitajio la watoto katika kupata uhuru.
- Kufuata matakwa ya mtoto kutaondoa maumivu ya moyo. Kama wanataka kuwang'ang'nia wazazi wao basi na waachwe wafanye hivyo. Kama wanataka kufanya vitu watakavyo wao basi wazazi wanatakiwa kukubaliana nao (kama tu kuna sababu ya msingi ya kufanya hivyo)
- Kumkanya mtoto ni njia nzuri sana. Pale ambapo mtoto anakataa kufuata maelekezo –vivyo hivyo watoto wanaweza kuruhusiwa kuchagua wanachotaka kukifanya na kupewa mwongozo na uangalizi.
- Yapaswa kuepuka amri na kauli za mwisho kwani zinachochea mabishano na kushindana kinguvu na kuleta vita isiyoisha kwa watoto wengi. Kufundisha kwa kuongoza kuna manufaa sana. Watoto huchukia aina yeyote ya kuamrishwa na wazazi. Hupendelea kula wenyewe (bila kulishwa) kuvaa wao wenyewe bila msaada wa wazazi, tabia hii ni ya kawaida japokuwa huonekana kuwakasirisha wazazi.

Hofu ya kutengana, kukabiliana na tabia ya ung'ang'anizi

Wazazi ndio watu wa muhimu zaidi kwa watoto wao ndio maana watoto wadogo walio wengi huogopa wageni na huogopa kutenganishwa na familia zao, hali hii ni kawaida. Kuishi mwaka au miaka miwili pamoja na wazazi na kuwa nao karibu huwafanya watoto wasikubali kutowaona wazazi wao! utengano baina ya watoto na wazazi ni jambo gumu kwa pande zote mbili. Zifuatazo ni dondoo muhimu kukabiliana na kutengana.

- Wazazi wanatakiwa kufanya kila liwezekanalo kujenga hisia ya ulinzi kwa kuwaonesha upendo na uangalizi kwa kadri iwezekanavyo au kucheza nao. Kujenga hisia za ulinzi inahitaji uvumilivu na inatakiwa iwe ni tabia endelevu mpaka pale mtoto atakapojisikia yupo tayari kuwa huru.
- Utengano unatakiwa uwe wa muda mfupi pale inapobidi kumuacha mtoto hasa kwa hatua za mwanzoni na inahitaji muda wa kutosha kwa mtoto kumfahamu mlezi wake mpya.
- Ni muhimu kumhakikishia mtoto hata kwa kutengana naye kwa muda mfupi kama vile kwenda shule ya chekechea wakati wa asubuhi, inaweza kuwa ngumu kwa mtoto

mwenye hisia kali. Wazazi wanapaswa kutenga muda kuzungumza na mtoto wao kiundani kuhusu mabadiliko ya malezi yao na kuwahikikishia kuwa watarudi.

- Hakikisha muachano hauwi wa namna ya kuwatoroka watoto.
- Wazazi hawapaswi kuwatoroka watoto wao, yaani kuondoka bila ya kuwaaga watoto wao. Japokuwa kuagana huumiza, lakini humuondoa mtoto hofu kuliko kuondoka bila kuaga. Ni muhimu kuwa na furaha na kuepuka kuondoka kwa muda mrefu, kwa sababu huonesha mfadhaiko na husababisha mtoto kujisikia muhitaji na mwenye kukosa kitu.
- "Mtoto king'ang'anizi." Pale mtoto atakapoonesha kumng'ang'ania mzazi hata katika shughuli za nyumbani za kila siku au kwenda sokoni, mzazi anapaswa kuwa mpole na kuendelea na shughuli zake kama kawaida. Japokuwa inaweza kuwa ngumu kupika au kuongea na mtu wakati mtoto anamng'ang'ania mzazi katika hali ya namna hiyo, mwisho mtoto atajisikia huru na atamuachia mzazi wake aendelee na shughuli zake. Ni kawaida kwa wazazi kujisikia huzuni pale mtoto wao anapotoka hatua moja ya ukuaji kwenda hatua nyingine.

Ujana – Hali halisi

Watoto wadogo uhitaji kuoneshwa unawajali katika njia ambayo ni ya kulindwa na kuongozwa kwani wanauzoefu na ujuzi mdogo sana kutokana na udogo wao. Watoto wadogo wanatakiwa kulindwa na kusaidiwa muda wote. Muda mwingine wazazi hawawezi kuelezea vizuri kwa nini wanafanya baadhi ya mambo, wanahitaji tu watoto wao wafanye kama wanavyotaka wao.

Kwa vijana ni tofauti. Badala ya wazazi kuwa waamrishaji wazazi wanapaswa kuwa na ujuzi wa kukubaliana na kufikia maafikiano. Vijana wanatakiwa kujifunza namna ya kuishi wao wenyewe; wataondoka nyumbani hivi karibuni na watatakiwa kuishi bila msaada wa mama wala baba. Ni jukumu la wazazi kutowang'ang'ania watoto waliowapenda na kuwadekeza, lakini wanapaswa kuwasaidia kujitegemea. Wazazi wanatakiwa kubadilika kutoka kwenye uangalizi wa karibu kwenda kwenye uangalizi hafifu na wa mbali kwa watoto wao. Vijana wanatakiwa kujifunza namna ya kuwa na utegemezi hafifu kwa wazazi. Hili ni gumu kama hakuna maelewano mazuri baina ya wazazi na mtoto.Vijana wanakuwa wavivu pale mama anapokuwa kama mtumishi wa nyumbani. Vijana hawa hawawezi kujitegemea na hukua wakitegemea kuna mtu wa kuwafanyia kila kitu.

Kitu kigumu kwa mama wa nyumbani kugundua ni kuwa pamoja na nia yake njema ya kufanya kazi zake hizo za nyumbani, inaweza sababisha vijana kumchukia na kufadhaishwa naye badala ya kumpenda na kumshukuru kama alivyotarajia. Kumchukia huko hutokana na watoto hao kukua wakihisi kuwa wanaweza fanya chochote bila kufuatiliwa kama mipaka haijawekwa wazi kwa vijana wanaweza wasiwe na uhakika juu ya mambo wanayoruhusiwa kuyafanya na wasivuke mipaka.

Wazazi wengine ni wakorofi na uhitaji kuwa na amri katika kila hali. Mtazamo huu husababisha ugomvi na vijana ambao wanajaribu kujifunza kuwa huru. Ni jukumu la wazazi kuwasaidia kuweza kuishi maisha yao wenyewe. Wazazi wao wenyewe watapoteza baadhi ya amri juu yao. Pindi wazazi wanapojadili mambo pamoja na marafiki zao mara nyingi hufika mahala wakahitilafiana kwa sababu fikra zao haziko sawasawa. Wazazi ni lazima wajifunze kuwaruhusu watoto wao pia kuwa huru katika tofauti za kimtazamo. Hawawezi kuzitawala fikra za vijana wao wanaweza tu kuwapa motisha ya kuwa na mtazamo mwingine. Wazazi hawapaswi kuwalazimisha watoto wao. Kuna wazazi watapata mshtuko itawabidi waondokane na mshtuko huo. Kama wataona mambo yamekuwa kinyume na matarajio yao basi waishi nayo vivyo hivyo (wakubaliane na hali hiyo). Kikawaida matokeo haya ni matatizo ya wazazi na si watoto.

Kwa baadhi ya akina baba wanawatengenezea mazingira mabinti zao ya kupoteza matumaini kwa kufanya maamuzi ambayo ni magumu. Wanawapa ulinzi uliopituka, hali inayosababisha mabinti kuwa tegemezi mno. Kwa msingi huo binti anashindwa kufanya maamuzi yake mwenyewe. Hawezi kufuatilia kupata leseni mpya baada ya awali kuisha muda, au kujaza fomu ya bima ya gari, au kufungua Akaunti ya benki, au kuendesha gari kwa muda wa saa mbili, mzazi asiruhusu hali hii kutokea, anaweza kumpa usaidizi kama binti yake akiwa ni mtoto, anaweza mpa ruhusa kulala kwa rafiki yake au kumpeleka katika kambi ya wiki moja chini ya uangalizi wa mtu anayemuamini anaweza kumsaidia.

Maana mojawapo ya kuwa huru!

Kuwa huru ni kuwa na machaguzi mengi, au kuwa na njia mbadala ambayo wazazi humpa mtoto.

Hata hivyo kuna tatizo kubwa linaloendelea kukua la Ukimwi, dawa za kulevya na uhalifu. Hatari kwa watoto ni nyingi sana kwa sasa na kujifunza kutokana na makosa ya wengine" kunaweza kuwa ni gharama kubwa sana,"nini kinampata mwanangu?" na "kwanini hukui tuu?" ni kauli za baadhi ya wazazi. Kipindi cha kubaleghe ni kipindi ambacho wazazi na watoto Kutafsiri upya mahusiano yao vizuri na ni muda ambao watu wazima wanapaswa kuwapa mwongozo na faraja vijana ambao watauheshimu na kuukumbuka.

Wazazi wengi wamegundua kuwa hawana sauti juu ya yale wanayofanya watoto wao hasa pale ambapo athari/matokeo ya yale wanayofanya yanapokuwa makubwa, wazazi hawana budi kukubali kwamba, watoto hawatahitaji wazazi wao kuwa kama watu wa kuazimwa au wasimamizi tena bali washauri wao ambao watatoa mwongozo na ushawishi kama mzazi atang'nga'nia kumuamanisha mtoto basi kutakuwa na mgogoro kati yao usioisha.

Ingawa vijana wanafahamika kwa kuwaambia wazazi wao wawaache wajitegemee wenyewe.Vijana waliopevuka Zaidi wanakubali kwamba vijana wengi waliokwenye baleghe wanahitaji kujua japo kwa siri kwamba wazazi wao wanawajali.

Kwa mfano, japokuwa Jimenez alikulia sehemu ambayo kulikuwa na vijiwe vya wahuni wengi, wazazi wake walimuonya juu ya kushirikiana na wahuni na alisema "Nilijua wazazi wangu wananijali, hivyo sikuhitaji aina nyingine ya familia ambayo huenda ningeipata kutoka kwa wale wahuni, na wazazi wangu walinifundisha jinsi ya kufikiri vizuri mimi mwenyewe na kuwa na mawazo mazuri na si kufuata watu wengine"

Uaminifu kwa watoto + mwongozo wa wazazi →kujitawala, Uwajibikaji

Athari za mitindo ya malezi: Malezi ya kimamlaka/ kujitawala dhidi ya malezi ya kuongozwa au kutumia nguvu

Malezi ya kimamlaka/kujitawala ni aina ya malezi yanayomkuza mtoto na kuweza kujitegemea hali malezi ya kutumia nguvu inamaanisha malezi yanayopelekea mtoto kuwa tegemezi. Japokuwa watu wazima wengi, mara kwa mara, hupata wakati mgumu katika kufanya maamuzi, kwa baadhi hili ni tataizo sugu ambalo huleta madhara kila siku kwenye maisha yao. Kuamua labda kwenda kula chakula cha jioni, kitu gani cha kununua au kwa kiwango gani cha ubora uchukue inaweza

> Vijana ambao ni wawajibikaji na waliohuru katika maisha yao si rahisi kuwakuta katika mambo ya hatari.

kuwa ni tukio linaloumiza, kwa baadhi linaonekana mara zote kuwa ni vyema kufuata mawazo ya watu wengine kuliko kufuata au kutengeneza mawazo yao wenyewe.

Kuna aina mbili za wasiwasi ambao humpata mtoto aliyepewa malezi ya kutumia nguvu, ya kwanza ni kuogopa kufeli. Kwa watu ambao wanaogopa kufanya maamuzi yao wenyewe ni wale ambao tangu utotoni mwao walikuwa na mtu wa

kuwaamulia kila kitu. Mara nyingi walikuwa na mtu aliyekuwa tayari kuwalinda kutokana na uwezekano wowote wa kushindwa au ilikuwa rahisi kufanyiwa maamuzi ya haraka na hao watu.

Watoto waliolelewa kwa kutumia njia ya kuongozwa kwa nguvu husema "kwa nini nishindwe wakati kuna mtu atakayefanya kwa ajili yangu?" watoto hawa hukaa wakiwa na uwezo mdogo wa kufikiri na hukwepa kufanya maamuzi, kwa kuongezea, kutokana na kulindwa ili wasishindwe, huwafanya kukosa hisia nzuri zinazoambatana na maamuzi yenye mafanikio.

Hofu ya pili ni hofu ya kukataliwa watoto waliokuzwa kuwa tegemezi ambao mara nyingi hutokana na malezi ya kutumia nguvu, huwa wanahitaji kila kitu akubali baba na mama japokuwa kwa miaka yao ya mwanzo jambo hili ni zuri na linapendwa lakini hatimaye uwezo wa mtoto wa kujikagua na kujikubali hupotea. Pale uwezo wa mtoto wa kujikubali unapokuwa dhaifu, watabadili ule uhitaji wa kukubaliwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa watu wengine katika maisha. Mtazamo wao waweza kuwa "kwa kuwa kufanya maamuzi yasiyosahihi kutasababisha kutokubalidilika na kukataliwa ni bora nibaki tegemezi"

Kwa upande mwingine, wazazi wanaolea watoto kwa kutumia njia ya kimamlaka/kujitawala, huwafundisha watoto wao busara ya namna ya kupambana na kufeli na kukataliwa. Wakati huo huo huwasaidia juu ya namna ya kukabiliana na athari za kitaaluma, ambalo ni jambo muhimu katika kufanya maamuzi mazuri. Kwa kuwatia moyo watoto juu ya suala la kujitegemea, wazazi huwapa watoto fursa ya kujifunza na kufanikiwa kwa kuwapa nafasi ya uhakika juu ya kufeli. Ule msemo wa "Nioneshe mafanikio ili nikuonesha kushindwa" inamaanisha kwamba mafanikio mengi huja baada ya kushindwa

Mtoto aliyelelewa kwa malezi ya kutumia nguvu Anaweza akawa na matatizo na mke/mume wake (mwenzawake) kwa shauku ya hali ya juu au kwa malumbano ya hali ya juu.

Matokeo ya kushindwa. Watoto watajifunza kutoka kwenye makosa hayo na kutathmini kipi kimeenda vibaya, na kuamua nini cha kuepuka wakati ujao na kujaribu tena. Andaa mwongozo, lakini epuka kuchanganya baina ya mabadiliko na kutokuwa na msimamo. Kwa kuwa msimamo unakuza usalama, uhakika na uelewa, wa chanzo na matukio, ni sifa muhimu ya malezi. Jambo la msingi ni kuwa tayari na kukubali mabadiliko na hiyo ni alama ya kuonesha ni mzazi mwenye mamlaka katika mambo yanayomaanisha usawa na ukweli katika kufanya tathmini ya maamuzi yanayohusiana na habari mpya itakayoonekana. Mwongozo uliowekwa na wazazi wenye mamlaka wakati mwingine hubadilika endapo kutakuwa na sababu za msingi.

Ugumu kwa upande mwingine ni kukataa kubadilika hata kama mambo mapya yanakuhitaji ubadilike. Ujumbe ambao watoto hupokea kutoka kwa wazazi wenye kutumia nguvu ni kwamba “mimi ni mzazi wako” au “fanya kama ninavyosema (bila ya kipingamizi). Hatimaye, watoto hufikia hatua ya kuchanganyikiwa itakayosababisha kukiuka taratibu za wazazi, hali inayosababisha watoto kuanza kufanya mambo kwa “namna watakavyo na wapendavyo” bila ya kufikiria athari na matokeo yatakayotokea, kwa sababu hawajajifunza jinsi ya kuendea mapungufu , makatazo na matukio katika kutatua migogoro, hali itakayopelekea kufanya makosa zaidi ambayo, baadaye hawataweza kumudu athari yake wala matokeo yasiyoepukika ambayo hupelekea kujiadhibu wenyewe.

Tunaona alama ya mambo haya kupitia jamii za leo kwa njia ya taabu na shida aipatayo mwanadamu.

Malezi ya kutumia nguvu husababisha matokeo mengi yasiyokusudiwa na kwamba baadhi ya watoto wanajibizana na wazazi wao kwa njia isiyoridhisha na watoto wanakuwa ni watu wasiosadiki chochote kutoka kwa mtu mwingine yeyote. Hali hii huendelea mpaka kwenye mahusiano ya kindoa ambayo hupelekea mmoja wa wanandoa kuhitaji kuongozwa na kutawaliwa jambo linasababisha ndoa hiyo kuwa na mahusiano yasiyoeleweka ambayo mara kwa mara huishia kwenye maumivu na huzuni.

Ujuzi katika Kumuandaa Mtoto Kujitegemea

- Mambo yanayohusiana na makundi maovu, dawa za kulevya au ngono husababisha hatari ya moja kwa moja na ni matokeo yanayosababisha mwisho mbaya. Hatari hizo wakati mwingine huchochea wazazi kuwa viongozi wabaya badala ya kuwa washauri. Jadiliana na watoto wako juu ya mambo hayo na uwaamini.

- Liz, kijana ambaye amekulia California alisema alikubali ukweli kwamba wazazi wake walijihusisha kwa uwazi na maswali yoyote aliyokuwa nayo kuhusu ngono au dawa za kulevya. Walitambua kwamba watoto walijaribu vitu vipya na punde walimpa taarifa za msingi kuhusu kujiweka mbali na ngono na dawa za kulevya. Wanafunzi wenzake ambao kwa kawaida hawakuwa na mjadala pamoja na wazazi wao juu ya masuala hayo, walijihusisha na unywaji pombe na kuwaghilibu wazazi wao.

- Kuwahamasisha watoto kujizoesha kufanya maamuzi yao wao wenyewe, ni busara zaidi kuliko kuwafanyia maamuzi, bila kujali uelewa mzuri walionao baba au mama. Kwa kijana ambaye anafahamu vizuri wajibu wake na si tegemezi ni mara chache sana hufanya mambo ya hatari.

- Mara nyingi watu wakiachwa wajitegemee, husababisha wajihisi hawasaidiwi, hawana maana, wanachukiwa na kuwa na hasira.

- Hii husababisha wazazi kuwa njia panda. Kwa upande mmoja, ni dhahiri watoto wanategemea sana juu yetu kwa sababu ya kutokuwa na uzoefu. Kuna mengi tunahitaji kufanya kwa ajili yao kwa kuwaambia na kuwaonesha.

Kwa upande mwingine utegemezi wao unaweza sababisha uadui. Kwa bahati nzuri fursa ya kuwatia moyo hufanywa na wao wenyewe kila siku. Zifuatazo ni njia ambazo unaweza kutumia ili kuwawezesha watoto kujitegemea wao wenyewe. (Faber na Mazlish, 2012)

- Wakati wowote endapo wazazi watasikiliza mawazo ya watoto wao au wakashirikiana nao katika mawazo yao au wakawa karibu nao katika kutatua matatizo yao, watawasaidia watoto waweze kujiamini na kuwa na imani.

- Mama mmoja alisema, “Bado ninamsikia bibi yangu akisema anampenda jirani yake,” ni mwanamke wa kipekee. Anafanya kila kitu kwa ajili ya mtoto wake!” watu wazima wengi, wanaamini kuwa mama mzuri ni yule anayemfanyia mtoto wake kila kitu.

- Wazazi wanatakiwa wajihusishe katika majukumu yanayotakiwa kufanywa na watoto. Endapo wazazi watahitaji kujihusisha wanatakiwa wajiulize maswali yafuatayo, "je nina chaguo lolote hapa? Je ni lazima niwe mbadala? Je, nina weza kumhusisha mtoto?"

- Tabia nzuri kwa wazazi ni kujiuliza maswali mara kwa mara kama vile "nilichosema kitakuwa na athari katika kumfanya mtoto awe tegemezi kwangu? Jizuie kusema na kutenda jambo hilo. Niseme nini au nifanye nini kumnyanyua mwanangu awe huru? Mzazi anatakiwa ajiulize maswali kama haya. Yaseme mambo hayo na uyatekeleze! Jaribu kumlinda mtoto kutokana na kuvunjika moyo pia kuwalinda kwa kuwaliwaza na kuwapa matumaini.

Kujaribu kuwapa ulinzi watoto kutokana na kukata tamaa pia huwazuia kutokuwa na matumaini, kujitahidi, kutimiza ndoto na kufanikiwa.

SIMULIZI YENYE MAAJABU YA KWELI

Mama mmoja alisimulia kuhusu habari ifuatayo: "Nakumbuka nilivyokuwa nahitajika na watoto wangu watatu. Kwa hiyo nilikuwa nimechanganyikiwa kwa mawazo mpaka nikagundua kuwa saa ya ukutani ingetumika kuwaamsha watoto kwa namna nzuri kuliko nitakavyo waamsha mimi, pia nilikua nimechanganyikiwa kwa mawazo pale nilipoacha kazi ya kuwahadithia visa mbalimbali wakati wanapoenda kulala, baada ya watoto kujua kusoma wenyewe.

Nilikuwa katika mgongano wa kimawazo kuhusu uhuru katika ukuaji wao na hali hii ilinisaidia kuelewa mkasa alioniambia mwalimu wa chekechea ambaye alitumia juhudi zake kumshawishi mama mmoja kuwa mtoto wake atakuwa salama tu kama hatakaa naye darasani. Dakika tano baada ya mama yule kuondoka, mtoto alitaka kwenda bafuni. Wakati mwalimu alipomwambia aende mwenyewe, mtoto alikosa furaha, na kusema "Hii ni kwa sababu mama yangu hayupo hapa.Ananipigiaga makofi wakati ninapomaliza."

"Mwalimu akamwambia, "Unaweza kwenda bafuni halafu ukimaliza utajipigia makofi mwenyewe. Mtoto hakuelewa lakini mwalimu alimpeleka bafuni na kumsubiri nje. Baada ya dakika chache, mwalimu alisikia sauti ya makofi.

Baada ya muda mama alimwita mwalimu na kumwambia kuwa mtoto wake alienda nyumbani na kumwambia, "Mama, ninaweza kupiga makofi mwenyewe. Sikuhitajii tena pindi niendapo bafuni; "Unaweza kuamini, "Mwalimu alishikwa na butwaa "Mama alisema hakufurahishwa na jambo hilo."

WAACHENI WATOTO WAWE HURU KUCHAGUA

Muulize mtoto kama anataka nusu glasi ya maziwa au glasi nzima au kama anataka chakula cha kawaida au chenye rangi. Kwa mtoto chaguo dogo tu huwakilisha nafasi moja zaidi kuweza kujihimili kimaisha. Anaweza akawa na hasira na msumbufu kama hatapewa uhuru wa kuchagua.

Imekuwa ni kawaida kwa watoto kusikia kauli za amri tu;

“Ni lazima umeze dawa zako”

“Acha kugongagonga kwenye meza”

“Nenda ukalale sasa hivi”

Kama tutampa uhuru wa kuchagua, kwa kawaida uhuru huo utasaidia kupunguza hasira zake. “Najua jinsi unavyozichukia dawa hizi. Je? itakuwa rahisi kwako kuzimeza kwa kutumia juisi ya tufaa (apple) au ya chungwa.

“Kugongagonga kunanikera sana. Unaweza ukaacha kugongagonga meza na kukaa kimya au unaweza ukaenda kugongagonga huko chumbani kwako. Uamuzi ni wako”.

“Ni muda sasa wa mama na baba kuongea, na wewe kwenda kulala. Unataka ulale sasa hivi au unataka ucheze kidogo kitandani halafu utatuita wakati utakapokuwa tayari kulala?

Chaguo la kulazimisha sio katika machaguo mazuri kabisa na inakuwa ni kama njia ya kumtawala mtoto. Njia nzuri ni kumuacha mtoto awe huru kuchagua kile ambacho kitakubaliwa na kila mtu. Baba mmoja alisema, “Mimi pamoja na mke wangu tulikuwa tunapita katika mtaa mmoja tulikuwa pamoja na mwanetu

> Watoto ndio watu wagumu sana kuwashawishi kuwa wameshachoka, unapofika wakati wa wao kwenda kulala.(Brown 1994)

Hany, ambaye ni mtoto wa miaka mitatu. Alikuwa anachukia kushikwa mikono yake, kwa hiyo alikuwa akilazimisha kuondoa mikono yake, tulipokuwa katikati ya mtaa. Kabla hatujavuka barabara, nilisema, “Hany, unaweza chagua kati ya kuushika mkono wa mama yako au wakwangu au una wazo zuri jingine? Alifikiri na kusema nitabeba mzigo: Chaguo lake lilikua zuri na tulilikubali.

HESHIMU JITIHADA ZA WATOTO

Wakati watoto wanapoambiwa kitu fulani ni ‘rahisi’ hii haitowasaidia, kama watafanikiwa kufanya jambo hilo rahisi, watahisi kuwa hawajafanikisha vya kutosha. Kama wakishindwa, watakuwa wameshindwa kufanya jambo jepesi.

Kwa vyovyote au kwa hali yoyote endapo mtoto ataambiwa kuwa kuna kazi nyepesi na anaweza ifanya au inaweza kuwa kazi ngumu, wanapata fikra nyingine, kama

wakifanikiwa, hupata faraja ya kuweza kufanya kazi ngumu. Kama watashindwa wataridhika na kuamini kuwa kweli kazi ilikuwa ngumu.

Baadhi hufikiri kuwa wazazi ni wanafiki wanaposema kuwaambia watoto wao kwamba "kazi hiyo ni ngumu" ingawa wakiitazama kazi yenyewe katika mtazamo wa mtoto asiye na uzoefu watakubali kwamba kwa mara ya kwanza kufanya jambo geni basi kwa hakika huwa pana ugumu. (Epuka kusema kwa watoto kuwa "Kitu au kazi hiyo itakuwa ngumu kwako)". Kwa kusema hivyo mtoto hufikiria "kwa nini mimi nisiweze" kwa nini isiwe kwa mtu mwingine yeyote na iwe kwangu mimi tu?"

Kwa baadhi ya wazazi ni vigumu au hawawezi vumilia kuona watoto wakihangaika na kupata tabu, huwaonea huruma au imani. Hata hivyo, badala ya kuwasaidia, ni vyema kuwapa maelezo kulingana na kitu wanachokifanya, kwani "muda mwingine inasaidia kama utamalizia kazi kuliko kuianza tangu mwanzo (kumalizia kufunga zipu ni jambo zuri kuliko kuanza kuivuta tangu mwanzo)"

JIZUIE KUULIZA MASWALI MENGI SANA

Jambo la maana ni kuwa makini na matokeo ya maswali tunayouliza. Moja ya swali linaloulizwa na wazazi wengi ambalo huwa ni kero kwa watoto ni: "je leo ulikuwa na furaha?" hili si hitajio la msingi la mtoto.

Wazazi wengi huwauliza watoto wao maswali mengi, pindi watoto warudipo nyumbani, "ulikwenda wapi?" mtoto hujibu kwa mkato "nje" ulifanya nini?" "sikufanya kitu" watoto hutumia mbinu za kujikinga kuzuia kuulizwa maswali, aidha hawako tayari au hawataki kujibu. "sifahamu" au "niache mwenyewe". Hii haimaanishi wazazi wasiulize maswali. Hakuna chochote hata kama wana tafsiri na wanafanya hivyo ili kuepuka maswali mengi kutoka kwa wazazi wao. Kinachotakiwa kwa wazazi ni kuwa na busara kuhusu maswali hayo.

Muda mwingine watoto waendapo kwenye sehemu za starehe au katika sherehe dhamira kuu huwa ni kupata furaha. Lakini kama hawakufurahi basi huhuzunika wao wenyewe, endapo hawakuridhika, na warudipo nyumbani wazazi huwauliza kama wanafuraha au la, swali hili hufanya mtoto kukasirika zaidi pale ambapo hajafurahi halafu mzazi anamuuliza kama amefurahi.



USIJIBU MASWALI KIMZAHA

Katika makuzi, watoto huuliza maswali mengi na ya kushangaza: upinde wa mvua ni nini? Kwa nini mtoto hawezi kurudi alipotoka? Je, na wewe baba/mama unataka kwenda chuo/shule kusoma? Mara nyingi mzazi hufanya haraka kufikiri na kutafuta majibu ya sawa kwa mtoto. Mara nyingi watoto huwa tayari wamefikiri kitu juu ya majibu ya maswali hayo, wanachotaka huwa ni kupata upembuzi zaidi juu ya maswali wayaulizayo, ingawa kikawaida ni lazima pawepo muda kwa watu wazima kutoa majibu sahihi kama patakuwa na ulazima wa kufanya hivyo. Kutoa jibu la haraka sio msaada mzuri kwa mtoto. Kufanya hivyo ni kana kwamba mzazi anafanya kazi zilizopaswa kufanywa na bongo zao, msaada mkubwa kwa mtoto ni kulirudisha swali kwa mtoto mwenyewe au kumpa jibu kupitia njia ya swali ambalo litamfanya yeye aweze kufikiria zaidi na kupanua uwezo wake wa kufikiri. “unashangaa kuhusu hilo, kwani wewe ulikuwa unafikra zipi?”wazazi wanaweza rudia swali. “unafikiri kwa nini watu hawafanyi watakavyo?”

Unaweza mpongeza muulizaji: kwa kumwambia “umeuliza swali la msingi sana, swali ambalo liliulizwa enzi za zamani na wanafalsafa,” hakuhitajiki haraka katika kutoa jibu, mchakato wenyewe wa kutafuta jawabu unathamani kubwa.

HIMIZA WATOTO KUTUMIA VYANZO NJE YA NYUMBANI

Njia mojawapo ya kupunguza fikra za kuwa tegemezi kwa familia ni kuwaonesha watoto ya kwamba ipo jamii kubwa sana kuliko ile ya nyumbani ambayo ina rasilimali nyingi zenye thamani zinazosubiri kutumiwa. Dunia si sehemu ngeni; upo msaada unaweza kukupa kama utauhitaji.

Mbali na msaada wa wazi kwa watoto, pia ni msaada kwa wazazi kwa kuwa wasimamizi kwa muda wote. Muuguzi wa shuleni anaweza fanya mjadala na watoto walio na uzito mkubwa juu ya tabia za ulaji. Muuza viatu anaweza toa maelezo juu ya utumiaji wa viatu vya aina fulani kwa kueleza faida na hasara zake. Mkutubi anaweza wasaidia vijana katika masuala ya uandishi wa kazi za kiuchunguzi. Mtaalamu wa masuala ya meno anaweza elezea madhara yapatikanayo kwa kutopiga mswaki au kuzidisha matumizi ya pipi. Vyanzo hivi vyote vya nje vyaweza ziba pengo la mafunzo toka kwa baba na mama.

USIWAKATISHE TAMAA

Mambo mengi katika maisha hutegemea ndoto, mawazo, matazamio na mipango. kwa kuwaepusha watoto kukata tamaa, wazazi wanaweza wasaidia watoto katika kuwapa zaidi uzoefu.

Vidokezo kwa wazazi

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ya ziada katika kuwajenga watoto kujitegemea.

WAACHE WAISHUGHULIKIE MIILI YAO WAO WENYEWE

Mzazi wanatakiwa wajizuie mara kwa mara kuchana nywele zao mbali na macho ya watoto wao, kujinyoosha mabega, kuvaa shati na kuwaweka kola vizuri. Watoto wanahisi tabia hii ni uvamizi dhidi ya faragha yao kimwili.

USIZUNGUMZE HABARI ZINAZOWAHUSU WATOTO WAKO MBELE YAO BILA KUJALI NI WADOGO

Mzazi hana budi kusimamia endapo atakuwa anamuelezea rafiki yake kuhusu mtoto wake mfano, akiwa anamuambia kuhusu masomo ya mtoto wake “mwanzoni alikuwa hafurahii masomo yake, lakini sasa anafanya vizuri.“Usimjali sana anahisi aibu” Pale watoto wanaposikia wamejadiliwa kwa namna hii wanafedheheka/ wanakereka. Endapo watoto watayasikia haya watajihisi vibaya. Na kujidhani kwamba wao ni kama kitu kinachomilikiwa.

WAACHE WATOTO WAJIBU WAO WENYEWE

Mara kwa mara wazazi, wakiwa mbele ya watoto wao huuliza maswali kama:

“je amemfurahia mtoto mpya?” “

“kwanini hachezei mdoli wake mpya?”

Alama nzuri ya kuonesha kujitegemea kwa mtoto ni kumwambia muulizaji,

“Amir atakuambia.

Yeye ndiye anayejua.”

ONESHA HESHIMA KWA HATAMU ZA MTOTO “UTAYARI”

Muda mwingine watoto hupenda kufanya vitu kwa namna nzuri sana, lakini kihisia na kimaumbile hawako tayari kwavyo hawezi kufanya kwa sababu za kihisia au kimaumbile. Kwa mfano: mtoto wa kike anataka kutumia bafu kama msichana aliyepevuka, lakini hawezi kufanya hivyo. Mtoto wa kiume anataka kwenda kwenye bwawa la kuogelea kama kaka yake, lakini anaogopa wingi wa maji. Anataka kuacha kunyonya kidole chake, wakati ambapo amechoka, huhisi ni jambo zuri zaidi, badala ya kutumia nguvu kuwalazimisha, kuzozana nao au kuwaaibisha vijana, wazazi wanaweza kuelezea uaminifu wao kwa watoto wao katika njia chanya.

“Mwambie ipo siku moja naye atatumia bafu kama baba au mama.”

“Sina wasiwasi naamini ukiwa tayari utakoga.” “Naamini ukiamua utaacha kunyonya kidole.”

USIKITHIRISHE "HAPANA!"

Kuna baaadhi ya wakati ambapo wazazi hudhibiti matamanio ya watoto wao. Ghafla watoto huwa na huzuni kwa kukatazwa, huyatazama kama ni shambulio katika hali ya kujitegemea, hii husababisha watoto wapige kelele, wafanye vurugu, wanatamka majina visivyo au kususa. Husababisha kuwauliza wazazi, kwa nini isiwe hivyo? Wewe ni katili? Sikupendi. "Inachosha hata kwa watoto wavumilivu kwa wazazi wao".

Kwa nini wazazi wasikubali na kusema ndio kwa kila kitu? Kawaida haiwezekani, kwa bahati nzuri kuna baadhi ya njia mbadala ambazo zinaruhusu wazazi kuwa na msimamo bila kuleta mabishano. Mifano yaweza tengeneza mazingira ya kumtuliza mtoto na kumfanya atulie ndani na kuweka mazingira ya nyumbani yakiwa salama, kwa watoto kuzunguka ndani, kinyume chake huharibu usikivu, utulivu kwa kitu kingine bila kusema hapana.

SHAURIANA NA MWANAO

Wazazi wengi hawajadiliani na watoto zao kuhusu mambo yanayowahusu watoto. Kama wakipanga kuwapatia zawadi kwa kufaulu mitihani, ni vyema kuwapa uhuru kuchagua mkahawa waupendao kwa ajili ya chakula cha jioni, ni sherehe yao siyo ya kwenu (wazazi). Pia kama wazazi wanapanga kuwanunulia vifaa vya kuchezea (midoli au michezo mingine) ni vyema, kuwaarifu watoto na kujua wanachokitaka la sivyo wazazi watanunua midoli wanayo pendelea wao, na wala siyo wapendavyo watoto. Hali inayosababisha wazazi wakiishia kuchezea hiyo midoli na watoto hubaki wakiwa wamechoshwa na kusababisha kulia. Ni muhimu kwa watoto kuhusishwa katika mambo ya wazazi wao badala ya wazazi kuwalazimisha wayapendayo au wanayoyachukia kwa watoto wao.

Pale ambapo watoto walichukuliwa kama watu wa karibu na wazazi wao itasaidia kuongeza ubora katika mitazamo kwa namna zote.

"Omar Ibn Al- Khattab alisema "Cheza na mwanao kwa miaka saba ya mwanzo, mfundishe na umuelekeze madili mema kwa miaka saba inayofuata, na kisha mfanye awe mtu wako wa karibu kwa miaka saba inayofuata na; kisha muache awe huru.

Kufanya ubaguzi wa tabia njema, ni kama kuchukua fuvu katika mwili ulio hai. Tabia hazihusishi chochote isipokuwa jinsi ulivyo kiujumla; Na jinsi ulivyo kiujumla ni kama mwanaume katika kila uthibitisho wa muonekano wake.

Kuwa na tabia njema haimaanishi kuwa umepanda baadhi ya sifa zenye majina (maarufu) na vinasaba vya kipekee; inamaanisha ni kuwa kamili na kujitosheleza jinsi vile unavyotakiwa kuwa kupita mahusiano yako na wengine katika sekta mbalimbali za maisha.

John dewey

WAPE WATOTO UHURU WA UWAJIBIKAJI

Uhuru tunaoukusudia ni ule wa uwajibikaji, uzito wenye thamani na ulio na mwongozo sahihi. Hii haihusu kufanya fujo wala kukosa hisia za uelekeo, ambazo

ndio zao la kumkomboa mtu binafsi kutoka katika taratibu, maadili na tamaduni, ambayo ni matokeo ya kuwa huru. Wazazi wanatakakiwa wawaandae watoto wema wakiwa huru, jambo litakalowasaidia watoto kufanya maamuzi sahihi wakiwa wao wenyewe. Waimarishe watoto kwa kujitegemea na kuwa watu wema, haya yatawasaidia katika kukabiliana na changamoto za aina yoyote.

USHAURI DHIDI YA UHURU; BINTI NA MAMA YAKE

Pindi wazazi wanapoambiwa wawape ushauri watoto wao, wanaweza wakaingilia uhuru wao, na wengi miongoni mwao huwakatisha tamaa. Jambo linalowasababisha wahisi wametengwa hawawezi kuelewa kwa nini wamenyimwa uhuru wa kupata hekima, busara na uzoefu wa wazazi.

Mfano 1. Tazama kisa cha mama ambaye ni mkaidi pamoja na mwanawe! Kwa nini mwanangu asifaidike na ushauri wangu anapokuwa na matatizo? Binti yangu hakuwa na uhakika kama atakwenda kwenye sherehe ya mahafali ya rafiki yake kwa sababu alikuwa hawapendi baadhi ya wasichana. Mara nyingi hunong'onezana na kuitana majina, "kuna tatizo gani ikiwa nitamwambia binti yangu aende kwa vyovyote iwavyo kwa kuwa kufanya hivyo atakuwa amewaangusha marafiki zake?"

Pindi ambapo wazazi wanawapa ushauri wa haraka, watoto huhisi wao ni wajinga (kwa nini sikufikiria mwenyewe?) kwa hasira anaweza sema (usiniambie\ usinifundishe jinsi ya kuendesha maisha yangu), au kwa kubeza (Nini kinakufanya ufikiri kwamba sikufikiria hivyo tangu mwanzo?). Kama watoto wataamua wao wenyewe nini wanachotaka kufanya, jambo hilo huwapelekea makuzi yao ya kujiamini na wanakuwa na moyo wa kujijengea uwajibikaji kwa ajili ya maamuzi yao.

Je, nisifanye chochote mwanangu anapokuwa na tatizo? Muda mchache niliomwambia ni tatizo lako, na kumwambia kuwa utashughulikia mwenyewe matatizo yako, binti alikasirika sana." Watoto huhisi maumivu kwa kutengwa na wazazi kwa kuhisi matatizo yao yamepuuzwa. Ingawa upeo wa juu wa kupuuza ama kushauri kwa haraka. Yapo mambo ambayo mzazi anaweza fanya. Kwa mfano;-

- Wazazi wanaweza kusaidia kutafuta

majibu ya fikra na hisia mgando za watoto wao "kutokana na ulichokisema, imeonekana ya kwamba una hisia mbili; unahitaji kwenda, lakini hautaki kushindana na wasichana usiowapenda.

- Wanaweza kurahisisha tatizo kwa kuliweka kama swali" hivyo swali hilo laweza kuwa hivi, "unawezaje kuwepo kwenye sherehe na kustahimili majina mabaya wakuitayo hao wasichana?" wazazi wanapaswa kukaa kimya bila ya kuuliza swali kama hilo. Ukimya wao unamruhusu mtoto kutafuta utatuzi / majibu.
- Wafahamishe watoto kwamba kuna vitu vinapatikana nje ya nyumbani "nimegundua ya kwamba sehemu ihusuyo vijana kwenye maktaba ina vitabu vingi kwa ajili ya vijana namna wanavyoweza kuyashinda matatizo mbalimbali yanayowahusu. Bila shaka ungetaka kujua watasema nini"
- "Chukulia ya kwamba nimefanya yote hayo huku nikifikiria kuwa hilo ni suluhisho, nikiwa na uhakika ya kwamba yeye hatoweza kuwaza hilo. Je, ninaweza kumueleza / kumfahamisha?" Ndio, lakini ni baada ya kumpatia muda wa kufikiri. Ataweza kusikiliza na kuheshimu mawazo ya wazazi, endapo tu kama mawazo hayo hayataonesha dharau dhidi ya maamuzi yake, "waonaje kama ukienda kwenye sherehe na nakala yako ya ucheshi, ile ambayo ni ya yule mcheshi mpya? Yawezekana hao wasichana wakatumia muda mwingi kufurahi kuliko kukusumbua"

Anza na wazo hili "utajisikiaje kuhusu …….au "utachukuliaje……" ushauri ambao unaonekana ni "uwerevu" kwa wazazi yawezekana ukawa si werevu" kwa watoto.

"Chukulia ya kwamba ninaamini kuwa binti atakwenda kwenye sherehe. Je, ni lazima nikae kimya? Au (je ina mlazimu kukaa kimya? Baada ya mtoto kulieleza tatizo lake yawezekana ikawa ni fursa / msaada kwake kusikiliza mawazo ya wazazi wake."

"Sitajisikia vyema kukosa furaha kwenye sherehe kutokana na vitendo vya baadhi ya wasichana. Ninafikiri ya kwamba ni muhimu kushiriki. Ili kutomfadhaisha rafiki yangu kwenye sherehe yake ya mahafali, hata kama itahitaji kujitoa mhanga."

Vijana wapewe nafasi ya kufahamu misingi ya kimaadili ya wazazi wao, hata kama wakichagua kutofanyia kazi hiyo misingi kwa wakati huo, wazazi watakuwa wamewapatia watoto wao kitu cha kufikirisha na cha kujifunza.

Mfano. 2: Mama mmoja alisema "Nimekuwa nikisumbuana na binti yangu kwa muda mrefu kuhusu mavazi. Nimeamua nimuache avae atakacho yeye mwenyewe pindi asipokwenda shule. Siku ambazo huenda shule huwa nina muandalia nguo za aina mbili juu ya kitanda chake na yeye huamua" faida ya sare ya shule ni kwamba hakuna uchaguzi mwingine na kwa hiyo hakuna upinzani kuhusu kipi kivaliwe!

Mfano. 3

Mama Samy alisema "hatimaye nimemaliza malumbano ya siku nyingi niliyokuwa nayo na kijana wangu, kuhusu uvaaji wa sweta au jaketi. Nilimwambia Samy "Samy nimekuwa nikifikiria ya kwamba badala ya kukueleza kila siku juu ya nini uvae, nafikiri unaweza kuamua mwenyewe. Tutengeneze jedwali ambalo litaonesha aina ya mavazi kulingana na nyuzi joto zilizopo tulichora jedwali pamoja.

NYUZI JOTO	VAZI LIFAALO
Nyuzi joto (69 farenheit) au 20^0c kwenda juu	Sweta halifai kuvaliwa
Kati ya nyuzi joto 50 na 68 fahrenheit au Nyuzi joto (10^0c hadi 20^0c)	Sweta
Nyuzi joto 49F au 9^0c kushuka chini	Jaketi zito (nguo nzito)

Tulinunua kipima joto na yeye akakining'iniza kwenye mti. Siku hizi kila asubuhi huenda kuangalia nyuzi joto, na hakuna tena malumbano. Najichukulia kama mtu mwenye akili nyingi sana.

Mfano: 4: Muna alimuuliza mama yake "kwa nini tusitembelee sehemu zote zenye kupendeza katika likizo hii kama vile Mlima Kilimanjaro …..na mbuga ya wanyama kama Ngorongoro? Nilitaka kumjibu, lakini nilikumbuka kuwa sikupaswa kufanya hivyo. Nilisema "kwa nini tufanye hivyo? Muna alitembea kwa kishindo huku akizunguka jikoni akisema "najua, najua …….. kwa sababu ni ghali mno …….Basi tunaweza hata kutembelea mbuga za wanyama zilizo karibu?

JE, UNALAZIMISHA UVAAJI HIJABU KWA BINTI YAKO? NA NOHA BESHIR

Wazazi wangu walikuwa hawanilazimu kufanya chochote. Sikumbuki hasa ni wakati gani wazazi wangu hawakunifanya nichague. Wakati nilipovaa mtandio kichwani, mama yangu hakusema kuwa " Ni lazima uvae hivyo kwa kuwa ni dini yako" Mama yangu hunieleza sababu juu ya kwa nini tunavaa hivyo na wakati mwingine inaweza usijisikie vizuri, na kwa hiyo kipindi cha joto haimaanishi uvae sweta na suruali ya jinsi. "Hapana, unaweza kuvaa suruali pana nyepesi ambayo inaruhusu upepo kupita, na shati jepesi lenye vifungo kwa njia hiyo, marafiki zako watakapo kuuliza kwa nini umevaa hivyo unaweza ukawapatia sababu ya uhakika ya kwamba unaamini hivyo, na si kwamba ni sehemu ya dini yangu au nimelazimishwa kuvaa hivi na wazazi wangu" kiukweli nilikutana na watu wengi sana ambao wamekuwa wakiniambia wanataka wavae kimojawapo, baada ya kuwaambia kwa nini navaa hivyo.

kiukweli ninajisikia vizuri sana kuwa na wazazi wangu. Hii haimaanishi kuwa siwezi kuishi bila ya wao. Kutokana na sababu fulani nimekuwa nikiishi nao na ninashukuru kwamba ninaweza kuwaeleza chochote. Mimi na dada yangu tuna uhusiano mzuri sana. Lakini kizuri zaidi kuhusu familia yangu ni kwamba hata kama kiongozi mkuu (Amirah) ndiye yule ambaye ni mkubwa kuliko wote, na hata kama mimi ni mdogo kuliko wote, katika familia yangu, sote tupo sawa.

Kama wazazi hawawapendi marafiki wa watoto zao

Wazazi hupendelea watoto zao wawe na marafiki wapole, wakarimu na wenye akili, na wasiwe ni walevi au wavutaji au wanaotumia dawa za kulevya. Wazazi wanapenda kuwapa ulinzi watoto na wakati huo huo huwashajiisha kujitegemea. Hofu kubwa ya wazazi juu ya urafiki ni kwa sababu urafiki huwa si jambo lenye kudumu. Ingawa watoto hudhani katika hatua za awali marafiki wawapatao huwa si watu wakorofi. Kuruhusu uchaguzi wa marafiki ni jambo zuri zaidi na linaweza kuwa na faida kuliko kujaribu kusitisha urafiki huo. Hapa sasa ni lazima kuelezea hitajio la msingi linalotosheleza urafiki kwa kuwauliza watoto kuhusu marafiki wawatakao. Jawabu linaweza kuwasaidia wazazi kujua sababu za msingi zilizowavutia kuwa na marafiki hao. Watoto lazima wafundishwe namna ya kuamiliana na watu wa aina tofautitofauti. Baadhi ya wakati marafiki waweza kuwa ni maadui na watu wa hatari, kama mtoto atahusiana na marafiki wabaya ambao wanajihusisha na mambo mabaya au mambo maovu. Wazazi watawajibika kuvunja urafiki huo na watu hao. Usaidizi, uvumilivu na uaminifu wa wazazi utawasaidia watoto kuwa na mahusiano mazuri na wanajamii. Watoto wanahitaji mwongozo wa kuwasaidia kuhusiana vyema na watu na kujihisi vizuri wanaposhirikiana nao jambo linalosababisha kujihisi ni wawajibikaji.



Kuwasaidia watoto kufanya maamuzi huwajengea kujitegemea

Wazazi wanaweza fundisha kujitegemea kwa kufanya mambo yafuatayo:

- Wape fursa ya kufanya maamuzi (kama vile wafanye uchaguzi juu ya wapi familia inaweza tembelea au agawe majukumu kwa wanafamilia)
- Kuonesha namna unavyojali maamuzi yao, namna unavyopokea taarifa zao za msingi, na namna unavyojali majibu ya maamuzi yao.(mfano: nguo gani ya kuvaa).

- Wafundishe ya kwamba maamuzi yeyote wanayoyafanya yatakuwa na athari kwao wenyewe na kwa wengine, tumia mfano wa uvutaji sigara. Kijana anaweza vuta sigara kwa kujidhania kwamba amekuwa, bila kujali athari itakayompata: kama vile meno kuwa ya njano, kutoa hewa chafu na hatari ya kupata saratani na magonjwa ya moyo. Uvunaji wa tumbaku ni uharibifu. Pia tumbaku hupunguza rutuba ya udongo, vivile ardhi itumikayo kulimia tumbaku ni vyema ingetumika kuzalisha chakula na mavazi kwa watu wenye mahitaji
- Ni lazima watoto waoneshwe ya kwamba kutofanya maamuzi wakati yanahitajika ni jambo baya kama ilivyo kufanya maamuzi mabaya.
- Wazazi ni lazima wakubali mawazo ya watoto kwa vyovyote yawavyo. Hakuna maamuzi ambayo ni sahihi, kwa hiyo wazazi wajitahidi kuwasapoti watoto wao juu ya kufanya maamuzi na wayaboreshe.
- Maamuzi ya watoto huegemea zaidi katika hisia zao na mahitajio yao na si lazima yafanane na ya wazazi wao.
- Sheria ama vidhibiti katika kufanya maamuzi lazima yapoozwe. Kwa hakika maamuzi ya hatari hayakubaliki, kwa hiyo wazazi lazima wajitahidi kuelezea kwa nini wanayakataa.

Hatua za kufuata katika kufanya maamuzi

- Uwezo wa kufanya maamuzi unasaidia kukuza kujiimarisha na kukuza utambuzi. Watoto ambao watafanya jitihada katika kujidhibiti huwa ni maandalizi ya kujitegemea, kuwa muwajibikaji na kuwa na furaha kipindi cha utu uzima.
- Ili kuweza kujenga watoto wenye kujitegemea ni muhimu kupitia hatua zifuatazo.

- Wakubali ya kwamba maamuzi yanahitaji kutengenezwa.
- Kukusanya taarifa kunasaidia katika kufanya maamuzi.
- Kuainisha maamuzi mbadala.
- Kuyafanyia uchunguzi matokeo ya maamuzi.
- Kadiria namna ambavyo njia mbadala yaweza faa kwa kutazama heshima na dhumuni la mtu.
- Tambua hoja dhaifu (kama vile vishawishi rika, matamanio kuthibitisha ukomavu, au fikra za uasi).
- Mpe mtoto muda kidogo aweze kufanya maamuzi. Uharaka katika kufanya maamuzi unaenda kinyume na umri wa mtoto.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 59: KUPIMA UFANISI WA UTAWALA WA WAZAZI
Jaribu kumuuliza mtoto mbele ya wazazi wake maswali kumi juu ya mada yeyote. Zingatia kama mtoto atatoa majawabu au mzazi atadakia na kujibu kwa niaba yake. Idadi ya maswali yatakayojibiwa na mzazi itakuwa ndio "kipimo cha utawala wa mzazi" tazama hamasa na shauku ya mzazi pindi mtoto anapojaribu kujibu maswali magumu!

Wazazi ni lazima wahame wao wenyewe kutoka katika hali ya kuwa viongozi watawala na wawe watoa miongozo na washauri (ili kurahisisha uhuru makini kwa watoto).

ZOEZI LA 60: ELEZEA MFUMO WENU WA KIMAADILI KWA WATOTO

Ni kosa kuwalazimisha watoto kufuata fani fulani au kuwaiga nyinyi wazazi, badala yake imarisha akida sahihi, maadili mema na mtazamo mzuri juu ya ulimwengu kwa namna wapendavyo. Pia shirikiana nao katika mambo ya heshima kwa kuhusianisha wawe na mapenzi kwa wanadamu,wanyama , mimea na mazingira.

Zama za leo watoto wanawashangaa wazazi wao kwa kuwa na njia nyingi za kufikia malengo na dhamira. Jadiliana na wanafamilia na waulize watoto namna watakavyoyasimamia maadili hayo.

ZOEZI LA 61: JE ,WEWE NI MZAZI UNAYEUNGA MKONO AU UNAYEINGILIA MAAMUZI
Tumeanza tukiwa mmoja mmoja, tukaoa na baadaye tukapata watoto. Miongo miwili baadaye, watoto wanatuhama na kuingia vyuoni. Jenerali McArthur na Rais Roosevalt walikuwa na wazazi ambao walikuwa karibu nao pindi walipojiunga na vyuo. Hakukuwa na simu wala baruapepe 24/7 (saa 24 kwa wiki) ili kuwasiliana nao.

Wazazi wengi wanadhani kufanya hivyo ni kuingilia mipaka ya watoto kwa hivyo, hawataki kuingilia maisha ya watoto wao. Yafuatayo ni maswali ambayo wazazi watajibu ili kugundua tabia zao za kweli:

- Mara ngapi unawasiliana na mwanao awapo chuoni? Kila siku, kila wiki, ama kila mwezi?
- Je, unawasiliana na Profesa/ mhadhiri/mwalimu wa mwanao?
- Je, unakagua mitihani ya mtoto na kugundua pale alipokwama?
- Je, ukimtembelea mtoto wako unatazama ustawi wake (kusafisha chumba chake, kufua nguo zake, kuweka nje vyombo vichafu)?
- Kama mtoto wako haelewani na mwenziwe anayeishi naye je! Umejaribu kuingilia kati?
- Jadili majawabu yako pamoja na wanafamilia. Yafuatayo ni baadhi ya maoni juu ya kushughulika na mtoto anayeishi mbali na nyumbani:
- Hakikisha anadumisha mawasiliano na wanafamilia. Itasaidia kukuza kujitegemea.
- Mitihani na kazi nyingine za darasani ni lazima zifanywe na mwanafunzi.
- Kijana wako wa chuoni ni mtu mzima ambaye anaweza kumudu mahitaji yake kwa hiyo ni lazima afanye kazi zake mwenyewe.

(kantrowitz na tyre 2006)



20

SURA YA SHIRINI

- KUSTAWISHA UBUNIFU

SURA YA ISHIRINI **490**

Kustawisha Ubunifu **490**

Utangulizi 492
Mbinu za kukuza ubunifu 494
Ugunduzi mbalimbali wa kihistoria 496
Kuimarisha Ubunifu wa watoto 497
Mambo yanayozuia ubunifu 497
Njia za kukuza ubunifu 500
Uandishi wa Watoto 501
Usanii kwa Watoto 502
Imani potofu: Mawazo ya ajabu au yasiyo na tija 504
Wazazi wafanye nini? 504
Ya kuzingatia katika midoli (wanasesere). 505
Kazi za Kufanya

Utangulizi

Ubunifu ni hali ya mtu kueleza hisia zake kupitia njia tofauti. Kuna hisia nyingine zinazojitosheleza wakati watoto wanajieleza kwa uwazi na bila kujihukumu, uwezo wa kubuni kitu mwanzoni ni sehemu muhimu ya tabia nzuri. Kwa kutazama aina mbalimbali za sanaa na ubunifu wa watoto. Watoto wanaweza kuelezea na kuendeleza hisia zao huku wakikuza vipaji vyao, kujaribu njia mpya ya kufikiri na kutatua matatizo ni sifa ya ubunifu wa mtoto.

Tunaweza kujua ubunifu wa mtu kama mtu huyo ana matamanio makubwa ya kuwa mbunifu, anayekubali changamoto, anayetarajia kitu kizuri kutokea, anauwezo wa kuona taswira. Watu wabunifu, huyatazama matatizo kama fursa, hukabiliana na changamoto, hufanya kwa jitihada kubwa, hawakati tamaa haraka na huwa na subira. Watu wengi wanashindwa kwa sababu wanatumia dakika tisa tu kwenye kutatua tatizo linalohitaji dakika kumi.

Watoto wanahitaji kuongezewa, na kutoharakishiwa muda wa kugundua na kufanya kazi zao vizuri. Hawatakiwi kukatazwa na kulizwa au kuondolewa kwenye shughuli wakati bado wanauwezo, wakishiriki na kuhamasika kwa kufanya kazi kidogo ya ubunifu. Wanahitaji wapewe sehemu ya kuacha kazi zao ambazo hazijakamilika ili kuziendeleza baadaye, na pia sehemu inayowavutia kufanya kazi katika mazingira mazuri. Mazingira ya nyumbani yasiyo na utulivu sio mazingira mazuri kwa kazi ya ubunifu. Watoto wanahitji sehemu yenye utulivu na yenye mwanga wa asili, rangi za kuvutia, mahali pazuri pa kukaa ambapo panalingana na wao. Vyumba vinatakiwa kuwa na kazi za mfano wa zile wazifanyazo na za wengine. Wazazi wanatakiwa wakubali makosa, wahamasishe kujitolea na kukuza hali ya



kufanya vitu vya kipekee, Ubunifu unahitajika hata kama kutakuwa na kiasi fulani cha makosa, mapambano na uhuru, bila vurugu au usimamizi wenye masharti magumu.

Kama mzazi, unahitajika kuwa mhamasishaji juu ya ubunifu wa watoto, ufuatiliaji na ujuzi wa kutatua matatizo unaweza kuendelezwa kwa misingi asilia na furaha. Kwa mtoto mdogo kufanya shughuli ni kitu cha muhimu, kuhitimisha jambo au kitu si katika mambo yenye mvuto mkubwa. Ondokana na hoja kama, "yenye muonekano wa kuchekesha" au umefanya kazi kwa bidii juu ya hiki" kuliko kuhoji kulingana na mtazamo wa shughuli za kipekee za mtoto na kuhoji upekee wa matokeo ya kazi zao, watoto wenye hisia kali wanaogopeshwa kutokana na shughuli za ubunifu wakati wanahitaji kuzalisha kitu. Mtoto ambaye ameanza kuchora au kutengeneza nyimbo kwa niaba ya kuwaridhisha watu wazima anakuwa tayari amepoteza shauku za ubunifu. Ruhusu na kubali matumizi ya vifaa vya nyumbani katika shughuli za ubunifu, vitu vya nyumbani kama vile sufuria, vyungu, madumu, wape watoto ambao bado hawajaanza shule vifaa vya kisanaa haraka iwezekanvyo, Mtoto mwenye umri wa miaka miwili na nusu anauwezo mdogo wa kuchora jikoni, na kuwa na ubunifu mkubwa kuliko mtoto mwingine mwenye miaka sawa ambaye anasubiri hadi mtu ampe kalamu ya kuchorea kutoka katika makabati marefu. Usipange sheria ngumu katika usimamizi wa kazi za sanaa pindi ambapo shughuli inapokuwa ngumu kuliko uwezo wa mtoto. Kurahisisha ni ufunguo wa mafanikio kwenye kazi za sanaa ya mtoto. Kadri umri wa watoto unavyoongezeka unatarajia uone usafi wa hali ya juu.

Nguvu inayotumika kulazimisha sheria za usafi hupunguza nguvu za ubunifu na ugunduzi. Kila mtoto anahitaji kujifunza haki ya wengine na sheria salama. Bila mfumo

wa matarajio ya hakika, uchunguzi na ugunduzi hupelekea migogoro.

Mtoto aliyechini ya usimamizi madhubuti japokuwa anaweza kujitolea ugunduzi wake na uchunguzi wake kwa ajili ya kuhakikiwa, kama mtoto atakuwa mwangalifu kwa kujithamini mwenyewe kwa ujumla atadumu kwa kuwa msafi na mwenye kufanya vitu katika njia nzuri, pia haitohitajika nguvu kubwa katika kukuza ubunifu wake. Ubunifu hupotea ikiwa "mambo yanaenda kwa amri tu" kuwa makini- safisha hapa, kama ulazimishaji wa ufanyaji kazi ndio mtindo unaotumika. Njia hiyo hiyo inatumika kwa shughuli zinazoendeleza udadisi na mapenzi ya ugunduzi. Hizi pia zinakataliwa kwa kuzidisha udhibiti.

Mbinu za kukuza ubunifu

Huu ni baadhi ya ushauri wa kukuza ubunifu.

- Iga mawazo ya watoto kuliko kujaribu kutengeneza mawazo yao, kukubali mawazo yako yasiyo ya kawaida na jadiliana nao.
- Tumia njia za kibunifu katika kutatua matatizo ambayo yanatokea kila siku. Wape uhuru wa kufanya makosa, waruhusu watoto wafanye majaribio bila woga.
- Watoto wapewe muda wa kugundua vinavyowezekana.
- Wahamasishe watoto kufanya majaribio wakiwa na mambo ambayo siyo ya kawaida. Orodhesha maswali na mitazamo yao. Fanya tathimini kujua ni yapi watoto wameyaona kwa kurudia uliyoyasikia na kuuliza maswali zaidi kuhusu jaribio.
- Wape fursa ya mazingira yenye kuchochea kuonesha mitazamo yao. Wape watoto vitabu, michezo na fursa ya kufanya jaribio wakiwa na vitendea kazi.
- Watoto waoneshwe tamaduni nyingi tofauti, vitu vilivyowahi kutokea, watu, mikoa ili waone kama kuna njia tofauti za kufikiria kuhusu tatizo ,hamasisha watoto waweze kujaribu juu ya uzoefu mpya walioupata uliondani ya uwezo wao pamoja na kutembelea makumbusho ya watoto.
- Kubali njia mpya ya kufikiria. Shirikiana na watoto katika shughuli za sanaa, sayansi na shughuli za ubunifu pamoja nao. Pia wanaweza kushiriki katika miradi inayohusu kujitambua.
- Himiza kujiepusha kukata tamaa, washawishi watoto kumalizia miradi kwa kuwashawishi kupitia kila hatua kwa umakini kwa kuwasaidia na kuwaelewa nguvu zao na udhaifu wao.

MWANAFUNZI MBUNIFU. UGUMU NA URAHISI

Mwanafunzi alifanyiwa usaili ili adahiliwe katika taasisi ya kifahari ya mambo ya utawala. Muuliza maswali akasema,

" Naweza kukuuliza maswali kumi rahisi au swali moja lililogumu zaidi. Jifikirie vizuri".

Mwanafunzi akasema, "niulizwe swali moja gumu zaidi"

Sasa nipe jibu, "kipi kinakuja mwanzo, mchana au usiku?"

Kijana alijibu "Ni mchana".

"Kivipi, muulizaji akauliza.

Kijana akasema "Samahani, uliniahidi kwamba usingeniuliza swali la pili ambalo ni gumu!"

Yule kijana akachaguliwa.

Utaalam ni kuweza kujua ugumu wa mambo, ambapo ubunifu ni kuweza kujua urahisi.

- Vumilia kila usichokitegemea. Waache watoto wajue kwamba si lazima muda wote wawe na majibu sahihi kwa tatizo linalowakabili, ugunduzi na mitazamo ya kipekee ni lazima ithaminiwe. Kubaliana na fikra za watoto, watu wabunifu hawaogopi upweke, bahati mbaya au fikra mpya. Bungua bongo zitahamasisha fikra nyingi na mawazo yenye mvuto.
- Kubali mawazo ya mtoto wako. Watu wabunifu hawana hofu na wanamsimamo, hawaogopi fikra ngeni. Kujipa changamoto kutakupa ujasiri wa fikra mbalimbali za kipekee na mawazo yanayovutia.
- Chochea imani ya kutoogopa kukosea. Kushindwa sio janga ni fursa ya kielimu ambayo itapelekea kufanikiwa. Mkuu mmoja aliwaonya mameneja wake kwa kuwaambia, "hakikisha unakuwa na idadi ya makosa ya msingi."
- Ona zuri katika baya. Wanatafakuri mahiri, wakikabiliwa na ugumu wa kupata suluhu husema, "kuna zuri gani katika hili?" kunaweza kuwa na jambo la maana hata katika wazo baya.

ONA ZURI KATIKA BAYA

Ni kwa namna ipi tunaweza kuwawezesha wanafunzi kujifunza vizuri zaidi? Je! Jawabu la sawa : Ni kuwapiga na fimbo! Hili siyo jibu zuri kwa sababu ni kinyume na utaratibu. Lakini, ni lazima tuwafungie nje? Kwanini usiulize, " Kipi ni kizuri katika hili ?" Inampa mtu binafsi umakini katika utendaji dhaifu; inahamasisha wanafunzi wengine na hata yule aliyepigwa kuwa dhoofu kwenye utendaji na inashinikiza wanafunzi wengine, vile vile adhabu ya viboko, ni rahisi na haigharimu kitu.

Swali jipya ni, "Tunaweza kurithi au kushirikisha baadhi ya vitu vizuri ndani zaidi ya majibu yanayowezekana, iwe iliyotolewa kwenye kitu halisi au siyo? Tunaanguka kirahisi kwenye aidha kufikiria na kuamini kwamba utatuzi mbaya, ni mbaya kwenye kila fani. Kiukweli, ubaya unaweza kuwa na sehemu nzuri tunazoweza azima au unaweza kufanya kitu kisicho sahihi ambacho ni kizuri zaidi basi kifanyike sawasawa. Na mara zote, jibu baya lina sehemu moja ambayo ni mbaya zaidi ambayo ikiondolewa huacha jibu moja zuri.

Ugunduzi mbalimbali wa kihistoria

1. Watu wabunifu hutafuta maendeleo, kwa mfano, siagi ya kwanza duniani ilitengenezwa kwa kutumia mafuta ya nyama, maziwa na maji. Na haikuwa na ladha na wala haikuwa nzuri kiafya. Lakini mwanzoni mwa karne ya 20 mafuta ya nyama yakawa adimu kwahiyo watengenezaji wa siagi wakajiuliza watumie nini? watengenezaji wa siagi wakaanza kutumia mafuta ya mbogamboga badala ya nyama. Wakatumia soya, nafaka za mafuta ya alizeti. Hivyo siagi ikaanza kuwa na ladha nzuri na nzuri kiafya. Na njia hiyo ndiyo inayotumika hadi leo.

2. Si lazima kuwa na maarifa mengi ndio uwe mbunifu. Wanasanyansi wa mambo ya anga mwanzoni hawakuweza kutengeneza peni ya kutumika angani. Kutokana na kukosekana kwa nguvu ya mvutano wa dunia (Force of gravity). Na kutokana na ubunifu, jawabu pekee ilikuwa ni kutumia penseli. Lakini baada ya miaka kadhaa waliweza kutengeneza peni hiyo na wakaipelekea NASA (shirika kubwa duniani la kisayansi) kwa ajili ya majaribio ilifanya kazi na inatumika Marekani na kampuni zote za masuala ya anga.

3. Tatizo linaweza kuwa suluhisho. Kitu ambacho mtu mmoja huweza kuona kama kikwazo. Mtu mwengine huweza kuona kama ni fursa nzuri. Kwa mfano, "Baada tu ya kutengenezwa gundi (super glue), ikagundulika kwamba kama hautakuwa makini, huweza kugandisha vidole vyako, lakini jambo hili madaktari wa Vietman wakachukulia kama fursa kwani walikuwa wakitumia gundi kufungia vidonda.

4. Mfano mwingine wa namna hii ni juu ya mtaalam wa masuala ya kemia ambaye alikuwa anafanya kazi katika kampuni ya 3M., nchini Marekani, alifanya uchunguzi wa gundi na kugundua gundi nyingine ambayo ni dhaifu ambayo haiweza kushikana na vidole. Ilionekana ni tatizo kabisa. Hata hivyo tatizo hilo lilibadilishwa kuwa suluhu. Katika mwaka wa 1980 bidhaa ilizinduliwa kama mbadala na kutumika ulimwenguni kote.

Kuimarisha Ubunifu wa watoto

Huenda mawazo ya watoto yakathaminiwa, lakini pia mara nyingi huwa yanapuuzwa, Amabile na Hennessey (1992) wameeleza mambo yanayopoteza au yanayoua ubunifu wa mtoto.

1. Uangalizi wa hali ya juu. Kumuandama au kumchunguza sana mtoto na kufanya ajue kwamba wakati wote yupo katika uangalizi, humfanya mtoto asijaribu mambo mbalimbali kwa sababu ya woga na hivyo kupoteza kipaji cha mtoto.
2. Ukali katika kumfanyia tathmini. Ikiwa tunawafanya watoto wawe waoga katika yale matendo wanayoyafanya, hupelekea ubunifu wao upungue.
3. Pongezi za kupitiliza. Utoaji wa zawadi sana kwa mtoto humfanya mtoto ashindwe kuwa mbunifu zaidi, kwani mtoto asiyepongezwa mara kwa mara hufanya jitihada zaidi ili aweze kupongezwa. Na mara nyingi watoto wanapojitahidi sana na kupewa zawadi huwafanya wajitume zaidi na hivyo kukuza ubunifu / kipaji chake. Lakini kinyume na hapo utafanya kipaji chake kipungue.
4. Ushindani wa hali ya juu. Humuweka mtoto katika mashindano yaliyo juu ya uwezo wake, humfanya awe mnyonge kwa kushindwa na hata kujidharau kwamba yeye ni mnyonge kwa kushindwa na hata kujidharau kwamba hawezi kufanya kitu muhimu. Hii humfanya asijaribu tena na tena na kumfanya apoteze kipawa chake.
5. Kulazimisha uchaguzi wa mambo mbalimbali: Kumlazimisha mtoto kufanya kitu asichokipenda badala ya kumuacha kufanya kitu anachokipenda na kukiweza zaidi hupoteza ubunifu wa mtoto.
6. Shinikizo:kumhakikishia mtoto matarajio makubwa katika shughuli anazofanya hupelekea kuporomoka katika ubunifu wake.

Mambo yanayozuia ubunifu

Kuna mambo mengi yanayozuia ubunifu yafuatayo ni baadhi ya mambo mbalimbali yanayoweza kuzuia ubunifu wa mtoto.

- Oh hapana, ni tatizo! Muda mwingine, namna ya kulitatua tatizo inaweza kuwa tatizo kubwa zaidi kuliko tatizo lenyewe. Tatizo linatakiwa lisiwe linatolewa kwa

makadirio. Watu wenye furaha huyapokea matatizo, huyatazama kama ni fursa na kutafuta namna nzuri ya kukabiliana nayo. Tatizo ni utofauti kati ya kile ulichonacho na kile unachokitaka. Kuna kitu kizuri zaidi kuliko hali ya sasa na ubunifu unaweza kukusaidia.

- Hakiwezi kufanyika. Hii ni kama kujisalimisha kabla ya vita kwa kufikiria kwamba baadhi ya vitu haviwezi kufanyika, mtu analipa tatizo nguvu kubwa ambayo haikuwa nayo mwanzo. Kukata tamaa kabla ya kuanza ni ugonjwa mbaya. Fikiria kama sisi sote tungekata tamaa katika kujaribu, mwanadamu asingeweza kuruka angani, tusingeweza kukabiliana na magonjwa na roketi zisingeweza kuruka angani. Mtazamo sahihi ungepaswa uwe hivi" jambo gumu tulifanye haraka, kila lisilowezekana tuhakikishe linachukua muda mdogo kukamilika".
- Huwezi kufanya. Au: Hamna unachoweza kukifanya. Watu wengine hufikiria, "ya kwamba matatizo yatatatuliwa na baadhi ya wataalam tu kwa sababu mimi sina ujuzi wa kutosha katika hilo. "Siwezi kutatua hilo kwa sababu mimi si mtaalam mahiri katika hilo" Kiukweli, ugunduzi mwingi kwenye viwanda umefanywa na watu binafsi (siyo vikundi vya watafiti) nje ya eneo la ugunduzi. Fikra chanya na ujuzi mzuri utatatua tatizo lolote. Kuzingatia masharti kwenye kutatua tatizo ndio msingi. Hata kama huwezi kabisa kulitatua lakini utakuwa umepiga hatua ya kukuza ufahamu.
- Huo ni utoto. Kwenye juhudi zetu ili uweze kuonesha ukomavu na usasa, mara kwa mara huwa tunakejeli ubunifu na kufanyia mzaha, ingawa ukitatua tatizo katika kunusuru ndoa yako, au kumuepusha rafiki yako na kujinyonga, je rafiki zako wanatazama mambo hayo kama utoto?" Mbali na hayo, siyo mchezo wala vituko?
- Watu watafikiri nini? Kuna kitu chenye nguvu kijamii kushinikiza kukubali, kuwa wa kipekee na wa kawaida, hii ni baadhi ya mifano:

Mtu mbunifu. Napenda kuweka maji kwenye juisi yangu ya chungwa, ili kupunguza utamu.

Mtu wa kawaida; wewe ni wa ajabu, unajua?

Mtu mbunifu: tunapika usiku sana.

Mtu wa kawaida : wewe ni chizi

Mtu mbunifu: kwanini tusiloweke majani ya vitunguu yenye ladha kali sana au majani yanayowekwa kwenye saladi

Mtu wa kawaida: kwa sababu maelekezo hayatuambii kufanya hivyo.

Maendeleo hufanywa na wale walio imara (madhubuti) kwa kuvumilia kuchekwa. Kukosea si jambo lenye kufurahisha lakini kwa hakika ni funzo (taaluma).

Thomas Edison katika uchunguzi wake wa kuhakikisha anapata taa ya uhakika, alijaribu kutumia mpaka mfano wa kidevu cha rafiki yake na vitu vingine 1800 baada ya majaribio 1000, mtu mmoja alimuuliza kama alikuwa amechanganyikiwa au? Alijibu kwa kusema! Nimejifunza mambo mengi sana mimi sasa hivi najua vitu takriban elfu moja ambavyo havifanyi kazi.

- Utashindwa, chukulia hofu yako ya kushindwa iongoze uthubutu wako na majaribio yako. Unajaribu vitu vitatu katika mwaka kwa kuwa unahakikia utafanikiwa, na mwisho wa mwaka kweli unafanikiwa 3 na kushindwa 0.
- Sasa chukulia mwaka unaofuatia hauogopi kushindwa, kwa hiyo unajaribu vitu 12, unashindwa 6 na kufanikiwa 6. Je umepataje ziada na nani kakufundisha hizo ulizoshinda

MJUZI ASIYE MIONGONI MWA WATAALAM:

- Kaka wa wright ambaye alivumbua ndege hakuwa injinia wa masuala ya anga, bali alikuwa fundi wa baiskeli
- Kalamu ya wino ilivumbuliwa na mhakiki taarifa zilizochapwa, bwana Ladislao Biro, na si fundi makenika.
- Utaalam wa hali ya juu wa masuala ya nyambizi ulivumbuliwa na muingereza clergy man G.W. Garrett na Muirish mkuu wa shule John Holland.
- Kitenganisha pamba na mbegu (cotton gin) kiligunduliwa na wakili na mwalimu, Eli Whitney
- Ugunduzi wa Kifaa maalumu cha kuzimia moto ulifanywa na ofisa wa jeshi, George Manbay
- Kamera ilivumbuliwa na wanamuziki wawili.
- Mtambo wa kuendelea kuchakata chuma na kukirusha ulivumbuliwa na fundi saa.(Uchezaji na kurusha shaba)
- Utaalam wa kutengeneza madawa ya kuchanganyia katika sabuni yaligunduliwa na wataalam wa kutengeneza Rangi.

Njia za kukuza ubunifu

Kuna mbinu kadhaa za kukuza ubunifu, baadhi yake ni hizi zifuatazo.

KUULIZA MASWALI YA KIBUNIFU: Muulize mtoto wako maswali ya hali ya juu, maswali haya yanahusisha ubongo mzima kwa sababu yanahusisha uwezo wa kuhisi, uwezo wa kujenga hoja na uwezo wa kufikiri zaidi au kwa upeo.

- Yupi atakuwa mbunifu zaidi anaye fanya mambo ya ajabu, mepesi, ya ufanisi na ya kufikirika au mwanatafakuri, au kasisi ambaye anatazama kiini cha sanaa na Imani katika namna ya kipekee?
- Je kuna yeyote anayebuni wazo jipya, au watu wanagundua yaleyale ya kale?
- Kipi ni kigumu – kuanza mradi wa ugunduzi, au kumalizia ? kwa nini?
- Ni aina ya ubunifu ambayo hupelekea watu kutatua matatizo katika misingi yake tofauti kuliko ubunifu wa kufanya sanaa

KAZI ZA VITENDO: Kuwa na siku ya kufanya mambo kinyumenyume, ukianza na mpango wa chakula kwa kufanya chakula cha usiku kuwa kifungua kinywa .

- Tumia kifaa cha kunakili au tarakilishi kukuza vitu vidogo na kupunguza ukubwa wa vitu vikubwa , tengeneza kolagi (picha itengenezwayo kwa kugandishwa vipande vipande vya karatasi, nguo, metali).
- Tengeneza mchezo wa kadi, unaweza kuanza kwa kubadilisha mchezo unaoufahamu na kisha kuubadili tena. Mfano, dhumna, mchezo wa kuzungusha vitu vyenye rangi na muunganiko wa seti mbili za dhumna.
- Jaribu kupika kwa kutumia viungo vipya na visivyo vya kawaida ambavyo hujawahi kutumia , tumia harufu kuongoza uchunguzi wa upishi wako.
- Tumia mtandao wa mawasiliano wa tarakilishi (intaneti) cheza mchezo ambapo unafuata viunganishi visivyozingatia taarifa iliyotolewa lakini kwenye herufi ya kwanza ya kiunganishi angalia ni maneno gani yasiyo na utaratibu au mpangilio maalumu na ya kufurahisha unayapata?
- Tengeneza mfano wa mazingira ambayo ungependa kuishi , tumia vitu vya kaya na vifaa vya asili tu.
- Tengeneza shairi lako mwenyewe ukitumia maneno yasiyo na mpangilio maalumu.

UZOEFU WA NAMNA NYINGI: Unganisha sikukuu mbalimbali za kikabila, kiutamaduni na kidini katika njia za kibunifu.Fikiria kwamba unatoka kwenye sayari nyingine na jifanye kwamba unatembelea sayari nyingine. Kwa kuwa kufikiria na kujisingizia au kuiga kunakuza ubunifu.

KAZI ZA BUNGUA BONGO: Mpe mtoto wako mfano wa udongo wa mfinyazi na mwambie adhani kuwa ni udongo wa mfinyazi.

- Muweke mtoto katika wakati tofauti.Kwa mfano, mwambie mtoto aeleze ni nam-na gani angepika chakula bila kutumia umeme au vyombo vya kupikia.
- Andaa orodha ya maswali ambayo unadhani hayawezi kujibika.

MCHEZO WA UBUNIFU: Wafanye watoto wako watumie vifaa vinavyo julikana katika njia mpya na isiyo ya kawaida, shiriki katika mchezo wa kuigiza na wa hiari, mchezo wa kujiongoza mwenyewe siku nzima. Anza kumfunza hayo tangu akiwa na umri mdogo sana , kucheza kunasaidia maendeleo ya mwili kwa kusaidia maendeleo ya uchunguzi kwa hisia na uwezo wa kufanya vitendo vinavyopelekea kutembea. Kwa kupitia michezo na marudio ya michezo ya viungo vya mwili watoto wanakuwa na uwezo wa kufanya kazi ngumu za kimwili kwa kadri zinavyoongezeka.Watoto wanaocheza na tofali wanakabiliwa na changamoto zinazohusishwa na vipimo, usawa, sura na mahusiano ya anga.Mchezo wa kuigiza una maanisha kuiga watu katika jamii, inasaidia jaribio la watoto na majukumu ya kijamii. Katika mchezo wa kuigiza watoto hupitia hatua kwa hatua hujifunza kupokea mahitaji ya mtu kwa mazingatio na kuthamini maadili mbalimbali. Kupitia kucheza watoto wanaweza kuonyesha na kukabiliana na hisia zao, kucheza pia kunasaidia kupunguza dhiki (msongo wa mambo) na shinikizo, watoto wanaweza kutokuwa huru kutokana na vikwazo vya watu wazima.Hakuna haja ya kuishi kwa viwango vya watu wazima wakati wa kucheza. Kama walezi tunatakiwa kuwa makini kuepuka kutawala mchezo sisi wenyewe. Mchezo unatakiwa kuwa ni matokeo ya mawazo ya watoto na usiongozwe na watu wazima, tunatakiwa kusaidia msukumo wao wenyewe na sio wetu. Kuwezesha ujuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusoma na kuwaelewa watu, unaweza kutunga mchezo wa kuandika na watoto wako, kila mtu akiwa na mhusika wa kumuiga ambaye anatakiwa kuzielewa hisia zake na kisha kujifunza sehemu yake kwa kusoma vifungu vinavyohusika nae. Waambie watoto waigize igizo zima kwa ajili yako na lote liandaliwe na wao wenyewe wakiwa na mavazi rahisi.

Uandishi wa Watoto

Watoto wasio na ujuzi wa kusoma wanaweza kukupa hadithi ya kuandika na kisha wanaweza kuionesha. Punde tu mtoto wako anapoweza kueleza baadhi ya maneno kwa ufasaha anaweza kuanza kuandika, usijali kuhusu usahihi wa kiuandishi kwa wakati huu. Usahihi wa kiuandishi na mambo mengine yatafuata baadaye. Punde tu mtoto wako anapokuwa na shauku kuhusu kuandika unaweza kuanza kumfundisha njia za uandishi zinazotumiwa na watunzi wa vitabu. Kwa kawaida mwandishi anaanza na rasimu isiyorasmi na hatua kwa hatua anaichukua mpaka inakuwa tayari kuchapishwa.

Njia nzuri ya kufundisha jambo hili ni kumwambia mtoto wako kuchagua hadithi anayoipenda na kisha kumsaidia namna ya kuandika hadithi hiyo kwa ufasaha zaidi. Hadithi hii inaweza kuandikwa katika kitabu kidogo, watoto ambao umri wao ni mkubwa wanaweza kufanya kazi bora na za ajabu kabisa katika kutengeneza vitabu kwa kutumia tarakilishi(kompyuta).Usisahau umuhimu wa kusoma, waandishi wazuri ni wasomaji wazuri na kusoma kutampa mtoto wako mawazo mengi ya ubunifu ya kuandika.

Usanii kwa Watoto

WAPATIE WATOTO KAZI ZA SANAA AMBAZO NI ENDELEVU

Badala ya kuonesha mfano wa kazi ya sanaa kwa watoto kuiga, hamasisha watoto watumie mawazo yao. Badala ya kupitia kurasa za vitabu vya rangi, yenye mistari ya michoro inayofanana, wasikilizishe mashairi au muziki wenye mafunzo na waambie waeleze wanachosikia.

TENGENEZA MAZINGIRA AMBAYO YANAIMARISHA MILANGO MITANO YA FAHAMU

Waruhusu watoto wahisi msokotano wa karatasi, wanuse harufu ya kalamu laini (chaki au kalamu ya risasi), wasikilize sauti ya kalamu inayochongwa na waangalie mabadiliko ya rangi zinapochanganywa.

HAMASISHA UCHUNGUZI WA HIARI (BINAFSI)

Mara kwa mara toa au sambaza vifaa vya msingi vipatikanavyo kwa urahisi kama vile chaki, kalamu ya risasi, brashi, karatasi za kujengea na rangi. Waruhusu watoto watambue sifa za vitu hivi.Watoto wanaweza kutumia vidole vyao kama brashi za rangi? watoto wanaweza kuchora picha kwenye ardhi ya vumbi kwa kutumia fimbo? kufanya miili yao kuwa na umbo linalofanana na mti? Kueleza rangi ya zambarau inafanana na kitu gani? Kutembea katika chumba kwa furaha, huzuni au kwa namna ya kuchekesha?

ACHA KUKOSOA KILE UNACHOFIKIRIA NI KAZI MBAYA

Tunatakiwa kuwalinda watoto wetu kutokana na suala zima la kukosoana na kuhukumiana kutoka kwa vijana wa rika lao , watu wazima na hata wao wenyewe. Hakuna baya au zuri, kila uumbaji ni wa kipekee.jambo hili ni muhimu hata kabla mtoto hajaanza shule. Katika sanaa kila mmoja ni bosi wa kazi yake mwenyewe na anaweza kuifanya kwa njia yoyote aitakayo, watoto wanakuwa na wasiwasi na mashaka ikiwa kazi zao mara kwa mara zinaelezwa kuwa mbaya au hazijakamilika

Imani potofu: Mawazo ya ajabu au yasiyo na tija

Baadhi ya sifa za kipekee ambazo watoto wabunifu wanazikuza zinaweza kutazamwa na wengine kama za ajabu au zisizo na tija. Ifuatayo ni mifano michache juu ya hayo;

Fikra huru: Pindi mtoto mbunifu anapozungumza juu ya fikra zake, anaweza tazamwa kama asiye na nidhamu na ni mwenye vurugu.

Mwenye kudanganya: Watoto wabunifu wanapata msisimko kuhusu mawazo ya ajabu na wanaweza wasione hasara au kasoro ambazo mtu mzima angeziona kwa urahisi.

Ucheshi: Watoto wabunifu wanapata vichekesho katika mawazo ambayo watu wazima wanayachukulia kuwa na uzito. Huu uwezo wa kuuliza na kuona mitazamo mingine inaweza kutafsiriwa kama mzaha na karaha.

Ndoto: watoto wabunifu wanajifunza kutokana na ndoto na wanatatua matatizo yao mengi kwa kutumia ndoto. kuunda mahusiano mapya ingawa inaweza kuonekana kama ni kughafilika au kuchanganyikiwa.

Upweke: Ubunifu unatokana na mawazo rahisi yasiyokomaa, watoto waweza hitaji kuwa peke yao wakati fikra zao zinaibuka.

Shughuli: Mawazo yaweza kuja katika wakati wa utulivu (mapumziko). Mawazo yanapokuja mtoto mbunifu atakuwa ameshughulishwa. Namna nzuri ni kuwa na kalamu ya risasi katika mahala au sehemu za kimkakati nyumbani kwa ajili ya watoto kuweka kumbukumbu ya mawazo yao.

Ubunifu ni zawadi yenye maana sana kwangu kuliko kipaji changu cha kujifunza maarifa mazuri.

ELBERT EINSTEIN

Wazazi wafanye nini?

Andaa mfano: Msifie mtoto wako kwa kumuonesha kuwa ni mdadisi, mwenye fikra za shauku na za kiuwendawazimu. Kuwa muwazi kwa ugunduzi mpya, shirikiana na wenzako kwa ubunifu wako, furahia maslahi ya mtoto wako.

Muamini mtoto wako: mtoto anayejihisi kupendwa na kuaminiwa anajenga kujiamini kwa kuwa tofauti na kuwa na shauku ya kuvumbua.

Kuongezeka kwa wasiwasi wa mapatano ya kijamii au kubaguana kijinsia kwaweza zuia hali ya ubunifu.

Mpe matumaini: zidisha matumaini kwa mtoto katika kufanya majaribio na uchunguzi. Kiutendaji msikilize mwanao kuliko kuwa mtoa hukumu.

Muunge mkono mtoto pindi anaposhindwa. Epuka matumaini hewa

Boresha mazingira: Mpatie mtoto vifaa ambavyo vitamsaidia katika ubunifu na kumuwezesha mtoto kuandaa kazi zake za sanaa yeye mwenyewe. Vitu vya kale kama magazeti, vitabu, majarida, michezo, nguo, vito vyaweza tumika katika miradi tofauti. Vitofali vya bandia vyaweza tumika katika utengenezaji wa mto na foronya.

Angalieni TV kwa pamoja: Mawazo yamebadilika kwa kuwa na ushawishi hasi kutoka katika TV. Lenga katika makala na uwaache watoto watoe fikra zao katika mjadala.

Msaidie mtoto katika kuweka kumbukumbu: Watoto wanapenda kuchora na kupaka rangi, tangu wakiwa katika umri mdogo, kabla hawajaanza kuandika, wanaweza kuelezea fikra zao kwa watu wazima au watoto wenzao. Baadaye waweza kumpa moyo wa kuandika katika shajara au jarida.

Ya kuzingatia katika midoli (wanasesere).

Fikiri juu ya midoli (wanasesere) unayowanunulia watoto zako lazima ununue midoli itakayokuza ubunifu na inayoendana na kujifunza. Sanamu zenye umbo la tofali za kujengea zinahamasisha kufikiri. Baadhi ya midoli kama (bratz) inaleta mkanganyiko katika masuala ya jinsia. Kuwapo kwa midoli ya kuchezea ni jambo la muhimu kwa afya ya watoto.



Fikiri juu ya wanasesere unayowanunulia watoto zako lazima ununue midoli itakayokuza ubunifu na inayoendana na kujifunza. Sanamu zenye umbo la tofali za kujengea zinahamasisha kufikiri.

Na pia ipo midoli maalumu kwa watoto wenye ulemavu ambayo imetengenezwa na wataalamu ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili watoto.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI 62: MAZOEZI NDANI YA FAMILIA KATIKA KUKUZA UBUNIFU

Jaribu nyenzo za kibunifu zifuatazo pamoja na watoto:

1. **Tumia michezo ya kibunifu:** michezo kama vile "kumfuata kiongozi" inawasaidia watoto katika masuala mazima ya kutembea na wanajenga tabia ya kuwakubali wengine na kuwa kama mfano wao. Shughuli za ujenzi unaweza tumia vifaa rahisi (matofali, udongo, mchanga, maji) ambavyo vinawawezesha watoto kujenga na kubuni maumbo tofauti tofauti.

2. **Tumia mitazamo ya hadithi endelevu:** mmoja wao anaanzisha hadithi na baadaye kila mmoja aendeleze kipande chake. Soma hadithi na kisha toa onesho. Tumia udadisi kufanya igizo hilo

3. **Tumia vitu kubuni mawazo mapya:** tumia mchezo wa kuvunjavunja mnyama- na kila mtoto achague kipande kimoja; na akizingatie, kisha mtoto aige kuwa kama mnyama yule kwa dakika 1-2. Tumia mwendo wa kubuni wa mnyama huyo kuwaonesha namna afanyavyo.

4. **Tumia michezo ya kuiga:** michezo ya kuiga huwasaidia watoto kuelewa mitazamo ya wengine na kuchukua fikra zao.

5. **Uliza maswali ya wazi:** waoneshe watoto picha kisha waulize maswali. Kwa mfano: "watu katika picha ile wanafanya nini?" wanasema nini? "Ulifurahia nini katika siku yako ya leo?" badala ya kuuliza: vipi leo siku yako imeenda vizuri?

6. **Waache watoto watumie milango yao ya fahamu:** Waambie watoto wafumbe macho yao na kisha uwaulize ulichoweka katika mikono (kipande cha jiwe, ufutio,) Waambie wazibe masikio yao kisha wakisie wanachosikia (tumia sauti kama mlio wa sarafu idondokapo, kusugua karatasi, kuchana karatasi, kuchanga karata,)

7. **Waulize watoto kuhusu mabadiliko:** waambie wabadili vitu ulivyowapa ili viwe katika namna waitakayo wao. Kwa mfano

- Nini tufanye ili, tubadili tamu kuwa chungu
- Nini tufanye ili, tubadili ndogo kuwa nzuri
- Nini tufanye ili, tubadili ya haraka iwe nzuri Zaidi
- Nini tufanye ili, tubadili tulivu iwe bora Zaidi
- Nini tufanye ili tubadili kikubwa kiwe cha kufurahisha
- Nini tufanye ili tubadili kilichopita kiwe na msisimko
- Vipi itakuwa kama matamshi ya kiingereza yataandikwa kama yanavyotamkwa. Jaribu kuandika ibara kwa kutumia mtindo huo. Je kuna lugha mfano wa hiyo, je unaweza kutupa mfano wa lugha hiyo

8. **Uliza maswali yenye majibu mengi:** ifuatayo ni baadhi ya mifano kwa kutumia dhana ya maji (dhana nyingine ni kama: moto, upepo, mchanga, gari, moshi, barafu):

- Maji yanamatumizi gani?
- Nini kinaweza elea kwenye maji?
- Maji yanamsaada gani kwetu?
- Kwanini maji baridi ni ya baridi?
- Vitu gani hukaa ndani ya maji
- Maji yanaweza yakawa na rangi gani nyingine tofauti?

9. **Uliza maswali katika mtindo wa "nini kitatokea ikiwa….."**

- Nini kitatokea kama miti yote itakuwa rangi ya bluu?
- Nini kitatokea kama magari yote yatatoweka?
- Nini kitatokea kama watu wote watavaa nguo zinazofanana?watakuwa na majina sawa?
- Nini kitatokea kama utakuwa na uwezo wa kupaa?
- Nini kitatokea kama watu wote hawatofanya usafi katika nyumba zao?
- Nini kitatokea kama watu wote watakuwa wema au watakuwa waovu?
- Nini kitatokea kama watu wote watakuwa wagonjwa au watakuwa na afya njema?

10. **Uliza maswali katika mtindo wa "namna zipi au tofauti ……"**

- Kijiko kinaweza tumika kufanya nini na nini?
- Kifungo kinaweza tumika kufanya nini na nini?

- Kamba inaweza tumika kufanya nini na nini?
- Kibandika picha chaweza tumika kufanya kazi gani nyingine?

ZOEZI 63: TABIA ZENYE TIJA!

Kipindi wahyi (ufunuo) wa kwanza unamshukia Mtume, aliogopa sana na kuamua kurudi nyumbani kwa mke wake. Mkewe akamliwaza na kumuorodheshea miongoni mwa tabia zake njema.

- Kutembelea majirani
- Kusaidia wanyonge
- Kujitolea kwa mafukara
- Kuwakirimu wageni na
- Kusaidia wagonjwa

Jadili na watoto wako umuhimu wa kila tabia mojawapo. Andika pamoja nao hadithi inayojumuisha tabia hizo.

ZOEZI 64: KUELEZEA MASWALI MAGUMU.

Kusanya baadhi ya wazazi na mjadili kwa pamoja namna ya kujibu maswali yafuatayo, ambayo huulizwa na watoto mara kwa mara. (uliza wenzako kwa msaada zaidi).

- "Nani kamuumba Mwenyezi Mungu?" kwa nini MwenyeziMungu atawaadhibu watu wasiomuamini?" "kwa nini watu wengi hawafuati mwongozo wa Mungu Muumba?" vipi tutaishi milele peponi bila kupata usumbufu wa aina yeyote
- Namna gani tutaelezea dhana ya "utashi" na "utambuzi" katika namna ya kutia moyo katika upande mmoja na kukubali matakwa ya Mungu katika upande mwingine?

Sisi tumetoka wapi? Sisi tutaishia wapi? Peponi kukoje? Tunaweza kumuona Mungu? Mungu anaweza kumfanya kila mtu amuamini yeye? Kwa nini hafanyi?

Haya ni maswali ya kimtego kutoka kwa watoto. Tunahitajika kuwajibu kutokana na umri wao na ukomavu wao.

Katika sura ya kuonekana pepo, Mtume (s.a.w)alieleza kwamba pepo ni nzuri sana na ya kipekee kiasi kwamba hakuna jicho lililowahi kuiona , hakuna sikio lililowahi kusikia na wala hakuna akili ambayo imewahi kufikiri , kwa ujumla ni mfumo mpya wa maisha ya milele ambao hakuna fikra za binadamu zenye kuuelewa.

ZOEZI 65: NI MTAZAMO WA WEZI NDIO UNAOSAIDIA!

SULUHISHO LA KIBUNIFU

Waache watoto wasome kisa cha kweli kifuatacho. Kisha fikirini kwa pamoja baadhi ya matatizo yanayo zikabili familia na namna ya kuyatatua.

> Pindi mkurugenzi mtendaji wa shirika la ndege la Amerika alipomuona mlinzi amesimama katika uwanja wa ndege alimuuliza meneja, "tunaweza punguza gharama?" meneja alijibu kwa kuuliza kivipi? Mkurugenzi alisema kwamba, kama watakuwa na mlinzi kwa nyakati za usiku kwa siku tatu tofauti tofauti. Wezi hawatojua usiku upi ndo kunakuwa na mlinzi. Mwaka uliofuata swali hilohilo likaibuka tena katika namna ya kupunguza gharama, na jibu lilelile likatolewa: kivipi?" mkurugenzi akapendekeza ya kwamba badala ya mlinzi awekwe mbwa mkali. Mwaka wa tatu swali lilelile likaulizwa, na suluhisho ikawa awekwe mbwa kwa muda wa ziada tu. Mwaka wa nne, mkurugenzi akamwambia meneja: kwa kuwa ni mtazamo wa wezi ndio unaosaidia, kwa nini usimuache mbwa na njaa kisha urekodi sauti yake kisha uwe unailiza nyakati za usiku kwa namna tofauti tofauti?" Itafaa, itasaidia kutokuwa na mlinzi wa usiku. (MSNBC, NOVEMBER, 3 2007)

24

SURA YA ISHIRINI NA MOJA

- WATOTO WANAODEKEZWA DHIDI YA WATOTO WANAOJITAMBUA

SURA YA ISHIRINI NA MOJA **512**

Watoto wanaodekezwa dhidi ya watoto wanaojitambua **512**

Kujitambua 514

Vipi tutadhibiti malezi ya watoto wanaodeka? 516

Kazi za Kufanya

Upendo, ujasiri, ubunifu, uaminifu na hali ya uwajibikaji vinajenga kujiamini na kujitambua.

Kujitambua

Watoto wanahitaji kutiwa moyo ikitokea wamefanya makosa kama vile wanavyotiwa moyo wanapokuwa wamepatia. Ukweli ni kuwa kukosea ni sehemu ya maisha. Lamsingi ni kuwafundisha watoto wayatazame makosa yao kama somo la kufanya maboresho pale walipokosea na si kuona kama wameshindwa. Kukosea kusifanywe kama ni sehemu ya kuwavunja moyo watoto. Tumia kukosea kama mbadala wa kuwatia moyo watoto. Ipo tofauti kubwa baina ya kusema!, “kwa nini unakuwa mpumbavu” na kusema “najua kwamba unajua na unao uwezo!” Kutia moyo kunawasaidia watoto kujifunza na kufanya vizuri zaidi wakati wa baadaye. Watoto walioambiwa na watu wanao waamini sana kwamba hawawezi basi hupelekea watoto hao kutoweza kweli kwa wakati wa baadaye.

Fikra zenye kuvunja moyo kama vile “Nimefeli, kwa hiyo mimi si chochote,” hupelekea kupunguza uwezo wa mtoto kufurahia maisha katika siku za mbeleni, hupunguza nguvu za hisia na kukuza uwezekano wa kutafuta njia rahisi ya kuondokana na msongo. Watoto wasio jitambua hawatoweza kutumia jitihada zao katika kufikia malengo wanayodhani hayawezekani.

Upendo, ujasiri, ubunifu,uaminifu na hali ya uwajibikaji-iwe moja kwa moja au kinyume chake inaimarisha kujiamini na kujitambua. Sifa hizi zote zinaingiliana na kuimarisha kati ya moja na nyingine.

Mafanikio kutokana na jitihada (kwa kusoma na kukataa shinikizo rika) yanahitaji kujitambua. Watoto wasio jitambua wana mihemko ya hali ya juu na hawajali matokeo ya matendo yao. Watoto wasiojitambua hawatoweza kutumia uwezo wao katika kufikia malengo waliyojiwekea. Wana ujasiri mdogo katika kufikia malengo yao. Watoto wasiojitambua wanakabiliwa na tatizo la kutaka kukidhi matamanio yao yawezekana kwa kutumia pombe, dawa za kulevya, vitendo vya kujamiiana na vurugu kama namna ya kujipatia furaha.

Watoto lazima wafundishwe kwamba wao hawana walichopungukiwa, na watazame makosa waliyoyafanya kama fursa muhimu ya kujifunza. Watoto hawa bado wana nguvu ya kufanya chaguzi muhimu juu ya kipi kizuri (kusoma kwa ajili ya maandalizi ya mtihani badala ya kufanya matembezi ya starehe pamoja na marafiki). Wana matumaini, na wanaamini kwamba watafanikiwa (kwa jitihada zao na kufanya kazi kwa bidii). Wanagundua faida za jitihada zao na kujiona wao wenyewe ni washindi. Furaha inayofuatiza mafanikio yao inadhihirisha ya kwamba watatafuta mafanikio zaidi wakati wa baadaye.

Vipi tutadhibiti malezi ya watoto wanaodeka?

Watoto ni lazima wajifunze namna ya kukabiliana na ushindani na msongo. Watoto wanahitaji wafundishwe namna ya kusema “hapana” kutoka kwa wazazi wao ama kwa marafiki, walimu, majirani na wageni. Fundisha watoto wako namna ya kujiepusha na kukata tamaa, kukanushwa na kukataliwa. Zifuatazo ni njia za kuzuia kutoharibika kwa mtoto.

USIDHOOFISHE MAADILI.

Baadhi ya wazazi wanatabia ya kudekeza watoto. Ziada ya namna yeyote, iwe mwanasesere (kidude cha kuchezea) michezo, fedha, au chokleti, vinaweza waharibu watoto katika umri mdogo kabisa. Watoto waliokulia katika familia za kitajiri wanaweza kuharibika kama watapatiwa kila kitu kwa kiwango cha juu zaidi. Wazazi hawatakiwi kuwapa watoto zaidi ya vile ambavyo vinahitajika. Lazima watoto waandaliwe kujua kwamba katika maisha kunakipindi cha hali ngumu na kipindi cha hali nzuri.

USITOSHELEZE KILA HITAJIO.

Wazazi hupata utulivu wanapotosheleza matakwa ya watoto zao. Ingawa mzazi anaweza kuacha kwa makusudi baadhi ya matakwa bila kuyatekeleza. Ikiwa kila hitajio na tamanio la mtoto litatoshelezwa, makuzi ya mtoto yanaweza kumfanya kuwa mtu mtukutu.Watoto wa namna hii si wenye mantiki, wakorofi, na waliokata tamaa.

Hawatokuwa na uwezo wa kukubali kuwa wameshindwa katika usaili kwa ajili ya kazi baadaye maishani mwao. Wana kuwa katika hatari ya kukabiliwa na msongo na hawawezi kujiepusha na kukata tamaa.

ZUIA ULINGANISHI

Wazazi wanatakiwa kuwafunza watoto wao kuacha tabia ya kulinganisha walivyo navyo na vile walivyo navyo wenzao. Ikiwa mtoto anahitaji kitu cha kuchezea kwa sababu tu amekiona kitu kama hicho kwa mwenzake, hitajio hilo lazima lipuuzwe. Watoto hawa huishia kujilinganisha mara zote na watu walio na ziada ya walivyonavyo wao.

EPUKA KURIDHISHA.

Ili kuepusha mizozo baadhi ya wazazi hupendelea mara kwa mara kuwaridhisha watoto wao. Kumridhisha mtoto kuna manufaa ya muda mfupi lakini kuna madhara ya muda mrefu. Watoto hupunguza heshima kwa wazazi wa namna hiyo. Wazazi wanatakiwa kuwa waaminifu na kusema hapana kwa hitajio lisilo la lazima. Huwezi egemeza maisha yako yote kwenye mahitajio ya mtoto.

USIJITIE HATIANI.

Baadhi ya wazazi wanakawaida ya kuridhisha watoto kwa kujitia hatiani. Kwa mfano, wazazi wa kike wanaofanya kazi hurejea nyumbani wakiwa wamechelewa, na hawana muda wa kuwasaidia watoto kazi za shule. Mtoto anaomba asikirimu kabla ya chakula cha usiku, mama anaridhia matakwa ya mtoto. Mto-

to anauelewa wa kutosha kujua kwanini anahongwa. Wazazi wanatakiwa wawe na ujasiri kuwaambia watoto hapana pasi na kujali hamaki ama ghadhabu kutoka kwa mtoto.

HAMAKI : USIRUHUSU KILIO KITUMIKE KUWA NI NYENZO

Kuna kilio ambacho huwa kinatokana na sababu za msingi (mfano: njaa, homa, maumivu na hofu). Mambo hayo yanahitaji uangalizi wa mzazi.

Kuna aina nyingine ya kulia ambayo ni zao la ghadhabu/hamaki. Mtoto anahitajia kitu fulani ambacho si muhimu kwa hiyo analia na kupiga kelele. Aina hii ya kilio ni lazima ipuuzwe. Isipopuuzwa itaanzisha tabia nyingine. Tabia ya kupiga mayowe itakuwa inaongezeka mpaka mzazi akidhi haja ya mtoto. Mtoto atajifunza ya kwamba anao uwezo wa kumdhibiti mzazi wake kwa mambo yasiyo na maana. Kama kilio ni sehemu ya kiburi basi puuzia. Usimkaripie mtoto, kaa kimya na umdhibiti na kubali hisia za mtoto. Usikubali kushindwa. Ghadhabu zikiisha mtoto atajifunza ya kwamba kulia kusikokuwa na sababu ni tabia isiyokubalika.

Watoto wanahitaji kufundishwa kusema “Hapana”, kutoka kwa wazazi, marafiki, walimu na majirani.

KAZI ZA KUFANYA



ZOEZI LA 66: (JARIBIO LA KUJIIMARISHA)

Sifa nyingi za haiba iliyo nzuri huwa zinaingiliana kati ya moja na nyingine. Katika mpango mzuri wa familia. Wahusika wote wa familia wajadili umuhimu wa kujiimarisha na kujibu maswali yafuatayo.

- Je ninatekeleza ahadi?
- Je nawaheshimu wakubwa zangu?
- Je naheshimu masharti niliyojiwekea?
- Je nalipa madeni kwa muda?
- Je narudisha nilivyoazima kwa muda?
- Je nazingatia tarehe ya mwisho iliyopangwa kukamilisha jambo?
- Je naswali kwa kuchunga muda?
- Je nipo sahihi katika utekelezaji wa majukumu?

ZOEZI LA 67: KURIDHIKA

Soma hadithi hii kisha akisi/linganisha utekelezaji katika familia yako, ndugu zako na marafiki zako.

Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) amesema: “Ridhika na kile alichokupa Mola wako, utakuwa ni tajiri wa watu”

Mmoja wa maswahaba wa Mtume (s.a.w) alikuwa ana tabia ya kuswali nyuma ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) na nguo yake ilikuwa joho lililochakaa ambalo hakuwa analibadilisha, Mtume alimnakili kwa kuwa alikuwa mara tu baada ya swala hutoka. Mtume aliuliza juu ya huyu bwana, yuko wapi? Akajibiwa ya kwamba amekwisha kwenda nyumbani kwake. Mtume akaomba aitiwe, yule bwana aliitwa akaja. Mtume akamuuliza kwa nini unaondoka haraka haraka na haukamilishi swala zako? Yule swahaba akajibu: Kwa sababu mimi na mke wangu tunategemea nguo hii moja, kwa hiyo natoka haraka mara baada ya swala ili nimuwahishie mke wangu nguo

hii hii naye akaswali ili asipitwe na muda. Kwa hali hiyo Mtume akampa shati lake, yule swahaba alilichukua lile shati kwa furaha na kwenda nalo kwa mke wake, mke akauliza: "hili shati ni la nani?" alijibu: "ni shati la Mtume; ametupa sisi." Ulilalamika kwa Mtume juu ya hali hii aliyotujaalia Mungu?" Alijibu: Naapa kwa Mungu sikulalamika kwa Mtume juu ya hali yetu aliyotujaalia Mungu, kwa hakika nimepokea shati hili kutoka kwa Mtume na itakuwa ndo sanda yangu nikiwa kaburini!"

IMAM AL-GHAZALI, IHYA' ULUM AL -DIN

ZOEZI LA 68: USHIRIKIANO WA PAMOJA

Soma na watoto wako taarifa ifuatayo, kisha husianisha vitu maalumu kutokana na uzoefu wao wenyewe.

Ufanisi katika kujifunza hutokea ikiwa watoto watashiriki moja kwa moja kufanya uchunguzi wa mazingira yaliyowazunguka: jaribu kuonesha vitu katika hali halisi,wakianguka na kutaka msaada. Kisha waache waeleze fikra, mawazo na hisia zao juu ya kile wanachokiona. Wazazi wafundishe mawazo yao, wakati watoto wakifanya uchunguzi. Wape watoto fursa ya kujaribu na kutumia taaluma yao katika kipindi chote cha mafunzo. Msemo ambao rais Obama alikuwa akiutumia katika kuonesha hali halisi.

Mpe mtoto muda wa kufikiri, kufanya mizunguko, avute pumzi ndefu, aeleze kuchanganyikiwa kwake na kufikiri kwake. Hii sio alama ya udhaifu, kiuhakika anafikiri na anajaribu kujua nini cha kufanya juu ya kile alichonacho. Kwa bahati mbaya, wazazi wengi hujibu maswali ya watoto kwa niaba yao, kuwapa suluhisho kipindi cha changamoto, na kuyachukua kama yao pindi mtoto anaposhindwa kuyatatua. Hali hii huleta athari mbaya katika kujiamini kwa mtoto, uwezo wa kutatua matatizo, uvumilivu,na kukosa ujuzi wa kufanya makubaliano. Wamejifunza kuwategemea wengine katika kutatua matatizo yao. Mzazi ni lazima achukue nafasi ya kuwa mtaalamu, kocha na kuwa mshauri. Mpe mtoto fursa ya kutumia maarifa yake, ujuzi na uwezo wake. Mzazi ni lazima awe muongozaji na msaidizi katika masuala ya kufikiri kwa mtoto anapokabiliwa na changamoto, kwa kutumia uwezo wa mtoto mwenyewe.

Wazazi wasiogope kukosea kwa watoto. Msaidie mtoto kuelewa wapi amepatia, alipokosea, kwa nini amefanya hivyo, vipi anaweza kufanya vizuri zaidi kwa baadaye. Kipi walichojifunza kutokana na uzoefu huu. Si lazima iwe ni kazi halisi. Jitihada katika kufikiri juu ya kazi iliyofanyika na kuepusha kurudia makosa kwa mara nyingine ni muhimu sana.

Kupitia ushirikiano wa moja kwa moja kati ya mzazi na mtoto hupelekea kukuza na kuimarisha mahusiano. Mara tu uhusiano huu unapoimarishwa hupelekea mtoto kuwa huru kumkabili/kuwasiliana na wazazi wake pindi changamoto zinapojitokeza na zinapokuwa ngumu katika nyakati za baadaye za kutafuta maisha.

22

SURA YA ISHIRINI NA MBILI

- KUMCHAGULIA MWANAO RAFIKI MWEMA

SURA YA ISHIRINI NA MBILI **520**

Kumchagulia Mwanao Rafiki Mwema **520**

Marafiki wa mtoto wako 522
Aina za marafiki 524
Matatizo yatokanayo na marafiki wabaya 525
Vishawishi vya kila siku vya makundi shuleni 525
Kuchagua rafiki wema 525
Itakuwaje endapo mtoto wako atachagua marafiki wasiofaa? 526
Kwanini kuna vitu vyenye kuwavutia zaidi vijana? 527
Mahusiano mbalimbali ya kijamii 528
Familia zinapokuwa katika mazingira mabaya 529
Kazi za Kufanya

"Ni siku ambayo mtu muovu atang'ata mikono yake huku akisema,...Laiti kama nisingemfanya fulani kuwa rafiki yangu mimi!...
(Qur,an 25:27-29)

Marafiki wa mtoto wako

Katika somo la fizikia, vitu vyenye chaji sawa hukwepana ila vile vyenye chaji tofauti huvutana. Kwa upande wa wanyama "ndege wafananao manyoya yao, huruka pamoja". Binadamu huwa tunaanzisha uhusiano wa kirafiki na watu tunaokutana nao kama vile majirani, watoto, wafanya biashara sokoni na kadhalika. Kila mmoja kati ya hawa tunatakiwa kuwaonesha ukarimu na heshima. Pia siyo vizuri kujenga urafiki na watu ambao wanaweza kuharibu maisha yetu. Chagua muumini wa kweli awe rafiki yako. Marafiki wa aina hii hawaoni tabu wanapokuwa katika mchezo kusitisha mchezo huo kwa ajili ya kwenda kufanya ibada pamoja nawe. Na wao huwa wanaweza kutambua kwanini wewe kama rafiki yao hutumii kilevi au dawa za kulevya.

Wakati mwingine inakuwa vigumu kuanzisha urafiki na watu wenye tabia kama yako sababu huwa mnaishi mbali mbali. Hata watoto wao hawaendi shule ambayo watoto wako wanasoma. Hata hivyo bado inawezekana kupata rafiki wa karibu kutoka katika familia nzuri ya Imani yoyote ambao wana maadili na tabia yenye kufanana na wewe na akaheshimu utamaduni wako. Vikundi vilivyopo katika jamii kama vile vikundi vya michezo, skauti na vikundi vya wanamazingira huweza kuwa sehemu muhimu katika kujenga urafiki.

Rafiki mzuri huwa mkweli, mkarimu, mwenye huruma na huelewana na wenzake. Mtu mzima huwa na taratibu zake katika maisha lakini taratibu hizi huenda zikapingana na taratibu za vijana na kufanya vijana kutozikubali taratibu zako mtu mzima. Marafiki wanamchango mkubwa sana katika kushawishi vijana.Watajaribu kwa namna ya mavazi, mwenendo na kujifananisha na watu wengine.

Watoto wa kike hupenda kuunda urafiki

na mtu mmoja mmoja au kikundi cha wasichana wachache. Ila watoto wa kiume hupendelea zaidi kuunda urafiki katika makundi makubwa ya watu au watu ambao huwa wanapenda kitu fulani kwa pamoja kama vile michezo. Urafiki huu ni muhimu na huweza kuwa wa karibu mno. Lakini pia urafiki huu unaweza kuvunjika pale itakapoonekana kuwa mmoja kati yao amevunja masharti ya utii.

Mzazi hatakiwi kuchukia pindi anapoona mtoto wake anapenda sana marafiki kuliko anavyoipenda familia yake. Hautatakiwa kujitahidi kutunza undugu tu kwa kuwa umezaliwa nao, unachotakiwa kufanya ni jinsi ya kuwa nao ndugu kwa furaha, kwa sababu wanakupenda na kukujali. Lakini marafiki, unatakiwa uwatafute mwenyewe, watatakiwa washawishike kwa kuwa ni mtu unaependeka, unatakiwa uugharamie urafiki wao. Zingatia kuwa marafiki ni chanzo cha familia za kesho. Kuna usemi wa Kiitaliano unaosema kuwa “Mnunue ng’ombe anayetoka katika zizi lako” ukiwa una maanisha kuwa ni bora kukiendea kitu ambacho unakifahamu vizuri.

Jenga marafiki zaidi ya elfu lakini usitengeneze adui hata mmoja

Swali: kuna ufanano gani kati ya mpira wa miguu nchini Marekani na kiongozi mwadilifu?

Jibu: ufanano wao upo katika kuhitaji uimara, ujasiri na matumaini

Swali: kuna ufanano upi kati ya wanajeshi na wanachama wa kundi la Mafia?

Jibu: wote wanahitaji ukweli na ujasiri, wanajeshi wanatakiwa kuwa hivyo kwa nchi yao na kundi la Mafia kwa wanachama wake. Wanajeshi wanafanya kazi isiyodhuru watu kwa manufaa ya watu wakati kundi la Mafia wanafanya maovu.

Aina za marafiki

- **Wafanyakazi wenza:** hawa ni marafiki ambao kijana hukutana na hujenga nao uhusiano wakiwa wanafanya shughuli fulani kwa pamoja kama vile ofisini au shuleni. Inaweza kutokea kutowapenda sana lakini huwa inawalazimu waunde urafiki ili waweze kufanikisha shughuli zao.
- **Marafiki wa kufahamiana tu:** hawa ni marafiki ambao huwa hatuwafahamu vizuri kiundani. Kutokana na sababu hii huwa hatuwajali na kuwapenda sana.
- **Marafiki wa kawaida:** hawa ni marafiki ambao tunawajua vizuri na tunawapenda. Huwa ni miongoni mwa wale tuliokutana nao shuleni ama kuwa majirani zetu
- **Marafiki wa karibu:** hawa ni marafiki ambao taarifa zao zinajulikana vizuri zaidi na huwa wanaweza kuwajali wanapokuwa na matatizo. Huwa wanafaa katika utetezi na pia kuwategemea kwa chochote.
- **Marafiki walio bora:** hawa huwa tunawapenda sana. Huwa tunawaweka wazi kila kitu ili waweze kufahamu na haijalishi namna wanavyoweza kutofautiana kimawazo na siku zote huendeleza urafiki katika ngazi ya urafiki bora.

Urafiki ni sawa na kamba yenye ncha mbili. Hakuna awezaye kuunda urafiki na mtu ambaye hayupo tayari kuunda urafiki nae. Unatakiwa ujitolee kwa rafiki yako kama yeye anavyojitolea kwa ajili yako, yaani uweze kumvumilia kama yeye anavyokuvumilia, umpende kama anavyokupenda, uweze kumjali kama yeye anavyokujali n.k. Lazima pia uwe karibu na rafiki yako.

Watu wengi huweza kubadilika. Wazazi wanatakiwa wawaeleze vijana wao kuwa hawapaswi kujilaumu pindi marafiki zao wanapokuwa katika wakati mgumu au matatizo au wanapokuwa wanafuraha zaidi ya kawaida yao. Urafiki unahitaji kila mmoja aweze kuwa mwazi kwa mwenzake hivyo mweleze mwenzako hali iliyopo.

Wazazi huchukia wanapoona watoto wao wanakuwa na marafiki wabaya kwa vile watoto hao (ambao ni marafiki kwa watoto wao) wana maadili yasiyokubalika na pia yenye kupingana na mafunzo waliyotoa kwa watoto wao.

Marafiki wabaya hawana tabia ya kumuogopa Allah, pia huwa wanavuta sigara, bangi, wanatumia dawa za kulevya, wanatumia lugha chafu, mara kwa mara wanaingia katika migogoro na askari polisi au kuhamasisha tabia mbaya na hatarishi. Zingatia kuwa baadhi ya hawa 'marafiki wabaya' wanaweza kuvutiwa na tabia nzuri ya watoto wako na familia yako pia.

Matatizo yatokanayo na marafiki wabaya

- Wanaweza kuharibu mali zako
- Ni wakatili na waovu
- Wanaweza kutawala nyumba yako
- Wanakutia uoga na kukupuuza
- Wanakuhuzunisha pindi wanapomchukua mtoto wako na kumhamasisha katika kutenda maovu

Vishawishi vya kila siku vya makundi shuleni

Mfumo wa elimu uliopo shule huweza kumfanya mtoto aingie katika makundi fulani ili aweze kukubalika kwa wenzake kama miongoni mwa wanafunzi katika darasa. Mtoto wa Kiislamu katika mazingira ambayo yanakinzana na taratibu za uislamu, huweza kupata hasara kwa sababu ya lugha inayotumika, mavazi yanayovaliwa(hususani watoto wa kike) na utaratibu wa kula chakula. Imani tofauti za kidini hutimizwa kwa vitendo vya aina fulani. Tofauti hizi za kiimani huweza kuwaathiri wanafunzi wengine darasani. Pia tofauti za rangi ya mwili humpa wakati mgumu mtoto anayekuwa katika sehemu ambayo ina ubaguzi wa rangi.

Kuchagua rafiki Wema

Mzazi unatakiwa kufahamu marafiki wa watoto wako. Wakaribishe marafiki wa watoto wako nyumbani kwako ili uweze kusikia mawazo yao, wajieleze wao ni watu wa aina gani na wana ushawishi gani kwa watoto wako. Kukaribisha watu kama hawa nyumbani kwako pia kunaweza kuwafunza wao ni jinsi gani nyumba ya muumini inatakiwa iwe katika muonekano upi. Tafakari ni namna gani familia yako inaweza kuathiri vijana.

Zungumza na watoto wako kuhusiana na marafiki wanaowachagua, hususani pale utakapokuwa na shaka kuhusu marafiki hao. Liendee jambo hili Kwa umakini. Acha watoto wako waamue kuhusu marafiki wao wenyewe. Ikiwa utawafanyia maamuzi unawafunza utegemezi, hili halitawasaidia wanapokuwa pekee yao, kwa sababu siyo kila siku utaweza kuwa karibu na mtoto wako.

Wakati unajadili na watoto kuhusu marafiki zake, unatakiwa kufanya vitu viwili;

1. Tumia neno “mimi”. Mueleze mtoto jinsi unavyojisikia ulipokuwa karibu na rafiki yake. Kwa mfano, “wakati ulipokuwa unacheza na Yasmin, nilihisi kama anatabia ya kuchukua vitu vya watu. Napoona mtoto anapenda kuwa mbinafsi huwa nahuzunika sana”. Au “wakati nazungumza na Sara, nilisikia akisema mambo mabaya kuhusu mama yake. Alinifanya nijisikie vibaya sana.”

   Hapa unampa mtoto kujifunza kile ulichokiona na ulichomueleza. Usiseme “Wewe unapenda sana kuchagua marafiki wabinafsi na wasiojielewa si ndio?”

2. Uliza maswali. Muulize mwanao kama amegundua tatizo ambalo wewe umeligundua kama na yeye limemfanya ajisikie vipi. Sikiliza kwa ma-

kini majibu yake. Kitu unachotaka kubaini ni vipi mtoto wako anaweza kuwa muwazi na mkweli. Kama mtoto anakuwa kahisi kama wewe, unaweza kusema “unadhani ni vizuri kutumia muda mwingi na marafiki wengine zaidi ya Yasmin au Sara?”Anza kufanya taratibu hizi mapema iwezekanavyo. Wape fursa watoto wako wajadili na wewe kuhusu marafiki zao. Njia hii inaweza ikawa nzuri kufikisha ujumbe wakiwa wakubwa na hatari zikiwa nyingi zaidi.

“Marafiki wabaya hawana tabia ya kumuogopa Allah, pia huwa wanavuta sigara, bangi, wanatumia dawa za kulevya, wanatumia lugha chafu, mara kwa mara wanaingia katika migogoro na askari polisi au kuhamasisha tabia mbaya na hatarishi.”

Itakuwaje endapo mtoto wako atachagua marafiki wasiofaa?

Iman El-Kadi(mfanyakazi wa Umma) alisema:

> “Mtoto anaweza kuchagua rafiki asiyekuwa na ukarimu wala heshima. Usiogope kwa sababu watoto wana kawaida ya kuvutiwa kufanya vitu wasivyovifahamu kutokana na udadisi wao na wakifanikiwa kujua kitu hicho basi wanaacha kudadisi. Wazazi tunapojaribu kuvunja urafiki kwa haraka haraka, tutashindwa na kuwafanya wawe karibu zaidi na rafiki huyu. Pindi rafiki huyu anapokuwa kaja nyumbani kwako kwa mwanao unatakiwa kumwambia “karibu lakini fuata kanuni na taratibu zilizopo katika nyumba hii”

Kitu hatari zaidi kwa mtoto ni kuwa na rafiki ambaye ana imani inayofanana na mtoto wako lakini akawa hafuati imani ya dini yake inavyoelekeza na badala yake akawa anafanya maovu. Nakumbuka wanangu (wenye umri wa miaka 7 na 9) waliokulia katika mazingira ya kidini Amerika walipotembelea Istanbul waliona watu wakinywa bia, wanatazama filamu za ngono na hawafungi kipindi cha mwezi wa Ramadhani. Hakika walishangazwa sana. Mimi nikiwa kama mzazi niliwafahamisha kuwa watu wanaweza kuzaliwa wakiwa Waislamu lakini wakafanya matendo ambayo hayaendani na Uislamu.

Watoto wanapata hamasa kutokana na taratibu za kimaisha pamoja na mawazo ya wazazi wao. Ni muhimu kwa wazazi kuweza kugundua kipindi watoto wakiwa hawafuati taratibu hizi. Je ni sababu zipi hupelekea watoto kuchagua marafiki wabaya? Kwanini unaweza kuona mtoto mmoja anavuta sigara au bangi wakati mwingine havuti? Je ni kitu gani kisichopatikana nyumbani ambacho rafiki anampa mtoto wako?

Kuhamasisha watoto kufanya shughuli zenye manufaa kwao huwasaidia hata kuchagua makundi yanayowafaa.Yafuatayo ni mambo ya kufanya:

- Kama mtoto (rafiki wa mwanao) anayekuja nyumbani kwako humpendi kutokana na tabia zake, pendekeza kwa mwanao alete marafiki wengine.
- Mshughulishe mtoto kwa kufanya vitu mbali mbali (kama vile kutembelea ndugu)
- Weka taratibu zenye kufuatwa na wote (mtoto na marafiki zake) kama vile hakuna kupiga kelele, hakuna kutumia lugha chafu wala hakuna kupigana.

MZAZI UNATAKIWA KUWAFAHAMU MARAFIKI WA WATOTO WAKO

Kwanini kuna vitu vyenye kuwavutia zaidi vijana?

- Vijana hushawishika na makundi kutokana na sababu kuu mbili;
- Kuwa na uwezo wa kuchagua marafiki wao wenyewe, tofauti na hali inavyokuwa kwa familia na ndugu ambapo vijana hukosa fursa ya kuchagua kwa vile hujikuta tayari wapo katika uhusiano na familia fulani au ndugu wa aina fulani.
- Uhusiano wao na makundi hutokana na ulingano wa umri wao, uzoefu wa hali fulani katika mazingira, hisia kuhusu vitu fulani, changamoto zinazowakabili na mazingira ya shuleni wanaposoma.

Vijana huunda makundi yao ya kipekee yenye kufuata mila na tamaduni fulani ikiwemo matumizi ya ishara na lugha katika mawasiliano, maadili na desturi zao ambazo ni tofauti na watu wengine.

Vijana huwa hawapendi kuwashirikisha sana wazazi wao hususani katika kuomba ushauri wa mambo yao isipokuwa hupenda kushirikishana wenyewe kwa wenyewe kadri wanavyokuwa wakubwa. Kadri wanavyopunguza ukaribu kwa kutowashirikisha wazazi, walimu na watu wazima katika mambo yao, hujikuta wanaongeza ukaribu kwa kushirikiana miongoni mwao. Katika nyanja ya kifedha, vijana hushawishiwa sana na wazazi wao ila katika vitu vingine kama mavazi, kustarehe katika kumbi za starehe, kupanga muda wa kufanya starehe, kusafiri na kupenda aina fulani ya magari vijana hushawishiwa na marafiki zao.

Mahusiano mbali mbali ya kijamii

- Watoto na watoto wenzao
- Waovu na waovu wenzao
- Kijana na kijana mwenzake
- Mvutaji na mvutaji mwenzake
- Wazee na wazee wenzao
- Watumiaji dawa za kulevya na watumiaji wenzao wa dawa za kulevya
- Wacha mungu na wacha mungu wenzao
- Wataalamu katika kada na wataalamu wenzao

Marafiki huwaathiri marafiki wenzao. Mtume Muhammad (s.a.w) anasema kuwa;

"Mtu huathiriwa na tabia za rafiki yake, kwa hiyo kila mmoja awe makini kuchagua yule anayetaka kumfanya awe rafiki".

(Al-Tirmidhi na Abu Dawud)

"Mtu atakuwa nae pamoja (atafufuliwa na yule) ampendae.

(Al Bukhari na Muslim)

Mfano wa rafiki mzuri na rafiki mbaya ni kama muuza uturi na mhunzi wa vyuma. Muuza uturi anaweza akakupa uturi, au ukanunua au unaweza tu ukapata ile harufu ya uturi wake unavyonukia. Lakini kwa mhunzi wa vyuma, anaweza akazichoma moto nguo zako au ukapata kuhisi harufu mbaya katika mwili wake kutokana na kazi anayoifanya.

(Al Bukhari na Muslim)

Aya ifuatayo inaelezea madhara yatokanayo na vishawishi viovu

> "Ni siku ambayo mtu muovu atang'ata mikono yake huku akisema, "oh, laiti kama ningefuata njia sahihi pamoja na Mtume wa Allah. Oh, najuta mimi leo! Laiti kama nisingemfanya fulani na fulani kuwa rafiki zangu mimi! Hakika wamenipotosha na kunisahaulisha kuhusu utukufu wa Allah baada ya ukweli kunibainikia mimi!". Hakika shetani ni adui mkubwa kwa binadamu….
> (Qur an 25:27-29)

Familia zinapokuwa katika mazingira mabaya

Marafiki wabaya wanaweza kuleta matatizo yenye athari kubwa yasiyoweza kupatiwa ufumbuzi. Marafiki wenye tabia mbaya shuleni na watoto wa jirani zetu wanaweza kuharibu taswira ya familia. Endapo familia itakuwa inaishi katika maeneo ambayo hakuna uwezekano wa kupata rafiki mzuri kwa ajili ya watoto, wazazi wanalazimika kuhamia sehemu yenye marafiki wema. Wazazi wengi huwahamisha watoto wao shule wanazosoma, au kuwahamisha katika mji jirani kama wamekosa kupata marafiki wazuri kwa watoto wao sehemu wanapoishi. Kitendo hiki huwagharimu kidogo sana wazazi ukilinganisha na faida ambazo watoto na wazazi wanaweza kuzipata hapo baadaye.

Maandiko yanaeleza kuwa hata mitume walikuwa wakihama kutoka katika jamii moja hadi nyingine

Wazazi: waruhusuni watoto wenu walete marafiki zao nyumbani ili utazame mwenendo wao. Fanya tafiti kuhusu tabia zao. Jaribu kuwa rafiki kwa rafiki wa mtoto wako.

Dkt. James S. Coleman, raisi wa zamani wa chama cha masomo yanayohusu watu na jamii nchini Marekani, akiwa kama miongoni mwa wataalamu maarufu kwenye fani hiyo alisisitiza wazazi watambue wazazi wa marafiki wa watoto wao. Kwa maelezo yote alisema kuwa hii inasaidia katika kukuza tabia nzuri na kuondoa tabia mbaya.

KAZI ZA KUFANYA



KAZI YA KUFANYA 69: MTU AMBAYE NI KIGEZO CHEMA KWA MTOTO WAKO

Muombe mtoto wako akutajie majina ya watu watatu ambao angependa kukutana nao na kwa nini amependa watu hao. Hii itakusaidia kujua uelewa wa mtoto wako kuhusu watu anaowaiga.Jadili na mtoto wako kuhusu watu wema na wabaya kuwaiga.

KAZI YA KUFANYA 70: MTOTO MWENYE USHAWISHI MBAYA

Jadili hali zifuatazo na jadili kuhusu mapendekezo yaliyotolewa chini yake;

Mtoto wa jirani yako mwenye umri wa miaka 9 (wa kike) anamshawishi vibaya mtoto wako mwenye umri wa miaka 7 (wa kike).

Watoto hawa huwa pamoja takribani kila siku kwa hiyo unahitaji kupunguza uwezo wao wa kukutana na kukaa pamoja.

1. Je utamwambia mtoto wako asicheze na huyo rafiki yake na asionane nae tena.
2. Je utamwambia mtoto huyo wa jirani mwenye kumuharibu mwanao asicheze na mwanao, asije tena kwenu kumfuata mtoto wako na mtoto wako asiende kwa huyo rafiki yake.
3. Je utawaacha wakae na wacheze pamoja endapo mzazi utakuwepo nao pamoja ili uweze kufuatilia tabia yao.
4. Je utazungumza na jirani yako (ambaye ni mzazi) kuhusu mtoto wake kuwa pamoja na mtoto wako.

Mtoto mwenye ushawishi mbaya kwa wengine huamsha hisia za wazazi wengi. Zifuatazo ni hoja za majibu ya hapo juu;

1. Usiwe chanzo cha kumfanya mtoto wako aeleze matatizo kwa mtoto mwingine. Huwenda watoto hao wakawa bado wadogo sana ndiyo maana wanashindwa

kufahamu unachokizuia kwao na hali hii itapelekea wewe kuwa adui wa kila mmoja kwa mtazamo.

2. Kueleza kinacho kuudhi au kumuwekea taratibu mtoto ambaye siyo wako haifai na siyo sahihi.

3. Hii inahitaji kazi ya ziada. Itakufanya muda wote uwe msimamizi wa mtoto na utawajibika kuwasimamia wakati wote watoto hao ambao ni marafiki wanapokuwa pamoja. Hali hii itakuchosha zaidi.

4. Ni vigumu sana kumkabili jirani kumueleza unachokiona si kizuri kwa mtoto wake. Hata hivyo, hii ni njia nzuri ya kuondoa tatizo kama hili.

KAZI YA KUFANYA 71: KAMA NINGEJUA, NINGEFANYA VINGINEVYO

Katika mazungumzo na familia, wazazi wanatakiwa wajibu swali lifuatalo: “kama ningepata fursa ya kuanza maisha tena upya, kitu gani ningefanya?” Kubali makosa yako uliyotenda kwa watoto wako. Hamasisha watoto wako nao waseme makosa yao waliyotenda.

SURA YA ISHIRINI NA TATU

▪ RUNINGA, VIDEO NA MICHEZO YA KOMPYUTA

Madhara yanayotokana na
Athari za matumizi yake

SURA YA ISHIRINI NA TATU 532

Runinga, Video na Michezo ya Kompyuta 532

Dodoso la wazazi 535
Madhara ya Runinga 537
Kabla ya Runinga 539
Mgeni 543
Weka mipaka katika kile ambacho watoto wako wanatazama. 544
Mambo mbadala wakati wa kutazama runinga katika familia 546
Njia mbadala 547
Mambo bora zaidi ya kuchagua 548
Shughuli za Jamii 548
Shughuli Asilia 549
Michezo ya kuchezesha 549
Sauti za asili 550
Wape fursa waweze kufahamu mazingira asilia 550
Kula chakula na watoto wako 551
Madhara ya kutumia Intaneti kupindukia 551
Michezo ya kompyuta 552
Michezo ya Video 552
Kuonekana kwa utofauti wa jinsi katika Runinga 553
Uharibifu wa familia 554
Kwa ufupisho 555
Kazi za Kufanya

Upendo, ujasiri, ubunifu, uaminifu na hali ya uwajibikaji vinajenga kujiamini na kujitambua.

Utangulizi

Kuna kitu katika nyumba zetu ambacho kina umuhimu mkubwa maishani mwetu lakini huwagharimu muda mwingi sana watoto wetu walio wengi kuliko hata sisi kinavyotugharimu na japokuwa wengi wetu hatufahamu, ukweli ni kuwa kitu hiki huchangia kuharibu familia zetu. Licha ya hali kuwa hivyo bado pia hatutilii maanani kuwa kitu hiki ndiyo chanzo cha kuharibu familia zetu. Kitu hiki ni runinga. Usidharau runinga au athari zake kwa ujumla katika maisha yetu. Ingawa televisheni imeleta ushawishi mkubwa kwa watu katika karne ya ishirini, tumegundua ya kwamba ujio

wa teknolojia mpya katika karne ya 21 umeathiri maisha yetu kupitia mtandao wa intaneti, simu za mkononi, tabiti, na vinavyofanana na hivyo. Ni dhahiri kwamba simu za mkononi zimekuwa mbadala wa namna nyingi za mawasiliano ikiwemo runinga. Kwa hiyo vifaa vitakavyoelezwa katika sura hii vitatumika kwenye simu kama vinavyotumika katika runinga, michezo ya kwenye runinga (video games), Kompyuta na mtandao wa intaneti.

Dodoso la wazazi

- Je, watoto wako hutazama runinga wakati wakipata kifungua kinywa asubuhi na kabla ya kwenda shule?
- Je, watoto wako wanatazama runinga baada ya kurudi shule? Je wakati wanafanya kazi zao za kimasomo nyumbani pia hutazama runinga?
- Je, familia yako hutazama runinga wakati wa kula?
- Je, ni kiasi gani maongezi ya mtoto wako na michezo yake inahusiana na vipindi vya runinga?
- Je, runinga huwa inawashwa wakati mtoto wako anacheza na rafiki zake au akichezea mwanasesere?
- Je, watoto huhitaji chakula na sanamu wanaowaona wanatangazwa kupitia runinga?
- Je, maisha ya familia yako hupangwa kutokana na ratiba au vipindi vya runinga?
- Je, mtoto wako huzima runinga baada ya kipindi fulani kuisha au huendelea kutazama?
- Je, mtoto wako huchoka kutazama runinga usiku?
- Je mtoto wako hupata hofu au hupata njozi mbaya kutokana na kipindi alichotazama katika runinga?
- Je, mtoto hupenda kutazama runinga zaidi ya kucheza?
- Je, mtoto hupuuza wageni wanapofika kutokana na kutazama runinga?
- Je, mtoto wako huchelewa kufanya ibada zake ndani ya muda kwa sababu ya kutazama runinga?

Kutazama runinga kupita kiasi hujenga mazoea na huwa hakuna tofauti na kuwa na mazoea ya kutumia dawa za kulevya. Watoto hudumaa na kupumbaa kiakili pindi wanapotazama runinga na hivyo kushindwa kujitambua na kujielewa. Hata ukiwaongelesha hawatoweza kusikia, na hata simu ikiwa inaita karibu yao hawawezi

kupokea. Hata sura zao hubadilika wakati wanatazama runinga na huacha wazi vinywa vyao huku ndimi zao zikiwa kando kando ya meno ya mbele. Macho yao pia huwa katika hali ya kutojielewa na kuduwaa. Wakati wa kutazama runinga watoto huwa hawajielewi (hawawezi kuhisi kitu kingine katika mazingira waliyopo na akili zao hudumaa na kushindwa kufanya kazi) kwa furaha wanayoipata kupitia runinga iliyopo mbele yao.

Vipindi vinavyorushwa kupitia runinga huzua mdahalo mkubwa kutokana na baadhi yao kuwa na manufaa kwa watoto na vingine kuwa na madhara kwa watoto. Hata hivyo, kilicho muhimu kuzingatia katika hili siyo urushwaji wa vipindi husika isipokuwa kujenga tabia ya kuwa na mazoea pamoja na muda unaotumiwa na watoto katika kutazama vipindi hivyo katika runinga kama huleta faida au madhara kwa watoto.

Kuna baadhi ya watoto hutazama sana runinga bila hata kupumzika na kuifanya runinga kama rafiki na kifaa cha kupotezea muda. Mtoto aliyejenga mazoea ya kutazama runinga mara kwa mara pasipo kuacha au kupumzika hupatwa na matatizo mengi sana ukilinganisha na watoto wengine ambao hawana tabia ya kuangalia runinga kupita kiasi. Matatizo haya ni kama vile kuwa na aibu sana, kuwa mkorofi, kuwa dhaifu kiumbile ama kiakili na kushindwa kushirikiana vizuri na wenzake. Endapo mtu mmoja tu katika familia akiwa na tabia ya kupenda kutazama runinga kupita hali ya kawaida, inaweza kuwa na madhara kwa familia nzima. Hii inatokana na kutokuwa na uwezekano wa kupanga na kufanya mambo ya msingi katika familia ikiwa mmoja kati yao anatazama runinga muda wote. Ni rahisi sana kuacha kusoma, kucheza michezo mbali mbali na kuandika kisha kuanza kutazama runinga kuliko kuacha kutazama runinga na kujihusisha na kusoma, kucheza au kufanya kitu kingine chochote ambacho hakina uhusiano na runinga kama mtoto alishajenga mazoea ya kutokukaa bila kutazama runinga. Mazoea ya kutazama runinga humshawishi mtoto kuhitaji kutazama runinga muda wote hivyo inakuwa ni vigumu kuacha.

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Marie Winn (2002) runinga inaweza kudhoofisha watu wengi sana kiakili na kiumbile. Runinga husababisha watu kuwa na uwezo mdogo wa kufikiri na kuamua, huwa wajinga na rahisi kuwatawala.

Matatizo madogo huweza kujitokeza wakati wa kutazama runinga lakini madhara makubwa hayajidhihirishi katika wakati huu. Watoto ambao hutumia maelfu na maelfu ya masaa katika kutazama runinga huathiri ukuaji wa ubongo wao, yaani hudumaa kiakili na pia hujiathiri kijamii yaani hushindwa kushirikiana vizuri na jamii anayoishi. Katika hali hii kunaweza kuwa na maneno mengi mno ambayo hayajazungumzwa lakini yakajibiwa, wakati huo huo kunaweza kuwa na maswali ambayo hayajaulizwa halafu yakajibiwa pia na mtu mwingine.

Madhara ya runinga



Wakati wa kufanya tathmini kuhusu runinga, wazazi wengi hujikita katika vipindi vinavyotangazwa badala ya kutathmini muda ambao watoto wanatumia kutazama runinga. Kwa mtindo huu, wazazi hujikuta wanatafakari mahitaji yao badala ya yale ya watoto wao. Wazazi wanahitaji vitu vyenye kuburudisha na kuwafurahisha watoto. Wazazi pia huhitaji amani na utulivu uwepo ndani ya nyumba. Wazazi wanahitaji kuwa na kifaa cha umeme chenye kutuliza watoto ambacho hakitoweza kuleta malalamiko na huweza kupatikana muda wote. Runinga haikidhi mahitaji ya watoto kuweza kuwa huru kubaini umahiri wao, udhaifu wao pamoja na kuwafunza kuwasiliana (lugha ya kuongea na kuandika). Watoto wanahitaji zaidi kujihusisha na vitu ambavyo huvibuni kwa fikra zao kuliko kuwa na vitu halisi ambavyo wanaweza kuundiwa na watu wazima kama wazazi wao. Watoto pia wanahitaji wapate changamoto kiakili kupitia utumiaji wa akili zao kwa kushika na kufanya mambo mbali mbali badala ya kukaa bila kujishughulisha na kutazama runinga.

Wazazi wengi wanatumia runinga kuwatuliza na kuwafurahisha watoto wao sababu runinga inaweza kutuliza akili badala ya kuishughulisha. Picha inayoonekana kwa macho katika kutazama runinga ni sawa na picha inayotokea wakati mtu amelala na kuota wakati wa mchana**.** Runinga hukosa kutoa uhalisia wa picha ilivyo, inatoa picha katika mfumo uliosawa na njozi. Wanaopenda sana kutazama runinga huwa na matatizo katika maisha yao kama ilivyokuwa kwa watu wenye kutumia dawa za kulevya au kilevi. Hujikuta wanapoteza fursa za kufanya mambo ya msingi ambayo yangeweza kuwaletea manufaa au kuleta mafanikio katika maisha yao. Runinga haina faida ukilinganisha na vitu vingine vingi sana. Ingawaje runinga haikidhi mahitaji ya watoto, watoto bado hupendelea kutazama badala ya kusoma, kupanda mimea na maua katika bustani, kushona, kucheza au kuzungumza. Shughuli kama hizi zenye umuhimu hazipendwi sana kama kutazama Runinga. Runinga huteka hisia za watoto kwa sababu huwaburudisha. Ingawaje burudani yake siyo sawa na kula au kukumbatiwa, runinga bado inasalia kuwa kitu chenye mvuto kwa watoto. Runinga ni kitu bandia sababu haina uwezo wa kukupa kila kitu katika uhalisia wake kama chakula kinavyoweza kukupatia virutubisho au familia yenye kukupenda inavyoweza kukupa kitu fulani, lakini bado huonekana kuwa kitu kizuri kwa vile inakuwa na mkusanyiko wa burudani katika chanzo kimoja: yani taswira, sauti mbali mbali na muziki, mandhari halisia na mandhari ya kubuni yasiyo halisia. Zaidi ya nusu ya wazazi wote wenye asili ya Marekani hutumia utaratibu wa kutoruhusu watoto wao kutazama runinga kama sehemu ya kuwaadhibu na hutumika sana nchini humo kuwa ni aina ya adhabu.

Runinga hutawala watoto ambao huweza kuonesha hisia zao pindi izimwapo na huwa hawajishughulishi na chochote na husalia kimya. Namna taswira inavyobadilika, au jinsi kamera inavyochukua taswira katika kona tofauti husababisha mtoto kuwa makini kwa muda fulani. Watoto walioathirika kwa kutazama runinga kwa muda mrefu hujaribu kudaka ubora wa taswira katika runinga kwa kubadili haraka mawazo yao. Hata vipindi vya watoto vinavyooneshwa katika runinga pia huwasisimua sana watoto. Huwa ni kitu kinachoua mfumo wa ufahamu kwa watoto wadogo ambao hawajaanza masomo ya shule, kwa kuwa hawajakomaa vya kutosha kuweza kuendana na kasi ya hisia za vifaa vya umeme. Hii huwa na uhusiano na hali ya mtoto kushindwa kuzuia hisia zake kama inavyobainika miongoni mwa watoto wengi kwa sasa. Pia hali hii inakuwa na uhusiano mkubwa na tatizo la mtoto kushindwa kuwa makini na baadhi ya vitu kwa muda fulani.

Weka vipindi vya watoto katika runinga na tathmini namna gani mandhari na taswira ya kamera inabadilika.

UZOEFU KUTOKA KIPINDI CHA SESAME

Hiki ni kipindi cha watoto cha kimataifa kinachofundisha watoto namna ya kusoma herufi mbali mbali pamoja na maneno. Mzalishaji wa kipindi hiki cha Sesame amedai kuwa kipindi chao ni muhimu kwa kutoa elimu kwa watoto wadogo. Hata hivyo kuna vitu vyenye ukweli katika kipindi hiki. Huwafanya watoto wawe waathirika wa kutazama runinga. Walimu wametambua kuwa baadhi ya watoto wanaingia shule za awali wakiwa



wanafahamu herufi kutokana na kipindi hiki. Hata hivyo, wahanga wa kutazama runinga huwa na michezo michache kinadharia ila hupenda kukimbia bila malengo na huwa hawatumii sesere na vifaa vya kuchezea watoto, huwa na tabia ya kukata tamaa na huchanganya uhalisia na vitu vya kufikirika.

Kujifunza kwenye kuleta mafanikio kunahitaji uzoefu shirikishi. Kipindi cha sesame na vipindi vingine vyenye kutoa elimu havina uhalisia na wala hakuna uzoefu shirikishi wa sura kwa sura katika ufundishaji. Kwa kweli kitabu chochote kizuri ni bora sana kuliko kipindi cha sesame.

Walimu wa shule za awali wamekatishwa tamaa na wanafunzi walio wengi kwa sababu wanafunzi hawataki kusoma na kufuatilia. Wakati runinga inaweza kuboresha uwezo wa kufikiria kwa vitu visivyohitaji mazungumzo, haisaidii kupata ujuzi wa vitu vingine ambavyo ni muhimu katika kufanikiwa shule. Kutumia masaa 100 katika utazamaji wa sesame humpatia mtoto mafunzo machache katika elimu kuliko kutumia masaa 10 kusoma kitabu kizuri. Mzazi na kitabu hufanya kazi nzuri kwa muda mfupi kuliko kipindi cha ses-

ame, na kuleta faida nyingi katika kuendeleza uwezo wa akili ya mtoto na bila kuwa na madhara yaletwayo na kipindi cha runinga. Kadri watoto wanavyotumia muda mwingi kutazama runinga, ndivyo huweza kufanya vibaya shuleni. Mafanikio ya shule huhitaji mapenzi ya kusoma vitabu, kuwa na uwezo wa kuwa pamoja na wengine na tabia ya kufuatilia kazi zenye kuchosha, kukera na kurejea rejea (kama vile kujifunza namna ya kusoma jedwali la kuzidisha). Ujuzi wa kufanya mambo mbalimbali hupunguzwa au kutoweka kutokana na kutazama sana runinga.

KABLA YA RUNINGA

Kabla ya runinga wazazi walikuwa karibu na salama na watoto wao, siyo kwa sababu ya kuamini kuwa ni njia sahihi ya kulea watoto isipokuwa ukaribu huu ulikuwa muhimu kwa wazazi kuishi. Kabla ya runinga, wazazi walikuwa wakiwatazama watoto wao. Waliwafundisha watoto kucheza peke yao kwa kipindi fulani na kufuatilia maendeleo ya watoto wao. Waliwafundisha watoto wao namna ya kujiburudisha peke yao. Waliwafundisha namna ya kulala kwa kuwa kulala ni muhimu kwa mtoto. Wazazi walihakikisha watoto wanalala au wanakuwa kimya katika vyumba vyao, wakiwa wanacheza au kusikiliza vipindi vya redio au kutembea kimya kimya.

Baada ya kugundulika kwa runinga, vitu vingi katika haya vilitoweka. Siku za hivi karibuni, watoto hawajui namna ya kujifurahisha wenyewe. Badala ya kuendelea na mambo wanayopenda, runinga inapozimwa watoto wanakuwa hawana cha kufanya. Wanakataa vyenye kuwaburudisha, hukosa kufanya vitu vyenye ubunifu, hukosa kusoma na hujikuta wamekereka.



Kabla ya runinga, watoto waliweza kujitegemea na kubadilika kutoka kutegemea wazazi na kuanza kutegemea mazingira yalivyo na kutenda jambo fulani husika. Kuweza kuishi vizuri katika jamii lazima mtu aweze kuendana na mazingira. Watoto wanapofikia umri wa miaka mitatu, wanaanza kujitegemea na kuanzisha muingiliano na watu wengine wa karibu yao. Runinga hata hivyo hutumika kama kitu chenye kulea watoto katika maisha yao ya utotoni.

Wakati wa kutazama runinga, watoto hujikuta wakiwa salama zaidi na kuweza kupokea vitu kama vile wakiwa viganjani mwa mama zao. Hawatakiwi kutoa kitu chochote kama wanavyofanya wakiwa wanacheza na mtoto mwenzao. Kwa watoto kitendo cha kutazama runinga hakina madhara kama yale yapatikanayo katika michezo mingine; watoto hawawezi kuumia kwa kutazama runinga na kuwakera wazazi wao. Kama wanavyoanza kukua bila kuhitaji msaada, runinga huwarejesha katika hali ya ukaribu na utegemezi.

Kabla ya runinga, watoto huvutiwa na vitu vingi na hivyo hupenda kujaribu jaribu; huzuia kukereka kwa kutumia ugunduzi wa michezo mipya, kusoma, kuandika barua na kufanya mambo mengine



wapendayo. Baada ya kuwepo kwa runinga,watoto wanalalamika kuwa hakuna kitu cha kufanya na kitu chochote kwao hakionekani kuwavutia zaidi. Hawakuwa wakiburudika zaidi wala kukereka zaidi, kutazama runinga imekuwa njia salama, isiyohitaji jitihada katika kufurahia maisha na kutafuta kitu chenye kuburudisha kuwa kama kazi. Filamu zinazohusu vitabu huondoa uwezo wa watoto wa kufikiria na kuwafanya wasiweze kufikiria badala ya kuwaendeleza kiakili.

Huwa hawawezi kukuwa na tabia za wahusika katika masimulizi au kuelewa mambo yao ya baadaye, vitu vya kupigania na thamani zao. Badala ya kutumia siku kadhaa kusoma simulizi hadi kuimaliza, simulizi yote huisha ndani ya dakika 90. Watoto huondoka katika kutazama runinga wakiwa wameburudika lakini hawakuridhika. Walau kidogo wakati wa kusoma kitabu wanaweza kupata uzoefu wa mazingira fulani, kujenga urafiki na wahusika na kufanyia kazi hali ya taswira zao. Kugusa, kunusa na kuhisi katika kitabu husaidia watoto kuunganisha simulizi na kuweza kusoma tena na tena. Runinga huhusisha hisia za kujitoa, aina ya msongo wa mawazo pindi filamu inapoisha ghafla na kuhitajika watoto waondoke. Kuna muungano mkubwa kati yetu na vitabu, muungano huu hauwezi kusomwa, kupimwa kiasi na kuelezewa. Hisia za muungano wa aina hii haupo katika runinga.

Runinga huongeza hitajio la misaada na utegemezi kwa watu wazima. Katika kipindi cha nyuma, muda huru ulikuwa ukimpatia mtu fursa ya kupunguza utegemezi kwa watu wazima. Leo, kwa watoto wengi, muda huru umekuwa kama laana. Kitu pekee wanachokiona kizuri kufanya katika muda huu ni kutazama runinga. Baadhi ya watoto wanakula, wanatumia muda wao na marafiki na kufanya kazi zao wakiwa wanatazama runinga.

Maisha ya familia yameathiriwa sana na utazamaji wa runinga. Ratiba za kila siku huwepo katika utazamaji wa runinga na hakuna utaratibu wa kufanya ibada katika familia. Ushiriki katika masuala ya dini na jamii umepungua na kutazama



runinga ndiyo chanzo kikuu. Wazazi wengi wanalalamika kuwa makazi yao yamekuwa hoteli na mgahawa; yaani imekuwa ni sehemu ya kula na kulala. Wazazi hawatambui kuwa utazamaji wa runinga unapokithiri, hayo ndiyo huwa madhara yake. Ili familia iwe nzuri, inahitaji kuwepo kwa mabadilishano ya uzoefu na ujuzi wa vitu. Shughuli mbali mbali zinazotokea, kubadilika na kukua katika miaka mingi ni miongoni mwa vitu vinavyounda familia nzuri yenye mahusiano mazuri na imara. Kinyume na hivyo wazazi wanakuwa waangalizi na walezi wa familia, wakihusika katika kuwalisha watoto, kuwavisha na wanakuwa hawana cha ziada; wazazi wanajificha kwa watu nyuma ya matendo wayafanyayo watoto wao katika maisha.

Kutazama runinga hurudisha nyuma familia kwa kuchukua muda mwingi kufanya hivyo badala ya kujihusisha na watu halisi. Familia nyingi za watu wa Marekani hutazama runinga wakati wa kula na siyo katika runinga moja. Hata kama wangekuwa wote wanatazama kipindi kizuri kinachohusu asili, maadili na matukio ya sasa, bado wangekuwa wamejinyima kitu muhimu sana. Je waliweza kubadilishana kile walichokifanya siku hiyo? Je waliweza kupanga pamoja, walibadilishana mawazo, walitaniana na kuzungumza kuhusu mafanikio na matatizo yao? Katika mazingira gani wanakuwa kama watu wa familia moja? Wakati runinga yenyewe haiwezi kuharibu maisha ya familia, kwa upande mwingine haiwezi kuimarisha maisha ya familia. Hata hivyo, huchukua muda wa kutengeneza uhusiano wenye imani miongoni mwao na hisia za usalama na huchukua nafasi ya wazazi katika kuelimisha na kuburudisha watoto.

IMANI POTOFU INAYOUNDWA NA RUNINGA

Niliwahi kuitwa na wanandoa wenye watoto wawili kwa lengo la kuwashauri kuhusiana na matatizo ya familia. Wazazi wote hao walikuwa Madaktari (waganga). Nilishangazwa, mama aliposema, “kabla ya ndoa nilidhani kuwa ndoa itakuwa na raha bila ya kuwa na majukumu, kama inavyooneshwa katika runinga na baadhi ya wasanii wa kike huko Hollywood. Kama wataalamu wanadanganyika kwa mfumo wa maisha unaoonekana katika runinga, je watoto wetu watakuwa na nafasi gani?

Wakati tukiwa darasa la pili, mwalimu alitusomea simulizi ya wanandoa ambao walikuwa na paka na mbwa. Paka aliwasaliti wanandoa wale hali ya kuwa mbwa aliendelea kuwa mwaminifu. Mbwa alimkimbiza paka ambaye nae alikimbia na kupanda juu ya mti kwa usalama wake. Simulizi ikaishia kwa maelezo "tangu siku hiyo, popote mbwa anapomuona paka, humkimbiza ili amng'ate". Kwa miaka mingi, nilikuwa nikiamini kuwa sababu ya mbwa kumshambulia paka inatokana na dhambi ya paka kuwasaliti wanandoa. Mwalimu angelielezea kuwa hizi simulizi ni za kubuni kwa sababu watoto huamini wanachosikia na kukiona. Pia wazazi wanatakiwa kuwaeleza watoto wao kuwa wanachokiona katika runinga siyo kweli.

KUTAZAMA RUNINGA KUPINDUKIA KUNAWEZA

- Kuchangia kuongezeka uzito na unene
- Kupunguza mafanikio ya kitaaluma
- Kuharibu muungano wa familia
- Kuhamasisha tabia zisizokubalika katika jamii

Daktari mpasuaji mstaafu- Generali C. Everett Koop, Marekani

BAADHI YA NUKUU MUHIMU KUHUSU RUNINGA

*Runinga imebadilisha mtoto kutoka kuwa mtoto mkaidi na kuwa mtoto asiyehama kutoka sehemu moja hadi nyingine. (***Mtunzi hafahamiki)**

*Ukija na kumuona mgeni…..akiwafundisha watoto wako namna ya kupigana au kuuza bidhaa zote unaweza kumfukuza katika nyumba yako, lakini hapa utakuwa sahihi, ingia ndani huku runinga ikiwa inawaka, hutoweza kufikiria mara mbili juu ya hilo. (***Jerome Singer)**

*Je hauhitaji kuwe na kitu katika runinga chenye kuongeza ufahamu? Kipo kitu kimoja "chenye nuru" lakini hakifanyi kazi. (***Gallagher)**

Runinga imesaidia watu wenye matatizo ya akili kwa kueneza taarifa na kuongeza hitaji lake kwao. **(Alfred Hitchcock)**

*Runinga. Kama watoto wanaburudika kwa herufi mbili, tafakari burudani ya namna gani wanaweza kupata kwa herufi ishirini na sita. Fungua fikra ya mtoto wako. Fungua kitabu. (***Mtunzi hafahamiki)**

(CHANZO:WWW.QUOTEGARDEN.COM)

Mgeni

"Miezi michache kabla ya kuzaliwa, baba yangu alikutana na mgeni ambaye alikuwa mgeni katika mji wetu uliokuwa mdogo. Tangu hapo awali, baba alikuwa kapendezewa na mgeni huyu na alimualika ili aweze kuishi na familia yetu. Mgeni alikubalika haraka na alinikaribisha ulimwenguni miezi michache baadaye. Kadri nilivyokuwa sikuuliza nafasi yake katika familia yetu. Mama alinifundisha kupenda neno Mwenyezi Mungu. Baba alinifundisha kumfuata/kumtii Mwenyezi Mungu. Lakini mgeni alikuwa mwenye kutusimulia hadithi. Alikuwa akisimulia hadithi nzuri. Hadithi za matukio mbali mbali, hadithi zenye kuhuzunisha na zenye kuchekesha zilikuwa nyingi kwake. Aliweza kuiteka familia yetu kwa masaa kadhaa kila wakati wa jioni. Alikuwa kama rafiki kwa familia yote. Alimchukua baba pamoja na mimi na kwenda katika mchezo wetu wa kwanza wa mpira wa wavu. Alikuwa siku zote anatuhamasisha tutazame maigizo na alikuwa akipanga kututambulisha kwa wasanii maarufu wa maigizo.

Mgeni alikuwa akizungumza kwa muda mrefu bila ya kupumzika. Baba hakuonekana kujali ila mama wakati mwingine alikuwa akiinuka wakati wengine tukiwa tunasikilza simulizi zake zinazohusu sehemu za mbali, mama alikuwa akienda chumbani kwake kusoma biblia na kufanya ibada. Mama alikuwa akiomba yule mgeni aweze kuondoka. Unaona, baba yangu ameijenga familia yenye maadili. Lakini mgeni huyu hakuhisi

kuwa na jukumu la kuheshimu maadili yaliyokuwepo. Maneno na tabia chafu hazikuwa zikiruhusiwa katika nyumba yetu- siyo kutoka kwetu tu au marafiki au watu wazima. Mgeni wetu hata hivyo alitumia maneno mabaya ambayo yalikuwa yakiunguza masikio yangu na kumkera baba. Mgeni alikuwa hakemewi. Baba yangu kamwe hakuruhusu pombe katika nyumba yake hata kwa kupikia. Lakini mgeni huyu alitununulia pombe na vilevi vingine tofauti tofauti. Alisababisha pia sigara zionekane nzuri, zenye mvuto na alitofautisha vifaa vya kuvutia.

Alikuwa akizungumza waziwazi kabisa kuhusu watu kuingiliana kimwili. Alikuwa akitoa kauli mbaya, wakati mwingine zenye kupendekeza jambo fulani lakini wakati mwingine zilikuwa zinafedhehesha. Nafahamu sasa kuwa ufahamu wangu wa mapenzi kuhusu uhusiano wa mwanaume na mwanamke ulichangiwa na mgeni yule. Nikijaribu kutazama kipindi cha nyuma, naamini ni Baraka za Mungu pekee zilizomzuia mgeni kuweza kutushawishi katika mabaya zaidi. Mgeni alikuwa akipingana na maadili ya wazazi wangu. Licha ya yote hayo, mara chache sana alikuwa akikemewa na hakutakiwa kuondoka nyumbani. Zaidi ya miaka 30 imepita tangu mgeni alipokuja kuishi nasi. Lakini laiti kama ningeenda katika nyumba ya wazazi wangu, ungemuona akiwa amekaa akiwa anasubiri mtu amsikilize wakati anazungumza na kuchora picha. Jina lake ni? Siku zote tumekuwa tunamuita runinga."(*Mtunzi Hafahamiki)*

WEKA MIPAKA KATIKA KILE AMBACHO WATOTO WAKO WANATAZAMA.

Pam aliamua kushiriki katika harakati za wiki kitaifa juu ya kuzima runinga. Watoto wake, ambao walikuwa na umri wa miaka 13, 11 na mwingine miaka 4 walikuwa wakilalamika hapo mwanzo lakini waliacha kulalamika baada ya kupata vitu vingine vya kufanya katika juma hilo. Watoto wa kiume waliokuwa wakubwa kiasi walisoma zaidi na kucheza pamoja na hata waliweza kuwafundisha wadogo zao kucheza mpira wa miguu. Watoto walifanya kazi za familia na walikuwa wakioneshana ukarimu miongoni mwao. Kutokuwa na runinga kulionesha tofauti kubwa. Muda wa familia sasa ulikuwa ukipatikana.

USITAZAME MBELE YAKO MAIGIZO YENYE VITENDO USIVYOPENDA WANAO WAVIFANYE

> Wazazi wengi wamekuwa wakizima runinga na kukiri kuwa kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Familia ya Kane iliweza kufanya mabadiliko katika safari. Hakukuwa na runinga wakati tukiwa safarini kwa hiyo ulikuwa ni muda sahihi kufanya mabadiliko. Mwanzo, mtoto wetu wa kike aliuliza kuhusu runinga, lakini tuliweza kuharibu malengo yake kila alipokuwa akiuliza.

Wazazi wanahisi kuwa watoto wanatakiwa muda wote waburudike. Wazazi huhisi wanalazimishwa kuwasaidia watoto wao. “oh, nitakutafutia kitu cha kufanya”. Baada ya muda, hujiamini kuwaacha watoto wao watafute shughuli ya kufanya.

Watoto hunufaika kwa kuwasaidia wazazi wao kazi za nyumbani. Waalike watoto kusaidia katika kupika chakula. Je wazazi wanafaa kuwa mfano kwa watoto wao? Kama watoto watawaona wazazi wao wako huru au wanajishughulisha na kazi bila ya kutazama runinga, watoto nao watajifunza kuwa hivyo.

WATAALAMU NA WATAFITI KUHUSU RUNINGA KWA WATOTO

Spock (1998) na kituo cha tafiti kuhusu watoto (1999) wanasema kuwa watoto wasitazame runinga kiujumla kwa kuwa kutazama runinga kunahusishwa na tatizo la kuchelewa kuongea, hupunguza uwezo wao wa kuwa makini na kujifunza mambo mbali mbali”. Ushahidi wa kisayansi unaohusiana na faida haupo bali kuna ushahidi wa kutosha kuhusiana na madhara”.

Spock anatambua kuwa mbinu hii (ya kuruhusu watoto kutazama runinga) hutumika zaidi kwa wazazi dhidi ya watoto wao.

Rosemond (1993) amependekeza kuzuia watoto kutazama runinga hadi watakapofikia hatua ya kuweza kusoma na kufurahia vitabu. Hata hivyo, wazuiliwe katika masaa matano ya juma.

Rankin (2003) anaelezea kuwa tafiti moja imebainisha kwamba kutazama runinga kwa masaa 3 au zaidi kwa siku moja huathiri uwezo wa watoto shuleni lakini baadhi ya vipindi vya kufundisha masuala ya elimu husaidia. Vipindi vyenye mafundisho ya elimu vimehusishwa na kuweza kuongeza ubunifu kwa watoto.

Shirikiana na mtoto wako katika simulizi na mashairi yenye kuhamasisha na kufundisha.

(BENNETT 1996)

Mambo mbadala wakati wa kutazama Runinga katika familia

Wazazi wengi huwaruhusu watoto wao kutazama runinga, kwa sababu ya kukosa vitu vya kubana muda wa watoto wao. Wazazi huwa wanachoka sana kiasi kwamba runinga huwapa muda wa kupumzika kwa kuwaondoa watoto wasiweze kuwasumbua. Suluhisho ni kuanza kujihusisha katika shughuli zenye faida. Tumetaja madhara tofauti ya kutazama runinga kwa watoto na wazazi. Tatizo kubwa linalosababishwa na runinga ni kuwa kuna madhara mengi katika familia lakini familia huyaona madhara hayo kuwa ni madogo na tatizo hili halifahamiki kwa walio wengi. Familia huwa hazina mahusiano mazuri miongoni mwao, runinga huwazuia kuwa pamoja. Zingatia njia mbadala zenye kuweza kuzuia kutazama runinga.

Unamfanyaje mwizi aliyeiba pesa zako? Je vipi kuhusu mwizi aliyekuibia muda wako na maisha ya familia yako? Runinga inakuwa na madhara makubwa zaidi kwako ukilinganisha na kuibiwa kwa pesa zako. Runinga huondoa furaha yako. Unaweza kuzipata pesa zako lakini hauwezi kurudisha muda wako na furaha.

Njia mbadala

Itategemea na umri wa mtoto katika kuchagua shughuli ya kufanya. Kuna vitabu ambavyo vimeainisha shughuli zaidi ya 1000 kwa familia kuweza kuchagua;

1. Kutengeneza ngome
2. Kufanya usafi katika kikundi (jamii)
3. Tembelea maktaba, azima vitabu na fanya kazi za maktaba
4. Sikiliza redio
5. Tembelea sehemu za kuoneshea wanyama au makumbusho
6. Paka rangi picha
7. Nenda katika kituo chako cha jamii au mbuga
8. Nenda kuogelea
9. Soma kitabu kwa sauti (kuwasomea wadogo zako)
10. Andaa hafla
11. Tembea, kimbia au endesha baiskeli
12. Imba wimbo au hifadhi shairi
13. Nenda katazame ndege
14. Ruka kamba
15. Jitolee katika shughuli za kijamii
16. Nenda sehemu ya kuweka kambi na wenzako
17. Andika barua kwa rafiki yako, ndugu au mjukuu
18. Panda maua, mboga mboga au bustani ya dawa za mimea
19. Soma magazeti
20. Cheza drafti
21. Tengeneza bangili za urafiki; weka moja katika mkono wa mmoja na nyingine katika mkono wa mwingine
22. Toa misaada kwa wakimbizi au toa sadaka
23. Anza kufuata ratiba yako
24. Tembelea duka la vitabu
25. Tafiti historia ya familia yako
26. Jifunze ufundi na tengeneza kasha la kuhifadhia vitabu
27. Tengeneza vitu utoe zawadi
28. Simulia na andika simulizi
29. Tembea umbali mrefu. Kusanya mbegu na majani. Tengeneza picha kwa kutumia vitu ulivyokusanya na vihifadhi katika kitu chenye kugandisha.
30. Tazama anga usiku kwa kutumia hadubini. Tambua nyota mbali mbali. Tazama mwezi. Soma kuhusu elimu ya unajimu.
31. Oka vyakula kwa ajili ya majirani zako.
32. Muombe mkubwa wako katika familia yenu akusimulie simulizi kuhusu utoto wake. Nawe uandike simulizi hiyo.
33. Tengeneza siagi
34. Tengeneza yogati
35. Fanya mazoezi
36. Tembea kuelekea kazini au shuleni
37. Cheza mchezo wa kutumia tufe
38. Cheza mpira wa miguu
39. Hudhuria shughuli za dini mbali mbali
40. Cheza mchezo wa kukimbia na viazi
41. Cheza mpira wa miguu, mpira wa wavu na mpira wa kikapu
42. Jifunze kuandika kwa kutumia kinanda cha kinakilishi
43. Jifunze kutumia kinakilishi
44. Jifunze kuendesha vyombo vya moto
45. Cheza mpira wa mezani
46. Winda katika kundi la jamii ili kubaini kitu kilichofichwa
47. Fua nguo kwa mikono
48. Safisha nyumba
49. Safisha madirisha
50. Pika chakula cha jioni na marafiki au familia.
51. Patanisha maelezo ya miamala ya benki
52. Andika marejeo ya kitabu
53. Jadili bajeti ya familia katika mwezi
54. Andaa sherehe
55. Fanya biashara ya kuuza magazeti na rafiki zako
56. Safisha chumba chako
57. Cheza mchezo wa barafu
58. Andika barua kwa mwandishi umpendae, akiwa bado yupo hai au amekufa.

59. Cheza na mnyama wa nyumbani au mnyama wa jirani yako
60. Fanya kazi za nyumbani
61. Rusha tiara
62. Nenda safari ya familia
63. Ning'iniza kipima joto au kipima mgandamizo wa hewa katika mkoba au mti.
64. Andaa maigizo
65. Cheza mchezo wa kuendesha vyombo katika barafu na kuwa mtu mwenye kucheza katika barafu
66. Andaa picha ya kuchora kutoka katika magazeti ya kipindi kilichopita
67. Tembelea sehemu ya kulelea watoto
68. Saidia wazazi kulea watoto
69. Nenda kutembea
70. Cheza mchezo wa mafumbo (chemsha bongo)
71. Tengeneza rafiki mpya
72. Anzisha kundi la kujisomea
73. Cheza michezo na familia au marafiki
74. Unda shamba la wadudu
75. Fanya sherehe katika bustani
76. Unda boti kisha iweke ielee juu ya maji
77. Chora picha ya watu wa familia yako
78. Jifunze namna ya kutumia dira na ramani
79. Jifunze namna ya kutumia vipimo
80. Fanya mazungumzo na watu wakubwa
81. Cheza mchezo wa kutazama
82. Jifunze kushona
83. Tembelea sehemu tofauti za nchi
84. Kamua maziwa ya ng'ombe
85. Panda mti
86. Kusanya vitu vyenye utani, andika katika kitabu na simulia kwa marafiki na familia.
87. Jifunze ngonjera
88. Tazama jua likizama na kuchomoza.
89. Andaa idadi ya vinywaji na vilaji
90. Jifunze kusema misemo rahisi katika lugha tofauti (asante, habari yako, ndiyo, hapana, hesabu 1 hadi 10, siku katika juma….)



Mambo bora zaidi ya kuchagua

Yafuatayo ni mambo bora zaidi kwa watoto kuweza kuyafanya (yamechukuliwa kutoka kwa Beshir na wengine 1998)

SHUGHULI ZA JAMII

1. Jifunze lugha nyingine katika kuongezea lugha zako mbili za msingi; lugha ya asili katika nchi yako na lugha ya kiarabu.
2. Tembelea vikundi vya vijana. Hakikisha kuwa kazi za msingi zinatolewa kwa watoto, hususani wakati wa likizo ya muda mrefu. Kwa kuongezea ukiachana na ufahamu wa elimu na roho, shughuli katika vikundi hivi zihusiane na maigizo ya kuigiza, michezo ya kucheza na mashindano.
3. Kujiunga katika vikundi vya watoto wa kiume na vikundi vya watoto wa kike
4. Kujiunga katika makundi ya kuimba (nashid). Chagua wimbo uliokuwa na maadili na ambao rahisi kwa watoto kujifunza na kuweza kuimba katika jamii.
5. Hudhuria sherehe za usiku; sherehe zilizoandaliwa na watoto na kusimamiwa na wazazi huburudisha zaidi watoto na huimarisha umoja miongoni mwao.
6. Cheza katika mvua, theluji au jua.

'umar ibn al-Khattab alisema

"wafundisheni watoto wenu namna ya kuogelea, kutumia mishale na kukimbiza farasi"

7. Jifunze namna ya kujilinda
8. Jifunze kusoma vizuri Qur'an (tajwid) na ushairi
9. Jifunze kanuni za usalama pindi janga la moto linapotokea
10. Jifunze kuongea katika hadhara ya watu
11. Jifunze kushindana kwa hoja
12. Jifunze kuandika kiingereza na kiarabu
13. Nenda kavue samaki
14. Jifunze namna ya kumpatia huduma ya kwanza mtu mwenye matatizo ya moyo
15. Jifunze jinsi ya kumhudia mtu mwenye matatizo ya kupumua.

SHUGHULI ASILIA

1. Chunguza mazingira asilia kwa kasi ya uwezo wako. Sehemu za kufanya matembezi zipatikane pale ambapo familia inahitaji kutembea kwa lengo la kuburudika au zaidi ya hivyo kwa lengo la kutazama maajabu ya asili katika mazingira: ndege, wadudu wanaotambaa na kuruka, nyoka, maua na miti. Watoto wanaweza kutumia masaa kutazama miamba katika mto. Pia watoto wanaweza kuendesha baiskeli

2. Tazama nyota. Kutazama nyota ni kitu kizuri. Tumia ramani ya maumbo ya nyota. Chukua fumbate na matunda kisha nenda sehemu yenye mwanga hafifu. Inaweza kuwa katika eneo la nyumbani kwako au hata katika mlima. Pindi kiza kinapoingia, jaribu kuonesha nyumba moja moja baada ya nyingine. Onesha nyota ya Leo na samba. Hatimaye watoto wataweza kubaini maumbo ya nyota kama wanavyoweza kubaini maumbo ya mawingu.

MICHEZO YA KUCHEZESHA

1. Cheza michezo ya kucheza kwa kutumia vidole vya miguu na vidole vya mkono kwa namna ya kulinganisha urefu wa vidole hivyo. Kila mtu akamate mkono wake kwa vidole. Utabaini kuwa kidole cha mwisho ni kidogo kuliko kile kidole kinachotumika katika kuvaa pete na kidole cha kati ndiyo kirefu kuliko vyote lakini mfuatano wa vidole hivi hutofautiana kati ya mtu na mtu. Kisha tazama vidole vyako vya miguu, vua soksi, lalia mgongo kando kando ya mwenzako na tazama miguu yako. Vidole vya miguu vinatofautiana pia.

2. Kuhesabu mbavu za watoto wako pia kunaweza kumfurahisha mtoto kama namna ya kuhesabu kutafanywa na babu au bibi wa watoto.

3. Cheza mchezo wa kusoma herufi. Kila mtu katika gari anatakiwa kukusanya herufi katika alama za barabarani. Herufi hizi lazima zikusanywe katika mpangilio maalumu. Hakuna mtu anayeruhusiwa kugeuka ili kutazama alama za upande wa pili wa barabara. Mtu wa kwanza kuona herufi "Z" atakuwa ameshinda.

4. Katika safari kusanya vibao vya leseni kutoka katika nchi mbali mbali.

5. Cheza mchezo wa "B.B Bumblebee". Naona kitu ambacho wewe hukioni". Unaweza kumshughulisha mtoto wa miaka miwili kwa dakika kadhaa. Unaenda kwanza na kusema "B.B Bumblebee, naona kitu ambacho wewe hukioni na kitu chenyewe kina rangi nyekundu". Kisha unampa

mtoto wako fursa ya kutazama chumba na kujaribu kuhisi na kutaja kipi kitu chekundu unaweza kuwa unakitazama. Kama akitoa jibu sahihi inakuwa zamu yake nae kucheza. Au nachunguza kitu kwa kutumia macho yangu, kitu chenyewe kinaanza na herufi "A" na mtoto anatakiwa aweze kuhisi ni kitu gani hicho ulichokitazama chenye kuanzia na herufi "A".

6. Cheza mchezo wa bao. Moja ya njia ya kuwafundisha watoto wako namna ya kufikiria na kuwa wabunifu ni kwa kucheza mchezo wa bao. Mchezo huu hufundisha uvumilivu na nidhamu ya akili. Pia unaweza kumfundisha muonekano wa mpinzani kwa kuchanganua mbinu zake katika mchezo. Je wanaweza kushambulia au wanajilinda tu? Je wanakuwa tayari kuhatarisha au hapana?

SAUTI ZA ASILI

Waweke watoto wako chini, wafumbe macho yao na wakae kimya kadri ya uwezo wao, wahesabu sauti tofauti wanazozisikia. Wafanye wasikilize sauti za ndege, wadudu na chura.

WAPE FURSA WAWEZE KUFAHAMU MAZINGIRA ASILIA

Watoto wetu wanatoweka katika ulimwengu wa miti, mito na milima kuelekea katika ulimwengu wa runinga, vinakilishi na michezo ya kuchezesha kwa kutumia runinga. Warudishe katika mazingira asilia.

Kula chakula na watoto wako

Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na taasisi ya Taifa ya matumizi mabaya ya vitu katika chuo kikuu huko Columbia.

- Wazazi ambao mara kwa mara hula chakula pamoja na watoto wao (5-7 kwa wiki) wanatazamiwa kuwa na uhusiano mzuri wa kifamilia. Chakula cha usiku cha pamoja ni zaidi ya kushirikiana katika kula. Mazungumzo huwasaidia wazazi kugundua maisha ya watoto, changamoto zao na shughuli ambazo watoto hupendelea kuzifanya (CASA 2012).
- Watoto ambao mara kwa mara hupata chakula cha jioni na wazazi wao wanatarajiwa kuepukana na hatari ya uvutaji, unywaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Ukilinganisha vijana wanaopata chakula cha jioni katika mjumuiko wa familia na wale wasiopata chakula cha jioni katika mjumuiko wa familia (chini ya kiwango cha mara 3 kwa wiki) ni zaidi ya mara mbili hutabiriwa kujaribu kutumia dawa za kulevya katika wakati wa baadaye (CASA 2010)
- Watoto wote wanaoshiriki mara kwa mara katika chakula cha jioni pamoja na familia zao, utafiti unaonesha kuwa huwa wanafanya vizuri katika masomo yao, huwa hawapati msongo wa mawazo wawapo nyumbani na wanawaamini zaidi wazazi wao (CASA 2003)

Madhara ya kutumia Intaneti kupindukia

Mijadala mingi inayotumika katika kuelezea athari za runinga inaweza kuwepo katika utumiaji wa mitandao na michezo ya kuchezesha kwa kutumia vinakilishi (computer). Baadhi ya wazazi hufikiria kuwa vinakilishi huweza kuleta faida tu katika maisha yetu. Sio kweli! Wazazi hutarajia kuwa watoto wao hutumia vinakilishi kwa kiasi kinachofaa na kistaarabu. Ukweli ni kwamba baadhi ya watoto hutumia vinakilishi kupoteza masaa kwa kuwasiliana, kutumia tovuti zisizokuwa na manufaa kwao na kutazama filamu za ngono.

Kama ilivyokuwa runinga, matumizi ya vinakilishi kupita kiasi huondoa hamasa ya kujishughulisha na kumfanya mtu asiweze kufanya kazi, kuongeza unene na huzuia mahusiano mazuri baina ya watoto. Watoto pia hupata mawazo mabaya na matangazo mengi sana kupitia vinakilishi.

Vinakilishi ni vitu vyenye nguvu kuweza kuleta manufaa na taarifa zinazohitajika. Hata hivyo, wazazi wanatakiwa kuwasimamia watoto wao katika utumiaji wao kwa kuweka kufuli, kuzuia baadhi ya tovuti, kutumia njia za usalama na kuwa na ufahamu wa ujumla namna watoto wanavyotumia. Usiruhusu watoto watumie muda mwingi katika mitandao na kuweka vinakilishi sehemu iliyo wazi ambayo familia nzima inaweza kutazama.

Michezo ya kompyuta

Michezo ya kompyuta pia huchukua muda mwingi wa watoto hususani watoto wa kiume. Mchezo ambao huonekana hauna madhara na unafaa kwa watoto, unaweza kudhuru watoto. Michezo ya aina hii huonesha matendo ya kikatili na huwajengea watoto mazoea ya kuicheza, hivyo ni ngumu kwao kuiacha. Hali hii ya kushindwa kuacha kucheza michezo ya aina hii imepelekea kupoteza maisha (vifo vingi vimetokea Korea Kusini) kwa mujibu wa Shirika la utangazaji nchini Uingereza 2005.

Michezo hii hupotosha ukweli, kwa hiyo uhalisia wa dunia huwekwa katika mfumo wa michezo hii na kuwa kama kiburudisho. Michezo yenye kuhamasisha kupigana na mauaji ya kikomandoo hushusha thamani ya maisha ya binadamu. Wanajeshi huwafundisha wenzao namna ya kufanya mauaji kwa kutumia michezo ya aina hii ambayo watoto huicheza. Baadhi ya dhamira nyingine katika michezo hiyo huwa uchawi, mashetani na ulimwengu wa nguvu za giza. Uchawi umekuwa kitu cha kawaida katika michezo ya vinakilishi.

Kwa bahati mbaya, kadri teknolojia inavyokuwa, michezo hii hufananishwa zaidi na maisha halisi na huwa kama maisha halisi. Hii ni hatari, kuchanganya maisha halisi na maisha ya kufikirika. Watoto wasihamasishwe kutokabiliana na ukweli isipokuwa wanatakiwa kukabiliana na changamoto zote zilizopo katika maisha.

Wazazi wanatakiwa kupunguza muda wa watoto wao wanaotumia katika kucheza michezo ya vinakilishi na wanatakiwa kudhibiti michezo ya aina hiyo wanayocheza watoto wao.

Michezo ya Video

Michezo hii ilitambulishwa miaka ya 1970. Tangu kuanzia hapo michezo hii imepata umaarufu kwa watoto. Vitendo vya ukatili navyo vimekuwa maarufu katika michezo hii.

Paducah (Kentucky), Jonesboro (Arkansas), Littleton (Colorado) na Blacksburg (Virginia) ni miongoni mwa miji minne nchini Marekani iliyokumbwa na wimbi la utumiaji wa silaha kwa wanafunzi shuleni kutokana na kucheza michezo yenye kuhusisha vitendo vya kikatili kupitia vinakilishi. Katika mwaka 1999 mauaji yalifanyika katika shule ya elimu ya juu ya Columbine (Gibbs 1999), kijana Eric Harris na Dylan

Klebold waliwapiga risasi watu 13 na kujeruhi wengine 23 kabla ya wao pia kujiua. Watoto hawa wawili walikuwa wakicheza mchezo wa kinakilishi uitwao "angamiza", mchezo wa kutumia risasi wenye dhumuni la kufundisha wanajeshi namna ya kufanya mauaji. Harris aliweza kuendelea na mchezo huu katika namna ya kipekee kwa kuunda watumiaji wa silaha kuwa wawili, kuwa na silaha zaidi na kuunda wahanga wa mashambulizi washindwe kujibu mashambulizi ya adui zao kitu ambacho kinafanana na uhalisia wa kutumia silaha ambao yeye alitaka kuufanya (Anderson na Dill 2000). Kadri watoto wanapokuwa wanafanya vitendo vya kikatili, ndivyo uwezekano wao wa kutenda vitendo hivyo unaongezeka (Clark 1993).

Kuna uhusiano mkubwa kati ya tabia za kikatili kwa watoto na ushirika wao wa kufanya vitendo vya ukatili kupitia michezo ya vinakilishi. Kadri watoto wanavyojihusisha katika vitendo vya kikatili kupitia michezo ya vinakilishi, ndivyo uwezo wao wa kushiriki katika vitendo vya kikatili huongezeka dhidi ya watu wengine.

Watoto wa kiume hucheza michezo ya vinakilishi mara nyingi zaidi ya watoto wa kike. Michezo hii huchochea tabia zisizokubalika katika jamii na dini kama vile mauaji, kauli chafu na wizi.

Mambo ya kijamii yanayopatikana katika michezo ya vinakilishi huathiri muonekano halisi wa wanawake. Katika mchezo wa Nintendo, wanawake wanaonekana kuwa tegemezi wa kufanyiwa vitu badala ya wao wenyewe kuwa watendaji, na katika mazingira yaliyokithiri huwa ni wahanga wa vitu fulani. Michezo mingi huwa inahusu mazingira ya wanawake kuwa wametekwa au kuokolewa (Funk 1993).

Kutazama runinga kupita kiasi kunahusiana na tabia ya ukatili, kufanya vibaya kitaaluma, kujihusisha na mahusiano ya kimwili mapema, kunenepa kupita kiasi, matumizi ya dawa za kulevya na vilevi. Michezo ya vinakilishi inahusiana na uadui na kupigana.

Kucheza michezo ya kikatili hupelekea:

1. Kupata hamasa kimwili
2. Kuongeza mawazo ya kufanya ukatili
3. Kuongeza fikra za kufanya ukatili
4. Kuongeza tabia za kufanya ukatili
5. Kupunguza tabia ya kuweza kusaidia katika jamii

Kuonekana kwa utofauti wa jinsi katika Runinga

1. katika suala la uhusiano wa mwanaume na mwanamke katika runinga, wanaume mara nyingi hutawala.
2. Wanaume katika runinga huwa na fikra sahihi, wana malengo, wasafi, wenye ushindani, wenye nguvu, imara na wavumilivu hali ya kuwa wanawake huwa wenye kupenda mapenzi, wanyenyekevu na waoga kinyume na hapo watakuwa waovu.

3. Kwa upande wa wanaume, msisitizo huwekwa katika uimara, ufanisi na ujuzi; kwa upande wa wanawake msisitizo wao huwekwa katika mvuto na matamanio.

4. Ndoa na familia siyo vitu vya msingi kwa wanaume katika vipindi vya runinga. Takribani nusu ya wanaume, ni vigumu kuambiwa kuwa wamefunga ndoa na hiki kitu huwa kweli kwa wanawake kwa asilimia 11 tu.

Wanawake wengi katika vipindi vya runinga nyakati za usiku huwa vijana, wenye mvuto, wembamba na wenye kujipamba. Wanawake huwekwa katika hali ambayo huwafanya waonekane kuwa na uwezo mzuri kiuchumi zaidi ya kuwa na akili, wasiokuwa na uwezo wa kusaidia na kutarajiwa kutokuwa na uwezo. Wanaume huonekana kuwa na uwezo wa kutatua matatizo mara mbili ya uwezo wa wanawake. Wanawake huonekana kuwa ni chombo cha kujistarehesha kimwili kuliko wanaume na wanaume huonekana kuwa kama hawastahili na hawawezi kukabiliana na mahitaji ya watoto (Seidman, 1999; Davis 1990; Beal 1994).

Katika runinga za muziki nchini Marekani wanawake huonekana kama vyombo vya ngono (kustarehesha wanaume kimwili). Katika picha za muziki wa rapu wanawake huonekana kuwa chombo cha kuleta matamanio. Wanawake huonekana mara nne zaidi ya wanaume katika kuvaa nguo ndogo wakati wanaume wanakuwa wamevaa vizuri kwa kujisitiri.

Uharibifu wa Familia

Michezo ya vinakilishi huhamasisha ubinafsi badala ya kuhamasisha ushirikiano. Mazingira ya michezo kama hii huwa ya mhusika asiyefahamika akitenda jambo la kikatili kwa adui ambaye pia hafahamiki. Ulimwengu wa michezo hii huwa na uchache wa kuonesha ushirikiano. Michezo mingi ya vinakilishi huwa hairuhusu kucheza zaidi ya mtu mmoja kwa wakati mmoja. Taasisi ya taifa ya vyombo vya habari na familia imekuwa ikifanya utafiti juu ya ushawishi wa michezo ya vinakilishi kwa miaka mingi. Tumebaini kuwa michezo ya aina hii iliyokuwa mingi inahamasisha vikundi viovu, ukatili na kuhamasisha vurugu na ukatili dhidi ya wanawake.

Kwa Ufupisho

- Watoto ambao hutumia muda mchache kucheza michezo ya vinakilishi hufanya vizuri shuleni na mara chache sana hupigana
- Hamasisha michezo yenye kuelimisha na piga vita michezo yenye kuchochea ukatili
- Runinga na michezo ya vinakilishi ina mchango mdogo sana kwa watoto wenye tabia nzuri
- Wazazi lazima waweke mipaka katika kipindi ambacho watoto hutumia katika kucheza michezo ya vinakilishi.

Jumla ya yote kama utalinganisha faida na hasara ya ugunduzi wa teknolojia ya kisasa kama intaneti, televisheni simu za mkononi na vinavyofanana na hivyo, utagundua ya kwamba maisha ya vijana wa kisasa ni mazuri na yakupendeza bila ya vitu hivyo. Vimekuwa ni uovu wa lazima. Ingawa ukweli ni kwamba ugunduzi huu umepelekea kuwepo umbali wa mawasiliano baina ya ndugu na kukuza wigo mpana wa maarifa katika alama za vidole vyao, wengi wao wamekuwa ni waathirika wa dawa za kulevya na familia zisizokuwa na kazi pamoja na kuongezeka kwa fikra za usekula. Kukosekana udhibiti wa vifaa hivi kumewafanya vijana kuwa watumwa wa vitu hivyo. Jukumu la wazazi ni kuwaongoza namna nzuri ya kutumia vifaa hivi. Tunatakiwa tuwaongoze katika matumizi ya vitu hivi na si kuacha viwaongoze.

Zima Runinga
WASHA MAISHA

Furahisha watoto zaidi na kuwa nao pamoja. Kulea ni changamoto kubwa sana na kazi nzito yenye malipo, huhitaji sayansi, sanaa na imani. Furahisha watoto wako kila siku zaidi ya runinga.

KAZI ZA KUFANYA



KAZI YA KUFANYA 72: ZIARA YA KITAALUMA

Wapeleke watoto wako katika taasisi tofauti. “ niambie na mimi nitasahau”. Nioneshe na mimi nitakumbuka. Nihusishe nami nitaelewa”.

- Wapeleke watoto wako mahakamani kuona majaji na wanasheria
- Wapeleke watoto wako katika vituo vya askari polisi na magereza
- Tembelea sehemu za ibada za watu wenye imani tofauti na yako pamoja na watoto wako
- Tembelea makumbusho, mbuga za wanyama, maktaba na mashambani

KAZI YA KUFANYA 73: WAFANYE WATAMBUE CHAKULA

Waulize watoto wako kuhusu vitu vyenye kutumika katika chakula na namna ya kuandaa vyakula vifuatavyo; supu, pizza, mkate, yogati, samli, chapati, maandazi, vitumbua, sambusa, biriyani, keki, asali, bisi, chai na kahawa.

Waoneshe watoto wako vifaa hivyo na waoneshe namna ya kuandaa; sabuni, shampuu, karatasi, wino, nguo, plastiki, asfalti, viatu, samani na tandiko.

Muache kila mtoto achague chakula na apike akiwa anapata msaada kutoka kwako.

KAZI YA KUFANYA 74: KIPI UNATHAMINI ZAIDI?

Katika kikao cha familia, muulize kila mwana familia “kama ungekuwa na siku moja tu ya kuishi, ungefanya nini? Kwanini?” kisha muache kila mmoja aweze kujadili jibu.

KAZI YA KUFANYA 75: UZURI WA BUSARA KWA WATOTO

Iweke familia pamoja na muombe mtoto asome kwa sauti yafuatayo: toa maana na toa mifano kwa kutumia uzoefu wako. Hamasisha watoto waweze kutoa mawazo miongoni mwao.

Mtoto wangu: kuwa na tahadhari ya……

- Mtu mwenye hadhi ya juu ukimtusi,
- Mtu mwenye busara unapomfedhehesha,
- Mtu asiyekuwa na maadili utakapomfanyia ukarimu,
- Mtu mpumbavu ukifanya nae utani
- Mtu mwenye kujitenga utakapotaka kushirikiana nae

Oh mtoto wangu mpendwa;

- Nimefurahia vitu vyote vizuri lakini sijaona kitamu kama afya nzuri.
- Nimetaabika kwa kila chenye uchungu lakini sijaona kichungu zaidi ya kuwa na hitajio la mtu mwingine
- Nimebeba mzigo mzito wa chuma na miamba lakini sijaona kitu kizito kama deni.
- Fahamu kuwa kipindi cha maisha yako kipo katika siku za aina mbili….. moja ipo katika upande wako na nyingine inapingana na wewe.
- Inapokuwa siku njema kwao, usiwe na majivuno na ukakosa shukrani, na inapokuwa mbaya kwako kuwa na subira.

KAZI YA KUFANYA 76: JE UNAONGOZA FAMILIA YAKO VIZURI?

JEDWALI:JE NINAFANYA VIPI KAMA MZAZI?

Kuwa mzazi ni changamoto pia ni jambo lenye malipo.Wazazi wanahusika katika kulea, kufundisha nidhamu, kuongoza,na kushauri.Wazazi huhusika katika kufundisha na kusimamia. Wazazi huwa kama mganga mwenye huruma ambaye lengo lake ni kuboresha na siyo kuleta madhara. Wazazi huwezesha watoto, huhamasisha, huwaendeleza na kuwasaidia watoto. Rejea namna unavyolelea watoto kila hatua.

Kama mzazi;

- Je, nilichagua mwenza wangu vizuri?
- Muda na jitihada nilizotumia katika kutafuta mchumba aliye sahihi si chochote ukilinganisha na muda nitakaotumia kushughulika na mke ambaye siye sahihi. Tafuta kwa makini unaweza kupata aliye sahihi.
- Je, nilieleza mipango ya familia yangu kwa watoto wangu kwa ufasaha?
- Je, niliwafundisha maadili yaliyo mema? Kitu kinachofanya nyumba iwe nzuri siyo kuta na vitu vya kuezekea isipokuwa tabia nzuri na maadili
- Je, nilihamasisha uwezo kwa watoto wangu? Kila mtoto anakuwa na vitu vyake anavyopenda,; tunatakiwa kuimarisha vipaji vyao.
- Je, nilitumia vizuri rasilimali za familia yetu: muda, pesa na vitu?
- Je, nilikuwa makini na hisia za watoto wangu na uelewa wao? Uelewa wao unaathari kubwa. Nahitaji kuwa katika akili yao kwa muda.

- Je, niliwafundisha watoto wangu? Watoto hawapendi kudharauliwa, hata kama wanakosea. Wanahitaji kushirishwa katika kazi, kutambuliwa na kupatiwa zawadi kwa walichofanya.
- Je, niliwapatia mwongozo watoto wangu? Wazazi wanatakiwa kufundisha nidhamu na kanuni kwa watoto wao.
- Je nilionesha mfano mzuri kwa watoto? Jinsi mnavyozungumza, jinsi ya kufanya mzaha, namna ya kutimiza ahadi, marafiki unaokuwa nao na heshima unayokuwa nayo….vyote ni muhimu
- Je nimefanya majukumu yangu yote kama mzazi kwa ajili ya Muumba, ambaye amenizawadia na kunipa familia hii?
- Je niliweka mipango ya kutimiza malengo ya familia? Mipango ya familia inatakiwa itoe majibu ya maswali haya.
  - ⏩ vitu gani vinatakiwa kutimizwa?
  - ⏩ kwa nini vitimizwe? Namna gani inakuwa na faida katika makusudio yetu?
  - ⏩ wakati gani wa kutimiza?
  - ⏩ tupo wapi sasa hivi kuhusiana na lengo hili?
  - ⏩ nani anatakiwa atimize?
  - ⏩ namna gani itatimizwa? Shughuli gani zifanyike na malighafi gani zinahitajika?

Watoto wako na mwenza wako wanakutegemea kama wewe unavyowategemea wao. Usiwaangushe.

Sehemu 4

Hitimisho

- Hitimisho 589

Kiambatanisho 1

- Aya za Qur'an 595
- Hadith za Mtume Muhammad (s.a.w) 597

Kiambatanisho 2

- Orodha ya Kazi za Kufanya 600

Kiambatanisho 3

- Marejeo ya Vitabu vya Kiingereza 604
- Marejeo ya Vitabu vya Kiarabu 613
- Hazina za Mitandao ya Tovuti 616
- Faharisi 618
- Indeksia 619

24 HITIMISHO



Chenye umuhimu siyo aina ya gari uliyokuwa nayo, nyumba au akaunti ya benki, isipokuwa ni namna gani ulikuwa mzazi mzuri!

HITIMISHO **560**

Hitimisho 562
Aya Teule za Qur'an na Hadithi za Mtume Kuhusu Malezi 565
Orodha ya Kazi za Kufanya 570
Orodha ya Marejeo ya Vitabu, Hazina ya tovuti, Faharisi na Indeksia 574



Chenye umuhimu siyo aina ya gari uliyokuwa nayo, nyumba au akaunti ya benki, isipokuwa ni namna gani ulikuwa mzazi mzuri!

Hitimisho

Tunaamini kuwa familia ina uwezo na inakusudiwa kuzalisha wananchi wenye maadili na wafanisi. Kazi hii ni vizuri kufanyika katika familia yenye furaha na msaada. Wazazi ndiyo walimu wa kwanza na bora kwa watoto wao. Wazazi wanatakiwa kuwa mfano wa kuigwa, wakombozi, walinganiaji, waelimishaji, wafundishaji maadili nk.

Kwa sasa, siyo ulimwengu wa magharibi wala ulimwengu wa Kiislamu wenye uwezo wa kutoa mfano wa kuigwa katika kulea. Tunahitaji tujifunze miongoni mwetu. Pande za magharibi zimekumbatia mfumo wa maisha wa mtu kujiridhisha mwenyewe. Maadili yameshuka sana. Mfumo huu umeathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, utumiaji wa vilevi, mahusiano ya mapenzi yaliyopindukia na kudhoofisha familia.

Kwa upande mwingine, ulimwengu wa Kiislamu umekumbwa na wimbi la ukandamizaji, utumiaji wa mabavu, hofu, rushwa na shaka. Baadhi ya Waislamu wamekuwa na mawazo ya utumwa, hivyo kuondoa ujasiri, ubunifu na uhuru wa kufikiria. Ulimwengu wa Waislamu umezalisha kizazi kisichokuwa na mawazo yasiyo sahihi, mawazo ya kishirikina na kizazi tegemezi kinachokuwa bila kuzingatia maslahi ya jamii.

Wasiokuwa Waislamu uhitaji kumuweka Mungu nyuma katika maisha yao ili kuweza kufanikiwa katika sayansi na teknolojia, katika hali ya udini kwa kutambua kuwa Mwenyezi Mungu ni mkubwa na yeye ni mjuzi. Waislamu wanatakiwa kuvumbua alivyoviumba Mwenyezi Mungu na kuhamasisha amani, kuwa jamii zilizokuwa huru, kuleta uvumilivu na demokrasia.

Katika ngazi ya chini, uleaji mzuri wa mzazi huwa ni kama mbegu ambayo hu-

weza kuleta yote haya. Ulezi ni kazi ya masaa 24 kwa wiki na sawa na siku 365 kwa mwaka. Ni jitihada yenye kufanyika bila mapumziko, wala usaidizi na hufanywa katika hali ya kuwa na karaha zisizohesabika na msongo mkubwa wa mawazo. Hii inahitaji baba na mama wawe na uamuzi sahihi na ujuzi unaokamilishwa na hisia. Saikolojia, somo la mahusiano ya watu katika jamii, sayansi ya utabibu, mawasiliano na imani vyote ni mahitaji muhimu katika ulezi. Hatuwezi kushindana vita na watoto wetu.Tunatakiwa tuwashinde wao kwa upendo, uvumilivu na mawasiliano ya pande mbili. Usisahau kuwa kila mtoto anapiga kelele; "tafadhali nifanye nijihisi mimi ni muhimu".

Wazazi wengi huhisi kuwa wanawafahamu watoto wao vizuri sana na kinyume chake, lakini ni mara chache sana huwa hivi. Watoto wanaweza kutafsiri kuwa msaada ni kama kuwaingilia mambo yao, ushauri kama kuwatawala na kuwajali kama kuwalea katika mazingira ya utoto zaidi. Kuna uelewa usiokuwa sahihi kwa watoto wengi kuwa wazazi wao hawana upendo kwao. Punguza mtazamo hasi na boresha mawazo chanya kwa mtoto wako. Wazazi wanatakiwa kufahamu aina gani ya malezi wanaonesha kwa watoto wao: kiutawala, kuwaweka huru kwa kuwaruhusu sana kuamua mambo yao, au kidemokrasia au ya kuwabana. Wazazi wajiulize "je, tunafanya kitu sahihi?" jibu linaweza kutafutwa kutokana na vyanzo vingi kadri inavyowezekana.

Jifunze hatua za ukuaji wa mtoto kiumbo na kihisia. Fanya vitu vya msingi kwa mtoto katika muda uliokuwa sahihi. Mfano, watoto wanaweza kukumbuka vizuri basi wafundishe lugha, nyimbo nzuri kabla ya umri wa miaka 10. Makundi yanakuwa na ushawishi mkubwa kwa watoto. Wazazi wanatakiwa kuwapatia mazingira mazuri marafiki wa watoto wao wanapokuja nyumbani kwao. Wazazi wanatakiwa kuwa marafiki na wazazi pia kuwa marafiki wa watoto wao ili kuweza kupata marafiki wazuri kwa watoto wao. Wazazi wanahitaji kupata ujuzi, elimu na dhana za kulea mtoto kiusahihi. Kupandikiza tabia kuna kipindi chake maalumu. Unyonyeshaji huzuia maradhi mengi na humpatia mtoto mtaji wa kisaikolojia na kihisia. Wafundishe watoto kupenda, ujasiri, ubunifu, ukweli, uhuru, kujiamini, ukarimu na uaminifu.

Wazazi wanatakiwa kumfundisha kila mtoto namna ya kutumia vizuri muda anaopata, namna ya kutumia pesa vizuri, maadili ya kujibizana, namna ya kutoa uamuzi, kufanya maombi, kutatua matatizo, maadili mema (ukarimu, heshima, uvumilivu), usikivu na haya.

Watoto ambao baba na mama zao wanakosa muda wa kuwa nao kutokana na kushughulishwa na kazi huwa kama yatima. Wazazi wengi hawapati muda wa kutosha kukaa na watoto wao na kuwafanya watoto wao kutafuta mbinu nyingine kama vile kutazama runinga, zawadi. Kutazama runinga kupita kiasi kuna madhara. Suluhisho ni kutumia muda vizuri na familia. Familia inayoundwa na ndugu wengine kama vile bibi, babu, shangazi, mjomba na binamu ni nzuri katika malezi na huwa mfano wa kuigwa. Jenga tabia ya upendo, ujasiri, ukweli, ubunifu, uwajibikaji na hali ya kujitegemea. Hivi vyote uhitaji kufanyika katika mazingira yenye furaha, ambayo huwa kama mashine ya kuzalisha watu wenye maadili. Nyumba yenye furaha huwa na msingi imara wa mawasiliano endelevu wa pande mbili kati ya wazazi na watoto. Kutoa sifa ni kitu muhimu, watoto

wanapofanya vizuri. Kufanya vikao vya kifamilia kila mwezi ni kitu kizuri katika kuleta amani kwenye familia. Kugusa, kubusu, kukumbatia na kutabasamu hujenga hisia ya upendo baina ya wazazi na watoto. Wazazi wanatakiwa wajue namna ya kuwasikiliza watoto wao.

Watoto ni watazamaji wazuri lakini wabaya wa kutafsiri. Wanatazama na kuona namna wazazi wao wanavyotendeana na namna wanavyowatendea bibi na babu zao, ndugu zao, ndugu, wageni, matajiri na masikini, watumishi na majirani. Wanatazama namna gani mnaishi na paka, mbwa na wanyama kwa ujumla, maua na mazingira. Wanalinganisha maneno ya wazazi na matendo yao na kubaini ukweli na uzandiki. “fanya kama nilivyosema, siyo kama ninavyofanya” haikubaliki. Wazazi wanatakiwa wafanye kila wanachosema. Hata hivyo, pindi wazazi wanapokuwa wanakosea, wanachoweza kufanya ni kukiri makosa yao kwa watoto. Watoto uhitaji kuwa na mtu wa mfano. Kama wazazi hawawezi kuwa kigezo cha kuigwa, watoto wanaweza mchagua mtu mwingine ambaye siyo sahihi. Mbora wa kuigwa katika viumbe vyote ni Mtume wa Mwenyezi Mungu akifuatiwa na viongozi wengine duniani wenye kuhamasisha maadili mema na tabia njema katika familia. Akina mama hufanya kazi ya msingi katika malezi ya mtoto. Siyo kitu cha bahati mbaya kwa nabii Musa, nabii Issa na Mtume Muhammad(s.a.w) kulelewa na mama zao. Kuonesha heshima kwa wanawake katika maisha yetu, wanaume wanatakiwa kuonesha heshima zao kwa maneno na matendo. Mzazi mmoja alisimama na kuwahi kusema “hakuna umuhimu wa kutofautisha!”. Hii kauli haina ukweli. Ulezi ni kazi muhimu isiyoweza kufanyika kwa kujitenga. Kuunda makundi ya kusaidia ni muhimu. Hauwezi kubadili wazee wa kale lakini unaweza kuboresha katika vizazi vya sasa. Kama mzazi, unaweza kuleta tofauti kubwa katika ulimwengu wa sasa kwa hiyo usipoteze matumaini. Bado haujachelewa!

Muonekano wa watoto hutokana na asili, malezi na kubwa katika yote hayo ni Qadari ya Allah. Ulezi ni sayansi pia ni sanaa.

Kitabu hiki ni kitabu cha kwanza katika mfuatano na kwa uwezo wa Allah vingine vitafuata. Tunakaribisha wanazuoni na wataalamu kutajirisha eneo la uzazi kwa kutoa mchango wao wenye kuhitajika kwa sana.

Katika mwisho wa maisha yako jiulize maswali yafuatayo “je ushawahi kuwa mzazi mzuri mwenye kujaribu kuboresha dunia?”

Onesha jitihada. Kuwa na imani kwa Mwenyezi Mungu kisha pumzika! Chenye umuhimu siyo aina ya gari uliyokuwa nayo, nyumba au akaunti ya benki uliyokuwa nayo isipokuwa ni namna gani ulikuwa mzazi mzuri! **Usisubiri hadi muda uwe umepita!**

KIAMBATANISHO 1

Aya Teule za Qur'an na Hadithi za Mtume ﷺ zilizochaguliwa Kuhusiana na Malezi

AYA TEULE ZA QUR'AN

"Na wale wanaosema: Mola wetu Mlezi! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na utujaalie tuwe waongozi kwa wachamngu."

(Qur,an 25:74)

"Na walio amini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao. Kila mtu lazima atapata alicho kichuma."

(Qur,an 52:21)

"Na si mali yenu wala watoto wenu watakao kukaribisheni kwetu muwe karibu, isipokuwa aliye amini na akatenda mema. Hao basi watapata malipo maradufu kwa walio yafanya. Nao watakuwa salama katika maghorofa.……

(Qur,an 34:37)

"Mwenyezi Mungu ndiye aliye kuumbeni kutokana na udhaifu kisha akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha akajaalia baada ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba atakavyo. Naye ndiye Mjuzi, Mwenye uweza."

(Qur,an 30:54)

"Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru."

(Qur,an 16:78)

"Enyi mlio amini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao. Na mkisamehe, na mkapuuza, na mkaghufiria basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu."

(Qur,an 64:14)

"Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu, wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio walio khasiri."

(Qur,an 63:9)

Basi nyinyi abuduni mpendacho badala yake yeye. Sema: Hakika walio khasirika ni wale walio jikhasiri nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama. Tambueni kuwa hiyo ndiyo khasara iliyo dhaahiri."

(Qur,an 39:15)

Na Luqman alipo mwambia mwanawe kwa kumpa mawaidha: Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu. Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa. Na tumemuusia mtu kwa wazazi wake wawili. Mama yake ameichukua mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha ziwa baada ya miaka miwili. (Tumemuusia): Nishukuru mimi na wazazi wako. Na kwangu mimi ndiyo marudio.Na pindi wakikushikilia kunishirikisha na ambayo huna ilimu nayo, basi usiwat'ii. Lakini kaa nao kwa wema duniani, nawe ishike njia ya anaye elekea kwangu. Kisha marejeo yenu ni kwangu mimi, na mimi nitakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda.

Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo fichika, Mwenye khabari ya yote.

Ewe mwanangu! Shika Sala, na amrisha mema, na kataza maovu, na subiri kwa yanayo kupata. Hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.

Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna na kujifakhirisha.

Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda."

(Qur,an 31:13-19)

"Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini."

(Qur,an 18:46)

"Ewe Mola wangu! Nifanye mimi niwe mwenye kusimamisha swala na mwenye kulea watoto wangu katika mazingira ya aina hiyo. Ewe mola wangu! Na unikubalie dua zangu"

(Qur,an 14:40)

"Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili, na Waumini, siku ya kusimama hisabu."

(Qur,an 14:41)

"Na ama ukuta, huo ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini. Na chini yake ilikuwako hazina yao; na baba yao alikuwa ni mtu mwema. Basi Mola wako Mlezi alitaka wafikie utu uzima na wajitolee hazina yao wenyewe, kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Wala mimi sikutenda hayo kwa amri yangu. Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria.."

(Qur,an 18:82)

HADITHI ZA MTUME MUHAMMAD ﷺ

Watu ni kama madini au metali kwa kuwa tabia zao ni tofauti na zisizo fanana, watu waliokuwa bora katika kipindi cha ujinga ni bora katika kipindi cha uislamu kama wanaelewa na kufahamu

(Al-Bukhari na Muslim)

Kitu chenye kuhitajika zaidi baada ya ibada ni kumfanya muislamu afurahi

(Al-Bukhari)

Ni bora kwa mtu kumfundisha heshima mtoto wake kuliko kutoa sadaka kila siku

(Al-Tirmidhi)

Pindi mtu anapofariki matendo yake nayo hufa isipokuwa matatu; sadaka endelevu au elimu ambayo watu watanufaika nayo au mtoto mwema mwenye kuwaombea dua wazazi wake waliofariki.

(Muslim)

Mola wako ana haki katika mwili wako nawe unayo haki katika mwili wako pia na familia yako ina haki kwako; kwa hiyo timiza haki za wote wanaostahili kutoka kwako.

(Al-Bukhari)

Ni dhambi kwa mtu kudharau majukumu yake na kucheleweshe riziki kwa wanaomtegemea.

(Abu Dawud)

Wote ni wachunga na mtawajibika kwa kila mlichokichunga. Imamu ni mchungaji kwa watu wake na ataulizwa kwa hao. Mwanaume ni mchungaji kwa familia yake na atawajibishwa kwa hilo. Mke ni mchungaji wa nyumba ya mume wake na atawajibika kwa hilo. Mtumishi ni mchungaji kwa mali za tajiri wake na atawajibika kwa hilo. Nyote ni wachungaji na mutawajibika kwa mlivyovichunga”

(Al-Bukhari)

USHAURI WA Mtume ﷺ KWA MTOTO

Ibn Abbas wakati alipokuwa mdogo aliambiwa na Mtume "ewe mtoto nakufundisha maneno machache. Jisikie kuwa karibu na Allah, mkumbuke Allah; Allah atakulinda.

Mkumbuke Allah, Allah atakuangalia. Kama utahitaji kitu rejea kwa Allah basi atakupatia. Kama pia utahitaji msaada, omba kwa Allah utapata.

Fahamu kuwa hata kama dunia nzima itaungana kukupinga wewe, hakutakuwa na uwezo wa wewe kudhurika isipokuwa pale tu atakapopenda Allah. Hata kama dunia nzima itaungana kukunufaisha wewe, hautoweza kunufaika hadi Allah awe amepanga iwe hivyo"

(Al-Tirmidhi Na Ahmad Ibn Hanbal)

KIAMBATANISHO 2

Orodha ya Kazi za Kufanya

ORODHA YA KAZI ZA KUFANYA

ZOEZI:	Ukurasa
1. Uliwahi kujiuliza kwanini?	25
2. Mtindo wako wa malezi!	25
3. Orodha ya tabia mbaya kwa watoto	25
4. Andaa orodha na ujiulize: “Mwanangu ana matatizo gani?”	26
5. Tathmini Kupitia Shairi	26
6. Wazazi Wa leo Wakilinganishwa na Wazazi Wa Jana	28
7. Watoto: kipi mnachotarajia kutoka kwa wazazi wenu?	29
8. Hofu Tatu Kubwa Za Karne Ya Ishirini Na Moja	81
9. Matumizi Ya Tabia Kwa Watoto ((Kwa Mfuatano)	81
10. Kujadili Sababu Halisi Za Ukatili kwa Watoto	82
11. Kushughulika Na Matatizo Ya Kijamii	82
12. Mtindo Wa Malezi Marekani Kwa Mujibu Wa Dkt. Spock	82
13. Mjadala Kuhusu Kutetereka Kwa Utamaduni	84
14. Uelewa Wa Viongozi Wazuri	84
15. Kubadilishana Mawazo Ya Historia Ya Familia	85
16. Mjadala Wa Mazingira Ya Nyumbani	97
17. Wazazi Funzeni Watoto Wenu	97
18. Makosa Katika Methali Za Tamaduni Za Waarabu	98
19. Mtazamo Wa Dunia Kuhusu Urafiki	98
20. Majadiliano Tulivu Ya Wanafamilia: Aghalabu	99
21. Mlinganisho wa Maendeleo ya Japani na Ujerumani; na Nchi Za Kiislamu	121
22. Kushukuru Neema Za Mungu Na Baraka Zake	124
23. Kuweka Makosa Katika Mtazamo	124

24. Mambo saba ya kuwafundisha watoto 125
25. Kuzungumzia fikra muhimu 137
26. Maswali na majibu kwa wazazi na vijana 163
27. Kazi yenye mfumo wa tatizo-utatuzi 164
28. Ushauri kwa wazazi 193
29. Jedwali la ratiba ya upimaji afya 233
30. Mpangilio wa mazoezi ya mwili kwa familia 233
31. Jenga utamaduni wa kutumia maamkizi yenye maana 233
32. Mwenendo wa kulala 234
33. Kujenga mazingira mazuri nyumbani 234
34. Kujadili kwa umakini alama za utumiaji dawa za kulevya 235
35. Igiza kama afisa polisi 235
36. Inaniudhi… 255
37. Andaa kitabu cha mwezi 281
38. Mazungumzo ya wazazi 318
39. Nakushukuru mwenyezi mungu 318
40. Barack obama: mfano wa malezi rahisi 318
41. Tajirisha ubongo wa mwanao 378
42. Mfumo wa jedwali la matendo mema kwa watoto 378
43. Kuhifadhi dua 390
44. Kupeana uzoefu juu ya woga 405
45. Njia tisa za kumlea mtoto mwoga 405
46. Ujasiri na imani 406
47. Ujasiri: mtihani kwa vijana 406
48. Kupunguza woga kwa watoto katika vita na majanga 406
49. Namna gani ya kusema “hapana” na kuendelea kuwa marafiki 408
50. Ujasiri ni … 409
51. Utaratibu wa mapenzi ya kila siku 428
52. Kubadilishana uzoefu 442
53. Moja kati ya tabia mbaya sana unayotaka watoto waachane nayo 442
54. Mwenyezi mungu anayatazama makundi yote 459
55. Mafunzo katika ajali na uwajibikaji 460
56. Kupima ufanisi wa utawala wa wazazi 488
57. Elezea mfumo wenu wa kimaadili kwa watoto 488
58. Je wewe ni mzazi unayeunga mkono au unayeingilia maamuzi 488
59. Mazoezi ndani ya familia katika kukuza ubunifu 508

60. Tabia zenye tija! 510
61. Kuelezea maswali magumu. 510
62. Ni mtazamo wa wezi ndio unaosaidia! 511
63. Suluhisho la kibunifu 511
64. Jaribio la kujiimarisha 518
65. Kuridhika 518
66. Ushirikiano wa pamoja 519
67. Mtu ambaye ni kigezo chema kwa mtoto wako 530
68. Mtoto mwenye ushawishi mbaya 530
69. Kama ningejua, ningefanya vinginevyo 531
70. Ziara ya kitaaluma 556
71. Wafanye watambue chakula 556
72. Kipi unathamini zaidi? 556
73. Uzuri wa busara kwa watoto 556
74. Je, unaongoza familia yako vizuri? 557

KIAMBATANISHO 3

Orodha ya Marejeo ya Vitabu (Kiingereza na Kiarabu), Hazina za Mitandao ya tovuti, Faharisi na Indeksia

ENGLISH

Abd al-Ati, Hammudah. *The Family Structure in Islam*. Indianapolis, IN: American Trust Publications, 1997.

———. *Islam in Focus*, 3rd rev. edn. Beltsville, MD: Amana Publications, 1998.

Abdul Hye, Hamid. "Islam on the Rearing of Children." *The Muslim World Journal*, vol. 18 (issues 11 & 12) India, May/June 1991.

Abdullah, Nina. "Qur'an Memorization and Memory." Unpublished paper. Reston, Virginia, 1994.

Abel, Gene and Nora Harlow. *The Stop Child Molestation Book*. La Vergne, Tennessee: Ingram Content Group, 2001.

AbuSulayman, AbdulHamid. "Islam and the Family." Unpublished paper presented at the Conference on 'Youth.' Brunei, April 4, 1984.

———. *Islamization of Knowledge: General Principles and Work Plan*. Herndon, VA: IIIT, 1995.

———. "Islamic Educational Reform: Top Priority in Intellectual Islamic Work." Editorial. *The American Journal of Islamic Social Sciences (AJISS)*, vol. 15, issue 1, USA, Spring 1998.

Abu-Talib, Ali. *Nahjul Balagha* (Peak of Eloquence). Elmhurst, New York: Tahrike Tarsile Qur'an, 1996.

Adler, Jerry and Pat Wingert. "Building a Better Dad." *Newsweek*, June 17, 1996.

Adolphus, Katie, Clare L. Lawton and Louise Dye. "The Effects of Breakfast on Behaviour and Academic Performance in Children and Adolescents." *Frontiers in Human Neuroscience*, vol. 7, August 8, 2013. http://www.frontiersin.org/Journal/Abstract.aspx?s=537&name=human_neuroscience&ART_DOI=10.3389/fnhum.2013.00425

Agnivesh, Swami, Rama Mani and Angelika Köster-Lossack. "Missing: 50 Million Indian Girls". *International Herald Tribune*, November 25, 2005.

AHDB Dairy. "UK Dairy Consumption." September 9, 2015. http://dairy.ahdb.org.uk/market-information/dairy-sales-consumption/uk-dairy-consumption/#.Vi34SNbA6qA

Ahmad, Imad-ad-Dean. *Islam and the Discovery of Freedom*. Beltsville, MD: Amana Publications; 1st edn., 1997.

Aids Education Global Information System (AEGIS), (website article dated August 31, 2001): http://www.aegis.com/news/afp/2001/af010886.html

Akhtar, et al. "Views on Breastfeeding in Medical Science and Islam." *Journal of Islamic Medical Association (JIMA)*, vol. 30, 1998.

Alcohol Concern. Factsheet: Young People and Alcohol. September 2009. http://www.alcoholconcern.org.uk/publications/factsheets-and-booklets/factsheet-young-people

'Ali, 'Abdullah Yusuf. *Translation of The Meaning of the Holy Qur'an*. Beltsville, MD: Amana Publications, 2004.

Allain, Annelies. *Protecting Infant Health*. Penang, Malaysia: International Baby Food Action Network, 1993.

Altalib, Ilham. The Muslim Family in North America. Ten Unpublished Articles. Reston, Virginia: 1984.

———. The Human Heart in the Qur'an, Seminar at ADAMS Center, Herndon, Virginia, September 2008.

Amabile, T.M. and B.A. Hennessey. "The Motivation For Creativity in Children" in T. Pittman & A. Boggiano (Eds.) *Achievement And Motivation: A Social Developmental Perspective*. New York: Cambridge University Press, 1992.

American College of Pediatricians. "Cohabitation: Effects of Parental Cohabitation and other Non-Marital Sexual Activity on Children – Part 2 of 2." July 2014. http://www.acpeds.org/the-college-speaks/position-statements/societal-issues/cohabitation-part-2-of-2

American Sexual Health Association. "Statistics." http://www.ashasexualhealth.org/stdsstis/statistics/

Anderson, Judith P. and John Blosnich. "Disparities in Adverse Childhood Experiences among Sexual Minority and Heterosexual Adults: Results from a Multi-State Probability-Based Sample." *PLoS One*, vol. 8 (1), 2013. http://journals.plos.org/plosone/article?id=10.1371/journal.pone.0054691

Athar, Shahid. "Sex Education for Muslim Youth and Their Parents." *Journal of Islamic Medical Association (JIMA)*, vol. 22, USA, 1990.

———. *Reflections of an American Muslim*. Chicago, IL: Kazi Publications, 1994.

———. (ed.) *Sex Education: An Islamic Perspective*. http://www.teachislam.com/ dmdocuments/33/BOOK/

Atkins, Andrea. "The Gender Divide." *Parenting Magazine*, August 1998.

Badaraco, Joseph. *Leading Quietly*. Harvard Business Review Press, 2002.

Badi, Jamal and Mustapha Tajudin. *Creative Thinking: An Islamic Perspective*. 2nd edn. International Islamic University Malaysia: Kuala Lumpur, Malaysia, 2005.

Bailey, Joseph. *The Serenity Principle*. San Francisco, CA: Harper & Row, 1990.

Ballard, Olivia and Ardythe L. Morrow. "Human Milk Composition: Nutrients and Bioactive Factors." *Pediatric Clinics of North America*, vol. 60 (1), February 2013. http://www.ncbi.nlm.nih.gov/pmc/articles/PMC3586783/

al-Bar, Mohammad Ali and Osama Kandil. "Breastfeeding and Islamic Teaching." *Islamic World Medical Journal*, July/August 1986.

Barazangi, Nimat Hafez. "The Education of North American Muslim Parents and Children: Conceptual Change as a Contribution to the Islamization of Education." *AJISS*. 7(3), 1990.

Baron-Cohen, Simon. "The Extreme Male Brain Theory of Autism." *Trends in Cognitive Sciences*, vol. 6, issue 6, June 2002.

Barzinji, Jamal. "The Prophet as a Father." Lecture at ADAMS Center, Herndon, VA, April, 11, 1993.

Bashir, Askia H. *How to Manage Your Parents (Without Manipulation)*. Atlanta, GA: KYD Publishers, 1995.

BBC News. "Breast Milk 'Boosts Babies' Brainpower." 8 May 2002. http://news.bbc.co.uk/1/hi/health/1974976.stm

BBC News. "South Korean Dies after Games Session." 10 August 2005. http://news.bbc.co.uk/1/hi/technology/4137782.stm

Beal, C. *Boys And Girls: The Development of Gender Roles*. New York: McGraw-Hill, Inc., 1994.

Begley, Sharon. "Your Child's Brain." *Newsweek*, vol. 127, no. 8, p.54, February 19, 1996.

———. "Your Child's Brain: Use It or Lose It." *Newsweek*, June 17, 1996.

———. and Pat Wingert. "Teach Your Parents Well." *Newsweek*, April 28, 1997.

———. "The Parent Trap." *Newsweek,* September 7, 1997.

———. "A Mother's Cocaine Use: They Call Them Snowbabies." *Newsweek*, September 29, 1998.

———. "Tuning Up the Brain." *Newsweek*, Fall/Winter 2000.

Bennett, William. *The Book of Virtues*. New York: Simon & Schuster, 1996.

Beresin, Eugene V. "The Impact of Media Violence on Children and Adolescents: Opportunities for Clinical Interventions." https://www.aacap.org/aacap/Medical_Students_and_Residents/Mentorship_Matters/DevelopMentor/The_Impact_of_Media_Violence_on_Children_and_Adolescents_Opportunities_for_Clinical_Interventions.aspx

Beshir, Ekram and Mohamed Rida. *Meeting the Challenge of Parenting in the West: An Islamic Perspective*. Beltsville, MD: Amana Publications, 1998.

Biller, Henry. *Fathers and Families: Paternal Factors in Child Development*. Westport, Connecticut: Auburn House, 1993.

———. "The Father Factor in Building a Better Dad." *Newsweek,* June 17, 1996.

Blum, Deborah. *Sex on the Brain: The Biological Differences Between Men and Women*. New York: Penguin Books, 1998.

Bohmer, Carol and Andrea Parrot. *Sexual Assault on Campus: The Problem and the Solution*. New York: Lexington Books, 1993.

Boorstein, Sylvia. *It's Easier Than You Think*. San Francisco, CA: HarperCollins, 1996.

Booth, Caroline and Mindy Henderson. *I Love My Grandmother Because….* Nashville, TN: Rutledge Hill Press, 1998.

Boydston, Jo Ann, ed. *The Collected Works of John Dewey*. Carbondale and Edwards-ville: Southern Illinois University Press, 1969-1991.

Bradley, Raymond Trevor, Mike Atkinson, Dana Tomasino and Robert A. Rees. *Facilitating Emotional Self-Regulation in Preschool Children*. Boulder Creek, California: Institute of HeartMath, 2009.

Brady, David and Rebekah Burroway. "Targeting, Universalism, and Single-Mother Poverty:

A Multilevel Analysis Across 18 Affluent Democracies." *Demography*, vol. 49, issue 2, 2012, pp.719-746.

Branden, Nathaniel. *The Psychology of Self-Esteem: A Revolutionary Approach to Self-Understanding that Launched a New Era in Modern Psychology*. San Francisco, CA: Jossey-Bass, 2001.

Brawer, Barney. "Raising Sons in a World of Changing Gender Roles." *Women in Higher Education*, November 1998.

Brazelton, Leach and Michael Lemonick. "War of the Diapers." *Time*, January 25, 1999, vol. 153, no. 3.

Brizendine, Louann. *The Female Brain*. New York: Morgan Road Books, 2006.

Brooks, Arthur. *Gross National Happiness*. New York: Basic Books, 2008.

Brown, H. Jackson, Jr. *Life's Little Treasure Book On Success*. Nashville, TN: Rutledge Hill Press, 1994.

———. *Life's Little Treasure Book On Marriage and the Family*. Nashville, TN: Rutledge Hill Press, 1994.

———. *Life's Little Treasure Book On Parenting*. Nashville, TN: Rutledge Hill Press, 1995.

———. *Life's Little Treasure Book On Friendship.* Nashville, TN: Rutledge Hill Press, 1996.

Burgess. *Fathers and Parenting Interventions*. London: Fatherhood Institute, 2009.

Burt, Sandra and Linda Perlis. *Parents as Mentors: A New Perspective on Parenting that Can Change Your Child's Life*. Rocklin, CA: Prima Publishing, 1999.

Campo, Juan. *Encyclopedia of Islam*. New York: Infobase Publishing, 2009.

Canadian Child Care Federation. "Children and Creativity." Resource Sheet no. 15, http://www.cccffcsge.ca/docs/cccf/rs015_en.htm

Cancer Research UK. "Cervical Cancer Research Factors." http://info.cancerresearchuk.org/cancerstats/types/cervix/riskfactors/

Canfield, Jack and Mark Victor Hansen. *Another Sip of Chicken Soup for the Soul.* Kansas City, MO: Andrews McMeel Publishing, 1997.

———. *Chicken Soup for the Father's Soul*. Deerfield Beach, Florida: Health Communications, 2001

Carlson, Richard. *Don't Sweat the Small Stuff – and It's All Small Stuff: Simple Ways to Keep the Little Things from Taking over Your Life*. New York: Hyperion, 1997.

Carmichael, Mary. "Stronger, Faster, Smarter." *Newsweek*, March 26, 2007.

———. "A Shot of Hope." *Newsweek,* October 1, 2007.

Cassidy, Anne. "Take Charge of Your Time." *Working Mother*, May 1998.

Cassidy, Jude and Phillip Shaver. *Handbook of Attachment: Theory, Research and Clinical Applications.* New York: Guilford Press, 1999.

Centers for Disease Control and Prevention [CDC]. "Sexual Violence: Facts at a Glance." 2012. http://www.cdc.gov/violenceprevention/pdf/sv-datasheet-a.pdf

CDC. "Trends in the Prevalence of Suicide–Related Behavior National YRBS: 1991—2013." http://www.cdc.gov/healthyyouth/data/yrbs/pdf/trends/us_suicide_trend_yrbs.pdf

CDC. "10 Leading Causes of Death by Age Group, United States – 2013." http://www.cdc.gov/injury/wisqars/pdf/leading_causes_of_death_by_age_group_2013-a.pdf

CDC. "Breastfeeding Report Card: United States/2013." July 2013. http://www.cdc.gov/breastfeeding/pdf/2013breastfeedingreportcard.pdf

CDC. "Breastfeeding Report Card: United States/2014." July 2014. http://www.cdc.gov/breastfeeding/pdf/2014breastfeedingreportcard.pdf

CDC. "Reported STDS in the United States: 2013 National Data for Chlamydia, Gonorrhea, and Syphilis." December 2014. http://www.cdc.gov/std/stats13/std-trends-508.pdf

CDC. "About Teen Pregnancy: Pregnancy in the United States." Last updated May 19, 2015. http://www.cdc.gov/teenpregnancy/about/index.htm

CDC. "Breastfeeding among U.S. Children Born 2002-2012 CDC National Immunization Surveys." Division of Nutrition, Physical Activity and Nutrition. Last updated July 31, 2015. http://www.cdc.gov/breastfeeding/data/NIS_data/

CDC. "Childhood Obesity Facts." Last updated August 27, 2015. http://www.cdc.gov/healthyschools/obesity/facts.htm

CDC. "Nutrition and the Health of Young People." Last updated August 28, 2015. http://www.cdc.gov/healthyschools/nutrition/facts.htm

CDC. "Adult Obesity Facts." Last updated September 21, 2015. http://www.cdc.gov/obesity/data/adult.html

CDC. "National Survey of Family Growth." October 2015. http://www.cdc.gov/nchs/data/factsheets/factsheet_nsfg.htm

Cesarone, Bernard. *"Video Games and Children*." Urbana, Illinois: ERIC Clearinghouse on Elementary and Early Childhood Education, University of Illinois, 1994.

Chandler, Michael Alison and Maria Glod. "More Schools Trying Separation of the Sexes." *The Washington Post*, June 15, 2008.

Cherry, Kendra. "Parenting Styles: The Four Styles of Parenting." Updated October 12, 2014. http://psychology.about.com/od/developmentalpsychology/a/parenting-style.htm

———. "What is Uninvolved Parenting?" Updated May 26, 2015. http://psychology.about.com/od/childcare/f/uninvolved-parenting.htm

Clark, C.S. "TV Violence." *CQ Researcher*, (3), March 26, 1993.

Clark, Reginald. *Family Life and School Achievement*. Chicago, IL: University of Chicago Press. 1983.

Clinton, Hillary R. *It Takes a Village To Raise a Child*. New York: Simon & Schuster, 1996.

Cohn, D'vera, Jeffrey S. Passel, Wendy Wang and Gretchen Livingston. "Barely Half of U.S. Adults Are Married – A Record Low." December 14, 2011. http://www.pewsocialtrends.org/2011/12/14/barely-half-of-u-s-adults-are-married-a-record-low/

Coleman, James Samuel. *Adolescent Society: The Social Life of the Teenager and Its Impact on Education*. New York: The Free Press, 1961; Macmillan, 1963.

Coloroso, Barbara. *Kids are Worth it! Giving Your Child the Gift of Inner Discipline*. New York: Harper Collins, 2002.

Copen, Casey E., Kimberley Daniels, Jonathan Vespa and William D. Mosher. "First Marriages in the United States: Data From the 2006-2010 National Survey of Family Growth." National Health Statistics Reports, no. 49, National Center for Health Statistics, March 22, 2012.
http://www.cdc.gov/nchs/data/nhsr/nhsr049.pdf#x2013;2010%20National%20Survey%20of%20Family%20Growth%20[PDF%20-%20419%20KB

Covey, Stephen R. "Secrets of Much, Much Better Family Relationships." *Bottom Line*, July 30, 1992.

Davidson, Maurice and Minnesota Fathering Alliance. *Working with Fathers: Methods and Perspectives*. Stillwater, Minnesota: Nu Ink, 1992.

Davis, D. "Portrayals of Women in Prime Time Network Television: Some Demographic Characteristics." *Sex Roles*, vol. 23, 1990, pp.325–332.

Davis, William B., Kate E. Gfeller and Michael H. Thaut. *An Introduction to Music Therapy*. Silver Spring, Maryland: American Music Therapy Association, 2008.

Dawson, Geraldine. "Imitation and Social Responsiveness in Autistic Children." *Journal of Abnormal Child Psychology*, vol. 12, 1984, pp.209–225.

Dodd, Virginia. "Implications of Kangaroo Care for Growth and Development in Preterm Infants." *Journal of Obstetric, Gynecologic, and Neonatal Nursing,* vol. 34, no. 2, March 2005, pp.218–232.

D'Oyen, Fatima M. *The Miracle of Life*. Leicester, UK: Islamic Foundation, 1996.

The Economist. "Arab Learning: Know Thyself." October 25, 2003.

eHow Website. How to Teach Kids to Say No to Peer Pressure. http://www.ehow.com/how_6108016_teach-kids-say-peer-pressure.html

Eidelman, Arthur I. and Richard J. Schanler. "Breastfeeding and the Use of Human Milk." *Pediatrics*, vol. 129 (3), March 1, 2012. http://pediatrics.aappublications.org/content/129/3/e827.full

Elbert, Thomas, Christo Pantev, Christian Wienruch, Brigitte Rockstroh and Edward Taub. "Increased Cortical Representation of the Fingers of the Left Hand in String Players." *Science Journal*, vol. 270, no. 5234, October 13, 1995, pp.305–307.

Elias, Maurice, Steven Tobias and Brian Friedlander. *Emotionally Intelligent Parenting, How to Raise A Self-Disciplined, Responsible, Socially Skilled Child.* London: Hodder and Stoughton, 2000.

Eliot, Lise. *Pink Brain, Blue Brain*. New York: Houghton Mifflin Harcourt, 2009.

Elkadi, Iman. "Construction of Muslim Communities: Raising Children." *Al-Ittihad*. Gary, Indiana: The MSA of the US and Canada, spring 1972.

Elkind, David. "The Family in the Postmodern World." *Phi Kappa Phi Journal*. 1995.

Elmore, Tim. *Nurturing the Leader within Your Child: What Every Parent Needs to Know*. Nashville, TN: Thomas Nelson Publishers, 2001.

Epinions. "Teaching our Children to Love." January 2001. http://www.epinions.com/ kifm-review-3E0B-2F84CB47-3A52CFB3-prod2

Exley, Helen. *Words of Wisdom*. New York: Exley, 1997.

———. *Words of Calm*. New York: Exley, 1998.

Eyre, Linda and Richard. *3 Steps to a Strong Family*. New York: Simon & Schuster. 1994.

———. *Teaching Your Children Values*. Sound recording: 2 cassettes. New

York: Simon & Schuster Audio, 1994.

Faber, Adele and Elaine Mazlish. *How to Talk so Kids Will Listen and Listen so Kids Will Talk*. New York: Avon Books. 1982.

———. *Siblings Without Rivalry*. New York: Avon Books. 1998.

Fannoun, Kathy. *Our Loving Grandparents*. Chicago, Illinois: Iqra, 1994.

Ferguson, Andrew. "Character Goes Back to School." *Time*, May, 24, 1999, vol. 153, no. 20, p.68.1

Field, T., Healy B., Goldstein S., Perry S., Bendell D., Schanberg S., Zimmernan E. A. and Kuhn C. "Infants of Depressed Mothers Show Depressed Behavior Even with Non-depressed Adults." *Child Development*, vol. 59, issue 6, December 1988, pp.1569–1579.

Fisher, Terri D, Zachary T Moore and Mary-Jo Pitteger. "Sex on the Brain." *Journal of Sex Research*, vol. 49, issue 1, 2012, pp.69–77.

Fisher, Max. "Chart: The U.S. Has Far More Gun-Related Killings than Any Other Developed Country." *The Washington Post*, December 14, 2012. https://www.washingtonpost.com/news/worldviews/wp/2012/12/14/chart-the-u-s-has-far-more-gun-related-killings-than-any-other-developed-country/

Food Research and Action Center [FRAC]. "Overweight and Obesity in the U.S." http://frac.org/initiatives/hunger-and-obesity/obesity-in-the-us/

Fowler, Lynda. "Encouraging Creativity in Children." Department of Family &

Consumer Sciences, Ohio State University. http://www.ohioline.osu.edu/flm97/nr04.html

Franklin, Benjamin. *The Autobiography of Benjamin Franklin*. New York: P. F. Collier and Son, 1909.

Freedman, Joshua. "Creativity for Emotional Intelligence: Ideas and Activities." http://www.kidsource.com/kidsource/content4/creativity.eq.html

Friedman, Jenny. "Avoiding Gender Stereotypes: Learn How to Overcome the Typical Stereotypes in Raising Your Son or Daughter." 1998. http://www.americanbaby.com/ab/story.jhtml?storyid=/templatedata/hk/story/data/1172.xml

Funk, J.B. "Reevaluating the Impact of Video Games." *Clinical Pediatrics*, vol. 32, February 2, 1993, pp.86–90.

Geoparent. http://geoparent.com/family/growth/independence.htm.

Gibbs, Nancy. "In Sorrow and Disbelief – Special Report: The Littleton Massacre." *Time*, May 3, 1999.

Gilbert, Michael. "Single-Sex Schools Help Children Thrive: Bleaching Out Gender Differences Hampers the Education of Both Girls and Boys." September 20, 2007. http://www. csmonitor.com/ 2007/0920/p09s01-coop. html.

Gilmartin, Patricia and Jeffrey Patton. "Comparing the Sexes on Spatial Abilities." *Annals of the Association of American Geographers*, vol. 74, issue 4, 1984.

Ginott, G. Haim. *Between Parent and Teenager*. New York: Avon Books, 1971.

Glod, Marie. "Schools Try Elementary Approach to Teaching Foreign Languages." *The Washington Post*, August 8, 2006.

Godfrey, Neale and Carolina Edwards. *Money Doesn't Grow on Trees: A Parent's Guide to Raising Financially Responsible Children*. A Fireside Book. New York: Simon & Schuster, 1994.

Goldscheider, Frances K. and Linda J. Waite. *New Families, No Families? The Transformation of the American Home*. Berkeley, CA: University of California Press, 1991.

Goleman, Daniel. *Emotional Intelligence*. New York: Bantam Doubleday Dell Publishing Group, 1996.

Gookin, Dan and Sandy. *Parenting for Dummies*, 2nd edn. New York: HarperCollins, 2002.
Gordon, Thomas. *Parent Effectiveness Training: The No-Lose Program for Raising Responsible Children*. New York: Three Rivers Press, 2000.
Gray, John. *Truly Mars and Venus: Men are from Mars, Women are from Venus: A Practical Guide for Improving Communication and Getting What You Want in Your Relationships*. New York: HarperCollins, 2003.
Gur, Ruben C., Bruce I. Turetsky, Mie Matsui, Michelle Yan, Warren Bilker, Paul Hughett and Raquel E. Gur. "Sex Differences in Brain Gray and White Matter in Healthy Young Adults." *The Journal of Neuroscience*, vol. 19, no. 10, May 15, 1999, pp.4065–4072.
Gurian, Anita and Alice Pope. "Do Kids Need Friends?" March 21, 2001. http://www.aboutourkids.org/articles/do_kids_need_friends
Gurian, Michael. *Boys and Girls Learn Differently: A Guide for Teachers and Parents*. San Fransisco, CA: Jossey-Bass, 2001.
Han, Euna and Lisa M. Powell. "Consumption Patterns of Sugar-Sweetened Beverages in the United States." *Journal of the Academy of Nutrition and Academics*, vol. 113, no. 1, January 2013, pp. 43-53.http://www.ncbi.nlm.nih.gov/pmc/articles/PMC3662243/
Ibn Sa'd. *Ibn Sa'd's Kitab Al-Tabaqat Al-Kabir* [The Book of Classes]. Translated by S. Moinul Haq. India: Islamic Book Service, 1967.
Harper, Cynthia C. and Sara S. McLanahan. "Father Absence and Youth Incarceration." *Journal of Research on Adolescence*, vol. 14, no. 3, September 2004, pp. 369–397.
Harris Interactive. "Are Americans Still Serving Up Family Dinners?" November 13, 2013. http://www.theharrispoll.com/health-and-life/Are_Americans_Still_Serving_Up_Family_Dinners_.html
Harris, Judith. *The Nurture Assumption*. New York: Free Press, 1998.
Harris, Robert. "Introduction to Creative Thinking." *Virtual Salt*, July 1, 1998 http://www.virtualsalt.com/crebook1.htm
Harrison, Harry H., Jr. *Father to Son: Life Lessons on Raising a Boy*. New York: Workman Publishing, 2000.
Hart, Michael H. *The 100: A Ranking of the Most Influential Persons in History*. New York: Hart Publishing, 1978.
Harvard T. H. Chan School of Public Health. "Sugary Drinks and Obesity Fact Sheet." http://www.hsph.harvard.edu/nutritionsource/sugary-drinks-fact-sheet/
Harvey, Eric, David Cottrell, Alexander D. Lucia, Steve Ventura and Melissa Hazlewood. *The Leadership Secrets of Santa Claus: How to Get Big Things Done in Your "Workshop" – All Year Round*. Dallas, Texas: Walk the Talk Company, 2003.
Al-Hashimi, Muhammad. *The Ideal Muslim*. Translated by Nasiruddin al-Khattab. Saudi Arabia: International Islamic Publishing House, 2005.
Al-Hassani, Salim. *1001 Inventions: Muslim Heritage in Our World*. Manchester, UK: Foundation for Science, Technology and Civilisation, 2011.
Head, Christina. *An Educated Decision: One Approach to the Vaccination Problem Using Homeopathy*. London: Lavender Hill Homeopathic Centre, 1999.
The Health and Social Care Information Centre. "Statistics on Obesity Physical Activity and Diet: England 2013." Version 2, May 2013. https://catalogue.ic.nhs.uk/publications/public-health/obesity/obes-phys-acti-diet-eng-2013/obes-phys-acti-diet-eng-2013-rep.pdf
The Henry J. Kaiser Family Foundation. "Sex on TV 4." Executive Summary 2005. https://kaiserfamilyfoundation.files.wordpress.com/2013/01/sex-on-tv-4-executive-summary.pdf
Al-Hewar, vol. 13, no. 4, Spring 2002.
Hicks, Felicity. "The Role of Music Therapy in the Care of the Newborn," *Nursing Times*, vol. 91, issue 38, September 1995, pp. 31–33.
Holy Bible: New King James Version. Austin, TX: National Publishing Company, 1982.
Home Office and Ministry of Justice. "An Overview of Sexual Offending England and Wales." January 10, 2013. https://www.gov.uk/government/statistics/an-overview-of-sexual-offending-in-england-and-wales
Hughes, Dominic. "The Size of the Average Family Is Getting Smaller." December 9, 2010.

http://www.bbc.co.uk/news/health-11960183
Hughes, Donna M., Laura Joy Sporcic, Nadine Z. Mendelsohn and Vanessa Chirgwin. *The Factbook on Global Sexual Exploitation*. New York: Coalition Against Trafficking in Women, 1999.
Huskinson, Tom, Katya Kostadintcheva, Helen Greevy, Cheryl Salmon, Sarah Dobie and Kathryn Medien. "Childcare and Early Years Survey of Parents 2012-2013." Department for Education, January 2014. https://www.gov.uk/government/statistics/childcare-and-early-years-survey-of-parents-2012-to-2013
Hwedy, Fahmy. "Islam is Greater than Waging a Battle against an Instrument or Art." (In Arabic). *Al-Mujtama*, vol. 933, January 1, 1998.
Hyde, Barbara and Brian Sansoni. "Women Better at Hand Habits, Hands Down." *American Society for Microbiology*, Washington DC. 2005. http://www.eurekalert.org/pub_releases/2005-09/asfm-wba091905.php.
Ibn Khaldun. *Al-Muqaddimah*, Beirut: Dr al-Qalam, 1992.
Ingalhalikar, Madhura, Alex Smith, Drew Parker, Theodore D. Satterthwaite, Mark A. Elliott, Kosha Ruparel, Hakon Hakonarson, Raquel E. Gur, Ruben C. Gur, and Ragini Verma. "Sex Differences in the Structural Connectome of the Human Brain."
PNAS, vol. 111 (2), published ahead of print December 2, 2013, pp. 823-828. http://www.pnas.org/content/111/2/823.full
Institute of Medicine. *The Hidden Epidemic. Confronting Sexually Transmitted Diseases*. Washington, DC: National Academy Press, 1997.
Ip, S., M. Chung, G. Raman, P. Chew, N. Magula, D. DeVine, T. Trikalimos and J. Lau. "Breastfeeding and Maternal and Infant Health Outcomes in Developed Countries." Evidence Report/Technology Assessment No. 153, Rockville, MD: Agency for Healthcare Research and Quality, April 2007. http://archive.ahrq.gov/downloads/pub/evidence/pdf/brfout/brfout.pdf
Irvin, McKinley. http://www.mckinleyirvin.com/Family-Law-Blog/2012/October/32-Shocking-Divorce-Statistics.aspx)
Islamic Schools Department. "Homework: Your Child and You." (Pamphlet). Plainfield, IN: Islamic Society of North America, 1994.
Islamic Society of North America. "Greatest Obstacles Confronting Muslim Children Raised in America." *Islamic Horizons*, vol. 11, no. 11, November 1986.
Ja'fari, Suzanne Fatimah. *Muslim Names*. Beltsville, MD: Amana Publications, 1998.
Jaffe, Charles A. "Your Money." *Chicago Tribune*, April 2, 1998.
Jameelah, Maryam. *The Generation Gap: Its Causes and Consequences*. Lahore, Pakistan: Muhammed Yusuf Khan, 1981.
Johnson, Anne. "Exploring Women's Creativity: The No-Push Method for Developing Creativity." 1999. http://www.womenfolk. com/creativity/kids.htm.
Josephson, Michael S.; Val J. Peter and Tom Dowd. *Parenting to Build Character in Your Teen*. Boys Town, NB: Boys Town Press, 2001.
Kalb, Claudia. "Farewell to Aunt Flo." *Newsweek*, February 3, 2003.
Kane, Frank L. and Leigh Anne Nicholson Bathke. "Parenting and Child Care." *Newsweek*, September 29, 1997.
Kantrowitz, Barbara and Pat Wingert. "How Well do You Know Your Kid?" *Newsweek*, May 10, 1999.
———. and Peg Tyre. "The Fine Art of Letting Go." *Newsweek*, May 22, 2006.
Karp, Miriam. "Make Room for Your Child's Creativity." *Natural Jewish Parenting*, issue 3, 1997. http://www.jewishholiday.com/creativity.html.
Kasule, Omar. "Character-Building." Unpublished paper presented at the Third International Seminar on "Medical Curriculum: The Holistic Approach," Kuala Lumpur, Malaysia, February 1999.
Keller, Nuh. *Becoming Muslim*. Jordan: Wakeel Books. 2001.
Kendall, Francis. *Super Parents, Super Kids*. Johannesburg: Delta Books. 1983.
Kessler, Suzanne J. and Wendy McKenna. "Some Children are Gender Nonconformists." http://www.webehave.com/hottopic.htm
KIDS COUNT Data Center. "Children in Single-Parent Families." http://datacenter.kidscount.org/data/tables/106-children-in-single-parent-families#detailed/1/any/false/36,868,867,133,38/any/429,430
Kilpatrick, William. *Why Johnny Can't Tell Right*

from Wrong and What We Can Do About It. New York: Simon & Schuster, 1993.
Kindlon, Daniel J. and Michael Thompson. *Raising Cain: Protecting the Emotional Life of Boys*. New York: Ballantine Books, 1999.
Knox, David and Caroline Schacht. *Parenting Choices in Relationships: An Introduction to Marriage and the Family*, 5th edn. Belmont, CA: Wadsworth Publishing, 1997.
Komurcu, Nuran. "Effect of Music Therapy on Anxiety in Pregnant Women During Labor" (in Turkish). *Hemsirelik Forumu*, vol. 2, 1999, pp. 89–96.
Kotulak, Ron. cited in: "Unlocking the Mind." *Chicago Tribune*, 1993.
Kreider, Rose M. and Renee Ellis. "Living Arrangements of Children: 2009." *Current Population Reports*, pp. 70-126. Washington, DC: U.S. Census Bureau, June 2011. https://www.census.gov/prod/2011pubs/p70-126.pdf
Kuczmarski, Robert J., Katherine M. Flegal, Stephen M. Campbell and Clifford L. Johnson. "Increasing Prevalence of Overweight Among US Adults." *American Medical Association*, vol. 272, no. 3. 1994.
Kulkarni, Chaya and Lynn Oldershaw. *Helping Children Overcome Their Fears. Comfort, Play and Teach: A Positive Approach to Parenting (Get Set for Life program)*. Toronto, Ontario, Canada: 2005.
Lazear, Jonathon and Wendy. *Meditations for Parents Who Do Too Much*. New York: Simon & Schuster, 1993.
Focus Adolescent Services. http://www.focusas.com.
Leland, John. "Tightening the Knot." *Newsweek*, February 19, 1996.
Lemonick, Michael D. "War of the Diapers." *Time*, January 25, 1999, vol. 153, no. 3.
———. "Eat Your Heart Out." *Time*, July 19, 1999.
Leonhardt, Mary. "It is Never Too Soon to Foster a Love of Reading in Young Children or Too Late to Help an Older Child Gain a Love of Books." *Bottom Line*, May 5, 1991.
Livingston, Gretchen. "The Rise of Single Fathers." July 2, 2013. http://www.pewsocialtrends.org/2013/07/02/the-rise-of-single-fathers/#fn-17500-1
Longfield, Anne and Mike Fitzpatrick. "Should Parenting be Taught?" *The Independent*, December 4, 1999.
Maier, Thomas. "Raised by Dr. Spock." *Newsweek*, March 30, 1998.
———. "On the Life of Dr. Spock." *Biography Magazine*, April 1998.
Maqsood, Ruqaiyyah Waris. *Living with Teenagers: A Guide for Muslim Parents.*
London: Ta-Ha Publishers, 1995.
Martin, Daniel. "Schoolgirls Aged Just Ten Falling Pregnant As Underage Pregnancies Continue To Rise." *Daily Mail*, February 8, 2010.
Martin, Joyce A., Brady E. Hamilton, Michelle J.K. Osterman, Sally C. Curtin and T.J. Mathews. "Births: Final Data for 2013." National Vital Statistics Reports (NVSS). vol. 64, no. 1, January 15, 2015. http://www.cdc.gov/nchs/data/nvsr/nvsr64/nvsr64_01.pdf
Martinez, Gladys, Kimberly Daniels and Anjani Chandra. "Fertility of Men and Women Aged 15-44 Years in the United States: National Survey of Family Growth, 2006-2010." National health statistics report no. 51. Hyattsville, MD: National Center for Health Statistics, April 12, 2012. http://www.cdc.gov/nchs/data/nhsr/nhsr051.pdf
Mason, Frances, Kathryn Rawe and Simon Wright. "Superfood for Babies: How Overcoming Barriers to Breastfeeding Will Save Children's Lives." London: Save the Children, 2013. https://www.savethechildren.org.uk/sites/default/files/images/Superfood_for_Babies_UK_version.pdf
Martino, Steven C., Rebecca L. Collins, Marc N. Elliot, Amy Strachman, David E. Kanouse and Sandra H. Berry. "Exposure to Nondegrading Music Lyrics and Sexual Behavior Among Youth." *Pediatrics*, vol. 118, 2006, pp. 430-441. http://ojp.gov/newsroom/events/pdfs/apa_exposure.pdf
Maternal and Child Health (MCH) Early Childhood Development and Parent Education Program. http://www.ok.gov/health/Child_and_Family_Health/Maternal_and_Child_Health_Service/
Matthews, Andrew. *Making Friends*. Singapore: Media Masters, 1990; Princes Risborough, UK: J. Wilson Booksales, 1998.
Mayhew, Mary M. *Your Star Child: Attracting, Birthing and Parenting an Evolved Soul*. Fairfield, IA: Sunstar Publishing, 1995.

Mazrui, Ali. "North American Muslims: Rising to the Challenge of Dual Identity." *Islamic Horizons*, March–April 1996.

McAndrew, Fiona, Jane Thompson, Lydia Fellows, Alice Large, Mark Speed and Mary J. Renfrew. "Infant Feeding Survey 2010." Health and Social Care Information Centre, November 20, 2012. http://www.hscic.gov.uk/catalogue/PUB08694/Infant-Feeding-Survey-2010-Consolidated-Report.pdf

McKinley Irvin Family Law. "32 Shocking Divorce Statistics." October 30, 2012. http://www.mckinleyirvin.com/Family-Law-Blog/2012/October/32-Shocking-Divorce-Statistics.aspx

Mead, M. Nathaniel. "Contaminants in Human Milk: Weighing the Risks against the Benefits of Breastfeeding." *Environmental Health Perspectives*, vol. 116 (10), October 2008. http://www.ncbi.nlm.nih.gov/pmc/articles/PMC2569122/

Meiji, Stewart. *Parenting: Part Joy, Part Guerrilla Warfare*. Novata, CA: Portal Publications, 1999.

Michigan State University. "Ewe! Only 5 Percent Wash Their Hands Correctly." June 10, 2013. http://msutoday.msu.edu/news/2013/eww-only-5-percent-wash-hands-correctly/

al-Minawi, Kawther M *The Child's Rights in Islam*. Riyadh: Safir Press, 1992.

Mirza, Tanveer Ahmad. "Parenting." Weekly Parenting Workshops at ADAMS Center, Herndon, VA, 1994–1999.

Moir, Anne and David Jessel. *The Real Difference Between Men and Women*. New York: Delta Books, 1991.

Moran, James D. III. Creativity in Young Children. http://www.kidsource.com/kidsource/content2/Creativity_in_kids.html

Morgan, Michael Hamilton. *Lost History: The Enduring Legacy of Muslim Scientists, Thinkers and Artists*. Washington, DC: National Geographic Books, 2007.

Morris, Sophie. "Sex for Sale: The Truth About Prostitution in Britain." *The Independent*. November 26, 2008.

Murad, Abdul Hakim. "Ramadan in Istanbul." *Meeting Point*, August 2009.

Murphy, Sam. "Why Barefoot Is Best For Children." *The Guardian*. August 9, 2010. http://www.guardian.co.uk/lifeandstyle/2010/aug/09/barefoot-best-for-children

Nash, J. Madeleine. "How a Child's Brain Develops." *Time*, February 3, 1997.

———. "Fertile Minds." *Time*, February 3, 1997.

———. "The Personality Genes." *Time*, April 27, 1998.

National Association for the Education of Young Children. www.naeyc.org

National Association of School Psychologists [NASP]. "Youth Gun Violence Fact Sheet." http://www.nasponline.org/resources/crisis_safety/youth_gun_violence_fact_sheet.pdf

The National Center on Addiction and Substance Abuse [CASA]. "The Importance of Family Dinners." September 2003. http://casafamilyday.org/familyday/files/themes/familyday/pdf/Family-Dinners.pdf

CASA. "The Importance of Family Dinners VIII." September 2012. http://www.casacolumbia.org/addiction-research/reports/importance-of-family-dinners-2012

CASA. "2010 Family Dinners Report Finds: Teens Who Have Infrequent Family Dinners Likelier to Expect to Use Drugs In the Future." September 22, 2010. http://www.casacolumbia.org/newsroom/press-releases/2010-family-dinners-report-finds

CASA Family Day. "Family Day – A Day to Eat Dinner with your Children." www.casafamilyday.org

National Conference of State Legislatures [NCSL]. "Postcard: Teen Pregnancy Affects Graduation Rates." http://www.ncsl.org/research/health/teen-pregnancy-affects-graduation-rates-postcard.aspx

NCSL. "Teen Pregnancy Prevention." May 5, 2015. http://www.ncsl.org/research/health/teen-pregnancy-prevention.aspx

National Health Service [NHS]. "Natural Family Planning (Fertility Awareness)." http://www.nhs.uk/Conditions/contraception-guide/Pages/natural-family-planning.aspx

National Institute on Alcohol Abuse and Alcoholism [NIAAA]. "Alcohol Facts and Statistics." March 2015. http://www.niaaa.nih.gov/alcohol-health/overview-alcohol-consumption/alcohol-facts-and-statistics

National PTA Parenting Guide. http://www.lausd.k12.ca.us/Haskell_EL/parent%20information/decision.htm

Natural Resources Defense Council. "Benefits of

Breastfeeding", 2010. http://www.nrdc.org/breastmilk/benefits.asp
Newport, Frank. "Americans Greatly Overestimate Percent Gay, Lesbian in U.S." May 21, 2015. http://www.gallup.com/poll/183383/americans-greatly-overestimate-percent-gay-lesbian.aspx
Nielson, Samara Joy; Lauren M. Rossen; Diane M. Harris and Cynthia L. Ogden. "Fruit and Vegetable Consumption of U.S. Youth, 2009-2010." NCHS Data Brief, no. 156, July 2014. http://www.cdc.gov/nchs/data/databriefs/db156.htm
Norris, Jeannette; Nurius, Paula and Graham, Thomas. "When a Date Changes from Fun to Dangerous." *Violence Against Women*, vol. 5, no. 3, March 1999, pp.230–250.
Office for National Statistics [ONS]. "Households and Families." *Social Trends* 40, 2010. http://www.ons.gov.uk/ons/rel/social-trends-rd/social-trends/social-trends-40/index.html
ONS. "Family size in the UK." http://www.ons.gov.uk/ons/infographics/census-2011--population---family-size/index.html
ONS. "13 Facts About Divorce." February 6, 2014. http://www.ons.gov.uk/ons/rel/vsob1/divorces-in-england-and-wales/2012/sty-13-facts.html
ONS. "Marriages in England and Wales (Provisional), 2012." June 11, 2014. http://www.ons.gov.uk/ons/publications/re-reference-tables.html?edition=tcm%3A77-333066
ONS. "Statistical Bulletin: Live Births in England and Wales by Characteristics of Mother 1, 2013." October 16, 2014. http://www.ons.gov.uk/ons/rel/vsob1/characteristics-of-Mother-1--england-and-wales/2013/stb-characteristics-of-mother-1--2013.html?-format=print
ONS. "Families and Households, 2014." January 28, 2015. http://www.ons.gov.uk/ons/rel/family-demography/families-and-households/2014/families-and-households-in-the-uk--2014.html
ONS. "Crime in England and Wales, Year Ending March 2015." July 16, 2015. http://www.ons.gov.uk/ons/rel/crime-stats/crime-statistics/year-ending-march-2015/index.html
Office of Adolescent Health [OAH]. "Sexually Transmitted Diseases." Last updated July 8, 2015. http://www.hhs.gov/ash/oah/adolescent-health-topics/reproductive-health/stds.html
OAH. "Trends in Teen Pregnancy and Childbearing." Last updated August 28, 2015. http://www.hhs.gov/ash/oah/adolescent-health-topics/reproductive-health/teen-pregnancy/trends.html
The Ohio State University. "In Dual-Career Couples, Mothers Still Do the Most Child Care." 2013. http://researchnews.osu.edu/archive/parentingtime.htm
Olasky, Marvin. *The Tragedy of American Compassion*. Regnery Publishing: 1994.
Osman, Fathi. *Concepts of the Qur'an*. Los Angeles, CA: Multimedia Vera International, 1997.
Parke, Ross, ed. *Review of Child Development Research*, vol. 7. Chicago, Illinois: University of Chicago Press, 1984.
———. *Fatherhood*. Cambridge, Massachusetts: Harvard University Press, 1996.
Parker, Kim and Wendy Wang. "Modern Parenthood: Roles of Moms and Dads Converge as They Balance Work and Family." March 14, 2014. http://www.pewsocialtrends.org/2013/03/14/modern-parenthood-roles-of-moms-and-dads-converge-as-they-balance-work-and-family/
Parkes, Peter. "Milk Kinship in Islam." *Social Anthropology*, vol. 13, issue 3, 2005.
Paul, Jay P., Joseph Catania, Lance Pollack and Ronald Stall. "Understanding Childhood Sexual Abuse as a Predictor of Sexual Risk-taking Among Men who have Sex with Men." *Child Abuse & Neglect*, vol. 25, issue 4, April 2001, pp.557–584.
Peck, Sally. "British Families Don't Eat Together – and, If They Do, It's Often in Front of the TV." *The Telegraph*, February 20, 2013. http://www.telegraph.co.uk/women/mother-tongue/9882717/British-familes-dont-eat-together-and-if-they-do-its-often-in-front-of-the-TV.html
Peterson, Andrea. "Smarter Ways to Discipline Children." December 24, 2012. http://www.wsj.com/articles/SB10001424127887323277504578189680452680490
Pilkington, Ed. "Twenty-Eight Killed in 44 US School shootings since Newton, Study Finds." *The Guardian*, February 12, 2014. http://www.theguardian.com/world/2014/feb/12/school-shootings-newtown-study-gun-violence

Piotrowski, Caroline. "Rules of Everyday Family Life." *International Journal of Behavioral Development*, vol. 21, no. 3, October 1997, pp.571–598.

Porter, Dalia and Gabriel Cervantes. *All About Dad: Insights, Thoughts, and Life Lessons on Fatherhood*. Cincinnati, Ohio: Adams Media Corporation, 2007

Positive Parenting. www.webehave.com

Preschool Education. *Encouraging Creativity in Children*, 1997–2006, http://www.preschool education.com/art60.shtml

President's Council on Fitness, Sports & Nutrition.
http://www.fitness.gov/resource-center/facts-and-statistics/

Pryor, Fred. *How to Manage Conflict, Anger, and Emotion*. Fred Pryor Seminars, 1994, 3-volume video set (6 audio cassettes).

Public Health England. "Infection Report." Health Protection Report, vol. 2, no. 22, June 23, 2015. https://www.gov.uk/government/uploads/system/uploads/attachment_data/file/437433/hpr2215_STI_NCSP_v6.pdf

Public Health England. "PHE Urges Parents to Cut Sugary Drinks from Children's Diets." July 17, 2015. https://www.gov.uk/government/news/phe-urges-parents-to-cut-sugary-drinks-from-childrens-diets

Rogers, Simon. "Gun Homicides and Gun Ownership Listed by Country." *The Guardian*, July 22, 2012. http://www.theguardian.com/news/datablog/2012/jul/22/gun-homicides-ownership-world-list

Ruggeri, Kai and Chloe E. Bird. "Single Parents and Employment in Europe." Short statistical report no. 3, European Commission, April 2014. http://ec.europa.eu/justice/gender-equality/files/documents/140502_gender_equality_workforce_ssr3_en.pdf

al-Qaradawi, Yusuf. *The Lawful and the Prohibited in Islam*. Translated by Kamal el-Helbawy and M. Moinuddin Siddiqui. New Revised Edition by Zaynab Alawiye. London: Al-Birr Foundation, 2003.

Qutb, Sayyid. *In the Shade of the Qur'an*. Translated and edited by Adil Salahi and Ashur Shamis. Leicester, UK: The Islamic Foundation and Islamonline.net, 2011.

Ramey, C.T. The Abecedarian Project. *Encyclopedia of Human Intelligence*. Edited by R.J. Sternberg. New York: Macmillan, 1994.

Rankin, Jane. *Parenting Experts: Their Advice, the Research and Getting it Right*. Westport, CT: Praeger, 2006.

Ricks, Shirley. "Father-Infant Interactions: A Review of Empirical Research." *Family Relations*, vol. 34, no. 4, October 1985, pp.505–511.

Riera, Michael. "Uncommon Sense with Parents of Teenagers." *Target The Family*, August 1996.

Robins, Joyce. *Naming Your Baby*. London, UK: Chancellor Press, 1996.

Robinson, Holly. "The Working Mother's Guide to Breastfeeding." *Working Mother*, May 1998.

Rosemond, John. "Tender Loving Discipline." *Hemisphere* (United Air Lines), June 1993, p.67.

———. "Is Your Family a Healthy One? Family Counselor." *Hemisphere* (United Air Lines), December 1994.

Rycus, Judith and Ronald Hughes. *Child Development and Child Welfare*. Washington, DC: Child Welfare League of America, 1998.

Samalin, Nancy. "Personal Responsibility: How to Teach Children Responsibility." *Bottom Line*, February 15, 1994.

Samon, Katherine Ann. "55 Ways to Make Your Kid Feel Loved." *Parents' Magazine*, January 1999.

Sample, Steven. *The Contrarian's Guide to Leadership*. San Francisco, CA: Jossey-Bass, 2001.

Save the Children. "Breastfeeding Could Save 830,000 Lives A Year." February 17, 2013. http://www.savethechildren.org.uk/news-and-comment/news/2013-02/breastfeeding-could-save-830000-lives-year

Save the Children. "The Power of the First Hour: Breastfeeding Saves Lives." Company Briefings: Nestlé and Danone. https://www.savethechildren.org.uk/sites/default/files/documents/nestle_danone_company_briefing.pdf

Sax, Leonard. *Why Gender Matters: What Parents and Teachers Need to Know about the Emerging Science of Sex Differences*. New York: Broadway, 2006.

Schachter, Robert and Carole Spearin McCauley. *When Your Child Is Afraid*. New York: Simon & Schuster, 1988.

Schirra, Walter. *Chicken Soup For the Father's Soul*. Deerfield Beach, Florida: Health Communications, 2001.
Scott, Buddy. *Relief for Hurting Parents: What to Do and How to Think*. Nashville, TN: Oliver Nelson Books, 1989.
Sears, William. *Keys to Calming the Fussy Baby*. New York: Barron's, 1991.
Seidman, S. A. "Revisiting Sex Role Stereotyping in MTV videos." *International Journal of Instructional Media*, vol. 26, 1999, pp.11–22.
Shamma, Freda. Literature for Muslim American Students in K-12 Islamic Schools and Homeschoolers. Presented at the Islamic Education Conference, Georgetown University, Washington, DC, April 2006.
Shapiro, Laura. "The Myth of Quality Time." *Newsweek*, May 12, 1997.
Shaw, Eva. *For the Love of Children*. Deerfield Beach, Florida: Health Communications, 1998.
Sherman, Paul and Jennifer Billing. "Antimicrobial Functions of Spices." *Quarterly Review of Biology*, vol. 73, issue 3, 1998.
Siddiqui, Dilnawaz. *The Muslim Observer*. April 30, 1999.
Silverstein, Shel. *The Giving Tree*. New York: HarperCollins Publishers, 1986.
Sinclair, Ian. *Health: The Only Immunity: The Alternative to Vaccination*. The Informed Parent Publications, 2009.
Smalley, Gary. "Hidden Keys to Loving Relationships." 16 video cassettes, 1995.
Smith, Charles. *Mighty Hearts: 8 Steps to Raising Kids with Courage*. Paper presented at a Workshop held by the Parenting Education Institute, State College, Pennsylvania, June 2004.
Smith, David and Gary Gates. *Gay and Lesbian Families in the United States.* Washington, DC: Human Rights Campaign, 2001.
Spegelhalter, David. "Is 10% of the Population Really Gay?" *The Guardian*, April 5, 2015. http://www.theguardian.com/society/2015/apr/05/10-per-cent-population-gay-alfred-kinsey-statistics
Spock, Benjamin. *Raising Children in a Difficult Time: A Philosophy of Parental Leadership and High Ideals*. New York: Norton, 1974.
Stanley, Gary. *What My Dog has Taught Me about Life: Meditations for Dog Lovers.* Tulsa, OK: Honor Books, 1999.
Staso, William. "Toddler Brain Development." *Washington Families*, July 1998.
Stein, Rob. "Scientists Finding Out What Losing Sleep Does to a Body." *The Washington Post*, October 9, 2005.
Steube, Alison. "The Risks of Not Breastfeeding for Mothers d Infants." *Reviews in Obstetrics and Gynecology*, vol. 2 (4), Fall 2009, pp. 22-231.
Stevens, Mitchell. "History of Television." Grolier Encyclopedia. https://www.nyu.edu/classes/stephens/History%20of%20Television%20page.htm
Stewart, Hayden, Diansheng Dong and Andrea Carlson. "Why Are Americans Drinking Less Fluid Milk? A Look at Generational Differences in Intake Frequency." Economic Research Report no. 149, U.S. Department of Agriculture, May 2013. http://www.ers.usda.gov/media/1118789/err149.pdf
Streight, David, ed. *Parenting for Character: Five Experts, Five Cases.* Portland, Oregon: Center for Spiritual and Ethical Education, 2008.
Suicide Awareness Voices of Education. "Suicide Facts." http://www.save.org/index.cfm?fuseaction=home.viewPage&page_id=705D5DF4-055B-F1EC-3F66462866F-CB4E6
Sutherland, John and Jane Stoever. "Important Facts about Children and Nutrition." Special Advertising Section, *Newsweek*, September 29, 1997.
———. "Parenting: Child Care." Special Advertising Section, *Newsweek*, September 29, 1997.
Taffel, Ron. *Why Parents Disagree: How Women and Men Parent Differently and How We Can Work Together*. New York: William Morrow, 1994.
———. *Getting Through to Difficult Kids and Parents*. New York: Guilford Press, 2001.
Takim, Liyakatali. Overcoming Dualities: Muslim Youth in North America. Unpublished paper presented at the ISNA Conference, Indianapolis, IN, July 5, 1997.
Taylor, Anna, Alan D Dangour and K Srinath Reddy. "Only Collective Action Will End Undernutrition." The Lancet, vol. 382

(9891), August 10, 2013, pp. 490-491. http://www.thelancet.com/journals/lancet/article/PIIS0140-6736(13)61084-3/fulltext

Time, June 29, 1998. "Giving Birth Online." http://www.time.com/time/community/transcripts/chattr061798.html

Tremblay, George, Allen Israel. "Children's Adjustment to Parental Death." *Clinical Psychology: Science and Practices*, vol. 5, issue 4, 1998.

Tsaliki, Lisa, Despina Chronaki and Kjartan Òlafsson. "Experiences with Sexual Content: What We Know from the Research so Far." EU Kids Online, October 2014. http://www.lse.ac.uk/media@lse/research/EUKidsOnline/EU%20Kids%20III/Reports/SexualContent.pdf

Turecki, Stanley and Sarah Wernick. "How to Put Your Foot Down without Squashing Your Child." *Family Circle*, March 16, 1994.

UBIC Consulting. "Ingredients for the World Infant Formula Market." Update 2014. http://www.ubic-consulting.com/food/ingredient/chemical-industries/ingredients-worl-infant-formula-market.html

Underwood, Anne and Anna Kuchment. "Fussy Kids, Flustered Mom." *Newsweek*, August 18, 2008, vol. 152, no. 7, pp.60–62.

UNICEF. *The State of the World's Children 2007*. New York: United Nations International Children's Emergency Fund, 2006.

UNICEF. *Hidden in Plain Sight: A Statistical Analysis of Violence against Children*. New York: Unicef, 2014. http://www.unicef.org/publications/index_74865.html

UNICEF. "Breastfeeding." Updated July 29, 2015. http://www.unicef.org/nutrition/index_24824.html

United Nations. *Arab Human Development Report*. New York: United Nations

Development Program, 2009.

United Nations. *World Population Prospects*. New York: UN Department of Economic and Social Affairs, 2010.

Unus, Iqbal. "A–Z Guide for Muslim Fathers," pamphlet. Herndon, VA: IIIT, 1994.

U.S. Census Bureau. Current Population Survey, Washington DC: March 2002.

U.S. Census Bureau. "Marital Events of Americans: 2009." American Community Survey Reports, August 2011. https://www.census.gov/prod/2011pubs/acs-13.pdf

U.S. Census Bureau. "About Poverty: 2014 Highlights." https://www.census.gov/hhes/www/poverty/about/overview/

U.S. Department of Labor. "Fact Sheet 73: Break Time for Nursing Mothers under the FLSA." Revised August 2013. http://www.dol.gov/whd/regs/compliance/whdfs73.htm

Vedantam, Shankar. "Plagued with Relationship Troubles? Blame Your Parents." *The Washington Post*, February 12, 2007. http://www.washingtonpost.com/wp-dyn/content/article/2007/02/11/AR2007021100931.html

Versi, Ahmed. "Wonder Boy in UK." *The Muslim News*, February 1998.

Vespa, Jonathan, Jamie M. Lewis and Rose M. Kreider, "America's Families and Living Arrangements: 2012." United States Census Bureau, August 2013. https://www.census.gov/prod/2013pubs/p20-570.pdf

Villani, Susan. "Violence in the Media." *Journal of the American Academy of Child and Adolescent Psychiatry*, vol. 38, issue 10, p.1208, 1999.

Walton, Stephen. "Types of Parenting Styles." 2012. http://www.the-positive-parenting-centre.com/types_of_parenting_styles.html

Wang, Wendy and Kim Parker. "Record Share of Americans Have Never Married." September 24, 2014. http://www.pewsocialtrends.org/2014/09/24/record-share-of-americans-have-never-married/

Weale, Sally. "Teenagers Who Watch Screens in Free Time 'Do Worse in GCSEs.'" *The Guardian*, September 4, 2015. http://www.theguardian.com/education/2015/sep/04/teenagers-who-watch-screens-in-free-time-do-worse-in-gcses

Weiss, Rick. "Study Debunks Theory on Teen Sex, Delinquency." *The Washington Post*. November 11, 2007. p.A.3

Wellcome Trust. "One in Ten Women in Britain Report Having Experienced Sex Against Their Will." November 26, 2013. http://www.wellcome.ac.uk/News/Media-office/Press-releases/2013/Press-releases/WTP054813.htm

Willatts, P., J.S. Forsyth, M.K. DiModugno, S. Varma and M. Colvin. "Effect of Long-Chain Polyunsaturated Fatty Acids in Infant Formula on Problem Solving at 10 Months of Age." *The Lancet*, vol. 352, no. 9129, August 29, 1998, pp.688–691.

Williams, Rowan. "Archbishop Damns Disney." *Daily Mail*, July 23, 2002, http://www.dailymail.co.uk/news/article-129452/Archbishop-damns-Disney.html#ixzz0rfbjTvIV

Wimberly, Ed. *A Parent's Guide to Raising Great Kids.* http://www.raisinggreatkids.com/

Winn, Marie. *The Plug-in Drug*. New York: Penguin, 2002.

Winnicott, D. W. *Babies and Their Mothers*. MA: De Capo Press, 1992.

Winterman, Denise. "Handwashing: Why are the British so bad at washing their hands?" October 15, 2012. http://www.bbc.co.uk/news/magazine-19834975

Wolgemuth, Robert D. *She Calls Me Daddy: Seven Things Every Man Needs to Know about Building a Complete Daughter*. Colorado Springs, CO: Focus on the Family Publishing, 1996.

The Women's Committee of the Muslim Students Association of the United States and Canada. *Parents' Manual: A Guide for Muslim Parents*. Baltimore, MD: American Trust Publications, 1976.

Wood, Joyce. "Quality Time." *Family Circle*, March 16, 1994.

Woolf, Marie. "Children to Learn Pitfalls of Being a Parent." *Daily Telegraph*, December 30, 1999.

World Food Programme. "Hunger Statistics." http://www.wfp.org/hunger/stats

World Health Organization. "Breastfeeding Key to Saving Children's Lives." July 30, 2010. http://www.who.int/mediacentre/news/notes/2010/breastfeeding_20100730/en/

World Health Organization. "Global Status Report on Alcohol and Health 2014." 2014. http://apps.who.int/iris/bitstream/10665/112736/1/9789240692763_eng.pdf?ua=1

Wright, Robert. "The Power of Their Peers." *Time*, vol. 152, no. 8, August 24, 1998.

Wulf, Steve. "What Makes a Good School." *Time*, October 27, 1997.

Yang, Sarah. "Helping Parents Navigate the 'New Puberty' for Today's Girls." November 6, 2014. http://news.berkeley.edu/2014/11/06/julianna-deardorff-new-puberty/

Yogman, Michael. "Games Fathers and Mothers Play with Their Infants." *Infant Mental Health Journal*, vol. 2, 1981, pp.241–248.

Zogby International. December 15, 2006.

Zorn, Eric. "Only Way to Teach Values: Help Kids Discover Them." *Chicago Tribune*, April 7, 1998.

المراجع العربية

محمد علي الصابوني. صفوة التفاسير ، بيروت: دار القرآن الكريم، 1981م.

محمد علي الصابوني. مختصر تفسير بن كثير ، بيروت: دار القرآن الكريم، 1981م.

محمد حسن الحمصي. تفسير وبيان مفردات القرآن مع أسباب النزول للسيوطي، دمشق: دار الرشيد ،1984م.

كتب وبحوث عربية

الجزيري، عبد الرحمن، الفقه على المذاهب الأربعة، دار الكتب العلمية، 2003 م.

سابق، السيد، فقه السنة، بيروت: دار الكتاب العربي، 1971م.

أبو الحب، ضياء، الطفل: هذا الكائن العجيب، بغداد: دار الحرية للطباعة، منشورات وزارة الثقافة والإعلام، 1979م.

أبو سلميان، عبد الحميد، "تأملات في ظاهرية ابن حزم وإعجاز الرسالة المحمدية"، مجلة التجديد (كوالالمبور) س2: ع3، 1998.

أبو سلميان، عبد الحميد، البعد النفسي في الخطاب الإسلامي المعاصر، بحث قدم في ندوة المعهد العالمي للفكر الإسلامي، الموسم الثقافي، القاهرة، 1999م.

أبو سلميان، عبد الحميد، أزمة الإرادة والوجدان المسلم: البعد الغائب في مشروع إصلاح الأمة، دمشق: دار الفكر، 2004م.

أبو سلميان، عبد الحميد، دليل مكتبة الأسرة المسلمة، فيرجينيا: المعهد العالمي للفكر الإسلامي، 1988م.

أحمد أحمد، حمد، نحو قانون موحد للأسرة في الأقطار الإسلامية، قطر: جامعة قطر، مكتبة الملك فيصل الإسلامية، 1990م.

البهي، محمد، الفكر الإسلامي والمجتمع المعاصر: مشكلات الأسرة والتكافل، القاهرة: مكتبة وهبة، 1982م.

أحمد التل، شادية، مراحل النمو الإنساني ومطالبها التربوية، إربد: جامعة اليرموك، قسم التربية، 1986م.

الجراجرة، عيسى حسن، ريادة الإسلام في تفهم خصوصية عالم الأطفال وفي تقرير وتطبيق حقوقهم الخاصة في الرعاية والتربية، عمان: دار ابن رشد، دار الكرمل، 1988م.

الجمالي، محمد فاضل، تربية الإنسان الجديد، دمشق: دار الحكمة، 1995م.

محمد، السيد محمد الزعبلاوي، تربية المراهق بين الإسلام وعلم النفس، الرياض: مكتبة التوبة ؛ بيروت: مؤسسة الكتب الثقافية، 1996م.

السيد، فؤاد البهي، الأسس النفسية للنمو من المهد إلى الشيخوخة، القاهرة: دار

النهضة العربية، 1975م.
الضامن، ريما كمال، الأسرة ورعاية الذات الإنسانية للأطفال من 6 إلى 12 سنة، عمان: منشورات دار البشير، 1989م.
العبادي، نضال محمد أمين، الأحاديث النبوية الواردة في الأطفال، جمع وتصنيف وتحقيق، عمان: كلية أصول الدين، رسالة ماجستير، الجامعة الأردنية، 1990م.
العظم، يوسف، براعم الإسلام (في الحياة، وفي العقيدة) ج2، عمان: المكتب الإسلامي، 1985م.
العلواني، طه جابر، أدب الاختلاف، فيرجينيا: المعهد العالمي للفكر الإسلامي، 1997م.
العيسوي، عبد الرحمن، مقومات الشخصية الإسلامية والعربية وأساليب تنميتها، الإسكندرية: دار الفكر الجامعي، 1986م.
الغزالي، محمد أبو حامد، إحياء علوم الدين، القاهرة: عالم الكتب للطباعة والنشر والتوزيع، 2005م.
الغزالي، محمد، كيف نتعامل مع القرآن، فيرجينيا: المعهد العالمي للفكر الإسلامي، 1992م.
الندوي، أبو الحسن، نحو التربية الإسلامية الحرة في الحكومات والبلاد الإسلامية، بيروت: مؤسسة الرسالة، 1985م.
النغيمشي، عبد العزيز محمد، المراهقون، دراسة نفسية إسلامية للآباء والمعلمين والدعاة، الرياض: جامعة الإمام محمد بن سعود الإسلامية، دار المسلم للنشر والتوزيع، الطبعة الثانية، 1993م.
الهاشمي، محمد علي، شخصية المسلم كما يصوغها الإسلام في الكتاب والسنة، دار البشائر الإسلامية، بيروت، 1986م.
بدرانة، سعد الدين أحمد سعد الدين، الأساليب التربوية في غرس القيم العقدية لدى الطفل المسلم، رسالة ماجستير بإشراف د. شادية التل ومروان القيسي، إربد: جامعة اليرموك، 1994م.
جابر، جابر عبد الحميد، علم النفس التربوي، القاهرة: دار النهضة العربية، 1977م.
الحامد، محمد، ردود على أباطيل وتمحيصات لحقائق ديني، دمشق: دار الفكر للطباعة والنشر والتوزيع، 2003م.
حماد، سهيلة زين العابدين، بناء الأسرة المسلمة، جدة: الدار السعودية للنشر والتوزيع، 1984م.
حمد، أحمد، الأسرة: التكوين، الحقوق، والواجبات: دراسة مقارنة في الشريعة والقانون، طنطا: دار الكتب الجامعية، 1986م.
زهران، حامد، علم نفس الطفل، القاهرة: عالم الكتب، 1977م.
زين العابدين، وجيه، الإسلام والتربية الجنسية، الكويت: مكتبة المنار الإسلامية، 1979م.
زين العابدين، وجيه، الإسلام والطفل، مكتبة المنار، الكويت، 1980م.
عفيفي، محمد الصادق، المجتمع الإسلامي وبناء الأسرة، موسوعة المجتمعات والنظم

الإسلامية، الكتاب الرابع، مكتبة الأنجلو المصرية، 1981م.
علوان، عبد الله ناصح، تربية الأولاد في الإسلام، دار السلام للطباعة والنشر والتوزيع، الطبعة الثالثة، جزءان، حلب: سوريا، 1981م.
فاضل، خليل، الصحة النفسية للأسرة، الدار السعودية للنشر والتوزيع، 1987م.
الرافع، رفاعة، المرشد الأمين للبنات والبنين، القاهرة: مطبعة المدارس الملكية، 1871م.
قطب، محمد، منهج التربية الإسلامية، الجزء الأول، القاهرة: دار الشروق، 1989م.
نافع، إبراهيم، في بيتنا مدمن: كيف نمنع الكارثة؟، القاهرة: مركز الأهرام للترجمة والنشر، 1991م.
النجار، عبد المجيد، عقيدة تكريم الإنسان وأثرها التربوي، القاهرة: المسلم المعاصر، س19، ع74-73، 1995م.
يالجن، مقداد والقاضي، يوسف، علم النفس التربوي في الإسلام، الرياض: دار المريخ، 1980م.

مجلات عربية

عبد الله، عبد الستار، في زواج الأقارب: متهم لم تثبت إدانته، مجلة الأسرة، 1996م.
فكار، رشدي، ندوة "الإسلام وتحديات القرن القادم"، القاهرة، 1996م.
الرشودي، فاطمة، مقتطفات، أمريكا: مجلة المرأة المسلمة.
"عشرة أخطاء يرتكبها الآباء مع المراهقين وكيفية تجنبها"، مجلة صحتك اليوم، أكتوبر/ديسمبر 1997م.
سافران، كلير، 6 أفكار تنجح ولدك في المدرسة، المختار، مارس 1987م.
ذكاء الطفل: فطري أم مكتسب؟، الكويت: مجلة المجتمع، 23/9/1999م.

- يالجن، مقداد والقاضي، يوسف، علم النفس التربوي في الإسلام، ؟

Arabic Magazines

مجلات عربية

- عبد الله، عبد الستار، في زواج الأقارب: متهم لم تثبت إدانته، مجلة الأسرة، شوال ١٤١٦هـ/آذار ١٩٩٦
- فكار، رشدي، ندوة "الإسلام وتحديات القرن القادم"، القاهرة، ١٩٩٦
- مجلة الأسرة، عدد ٦١، ٢٠٠٥
- مجلة المرأة المسلمة، أمريكا، مقتطفات من إعداد فاطمة الرشودي
- مجلة صحتك اليوم، عشرة أخطاء يرتكبها الآباء مع المراهقين وكيفية تجنبها، أكتوبر/ديسمبر ١٩٩٧
- سافران، كلير، ٦ أفكار تنجح ولدك في المدرسة، المختار، مارس ١٩٨٧
- ذكاء الطفل: فطري أم مكتسب؟، ١٩٩٩/٩/٢٣، مجلة المجتمع، الكويت

MAHUSIANO YA MZAZI NA MTOTO

Mwongozo huu rahisi kuusoma uliosheheni mafunzo ya kina, umebeba yote unayohitaji kuyajua kuhusu namna gani unaweza kulea kwa kujiamini. Umesheheni ushauri na vidokezo vyenye nguvu, mwongozo huu umeandikwa kwa kutumia tafiti za kisasa na mbinu bora kuhusu namna bora ya kumuendeleza mtoto, ni hazina iliyobeba habari za kila namna kuhusu kumstawisha mtoto, kupunguza msongo utokanao na malezi na kuendeleza mahusiano ya furaha kwa familia. Waandishi wametoa mwongozo wa namna ya kuimarisha tabia, maarifa, maadili na ujuzi pamoja na mtazamo wa imani kwa watoto, unawafaa kwa wazazi wenye watoto wa umri wowote. Mikakati na mbinu nyingi zinazotolewa ni pamoja na: kufundisha watoto jinsi ya kutatua tatizo, kufanya maamuzi, na kuendeleza kujiheshimu. Miongoni mwa kazi ngumu katika dunia ya leo ni kuandaa watoto wachamungu, wenye maadili na wenye mafanikio, raia makini waliotayari kubeba majukumu ya kijamii. Sio kazi rahisi lakini pia inawezekana sana. Ufanisi katika malezi ndio jambo la msingi.

Kwa kiasi kikubwa kitabu kinapendekeza ufumbuzi wa matatizo mengi katika malezi kwa mujibu wa Uislamu. Nimevutiwa na maelezo ya kina kuhusu nadharia nyingi zilizopo zinazoeleza makuzi ya watoto. Waandishi hawakuacha kuzungumzia dhana potofu ambazo ni maarufu katika Saikolojia.

Dkt.KUTAIBA CHALEY, mtaalamu wa akili za watoto, ambaye amethibitishwa na bodi inayoshughulikia akili na neurologia nchini Marekani, pia amewahi kuwa mkuu katika idara inayoshughulikia akili katika Hospitali na Kituo Cha Utafiti Cha Mfalme Faisal Nchini Saudi Arabia.

Kitabu hiki ni miongoni mwa vitabu vilivyojaribu kutazama kwa kina na kwa uweledi wa hali ya juu namna ya kutekeleza malezi bora.

EDRIS KHAMISSA, Mshauri wa Kimataifa Katika Masuala ya Elimu na Maendeleo Ya Binaadamu.

Kitabu hiki kina mambo mengi muhimu na nasema (haya) kama mwandishi wa vitabu vingi juu ya mada ya malezi na mambo ya familia, ambavyo vimefasiriwa katika lugha mbalimbali. Kinawasilisha hazina nyingi na rejea zenye thamani kuwasaidia wazazi kuchambua fikra sahihi na za sawa kutekeleza kwa watoto na kuhimiza kwamba hayo yatapatikana kutokana na kuchanganyika na jamii, na kuamiliana nao pamoja na kushikamana nao kama familia moja, pamoja na hayo mwisho wa kila sura pana orodha ya kazi za kufanya, kama zitatekelezwa na wazazi, zitahakikisha uwepo wa mazingira ya kifamilia yenye afya bora na salama.

Dkt. MOHAMED R. BESHIR, mwanachama wa bodi ya ushauri ya SIFCA "Shura of Islamic Family Councilors of America (Baraza la umoja wa washauri wa familia za kiislamu nchini Marekani)". Pia mshauri kwa Umoja wa Waislamu Canada "(MAC)" na Jumuiya ya Waislamu Marekani kitengo cha Elimu na Malezi.

Kitabu hiki ni zao la utafiti wa kina na mawazo ya kufikirisha kwa kila mtu anayeshiriki katika malezi na kinatoa mwongozo wenye mawazo ya kina juu ya namna gani unaweza kuwa mzazi mahiri katika Dunia ya sasa. Waandishi wamejaribu kuzungukia kila Nyanja inayohusiana na malezi bora pamoja na nyongeza ya nadharia, katika mfumo rafiki wa kiusomaji ambao unaweza tumika na familia za kisasa na za kizamani bila kumchosha msomaji. Binafsi nimependa namna ambavyo kila sura ilivyokuwa na mazoezi ya kutosha juu ya namna ya kuhamisha nadharia kuwa vitendo vya kushirikisha familia nzima ambayo ipo katika changamoto kubwa ya malezi.

FATIMA DESAI, Mwanasheria wa kutetea watoto, LLB Hons; Dip L.G;MA (Child Studies)

International Institute of Islamic Thought